translationWords

Toleo. 7.3

[sw]

Haki miliki na leseni.

translationWords
Tarehe: 2018-09-25
Toleo.: 7.3
Iliyochapishwa na: Door43

unfoldingWord® Translation Academy
Tarehe: 2022-04-29
Toleo.: 27
Iliyochapishwa na: unfoldingWord®

License

Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International (CC BY-SA 4.0)

This is a human-readable summary of (and not a substitute for) the license.

You are free to:

- **Share** — copy and redistribute the material in any medium or format
- **Adapt** — remix, transform, and build upon the material

for any purpose, even commercially.

The licensor cannot revoke these freedoms as long as you follow the license terms.

Under the following conditions:

- **Attribution** — You must attribute the work as follows: "Original work available at https://door43.org/." Attribution statements in derivative works should not in any way suggest that we endorse you or your use of this work.
- **ShareAlike** — If you remix, transform, or build upon the material, you must distribute your contributions under the same license as the original.

No additional restrictions — You may not apply legal terms or technological measures that legally restrict others from doing anything the license permits.

Notices:

You do not have to comply with the license for elements of the material in the public domain or where your use is permitted by an applicable exception or limitation.

No warranties are given. The license may not give you all of the permissions necessary for your intended use. For example, other rights such as publicity, privacy, or moral rights may limit how you use the material.

Jedwali la Yaliyomo

translationWords **24**
Key Terms 24
Abudu 25
Adili, uadilifu 26
Agano 27
Ahadi 28
Aliye Juu 29
Aliyechaguliwa, chagua, watu waliochaguliwa, Aliyechaguliwa, Mteule 30
Amina, kweli 31
amri, kuamuru 32
Batiza, ubatizo 33
baya, ovu, uovu 34
Bila mawaa 35
Binti Sayuni 36
Busara, hekima 37
Bwana wa Majeshi, Mungu wa majeshi, Majeshi 38
Bwana Yahwe, Yahwe Mungu 39
bwana, mkuu 40
chakula cha Bwana 41
Chukizo, mbaya 42
damu 43
dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi 44
Dhamira 45
Dunia, kidunia 46
fadhila, yenye kufaa, upendeleo 47
Farisayo. 48
Fidia 49
funga 50
ghadhabu, hasira 51
habari njema, injili 52
Haki ya uzaliwa 53
haki, adilifu 54
hatia, mwenye hatia 55
hekalu 56
heshima, kuheshimu 57
hukumu 58
Huruma 59
imani 60
imani, aminifu, 61
ingia bila ruhusa 62
ishara, kithibitisho, ukumbusho 63
Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli 64
Jehanamu, ziwa la moto 65
Jemadari 66
jina 67
Jiwe la pembeni 68
jiwe, kupiga jiwe 69
Kanisa 70
katika Kristo, katika Yesu, katika Bwana, katika yeye 71

kazi, vitendo, matendo 72
Kiapo 73
kicho, uchaji 74
Kipatanisho 75
Kristo, Masihi 76
Kuamini, kuamini katika 77
Kuasili 78
Kubariki 79
Kuchaguliwa tangu asili 80
kuhani mkuu 81
Kuhani, ukuhani 82
Kuhukumu, hukumu 83
kujaribu, jaribu 84
kujazwa kwa Roho 85
Kujivuna 86
Kukiri 87
kukomboa, ukombozi, mkombozi 88
Kumkufuru 89
Kumtia mafuta 90
Kuomba, maombi 91
Kupatanisha, maridhiano 92
Kupotea, kuharibika 93
Kurejesha, marejesho 94
kutenga 95
Kuteua, Kuteuliwa 96
kutokuwa na imani, upotofu wa imani 97
Kutubu, toba 98
Kuwa na mapepo 99
Kuzaliwa upya, kuzaliwa na Mungu, kuzaliwa kwa roho 100
kuzimu 101
kweli, ukweli, kuwa kweli 102
Laana, kulaaniwa 103
liwali 104
Mabaki 105
Madhabahu 106
mahali takatifu 107
maisha, uhai, kuishi, kuwa hai 108
Malaika, Malaika mkuu 109
Mamlaka 110
manemane 111
manna 112
Mapenzi ya Mungu 113
maskani 114
Mataifa 115
Matumaini 116
mbingu, anga, mbinguni 117
Mchungaji 118
Mfalme wa Wayahudi 119
Mfano 120
mfano wa Mungu, mfano 121
mfuasi 122
Mfuniko wa upatanisho 123

milele 124
mkate usiyotiwa chachu 125
Mkono wa kulia. 126
Mkristo 127
Mnafiki, unafiki 128
Mnaziri, Naziri 129
Moyo 130
mpendwa 131
Mpinga Kristo 132
mpumbavu, upumbavu, upuuzi 133
Msalaba 134
mtakatifu 135
mtukufu 136
Mtume, utume 137
muhudumu, huduma 138
Mungu 139
Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba 140
mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike 141
muujiza, ajabu, ishara 142
mwaminifu, uaminifu 143
Mwana wa Adamu, mwana wa adamu 144
Mwana wa Mungu, Mwana 145
mwana, mwana wa 146
mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu 147
mwandishi, mtaalamu katika sheria ya Kiyahudi 148
Mwenyezi 149
mwili 150
mwinjilisti 151
Mwokozi 152
Myahudi, Yahudi, Wayahudi 153
Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke. 154
nafsi 155
naivera 156
Nchi ya ahadi 157
ndugu 158
neema, mwenye neema 159
Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko 160
Nguvu 161
nidhamu, nidhamu binafsi 162
nyenyekea, unyenyekevu 163
Nyumba ya Mungu, Nyumba ya Yahweh 164
okoa, salama 165
ombea, sala ya kuombea 166
omboleza, maombolezo 167
Onesha, ufunuo 168
Pasaka 169
Pentekoste au sikukuu za majuma 170
pepo mbaya, roho ovu, roho chafu 171
Rabi, Raboni 172
rehema 173
rithi, urithi, mrithi 174
Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana. 175

roho, kiroho 176
Sabato 177
Sadukayo 178
Safi, kusafisha 179
safi, kusafisha 180
samehe, kusamehe 181
Sanduku 182
Sanduku la agano, Sanduku la Yahweh. 183
Sayuni, Mlima Sayuni 184
Sehemu takatifu, sehemu takatifu sana (patakatifu pa patakatifu) 185
shawishi, ushawishi 186
shemasi 187
sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe 188
Shetani, ibilisi, yule muovu 189
siku ya Bwana, siku ya Yahwe 190
siku ya hukumu 191
siku ya mwisho, siku za mwisho 192
sinagogi 193
sio na hatia 194
stahili, yenye thamani ya, wasiofaa, isiyo na maana 195
Sulubisha 196
tahini, pima 197
takasa, utakaso 198
takatifu 199
takatifu, utakatifu 200
telekeza, kutelekezwa, totoka 201
timiza 202
Tohara 203
towashi 204
tukuza, kutukuza 205
Uaminifu wa agano, fadhili, upendo wa kudumu 206
ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni 207
Ufufuo 208
uovu 209
Upatanisho, kulipia 210
upendo 211
ushirika 212
ushuhuda, shuhudia 213
utauwa, utauwa 214
utawala 215
utukufu, fahari 216
Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi 217
vuka mpaka, kosa 218
Waebrania 219
Wakfu 220
wale kumi na mbili, wale kumi na moja 221
wana wa Mungu 222
watakatifu 223
Watoto, mtoto 224
Watu wa Mungu, watu wangu 225
wema, uzuri 226
wito, kuita, ita 227

wivu 228
woe 229
woga, hofu, hofu ya Yahwe 230
Yaweh 231
Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu 232
Zaburi 233
zawadi 234

Names 235
Abiathari 236
Abimeleki 237
Abinieri 238
Abiya 239
Abrahamu, Abramu 240
Abusalomu 241
Adamu 242
Adoniya. 243
Ahabu 244
Ahazi 245
Ahazia 246
Ahusuero 247
Ai 248
Akila 249
Amaleki, Mwamaleki 250
Amazia 251
Amnoni 252
Amoni, Waamoni wanaume, Waamoni wanawake. 253
Amosi 254
Amozi 255
Anasi 256
Andrea 257
Antiokia 258
Apolo 259
Araba 260
Arami, Waarami 261
Ararati 262
Artashasta 263
Asa 264
Asafu 265
Ashdodi, Azoto 266
Ashera, sanamu ya ashera, Ashtorethi 267
Asheri 268
Ashikelo 269
Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru 270
Asia 271
Athalia. 272
Ayubu 273
Azaria 274
Baali 275
Baasha 276
Babeli 277
Bahari ya Chumvi, Bahari iliyo Kufa 278
Bahari ya Galilaya, Bahari ya Shinerethi, Ziwa la Genezareti, Bahari ... 279

Bahari ya shamu 280
bahari, Bahari Kuu, bahari ya magharibi, Bahari ya Medeterenia 281
Balaamu 282
Baraba 283
Barnaba 284
Baruku 285
Bashani 286
Batholomayo 287
Bathsheba 288
Beelzebuli 289
Beersheba 290
Benaya 291
Benjamini 292
Berea (Beroya) 293
Beth Shemeshi 294
Betheli 295
Bethlehemu 296
Bethueli 297
Boazi 298
Bonde la Kidroni 299
Dameski 300
Dani 301
Danieli 302
Dario 303
Daudi 304
Delila 305
Edeni, bustani ya Edeni 306
Edomu, Muedomu, Idumaya 307
Efeso 308
Efraimu 309
Efrata, Mwefrathi 310
Ekroni 311
Elamu 312
Eleazari 313
Eliakimu 314
Elisabeti 315
Elisha 316
Eliya 317
Engedi 318
Esau 319
Esta 320
Ethiopia, Mtu wa Ethiopia 321
Ezekieli 322
Ezra 323
Farao, mfalme wa Misri. 324
Filipi 325
Filipo, mtume 326
Filipo, mwinjilisti 327
Finehasi 328
Finisia 329
Gabrieli 330
Gadi 331

Galatia 332
Galilaya, Mgalilaya 333
Gathi 334
Gaza 335
Gerari 336
Geshuri 337
Gethsemane 338
Gibea 339
Gibeoni. Wagibeoni 340
Gideoni 341
Gileadi 342
Gilgali 343
Giriki 344
Golgotha 345
Goliati 346
Gomora 347
Gosheni 348
Habakuki 349
Habili 350
Hagai 351
Hajiri 352
Hamathi, Lebo Hamathi, Wahamathi 353
Hamori 354
Hamu 355
Hana 356
Hanania 357
Harani 358
Haruni 359
Hawa 360
Hebroni 361
Henoko 362
Herode Antipa 363
Herode Mkuu 364
Herodia 365
Hezekia 366
Hilikia 367
Horebu 368
Hosea 369
Hoshea 370
Ikonio 371
Isaka 372
Isakari 373
Isaya 374
Ishmaeli 375
Kadeshi, Kadesh-Barnea, Meriba Kadeshi 376
Kaini 377
Kaisari 378
Kaisaria, Kaisaria Filipi 379
Kalebu 380
Kana 381
Kanaani, Mkanaani 382
Kapranaumu 383

Karmeli, Mlima Karmeli 384
Kedari 385
Kedeshi 386
Kefa 387
Kilikia 388
Kipro 389
Kolosai, Wakolosai 390
Kora 391
Koreshi 392
Korintho, Wakorintho 393
Kornelio 394
Krene 395
Krete, Mkrete 396
Kushi 397
Labani 398
Lameki 399
Lazaro 400
Lea 401
Lebanoni 402
Lewiathani 403
Listra 404
Luka 405
Lutu 406
Maaka 407
Makedonia 408
Malaki 409
Manase 410
Mariamu (dada wa Martha) 411
Mariamu Magdalena 412
Mariamu, mama yake Yesu 413
Martha 414
Mathayo, Lawi 415
Mede, Media 416
Melkizedeki 417
Memfisi 418
Mesheki 419
Mesopotamia, Aramu Naharaimu 420
Mgirgashi 421
Mgiriki, Kigiriki 422
Mhiti 423
Mhivi 424
Midiani, Wamidiani 425
Mika 426
Mikaeli 427
Miriamu 428
Misri, Mmisri 429
Mizpa 430
Mji wa Babeli 431
Mji wa Bethani 432
Mji wa Daudi 433
Mlawi, Lawi 434
Mlima Hermoni 435

Mlima wa Mizeituni 436
Moabu, Mmoabu 437
Modekai 438
Moleki, Moloki 439
Mperizi 440
Mshaeli 441
Mto Frati 442
Mto Nili, Mto wa Misri 443
Mto Yordani, Yordani 444
mtu wa Mungu 445
Musa 446
Muumbaji 447
Mwamori 448
Myebusi, Yebusi 449
Naamani 450
Naftali 451
Nahori 452
Nahumu 453
Nathani 454
Nazarethi, Nazarini 455
Nebukadneza 456
Negevi 457
Nehemia 458
Ninawi, Mninwai 459
Nuhu 460
Nyumba ya Daudi. 461
Obadia 462
Omri 463
Padan-aramu 464
Parani 465
Paulo, Sauli 466
Peori, Mlima Peori, Baali Peori 467
Petro, Simoni Petro, Kefa 468
Pilato 469
Ponto 470
Potifa 471
Prisila 472
Rabai 473
Rahabu 474
Raheli 475
Rama 476
Ramothi 477
Rebeka 478
Rehoboamu 479
Rimoni 480
Rubeni 481
Rumi 482
Ruthu 483
Sadoki 484
Sakothi 485
Samaria, Msamaria 486
Samsoni 487

Samweli 488
Sara, Sarai 489
Sauli (A K) 490
Sedekia 491
Senakeribu 492
Sethi 493
Sharoni, Milima ya Sharoni 494
Sheba 495
Shekemi 496
Shemu 497
Shilo 498
Shimei 499
Shinari 500
Sidoni, Wasidoni 501
Sila, Silivanu 502
Simeoni 503
Simoni 504
Sinai, Mlima Sinai 505
Soari 506
Sodoma 507
Stefano 508
Sulemani 509
Syria 510
Tairi, Watairi 511
Tamari 512
Tarishishi 513
Tarso 514
Tera 515
Thesalonike, Wathesalonike 516
Thomaso 517
Tikiko 518
Timotheo 519
Tirza 520
Tito 521
Troa 522
Tubali 523
Uajemi, Waajemi 524
Uarabuni, mwarabu 525
ufalme wa Israeli 526
Ufilisti 527
Ukaldayo, Wakaldayo 528
Uri 529
Uria 530
Uzia, Azaria 531
Vashti 532
Wafilisti 533
Wakerethi 534
Yafa 535
Yafethi 536
Yakobo (mwana wa Alfayo) 537
Yakobo (mwana wa Zebedayo) 538
Yakobo (ndugu wa Yesu) 539

Yakobo, Israeli 540
Yeftha 541
Yehoramu, Yoramu 542
Yehoshafati 543
Yehoyada 544
Yehoyakimu 545
Yehu 546
Yeremia 547
Yeriko 548
Yeroboamu 549
Yerusalemu 550
Yese 551
Yethro, Reueli 552
Yezebeli 553
Yezreeli 554
Yoabu 555
Yoashi 556
Yoeli 557
Yohana (Mbatizaji) 558
Yohana (mtume) 559
Yohana Marko 560
Yona 561
Yonathani 562
Yoramu 563
Yoshua 564
Yosia 565
Yothamu 566
Yuda 567
Yuda Iskariote 568
Yuda mwana wa Yakobo 569
Yuda, ufalme wa Yuda 570
Yusufu (Agano Jipya) 571
Yusufu (Agano la Kale) 572
Zabuloni 573
Zakaria 574
Zakaria (Agano Jipya) 575
Zakayo 576
Zebedayo 577
Zefania 578
Zerubabeli 579

Other 580
Adui 581
agano jipya 582
agizo 583
Ahadi 584
aibisha, ya kuaibisha 585
aibu, fedhehesha 586
aina 587
Amani 588
amri 589
Amri kumi 590
Angalia, Mlinzi 591

angika au nyonga 592
Asali, sega la asali 593
asiye amini, kuto amini 594
Balozi, mwakilishi 595
barua, waraka 596
Bibi harusi 597
Bikira 598
Bure, ubatili 599
Busara 600
Busu 601
Bwana 602
Bwana harusi 603
chafu 604
chemchem, kisima 605
chinja, chinjwa 606
Chochea 607
chui 608
chukiza, chukia 609
dada 610
desturi 611
dhabihu, sadaka 612
dhahabu 613
dhalimu, kwa dhalimu, udhalimu 614
Dharau, kudharauliwa 615
Dhifa 616
dhihaki 617
dhiki 618
Divai, kiriba, divai mpya 619
Dubu 620
dunia, kidunia 621
elekeza, maelekezo 622
erevu 623
fagia 624
fahamu, ufahamu 625
Faida 626
familia 627
Faraja, mfariji 628
Farasi 629
fedha 630
fedhehesha. fedheha 631
filimbi, zumari 632
Fimbo 633
fimbo ya kifalme 634
fundisha, kufundisha, mwalimu, fundishwa 635
funga 636
Furaha 637
furaha, mwenye furaha 638
furahia sana, mwenye furaha 639
fuvu 640
Gari 641
gavana, kutawala, mtawala, serikali 642
Gereza, mfungwa , jela 643

geuka, geuka kando, geuka nyuma 644
Ghadhabu 645
Giza 646
gongo 647
gumia 648
hakimu 649
halali, ipasavyo, kinyume na sheria 650
hali ya chini, kuwa chini 651
Halmashauri 652
Hamira, Chachu 653
Hasira 654
hati 655
haya, aibu 656
hema 657
hema la kukutania 658
Heshima 659
hudumu, huduma 660
huru, uhuru 661
iga, mwigaji 662
Ikulu 663
Imeandikwa 664
inua, inuka 665
jamaa wa karibu 666
jangwa, njika 667
jasiri, ujasiri, ushujaa 668
jikwaa 669
jirani 670
jitu 671
jiwe la kujikwaa 672
joho 673
juma 674
juu, juu sana 675
kabila 676
kaburi 677
Kahaba 678
kama, mfano 679
Kamanda, amri 680
kamata 681
Kamili 682
kanuni 683
kanyaga 684
kanzu au vazi 685
karamu 686
kashfa, mtoa kashfa 687
kaya/famlia 688
kazi, mfanyakazi 689
kereza meno, saga meno 690
kiapo, kuapa, 691
kiasi 692
Kiburi 693
Kichwa 694
kifo, kufa, mfu 695

kifuko cha kifuani 696
kikapu 697
Kimbia 698
Kimbilio, malazi 699
kinanda, kinubi 700
kinara cha taa. 701
kinubi 702
kinyume cha sheria 703
kinywaji kikali 704
Kisasi 705
Kisima,birika 706
Kitabu cha uzima 707
kiti cha enzi 708
Kiumbe 709
Kivuli 710
kizazi 711
kizingiti 712
Komamanga 713
komboa, mkombozi, ukombozi 714
kondoo, kondoo dume, kondoo jike 715
Kosa, mateso, kuumiza 716
kuachwa, kuacha 717
Kuadhibu, adhabu 718
kubeba 719
kuchinja 720
kudanganya, udanganyifu, hila, mdanganyifu 721
Kufanikiwa, mafanikio 722
Kufanya, nia, kujituma 723
kufanywa haki 724
kufinyanga 725
Kufurani 726
kufuru 727
kufuta 728
Kugawa, kupewa 729
kuhamisha, Uhamisho 730
Kuhani mkuu 731
Kuharibu 732
Kuhitimu, waliohitimu 733
Kuhubiri 734
Kuinama chini 735
kujiamini, ujasiri 736
Kujivuna 737
Kujua kabla 738
kujua, ufahamu, kufanya kujulikana 739
kukandamiza, ukandamizaji, mkandamizaji 740
Kukataa 741
Kukatwa 742
Kukemea 743
kukesha 744
Kula 745
kulala na, kuwa na mahusiano na, fanya mapenzi 746
kulewa, mlevi 747

kumbukumbu, sadaka ya kumbukumbu 748
Kumiliki, Miliki 749
Kumuachia 750
kumwaga damu 751
Kundi la watu, watu 752
kundi, mifugo 753
kuomba 754
kuomboleza 755
kupiku 756
Kupokea 757
Kupotea, akipotea, kupotoshwa 758
kupumua, pumzi 759
kura, kupiga kura 760
kusaliti 761
kusanya, kukusanya 762
Kushangaa, kushangaza 763
Kushangaa, mshangao 764
Kusifu 765
Kusihi, ng'ang'ania 766
kusimika 767
Kusujudu 768
Kusukuma 769
Kutangaza, tangazo 770
Kutawala 771
Kutoboa 772
Kutupwa nje, kutupa nje 773
Kuvika 774
Kuvuna, mvunaji 775
Kuwa "tasa" maana yake ni kutoweza kuzaa. 776
Kuwatesa, mateso 777
kuza 778
kuzidisha 779
kuzika, zika 780
Kuzima 781
kwato, 782
la kumi, zaka 783
lala, kulala, aliye lala 784
lango, nguzo ya lango 785
Laumu 786
Lia, kupiga kelele 787
lsio huru, kuwa chini ya, chini ya 788
maangamizi 789
Madhabahu ya kufukizia. 790
mafuriko 791
mafuta 792
Maji 793
majivu, vumbi 794
Majuto 795
Makabila kumi na mbili ya Israeli 796
makapi 797
Makerubi, Kerubi 798
Malkia 799

Mambo ya nyakati 800
Maono 801
mateka, kifungo 802
Mateso 803
Matete 804
maumivu makali 805
mavi, mbolea 806
mavuno/kuvuna 807
mawaa 808
Mawaidha 809
Mawindo, kwa mawindo ya 810
mazao ya kwanza 811
mbawala, paa, paa dume, paa mdogo 812
mbegu, manii 813
mbuzi, mwanakibuzi 814
mbwa mwitu 815
mchungaji, kuchunga 816
meneja, wakili 817
Methali 818
meza 819
mfalme 820
mgeni, ugeni, mgeni 821
mhenga, baba, mababu 822
mifugo 823
milele 824
Mimi, Yahwe 825
Mizabibu 826
Mji mtakatifu 827
mjumbe 828
Mkate 829
Mkoa, wilaya 830
mkono, mkono wa kuume, 831
mkuki 832
Mkutano, kukusanyika 833
Mkuu 834
Mkuu, Binti wa Mfalme 835
mkuyu 836
Mnara 837
mnyama 838
Mnyweshaji 839
moto 840
mpagao 841
Mpanda farasi 842
Mpatanishi 843
mpenzi 844
Mpiga mishale 845
Mrithi 846
Msamaha 847
mshiriki 848
Mshita 849
msimamizi 850
msingi, kuanzishwa 851

msonobari 852
Mtamba/Mfarika wa ng'ombe 853
Mtawala, watawala, tawala 854
mtego 855
mtenda uovu 856
Mtende 857
Mteserusi 858
mtini 859
mtumishi, mtumwa, utumwa 860
muamuzi, waamuzi 861
muda 862
muhuri, kutia muhuri 863
Mvua ya mawe 864
mwaka linapotumika 865
mwalimu,Mwalimu 866
mwamini 867
Mwananchi 868
Mwangamizi 869
mwenzi 870
mwerezi 871
mwezi 872
mwezi mpya 873
mwiba, mbaruti 874
mwizi, wezi, jambazi 875
mwokovu 876
Mzabibu 877
mzaliwa 878
mzawa wa kwanza 879
mzeituni 880
mzigo 881
nabii wa uongo 882
nafaka 883
Najisi 884
najisi, kunajisiwa 885
ndara 886
ndoto 887
Neno 888
Neno la kweli 889
ng'ombe 890
Ng'ombe, fahali, ndama, mifugo 891
Ngamia 892
Ngano 893
ngao 894
ngome, kimbilio 895
ngumu, ugumu, fanya - gumu 896
nguo ya gunia 897
Nguruwe 898
nguva 899
nguzo ya mlango 900
nguzo, safu 901
nia 902
Nira 903

njaa 904
njiwa, ninga 905
nuru 906
nyakuliwa, nyakuliwa pamoja 907
nyenyekea, kwa unyenyekevu 908
nyoka 909
Nyumba 910
nyumba ya ghala 911
nzige 912
Onyo 913
Pagani 914
panda, mpandaji, mmea 915
Pazia 916
Pembe, Mapembe 917
pepeta, chekecha 918
Pigo 919
Plau 920
Ponya, tibu 921
pukuta, pukuchua 922
Pumzika 923
punda, nyumbu 924
Ripoti 925
Rudi 926
rushwa 927
Rushwa 928
saa 929
Saa 930
Sadaka 931
Sadaka ya amani. 932
sadaka ya dhambi 933
sadaka ya hatia 934
sadaka ya kinywaji 935
sadaka ya kujitolea 936
Sadaka ya kuteketezwa 937
sadaka ya mlo 938
sadaka ya nafaka 939
sadaka ya ushirika 940
salfa 941
sanamu, waabudu sanamu 942
Sauti 943
Sehemu za juu 944
sela 945
sensa 946
shaba 947
shahidi wa uongo, shahidi aliyepotoka, ushuhuda wa uongo, taarifa ya ... 948
shahidi, Shahidi 949
shayiri 950
sheria, kanuni 951
Shimo 952
Shimo lisilo na mwisho 953
shingo ngumu, kiburi 954
Shinikizo la divai 955

Shoka 956
Shtaki, Mashtaka, Mshtaki 957
shtakio 958
Shujaa, askari 959
si mcha Mungu, siye na Mungu 960
si takatifu 961
si wa haki, 962
sifa, mashuhuri 963
siku 964
sikukuu 965
Silaha 966
simba 967
sio aminifu, kosa uaminifu 968
sio leta faida 969
siotahiriwa, kutotahiriwa 970
siri, ukweli uliyo fichika 971
stuli ya mguu 972
Suria 973
taa 974
taabu, mataabiko, taabika 975
tafakari 976
tafsiri, ufafanuzi 977
tafuta 978
tai 979
Taifa 980
Taji, kuvalisha taji 981
takatifu 982
takdiri, majaliwa, jaliwa 983
Talaka 984
tamaa 985
Tambua 986
tambua, tambuzi 987
tamka, tamko 988
tanuu 989
Tapanya, nyika 990
tarumbeta 991
tawanya, mtawanyiko 992
teketeza, uharibifu 993
Tembea 994
teseka, kuteseka 995
tetemeka 996
Thamani 997
theluji 998
thibitisha, uthibitisho 999
tia moyo, kutia moyo 1000
tia utumwani, katika kifungo 1001
tii, mtiifu, utiifu 1002
totii, mkaidi, kutotii 1003
tukuza 1004
tuma, kutuma nje, kutumwa 1005
Tumbo la uzazi 1006
tunda, kuzaa 1007

Tunga mimba 1008
ua, mahakama 1009
uadilifu 1010
uaguzi, mwaguzi, kutabiri, mtabiri 1011
Ubaguzi 1012
ubani 1013
Uchawi, mchawi 1014
uchawi, mchawi, uganga 1015
uchungu wa kuzaa 1016
udaku 1017
ufalme 1018
Ufalme 1019
ugomvi 1020
Uhalifu, mhalifu 1021
uhalifu, uasi 1022
ujasiri, jasiri 1023
ukoma, mkoma 1024
Ukoo 1025
ulimi 1026
ulizia 1027
Umba, Uumbaji, Muumbaji 1028
umbo, sanamu ya kuchonga, umbo la kuchonga, umbo la chuma 1029
Umri 1030
unyofu 1031
uongo, ukaidi, kuipotosha 1032
upanga 1033
upinde 1034
upole 1035
ushauri, mshauri 1036
ushuru 1037
uso 1038
Utaji 1039
Utawala, mtawala 1040
utukufu 1041
uvumba 1042
Uvumilivu 1043
uwezo 1044
Uyahudi, dini ya Kiyahudi 1045
uzao, kutokana na 1046
viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini 1047
viuno 1048
vumilia, uvumilivu 1049
Vumilia, uvumilivu 1050
Waasi, uasi. 1051
waheshima, heshima 1052
wanaume wasomi, mamajusi 1053
watoza ushuru 1054
watu wenye busara 1055
wavuvi 1056
Wazee 1057
Wazee wa ukoo 1058
weka wakfu, kuwekwa wakfu kwa 1059

wivu, tamani 1060
woga, kutishwa 1061
woga, kuogopesha 1062
yayuka, yayushwa 1063
Zabibu 1064
Zambarau 1065
Zawadi 1066
zinaa 1067
zingira, kuzingira 1068

Washiriki 1069
translationWords Washiriki 1069
unfoldingWord® Translation Academy Washiriki 1069

translationWords

Key Terms

Abudu

Ufafanuzi

"Kuabudu" ni kuheshimu, kusifu na kumtii mtu hasa Mungu.

- Neno hili lina maana ya kawaida ya kuinama kumnyenyekea mtu.
- Tunamwabudu Mungu tunapo muheshimu, kumsifu na kumtii yeye.
- Waisraeli walimwabudu Mungu kwa kutoa sadaka ya wanyama kwenye madhabahu.
- Watu wengine wanaabudu miungu ya uongo.

Adili, uadilifu

Ufafanuzi

Adili au uadilifu ni wema wa Mungu, haki, uaminifu na upendo. Kwa sababu Mungu ni wa adili hukemea dhambi.

- Maneno haya pia hutumika kumuelezea mtu anayemtii Mungu na mwenye maadili mema. Kwa sababu wote wametenda dhambi Mungu pekee ndiye mwenye adili.
- Mfano wa watu waliokuwa waadilifu kwenye Biblia walikuwa Nuhu, Ayubu, Abrahamu, Zakaria na Elizabeti.
- Watu wakimwamini Mungu awaokoe, Mungu anawasafisha na kuwafanya kuwa waadilifu katika uadilifu wa Yesu.

Agano

Ufafanuzi

Agano ni makubaliano kati ya pande mbili kuwa upande mmoja au zote unapaswa kutekeleza.

- Makubaliano haya yanaweza kuwa ya mmoja mmoja, kati ya makundi ya watu au kati ya Mungu na watu.
- Watu wanapoweka agano kati yao wanaahidi kufanya jambpo fulani ambalo wanapaswa wafanye.
- Mfano wa maagano ya wanadamu ni maagano ya ndoa, makubaliano ya biashara na mikataba kati ya nchi.
- Katika Biblia Mungu ameweka maagano mbalimbali na watu wake.
- Katika baadhi ya maagano Mungu aliahidi kutekeleza bila masharti yoyote. Kwa mfano Mungu alipoweka agano na mwanadamu kuwa hataiangamiza duinia kwa mafuriko.
- Katika maagano mengine Mungu ameahidi kutekeleza kama watu watamtii yeye.

Ahadi

Ufafanuzi

Ahadi ni hali ya kuahidi kufanya jambo fulani. Mtu anapokuahidi kitu inamaana yupo tayari kufanya jambo hilo.

- Biblia imeandika ahadi nyingi ambazo Mungu aliahidi watu wake.
- Ahadi ni sehemu muhimu ya makubaliano kama maagano.
- Ahadi mara nyingi huambatana na kiapo cha kuthibitisha kuwa itafanyika.

Aliye Juu

Ufafanuzi

Neno "Aliye Juu" ni cheo cha Mungu. kina husu ukuu wake au mamlaka.

- Maana ya hili neno ni sawa na "Ukuu"
- Neno "juu" katika hichi cheo halihusu urefu wa kimwili au umbali. Lina husu ukuu.

Aliyechaguliwa, chagua, watu waliochaguliwa, Aliyechaguliwa, Mteule

Ufafanuzi

Msemo, "wateule" una maana ya "waliochaguliwa" au "watu waliochaguliwa" na una maana ya wale ambao Mungu amewateua au chagua kuwa watu wake. "Aliyechaguliwa" au "Aliyechaguliwa na Mungu" ni jina ambalo lina maana ya Yesu, ambaye ni Masihi aliyechaguliwa.

Msemo "chagua" una maana ya kuchagua kitu au mtu au kuamua jambo. Mara kwa mara hutumika kumaanisha Mungu kuteua watu wawe wake na wamtumikie.

"Kuchaguliwa" ina maana ya "kuchaguliwa" au "kuteuliwa" kuwa au kufanya jambo.

Mungu alichagua watu kuwa wasafi, kutengwa kando na yeye kwa kusudi la kuzaa matunda mema ya kiroho. Hiyo ni sababu kwa nini wanaitwa "wateule" au "waliochaguliwa".

Msemo "aliyechaguliwa" hutumika mara nyingine katika Biblia kumaanisha baadhi ya watu kama Musa na Mfalme Daudi ambao Mungu aliwateua kama viongozi wa watu wake. Pia inatumika kumaanisha taifa la Israeli kama watu waliochaguliwa na Mungu.

Msemo "wateule" ni msemo wa zamani ambao humaanisha "waliochaguliwa" au "watu waliochaguliwa". Msemo huu katika lugha asili ni wingi inapomaanisha waumini wa Kristo.

Katika tafsiri za Biblia ya Kingereza za zamani, msemo "mteule" unatumika pote katika Agano la Kale na Jipya kutafsiri neno kwa ajili ya "waliochaguliwa". Tafsiri zaidi za kisasa hutumia "mteule" katika Agano Jipya pekee, kumaanisha watu ambao wameokolewa na Mungu kupitia imani kwa Yesu. Kwingineko katika Biblia, wanatafsiri neno hili kwa uwazi zaidi kama "waliochaguliwa".

Mapendekezo ya Tafsiri

Ni bora kutafsiri "mteule" kwa neno au msemo ambao una maana ya "waliochaguliwa" au "watu waliochaguliwa". Hizi zinaweza kutafsiriwa kama "watu ambao Mungu amechagua" au "wale ambao Mungu ameteua kuwa watu wake".

Msemo, "ambao wamechaguliwa" unaweza kutafsiriwa kama "ambao wameteuliwa" au "ambao waliteuliwa" au "ambao Mungu amewachagua".

"Ninakuchagua" inaweza kutafsiriwa kama, "ninakuteua" au "ninakuchagua".

Kwa kulinganisha na Yesu, "Aliyeteuliwa" inaweza pia kutafsiriwa kama, "Aliyechaguliwa na Mungu" au "Masihi aliyeteuliwa mahsusi na Mungu" au "Yule ambaye Mungu alimteua"

Amina, kweli

Ufafanuzi

Neno "Amina" hutumika kusisitiza au kuweka mkazo jambo ambalo mtu amesema. Mara nyingi hutumika mwisho wa sala. Mara nyingine hutafsiriwa kama "kweli."

- Ikitumika mwisho wa sala, "amina" inaonesha kukubaliana na maombi au kuelezea shauku ya kutimizwa kwa maombi yale.
- Katika mafundisho yake, Yesu alitumia neno "Amina" kusisitiza ukweli wa alichokisema. Mara nyinyi aliunganisha kwa kutumia " nawaambia ninyi" katika kutambulisha mafundisho mengine ambayo yaliendana na mafundisho yaliyopita.
- Maana nyingine ya "kweli" yaweza kutafsiriwa kama "hakika" na pia hutumika kusisitiza jambo ambalo msemaji analisema.

amri, kuamuru

Ufafanuzi

Kuamuru ni kutoa amri kwa mtu afanye jambo fulani. Amri ni jambo ambalo mtu ameamriwa afanye.

- Japokuwa maneno haya yana maana inayofanana amri mara nyingi ni inamaanisha amri za Mungu ambazo ni "amri kumi."
- Amri yaweza kuwa nzuri chanya kama "waheshimu wazazi wako" au hasi kama "usiibe."
- Kuwa na amri inamaanisha "kuamuru" kitu au mtu.

Batiza, ubatizo

Ufafanuzi

Katika Agano Jipya, maneno "batiza" na "ubatizo" kwa kawaida utaratibu wa kuoshwa kwa Mkiristo kwa kutumia maji kuonesha kwamba ameoshwa kutoka katika dhambi na ameungana na Kristo.

- Mbali na ubatizo wa maji, Biblia inazungumzia "kubatizwa kwa Roho Mtakatifu" na "kubatizwa kwa moto."
- Neno "ubatizo" katika Biblia limetumika pia kuonesha hali ya kupitia matiso makubwa.

Maono ya Kutafasiri

- Wakristo wanamaoni tofauti jinsi mtu anavyopaswa kubatizwa kwa maji. Pengine inafaa zaidi kutafasiri neno hili kwa njia ya jumla inayoruhusu njia mbalimbali ya kutumia maji.
- Kwa kutegemea mazingira, neno "batiza" laweza kutafasiriwa kama "kutakasa," "kumimina juu, "kuzamisha"

baya, ovu, uovu

Ufafanuzi

Msemo "baya" na "uovu" yote ina maana ya chochote ambacho kinapingana na tabia takatifu na mapenzi ya Mungu.

Wakati "ubaya" unaweza kuelezea tabia ya mtu, "ovu" unaweza kumaanisha zaidi ya tabia ya mtu. Hata hivyo, misemo yote inafanana maana.

Msemo "uovu" una maana ya hali ambayo watu hufanya maovu.

Matokeo ya uovu yanaonywesha kwa uwazi kwa jinsi watu wanavyotenda vibaya wengine kwa kuwaua, kuiba, kusengenya au kuwa katili na kutokuwa mwema.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, misemo "uovu" na "ovu" inaweza kutafsiriwa kama "ubaya" au "dhambi" au "kinyume na maadili".

Njia zingine za kutafsiri hii zinaweza kujumuisha "isiyo nzuri" au "sio takatifu" au "sio adilifu".

Hakikisha maneno au misemo ambayo inatumika kutafsiri misemo hii kutosha muktadha ambayo ni kawaida katika lugha husika.

Bila mawaa

Ufafanuzi

Neno "bila mawaa" kwa kawaida linamaanisha "bila lawama". Linatumika kumtaja mtu anayemtii Mungu kwa moyo wake wote, lakini haimaanisha kwamba hana dhambi.

- Ibrahimu na Nuhu walihesabiwa kutokuwa na lawama mbele za Mungu.
- Mtu mwenye heshima ya kuwa "bila lawama" anaenenda kwa namna inayomweshimu Mungu.
- Kwa mjibu wa msitari mmoja, mtu asiye na lawama ni "yule anayemcha Mungu na kujiepusha na uovu."

Maoni ya Ufasiri

- Hii pia yaweza kutafasiriwa kama, "asiye na kasoro katika mwenendo wake" au "mwenye kumtii Mungu kikamilifu" au "kujiepusha na dhambi" au "kujilinda na uovu.

Binti Sayuni

Ufafanuzi

"Binti Sayuni" ni njia ya kitamathali inayomaanisha watu wa Israeli. Inatumika haswa katika unabii.

Katika Agano la Kale, "Sayuni" hutumika sana kama jina jingine la mji wa Yerusalemu.

"Sayuni" na "Yerusalemu" zote zina maana ya Israeli.

Msemo "Binti" ni msemo wa ubembelezi au mapenzi. Ni sitiari ya uvumilivu na utunzaji ambao Mungu anao kwa watu wake.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia za kutafsiri hili yaweza kuwa, "binti yangu wa Israeli, kutoka Sayuni" au "watu kutoka Sayuni, ambao ni kama binti kwangu" au "Sayuni, watu wangu wapendwa Israeli".

Ni vyema kubaki na msemo "Sayuni" katika usemi huu kwa maana unatumika mara nyingi katika Biblia. Maandishi yanaweza kuwekwa katika tafsiri kuelezea maana yake ya kitamathali na matumizi ya kinabii.

Ni bora kukaa na msemo "Binti" katika tafsiri ya usemi huu, ikiwa inaeleweka kwa sahihi.

Busara, hekima

Ufafanuzi

Busara inamuelezea mtu anayeelewa jambo la haki na mambo ya maadili na akayafanya. Hekima ni uelewa na kutenda yaliyo sahihi na maadili ya haki.

- Kuwa na busara inajumuisha uwezo wa kufanya maamuzi mazuri hasa kuchagua kufanya yanayompendeza Mungu.
- Katika Biblia "busara za dunia" inamaanisha kitu ambacho watu wa dunia wanafikiri ni burasa lakini ni upuuzi.
- Watu huwa na busara wanapomsikiliza Mungu na kunyeyekea kutii mapenzi yake.
- Mtu mwenye busara ataonesha matunda ya roho mtakatifu kwenye maisha yake kama furaha, upendo na uvumilivu.

Bwana wa Majeshi, Mungu wa majeshi, Majeshi

Ufafanuzi

Bwana wa majeshi ay Mungu wa majeshi ni vyeo vinavyoelezea mamlaka ya Mungu juu ya malaika maelfu wanaomtii yeye.

- Majeshi linaelezea idadi kubwa ya vitu kama vile jeshi au idadi kubwa ya nyota. Pia yaweza kuwa na maana ya viumbe vyote vya kiroho ikiwemo roho wachafu.
- Majeshi ya mbinguni ni nyota zote, sayari na vitu vingine vilivyoko mbinguni.
- Katika agano jipya Bwana wa majeshi inamaanisha "Yaweh wa majeshi" lakini haiwezi kutafsiriwa hivyo kwa sababu neno la Kiebrania Yaweh halijatumika kwenye agano jipya.

Bwana Yahwe, Yahwe Mungu

Ufafanuzi

Katika Agano la Kale, "Bwana Yahwe" inatumika mara kwa mara kumaanisha Mungu mmoja wa kweli.

Neno "Bwana" ni cheo cha Mungu na "Yahwe" ni jina la Mungu mwenyewe. "Yahwe" mara nyingi huunganishwa na neno "Mungu" kuunda "Yahwe Mungu."

bwana, mkuu

Ufafanuzi

Neno "bwana" linamaanisha mtu anayemiliki na mwenye mamlaka juu ya watu wengine.

Neno hili wakati mwingine linatafsiriwa kama "mkuu" wakati wakumuita Yesu au wakati wakumaanisha mtu anayemiliki watumwa.

chakula cha Bwana

Ufafanuzi

Msemo "Chakula cha Bwana" unatumika na mtume Paulo kumaanisha mlo wa Pasaka ambao Yesu alikula na wanafunzi wake usiku alipokamatwa na viongozi wa Kiyahudi.

Katika mlo huu, Yesu aliuvunja mkate wa Pasaka katika vipande na kuuita mwili wake ambao punde utapigwa na kuuliwa pia. Aliita kikombe cha divai damu yake, ambayo itamwagwa hapo punde atakapokufa kama sadaka ya dhambi. Yesu aliamuru kila mara wafuasi wake wanapokula mlo huu pamoja, wanapaswa kukumbuka kifo chake na ufufuo. Katika barua yake kwa Wakorintho, mtume Paulo aliendeleza kuimarisha zaidi chakula cha Bwana kama zoezi la mara kwa mara la waumini wa Yesu. Makanisa siku hizi husema "ushirika" kumaanisha chakula cha Bwana. Usemi "Meza ya Bwana" hutumika wakati mwingine.

Chukizo, mbaya

Ufafanuzi

Neno "chukizo" hutumika kuelezea jambo linalosababisha karahaau chuki iliyokithiri. Wamisri waliwaona Waebrania kama "chukizo." Hii ina maana kuwa Wamisri waliwachukia Waebrania na hawakutaka kushirikiana nao au kuwa karibu nao. Vitu ambavyo Biblia imeviona kama "Chukizo kwa Yahweh" ni; uongo, kujivuna, kafara za binadamu, kuua na dhambi za zinaa kama uzinzi na matendo ya zinaa kinyume na maumbile. Katika kuwafundisha wanafunzi wake kuhusu siku za mwisho, Yesu anarejea unabii wa nabii Danieli kuhusu "chukizo la uharibifu" kwamba itakuwa kama uasi dhidi ya Mungu, Kuchafua sehemu yake ya kuabudia.

damu

Ufafanuzi

Neno "damu" linamaanisha kimiminika chekundu kinachotoka katika ngozi ya mtu panapokuwa na jeraha au kidonda. Damu inaleta viini lishe vya uhai katika mwili wote wa mtu.

- Damu inaashiria uhai na inapomwagwa, inaashiria kifo.
- Watu walipotoa sadaka kwa Mungu, walimwua mnyama na kumimina damu yake juu ya madhabahu. Hii inaashiria kutolewa kwa uhai wa mnyama kulipa dhambi za watu.
- Kupitia kifo chake msalabani, Damu ya Yesu hutakasa watu kutokana na dhambi zao na kulipa kwa ajili ya adhabu wanayostahili kwa ajili ya dhambi zao.
- Kifungu "mwili na damu" kinarejerea wanadamu.
- Kifungu "mwili wake na damu yake" inarejerea kwa watu wanaohusiana kibaolojia.

Maoni ya Kutafasiri

- Neno hili litumika kwa kulingana na neno lifaalo katika lugha lengwa.
- Kielezi "mwili na damu" chaweza kutafasiriwa kama "watu" au "wanadamu".
- Kwa kutegemea mazingira, kifungu "mwili wangu na damu yangu mwenyewe" yaweza kutafasiriwa kama "familia yangu" au "ndugu zangu" au "watu wangu."
- Ikiwa kuna kionyeshi katika lugha lengwa kinachotumika kwa maana hii, kifungu hicho kitumike kutafasiri "mwili na damu"

dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

Ufafanuzi

Neno "dhambi" la husu matendo, mawazo, na maneno yaliyo kinyume dhidi ya mapenzi ya Mungu na Sheria. Dhambi yaweza maanisha kutofanya kitu Mungu alicho tuambia tufanye.

- Dhambi ya jumuisha chochote tunacho fanya kisicho mtii au mpendeza Mungu, ata vitu watu wasivyo vijua.
- Mawazo na matendo yanayo kosea mapenzi ya Mungu yanaitwa "yenye dhambi"
- Kwasababu Adamu alitenda dhambi, wanadamu wote wanazaliwa na hasili ya dhambi inayo watawala.
- "mwenye dhambi" ni mtu anaye tenda dhambi, hivyo kila mwanadamu ni mwenye dhambi.
- Wakati mwingine neno "mwenye dhambi" lilitumika na watu wa dini kama Mafarisayo kueleza watu wasio shika sheria.

Dhamira

Ufafanuzi

Dhamira ni sehemu ya fikra za mwanadamu ambazo Mungu anamfanya atambue kuwa anafanya dhambi.

- Mungu amewapa watu dhamira ili awasaidie wafahamu tofauti kati ya mema na mabaya.
- Mtu anayemtii Mungu ana dhamira safi.
- Mtu akiwa na dhamira safi inamaana kuwa hafichi dhambi yoyote.
- Mtu anayedharau dhamira yake na hajisikii kuhukumiwa anapofanya dhambi inamaana kuwa dhamira yake haishituki kwa mabaya.

Dunia, kidunia

Ufafanuzi

Dunia ni sehemu ya ulimwengu ambapo watu wanaishi ndani yake. Kidunia inaelezea maadili na tabia mbaya za watu wanaoishi kwenye hii dunia.

- Dunia inajumuisha mbingu, nchi na vyote vilivyopo ndani yake.
- Katika sehemu nyingi "dunia" inamanisha watu wa duniani.
- Mara nyingine inaelezea kuwa watu waovu wa duniani au watu wasiomtii Mungu.
- Mitumi waliotumia "dunia" walielezea tabia za ubinafsi za watu wanaoishi kwenye dunia hii.
- Watu au vitu wenye tabia hizi waliitwa wa kidunia.

fadhila, yenye kufaa, upendeleo

Ufafanuzi

Msemo "fadhila" una maana ya kufanya jambo kumnufaisha mtu ambaye anachukuliwa ki chanya. Kitu ambacho "kinafaa" ni chanya, kinakubalika, au kina manufaa.

Msemo "upendeleo" ina maana ya kutenda kwa upendeleo kwa baadhi ya watu lakini sio wengine kuonyeshwa kwa watu ambao ni matajiri au wanafikiriwa.

Yesu alikua "kwa fadhila za" Mungu na wanadamu. Hii ina maana walimkubali silika na tabia yake .

Msemo "kupata fadhila" ina maana ya kwamba mtu anakubalika na mtu mwingine.

Mfalme anapoonyesha upendeleo kwa mtu, mara nyingi humaanisha anakubali maombi ya huyo mtu na kumpatia.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri msemo "fadhila" zinawvza kujumuisha "baraka" au "faida".

"Mwaka wa baraka wa Yahwe" unaweza kutafsiriwa kama "mwaka

Farisayo.

Ufafanuzi

Mafarisayo walikuwa watu wa muhimu sana, kundi la watu lenye nguvula dini ya Kiyahudi katika nyakati za Yesu.

- Wengi wao walikuwa katika daraja la kati la wafanyabiashara na wengine walikuwa makuhani.
- Katika viongozi wote wa Kiyahudi Mafarisayo walikuwa wakitii kwa nguvu sheria ya Musa na sheria nyingine za Kiyahudi na tamaduni.
- Walikuwa makini sana katika kuwatenga Wayahudi toka kwenye ushawishi wa Mataifa yanayowazunguka. Neno "Farisayo" linatokana na neno "kutenganisha"
- Mafarisayo wanaamini kuna maisha baada ya kifo pia wanaamini kuwepo kwa malaika na viumbe wengine wa kiroho.
- Mafarisayo na Masadukayo walimpinga Yesu na kanisa la kwanza.

Fidia

Ufafanuzi

Fidia ni kiasi cha pesa au malipo mengine yanayohitajika kwa ajili ya kumuachia mtu aliyefungwa.

- "Kutoa fidia" ni kufanya malipo au kutoa kitu ili kumkomboa mtu aliyepo kifungoni au utumwani.
- Yesu alikubali kuuawa kama fidia ya kuwaweka huru wenye dhambi toka kwenye utumwa wa dhambi. Hiki kitendo cha Mungu kuwanunua watu wake ki kitendo cha ukombozi.

funga

Ufafanuzi

Neno "funga" linamaanisha kukaza kitu kwa usalama. Kitu kilichofungwa au kuunganishwa pamoja kinaitwa "muungano". Neno "kufunga" ni sehemu ya neno hili katika wakati uliopita.

- "Kufungwa" inamaanisha kufunga au kuzonga katika kitu kingine.
- Katika hali ya tamathari, mtu anaweza "kufungwa" katika nadhiri, kumaanisha "analazimika kutimiza" alichokiahidi.
- Neno "vifungo" linamaanisha chochote kinachofunga, "weka pamoja, au kumweka mtu gerezani. Kwa kawaida inamaanisha vifungo vya kimwili, pingu au kamba zinazomfanya mtu asiwe huru kuondoka alipo.
- Katika nyakati za Biblia, vifungo kama vile kamba au minyororo ilitumika kumfunga mfungwa katika ukuta au chini ya jiwe la gereza.
- Neno "funga" laweza pia kutumika kuzungumzia kufunga kidonda kwa kitambaa ili kukisaidia kupona.
- Mfu aweza "kuzongwa" kwa sanda katika maandalio ya mazishi.
- Neno "kifungo" hutumika kitamathari kurejerea kitu fulani, kama vile dhambi, inayomwongoza au kumfanya mtumwa.
- Kifungu chaweza kuwa uhusiano wa karibu kati ya watu ambao wanasaidiana kihisia, kiroho na kimwili. Hii inatumika katika kifungo cha ndoa.
- Kwa mfano, mwanamke na mwanamme "wamefunwa" au "kuunganishwa. Ni kifungo ambacho Mungu hapendi kivunjike.

Maoni ya Tafasiri

Neno "funga" laweza pia kutafasiriwa kama "kaza" au "zungushia"

ghadhabu, hasira

Ufafanuzi

Ghadabu ni hasira kali ambayo mara nyingine hudumu kwa mda mrefu. Hii maranyingi huelezea hukumu ya Mungu ya haki na adhabu ya watu walioasi dhidi yake.

- Katika Biblia "ghadhabu" ni hasira ya Mungu juu ya wao wanaomtenda dhambi.
- Ghadhabu ya Mungu ni hukumu na adhabu ya dhambi.
- Ghadhabu ya Mungu ni adhabu ya haki kwa wale wasiotubu dhambi zao.

habari njema, injili

Ufafanuzi

Msemo "injili" una maana ya "habari njema" na una maana ya ujumbe au tangazo ambalo linawaambia watu jambo ambalo lina manufaa kwako na kuwapa furaha.

Katika Biblia, msemo huu humaanisha ujumbe kuhusu wokovu wa Mungu kwa watu kupitia sadaka ya Yesu msalabani.

Katika Biblia nyingi za Kiingereza, "habari njema" mara nyingi hutafsiriwa kama "injili" na pia hutumika katika misemo kama vile "injili ya Yesu Kristo" au "injili ya Mungu" na "injili ya ufalme".

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia tofauti za kutafsiri msemo huu zinaweza kujumuisha "jumbe mzuri" au "tangazo zuri" au "ujumbe wa Mungu wa wokovu" au "mambo mazuri Mungu anayofundisha kuhusu Yesu".

Kulingana na muktadha, njia za kutafsiri msemo "habari njema ya" inaweza kujumuisha "ujumbe/havbari njema" au "ujumbe mzuri kutoka" au "mambo mazuri Mungu husema juu ya" au "kile Mungu anasema kuhusu jinsi anavyookoa watu".

Haki ya uzaliwa

Ufafanuzi

Neno "haki ya uzaliwa" inamaanisha heshima katika Biblia, jina la familia, na mali iliyokuwa ikitolewa kwa mzaliwa wa kwanza katika familia.

- Haki ya mzaliwa wa kwanza ilijumuisha mara mbili katika urithi wa baba.
- Mwana wa kwanza wa mfalme kwa kawaida alipewa haki ya uzaliwa ya kurithi baada ya kifo cha baba yake.
- Esau aliuza haki ya uzaliwa kwa Yakobo mdogo wake, kwa sababu hii, Yakobo alirithi baraka ya mzaliwa wa kwanza badala ya Esau.
- Haki ya kuzaliwa pia ilihusisha kuhesabiwa kwa vizazi vya familia kupitia mzaliwa wa kwanza.

Maoni ya Kutafasiri.

- Njia iwezekanayo kutafasiri "haki ya kuzaliwa" ni pamoja na "haki na utajiri wa mzaliwa wa kwanza" au "heshima ya familia" au "faida na urithi wa mzaliwa wa kwanza."

haki, adilifu

Ufafanuzi

Maneno haya yanamaanisha kuwatendea watu vyema kulingana na sheria za Mungu. Sheria za binadamu zinazo onesha kiwango cha Mungu cha tabia sawa kwa watu wengine.

Kuwa wa "haki" ni kutenda ya haki na mema kwa mtu mwingine. Pia inaashiria uaminifu na msimamo kufanya kilicho adilifu machoni pa Mungu. Kutenda kwa "haki" inamaanisha kuwatendea watu kwa njia iliyo sawa, nzuri na ya kufaa kulingana na sheria za Mungu. Kupokea "haki" inamaanisha kutendewa vyema chini ya sheria, aidha kulindwa kwa sheria au kuadhibiwa kwa kuvunja sheria. Wakati mwingine neno "haki" lina maana pana ya "utakatifu"au "kufuata sheria za Mungu."

hatia, mwenye hatia

Ufafanuzi

Msemo "hatia" una maana ya ukweli wa kufanya dhambi au kutenda kosa.

Kuwa na "hatia" ina maana ya kuwa umefanya kitu kiouvu kimaadili, yaani, kutomtii Mungu.

Kinyume cha "mwenye hatia" ni "asiye na hatia".

Mapendekezo ya Tafsiri

Baadhi ya lugha zinaweza kutafsiri "hatia" kama "uzito wa dhambi" au "hesabu ya dhambi".

Njia za kutafsiri "kuwa na hatia" inaweza kujumuisha neno au msemo ambayo ina maana ya "kuwa katika kosa" au "kuwa umefanya jambo ovu kimaadili" au "kuwa umefanya dhambi".

hekalu

Ufafanuzi

Hekalu lilikuwa ni jengo lililo zungukwa na kuta za nyuani ambapo Waisraeli walikuja kuombaa na kutoa dhabihu kwa Mungu. Lilikuwa Mlima Moria katika mji wa Yerusalemu.

- Mara nyingi neno "hekalu" lina husu jengo zima, pamoja na nyuani iliyo zunguka jengo lote. Wakati mwingine lina husu tu jengo.
- Jengo la hekalu lilikuwa na vyumba viwili, Pa Takatifu na Pa Takatifu pa Pa Takatifu.
- Mungu alitaja hekalu kama sehemu yake ya kuishi.
- Wakati wa utawala wa Mfalme Sulemani alijenga Hekalu, ambalo lilikuwa sehemu ya kudumu ya kuabudu Yerusalemu.
- Katika Agano Jipya, neno "hakalu la Roho Mtakatifu" linatumika kuelezea waamini wa Yeu, kwasababu ya Roho Mtakatifu kuishi ndani yao.

heshima, kuheshimu

Ufafanuzi

Istilahi 'heshima' na 'kuheshimu' hurejelea kitendo cha kumpa mtu heshima au kumstahi mtu. Heshima mara kwa mara hutolewa kwa mtu mwenye hadhi ya juu na umuhimu wa juu kama vile mfalme au Mungu. Mungu pia huwaagiza Wakristo wote kuwaheshimu watu wengine, lakini si kutafuta heshima zao wenyewe. Watoto wameagizwa kuwatii wazazi wao na kuwatii. Maneno kama 'heshima' na 'utukufu' ni maneno yanayoenda kwa pamoja hasa yanapomrejelea Yesu. Heshima kwa Mungu inajumuisha kumshukuru na kumsifu Mungu, na kuonesha heshima kwa kumtii Mungu na kuishi katika njia inayoonesha kuwa Mungu ni Mkuu.

Mapendekezo Njia nyingine za kutafsiri neno 'heshima' linajumuisha 'staha' Neno 'kuheshimu' laweza kutafsiriwa kama 'kuonesha heshima maalumu kwa au kuonesha mtu thamani ya juu.

hukumu

Ufafanuzi

Neno "hukumu" mara nyingi humaanisha kufanya maamuzi kama jambo liko sawa kimaadili au kama haliko sawa.

"Hukumu ya Mungu" mara nyingi humaanisha uamuzi wake kulaani kitu au mtu muovu. Hukumu ya Mungu mara nyingi huhusisha kuwaadhibu watu kwa dhambi zao. Neno "hukumu" inaweza pia kumaanisha "kulaani." Mungu anawaagiza watu wake kutowahukumu wengine kwa naamna hii. Maana nyingine ni "uamuzi kati ya" au "kuhukumu kati ya", yaani kuchagua ni mtu gani yuko sahihi katika ugomvi kati yao. Katika mazingira mengine, "hukumu" za Mungu ni yale aliyeamua ni mema na yenye haki. Zinafanana na amri, sheria na maagizo yake. "Hukumu" inaweza kumaanisha uwezo wa busara wa kufanya maamuzi. Mtu anayekosa "hukumu" hana hekima kufanya maamuzi ya busara.

Huruma

Ufafanuzi

Huruma ni hisia za kujali wengine hasa wanaoteseka. Pia huruma ni kujali wengine na kuwasaidia.

- Huruma pia inajumuisha kuwajali wenye uhitaji na kuchukua hatua ya kuwasaidia.
- Biblia inasema Mungu ni wa huruma, ana upendo na rehema tele.
- Katika barua ya Paulo kwa Wakolosai anawaambia "wajivike huruma." Anawaagiza wawajali watu na wawasaidie wenye uhitaji.

imani

Ufafanuzi

Kwa ujumla, msemo "imani" una maana ya imani, au matumaini ndani ya mtu au jambo.

"Kuwa na imani" na mtu ni kuamini ya kwamba kile anachosema na kufanya ni kweli na kuaminika.

"Kuwa na imani na Yesu" ina maana ya kuamini mafundisho yote ya Mungu kuhusu Yesu. Ina maana haswa ya kwamba watu wanamuamini Yesu na sadaka yake kuwasafisha kutoka kwa dhambi zao na kuwakomboa kutoka na adhabu wanayostahili kwa sababu ya dhambi yao.

Imani ya kweli kwa Yesu itamsababisha mtu kuzaa matunda mazuri ya kiroho au tabia kwa sababu ya Roho Mtakatifu anayeishi ndani yake.

Mara kwa mara "imani" kwa ujumla ina maana ya mafundisho yote kuhusu Yesu, yaani kama msemo, "ukweli wa imani".

Katika muktadha kama wa "tunza imani" au "telekeza imani", msemo "imani" una maana ya hali ya kuamini mafundisho yote kuhusu Yesu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika baadhi ya muktadha, "imani" inaweza kutafsiriwa kama "imani" au "hatia" au "kujiamini" au "kuamini".

Kwa baadhi ya lugha misemo hii inaweza kutafsiriwa kutumia aina za kitenzi cha "imani".

imani, aminifu,

Ufafanuzi

Neno "imani" la eleza kuamini kwamba kitu au mtu ni wa kweli au tegemeo. Mtu "mwaminifu" na weza kuwa tegemevu kufanya kitu na kusema kilicho sawa na kweli.

- Imani ni ina maana ya karibu na imani ya Mungu. Kama tuna mwamini mtu, tuna imani kwamba mtu huyo atafanya alicho ahidi.
- Kuwa na imani kwa mtu pia ina maana ya kumtegemea huyo mtu.
- Kumuamini Yesu ina maana ya kukubali kuwa yeye ni Mungu na kwamba alikufa kwenye msalaba kulipa dhambi zetu, na kumtegemea kutuokoa.
- "msemo aminifu" ni kitu kilicho semwa na kinaweza hesabiwa kuwa kweli.

ingia bila ruhusa

Ufafanuzi

"Ingia bila ruhusa" ina maana ya kuvunja sheria au kukosea haki za mtu mwingine.

- Ingia bila ruhusa ni kosa la kijamii au la kisheria au dhambi iliyo tendwa dhidi ya mwingine.
- Huu msemo una maana ya "dhambi," haswa kwa kumkosea Mungu.
- Dhambi zote ni kosa kwa Mungu

ishara, kithibitisho, ukumbusho

Ufafanuzi

Ishara ni kitu, tukio, au kitendo kinacho wasilisha maana maalumu.

- Ishara zinaweza kuwa kumbusho cha kitu kilicho ahaidiwa.
- Upinde wa mvua Mungu aliyo uumba kwenye anga ulikuwa ni ishara ya kuwa kumbusha watu kwamba hataharibu maisha ya watu kwa gharika.
- Mungu aliamuru Waisraeli kutairi wana wao kama ishara ya agano lake kwao.
- Ishara zinaweza dhihirisha au kuelekeza kwa kitu.
- Malaika aliwambia wachungaji ishara itakayo wasaidia wao mtoto yupi Bethilehemu ndiye mzaliwa Mesiya mpaya.
- Yuda alimbusu Yesu kama ishara kwa viongozi wa kidini kwamba Yesu ndiye wamkamate.
- Ishara yaweza thibitisha kwamba kitu ni kweli.
- Miujiza iliyo fanywa na manabii na mitume ilikuwa ishara iliyo thibitisha walikuwa wanazungumza ujumbe wa Mungu.
- Miujiza Yesu aliyo tenda ilikuwa ishara kuwa yeye ndiye Mesiya.

Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

Ufafanuzi

Neno "Israeli" ni jina ambalo Mungu alimpa Yakobo. Linamaanisha, "anashindana na Mungu."

Uzao wa Yakobo walijulikana kama "watu wa Israeli," "taifa la Israeli" au "Waisraeli." Mungu aliunda agano lake na watu wa Israeli. Walikuwa watu wake aliowachagua. Taifa la Israeli liliundwa na makabila kumi na mbili. Mara baada ya mfalme Sulemani kufa, Israeli iligawanyika katika falme mbili: ufalme wa kusini, uliitwa "Yuda" na ufalme wa kaskazini, uliitwa "Israeli."

Jehanamu, ziwa la moto

Ufafanuzi

Jehanamu ni sehemu ya mwisho iliyo na maumivu na mateso yasiyokoma, mahali ambapo Mungu atamhukumu kila mmoja anayemwasi Yeye na kuukataa mpango wake wa kuwaokoa kupitia kwa sadaka ya Yesu. Pia inarejelewa kama 'ziwa la moto. Jehanamu au Kuzimu kunatajwa kama sehemu ya moto na mateso makali. Shetani na roho chafu zinazomfuata zitatupwa katika Jehanamu kwa ajli ya hukumu ya milele. Watu wasioamini sadaka ya Yesu kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, na wasiomtumaini Yeye, watahukumiwa Jehanamu milele

Mapendekezo ya tafsiri Maneno haya yanapaswa kutafsiriwa tofauti tofuauti kwasababu yanatokea tofauti katika muktadaha tofauti. Katika baadhi ya lugha haziwezi kutumia neno 'ziwa' kwa sababu kwao ziwa ni 'maji' Neno Jehanamu laweza kutafsiriwa kama 'sehemu ya mateso au sehemu yenye giza na maumivu' Maneno 'ziwa la moto' yanaweza pia kutafsiriwa kama 'bahari ya moto' au 'moto mkubwa.'

Jemadari

Ufafanuzi

Jemadari ni afisa wa jeshi la Rumi aliyekuwa na kundi la askari 100 juni ya amri yake.

- Hii pia inaweza kutafsiriwa kama "kiongozi wa watu mia" au "kiongozi wa jeshi."
- Jemadari mmoja wa Rumi alikwenda kwa Yesu akamwomba amponye mtumishi wake.
- Jemadari aliyekuwa akihusika kumsulubisha Yesu alishangazwa kwa namna ambavyo Yesu alikufa.
- Mungu alimtuma jemadari kwa Petro ili Petro amuelezee habari njema juu ya Yesu.

jina

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "jina" linatumika kwa mifano kadhaa.

- Katika muktadha kadhaa, "jina" la weza eleza tabia ya mtu, kama, "tujifanyie jina letu"
- Neno "jina" pia laweza husu kumbukumbu ya kitu. Kwa mfano, "katilia majina ya sanamu" ina maana kuharibu hizo sanamu ili zisikumbukwe au kuabudiwa.
- Kuzungumza "katika jina la Mungu" ina maana ya kuongea kwa nguvu zake na mamlaka, au kama mwakilishi.
- "Jina" la mtu laweza husu mtu wote, kama "hakuna jina lingine chini ya jua ambalo twapaswa kuokolewa."

Jiwe la pembeni

Ufafanuzi

"Jiwe la pembeni" ni jiwe kubwa mabalo limekatwa na kuwekwa katika kona ya msingi wa jengo.

- Mawe yote ya jengo hupimwa na kuwekwa kutokana na jiwe la pembeni.
- Ni la muhimu sana kwa uwezo na ustahimili wa jengo zima.
- Katika agano jipya kusanyiko la waamini linafananishwa na jengo ambalo Yesu Kristo ndiye jiwe la pembeni.
- Katika namna hiyo hiyo ambayo jiwe la pembeni linashikilia na kuweka msingi wa jengo zima hivyo Yesu Kristo ni jiwe la pembeni ambalo waamini wanajitegemeza kwake.

jiwe, kupiga jiwe

Ufafanuzi

Jiwe ni mwamba mdogo. Neno "kupiga jiwe" la husu kurusha mawe na majabali makubwa kwa mtu kuweza kumuua.

- Wakati wa Kale, kupiga mawe ilikuwa namna iliyo zoeleka ya kuua watu kama adhabu kwa makosa waliyo fanya.
- Mungu aliamuru viongozi wa Israeli kupiga mawe watu kwa dhambi kadhaa, kama uasherati.
- Agano Jipya ina eleza wakati Yesu alipo samehe mwanamke aliya kamatwa katika uasherati na kuzuia watu kumtupia mawe.

Kanisa

Ufafanuzi

Katika agano jipya kanisa ni kundi la watu wanaomwamini Yesu wanaokutana na kuomba pamoja na kusikiliza mafundisho ya Mungu.

- Yaweza kuwa na maana ya watu walioitwa kukutana pamoja kwa ajili ya jambo la muhimu.
- Neno hili linapotumika linamaanisha waamini wote popote ni mwili wa Kristo, Baadhi ya Biblia zimeandika kwa kuanza na herufi kubwa ("Kanisa") Kutofautisha na kanisa la kawaida.
- Mara nyingine waamini wa mji fulani hukutana katika nyumba ya mtu. Makanisa haya yalipewa majina ya miji mfano "Kanisa la Efeso."
- Katika Biblia kanisa halimaanishi jengo.

katika Kristo, katika Yesu, katika Bwana, katika yeye

Ufafanuzi

Usemi "katika Kristo" na maneno ya kukaribiana yanamaanisha hali ya kuwa na uhusiano na Yesu Kristo kwa imani katika yeye.

Maneno mengine ya kukaribiana ni pamoja na, "katika Kristo Yesu, katika Yesu Kristo, katika Bwana Yesu, katika Bwana Yesu Kristo." Maana zinazowezekana kwa ajili ya maneno "katika Kristo" yanaweza kuwa pamoja na, "kwa sababu wewe ni wa Kristo" au "katika uhusiano ulionao na Kristo" au "kutokana na imani yako katika Kristo." Maneno haya ya kukaribiana yote yana maana sawa ya kuwa katika hali ya kumuamini Yesu na kuwa mwanafuzi wake. Noti: Wakati mwingine neno "katika" lina paswa kuwa na kitenzi. Kwa mfano, "gawana katika Kristo" inamaana "kugawana katika" faida zinazokuja kwa kumjua kristo. "Kusifu katika" Kristo inamaana kuwa na furaha na kutoa sifa kwa Mungu ambavyo Yesu alivyo na alichofanya. "Kuamini katika" Kristo inamaanisha kumuamini yeye kama Mwokozi na kumjua.

kazi, vitendo, matendo

Ufafanuzi

Katika Biblia maneno kazi, vitendo, matendo ni vitu ambavyo Mungu au watu hufanya.

- Neno kazi linamaana ya kufanya kazi kwa ajili ya kuwatumikia watu wengine.
- Kazi ya Mungu na kazi ya mikono yake ni kazi zote anazzozifanya ikiwemo kuumba dunia, kuokoa wenye dhambi, kuwapatia mahitaji wale aliowaumba. Matendo ni miujiza ya Mungu kama "matendo makuu."
- Matendo anayofanya mwanadamu yaweza kuwa mazuri au mabaya.
- Roho mtakatifu anatatia nguvu waamini kufanya kazi njema ambazo huitwa "matunda mema."
- Watu hawaokolewi kwa kazi zao nzuri bali kwa imani yao kwa Yesu.

Kiapo

Ufafanuzi

Kiapo ni ahadi ambayo mtu anaiweka kwa Mungu. Mtu anaahidi kufanya jambo fulani kwa ajili ya kumuheshimu Mungu na kuonesha ibada kwake.

- Baada ya mtu kufanya kiapo anapaswa atekeleze kiapo kile.
- Biblia inatufundisha kuwa mtu anaweza kuhukumiwa na Mungu asipitimiza kiapo chake.
- Mara nyingine mtu anaweza kumuomba Mungu amlinde au amfanyie jambo fulani na akaweka kiapo kwa Mungu.

Lakini Mungu hatakiwi kutimiza ombo la mtu aliloomba katika kiapo.

kicho, uchaji

Ufafanuzi

Maneno "kicho" na "uchaji" yanamaanisha kujitoa kwa nguvu zote kumuunga mkono mtu au wazo.

- Kicho inahusisha tamaa kubwa na matendo yanayoimiza jambo jema. Mara kwa mara inatumika kumwelezea mtu ambaye kwa uaminifu anamtii Mungu na kuwafundisha wengine kufanya hivyo pia.
- Uchaji unahusisha kuweka bidii kubwa katika kufanya jambo na kuendelea katika bidii hiyo.
- "Kicho cha Bwana" au "kicho cha Yahwe" yarejerea matendo ya Mungu yenye nguvu na endelevu katika kuwabariki watu wake au kuona haki ikitendeka.

Maoni ya Ufasiri

- Kuwa "mchaji" yaweza pia kufasiriwa, "kuwa na bidii kubwa" au kufanya jitihada "zaidi."
- Neno "kicho" laweza pia kufasiriwa kama "uchaji wa ndani" au "maamuzi ya kina" au "hamu ya haki."
- Kirai, "kicho cha nyumba yako" yaweza kufasiriwa, "kuliheshimu sana hekalu lako" au "tamaa ya kuitunza nyumba yako."

Kipatanisho

Ufafanuzi

"Kipatanisho" ni sadaka inayotolewa ili kutimiza haki ya Mungu au kutuliza hasira yake.

- Sadaka ya damu ya Yesu ni upatanisho kati ya Mungu na wanadamu.
- Kifo cha Yesu msalabani kimetuliza hasira ya MUNGU dhidi ya dhambi. Hii imetengeneza njia ya Mungu kuwaangalia wanadamu na kuwahurumia na kuwapatia uzima wa milele.

Kristo, Masihi

Ufafanuzi

Masihi na Kristo inamaana ya mpakwa mafuta na inamuelezea Yesu mwana wa Mungu.

- Masihi na Kristo vimetumika katika agano jipya kumuelezea mwana wa Mungu ambaye Mungu baba alimpaka mafuta kutawala kama mfalme juu ya watu wake na kuwaokoa toka kwenye dhambi.
- Katika agano la kale manabii waliandika unabii juu ya Masihi miaka mia kabla ya kuja kwake duniani.
- Neno mpakwa mafuta limetumika katika agano la kale kumuelezea Masihi atakayekuja.
- Yesu alitimiza unabii huo na alifanya miujiza mingi iliyothibitisha kuwa yeye ni Masihi, unabii uliobaki utatimia atakaporudi.
- Neno Kristo hutumika kama jina "Kristo Yesu."

Kuamini, kuamini katika

Ufafanuzi

Neno "kuamini" na "kuamini katika" yanahusiana kwa karibu, lakini yana maana tofauti:

Maoni ya Kutafasiri

- "Kuamini" laweza kutafasiriwa kama "kujua kuwa ni kweli" au "Jua kuwa sawa."
- "Kuwa na imani" laweza kufasiriwa kama "kuamini kikamilifu" au "kuamini na Kutii" au "kutegemea kwa ukamilifu na kufuata."

Kuasili

Ufafanuzi

Neno "kuasili" ni hatua za kisheria za mtoto kuwa na wazazi fulani ambao sio wazazi wake wa kumzaa.

- Biblia imetumia "kuasili" kuelezea namna ambavyo Mungu alivyosababisha watu kuwa sehemu ya familia yake, kuwafanya watu wawe watoto wake wa kiroho.
- Watoto walioasiliwa pamoja na waamini ni warithi pamoja na Yesu Kristo wakiwa na haki zote kama wana wa Mungu.

Kubariki

Ufafanuzi

"kubariki" mtu au kitu maana yake ni kusababisha mema na mambo ya manufaa kufanyika kwa mtu au kitu kinachobarikiwa.

- Kumbariki mtu pia inamaanisha kuonesha nia chanya na vitu vyenye manufaa kumpata mtu huyo.
- Katika nyakati za Biblia, kwa kawaida baba alitamka baraka maalumu kwa wanawe.
- Watu "wanapombariki" Mungu au kuonesha hamu ya kuwa Mungu abarikiwe, inamaanisha wanamwinua.
- Neno "baraka" wakati mwingine linatumika kwa kukitakasa chakula kabla hakijaliwa, au kwa kumshukuru na kumsifu Mungu kwa ajili ya chakula.

//kutokana na maoni hapa chini: Ni mhimu kutoa maana, lengo, au kuzingatia matumizi ya mzizi wa neno "bariki" ambalo kimsingi linapendekea kustawi au kuwa na wingi wa vitu au utajiri. Kwa kuzingatia wingi wa mafundisho ya kimaandiko juu ya upendo wa Mungu, rehema na neema ambayo siyo ya kale tu bali hata sasa. Kwa kuzingatia uangalizi, ulinzi, na uwepo wa Roho wa Mungu. Na kwa ajili yetu kumbariki Mungu, kwa kutoa shukurani, kuthamini, na kuelewa kama tunavyojifunza na kumfuata(kumtii)//

Maoni ya Kutafasiri

- "Kubariki" kwaweza kutafasiriwa kama "kuandaa kwa wingi" au "kuwa mwema ."
- "Mungu ameleta baraka kuu" ifasiriwe kama "Mungu ametoa mambo mengi mema kwa" au "Mungu ametoa kwa wingi kwa ajiri" au "Mungu amesababisha Mambo mema kutokea kwa".
- "Amebarikiwa" ifasiriwe kama "atanufaika sana" au "atapitia mambo mema" au "Mungu atamfanya kustawi".
- "Amebarikiwa mtu yule" yaweza kutafasiriwa kama "Ni vema kiasi gani kwa mtu ambaye".
- Vioneshi kama vile, "abarikiwe Bwana" yaweza kutafasiriwa kama, "na asifiwe Bwana" au "Bwana asifiwe" au "Ninamtukuza Bwana".
- Katika mazingira ya kubariki chakula, hii yaweza kutafasiriwa kama, "alimshukuru Mungu kwa ajili ya chakula" au "alimshukuru Mungu kwa kuwapa chakula" au "alikitakasa chakula kwa kumsifu Mungu.

Kuchaguliwa tangu asili

Ufafanuzi

Kuchaguliwa tangu asili nikitendo cha kuamua au kupanga kabla ya jambo hilo kutokea.

- Neno hili linamuelezea Mungu aliwachagua watu kupokea uzima wa milele.
- Mara nyingine neno "kuteuliwa" hutumika likuwa na maana ya kuamua kabla.

kuhani mkuu

Ufafanuzi

Neno 'kuhani mkuu' hurejelea kuhani maalumu aliyekuwa ameteuliwa kutumika kwa mwaka mmoja kama kiongozi wa makuhani wote wa Wayahudi. Kuhani mkuu alikuwa na majukuu mahususi. Alikuwa ni mtu pekee aliyeruhusiwa kuingia mahali patakatifu sana katika hekalu ili kutoa sadaka maalumu mara moja kwa mwaka. Waisraeli walikuwa na makuhani wengi sana, lakini walikuwa na kuhani mkuu mmoja kwa muda fulani. Kipindi alichokamatwa Yesu, Kayafa alikuwa kuhani mkuu. Anasi, Baba mkwe wa Kayafa anatajwa mara kadhaa kwasababu alikuwa kuhani mkuu hapo awali, huenda alikuwa bado na mamlaka na nguvu fulani juu ya watu.

Mapendekezo ya tafsiri 'Kuhani mkuu" tunaweza kutafsiri kama "kuhani wa daraja la juu"

Kuhani, ukuhani

Ufafanuzi

Katika Biblia Kuhani alikuwa mtu aliyechaguliwa kutoa sadaka ya kuteketezwa kwa Mungu kwa niaba ya watu wa Mungu. Ukuhani lilikuwa jina au masharti ya kuwa kuhani.

- Katika agano la kale Mungu alimchagua Haruni na uzao wake kuwa makuhani wa Israeli.
- Ukuhani ilikuwa haki na majukumu yaliyorithishwa toka kwa baba kwenda kwa mtoto katika kabila ka Lawi.
- Makuhani wa Israeli walikuwa na jukumu la kutoa sadaka za watu kwa Mungu pamoja na kazi nyingine katika hekalu.
- Makuhani pia walitoa maombi kwa Mungu kawa niaba ya watu wake na kufanya kazi nyingine za kidini.
- Makuhani walitangaza baraka kwa watu na kuwafundisha sheria za Mungu.
- Katika wakati wa Yesu kulikuwa na ngazi mbalimbali za makuhani kama Makuhani Wakuu na Kuhani mkuu.
- Yesu ni kuhani wetu mkuu anayetuombea mbele za Mungu. Alijitoa mwenyewe kama sadaka kwa dhambi zetu.
- Katika agano jipya hata anayemwamini Mungu ni kuhani ambaye anaweza kwenda moja kwa moja kwa Mungu kwa njia ya maombi kujiombea mwenyewe na kuombea watu wengine.
- Hapo kale kulikuwa pia na makuhani wa kipagani walioleta sadaka kwa miungu ya uongo kama Baali.

Kuhukumu, hukumu

Ufafanuzi

"Kuhukumu" au "hukumu" ni kitendo cha kumpa mtu kumhukumu mtu baada ya kufanya jambo baya.

- Maranyingine kuhukumu inamaanaisha kumshitaki mtu au kumhukumu vibaya mtu.
- Hukumu ni kitendo cha kuhukumu au kumshitaki mtu.

kujaribu, jaribu

Ufafanuzi

Kumjaribu mtu ni kufanya huyo mtu kufanya kitu kibaya.

- Jaribu ni kitu kinacho sababisha mtu kutaka kufanya kitu kibaya.
- Watu wanajaribiwa kwa dhambi zao na kwa watu wengine.
- Shetani pia anajaribu watu kutomtii Mungu na kufanya dhambi dhidi ya Mungu na kwa kufanya vitu vibaya.
- Shetani alimjaribu Yesu na kumtaka afanye kitu kibaya, lakini Yesu alizuia majaribu yote ya Shetani na hakutenda dhambi.

kujazwa kwa Roho

Ufafanuzi

Msemo "kujazwa kwa Roho" ni msemo wa kitamathali ambao una maana ya Roho Mtakatifu kumwezesha kufanya mapenzi ya Mungu.

Msemo "kujazwa na" ni msemo ambao hutumika mara kwa mara kumaanisha "kutawalwa na".

Watu "wanajazwa na Roho" wanapofuata uongozi wa Roho Mtakatifu na kumtegemea kabisa kuwasaidia kufanya kile Mungu anachotaka.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "kuwezeshwa na Roho Mtakatifu" au "kutawaliwa na Roho Mtakatifu". Lakini haitakiwi kuonekana kana kwamba Roho Mtakatifu analazimisha mtu kufanya kitu.

Sentensi kama "alijazwa na Roho" inaweza kutafsiriwa kama "alikuwa akiishi kikamilifu kwa nguvu ya Roho" au "Roho Mtakatifu alikuwa akimuongoza kikamilifu".

Msemo huu ni sawa kwa maana na msemo "kuishi kwa Roho" lakini "kujazwa na Roho" inasisitiza ukamilifu ambao mtu huruhusu Roho Mtakatifu kuwa na utawala au ushawishi juu ya maisha yake. Kwa hiyo misemo hii miwili inatakiwa kutafsiriwa tofauti, ikiwezekana.

Kujivuna

Ufafanuzi

Neno "kujivuna" humaaanisha kuongea kwa kiburi kuhusu mtu au kitu. Mara kwa mara inamaanisha kujivuna mwenyewe.

- Mtu "mwenye majivuno" anajiongelea kwa njia ya kiburi.
- Mungu aliwakemea Waisraeli kwa "kujivunia" sanamu zao. Kwa ujinga waliabudu miungu badala ya Mungu wa kweli.
- Biblia inazungumzia pia watu wajivunao utajiri wao, nguvu, mashamba yenye rutuba, na sharia zao. Hii inamaanisha kwamba walijivunia vitu hivi hata awakumtambua Mungu awapaye vitu hivyo.
- Mungu aliwaamru badala yake "wajivune" kwa sababu wanamfahamu yeye.
- Mtume Paulo, pia alizungumzia kuhusu kujivuna katika Bwana, kumaanisha kufurahi na kumshukuru Mungu kwa yote aliyowafanyia.

Maoni ya Tafasiri

- Njia nyingine ya kutafasiri "majivuno" inahusisha "kuongea kwa kiburi" au kuwa na kiburi."
- Neno "enye kujivuna" yaweza kutafasiriwa kwa kifungu kimaanishacho, "mwenye kujazwa na maneno ya kiburi" au "enye kiburi" au "kuongea kwa kiburi kuhusu mwenyewe."
- Katika mazingira ya kujivuna katika au kuhusu Mungu, yaweza kufasiriwa kama "kujivunia" au "kujisifu katika" au kuwa na furaha kuhusu" au "kumshukuru Mungu kwa ajili ya".
- Baadhi ya lugha zina maneno mawili kwa ajili ya "kiburi": moja ni hasi lenye maana mbaya, na lingine lenye maana nzuri, lenye maana ya kujivunia kazi , familia, au nchi.

Kukiri

Ufafanuzi

Kukiri inamaana ya kukubali kuwa jambo fulani ni la kweli. Kukiri ni kauli ya kuwa kitu fulani ni kweli.

- Kukiri pia yaweza kuwa na maana ya kusema ukweli kuhusu Mungu. Pia yaweza kuonesha kukubali kuwa sisi ni wenye dhambi.
- Biblia inasema watu wakikiri dhambi zao kwa Mungu atawasamehe.
- Mtume Yakobo aliandika kwenye barua yake kuwa waamini wakikiri dhambi zao wao wenyewe inawaletea uponyaji wa kiroho.
- Mtume Paulo aliwaandikia Wafilipi kuwa siku moja kila mtu atakiri kuwa Yesu ni Bwana.
- Paulo pia anasema watu wakikiri kuwa Yesu ni Bwana na kuamini kuwa Mungu alimfufua toka kwa wafu wataokolewa.

kukomboa, ukombozi, mkombozi

Ufafanuzi

"Kukomboa" au "ukombozi" ni kununua kitu kilichokuwa kinamilikiwa hapo mwanzo au kilichochukuliwa mateka. "Mkombozi" ni mtu anayekikomboa kitu au mtu.

- Mungu alitoa sheria kwa Waisraeli kuhusu kukomboa watu wau vitu.
- Kwa mfano mtu anaweza kumkomboa mtu aliyekuwa utumwani kwa kumlipia kiasi ambacho mtumwa yule atakuwa huru.
- Kama ardhi ya mtu imeuzwa, ndugu wa yule mtu anaweza kuikomboa au kuinunua tena ardhi ile ili ibaki kwenye familia.
- Tendo hili linaonesha namna ambavyo Mungu aliwakomboa watu wake toka kwenye utumwa wa dhambi. Yesu alipokufa msalabani alilipia dhambi za watu nakukomboa watu wote wanaoamini ukombozi wake. Watu waliokombolewa na Mungu wapo huru toka kwenye dhambi na adhabu.

Kumkufuru

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "kufuru" inamaanisha kuzungumza kwa njia ambayo inaonesha dharau kubwa kwa Mungu au watu. "Kumkufuru" mtu ni kuongea kinyume cha mtu huyo ili watu wafikiri vibaya juu ya mtu huyo.

- Mara nyingi, kumkufuru Mungu humaanisha kumtukana kwa kusema mambo ambayo siyo kweli kuhusu yeye au kwa kuenenda kwa njia isiyo na maadili hata kumvunjia heshima.
- Ni kufuru kwa mwanadamu kudai kuwa Mungu au kudai kwamba kuna Mungu mwingine zaidi ya Mungu wa kweli.
- Baadhi ya matoleo mengine yanatafasiri neno hili kama "kumtukana" linaporejerea kuwakufuru watu.

Maoni ya Tafasiri

- "Kukufuru" kwaweza kutafasiriwa kama, "kusema vibaya dhidi ya" au "kumdharau Mungu" au "kumtukana".
- Jinsi ya kutafasiri "kufuru" ni pamoja na. "kusema vibaya kuhusu wengine" au "kutukana" au "kusambaza tetesi za uongo."

Kumtia mafuta

Ufafanuzi

"Kumtia mafuta" ina maana ya kupaka au kummiminia mafuta mtu au kitu. Mara nyingine mafuta haya huchanganywa na viungo ambavyo huleta ladha au harufu ya manukato. Pia hutumika kama lugha ya picha kuonesha namna ambavyo Roho Mtakatifu anawachagua watu na kuwatia nguvu.

- Katika agano la kale makuhani, wafalme na manabii walipakwa mafuta ili kuwatenga kwa ajili ya kazi maalumu ya kumtumikia Mungu.
- Vitu kama madhabahu na hema vilipakwa mafuta kuonesha kuwa vilitakiwa kutumika kwa ajili ya kumuabudu Mungu na kumtukuza yeye.
- Katika agano jipya mara mbili Yesu anapakwa mafuta ya manukato na mwanamke kama tendo la kumuabudu. Sehemu moja Yesu alionesha kuwa kwa kufanya hivyo yule mwanamke alikuwa akimuandaa kwa ajili ya maziko yake.
- Baada ya Yesu kufan rafiki zake waliuandaa mwwili wa Yesu kwa ajili ya maziko kwa kuupaka mafuta na manukato.
- Neno "Masihi" au "Kristo" lina maana ya mpakwa mafuta.

Kuomba, maombi

Ufafanuzi

"Maombi" au "kuomba" ni kitendo cha kuongea na Mungu. Neno hili pia laweza kutumika kama kitendo cha watu kujaribu kuongea na miungu ya uongo.

- Mtu anaweza kuomba taratibu, kuzungumza na Mungu katika mawazo au kuomba kwa nguvu kuzungunza na Mungu kwa sauti. Mra nyingine maombi huandikwa mfano kama Daudi alipoandika maombi yake katika kitabu cha Zaburi.
- Mambi yanaweza kujumuisha kumuomba Mungu rehema, msaada kwa tatizo fulani au hekima ya kufanya maamuzi.
- Mara nyingine watu humuomba Mungu awaponye wagonjwa au wanaohitaji msaada wake.
- Pia watu hushukuru na kumsifu Mungu katika maombi.
- Maombi yanajumuisha kukiri dhambi zetu na kumuomba Mungu atusamehe.
- Kuongea na Mungu huitwa kunong'onezana naye roho zetu zikiwa na mazungumzo na roho yake na kufurahia uwepo wake.
- Hii inaweza kutafsiriwa kama kuzungumza na Mungu au kuwasiliana na Mungu.

Kupatanisha, maridhiano

Ufafanuzi

Kupatanisha na maridhiano ni kutengeneza amani kati ya watu waliokuwa maadui.

- Katika Biblia neno hili linamuelezea Mungu kuwapatanisha watu na yeye mwenyewe kwa kumtoa mwana wake Yesu Kristo.
- Kwa sababu ya dhambi watu wote ni adui wa Mungu. Lakini kwa sababu ya upendo wake Mungu anatoa njia ya watu kupatanishwa naye kupitia Yesu.
- Kwa kuamini kujitoa kwa Yesu kama malipo ya dhambi zao watu wanaweza kusamehewa na kuwa na amani na Mungu.

Kupotea, kuharibika

Ufafanuzi

"Kupotea" inamaanisha kufa au kuharibiwa maranyingi huwa ni baada ya mapigano au majanga. Katika Biblia inamaana zaidi ya kuhukumiwa milele jehanamu.

- Watu waliopotea ni wale wanaoenda jehanamu kwa sababu walikataa kumwamini Yesu kwa ajili ya wokovu wao.
- Yohana 3:16 inatufundisha "kupotea" ni kutokuishi milele mbinguni.

Kurejesha, marejesho

Ufafanuzi

Kurejesha au marejesho ni kusababisha kitu kirudi katika uhalisia wake au katika hali nzuri.

- Mwili wa mgonjwa unaporejeshwa inamaana kuwa unaponywa.
- Mahusiana yaliyovunjika yakirejeshwa inakuwa kitendo cha kurudiana. Mungu huwarejesha wenye dhambi na kuwarudisha kwake.
- Watu wakirejeshwa kwenye nchi zao inamaana "wanarudishwa" kwenye nchi hizo.

kutenga

Ufafanuzi

Neno "kutenga" lina maana ya kutengwa kutoka kwenye kitu kutimiza aina ya kusudi.

- Waisraeli walitengwa kwa huduma ya Mungu.
- Roho Mtakatifu aliamuru Wakristo wa Antioki kumtenga Paulo na Barnabas kwa kazi Mungu aliyo taka wafanye.
- Muamini aliye "tengwa" kwa kazi ya Mungu "ametolewa kutimiza" kazi ya Mungu.
- Maana moja ya neno "takatifu" ni kutenga kama kuwa wa Mungu na kutengwa na dhambi za dunia.

Kuteua, Kuteuliwa

Ufafanuzi

"Kuteua au kuteuliwa" linamaana ya kumchagua mtu ili aikamilishe kazi fulani.

- Kuteuliwa pia inaweza kuwa kuchaguliwa ili kupokea kitu fulani. kuteuliwa kwenye uzima wa milele hii inamaanisha walichaguliwa kupokea uzima wa milele.
- Neno "wakati ulioteuliwa" ina maana ya wakati ambao Mungu amepanga kufanya jambo fulani.
- Neno "kuteua" pia laweza kuwa na maana ya kuamuru, kumpa mtu kazi fulani ya kufanya.

kutokuwa na imani, upotofu wa imani

Ufafanuzi

Msemo "kutokuwa na imani" una maana ya kutokuwa na imani au kutoamini.

Neno hili linatumika kuelezea watu ambao hawamuamini Mungu, ambayo inaonekana kwa njia ya chafu wanayofanya.

Nabii Yeremia alimshtaki Israeli kwa kutokuwa na imani na kutomtii Mungu.

Waliabudi sanamu na kufuata tamaduni zinginge ambazo si za kiungu za kundi la watu ambao hawakumwabudu au kumtii Mungu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, msemo "kutokuwa na imani" unaweza kutafsiriwa kama "upotofu wa uaminifu" au "kutoamini" au "kutomtii Mungu".

Msemo "upotofu wa imani" unaweza kutafsiriwa kama "ukosefu wa imani" au "uasi dhidi ya Mungu"

Kutubu, toba

Ufafanuzi

Kutubu na toba ni hali ya kuacha dhambi na kumrudia Mungu.

- "Kutubu" ni hali ya kubadili nia ya mtu.
- Katika Biblia "kutubu" inamaanisha kuacha dhambi, namna ya kufikiri kibinadamu na kutenda na kumrudia Mungu na njia zake na matendo yake.
- Watu wanapotubu kabisa dhambi zao, Mungu anawasamehe na kuwasaidia kuanza kumtii.

Kuwa na mapepo

Ufafanuzi

Mtu ambaye ana mapepo ana pepo au roho chafu ambalo humuongoza kile afanyacho au kufikiri.

Mara kwa mara mtu mwenye pepo hujiumiza mwenyewe au watu wengine kwa sababu peopo husababisha afanye hivyo.

Yesu aliponya watu waliokuwa na mapepo kwa kuwaamuru mapeopo kuwatoka . Hii mara kwa mara hujulikana kama "kutoa" mapepo.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri msemo huu zinaweza kujumuisha, "kutawaliwa na pepo" au "kutawaliwa na roho mchafu" au "kuwa na roho mchafu aishiye ndani".

Kuzaliwa upya, kuzaliwa na Mungu, kuzaliwa kwa roho

Ufafanuzi

Neno "kuzaliwa upya" lilitumiwa mara ya kwanza na Yesu kuelezea maana ya Mungu kumbadilisha mtu kutoka kuwa mfu kiroho na kuwa hai kiroho. Neno "kuzaliwa na Mungu" na "kuzaliwa kwa roho" pia hurejerea hali ya mtu kupewa uzima mpya kiroho.

- Watu wote wanazaliwa wafu kiroho na wanapewa "kuzaliwa upya" wanapomwamini Yesu Kristo kama mwokozi wao.
- Katika wakati wa kuzaliwa upya kiroho, Roho wa Mungu uanza kuishi ndani ya muumini mpya na kumtia nguvu ili azae matunda mema ya kiroho katika maisha yake.
- Ni kazi ya Mungu kumfanya mtu kuzaliwa upya na kuwa mwana wake.

Maoni ya Tafasiri

- Njia nyingine ya kutafasiri "kuzaliwa tena" inahusisha, "kuzaliwa upya" au "kuzaliwa kiroho."
- Ni vizuri kutafasiri neno hili katika maana ya kawaida na kutumia neno la kawaida katika lugha litumikalo kwa kuzaliwa.
- Neno "uzao mpya" laweza kutafasiriwa kama "kuzaliwa kiroho."
- Kirai "liyezaliwa na Mungu" laweza kutafasiriwa kama "kufanywa na Mungu kuwa na uzima mpya kama mtoto aliyezaliwa upya au "kupewa uzima mpya na Mungu."
- Kwa njia ileile, "amewezeshwa na Roho Mtakatifu kuwa mtoto wa Mungu" au "kufanywa na Roho kuwa na uzima mpya kama mtoto mchanga."

kuzimu

Ufafanuzi

katika Biblia kuna maneno mawili yametumika, neno la Kiebrania 'sheol' na neno la Kigriki 'hades.' Maneno haya yametumika katika Biblia kumaanisha kifo na sehemu ambako roho za watu waliokufa huenda. katika Kiebrania neno 'sheol' limetumika katika Agano la Kale kurejelea sehemu ya watu waliokufa au sehemu ya kifo. katika agano jipya, neno la Kigriki 'hades" limetumika kumaanisha sehemu ya roho za watu waliomwasi Mungu. Roho hizi hurejelewa kama zinaenda "chini." Wakati mwingine linaweza kutofautishwa na 'kwenda juu' mbinguni mahali ambako roho za watu za watu wanaomwamini Yesu zinaishi.

Mapendekezo ya tafsiri Katika Agano la Kale neno "sheol" linaweza kutafsiriwa kama " sehemu ya wafu" au "sehemu kwa ajli ya roho za wafu" Baadhi ya tafsiri hufasiri neno hili kama "shimo" au "kifo" kwa kutegemea na muktadha. Neno "hades" limetumika sana katika Agano Jipya ambalo laweza kutafsiriwa kama "sehemu kwa ajili ya roho za wafu za watu wasioamini" au " sehemu ya mateso na adhabu ya kwa roho za wafu wasioamini." Baadhi ya tafsiri hutunza neno ''sheol" au ''Hades'' kwa kutumia herufi ambazo zinakubaliana katika mfumo wa sauti wa lugha husika. kwa kiswahili twaweza kusema 'sheoli" na 'hadesi'

kweli, ukweli, kuwa kweli

Ufafanuzi

Maneno "kweli" na "ukweli" yana eleza mambo ambyo ni halisi, matukio yaliyo tukia, na maneno yaliyo semwa.

- Vitu vya kweli ni halisi, thabiti, uhakika, sawasawa, halali.
- Ukweli ni ufahamu, uamini, uhalisia, au maneno yaliyo kweli.
- Msemo kuwa "kuwa kweli" au "kuja kuwa kweli" ni msemo unao maanisha kuwa unabii ulitokea hakika kama iliyo tabirika kuwa itakuwa.
- Ukweli una jumuisha maelezo ya kutenda kwa namna iliyo tegemevu na aminifu.
- Yesu alidhihirisha ukweli wa Mungu katika maneno aliyo zungumza.
- Neno la Mungu ni kweli. Lina eleza vitu vilivyo tokea na kufundisha yaliyo kweli kuhusu Mungu na kuhusu kila kitu alicho fanya.

Laana, kulaaniwa

Ufafanuzi

Laana ni kusababisha mambo mabaya yatokee kwa mtu au kitu kilicholaaniwa.

- Laana yaweza kuwa kauli ya kusababisha madhara yatokee kwa mtu au vitu.
- Kumlaani mtu ni kutamani mabaya yatokee kwake.
- Pia inaweza kuwa adhabu au mambo mabaya ambayo mtu amesababisha yatokee kwa mtu.

liwali

Ufafanuzi

Neno "liwali" la eleza afisa wa serikali aliye tawala sehemu ya Serikali ya Rumi. Kila liwali alikuwa chini ya mamlaka ya mfalme mkuu wa Kirumi.

- Cheo "liwali" lina maana "mmoja wa watawala wa nne waliyo ungana."
- Kwa kuanza na Mfalme Mkuu Diokletia, kulikuwa na migawanyiko minne ya Serikali ya Kirumi na kila liwali alitawala mmoja.
- Ufalme wa Herode "Mkuu", aliye kuwa mfalme wa kipindi cha kuzaliwa kwa Yesu.
- Kila mgawanyiko ulikuwa na moja au zaidi ya "mikoa" midogo, kama Galilaya au Samaria.
- "Herode liwali" anatajwa mara kadhaa katika Agano Jipya. Pia ujulikana kama "Herode Antipasi."

Mabaki

Ufafanuzi

Mabaki ni watu au vitu vilivyosalia toka kwenye kundi kubwa.

- Mabaki mara nyingi huwa watu walioishi baada ya maisha yao kuwa mashakani au waliobaki kuwa waaminifu kwa mungu wakati wakipitia mateso.
- Isaya anazungumzia kundi la Wayahudi kama mabaki ya waliosalia baada ya mashambulizi toka kwa watu wa nje na kurudi katika nchi ya Kanaani.
- Paulo anazungumza kuhusu kuwa "mabaki" ya watu waliochaguliwa na Mungu kupokea rehema yake.
- Neno "Mabaki" inaonesha kuwa kuwa watu wengine ambao hawakuwa waaminifu na hawakusalia au hawakuchaguliwa.

Madhabahu

Ufafanuzi

Madhabahu ilikuwa sehemu yenye muundo ulioinuka ambao wana wa Israeli walichoma wanyama na mazao kama sadaka kwa Mungu.

- Katika nyakati za Biblia madhabahu rahisi zilikuwa zinatengenezwa kwa kilima chenye udongo au mawe makubwa yaliyopangwa na kupafanya pawe imara.
- Madhabahu nyingine zilitengenezwa kwa mbao pamoja na dhahabu na shaba.
- Watu wengine walioishi karibu na Israeli walitengeneza pia madhabahu na kutoa sadaka kwa miungu yao.

mahali takatifu

Ufafanuzi

Neno "mahali takatifu" ya husu sehemu ambayo Mungu amefanya takatifu. Inaweza maanisha eneo linalo toa ulinzi na usalama.

- Katika Agano la Kale, neno "mahali takatifu" mara nyingi lilitumika kueleza maskani au hekalu ambapo "patakatifu" na "patakatifu pa patakafitu" kulikuwepo.
- Mungu alitaja mahali takatifu kama sehemu aliyo ishi miongoni mwa watu wake, Waisraeli.
- Pia alijiita "mahali takatifu" au sehemu salama watu wake wanaweza pata ulinzi.

maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

Ufafanuzi

Maneno haya yote yanamaanisha kuwa hai kimwili, sio kufa. Yanatumika pia kimafumbo kumaanisha kuwa hai kiroho. Yanayofuata yanaelezea nini kinamaanishwa na "maisha ya kimwili" na "maisha ya kiroho."

Kulingana na mazingira, "maisha" inaweza kuetafsiriwa kama "kuwepo" au "mtu" au "roho" au "kuwa" au "kupitia." Neno "uhai" inaweza kutafsiriwa kama "kuishi" au "kukaa" au "kuwepo." Msemo "mwisho wa maisha yake" inaweza kutafsiriwa kama, "alipoacha kuishi." Msemo "alinusuru maisha yao" unaweza kutafisiri kama, "aliwaruhusu waishi" au "hakuwaua." Msemo "walihatarisha maisha yao" unaweza kutafsiriwa kama, "walijiweka hatarini" au "walifanya kitu ambacho kingiweza kuwaua." Bibilia inapozungumzia kuwa hai kiroho, "maisha" yanaweza kutafsiriwa kama "maisha ya kiroho" au "maisha ya milele," kulingana na mazingira. Wazo la "maisha ya kiroho" linaweza pia kutafsiriwa kama, "Mungu kutufanya kuwa hai katika roho zetu" au "maisha mapya kwa Roho wa Mungu" au "kufanywa hai ndani yetu." Kulingana na mazingira, msemo "toa maisha" unaweza kutafsiriwa kama, "kusababisha kuishi" au "kutoa uzima wa milele" au "kusababisha kuishi milele."

Malaika, Malaika mkuu

Ufafanuzi

Malaika ni kiumbe chenye roho na chenye nguvu kilichoumbwa na Mungu. Malaika wanamtumikia Mungu kwa kufanya yale wanayoagizwa kuyafanya na Mungu. Malaika mkuu ni malaika anayewaongoza malaika wengine.

- Malaika maana yake ni mjumbe.
- Malaika mkuu maana yake ni mjumbe mkuu. Malaika pekee kwenye Biblia anayesemwa kama malaika mkuu ni Mikaeli.
- Katika Biblia malaika wanafikisha ujumbe kwa watu toka kwa Mungu. Ujimbe huu ni pamoja na maelekezo juu ya nini Mungu anataka watu wafanye.
- Malaika pia waliwaambia watu mambo yajayo.
- Malaika wana mamlaka ya Mungu katika kumuwakilisha na wakati mwingine kwenye Biblia wamezungumza kama vile Mungu anazungumza.
- Njia nyingine ambazo Malaika wanamtumikia Mungu nu kwa kuwalinda na kuwapa watu nguvu.
- Malaika wa Yahweh ina maana mbili 1) "malaika wanaomwakilisha Yahweh" au "wajumbe wanaomtumikia Yahweh." 2) Yaweza kuwa na maana ya Yahweh mwenyewe aliyeonekana kama malaika alipoongea na mtu.

Mamlaka

Ufafanuzi

Mamlaka ni nguvu ya kushawishi na kutawala ambayo mtu anakuwa nayo juu ya mtu mwingine.

- Wafalme na viongozi wengine wanamamlaka juu ya watu wanaowaongoza.
- Mamlaka pia yaweza kuwa watu, serikali au taasisi fulani yenye nguvu juu ya wengine.
- Mabwana wana mamlaka juu ya watumwa wao. Wazazi wana mamlaka juu ya watoto wao.
- Serikali ina mamlaka juu ya kuweka sheria zitakazowaongoza wananchi wake.

manemane

Ufafanuzi

Manemane ni mafuta au manukato yanayo tengenezwa kwa majani ya manemane yanayo ota Africa na Asia.

- Manemane utumika kutengeneza uvumba, marashi, na dawa, na kuanda miili kwa maazishi.
- Manemane ni baadhi ya wasomi waliyo mpa Yesu alipo zaliwa.
- Yesu alipewa mvinyo iliyo changanywa na manemane ili kupunguza maumivu alipo sulubiwa.

manna

Ufafanuzi

Manna ili kuwa nyeupe, aina ya chakula cha unga ambacho Mungu alikitoa kwa ajili ya Waisraeli kula kipindi cha miaka 40 waliyo ishi nyikani baada ya kutoka Misri.

- Manna ilikuwa kama theluji iliyo tokea kila asubui katika ardhi chini ya umande. Ladha yake ilikuwa tamu, kama asali.
- Waisraeli walikusanya theluji za manna kila siku kasoro Sabato.
- Katika siku kabla ya Sabato, Mungu aliwambia Waisraeli kukusanya mara mbili kiasi cha manna ili wasikusanye siku yao ya mapumziko.
- Neno "manna" lina maana ya "nini hiki?"
- Katika Biblia, manna pia ya tajwa kama "mkate kutoka mbinguni"

Mapenzi ya Mungu

Ufafanuzi

Mapenzi ya Mungu ni kitu anachotamani Mungu au mipango.

- Mungu atafananisha mahusiano yake na watu na namna anavyotaka watu waitikie kwake.
- Pia mapenzi ya Mungu ni mipango yake kwa alivyoviumba.
- Mapenzi ya Mungu pia yanaweza kutafsiriwa kama "Kusudi la Mungu" au "Linalompendeza Mungu."

maskani

Ufafanuzi

Maskani ilikuwa hema muhimu Waisraeli walimuabudu Mungu kipindi cha miaka 40 walipo zunguka jangwani.

- Mungu aliwapa Waisraeli maelekezo ya kujenga hema kubwa, iliyo kuwa na vyumba viwili na ilizungukwa na ua ya ndani.
- Kila mara Waisraeli walipo enda sehemu tofauti jangwani kuishi, makuhani alitengua maskani na kuibeba kwenye kambi yao ifauatayo.
- Maskani ilijengwa na mbao iliyo kuwa na mapazia na vitambaa, nywele za mbuzi, na ngozi za wanyama.
- Sehemu mbili za maskani zilikuwa Pa Takatifu (ambapo madhabahu ya kufukiza uvumba ilikuwa) na Pa Takatifu Pa Patakatifu (ambapo sanduku la agano lilihifadhiwa.)
- Uani ya maskani ilikuwa na madhabahu ya kuteketeza dhabihu za wanyama na beseni maalumu la kusafishia kimila.

Mataifa

Ufafanuzi

Msemo "mataifa" una maana ya mtu yeyote ambaye sio Myahudi. Watu wa mataifa ni watu ambao sio uzao wa Yakobo.

Katika Biblia, msemo "kutotahiriwa" pia hutumika kitamathali kumaanisha watu wa Mataifa kwa sababu wengi wao hawakutahiri watoto wao wa kiume kama Waisraeli walivyofanya.

Kwa sababu Mungu aliwachagua Wayahudi kuwa watu maalumu, walifikiria juu ya watu wa mataifa kama watu wa nje ambao wasingeweza kuwa watu wa Mungu.

Wayahudi pia waliitwa "Waisraeli" au "Waebrania" katika vipindi tofauti vya historia. Waliwajua wengine wote kama "watu wa Mataifa".

Watu wa mataifa pia inaweza kutafsiriwa kama "asiye Myahudi" au "asiye Muisraeli" (Agano la Kale).

Kitamaduni, Wayahudi hawakula na watu wa mataifa au kujihusishanao, ambapo mara ya kwanza ilisababisha matatizo miongoni mwa kanisa la kwanza.

Matumaini

Ufafanuzi

Neno 'matumaini' hurejelea matarajio na hamu kubwa juu ya kitu fulani kitokee. Lakini pia inaweza kumaanisha kutokuwa na uhakika kwamba kitu fulani kitatokea. Katika Biblia, neno matumaini lina maana ya matarajio. mfano, matumaini yangu yako katika Bwana. Ina maana ya kuwa na matarajio ya kupokea kile ambacho Mungu amewaahidi watu wake. Wakati mwingine neno 'matumaini' laweza kutafsiriwa kama 'uhakika' au hali ya kujiamini. Hasa katika Agano Jipya neno uhakika hutumika zaidi kuonesha matumaini waliyo nayo watu waliomwamini Yesu juu ya kupokea ahadi walizoahidiwa na Mungu.

Mapendekezo ya tafsiri katika mazingira tofauti, neno ' tumaini' lina maana ya ' kutaka ' au kutamani' au kutarajia. Maneno kama ' hakuna cha kutumaini' yana maana ya ' hakuna cha kutegemea. Maneno kama 'mtegemee Mungu' yana maana ya 'mtumaini Mungu.

mbingu, anga, mbinguni

Ufafanuzi

Neno linalotafsiriwa kama "mbingu" hurejelea mahali anapoishi Mungu. Neno hilo hilo laweza kumaanisha " anga" kwa kutegemea na muktadha. Neno 'mbingu' hurejelea kila kitu tunachokiona juu mawinguni kama vile jua, mwezi, na nyota. Inaweza pia kujumuisha vitu vingine vya anga la mbali kama vile sayari, vitu ambavyo hatuwezi kuviona tukiwa hapa duniani. Neno "anga' hurejelea anga la bluu lililo juu ya dunia ambalo lina mawingu na hewa tunayopumua. Mara kwa mara, jua na mwezi husemwa kuwa ziko 'juu angani. Neno 'mbingu' laweza kumaanisha 'anga' au sehemu ambako Mungu anaishi' hii hutegemea na muktadha mbalimbali. Wakati neno 'mbingu' linapotumika kama tamathali ya semi, humrejelea Mungu mwenyewe. Kwa mfano, Mathayo anapoandika juu ya 'ufalme wa mbinguni' anarejelea ufalme wa Mungu.

Mapendekezo ya tafsiri Wakati neno 'mbingu' linapotumika kimfano laweza kutafsiriwa kama 'Mungu" Maneno 'mbingu' au " vitu vya kimbingu' yaweza kutafsiriwa kama 'jua, mwezi na nyota. Kirai "nyota za mbinguni" chaweza kutafsiriwa kama " nyota za angani."

Mchungaji

Ufafanuzi

Mchungaji inatumika kama cheo cha mtu ambaye ni kiongozi wa kiroho wa kundi fulani la waamini.

- Katika toleo la Biblia kwa Kingereza neno "mchungaji" limeonekana mara moja katika kitabu cha Waefeso.
- Katika lugha zingine neno mchungaji ni sawa sawa na neno mchungaji wa kundi fulani la wanyama.
- Yesu pia anafananishwa na mchungaji mwema.

Mfalme wa Wayahudi

Ufafanuzi

Usemi, "Mfalme wa Wayahudi" ni jina linalomaanisha Yesu, Masihi.

Mara ya kwanza Biblia inaandika hili jina wakati linapotumika na wanaume wenye hekima waliosafiri kwenda Bethlehemu wakimtafuta mtoto aliye "Mfalme wa Wayahudi." Malaika alimfunulia Mariamu kuwa mwanaye, mzawa wa mfalme Daudi, atakuwa mfalme ambaye ufalme wake utadumu milele. Kabla Yesu hajasulibishwa, askari Wakirumi walimdhihaki Yesu kwa kumuita "Mfalme wa Wayahudi." JIna hili liliandikwa pia katika kipande cha mbao na kupigwa msumari juu ya msalaba wa Yesu. Yesu kweli ni Mfalme wa Wayahudi na mfalme wa viumbe vyote.

Mfano

Ufafanuzi

"Mfano" ni simulizi fupi au somo fulani linalotumika kuelezea au kufundisha ukweli wa maadili.

- Yesu alitumia mifano akiwafundisha wanafunzi wake. Japokuwa pia aliwaambia mifano makutano ya watu, mara nyingi hakuielezea mifano.
- Mfano ulitumika kuonesha ukweli kwa wanafunzi wake wakati akificha ukweli huo kwa watu kama Mafarisayo ambao hawakumwamini Yesu.
- Nabii Nathani alimwambia Daudi mfano wa kumuonesha mfalme dhambi zake.
- Simulizi ya msamaria mwema ni moja ya mfano. Mfano wa Yesu wa viriba vipya na vya zamani ni moja ya mfano kama somo kwa wanafunzi wake ili kuwasaidia kuelewa mafundisho ya Yesu.

mfano wa Mungu, mfano

Ufafanuzi

Neno "mfano" inamaanisha kitu kinachofanana na kitu kingine au ni kama tabia ya mtu au asili yake. Neno "mfano wa Mungu" inatumika katika njia tofauti, kulingana na mazingira.

Katika mwanzo wa nyakati, Mungu aliwaumba binadamu "katika mfano wake", ambayo ni "kwa kumfanana." Hii inamaanisha kuwa binadamu wana sifa fulani zinazoonesha mfano wa Mungu, kama uwezo wa kusikia hisia, uwezo wa kufikiri na kuwasiliana, na roho inayoishi milele. Biblia inafundisha kwamba Yesu, Mwana wa Mungu, ni "mfano wa Mungu," kwamba yeye ni Mungu mwenyewe. Tofauti na binadamu, Yesu hakuumbwa. Kutoka milele yote. Mungu Mwana ana sifa zote za Mungu kwa sababu ana asili sawa na ya Mungu Baba.

mfuasi

Ufafanuzi

Msemo wa "mfuasi" una maana ya mtu anayetumia muda mwingi na mwalimu, akijifunza kutoka kwa tabia na mafunzo ya mwalimu huyo.

Watu waliomfuata Yesu, wakimsikiliza mafundisho yake na kuyatii, walijulikana kama "wanafunzi" wake.

Yohana Mbatizaji pia alikuwa na wanafunzi.

Katika kipindi cha huduma ya Yesu, kulikuwa na wanafunzi wengi waliomfuata na kusikiliza mafunzo yake.

Yesu alichagua watume kumi na wawili wawe wafuasi wake wa karibu; wanamume hawa wakaja kujulikana kama "mitume" wake.

Watume kumi na wawili waliendelea kujulikana kama "wanafunzi" wake au "wale kumi na wawili".

Kabla tu ya Yesu kwenda juu mbinguni, aliwaamuru wanafunzi wake kuwafundisha watu wengine juu ya kuwa wafuasi wa Yesu pia.

Yeyote anayemwamini Yesu na kumtii mafunzo yake anaitwa mfuasi wa Yesu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "mwanafunzi" unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo wenye maana ya "mfuasi" au "mwanafunzi".

Hakikisha ya kwamba tafsiri ya msemo huu haimaanishi mwanafunzi anayejifunza darasani.

Tafsiri ya msemo huu unatakiwa kuwa tofauti na tafsiri ya "mtume".

Mfuniko wa upatanisho

Ufafanuzi

Mfuniko wa upatanisho ulikuwa mfuniko wa dhahabu uliotumika kufunika juu ya sanduku la agano.

- Mfuniko wa agano ulikuwa na sentimeta 115 urefu na 70 upana.
- Juu ya mfuniko wa upatanisho kulikuwa na Makerubi wawili wa dhahabu wakiwa wameshika na mabawa yao.
- Yahweh alisema atakutana na Waisraeli juu ya mfuniko wa upatanisho chini ya mbawa za makerubi. Kuhani mkuu pekee ndiye aluyeruhusiwa kufanya hivyo na kuwawakilisha watu.
- Mara nyingine Mfuniko wa upatanisho ulijulikana kama kiti cha rehema kwa sababu Mungu alishuka na kuonesha rehema zake kwa watu wenye dhambi na kuwasamehe.

milele

Ufafanuzi

Msemo huu "milele" una maana ya kitu ambacho kitaendelea kuwepo au kutadumu daima.

Msemo "milele" una maana ya hali ya kutokuwa na mwanzo au mwisho. Pia inaweza kumaanisha maisha ambayo hayana mwisho.

Baada ya maisha haya ya sasa ya duniani, binadamu wataishi milele aidha mbinguni na Mungu au jehanamu kutengana na Mungu.

Misemo "maisha ya milele" inatumika katika Agano Jipya kumaanisha kuishi milele pamoja na Mungu mbinguni.

Msemo "milele na milele" ina wazo la muda ambao hauna mwisho na huelezea nini milele au maisha ya milele yakoje.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri "milele" zinaweza kujumuisha "kutokuwa na mwisho" au "kuendelea siku zote".

Msemo "maisha ya milele" unaweza kutafsiriwa kama "maisha ambayo hayana mwisho" au "maisha ambayo yanaendelea bila kikomo" au "kufufua miili yetu kuishi milele".

Kulingana na muktadha, njia tofauti za kutafsiri "milele" zinaweza kujumuisha "kuwepo nje ya muda" au "maisha yasiyo na mwisho" au "maisha mbinguni".

Pia fikiria namna neno hili linatafsiriwa katika Biblia katika lugha ya taifa.

mkate usiyotiwa chachu

Ufafanuzi

Neno "mkate usiyotiwa chachu" una lina maana mkate unatengenezwa pasipo hamira. Aina huu wa mkate ni bapa kwasababu hauna hamira kuufanya uumuke.

- Mungu alipo wachia Waisraeli kutoka utumwani Misri, aliwaambia wakimbie Misri haraka pasipo kusubiri mkate wao uumuke. Hivyo walikula mkate usiyotiwa chachu na vyakula vyao. Tangu hapo mkate usiyotiwa chachu unatumika kwenye Pasaka zao za mwaka kuwa kumbusha hicho kipindi.
- Maana chachu wakati mwingine utumika kama picha ya dhambi, "mkate usiyotiwa chachu" una wakilisha ondoleo la dhambi kwenye maisha ya mtu ilikuweza ishi namna inayo mpendeza Mungu.

Mkono wa kulia.

Ufafanuzi

Mkono wa kulia humaanisha mahali pa heshima au nguvu ya mkono wa kiume wa mtawala au mtu wa muhimu.

- Mkono wa kulia ulitumika kama alama ya nguvu na mamlaka.
- Biblia inaeleza Yesu amekaa mkono wa kulia wa Mungu Baba kama kichwa cha kanisa na mwenye nguvu ya kutawala viumbe vyote.
- Mkono wa kulia wa mtu ulitumika kuonesha heshima ya pekee unapowekwa kichwani mwa mtu akipewa baraka. (Kama Yakobo alivyombariki Mtoto wa Efraimu, Yusufu)

Mkristo

Ufafanuzi

Baada ya Yesu kurudi mbinguni watu wakaanza kuitwa Wakristo ikiwa na maana ya wafuasi wa Kristo.

- Ilikuwa katika mji wa Antiokia ambapo wafuasi wa Yesu waliitwa Wakristo kwa mara ya kwanza.
- Mkristo ni mtu anayeamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na anayeamini kuwa Yesu anaweza kumuokoa toka kwenye dhambi.
- Katika wakati wa sasa Mkristo ni mtu anayetambulishwa na dini ya Kikristo lakini sio mfuasi wa Yesu kabisa. Hii sio maana ya Mkristo ki Biblia.
- Kwa sabau Mkristo kwenye Biblia inamaanisha mtu anayemwamini Yesu kabisa Mkristo pia anaitwa mwamini.

Mnafiki, unafiki

Ufafanuzi

Neno 'mnafiki' humrejelea mtu ambaye hufanya mambo ili aonekane mwema, ingawa kwa siri hufanya mambo maovu. Neno 'unafiki' hurejelea tabia ambayo huwahadaa watu kwa kufikiri kuwa mtu huyo ni mwenye haki. Wanafiki wanapenda kuonekana wakiwa wanafanya mambo mazuri, hivyo watu hufikiri kuwa ni watu wazuri. Mara kwa mara watu wanafiki huwakosoa watu wengine kwa kufanya mambo yale yale ya dhambi ambayo wao wenyewe huyafanya. Yesu aliwaita Mafarisayo kuwa ni wanafiki kwasababu walifanya matendo ya kidini kama vile kuvaa aina fulani ya nguo na kula chakula fulani, lakini hawakuwa wema na wenye haki kwa watu. Mtu mnafiki huweka wazi makosa ya watu wengine, lakini yeye mwenyewe hakubali makosa yake.

Mapendekezo ya tafsiri Baadhi ya lugha huwa na maneno kama "sura mbili" ambayo hutumika kumrejelea mnafiki au matendo ya mnafiki. Namna nyingine ya kutafsiri neno mnafiki ni "mdanganyifu, mtu anayejifanya, mwongo,"

Mnaziri, Naziri

Ufafanuzi

Neno "Mnaziri" ni mtu aliye toa kiapo cha "Naziri." Sana wanaume wana toa hichi kiapo, pia wanawake waliweza kutoa.

- Mtu aliye toa kiapo cha Naziri alikubali kuto kula chakula au kunywa kinywaji cha mizabibu kwa siku, wiki, au miezi ili kutimiza kiapo. Pia kipindi hicho hakukata nywele na hakukaribia maiti.
- Baada ya muda kupita na kutimiza kiapo, Mnaziri alienda kwa kuhani na kutoa sadaka. Hii ilikuwa ni kukata na kuchoma nywele zake. Pia vizuizi vyote viliondolewa.
- Samsoni ni maarufu katika Agano la Kale aliye kuwa chini ya kiapo cha Naziri.
- Malaika aliye tangaza kuzaliwa kwa Yohana mbatizaji alimwambia Zekaria mwanae hatakunywa kinywaji kikali, iliyo ashiria kuwa Yohana alikuwa chini ya kiapo cha Naziri.
- Mtume Paulo pia kwa wakati moja alichukuwa hichi kiapop, kulingana na kurasa moja katika Matendo.

Moyo

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno 'moyo' limetumika mara nyingi kimfano kurejelea mawazo ya mtu, hisia, tamaa au utashi. Kuwa na 'moyo mgumu' ni msemo wa kawaida wenye maana ya mtu anayemwasi Mungu kwa ukaidi. Msemo "kwa moyo wote'' au '' kwa moyo wangu wote'' una maana ya kufanya kitu kwa kujitoa kikamilifu na kwa uhiari. Msemo mwingine '' weka moyoni" una maana kuchukulia kitu kwa umakini na kukitumia katika maisha. Maneno " kuvunjika moyo'' humwelezea mtu ambaye ana huzuni. Wamekuwa wameumizwa kihisia za ndani

Mapendekezo ya tafsiri Baadhi ya lugha hutumia sehemu tofauti za mwili kama vile 'tumbo' au 'ini' kurejelea mawazo haya. Lugha zingine zaweza kutumia neno moja kuelezea dhana hizi na neno jingine kueleza dhana zingine. kama 'moyo' au sehemu nyingine ya mwili haina maana hii, lugha zingine zaweza kuhitaji kutumia maneno ya moja kwa moja kama vile 'fikra' au 'hisia' au 'tamaa.' Kwa kutegemeana na muktadha, maneno "kwa moyo wangu wote" yaweza kutafsiriwa kama "kwa nguvu zangu zote" au "kwa kujitoa kimamilfu" Maneno kama "weka moyoni" yaweza kutafsiriwa kama 'shughulikia kwa umakini' au fikiria kwa uangalifu" "kuvunjika moyo" ina maana ya kuwa 'mwenye huzuni' au 'kujisikia kuumizwa kwa ndani"

mpendwa

Ufafanuzi

Neno "mpendwa" ni kifungu cha kitabia kinachomweleza mtu anayependa na mwingine.

- Neno "aliyependwa" kwa kawaida limanaanisha "kupendwa" au "anayependwa".
- Mungu anamtaja Yesu kama "Mwanawe mpedwa".
- Katika barua zao kwa makanisa ya Kikristo, mitume mara kwa mara waliwataja waumini wenzao kama "wapendwa."

Maoni ya Ufasiri

- Neno hili pia laweza kufasiriwa kama "mpendwa" au "apendwaye" au "anayependwa sana" au "mpenzi."
- Katika mazingira ya kuzungumzia rafiki wa karibu, yaweza kutafasiriwa kama "rafiki yangu mpenzi" au "rafiki yangu wa karibu." Katika Kiingereza ni kawaida tu kusema, "rafiki yangu mpenzi, Paulo" au Paulo, ambaye ni rafiki yangu mpenzi." Lugha nyingine zaweza kuwa na njia nyingine ya kueleza hali hii.
- Angalia kwamba neno "mpendwa" linatokana na neno la upendo wa Mungu, ambao hauna masharti, ubinafsi, na wa kujitoa.

Mpinga Kristo

Ufafanuzi

"Mpinga Kristo" linamaanisha mtu au mafundisho ambayo ni kinyume na Yesu Kristo na kazi zake. Wapo wapinga Kristo wengi sana duniani.

- Mtume Yohana anaandika kwamba mtu anaweza kuwa mpinga Kristo pale anapowapotosha watu kwa kuwaambia kuwa Yesu sio Masihi na kukataa kuwa Yesu ni Mungu.
- Biblia pia inatufundisha kuwa kuna roho ya mpinga Kristo duniani ambayo inapinga kazi za Mungu.
- Kitabu cha ufunuo kinaeleza kuwa kutakuwa na mtu atakayeitwa "mpinga Kristo" atakayejidhihirisha siku za mwisho. mtu huyu atajaribu kuwaangamiza watu wa Mungu Yesu atamshinda.

mpumbavu, upumbavu, upuuzi

Ufafanuzi

Msemo "mpumbavu" una maana ya mtu ambaye mara kwa mara hutengeneza uchaguzi mbaya, haswa kuchagua kutokutii. Msemo "upumbavu" unaelezea mtu au tabia ambayo siyo ya hekima.

Katika Biblia, msemo "mpumbavu" mara kwa mara una maana ya mtu ambaye haamini au kumtii Mungu. Mara nyingi hii hutofautishwa na mtu mwenye hekima, ambaye humwamini Mungu na kumtii.

Katika Zaburi, Daudi anaelezea mtu mpumbavu kama mtu ambaye hamwamini Mungu, ambaye hupuuza ushahidi wote wa Mungu na uumbaji wake.

Kitabu cha Agano la Kale cha Mithali pia hutoa maelezo mengi ya mpumbavu ni nani, mtu mpumbavu yukoje.

Msemo "upuuzi" una maana ya tendo ambao sio la hekima kwa sababu ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Mara nyingi "upuuzi" pia hujumuisha maana ya kitu ambacho ni cha kudharaulika au hatari.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "mpumbavu" unaweza kutafsiriwa kama "mtu mpumbavu" au "mtu asiye na hekima" au "mtu asiyejitambua" au "mtu asiyemcha Mungu"

Njia za kutafsiri "mpumbavu" zinawvza kujumuisha "upungufu wa uelewa" au "kutokuwa na hekima" au "kutojitambua".

Msalaba

Ufafanuzi

Katika Biblia msalaba ni mbao iliyosimama wima inayochimbiwa kwenye ardhi na yenye mbao nyingine inayopita kwa mlalo na inayoshikizwa karibu na juu.

- Katika wanyati wa utawala wa Rumi serikali ya Rumi ilimhukumu mhalifu kwa kumgongelea msalabani na kumuacha afe hapo.
- Yesu alihukumuwa bila kosa na walimuua msalabani.

mtakatifu

Ufafanuzi

Neno "mtakatifu'' ni jina ambalo katika Biblia mara zote humrejelea Mungu. Katika Agano la kale, jina hili mara kwa mara lilitokea katika kirai ''mtakatifu wa Israeli" Katika Agano Jipya, jina mtakatifu lilitumika kumrejelea Yesu Mara nyingine katika Biblia, neno mtakatifu hutumika kumrejelea malaika.

mtukufu

Ufafanuzi

Neno "mtukufu" la husu ukubwa na utukufu, mara nying katika sifa za mfalme.

- Katika Biblia, "mtukufu" mara nyingi la husu ukuu wa Mungu, ambaye ndiye mtawala wa ulimwengu.
- "mtukufu" ni namna ya kumwita mfalme katika mazungumzo.

Mtume, utume

Ufafanuzi

Mitume walikuwa watu waliotumwa na Yesu kuhubiri kuhusu ufalme wa Mungu. Utume ni nafasi au mamlaka ya wale waliochaguliwa kuwa mitume.

- "Mtume" maana yake ni mtu aliyetumwa kwa ajili ya lengo maalumu. Mtume ana mamlaka sawa na ya yule aliyemtuma.
- Kwa nguvu za Mungu, Mitume waliweza kuhubiri injili na kuponya watu na kuwatoa watu mapepo.

muhudumu, huduma

Ufafanuzi

Katika Biblia, maneno "muhudumu" na "huduma" ya husu kutumikia wengine kwa mafundisho kuhusu Mungu na kujali mahitaji yao ya kiroho. Neno "muhudumu" pia laweza eleza mtu anaye tumikia watu kwa namna hii.

- Katika Agano la Kale, makuhani "walitumika" kwa Mungu ndani ya hekalu kwa kutoa sadaka za dhabihu kwake.
- "Huduma" zao pia ilihusisha kuhudumia hekalu na kutoa maombi kwa Mungu kwa niaba ya watu.
- Katika Agano Jipya, "muhudumu" wa injili alikuwa mtu aliye fundisha watu wengine ujumbe wa wokovu kupitia imani ya Yesu. Wakati mwingine muhudumu anatwa "mtumishi"
- Kazi ya kuhudumu kwa watu yaweza maanisha kuwatumikia kiroho kwa kuwa fundisha kuhusu Mungu.

Mungu

Ufafanuzi

Katika Biblia, msemo "Mungu" una maana ya kiumbe wa milele ambaye aliumba ulimwengu bila chochote. Mungu alikuwepo kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Jina binafsi la Mungu ni "Yahwe".

Mungu mara zote alikuwepo; alikuwepo kabla ya kitu chochote kuwepo, na ataendelea kuwepo milele.

Yeye ni Mungu mmoja wa kweli na ana mamlaka juu ya kila kitu ulimwenguni.

Mungu ana haki timilifu, hekima isiyo na mwisho, mtakatifu, bila dhambi, wa haki, wa rehema, na upendo.

Ni Mungu wa kutunza agano, ambaye hutimiza ahadi zake daima.

Watu waliumvwa kumwabudu Mungu na ni yeye pekee wanaopaswa kumwabudu.

Mungu alifunua jina lake kama "Yahwe" ambayo ina maana ya "yeye ni" au "Mimi ni" au "Yule anayekuwepo daima".

Biblia pia hufundisha kuhusu "miungu" wa uongo ambao ni sanamu wasioishi ambao watu huabudu kwa makosa.

Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba

Ufafanuzi

Misemo, "Mungu Baba" na "Baba wa mbinguni" ina maana ya Yahwe, Mungu mmoja wa kweli. Msemo huu hujitokeza kama "Baba" haswa pale Yesu anamaan ya yeye.

Mungu alikuwepo kama Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Kila mmoja ni Mungu kamili, na bado wote ni Mungu mmoja. Hii ni siri ambayo binadamu wa kawaia hawezi kuelewa kikamilifu.

Mungu Baba alimtuma Mungu Mwana (Yesu) duniani na yeye humtuma Roho Mtakatifu kwa watu wake.

Yeyote anayemwamini Mungu Mwana anakuwa mtoto wa Mungu Baba, na Mungu Roho Mtakatifu huja kuishi ndani ya mtu huyo. Hii ni siri nyingine ambayo binadamu hawawezi kuelewa kikamilifu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika msemo "Mungu Baba" ni bora kutafsiri "Baba" na neno sawa ambalo lugha hutumia kikawaida kumaanisha baba wa kimwili.

Msemo "Baba wa mbinguni" unaweza kutafsiriwa na "Baba anayeishi mbinguni" au "Baba Mungu ambaye anaishi mbinguni" au "Mungu Baba kutoka mbinguni".

Kawaida "Baba" inaandikwa kwa herufi kubwa, kuonyesha ya kwamba hii inamaanisha Mungu.

mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike

Ufafanuzi

Mungu wa uongo ni kitu ambacho watu huabudu badala ya Mungu mmoja wa ukweli. Msemo "mungu wa kike" una maana haswa kwa mungu wa uongo wa kike.

Miungu hawa wa uongo hawapo. Yahwe ni Mumngu wa pekee.

Watu mara kwa mara hutengeneza vitu kuwa sanamu ili kuabudu kama ishara ya miungu yao ya uongo.

Katika Biblia, watu wa Mungu mara kwa mara waligeuka kutoka kumtii yeye ili kuabudu miungu ya uongo.

Mapepo mara kwa mara hudanganya watu kuamini ya kwamba miungu ya uongo na sanamu wanazoabudu ina nguvu.

Baali, Dagoni, na Moleki walikuwa miungu watatu wa uongo ambao waliabudiwa na watu katika kipindi cha Biblia.

Ashera na Artemi (Diana) walikuwa miungu wa kike wawili ambao watu wa zamani waliwaabudu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kunaweza kuwa tayari na neno kwa ajili ya "mungu" au "mungu wa uongo" katika lugha yako.

Msemo "sanamu" unaweza kutumika kumaanisha miungu wa uongo.

Katika Kiingereza, herufi ndogo ya "m" inatumika kumaanisha miungu wa uongo, na herufi kubwa ya "M" hutumika kwa ajili ya Mungu wa ukweli. Lugha zingine pia hufanya hivi.

Njia nyingine inakuwa kutumia neno tofauti kabisa kumaanisha miungu wa uongo.

Baadhi ya lugha zinaweza kuongeza neno kuelezea kama mungu wa uongo ni wa kiume au wa kike.

muujiza, ajabu, ishara

Ufafanuzi

"Muujiza" ni kitu kinacho shangaza ambacho hakiwezekani pasipo Mungu kusababisha kitokee.

- Mifano ya miujiza Yesu aliyo fanya ni kutuliza dhoruba na kumponya kipofu.
- Miujiza wakati mwingine inaitwa "maajabu" kwasababu ina sababisha watu kujawa na mshangao au kustaajabika.
- Neno "ajabu" pia laweza kwa ujumla kueleza nguvu za Mungu, kama alivyo umba mbingu na nchi.
- Miujiza pia ya weza itwa "ishara" kwasababu inatumika kama kiashiria au ushaidi kwamba Mungu ni mwenye nguvu kamilifu juu ya ulimwengu.
- Miujiza mingine ilikuwa matendo ya urejesho wa Mungu, kama vile alipo waokoa Waisraeli kutoka utumwani Misri na alipo mlinda Danieli kuto umizwa na simba.
- Maajabu mengine yalikuwa matendo ya hukumu ya Mungu, kama alivyo tuma garika ulimwenguni kote kipindi cha Nuhu na alipo leta mapigo katika nchi ya Misri kipindi cha Musa.
- Miujiza mingi ya Mungu ilikuwa uponyaji wa mwili wa wagonjwa au kuleta wafu kuwa hai.

mwaminifu, uaminifu

Ufafanuzi

Kuwa "mwaminifu" kwa Mungu ina maana kuwa na desturi ya kuishi kulingana na mafunzo ya Mungu. Ina maana ya kuwa mwaminifu kwake na kumuamini. Hali ya kuwa mwaminifu ni "uaminifu".

Mtu ambaye ni mwaminifu anaweza kuaminiwa kuweza kushika ahadi zake na kutimiza majukumu yake daima kwa watu wengine.

Mtu mwaminifu huvumilia katika kutenda kazi, hata pale ambapo ni ndefu au ngumu.

Uaminifu kwa Mungu ni matendo ya daima ya kutenda ambacho Mungu anatutaka kufanya.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika muktadha nyingi, "mwaminifu" inaweza kutafsiriwa kama "uaminifu" au "kujitolea" au "kutegemea".

Katika muktadha zingine, "mwaminifu" inaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo ambao una maana ya "kuendelea kuamini" au "kuvumilia katika kuamini na kumtii Mungu".

Njia ambazo "uaminifu" inaweza kutafsiriwa inaweza kumaanisha "kuvumilia katika kuamini" au "uaminifu" au "kuamini na kumtii Mungu".

Mwana wa Adamu, mwana wa adamu

Ufafanuzi

Jina, "Mwana wa Adamu" lilitumika na Yesu akijieleza. Mara nyingi alitumia hili jina badala ya kusema "mimi."

- Katika Biblia, mwana wa adamu" ina weza kuwa ya kumueleza mtu au kumtaja mtu. Yaweza pia maanisha "binadamu."
- Katika Agano la Kale la kitabu cha Ezekieli, Mungu mara nyingi anamtaja Ezekieli kama "mwana wa adamu." Kwa mfano anasema, "Wewe, mwana wa adamu, utabiri."
- Nabii Danieli aliona maono ya "mwana wa adamu" akija na mawingu, ambayo ni mfano wa kuja kwa Mesiya.
- Yesu pia alisema Mwana wa Adamu atarudi siku moja na mawingu.

Mwana wa Mungu, Mwana

Ufafanuzi

Neno "Mwana wa Mungu la husu Yesu, Neno la Mungu aliye kuja duniani kama binadamu. Anajulikana kama "Mwana."

- Mwana wa Mungu ana tabia moja na Mungu Baba, na ni Mungu timilifu.
- Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu yote ni maana moja.
- Tofauti na wana wa binadamu, Mwana wa Mungu alikuwepo siku zote.
- Mwanzo, Mwana wa Mungu alikuwepo katika uumbaji wa ulimwengu, pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.
- Kwasababu Yesu ni Mwana wa Mungu, na penda na kumtii Baba yake, na Baba yake anampenda.

mwana, mwana wa

Ufafanuzi

Neno "mwana" la husu mvulana au mwanaume na wazazi wake. La weza eleza mzao wa kiume wa mwanaume au mwana aliye pangwa.

- "Mwana" ni linatumika sana kifumbo katika Biblia kueleza mzao wa kiume, kama mjukuu au kitukuu.
- Neno "mwana" pia la weza kama rasmi ya kumtaja mvulana au mwanaume aliye mdogo.
- Wakati mwingine "wana wa Mungu" lina tumika katika Agano Jipya kueleza waamini wa Yesu.
- Mungu anamuita Israeli "mwana wake wa kwanza." Hii yaeleza Mungu kuchagua taifa la Israeli kuwa watu wake maalumu. Ni kupitia wao kuwa ujumbe wa Mungu wa wokovu ulikuja, kwa matokeo kwamba wengi wamekuwa wana wake wa kiroho.
- Maneno "mwana wa" mara nyingi ina maana ya kimafumbo, "kuwa na tabia ya."
- Maneno "mwana wa" pia linatumika kueleza baba wa mtu. Hili neno linatumika katika vizazi na sehemu nyingine.

mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu

Ufafanuzi

Neno "mwanakondoo" linamaanisha kondoo mchanga. Kondoo ni wanyama wenye miguu minne na wana nywele nene ya sufu, waliotumika kwa sadaka kwa Mungu. Yesu anaitwa "Mwanakondoo wa Mungu" kwa sababu alitolewa kulipia dhambi za watu.

Wanyama hawa huongozwa nje ya mstari kirahisi na wanahitaji ulinzi. Mungu anawafananisha binadamu na kondoo. Mungu anawaagiza watu wake kutoa sadaka kimwili kama kondoo na wanakondoo kamili kwake. Yesu anaitwa "Mwanakondoo wa Mungu" aliyetolewa sadaka kwa ajili ya dhambi za watu. Alikuwa sadaka kamili, bila kasoro kwa sababu alikuwa hata dhambi kabisa.

mwandishi, mtaalamu katika sheria ya Kiyahudi

Ufafanuzi

Waandishi walikuwa wasimamizi waliyo wajibika katika kuandika au kunakili nyaraka muhimu za serikali au za kidini kwa mkono. Jina lingine la mwandishi wa Kiyahudi ni "mtaalamu katika sheria ya Kiyahudi."

- Waandishi waliwajibika kunakili na kutunza vitabu vya Agano la Kale.
- Pia walinakili, hifadhi, na kutafsiri maoni ya kidini na maelezo katika sheria ya Mungu.
- Wakati mwingine, waandishi walikuwa wasimamizi muhimu wa serikali.
- Waandishi muhimu katika Biblia walikuwa Baruku na Ezra.
- Katika Agano Jipya, neno "waandishi" lina tafsiriwa pia kama "waalimu wa sheria"
- Katika Agano Jipya, waandishi walikuwa sehemu ya makundi ya kidini yaliyo itwa "Mafarisayo" na makundi haya mawili mara nyingi utajwa pamoja.

Mwenyezi

Ufafanuzi

"Mwenyezi" linamaanisha "nguvu yote. Kwenye Biblia inamaanisha Mungu. Cheo "mwenyezi" linamuelezea Mungu na kudhihirisha kuwa ana nguvu zote na mamlaka kwa kila kitu.

- Pia linatumika kumuelezea Mungu kwa cheo chake "Mwenyezi Mungu" au Mungu Mwenyezi" au "Bwana Mwenyezi" au "Bwana Mungu Mwenyezi"

mwili

Ufafanuzi

Katika Biblia, msemo "mwili" una maana ya tishu laini ya mwili wa mwanadamu au mnyama.

Biblia pia hutumia msemo "mwili" kitamathali kumaanisha wanadamu wote au viumbe wote.

Katika Agano Jipya, msemo "mwili" unatumika kumaanisha asili ya dhambi ya wanadamu. Hii hutumika mara kwa mara kinyume na asili yao ya kiroho.

Msemo, "mwili na damu yake" ina maana ya mtu ambaye anahusiana kibiolojia na mtu mwingine, kama vile mzazi, ndugu, mtoto au mjukuu.

Msemo "mwili na damu" pia unaweza kumaanisha mababu au vizazi vya mtu.

Msemo "mwili mmoja" una maana ya muungano wa kimwili wa mwanamume na mwanamke katika ndoa.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika muktadha wa mwili wa mnyama, "mwili" unaweza kutafsiriwa kama "mwili" au "ngozi" au "nyama".

Inapotumika kumaanisha viumbe wote hai, msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "viumbe hai" au "kila kitu chenye uhai".

Inapomaanisha kwa jumla watu wote, msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "watu" au "binadamu" au "kila mtu anayeishi".

Msemo "mwili na damu" unaweza kutafsiriwa kama "jamaa" au "familia" au "ndugu wa karibu" au "ukoo wa familia". Kunaweza kuwa na muktadha ambapo inaweza kutafsiriwa kama "mababu" au "vizazi".

Baadhi ya lugha zinaweza kuwa na msemo ambao unafanana na "mwili na damu".

Msemo "kuwa mwili mmoja" unaweza kutafsiriwa kama "kuungana kimapenzi" au "kuwa kama mwili mmoja" au "kuwa kama mtu mmoja kimwili na roho". Tafsiri ya msemo huu unaweza kuangaliwa kuhakikisha inakubalika katika lugha na utamaduni wako.

mwinjilisti

Ufafanuzi

"mwinjilisti" ni mtu ambaye huwaambia watu wengine habari njema juu ya Yesu Kristo.

Maana halisi ya "mwinjilisti" ni "mtu ambaye anahubiri habari njema".

Yesu aliwatuma mitume wake kusambaza habari njema kuhusu namna ya kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu kupitia kumuamini Yesu na sadaka yake kwa ajili ya dhambi.

Wakristo wote wanashawishiwa kutangaza hii habari njema.

Baadhi ya Wakristo wanapatiwa karama maalumu kuwaambia kwa ufasaha watu wengine injili. Watu hawa wanasemwa kuwa na karama ya uinjilisti na wanaitwa "wainjilisti".

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "mwinjilisti" unaweza kutafsiriwa kama, " mtu anayehubiri habari njema" au "mwalimu wa habari njema" au "mtu ambaye anatangaza habari njema"

Mwokozi

Ufafanuzi

Neno "Mwokozi" lina husu mtu anaye okoa au komboa wengine na hatari. Pia yaweza maanisha mtu anaye wapa wengine uwezo au waitaji yao.

- Katika Agano la Kale, Mungu anatajwa kama Mwokozi wa Waisraeli kwasababu mara nyingi aliwaokoa na maadui zao, akawapa uwezo, na kuwapa maitaji yao.
- Katika Agano Jipya, "Mwokozi" linatumika kama elezo au cheo cha Yesu Kristo kwasababu anaokoa watu kutoadhibiwa milele kwa dhambi zao. Pia ana waokoa na kutawaliwa na dhambi zao.

Myahudi, Yahudi, Wayahudi

Ufafanuzi

Wayahudi ni watu ambao ni uzao wa mjukuu wa Abrahamu, Yakobo. Neno "Yahudi" linatoka katika neno "Yuda"

Watu walianza kuwaita Waisraeli "Wayahudi" baada ya kurudi Yuda kutoka katika uhamisho kutoka Babeli. Yesu Masihi alikuwa Myahudi. Isipokuwa, viongozi wa dini wa Kiyahudi walitaka kwamba auliwe. Mara nyingi msemo "Wayahudi" inamaanisha viongozi wa Wayahudi, sio watu wote Wayahudi. Kwa mazingira hayo, tafsiri zingine huongeza "viongozi wa" kuiweka wazi.

Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

Ufafanuzi

"Nabii ni mtu anayesema ujumbe wa Mungu kwa watu. Mwanamke anayefanya hivi anaitwa "nabii mwanamke."

- Mara nyingi manabii waliwaonya watu kuacha dhambi zao na kumtii Mungu.
- Unabii ni ujumbe unaozungumzwa na nabii.
- Ujumbe wa unabii mara nyingi ulikuwa unahusu mambo yatakayotokea hapo baadae.
- Unabii mwingi wa agano la kale umeshatimia.
- Katika Biblia mkusanyiko wa vitabu vilivyoandikwa na manabii mara nyingine vinajulikana kama "manabii."
- Kwa mfano maneno "sheria na manabii" ni namna ya kuelezea maandiko ya kiebrania ambayo yanajulikana kama "agano la kale"
- Jina la zamani la nabii lilikuwa "mwonaji" au "mtu anayeona."
- Mara nyingine "mwonaji" inamana ya nabii wa uongo au mtu anayefanya uganga.

nafsi

Ufafanuzi

Nafsi ni sehemu ya ndani, isiyo onekana ya mtu. Ya husu sehemu isiyo ya kimwili ya mtu.

- Maneno "nafsi" na "roho" yanaweza kuwa mitazamo miwili tofauti, au inaweza kuwa maneno mawili yanayo eleza mtazamo mmoja.
- Mtu anapo kufa, nafsi yake ya acha mwili.
- Neno "nafsi" wakati mwingine utumika kimafumbo kueleza mtu kamilifu. Kwa mfano, "nafsi inayo fanya dhambi" ina maana, "mtu anaye fanya dhambi" na "nafsi yangu imechoka," ina maana "nimechoka"

naivera

Ufafanuzi

Naivera ilikuwa vazi kama aproni iliyovaliwa na makuhani wa Kiisraeli. Ilikuwa na sehemu mbili, mbele na nyuma, amnazo ziliunganishwa pamoja mabegani na kufungwa kuzunguka kiuno na mkanda wa kitambaa.

Aina moja ya naivera ilitengenezwa na sufi ya kawaida na ilivaliwa na makuhani wa kawaida.

Naivera iliyovaliwa na kuhani mkuu ilishonwa maalumu kwa kitani cha dhahabu, bluu, zambarau, na chekundu.

Deraya ya kifua ya kuhani mkuu iliunganishwa na sehemu ya mbele ya naivera. Nyuma ya deraya ya kifuani kulitunzwa Urimu na Thumimu, ambaya yalikuwa mawe yaliyotumiwa kumuuliza Mungu mapenzi yake yalikuwa yapi katika baadhi ya masuala.

Mwamuzi Gideoni kwa upumbavu alitengeneza naivera kwa dhahabu na ikawa kitu ambacho Waisraeli waliabudu kama sanamu.

Nchi ya ahadi

Ufafanuzi

"Nchi ya ahadi" imaonekana tuu katika simulizi za Biblis. Ni namna ya kuelezea nchi ya Kanaani ambayo Mungu aliahidi kumpa Abrahamu na uzao wake.

- Abramu alipokuwa akiishi katika nchi ya Uru Mungu aliwamuri kwenda kuishi katika nchi ya Kanaani. Yeye na uzao wake, Waisraeli waliishi huko kwa miaka mingi.
- Wakata njaa kuu iliposababisha uhaba wa chakula Waisraeli wakahamiaMisri.
- Miaka mia nne baadae Mungu akawaokoa Israeli kutoka utumwani Misri na kuwarudisha katika nchi yao ya Kanaani nchi ambayo aliahidi atawapa.

ndugu

Ufafanuzi

Neno "ndugu" kwa kawaida linamaanisha ndugu wa kiume ambaye wanaunganishwa angalau na mzazi mmoja.

- Katika Agano la Kale, neno "ndugu" lilitumika kama neno la taarifa ya jumla kwa ndugu, kama vile watu wa kabila moja, ukoo, au kikundi.
- Katika Agano Jipya, mitume kwa kawaida walitumia "ndugu" kuwalejerea Wakristo wenzao, wakiwemo wa kike na wa kiume, kwa kuwa waumini wote katika Kristo ni washirika wa familia moja ya kiroho, wakiwa na Mungu kuwa Baba yao wa mbinguni.
- Mara chache katika Agano Jipya, mitume kutumia neno "dada" wanaporejerea hasa kwa Mkristo mwenza aliyekuwa mwanamke, au katika kusisitiza kwamba wote wanaume na wanawake wanajumuishwa. Kwa mfano, Yakobo alisisitiza kwamba anazungumzia waumini wote anaporejerea "ndugu au dada aliye na mahitaji ya chakula au nguo."

Maoni ya Kutafasiri

- Ni vema zaidi kutafasiri neno hili kwa neno halisi litumikalo katika lugha lengwa kurejerea kwa ndugu wa kibayolojia, isipokuwa neno hili linatoa maana potofu.
- Katika Agano la Kale hasa, neno"ndugu" linapotumika kwa ujumla sana kurejerea watu wa familia moja, ukoo, au kikundi, maana pendekezwa ni pamoja na "ndugu" au "wanaukoo" au "Waisraeli wenzao."
- Katika mazingira ya kurejerea kwa washiriki wenzao katika Kristo, neno hili liliweza kutafasiriwa kama, "ngugu katika Kristo" au "ndugu wa kiroho."
- Ikiwa wote, wanaume na wanawake wametajwa na "ndugu" lingetoa maana potofu, hivyo neno la jumla zaidi la kindugu lingetumika ili kuwahusishawa wote wanaume na wanawake.
- Njia nyingine ya kutafasiri neno hili ili kuwahusisha waumini wote wa kiume na wa kike lingekuwa, "waumini wenzao" au "Wakristo wa kike na wa kiume."
- Hakikisha unaangalia mazingira kuamua kwamba ni wanaume pekee wametajwa, au kwamba wote wamehusishwa.

neema, mwenye neema

Ufafanuzi

Neno "neema" lina maana ya msaada au baraka ambayo hutolewa kwa mtu ambaye hajastahili. Msemo "mwenye neema" inamwelezea mtu ambaye huonyesha neema kwa wengine.

Neema ya Mungu kwa wanadamu wenye dhambi ni zawadi ambayo inatolewa bure.

Dhana ya neema pia ina maana ya kuwa na huruma na kusamehe mtu ambaye amefanya kosa au mambo ya kuumiza.

Msemo "kupata neema" ni msemo ambao una maan aya kupokea msaada na rehema kutoka kwa Mungu. Mara nyngi inajumuisha maana ya kwamba Mughu anafurahishwa na mtu na kumsaidia.

Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko

Ufafanuzi

Katika Biblia neno la Mungu ni kitu chochote ambacho Mungu anawaambia wanadamu. Hii ni pamoja na lililoandikwa au kutamkwa. Yesu pia anaitwa "neno la Mungu.

- "Maandiko" ni maandishi . Imetumika tuu katika agano jipya na imeelezea maandiko ya Kiebrania au agano la kale. Maandishi haya yalikuwa ujumbe toka kwa Mungu aliowaambia watu kuandika ili miaka ya baadae watu waweze kuyasoma.
- Neno la Yaweh au neno la Bwana ni ujumbe toka kwa Mungu aliopewa nabii au mtu mwingine katika Biblia.
- Mara nyingine neno hili hutokea kama "neno" au "neno langu" au "neno la Mungu.
- Katika agano jipya Yesu anaitwa "neno" na "neno la Mungu." Cheo hiki kinamaanisha kuwa Yesu alidhihiridha Mungu ni nani kwa sababu yeye ni Mungu.

Nguvu

Ufafanuzi

"Nguvu" ni uwezo wa kufanya jambo au kusababisha mambo yatokee mara nyingi hutumia nguvu. Pia nguvu yaweza kumaanisha watu au roho zenye uwezo wa kusababisha mambo yatokee.

- "Nguvu ya Mungu ni uweza wa Mungu kufanya jambo hasa ambalo ni ngumu kufanywa na mwanadamu.
- Mungu ana nguvu juu ya vyote alivyoviumba.
- Mungu huwapa watu wake nguvuza kufanya anayoyataka ili kwamba wakiponya watu au kufanya miujiza wafanye kwa nguvu za Mungu.
- Kwa sababuYesu na Roho mtakatifu ni Mungu wana hizi nguvu.

nidhamu, nidhamu binafsi

Ufafanuzi

Msemo wa "nidhamu" una maana ya kufundisha watu kutii maelekezo kadhaa ya tabia za maadili.

Wazazi huwafundisha watoto wao kwa kutoa maelekezo ya kimaadili na mwelekeo kwa ajili yao na kuwafundisha kutii.

Vivyohivyo, Mungu huadhibu watoto wake kuwasaidia kuzaa matunda mazuri ya kiroho katika maisha yao, kama vile furaha, upendo, na uvumilivu.

Nidhamu inashirikisha maelekezo yahusuyo jinsi ya kuishi namna ya kumpendeza Mungu, na pia adhabu kwa tabia ambayo ipo kinyume na mapenzi ya Mungu.

Nidhamu binafsi ni njia ya kutumia kanuni za kimaadili na kiroho kwa maisha ya mtu mwenyewe.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kutegemea na muktadha, "nidhamu" inaweza kutafsiriwa kama, "fundisha na kuelekeza" au "ongoza kimaadili" au "adhibu kwa kutenda mabaya".

Nomino ya "nidhamu" inaweza kutafsiriwa kama "mafunzo ya maadili" au "adhabu" au "marekebisho ya maadili" au "mwongozo na maelekezo ya kimaadili".

nyenyekea, unyenyekevu

Ufafanuzi

Neno 'nyenyekea' humwelezea mtu ambaye hufikirii kuwa ni bora kuliko watu wengine. Ni mtu asiye na kiburi au majivuno. Unyenyekevu ni sifa au hali ya kuwa mnyenyekevu. Kuwa mnyenyekevu mbele za Mungu ina maana ya kujua udhaifu na hali ya kutokamilika, huku ukilinganisha na ukuu , hekima na ukamilifu wa Mungu. Mtu anapojinyenyekesha, hujiweka katika daraja la chini. 'Unyenyekevu' ni hali ya kujali mahitaji ya watu wengi kuliko mahitaji yako binafsi. Kirai 'uwe mnyenyekevu' kinaweza kutafsiriwa kama ' ''usiwe mwenye kiburi/majivuno.'' "Nyenyekea mbele za Mungu'' ina maana ya " wasilisha utashi wako kwa Mungu, kwa kuutambua ukuu wake.

Nyumba ya Mungu, Nyumba ya Yahweh

Ufafanuzi

Katika Biblia, vifungu vya maneno "nyumba ya Mungu'' na "nyumba ya Yahweh'' hurejelea sehemu ambapo Mungu huabudiwa'' au 'sehemu ya kumwabudia Mungu.' Neno hili piakimahususi laweza kurejelea 'hema la kukutania au hekalu' Wakati mwingine neno 'nyumba ya Mungu' humaanisha ''watu wa Mungu"

Mapendekezo ya tafsiri Wakati neno la nyumba ya Mungu linaporejelea sehemu ya kuabudia ina maana ya 'nyumba au sehemu ya kumwabudia Mungu.

okoa, salama

Ufafanuzi

Neno "okoa" la husu kumzuia mtu kutopitia kitu kibaya au cha hatari. Kuwa "salama" ya maanisha kulindwa na hatari au majanga.

- Kwa hali ya kawaida, watu wanaweza okolewa au kombolewa kutoka kwenye hatari, au kifo.
- Katika hali ya kiroho, kama mtu ameokolewa ina maana kupitia kifo cha Yesu msalabani, Mungu amemsamehe na kumkomboa kutoadhibiwa jehanamu kwa dhambi zake.
- Watu wanaweza okoa au kukomboa watu na hatari, lakini Mungu tu anaweza okoa watu kutoadhibiwa milele kwa dhambi zao.

ombea, sala ya kuombea

Ufafanuzi

Msemo "ombea" na "sala ya kuombea" inamaanisha kufanya maombi kwa mtu kwa niaba ya mtu mwingine. Katika Biblia hii kawaida humaanisha kuwaombea watu wengine.

Usemi "kuomba kwa ajili ya" na "kuombea" inamaanisha kufanya maombi kwa Mungu kwa faida ya watu wengine. Biblia inafundisha kuwa Roho Mtakatifu hutuombea, kwamba, humsihi Mungu kwa ajili yetu. Mtu huombea watu wengine kwa mtu mwenye mamlaka.

omboleza, maombolezo

Ufafanuzi

usemi "omboleza" na "maombolezo" yanamaanisha hisia kali ya kulia, majonzi au huzuni.

Wakati mwingine hii ni pamoja na kujuta kwa kina kwa ajili ya dhambi, au huruma kwa watu waliopitia maafa. Maombolezo yanaweza kujumuisha kulia, kutoa machozi au kulia kwa sauti.

Onesha, ufunuo

Ufafanuzi

Kuonesha ni kusababisha kitu fulani kujulikana. Ufunuo ni kitu kilichojulikana.

- Katika Biblia "kuonesha" limetumika kuelezea namna ambayo Mungu alijionesha mwenyewe kwa watu.
- Mungu alijionesha mwenyewe kupitia kila kitu alichokiumba na kwa kupitia mawasiliano na watu kwa kuzungumzwa na kuandika ujumbe.
- Mungu alijionesha mwenyewe kupitia ndoto na maono.
- Paulo aliposema kwamba amepokea injili kwa "ufunuo toka kwa Yesu Kristo" anamaanisha kuwa Yesu mwenyewe alimuelezea injili.
- Katika agano jipya kitabu cha "ufunuo" kinahusu namna ambayo Mungu anaonesha matukio yatakayotokea siku za mwisho. Aliyaonesha haya kwa mtume Yohana kupitia maono.

Pasaka

Ufafanuzi

"Pasaka " ni jina la sherehe ya kidini ambayo Wayahudi walisherehekea kila mwaka kukumbuka mi kwa namna gani Mungu aliwaokoa mababu zao Waisraeli toka utumwani Misri.

- Jina la sikukuu hii lilitokana na namna ambayo Mungu "alizipita" nyumba za Waisraeli na hakuwaua watoto wake pale alipowaua wazaliwa wa kwanza wa Misri.
- Sikukuu ya pasaka inajumuisha chakula maalumu yaani kondoo mzuri waliomuua na kumpika, pia mkate usio na amira. Vyakula hivi vinawakumbusha chakula walichokula Waisraeli usiku ule kabla ya kuondoka Mirsi.
- Mungu aliwaambia Waisraeli wale chakula hiki kila mwaka kama kumbukumbu na kusherehekea namna ambavyo Mungu "alizipita" nyumba zao na namna alivyowaweka huru toka utumwa nchini Misri.

Pentekoste au sikukuu za majuma

Ufafanuzi

Sikukuu za majuma ilikuwa ni sikukuu ya Kiyahudi iliyofanyika siku hamsini kabla ya Pasaka. Baadae ilikuja kuitwa Pentekoste.

- Sikukuu za majuma ilikuwa wiki sabini (siku hamsini) baada ya sherehe ya matunda ya kwanza. Katika agano jipya sikukuu hii iliitwa "pantekoste."
- Sikukuu za majuma zilikuwa maalumu kwa ajili ya kusherehekea mwanzo wa mavuno ya nafaka. Pia ilikuwa muda wa kumkumbuka siku ambayo Mungu aliwapa sheria Waisraeli katika vibao vya mawe alivyopewa Musa.
- Katika agano jipya siku ya Pentekoste imeelezewa moja kwa moja kwa sababu ilikuwa siku ambayo waliomwamii wa Yesu walipokea roho mtakatifu kwa njia mpya.

pepo mbaya, roho ovu, roho chafu

Ufafanuzi

Misemo hii yote ina maana ya mapepo, ambayo ni viumbe vya roho vinavyopingana na mapenzi ya Mungu.

Mungu aliwaumba malaika kumtumikia. Shetani alipomwasi Mungu, baadhi ya malaika pia waliasi na kutupwa kutoka mbinguni. Inaaminika ya kwamba mapepo na roho mbaya ndio hawa "mailak walioanguka".

Mara kwa mara haya mapepo yanajulikana kama "roho chafu". Msemo "chafu" una maana ya "isiyo safi" au "uovu" au "isiyo takatifu".

Kwa sababu mapepo humtumikia shetani, wanafanya mambo maovu. Mara kwa mara wanaishi ndani ya watu na kuwaendesha.

Mapepo wana nguvu kuliko wanadamu, lakini hawana nguvu kama ya Mungu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo wa "pepo" unaweza kutafsiriwa kama "roho mchafu".

Msemo wa "roho mchafu" unaweza kutafsiriwa kama "roho chafu" au "roho iliyoharibika" au "roho mchafu".

Hakikisha ya kwamba neno au msemo unaotumika kutafsiri msemo huu ni tofauti na msemo unaotumika kumaanisha shetani.

Pia fikiria jinsi msemo wa "pepo" unaweza kutafsiriwa katika lugha ya kawaida au ya taifa.

Rabi, Raboni

Ufafanuzi

Rabi ina maana ya bwana wangu au mwalimu wangu.

- Kilikuwa cheo cha heshima kilichotumiwa kumuelezea mtu aliyekuwa kiongozi wa dini ya Kiyahudi hasi aliyefundisha sheria za Mungu.
- Yohana mbatizaji na Yesu mara nyingine waliitwa Rabi na wanafunzi wao.

rehema

Ufafanuzi

Neno "rehema" lina husu kusaidia mtu waliyo na shida, hususani wanapo kuwa chini au hali ngumu.

- Neno "rehema" linaweza maanisha maana yakuto adhibu watu kitu walicho kosea.
- Mtu mwenye nguvu kama mfalme anaelezwa kama mwenye "rehema" anapo tendea watu wema badala ya kuwaua.
- Kuwa mwenye Rehema ina maana ya kusamehe mtu aliye kukosea.
- Tuna onyesha rehema tunapo saidia watu mwenye shida kubwa.
- Mungu ni wa rehema kwetu, na anataka tuwe na rehema kwa wengine.

rithi, urithi, mrithi

Ufafanuzi

Maneno "rithi" na "urithi" zinamaanisha kupokea kitu cha dhamani kutoka kwa mzazi au mtu mwingine kwa sababu ya uhusiano maalumu na huyo mtu. "Mrithi" ni mtu ambaye anapokea urithi.

Urithi wa halisia ambao unapokelewa unaweza kuwa fedha, ardhi, au aina zingine za mali. Urithi wa kiroho ni vyote ambavyo Mungu huwapa watu wanaomuamini Yesu, zikiwemo baraka za maisha ya sasa pamoja na maisha ya milele pamoja naye. Biblia pia inawaiita watu wa Mungu urithi wake, kinachomaanisha kuwa ni wake, ni mali yake ya dhamani. Mungu alimuahidi Abrahamu na uzao wake kuwa watarithi nchi ya Kanaani, kwamba itakuwa yao milele. Kuna maana ya kitamathali na kiroho ya jinsi watu walio wa Mungu wanasemwa "kurithi nchi." Hii inamaanisha kuwa watafanikiwa na kubarikiwa na Mungu kwa mambo ya kimwili na kiroho. Katika Agano Jipya, Mungu anaahidi kuwa wale wanaomuamini Yesu "watarithi wokovu" na "kurithi uzima wa milele." Pia inaelezwa kama, "kurithi ufalme wa Mungu." Huu ni urithi wa milele unaodumu milele. Kuna maana zingine za kitamathali za haya maneno: Biblia inasema kuwa watu wenye hekima "watarithi utukufu" na watakatifu "watarithi vitu vizuri." "Kurithi ahadi" inamaanisha kupokea vitu vizuri ambavyo Mungu ameahidi kuwapa watu wake. Msemo huu pia unatumika kwa njia ya uhasi kumaanisha watu wapumbavu au wasiotii ambao "wanarithi upepo" au "kurithi upumbavu." Hii inamaanisha wanapokea matokeo ya matendo yao ya dhambi, ikiwemo adhabu na maisha yasiyo na maana.

Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.

Ufafanuzi

Maneno haya yote humrejelea Roho Mtakatifu ambaye ni Mungu. Mungu mmoja na wa kweli aishiye milele katika nafsi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu mara zingine hutajwa kama 'Roho' na 'Roho ya Yahweh' au 'Roho wa ukweli' Roho Mtakatifu ni mtakatifu kwa sababu yeye ni Mungu. Yeye yuko kamili na mwadilifu katika kila jambo alifanyalo. Roho Mtakatifu alishiriki kikamilifu katika uumbaji wa ulimwengu pamoja na Baba na Mwana. Wakati Mwana wa Mungu, Yesu aliporudi mbinguni, Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kwa watu ili awaongoze, kuwafundisha, kuwafariji na kuwawezesha kufunya mapenzi ya Mungu. Roho Mtakatifu alimwongoza Yesu na pia anawaongoza wale wanaomwamini Yesu.

Mapendekezo ya tafsiri Neno hili laweza kutafsiriwa tu kwa kutumia maneno yenye kumaanisha 'roho' na 'mtakatifu' Lakini maneno mengine ambayo yaweza kutumika ni kama 'Roho Safi' au 'Roho aliye Mtakatifu' au 'Mungu Roho.'

roho, kiroho

Ufafanuzi

Neno "roho" la eleza sehemu isiyo ya kimwili ya watu isiyo onekana. Mtu anapo kufa, roho yake inaacha mwili wake. "Roho" inaweza eleza tabia au hali ya kihisia ya mtu.

- Neno "roho" la eleza kiumbe kisicho kuwa na mwili, hususani roho chafu.
- Roho ya mtu ni sehemu yake inayo weza mjua Mungu na kumuamini.
- Kwa ujumla, neno "kiroho" la eleza chochote kisicho katika dunia ya mwili.
- Katika Biblia, sana ueleza chochote kinacho muhusu Mungu, sana Roho Mtakatifu.
- Mungu ni roho na ameumba roho za viumbe wengine wasiyo na miili.
- Malaika ni roho, pamoja na hao waliyo hasi dhidi ya Mungu na kuwa roho chafu.
- Neno "roho ya" la weza maanisha "kuwa na tabia za," kama vile, "roho ya hekima" au "katika roho ya Eliya."
- Mifano ya "roho" kama tabia au hisia itahusisha "roho ya hofu" au "roho ya wivu"

Sabato

Ufafanuzi

Neno "Sabato" la husu siku ya saba ya wiki, ambayo Mungu aliwaamuru Waisraeli waitenge kama siku ya kupumzika na kutofanya kazi.

- Baada ya Mungu kumaliza kuumba dunia kwa siku sita, alipumzika siku ya saba. Kwa namna hiyo hiyo, Mungu aliwaamuru Waisraeli kutenga siku ya saba kama siku maalumu ya kupumzika na kumuabudu.
- Amri "kutakasa Sabato" ni moja ya amri kumi Mungu alizo andika katika jiwe alilo mpa Musa kwa ajili ya Waisraeli.
- Kwa kufuata kanuni ya Wayahudi ya kuhesabu siku, Sabato ya anza Ijumaa jua linapo zama na kudumu hadi Juma Mosi jua linapo zama.
- Wakati mwingine katika Biblia Sabato yaitwa "siku ya Sabato" kuliko tu Sabato.

Sadukayo

Ufafanuzi

Masadukayo walikuwa kikundi cha makuhani wa Kiyahudi kipindi cha Yesu Kristo waliyo unga mkono utawala wa Warumi na ambao hawakuamini ufufuo.

- Masadukayo wengi walikuwa matajiri, Wayahudi wa daraja la juu waliyo shika vyeo vikubwa kama vile chifu kuhani na kuhani mkuu.
- Majukumu ya Masadukayo yali husisha kutunza hekalu na kazi za kikuhani kama kutoa dhabihu.
- Masadukayo na Mafarisayo walishawishi viongozi wa Kirumi kumsulubisha Yesu.
- Yesu alizungumza kuhusu haya makundi mawili ya kidini kwasababu ya ubinafsi na unafiki wao.

Safi, kusafisha

Ufafanuzi

Neno "safi" inamaana ya kawaida ya kutokuwa na uchafu au doa. Katika Biblia hutumika kuwa na maana ya "takatifu" au "kuwa huru na dhambi."

- Kusafisha ni hatua ya kufanya kitu kiwe kisafi. Inaweza kutafsiriwa kama "kuosha" au "kutakasa."
- Katika agano la kale Mungu aliwaambia Waisraeli ni wanyama gani waliokuwa safi na ambao hawakuwa safi. Wanyama wasafi tuu ndio walioruhusiwa kutumika kwa ajili ya chakula na dhabihu.
- Mtu aliyekuwa na ugonjwa fulani wa ngozi hakuwa safi mpaka ngozi yake itakapopona.
- Mara nyingine safi inaweza kutafsiriwa kama kuwa na usafi wa maadili.

safi, kusafisha

Ufafanuzi

Kuwa "safi" inamaana kutokuwa na mapungufu au kutochanganya kitu ndani ya kitu ambacho hakitakiwi kuchanganywa. Kukisafisha kitu ni kitendo cha kukisafisha na kuondoa chochote kinachoweza kuchafua.

- Kwa kutumia sheria za agano la kale "kusafisha" ni kitendo cha kuondoa uchafu kiibada kwenye kitu au mtu kinachoweza kumfanya asiwe msafi kama magonjwa, kutokwa damu au kujifungua.
- Katika agano jipya pia kuna sheria zinazowaambia watu namna ya kujisafisha toka kwenye dhambi hasa kwa kutoa sadaka ya wanyama. Hii ilikuwa ya muda tuu na sadaka hii ilirudiwa mara kwa mara.
- Katika agano jipya kusafishwa ni kitendo cha kusafishwa toka kwenye dhambi.
- Njia pekee ya watu kusafishwa kabisa toka kwenye dhambi ni kwa kutubu dhambi zao na kupokea msamaha wa Mungu kwa kumwamini Yesu.

samehe, kusamehe

Ufafanuzi

Kumsamehe mtu ina maana ya kutokaa na kinyongo dhidi ya mtu ambaye alifanya jambo la kuumiza. "Kusamehe" ni tendo la kumsamehe mtu.

Kumsamehe mtu mara nyingi humaanisha kutomuadhibu mtu huyo kwa jambo ambalo amekosa.

Msemo huu unaweza kutumika kitamathali kumaanisha, "katisha" kama msemo "kusamehe deni".

Watu wanapokiri dhambi zao, Mungu huwasamehe kutokana na sadaka ya kifo cha Yesu msalabani.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kusamehe wengine kama jinsi alivyowasamehe wao.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "samehe" inaweza kutafsiriwa kama "omba radhi" au "katisha" au "achilia" au "kutoshikilia dhidi ya"

Sanduku

Ufafanuzi

Maana ya kawaida ya "sanduku" ni sanduku la mbao la mstatili lililotengenezwa kwa ajili ya kushikilia au kulinda kitu fulani. Sanduku laweza kuwa kubwa au dogo kutokana na matumizi yake.

- Kiingereza cha Biblia "Sanduku" limetumika kwa mara ya kwanza kuonesha kitu kikubwa, mashua ya mbao ya mstatili ambayo Nuhu aliitengeneza ili kuepuka mafuriko. Sanduku lilikuwa na gorofa chini, paa na kuta.
- Njia za kutafsiri neno hili ni kusema "mashua kubwa" au "jahazi" au "meli ya mizigo."
- Kwa Kiebrania neno ambalo linaweza kutumika kuelezea hii meli kubwa ni neno lile lile lililoumika kuelezea kikapu au sanduku lililotumika kumuweka Musa katika mto Nile ili kumficha.
- Katika kuchagua neno la kutafsiri "sanduku" ni muhimu kujua ukubwa na limetumika kwa kazi gani.

Sanduku la agano, Sanduku la Yahweh.

Ufafanuzi

Sanduku la agano ni sanduku la mbao maalumu lililofunikwa na dhahabu na lenye vibao viwili vya mawe vyenye amri kumi. Pia lina fimbo ya Haruni na mana.

- Neno "Sanduku" lina maana ya "chombo."
- Lengo la sanduku hili ni kuwakumbusha Wana wa Israeli agano lao na Mungu.
- Sanduku la agano liliwekwa sehemu takatifu sana.
- Uwepo wa Mungu ulikuwepo juu ya sanduku la agano mahali pa juu katika hema, ambapo aliongea na Musa kwa niaba ya Waisraeli.
- Kipindi ambacho sanduku la agano lilikuwepo patakatifu pa patakatifu, kuhani mkuu pakeyake ndiye aliyeruhusiwa kulisogelea sanduku mara moja kwa mwaka.

Sayuni, Mlima Sayuni

Ufafanuzi

Hapo awali, neno "Sayuni" au "Mlima Sayuni" lilimaanisha ngome ambayo Mfalme Daudi aliiteka kutoka kwa Wayebusi. Majina haya yakawa njia nyingine ya kuitaja Yerusalemu.

- Mlima Sayuni na Mlima Moria ilikuwa milima miwili mji wa Yerusalemu ulipojengwa juu yake. Baadaye, "Sayuni" na "Mlima Sayuni" ikawa ikitumika kama maneno ya jumla kuitaja milima yote na mji wa Yerusalemu. Wakati mwingine pia yalitumika kutaja hekalu lililokuwako Yerualemu. (Tazama: [aina hii ya maana] (https://git.door43.org/Door43/en-ta-translate-vol2/src/master/content/figs_metonymy.md))
- Daudi aliita Sayuni, au Yerusalemu, kama "Mji wa Daudi." Hii ni tofauti na mji wa alikozaliwa Daudi, Bethlehemu, ambao pia uliitwa Mji wa Daudi.
- Neno "Sayuni" limetumika katika njia nyingine za tamathali za semi, kuitaja Israeli au Ufalme wa kiroho wa Mungu au katika mji mpya wa Yerusalemu atakaouanzisha Mungu.

Sehemu takatifu, sehemu takatifu sana (patakatifu pa patakatifu)

Ufafanuzi

Katika Biblia, maneno kama 'sehemu takatifu' na ' sehemu takatifu sana' yanarejelea sehemu mbili za hema la kukutania au jengo la hekalu. 'Sehemu takatifu' ni chumba cha kwanza kilicho na madhabahu ya uvumba na meza iliyo na 'mkate wa uwepo' juu yake. 'Sehemu takatifu sana' (patakatifu pa patakatifu) kilikuwa ni chumba cha pili cha ndani sana kilicho na sanduku la agano. Kulikuwa na pazia kubwa na pana lililotenganisha kati ya chumba cha nje na chumba cha ndani. Kuhani mkuu ndiye pekee aliyeruhusiwa kuingia sehemu takatifu sana yaani Patakatifu pa patakatifu. Wakati mwingine 'sehemu takatifu' hurejelea jengo na sehemu za nje za hekalu au hema la kukutania. Pia neno hili laweza kumaanisha eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya Mungu.

Mapendekezo ya tafsiri Maneno 'sehemu takatifu' yanaweza kutafsiriwa kama "chumba kilichotengwa kwa ajili ya Mungu'' au '' chumba maalumu kwa ajili ya kukutana na Mungu'' au chumba kilichotunzwa kwa ajli ya Mungu. ''sehemu takatifu'' yaweza kujumuisha sehemu iliyotakaswa' au hekaluni.

shawishi, ushawishi

Ufafanuzi

Msemo "shawishi" una maana ya kumsihi mtu kwa nguvu na kumbembeleza mtu kufanya kilicho sahihi. Aini hii ya kusihi inaitwa "kushawishi".

Kusudi la kushawishi ni kusihi watu wengine kuepukana na dhambi na kufuata mapenzi ya Mungu.

Agano Jipya hufundisha Wakristo kujishawishi baina yao kwa upendo, sio kwa ukali au ghafula.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "kushawishi" pia inaweza kutafsiriwa kama "kubembeleza kwa nguvu" au "kusihi" au "kushauri".

Hakikisha tafsiri ya msemo huu hainyoeshi ya kuwa anayeshawishi ana hasira. Msemo unatakiwa kuonyesha nguvu na uzito, lakini usionyeshe kauli ya ukali.

Katika muktadha nyingi, msemo "shawishi" unatakiwa kutafsiriwa tofauti na "kutia moyo" ambayo ina maana ya kutia msukumo, aminisha, au kufariji mtu.

Mara kwa mara msemo huu pia unatafsiriwa tofauti na "onya" ambayo ina maana ya kuonya au kusahisha mtu kwa tabia yake mbaya.

shemasi

Ufafanuzi

Shemasi ni mtu ambaye anatumika katika kanisa lake, akiwasaidia waumini kwa mahitaji ya kiutendaji, kama vile chakula au pesa.

Neno "shemasi" limechukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye neno la Kigiriki lenye maana ya "mtumishi" au "mchungaji".

Tangu kipindi cha Wakristo wa awali, kuwa shemasi ilikuwa ni nafasi na huduma iliyobainishwa katika mwili wa Kanisa.

Kwa mfano, katika Agano Jipya, mashemasi walikuwa wanahakikisha ya kuwa kila pesa au chakula ambacho waumini hutoa zingegawanywa sawa sawa kwa wajane miongoni mwao.

Msemo wa "shemasi" pia unaweza kutafsiriwa kama, "mchungaji wa kanisa" au "mfanyakazi wa kanisani" au "mtumishi wa kanisani", au msemo mwingine ambo unaonyesha ya kwamba mtu huyu amewekwa mahususi kufanya kazi maalumu ambayo ina manufaa kwa jamii yake ya Kikristo.

sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe

Ufafanuzi

Misemo hii yote inamaanisha amri na maelekezo ambayo Mungu alimpa Musa kwa ajili ya Waisraeli kutii. Misemo "sheria" na "sheria ya Mungu" zinatumika pia kwa ujumla kumaanisha kila kitu Mungu anachotaka watu wake kutii.

Kulingana na mazingira, "sheria" inaweza kumaanisha: Amri kumi ambazo Mungu aliandika katika jiwe kwa ajili ya Waisraeli. sheria zote alizopewa Musa vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale. Agano lote la Kale (pia inajulikana kama "maandiko" katika Agano Jipya). maelekezo yote ya Mungu na mapenzi yake. Usemi "sheria na manabii" inatumika katika Agano Jipya kumaanisha maandiko ya Kihebrania (au "Agano la Kale").

Shetani, ibilisi, yule muovu

Ufafanuzi

Ibilisi ni roho hai Mungu aliyo umba, lakini aliasi dhidi ya Mungu na kuwa adui wa Mungu. Ibilisi anaitwa "Shetani" na "yule muovu."

- Ibilisi ana

siku ya Bwana, siku ya Yahwe

Ufafanuzi

Msemo wa Agano la Kale wa "siku ya Yahwe" unatumika kumaanisha kipindi/vipindi maalumu ambapo Mungu angewaadhibu watu kwa dhambi zao.

Msemo wa Agano Jipya wa "siku ya Bwana" huwa una maana ya siku au kipindi ambapo Bwana Yesu atarudi kuwahukumu watu katika wakati wa mwisho.

Huu wakati wa mwisho, wa baadaye wa hukumu na ufufuo, pia hujulikana kama "siku ya mwisho". Kipindi hiki kitaanza pale ambapo Bwana Yesu atakaporudi kuhukumu wenye dhambi na kuunda mamlaka yake ya kudumu.

Neno "siku" katika misemo hii inaweza kumaanisha siku haswa au inaweza kumaanisha "kipindi" au "wakati maalumu" ambao ni mrefu zaidi ya siku moja.

Mara nyingine adhabu huwa ina maana ya "kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu" juu ya wale wasioamini.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, njia zingine za kutafsiri "siku ya Yahwe" zinaweza kujumuisha, "kipindi cha Yahwe" au "kipindi ambapo Yahwe atawaadhibu adui zake" au "kipindi cha hasira ya Yahwe".

Njia zingine za kutafsiri "siku ya Bwana" zinaweza kujumuisha "kipindi cha hukumu ya Bwana" au "kipindi ambacho Bwana Yesu atarudi kuhukumu watu".

siku ya hukumu

Ufafanuzi

Usemi "siku ya hukumu" inamaanisha siku ya usoni ambapo Mungu atamhukumu kila mtu.

Mungu amemfanya Mwanaye, Yesu Kristo, kuhukumu watu wote. Katika siku ya hukumu, Kristo atawahukumu watu kulingana na asili yake ya haki.

siku ya mwisho, siku za mwisho

Ufafanuzi

Usemi wa "siku za mwisho" inamaanisha kwa ujumla kipindi cha mwisho wa muda wa sasa.

Muda huu utakuwa muda usiojulikana. "Siku za mwisho" ni wakati wa hukumu kwa wale waliomgeuka Mungu.

sinagogi

Ufafanuzi

Sinagogi ni jengo la watu wa Kiyahudi wanapo kutania pamoja kumuabudu Mungu.

- Tangu zama za kale, huduma za sinagogi zimekuwa na maombi, kusoma maandiko, na kufundisha kuhusu maandiko.
- Wayahudi walianza jenga masinagogi kama sehemu za kuomba na kumuabudu Mungu katika miji yao, kwasababu wengi waliishi mbali na hekalu lililo Yerusalemu.
- Yesu alifundisha katika masinagogi na kuponya watu.
- Neno "sinagogi" linaweza tumika kifumbo kueleza kundi la watu waliyo kusanyika hapo.

sio na hatia

Ufafanuzi

Usemi "sio na hatia" unamaanisha kutokuwa na hatia la uhalifu au makosa mengine. Inaweza pia kumaanisha kwa ujumla watu ambayo hawahusiki na matendo maovu.

Mtu anayetuhumiwa kwa kufanya kitu kibaya hana hatia kama hataambatanishwa na hilo kosa. Wakati mwingine usemi "sio na hatia" unatumika kumaanisha watu ambao hawajafanya kosa kustahili ubaya wanaoupata, kama jeshi la adui kushambulia "watu wasio na hatia."

stahili, yenye thamani ya, wasiofaa, isiyo na maana

Ufafanuzi

"Stahili" linaelezea mtu au kitu kinachofaa kupewa heshima. "Kustahilisha" inamaana ya kuwa na thamani au muhimu. "isiyo na maana" inamaanisha isiyo na thamani.

- Kustahili inamaana ya kuwa na thamani au kuwa na umuhimu.
- Kutofaa imanaana ya kutostahili kuwa na nafasi maalumu.
- Kuhisi kutothaminiwani kuhisi huna umuhimu zaidi ya mtu mwingine.
- Maneno "wasiofaa" na "isiyo na thamani" yanaendana japokuwa yana maana tofauti. "Kutofaa" inamaana ya kutostahili heshima au kujulikana. "kutokuwa na maana" ni kutokuwa na thamani au lengo."

Sulubisha

Ufafanuzi

Sulubisha inamaana ya kumuhukumu mtu kwa kumuweka msalabani na kumuacha ateseke mpaka afe.

- Mtu huyo anaweza kufungwa msalabani au kugongewa misumari. Watu wanaosulubishwa hufa kwa kupoteza damu nyingi.
- Huko Rumi walitumia sana njia hii kuwaadhibu watu na kuwaua wahalifu au watu walioasi dhidi ya serikali.
- Viongozi wa Kiyahudi walimuomba gavana wa Rumi kuwaamuru askari wake wamsulubishe Yesu. Askari walimweka Yesu msalabani. aliteseka masaa siti kisha akafa.

tahini, pima

Ufafanuzi

Neno "tahini" yaeleza hali ngumu au inayo umiza yenye kudhihirisha uweza na udhahifu wa mtu.

- Mungu pima watu, lakini hawa jaribu. Shetani, vinginevyo ana jaribu watu kufanya dhambi.
- Wakati mwingine Mungu anatumia tahini kuweka wazi dhambi za watu. Kipimo kina msaidia mtu kutogeukia dhambi na kwenda kwa karibu na Mungu.
- Dhahabu na vyuma vinapimwa kwenye moto kugundua usafi na uimara wake. Hii ni picha ya jinsi Mungu anavyo tumia mazingira magumu kujaribu watu.

takasa, utakaso

Ufafanuzi

Kutakasa ni kutenga kando au kufanya takatifu. Utakaso ni hatua ya kufanya takatifu.

- Katika Agano la Kale, baadhi ya watu na vitu vilitakaswa, au kutengwa kando, kwa hudumu ya Mungu.
- Agano Jipya lina fundisha kuwa Mungu anatakasa watu wanao mwamini Yesu. Hiyo ni kwamba, anawafanya watakatifu na kuwatenga kumtumikia.
- Waamini katika Yesu wanaamriwa kujitakasa kwa Mungu, kuwa watakatifu katika kila kitu wanacho fanya.

takatifu

Ufafanuzi

Msemo "takatifu" una maana ya kitu chochote kinachomhusu Mungu.

Baadhi ya njia ambazo msemo huu unatumika ni, "mamlaka takatifu", "hukumu takatifu", "asili takatifu", "nguvu takatifu", na "utukufu mtakatifu".

Katika sehemu moja ndani ya Biblia, msemo "takatifu" unatumika kuelezea jambo juu ya uungu wa uongo.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia za kutafsiri msemo wa "takatifu" zinaweza kujumuisha "ya Mungu" au "kutoka kwa Mungu" au "fungamana na Mungu" au "huonyesha ni ya Mungu".

Kwa mfano, "mamlaka takatifu" inaweza kutafsiriwa kama "mamlaka ya Mungu" au "mamlaka ambayo yanatoka kwa Mungu".

Msemo wa "utukutufu takatifu" unaweza kutafsiriwa kama "utukufu wa Mungu" au "utukufu ambao Mungu ame" au "utukufu unatoka kwa Mungu".

Baadhi ya tafsiri zinapendelea kutumia neno tofauti wanapofafanua jambo ambalo linafungamana na mungu wa uongo.

takatifu, utakatifu

Ufafanuzi

Maneno 'takatifu' na 'utakatifu' hurejelea tabia ya Mungu ambayo imetengwa na kutofautishwa na kila kitu ambacho ni chenye dhambi na kisicho kamili. Mungu pekee ndiye mtakatifu kweli. Hufawafanya watu na vitu kuwa vitakatifu. Mtu aliye mtakatifu ni mali ya Mungu na ametengwa maalumu kwa kusudi la kumtumika Mungu na kumpa utukufu Yeye. Na kitu ambacho Mungu amekitangaza kuwa ni kitakatifu ni kile ambacho Mungu amekitenga kwa ajili ya utukufu wake na matumizi yake, kwa mfano madhabahu ambayo makusudi yake ni kumtolea Mungu sadaka. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu, hakuna mtu awezaye kumkaribia Mungu isipokuwa awe ameruhusiwa na Yeye kufanya hivyo, hii ni kwasababu wao ni watu tu, wenye dhambi na wasiokamili. katika Agano la Kale, Mungu alitenga makuhani kama watakatifu kwa huduma maalumu kwake. Walitakiwa kutakaswa kwa sherehe maalumu ili waweze kumkaribia Mungu. Mungu pia aliweza kutenga sehemu na vitu maalumu kuwa vitakatifu vilivyo mali yake au kupitia kwa vitu hivyo aweze kujifunua mwenyewe, vitu hivi ni kama hekalu.

Mapendekezo ya tafsiri Njia za kutafsiri neno 'takatifu' zinaweza kuwa ' kutengwa kwa ajili ya Mungu,' au "kuwa mali ya Mungu" au "hali ya kutokuwa na dhambi" au "kuwa safi." kufanya kitu/kuwa kuwa mtakatifu ina maana ya "kutakasa'' au ''kutenga''

telekeza, kutelekezwa, totoka

Ufafanuzi

Msemo "telekeza" ina maana ya kuacha mtu au kuacha kitu. Mtu ambaye "ametelekezwa" amekuwa ameachwa au kutorokwa na mtu mwingine.

Pale watu "wanapomtelekeza" Mungu, ina maana wanakuwa bila uaminifu kwake kwa kutomtii yeye.

Mungu "anapotelekeza" watu, ina maana ameacha kuwasaidia na kuruhu wapitia mateso ili kwamba kuwafanya wamgeukie na kumrudia yeye.

Msemo huu unaweza kumaanisha kutelekeza vitu, kama vile kuacha, au kutomfuata mafundisho ya Mungu.

Msemo "kutelekezwa" unaweza kutumika katika kisarufi cha nyuma kama vile "amekutelekeza" au kumaanisha mtu ambaye "ametelekezwa".

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri msemo huu zinaweza kujumuisha "kuacha" au "kutojali" au "kuachana" au "kuondoka mbali na" au "kuacha nyuma" kulinga na muktadha.

"Kutelekeza" sheria ya Mungu inaweza kutafsiriwa "kutotii sheria ya Mungu". Hii inaweza kutafsiriwa kama "kutenga" au "kukata tamaa juu ya" au "kuacha kutii" mafunzo au sheria zake.

Msemo "kutelekezwa" unaweza kutafsiriwa kama "kuachwa" au "kutengwa".

Lugha ya mradi inaweza kupata kwa uwazi zaidi kutumia maneno tofauti kutafsiri msemo huu, kulingana na maandishi yanaongelea juu ya kutelekeza kitu au mtu.

timiza

Ufafanuzi

Msemo "timiza" una maana ya kukamilisha au fanikisha jambo ambalo lilitarajiwa.

Pale ambapo unabii unatimizwa, ina maana ya kwamba Mungu alisababisha itokee kile kilichotabiriwa katika unabii.

Kama mtu anatimiza ahadi au kiapo, ina maana ya kwamba anafanya kile alichoahidi kufanya.

Kutimiza jukumu ina maana kufanya kazi ambayo ulipangiwa au unapaswa kufanya.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "timiza" unaweza kutafsiriwa kama "fanikisha" au "kamilisha" au "kusababisha kutokea" au "kutii" au "kutenda".

Msemo "imetimizwa" inaweza kutafsiriwa kama "imekuwa kweli" au "imetokea".

Njia za kutafsiri "timiza" kama vile "timiza huduma yako" inaweza kujumuisha, "maliza" au "fanya" au "mazoezi" au "tumikia watu wengine kama vile Mungu amekuita kufanya"

Tohara

Ufafanuzi

Tohara ni kitendo cha kukata govi la mwanaume au mtoto wa kiume. Sherehe ya tohara hufanyika pamoja na tendo hili.

- Mungu alimuamuru Abrahamu awatahiri wanaume wote katika familia yake na watumishi wake kama ishara ya agano lao na Mungu.
- Mungu aliamuru uzao wa Abrahamu waendelee kufanya hivi kwa kila mtoto wa kiume katika nyumba hiyo.
- "Kutahiri moyo" ni mitendo cha kuondoa uovu wa mtu.
- Kwa namna ya kiroho "aliyetahiriwa" ni mtu ambaye ametakaswa na Mungu toka kwenye dhambi kupitia damu ya Yesu.
- "Wasiotairiwa" ni watu ambao hawajatahiriwa kimwili. Pia yaweza kuwa na maana ya ambao hawajatahiriwa kiroho wasiokuwa na mahusiano na Mungu.

towashi

Ufafanuzi

Mara kwa mara, "towashi" ina maana ya mwanamume ambaye amehanithishwa. Msemo baadaye ukawa msemo wa jumla kumaanisha afisa yeyote wa serikali, hata wale ambao hawana ulemavu huu.

Yesu alisema ya kwamba baadhi ya towashi walizaliwa vile, yawezekana kwa sababu ya uharibifu ya viuongo vya siri au kwa sababu ya kutokuwa kutekeleza jukumu la kuingiliana. Wengine huchagua kuishi kama towashi kwa maisha ya mseja.

Katika nyakati za kale, matowashi mara nyingi walikuwa watumishi wa wafalme ambao waliwekwa kama walinzi katika maeneo ya wanawake.

Baadhi ya matowashi walikuwa maafisa muhimu wa serikali, kama vile towashi wa Ethiopia ambaye alikutana na mtume Filipo katika jangwa.

tukuza, kutukuza

Ufafanuzi

Kutukuza ni kusifu kwa juu sana na kumheshimu mtu. Inaweza kumaanisha kumweka mtu katika nafasi ya juu.

Katika Biblia, msemo "tukuza" unatumika sana kwa ajili ya kumtukuza Mungu.

Mtu anapojitukuza mwenyewe, ina maana anawaza juu yake mwenyewe kwa hali ya kujiinua au namna ya kiburi.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia za kutafsiri "tukuza" zinaweza kujumuisha "kusifu kwa juu" au "kuheshimu sana" au "sifu sana" au "kuzungumza kwa juu sana"

Katika baadhi ya muktadha, inaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo ambao una maana ya "kuweka nafasi ya juu zaidi" au "kutoa heshima zaidi" au "kuzungumza kuhusu kwa kiburi".

"Usijitukuze mwenyewe" inaweza kutafsiriwa kama "Usijiwazie kuwa juu sana" au "Usijidai juu yako mwenyewe".

"Wale wanaojiinua wenyewe" inaweza kutafsiriwa kama "Wale ambao hufikiri kwa kiburi kuhusu wao wenyewe" au "Wale wanaojidai juu yao wenyewe"

Uaminifu wa agano, fadhili, upendo wa kudumu

Ufafanuzi

Maneno haya hutumika kuelezea Mungu alivyijitoa kikamilivu kutimiza ahadi alizoweka kwa watu wake.

- Mungu amewaahidi Waisraeli kwa kutumia Agano.
- Uaminifu wa agano wa Bwana ni kitendo cha yeye kushika ahadi alizowaahidi watu wake.
- Uaminifu wa Mungu unajionesha kwa rehema zake kwa watu wake.
- Uaminifu ni neno lingine linaloelezea kujitoa kufanya au kusema kilichoahidiwa na kitakachomfaidisha mtu mwingine.

ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni

Ufafanuzi

Usemi wa "ufalme wa Mungu" na "ufalme wa mbinguni" zote zinamaanisha utawala wa Mungu na madaraka yake juu ya watu wake na viumbe vyote.

Wayahudi mara nyingi hutumia neno "mbingu" kumaanisha Mungu, ili kuepuka kutaja jina lake moja kwa moja. Katika kitabu cha Agano Jipya alichoandika Mathayo, aliuita ufalme wa Mungu kama "ufalme wa mbinguni," inawezekana kwa sababu alikuwa akiwaandikia zaidi Wayahudi. Ufalme wa Mungu unamaanisha Mungu kuwatawala watu kiroho pamoja na kuwatawala katika dunia ya kimwili. Manabii wa Agano la Kale walisema kuwa Mungu atamtuma Masihi kutawala kwa haki. Yesu, mwana wa Mungu, ndiye Masihi atakaye tawala juu ya watu wa Mungu milele.

Ufufuo

Ufafanuzi

Ufufuo ni kitendo cha kuwa hai tena baada ya kufa.

- Kumfufua mtu inamaana kumrudisha mtu katika hali ya kuwa hai tena. Mungu pekee ndio mwenye nguvu ya kufanya hivi.
- Neno "ufufuo" mara nyingi humwelezea Yesu aliyekuwa hai tena baada ya kufa.
- Yesu aliposema "yeye ni ufufuo na uzima" alimaanisha kuwa yeye ni chanzo cha ufufuo na ndiye husababisha watu wawe hai tena.

uovu

Ufafanuzi

Neno "uovu" ni neno ambalo liko karibu kwa maana na neno "dhambi," lakini inaweza kumaanisha zaidi matendo ya ufahamu mabaya au uovu mkubwa.

Neno "uovu" ina maana halisi ya kupindisha au kupotosha (sheria). Inamaanisha udhalimu mkubwa. Uovu unaweza kuelezwa kama matendo ya kudhuru ya makusudi dhidi ya watu wengine. Maana zingine za uovu ni pamoja na "ukaidi" na "kunyima," ambayo yote ni maneno yanayoeleza hali za dhambi mbaya.

Upatanisho, kulipia

Ufafanuzi

"Upatanisho au kulipia" inaonesha ni jinsi gani Mungu alitoa sadaka ili kulipia dhambi za watu.

- Katika agano la kale Mungu aliruhusu upatanisho wa muda ufanyike kwa ajili ya utakaso wa dhambi za wana wa Israeli, ambapo ilitolewa sadaka ya damu iliyohusisha kuchinjwa kwa mnyama.
- Katika agano jipya kifo cha Kristo msalabani ni upatanisho wa pekee na wa kudumu kwa ondoleo la dhambi.
- Yesu alipokufa alichukua adhabu ya watu waliostahili adhabu ile kwa sababu ya dhambi.

upendo

Ufafanuzi

Kumpenda mtu mwingine ni kumjali huyo mtu na kufanya vitu vitakavyo msaidia. Kuna maana tofauti za "upendo" ambazo lugha zingine zinawezakueleza kwa kutumia maneno tofauti:

Aina ya upendo utokao kwa Mungu unalenga kwa ajili ya mema ya wengine, hata kama hayamnufaishi mtu anayependa. Aina hii ya upendo inawajali watu bila kujali wanachokifanya. Mungu mwenyewe ni upendo na ndiye chanzo cha upendo wa kweli.

Yesu alionesha aina hii ya upendo kwa kujitolea maisha yake kama sadak ili kutuokoa kutoka kwenye dhambi na mauti. Aliwafundisha pia wafuasi wake kuwapenda wengine kwa kujitolea. Watu wanapowapenda wengine na aina hii ya upendo, inahusisha matendo yanayoonesha kuwa mtu anafikiria yale yatakomsaidia mtu mwingine kufanikiwa. Aina hii ya upendo inahusisha zaidi kusamehe wengine. Katika ULB, neno "upendo" linamaanisha aina hiiya upendo wa kujitoa, isipokuwa noti ya tafsiri iashirie maana tofauti.

Neno jingine katika Agano Jipya linamaanisha upendo wa kindugu au upendo kwa ajili ya rafiki au mwana familia.

Neno hili linamaanisha upendo wa asili wa binadamu kati ya marafiki na ndugu. Inawezekana kutumika katika mazingira kama, "Wanapenda kukaa kwenye viti muhimu katika sherehe." Hii inamaanisha "wanatamani sana" kufanya hivyo.

Neno "upendo" linaweza pia kumaanisha upendo wa kimapenzi kati ya mwanamme na mwanamke.
Katika hali ya kimithali, "Yakobo nimempenda, lakini Esau nimemchukia", neno "mpenda" linamaanisha Mungu kumchagua Yakobo kuwa katika mahusiano ya maagano na yeye. Hii inaweza pia kutafsiriwa kama "kuchaguliwa." Ingawa Esau alibarikiwa pia na Mungu, hakupewa heshima ya kuwa katika maagano. Neno "kuchukia" linatumika kimithali hapa kumaanisha "kukataliwa" au "kutokuchaguliwa."

ushirika

Ufafanuzi

Kwa ujumla, msemo "ushirika" ina maana ya muingiliano wa kirafiki kati ya wanajumuiya wa kundi la watu ambao huwa na upendeleo na mambo ya kufanana.

Katika Biblia, msemo "ushirika" mara kwa mara humaanisha umoja wa waumini katika Kristo.

Ushirika wa Kikristo na uhusiano ambao waumini wanao baina yao kupitia uhusiano wao na Kristo na Roho Mtakatifu.

Wakristo wa awali walionyesha ushirika wao kwa kusikiliza mafundisho ya Neno la Mungu na kuomba pamoja, katika kugawa vitu vyao, na kula milo pamoja.

Wakristo pia wana ushirika na Mungu kupitia imani ndani ya Yesu na kifo chake cha kujitolea cha msalabani ambacho kilitoa mpaka kati ya Mungu na watu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia za kutafsiri "ushirika" zinaweza kujumuisha "kugawana pamoja" au "uhusiano" au "umoja" au "jamii ya Kikristo"

ushuhuda, shuhudia

Ufafanuzi

Maneno, "ushuhuda" na "shuhudia" yanaeleza kutamka tamko kuhusu kitu ambacho mtu anajua kuwa ni kweli.

- Mara nyingi mtu anaye "shuhudia" kuhusu kitu alicho nacho amepitia moja kwa moja.
- Shahidi anaye toa "ushahidi wa uongo" hasemi ukweli kuhusu kilicho tokea.
- Wakati mwingine neno "ushuhuda" wa husu unabii ambao nabii amesema.
- Katika Agano la Kale, hili neno linatumika mara kadhaa kueleza jinsi wafuasi wa Yesu wana shuhudia kuhusu matukio ya maisha ya Yesu, kifo, na ufufuo.

utauwa, utauwa

Ufafanuzi

Msemo "utauwa" unatumika kumwelezea mtu ambaye hufanya matendo kwa njia ambayo humheshimu Mungu na kuonyesha jinsi Mungu alivyo. "Utauwa" ni sifa ya tabia ya kumheshimu Mungu kwa kufanya mapenzi yake.

Mtu ambaye ana tabia ya kiutauwa ataonyesha matunda ya Roho Mtakatifu, kama vile upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole na kiasi.

Sifa ya utauwa inaonyesha ya kwamba mtu ana Roho Mtakatifu na anamtii.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "watauwa" unaweza kutafsiriwa kama "watu wenye utauwa" au "watu ambao wanamtii Mungu"

utawala

Ufafanuzi

Msemo wa "utawala" una maana ya nguvu, madaraka, au mamlaka juu ya watu, wanyama, au nchi.

Yesu Kristo anasemekana kuwa na utawala juu ya nchi yote, kama nabii, kuhani na mfalme.

Utawala wa Shetani umeshashindwa milele na kifo cha Yesu Kristo juu ya msalaba.

Katika uumbaji, Mungu alisema ya kwamba mtu anatakiwa kuwa na utawala juu ya samaki, ndege, na viumbe wote juu ya nchi.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kutegemea na muktadha, njia zingine za kutafsiri msemo huu zinaweza kujumuisha "mamlaka" au "nguvu" au "madaraka".

Msemo "kuwa na utawala juu ya" unaweza kutafsiriwa kama "tawala juu ya" au "simamia".

utukufu, fahari

Ufafanuzi

Kwa ujumla, msemo "utukufu" una maana ya heshima, fahari, na ukuu wa hali ya juu sana. Kitu chochote ambacho kina utukufu kinasemekana kuwa na "fahari".

Mara nyingi, "utukufu" ina maana ya kitu chenye thamani kubwa na umuhimu. Katika muktadha zingine inawasilisha ufahari, mwanga, au hukumu.

Kwa mfano, msemo "utukufu wa wafugaji" una maana ya malisho yaliyostawi sana ambapo kondoo wao walikuwa na nyasi nyingi za kula.

Utukufu haswa hutumika kumfafanua Mungu, ambay ana ufahari zaidi ya yeyote au chochote katika ulimwengu. Kila kitu katika tabia yake huonyesha utukufu na ufahari wake.

Msemo "kutukuzwa na" una maana ya kujidai juu ya au kujivunia na kitu.

Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi

Ufafanuzi

Neno "uzinzi" hii ni dhambi ambayo inahusisha mwanandoa ambaye ana uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye sio mwenza wake.

- "Mzinifu" ni mtu yeyote anayefanya uzinzi.
- Mara nyingine mzinzi hutumika kuonesha kuwa ni mwanamke ndiye anayefanya uzinzi.
- Uzinzi huvunja ahadi ambayo mke na mume wamewekeana katika agano la ndoa.
- Mungu aliwaamuru Wana wa Israeli wasizini.
- Pia "zinaa" hutumika kama lugha ya picha kuwaelezea wana wa Israeli namna ambavyo hawakuwa waaminifu kwa Mungu, hasa walipokuwa wakiabudu miungu mingine.

vuka mpaka, kosa

Ufafanuzi

Maneno "vuka mpaka" na "kosa" ina eleza kuvunja amri, sheria.

- Kifumbo, "vunja mpaka" yaweza elezwa kama "vuka mstari," yani, kwenda zaidi ya kiwango, kilicho wekwa kwa wema wa huyo mtu na wengine.
- Maneno "vuka mpaka," "dhambi" "kosa," yote ina maana ya kutenda dhidi ya mapenzi ya Mungu na kutotii amri zake.

Waebrania

Ufafanuzi

'Waebrania' walikuwa ni watu wa uzao wa Ibrahimu kupitia kwa Isaka na Yakobo. Ibrahimu ni mtu wa kwanza kuitwa 'mwebrania' katika Biblia. Neno 'kiebrania' linarejelea pia lugha ambayo waebrania wanaongea. Agano la kale liliandikwa kwa lugha ya Kiebrania. Katika sehemu mbalimbali za Biblia, Waebrania waliitwa 'Wayahudi,' au 'Waisraeli' Ni vizuri kutunza maneno yote matatu katika muktadha wake, kwa kuwa majina yote matatu yanazungumzia kundi moja la watu.

Wakfu

Ufafanuzi

Kuweka wakfu ni kutenga kitu fulani au watu ili wamtumikie Mungu. Kitu au vitu vinavyowekwa wakfu ni vitakatifu na vinatengwa kwa ajili ya Mungu.

- Maana yaneno hili ni sawa na "kutakasa" lakini maana ya zaidi ni kumtenga mtu kwa ajili ya kumtumikia Mungu.
- Vitu vilivyowekwa wakfu kwa ajili ya Mungu ni pamoja na wanyama, madhabahu ya kuteketezea dhabihu na maskani.
- Watu waliowekwa wakfu kwa Mungu ni pamoja na makuhani, wana wa Israeli na watoto wa kwanza wa kiume .

wale kumi na mbili, wale kumi na moja

Ufafanuzi

Neno "wale kumi na mbili" la husu wanaume kumi na mbili Yesu aliyo wachagua kuwa wanafunzi wake wa karibu. Baada ya Yuda kujiua, waliitwa "wale kumi na moja."

- Yesu alikuwa na wanafunzi wengi, lakini jina "wale kumi na mbili" liliwa tofautisha waliyo mfuata kipindi chote cha miaka mitatu ya huduma.
- Majina ya hawa kumi na mbili yameorodheshwa katika Mathayo 10, Marko 3, na Luka 6.
- Wakati mwingine baada ya Yesu kurudi mbinguni, "wale kumi na moja" walimchagua wanafunzi jina lake Mathiasi kuchukuwa nafasi ya Yuda. Kisha wakaitwa "wale kumi na mbili" tena.

wana wa Mungu

Ufafanuzi

Jina, "wana wa Mungu" ni msemo wa mfano wenye maana kadhaa.

- Katika Agano Jipya, maneno "wana wa Mungu" ya husu waamini katika Yesu na mara nyingi utafsiriwa kama "watoto wa Mungu" maana ina jumuisha wakiume na wakike.
- Haya matumizi ya jina la zungumzia mahusiano na Mungu ambayo ni kama mahusiano kati ya mwana na baba.
- Katika Mwanzo 6, baadhi ya watu wanatafsiri "wana wa Mungu" kama malaika waliyo hasi, yani, roho chafu au mapepo. Wengine wanadhani inaweza maanisha viongozi wenye nguvu wa kisiasa au wazao wa Sethi.
- Katika Agano la Kale, neno "wana wa Mungu" la husu waamini wote wa Yesu na mara nyingi utafsiriwa kama "watoto wa Mungu."
- Jina, "Mwana wa Mungu" ni neno tofauti, linalo mtaja Yesu, ambaye ni Mwana wa Mungu

watakatifu

Ufafanuzi

Neno "watakatifu" lina maana ya halisi ya "waliyo wasafi" na kueleza waamini wa Yesu.

- Baadae katika historia ya Biblia, mtu aliye julikana kwa kazi yake njema alipewa cheo "mtakatifu," lakini sivyo jinsi hili neno lilitumika katika Agano Jipya.
- Waamini katika Yesu ni watakatifu au waliyo wasafi, sio kwasababu kwa walicho fanya, lakini bali kupitia imani katika kazi ya kuokoa ya Yesu Kristo. Yeye ndiye anao wafanya kuwa wasafi.

Watoto, mtoto

Ufafanuzi

Katika Biblia mtoto limetumika kwa namna ya jumla kuelezea mtu ambaye ni mdogo kwa umri. Watoto ni wingi wa neno mtoto.

- Katika Biblia wanafunzi na wafuasi mara nyingine waliitwa watoto.
- Watoto pia hutumika kuelezea uzao wa mtu.
- Watoto wa mara nyingine hutumika kuelezea kitu fulani. kwa mfano
- Watoto wa nuruni.
- Watoto watii
- Watoto wa muovu
- Neno hili pia linaweza kumaanisha watu ambao ni watoto wa kiroho. Kwa mfano "Watoto wa Mungu" ni watu wa Mungu wenye imani kwa Yesu.

Watu wa Mungu, watu wangu

Ufafanuzi

"Watu wa Mungu" ni watu ambao Mungu aliwaita toka duniami ili wawe na mahusiano ya kipekee naye.

- Mungu anaposema "watu wangu" anazungumza juu ya watu aliowachagua na wenye uhusiano naye.
- Watu wa Mungu wanachaguliwa na yeye na wanatengwa na ulimwengu ili kuishi maisha yanayompendeza yeye. Pia anawaita watoto wake.
- Katika agano la kale "watu wa Mungu" ni taifa la Israeli ambao walichaguliwa na Mungu na kutengwa toka kwenye mataifa mengine ya ulimwengu ili wamtumikie na kumtii yeye.
- Katika agano jipya "Watu wa Mungu" ni watu wote wanaomwamini Yesu na wanaitwa kanisa. Hii inajumuisha Wayahudi na Mataifa.

wema, uzuri

Ufafanuzi

Neno "uzuri" una maana nyingi kutegemea na muktadha. Lugha nyingi hutumia maneno tofauti kutafsiri maana hizi tofauti.

Kwa ujumla, kitu ni kizuri kama kinalingana na tabia ya Mungu, kusudi na mapenzi.

Kitu ambacho ni "kizuri" kinaweza kufurahisha, bora, msaada, kinachofaa, chenye manufaa, au sahihi kimaadili.

Ardhi ambayo ni "nzuri" inaweza kuitwa "yenye rutuba" au "yenye kuzaa".

Zao "zuri" linaweza kuwa zao "la wingi".

Mtu anaweza kuwa "mzuri" katika kile afanyacho kama ana ujuzi katika kazi yao, yaani "mkulima mzuri".

Katika Biblia, maana ya jumla ya "nzuri" mara nyingi hutofautishwa na "uovu".

Msemo "wema" mara nyingi humaanisha kuwa mzuri kimaadili kwa kutoa mambo mazuri na yenye manufaa. Inaweza kumaanisha utimilifu wake wa kimaadili.

wito, kuita, ita

Ufafanuzi

wito, kuita ni kitendo cha kusema kitu kwa nguvu kwa mtu ambaye hayuko karibu. Pia kuna maana mbali mbali kama

- Kuita mtu inamaana ya kupiga kelele au kuongea kwa sauti na mtu aliye mbali. Pia yaweza kuwa na maana ya kuomba msaada hasa kwa Mungu.
- "wito" katika Biblia mara nyingi huwa na maana ya "kumwita" au "kuamuru aje" au "kumuomba aje."
- Mungu huwaita watu kwake na kuwa watu wake. Huu ni wito wao.
- Neno "kuitwa" limetumika kwenye Biblia kumaanisha kuwa Mungu aliwachagua au kuwateua watu kuwa watoto wake, watumishi wake na wasemaji wa ujumbe wa ukombozi kupitia Yesu.
- Pia neno hili hutumika kwenye mukhtadha wa kumuita mju jina. Kwa mfano "Anaitwa Yohana," au "Jina lake ni Yohana."
- "Nimekuita kwa jina lako" inamaana kuwa Mungu anafahamu jina la mtu na amemchagua yeye.

wivu

Ufafanuzi

Neno "wivu" inaashiria hamu kubwa ya kulinda usafi wa uhusiano. Inaweza pia kumaanisha hamu kubwa ya kumili kitu au mtu.

Msemo huu mara nyingi unatumika kuelezea hisia ya hasira ambayo mtu anayo juu ya mwenzi wake ambaye amekuwa sio mwaminifu katika ndoa yao. Inapotumika katika Biblia, neno hili huwa humaanisha hamu kubwa ya Mungu kwa watu wake kubaki watakatifu na kutochafuliwa na dhambi. Mungu ana "wivu" kwa ajili ya jina lake, kwamba litunzwe kwa utukufu na heshima. Maana nyingine ya wivu inahusisha kuwa na hasira kwa kuwa mtu mwingine ana mafanikio au ana umaarufu zaidi. Hii ina maana ya kukaribiana na neno "husuda."

woe

Ufafanuzi

Ole ni hisia za dhiki kubwa. Pia inatupa onyo kuwa mtu fulani atapata shida kubwa.

- Neno "ole wa" inafuatiwa na onyo kwa watu kuwa watapata mateso kama adhabu ya dhambi zao.
- Sehemu mbalimbali katika Biblia neno "ole" limerudiwa ili kusisitiza hukumu mbaya inayokuja.
- Mtu anaposema "ole wangu mimi" inaelezea huzuni ya mateso anayopitia.

woga, hofu, hofu ya Yahwe

Ufafanuzi

Msemo "woga" au "hofu" ina maana ya hisia zisizo nzuri mtu huwa nazo ambapo kuna tishio la kudhuriwa kwake au kwa wengine.

Msemo "hofu" unaweza kumaanisha heshima kubwa na hofu mtu huwa nayo kwa mamlaka.

Msemo "hofu ya Yahwe" na misemo ya kufanana "hofu ya Mungu" an "hofu ya Bwana" ina maana ya kumheshimu sana Mungu na konyesha heshima kwa kumtii yeye. Hofu hii inahamasishwa kwa kujua ya kwamba Mungu ni mtakatifu na anachukia dhambi.

Biblia inafundisha ya kwamba mtu anayemwogopa Yahwe atakuwa na hekima.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "kuwa na hofu" kunaweza kutafsiriwa kama "kuogopa" au "kuheshimu sana" au "kuhofu" au " kuwa na hofu ya"

Msemo "woga" inaweza kutafsiriwa kama "kuogopa".

Sentensi, "Hofu ya Mungu ilianguka juu yao wote" inaweza kutafsiriwa kama, "Ghafla wote wakapatwa na hofu kuu na heshima kwa Mungu" au "Mara ghafla wote wakahisi kushangazwa sana na kumhofu Mungu sana" au "Wakati huo huo, wote wakapatwa na hofu ya Mungu"

Yaweh

Ufafanuzi

Yaweh ni jina la Mungu alilolithihirisha alipozungumza na Musa katika kichaka kinachowaka moto.

- Jina Yaweh linatokana na neno lenye maana ya "kuwepo."
- Maana nyingine ya Yaweh ni "Niko" au "anayesababisha kuwepo."
- Jina hili linadhihirisha kuwa Mungu alikuwepo na ataendelea kuishi daima. Pia inamaanisha kuwa yupo sasa.
- Tafsiri nyingi za Biblia zimetumia neno "BWANA" kuwakilisha Yaweh. Biblia za kisasa zimeandika BWANA kwa herufi kubwa kuonesha heshima kwa jina la Mungu na kutofautisha na Bwana ambayo ilitumika katika maneno ya Kiebrania.

Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

Ufafanuzi

Yesu ni mwana wa Mungu. Jina "Yesu" linamaanisha, "Yahwe anaokoa." Neno "Kristo" ni jina linalomaanisha "mtiwa mafuta" na ni jina jingine la Masihi.

Majina mawili mara nyingi yanaunganishwa kama "Yesu Kristo" au "Kristo Yesu." Majina haya yanasisitiza kuwa mwana wa Mungu ndiye Masihi aliyekuja kuwaokoa watu kutoadhibiwa milele kwa dhambi zao. Katika njia za kimiujiza, Roho Mtakatifu alisababisha mwana wa milele wa Mungu kuzaliwa kama binadamu. Wazazi wake wa duniani waliambiwa na malaika kumuita "Yesu" kwa sababu alikusudiwa kuwaokoa watu kutoka katika dhambi zao. Yesu alifanya miujiza mingi iliyoonesha kuwa yeye ni Mungu na ni Kristo, au Masihi.

Zaburi

Ufafanuzi

Zaburi ni nyimbo takatifu ambazo zipo kwenye mfumo wa ushairi zilizoandikwa ili ziimbwe.

- Katika agano la kale kitabu cha Zaburi kina mkusanyiko wa nyimbo hizo zilizoandikwa na mfalme Daudi na Waisraeli wengine kama Musa, Sulemani na Asafu.
- Zaburi zilitumiwa na taifa la Israeli katika kumwabudu Mungu.
- Zaburi zilitumika kuelezea furaha, imani na heshima pamoja na maumivu na maombolezo.
- Katika agano jipya Yesu aliwaelekeza waimbe Zaburi kwa Mungu kama njia ya kumwabudu yeye.

zawadi

Ufafanuzi

Msemo "zawadi" una maana ya kitu chochote ambacho hupewa au kutolvwa kwa mtu. Zawadi inatolewa bila matarajio ya kurudishiwa kitu chochote.

Pesa, chakula, mavazi, au vitu vingine zitolewazo kwa watu maskini zinaitwa "zawadi".

Katika Biblia, sadaka itolewayo kwa Mungu pia hujulikana kama zawadi.

Zawadi ya wokovu ni kitu ambacho Mungu anatupatia kupitia imani kwa Yesu.

Katika Agano Jipya, msemo "zawadi" pia hutumika kumaanisha uwezo maalumu wa kiroho ambao Mungu hutoa kwa Wakristo wote kutumikia watu wengine.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo wa jumla wa "zawadi" unaweza kutafsiriwa na neno au msemo ambao una maana ya "kitu ambacho kinatolewa".

Katika muktadha wa mtu kuwa na zawadi au uwezo maalumu ambao unatoka kwa Mungu, msemo "zawadi kutoka kwa Roho" unaweza kutafsiriwa kama "uwezo wa kiroho" au "uwezo maalumu kutoka kwa Roho Mtakatifu" au "kipaji maalumu cha kiroho ambacho Mungu ametoa"

translationWords

Names

Abiathari

Ufafanuzi

Abiathari alikuwa kuhani mkuu wa taifa la Israeli wakati wa mfalme Daudi. Mfalme Sauli alipowaua manabii, alitoroka na kwenda kwa Daudi nyikani. Abiathari na kuhani mkuu mwingine aitwaye Zadoki walimhudumia Daudi kwa uaminifu katika kipindi chote cha utawala wake. Baada ya kifo cha Daudi, Abiathari alijaribu kumsaidia Adoniya kuwa mfalme badala ya Sulemani. Kwa sababu hii mfalme Sulemani alimuondoa Abiathari kutoka kwenye ukuhani.

Abimeleki

Ufafanuzi

Abimeleki alikuwa mfalme wa Wafilisti huko Gera katika kipindi ambacho Abrahamu na Isaka wanaishi katika nchi ya Kaanani. Abrahamu alimdanganya Abimeleki kwa kumwambia kuwa Sara alikuwa dada yake badala ya mke wake. Abrahamu na Abimeleki walikubaliana kuhusu umiliki wa visima vilivyopo Belisheba. Miaka mingi baadaye Isaka naye akamdanganya Abimeleki na watu wengine wa Gera kwa kumwambia kuwa Rebeka alikuwa dada yake na sio mke wake. Mfalme Abimeleki alimkemea Abrahamu na Isaka kwa kumdanganya. Mtu mwingine aliyeitwa Abimeleki alikuwa mtoto wa Gidioni na kaka wa Yoramu.

Abinieri

Ufafanuzi

Abinieri alikuwa binamu wa mfalme Sauli katika agano la Kale. Abinieri alikuwa mkuu wa majeshi ya Sauli na alimtambulisha kijana Daudi kwa Sauli baada ya Daudi kumuua Goliati. Baada ya kifo cha Sauli Abinieri alichaguliwa na mtoto wa Sauli Ishibosheti kuwa mfalme wa Israeli wakati Daudi akiteuliwa kuwa mfalme katika Yuda. Baadaye Abinieri aliuawa kikatili na mkuu wa majeshi ya Daudi, Yoabu.

Abiya

Ufafanuzi

Abiya ni jina la watu mbalimbali katika agano la kale. Wafuatao ni watu hao:

- Abiya lilikuwa jina la nabii katika kipindi cha Sauli.
- Abiya alikuwa katibu katika kipindi cha utawala wa Sulemani.
- Abiya lilikuwa jina la nabii toka Shilo aliyetabiri kuwa ufalme wa Israeli utagawanyika mara mbili.
- Baba wa mfalme Baasha wa Israeli aliitwa Abiya.

Abrahamu, Abramu

Ufafanuzi

Abramu alikuwa Mkalidayo toka mji wa Urialiyechaguliwa na Mungu kuwa baba wa Waisraeli. Mungu alibadilisha jina lake na kuwa "Abrahamu."

- Jina "Abramu" lina maana ya "baba aliyeinuliwa."
- "Abrahamu" lina maana ya "baba wa wengi."
- Mungu alimuahidi Abrahamu kuwa atakuwa na uzao mwingi, na atakuwa taifa kubwa.
- Abrahamu alimuaminina kumtii Mungu. Mungu alimuongoza Abrahamu toka Kaldayo mpaka nchi ya Kaanani.
- Alipokuwa akiishi katika nchi ya Kaanani, walipokuwa wazee sana Abrahamu na mke wake Sara walipata mtoto, Isaka.

Abusalomu

Ufafanuzi

Abusalomu alikuwa mtoto wa tatu wa mfalme Daudi. Alijulikana kwa utanashati wake pamoja na hasira kali.

- Tamari Dada yake na Abusalomu alipobakwa na kaka yake Amnoni, Abusalomu alipanga mpango wa kumuua Amnoni.
- Baada ya kumuua Amnoni, Abusalomu alikwenda mpaka mji ya Geshuri (mahali alipotokea Mika mama yake) na kuishi kule miaka mitatu. Kisha mfalme Daudi akaagiza arudi Yerusalemu, lakini hakumruhusu Abusalomu akaribie kwenye uwepo wake kwa miaka miwili.
- Abusalomu aliwafanya baadhi ya watu kuwa kinyume na mfalme Daudi na kuwaongoza katika uasi dhidi ya mfalme.
- Jeshi la Daudi lilipigana na Abusalomu na kumuua. Daudi alikuwa na huzuni sana yalipotokea haya.

Adamu

Ufafanuzi

Adamu alikuwa binadamu wa kwanza aliyeumbwa na Mungu. Yeye na mke wake Hawa walitengenezwa kwa mfano wa Mungu.

- Mungu alimtengeneza Adamu toka kwenye mavumbi na kumpulizia pumzi ya uhai.
- Jina la Adamu linafanana naneno la Kiebrania linalomaanisha "udongo mwekundu"
- Jina "Adamu" ni sawa na neno kwenye Agano la kale linalomaanisha "mwanadamu" au binadamu."
- Watu wote ni uzao wa Adamu na Hawa.
- Adamu na Hawa walimuasi Mungu. Mungu alijitenga nao hivyo dhambi na mauti vikaingia duniani.

Adoniya.

Ufafanuzi

Adoniya alikuwa mtoto wa nne wa mfalme Daudi.

- Adoniya alijaribu kutaka kuwa mfalme wa Israeli baada ya kifo cha kaka yake Abusalomu na Amnoni.
- Kwa kuwa Mungu aliahidi ufalme kwa mtoto wa Daudi Sulemani, hivyo mpango wa Adoniya ulipinduliwa na Sulemani akapewa ufalme.

Ahabu

Ufafanuzi

Ahabu alikuwa mfalme muovu sana katika ufalme wa Kaskazini mwa Israeli toka 875-854 BC.

- Mfalme Ahabu aliwashawishi watu wa Israeli kuabudu miungu.
- Nabii Eliya alimkabidi Ahabu na kumwambiakuwa kutakuwa na ukame mkubwa kwa miaka mitatu na nusu kwa dhambi ambazo Ahabu alisababisha wana wa Israeli wafanye.

Ahabu na mkewe walifanya mambo mengi maovu ikiwemu kutumia nguvu zao kuwaua watu wasio na hatia.

Ahazi

Ufafanuzi

Ahazi alikuwa mfalme muovu aliyetawala ufalme wa Yuda toka 732-716 BC. Hii ilikuwa yapata miaka 140 kabla ya wakati ambao wana wa Israeli na Yuda walichukuliwa mateka Babiloni.

- Alipokuwa akitawala Yuda, Ahazi alikuwa na madhabahu ya kuabudu miungu ya Asiria, iliyosababisha watu kumuacha Mungu wa kweli, Yahweh.
- Mfalme ahazi alikuwa na miaka 20 alipoanza kutawala Yuda, na alitawala miaka 16.

Ahazia

Ufafanuzi

Lilikuwa jina la wafalme wawili: mmoja alitawala Israeli mwingine alitawala ufalme wa Yuda.

- Ahazia mfalme wa Yuda alikuwa mtoto wa mfalme Yehoramu. alitawala mwaka mmoja (841BC) kisha akauawa na Yehu. Mtoto mdogo wa Ahazia Yoashi akachukua nafasi yake kama mfalme.
- Ahazia mfalme wa Israeli alikuwa mtoto wa Ahabu. Alitawala miaka miwili 850-849 BC. Alikufa kutokana na majeraha yaliyomtesa alipoanguka toka kwenye ikulu yake na kaka yake Yoramu akawa mfalme.

Ahusuero

Ufafanuzi

Ahusuero alikuwa mfalme aliyetawala ufalme wa Perusia kwa miaka ishirini.

- Hiki ni kipindi ambacho Wayahudi waliokuwepo Babiloni kweye mateka, iliyokuja chini ya utawala wa Perusia.
- Jina lingine la mfalme huyu aliitwa Ahasuero.
- Baada ya kumfukuza malkia wake kwa hasira kubwa, mfalme Ahusuero alimchagua mwanamke wa Kiyahudi Esta kuwa mke wake na malkia.

Ai

Ufafanuzi

Katika agano la kale, Ai lilikuwa jina la mji wa Kaanani uliopo kusini mwa Betheli na takribani kilometa 8 kaskazini mashariki mwa Yeriko.

- Baada ya kuishinda Yeriko, Yoshua anawaongoza Waisraeli kuiteka Ai. Lakini walishindwa kwa sababu Mungu hakupendezwa nao.
- Muisraeli aitwaye Akani aliiba nyara toka Yeriko na Mungu akaamuru kuwa yeye na familia yake wauawe. Kisha Mungu akawasaidia Waisraeli kuishinda Ai.

Akila

Ufafanuzi

Alikuwa Mkristo wa kiyahudi aliyeishi Ponto.

- akila na Prisila waliishi Rumi, Italia kwa mda lakini ,tawala wa Rumi aliwafukuza kwa nguvu Wayahudi waondoke Rumi.
- Baada ya hayo Akila na Prisila walisafiri kwenda Korintho na kukutana na Paulo.
- walifanya kazi ya kutengeneza mahema na Paulo pamoja na kumsaidia kazi za kimisionari.
- Akila na Prisila waliwafundisha waamini ukweli kuhusu Yesu, mmoja wa waamini hao alikuwa mwalimu aliyeitwa Apolo.

Amaleki, Mwamaleki

Ufafanuzi

Waamaleki ni wafugaji walioishi Kusini mwa Kaanani, toka jangwa na Negevu mpaka nchi za uarabuni. Watu hawa walikuwa uzao wa Ameleki, mjukuu wa Esau.

- Waamaleki walikuwa maadui wakubwa wa Israeli toka kipindi ambacho Waisraeli walienda kuishi Kaanani.
- Mara nyingine Amaleki hutumika kuelezea Waamaleki wote.
- Katika vita moja dhidi ya Waamaleki, Musa alikuwa akinyanyua mikono yake juu Waisraeli walishinda na alipochoka na kushusha mikono yake chini Waisraeli walishindwa. Hivyo Haruni na Huri walimsaidia Musa kuishikilia mikono yake juu mpaka jeshi la Israeli lilipowashinda Waamaleki.
- Wafalme wote Sauli na Daudi waliyaongoza majeshi dhidi ya Waamaleki.
- Baada ya ushindi juu ya Waamaleki Sauli hakumtii Mungu kwa kuchukua baadhi ya nyara na kutokumuua mfalme wa Waamaleki kama Mungu alivyomuamuru.

Amazia

Ufafanuzi

Amazia alikuwa mfalme ya Yuda baada ya baba yake mfalme Yuashi kuuawa.

- Mfalme Amazia alitawala Yuda kwa miaka ishirini na tisa toka 796-767 BC.
- Alikuwa mfalme mzuri, lakini hakuharibu mahali ambapo miungu iliabudiwa.
- Amazia aliwahukumu kifo wote waliohusika na kumuua baba yake.
- Aliwashinda waasi wa Edomu na kuwarejesha chini ya ufalme ya Yuda.
- Alimtaka Mfalme Yoashi wa Israeli wapigane katika vita lakini alishindwa. Sehemu ya ukuta wa Yerusalemu ulivunjwa shaba na vyombo vya dhahabu vya hekali vikaibiwa.
- Miaka michache baadaye mfalme Amazia alimuacha Yahweh na baadhi ya watu katika Yerusalemu wakakusanyika pamoja na kumuua.

Amnoni

Ufafanuzi

Amnoni alikuwa mtoto mdogo wa mfalme Daudi na mke wake Ahinoamu.

- Amnoni alimbaka dada yake Tamari ambaye alikuwa dada yake na Abusalomu.
- Kwa sababu hii Abusalomu akapanga kumuua Amnoni.

Amoni, Waamoni wanaume, Waamoni wanawake.

Ufafanuzi

"Waamoni" lilikuwa kundi la watu walioishi Kaanani. Walikuwa uzao wa Benyamini, aliyekuwa mtoto wa Lutu.

- Waamoni wanawake walitafsiriwa moja kwa moja kuelezea kuwa walikuwa wanawake.
- Wakati fulani Waamoni walimlipa nabii Balamu ili awalaani Waisraeli, lakini Mungu hakuliruhusu hilo.

Amosi

Ufafanuzi

Amosi alikuwa Nabii wa Kiisraeli aliyeishi kipindi cha mfalme Uzia wa Yuda.

- Kabla ya kuwa nabii, Amosi alikuwa mchungaji na mkulima wa mtini aliyeishi katika ufalme wa Yuda.
- Amosi alitoa unabii dhidi ya kaskazini mwa ufalme wa Israeli kwa namna ambavyo wanadhulumu watu haki zao.

Amozi

Ufafanuzi

Amozi alikuwa baba wa nabii Isaya.

- Ametajwa mara moja tuu kwenye Biblia Isaya akiwa anatambulishwa kama "mtoto wa Amozi.
- Jina hili ni tofauti na jina la nabii Amosi na linapaswa kutamkwa tofauti.

Anasi

Ufafanuzi

Anasi alikuwa kuhani mkuu wa Kiyahudi kwa miaka 20 toka AD 6-AD 15. Kisha akaondolewa kwenye ukuhani mkuu na serikali ya Kirumi japokuwa aliendelea kuwa kiongozi mwenye ushawishi kati ya Wayahudi.

- Anasi alikuwa baba mkwe wa Kaefa, kuhani mkuu katika kipindi cha Yesu.
- Baada ya kuhani mkuu kustaafu, aliendelea kutumia cheo hicho na kufanya baadhi ya majukumu, hivyo Anasi bado aliendelea kuitwa kuhani mkuu katika kipindi cha ukuhani wa Kaefa na wengine.
- Katika kesi yake mbele ya viongozi wa Kiyahudi, kwa mara ya kwanza Yesu alipelekwa kwa Anasi kwa ajili ya kuhojiwa maswali.

Andrea

Ufafanuzi

Andrea alikuwa mmoja kati ya wanafunzi kumi na wawili aliowachangua Yesu kuwa karibu naye ambao baadaye waliitwa Mitume.

- Kaka yake na Andrea aliitwa Simoni Petro. Wote walikuwa wavuvi.
- Petro na Andrea walikuwa wakivua katika bahari ya Galilaya ambapo Yesu aliwaita kuwa wanafunzi wake.
- Kabla Petro na Andrea hawajakutana na Yesu walikuwa wanafunzi wa Yohana Mbatizaji.

Antiokia

Ufafanuzi

Antiokia ni jina la miji miwili katika agano jipya. Mji wa kwanza ulikuwa Siria karibu na bahari ya Mediterania na mji mwingine ulikuwa Rumi katika jimbo la Pisidia.

- Kanisa la Antiokia huko Siria ilikuwa ni sehemu ya kwanza ambayo waliomwamini Yesu waliitwa Wakristo. Kanisa pia lilitoa wamishenari wakaenda kuwafikia mataifa.
- Viongozi wa kanisa Yerusalemu alituma barua kwa waamini wa kanisa la Antiokia Siria kuwajulisha kuwa wao kuwa Wakristo sio lazima washike sheria za Kiyahudi.
- Paulo, Barnaba na Yohana Marko walisafiri mpaka Antiokia ya Pisidia kuwashirikisha injili. Baadhi ya Wayahudi walikuja kuleta vurugu na kutaka kumuua Paulo. Lakini watu wengi Wayahudi na watu wa mataifa walisikiliza mafundisho na kumwamini Yesu.

Apolo

Ufafanuzi

Apolo alikuwa Myahudi toka katika nchi ya Misri aliyekuwa na uwezo wa kipekee wa kufundisha kuhusu Yesu.

- Apolo alikuwa msomiwa maandiko ya Kiebrania na alikuwa mzungumzaji mzuri.
- Alipewa maelekezo na Wakristo wawili kule Efeso, Akila na Prisila.
- Paulo alisisitiza kuwa yeye na Apolo pamoja na wainjilisti wengine na waalimu, walifanya kazi kwa lengo moja la kuwasaidia watu kumwamini Yesu.

Araba

Ufafanuzi

Katika agano la kale "Araba" imetumika kuelezea jangwa kubwa au maeneo tambarare yanayojumuisha bonde jirani na mto Yordani hadi kusini kwenye ncha ya kaskazini mwa bahari ya shamu.

- Waisraeli walisafiri kupitia jangwa toka Misri kwenda Kaanani.
- "Bahari ya Araba" inaweza kutafsiriwa kama "bahari iliyopo kwenye mji wa jangwa la Araba" au "bahari ya chunvi" au "bahari iliyokufa."

Araba pia yaweza kuwa sehemu yoyote yenye jangwa.

Arami, Waarami

Ufafanuzi

"Arami" ni jina la watu wawili katika agano la kale. Pia lilikuwa jina la mji uliopo kaskazini mashariki mwa Kaanani, ambayo kwa sasa ni Siria.

- Watu wanaoishi Arami wanajulikana kama Waarami wanaozungumza Kiarami. Yesu na Wayahudi wengine pia walizungumza Kiarami.
- Moja ya watoto wa Shemu aliitwa Arami. Mtu mwingine aliyeitwa Arami alikuwa binamu yake na Rebeka.
- Arami baadaye ikaja kujulikana kwa jina la Kigiriki kama Siria.
- "Padani Arami" ina maanisha "Tambarare ya Arami" na ilikuwa kaskazini mwa Arami.
- Baadhi ya ndugu wa Abrahamu walioishi Harani ambayo ilikuwepo Padani Arami.
- Katika agano la kale neno Arami na Padani Arami linamaanisha sehemu moja.
- Neno "Arami Naharaimu" ina maana ya "Arami ya mito miwili" Mji huu ulikuwepo Kaskazini mwa Mesopitamia na mashariki mwa Padani Arami.

Ararati

Ufafanuzi

Kwenye Biblia "Ararati" ni jina la mahali, ufalme na milima mbalimbali.

- "Nchi ya Ararati" ipo kaskazini mashariki mwa Uturuki.
- Ararati hujulikana zaidi kama mlima ambao safina ya Nuhu ilitua baada ya maji ya mafuriko kupungua.
- Kwa sasa mlima unaoitwa "Mlima Ararati" unadhaniwa kuwa ni ule uliopo katika "Milima Ararati" ya kwenye Biblia.

Artashasta

Ufafanuzi

Artashasta alikuwa mfalme aliyetawala ngome ya Peru toka 464-424 BC.

- Katika utawala wa Artashasta Waisraeli toka Yuda walikuwa mateka huko Babiloni, ambayo ilikuwa chini ya usimamizi wa Peru kwa wakati ule.
- Artashasta alimruhusu Ezra kuhani na Wayahudi wengine kuondoka Babiloni na kurudi Yerusalemu kuwafundisha Waisraeli sheria za Mungu.
- Baadaye Artashasta alimruhusu Nehemia kurudi Yerusalemu ili awaongoze Wayahudi katika kujenga ukuta uliozunguka mji.
- Kwa kuwa Babiloni ilikuwa chini ya utawala wa Peru wakati mwingine Artashasta aliitwa mfalme wa Babiloni.

Asa

Ufafanuzi

Asa alikuwa mfalme aliyetawana ufalme wa Yuda kwa miaka arobaini. toka 913-873 BC.

- Mfalme Asa alikuwa mfalme mzuri aliyeondoa sanamu nyingi za miungu na kusababisha Waisraeli waanze kumuabudu tena Yahweh.
- Yahweh alimpa mfalme Asa mafanikio ya utajiri dhidi ya mataifa mengine.
- Baadae katika utawala wake Asa aliacha kumuamini Yahweh na akaugua ugonjwa ambao ulipelekea kifo chake.

Asafu

Ufafanuzi

Asafu alikuwa kuhani wa Kilawi na mtaalamu wa muziki aliyetunga mziki wa Zaburi ya mfalme Daudi. Pia aliandika zaburi yake mwenyewe.

- Asafu alichaguliwa na mfalme Daudi kuwa moja ya wanamuziki watatu waliokuwa wakitengeneza nyimbo za kuabudu hekaluni. Baadhi ya nyimbo hizi zilikuwa unabii.
- Asafu aliwafundisha watoto wake na wakabeba majukumu ya kutumia vyombo vya muziki na kutoa unabii hekaluni.
- Baadhi ya vyombo vya mziki vilivyokuwepo ni kinanda, kinubi, tarumbeta na matoazi.
- Zaburi ya 50, 73-83 inasemekana zimetoka kwa Asafu. Na pia inawezekana baadhi ya zaburi hizi zimeandikwa na wanafamilia wake.

Ashdodi, Azoto

Ufafanuzi

Ashdodi ulikuwa ni moja kati ya miji mitano muhimu kwa Wafilisti. Mji huu ulikuwa kusinimagharibi mwa Kanani karibu na bahari ya Mediterranean, kkati ya miji ya Gaza na Jopa.

- Hekalu la Wafilisti lililokuwa mungu wa uongo dagoni lilikuwa Ashdodi.
- Mungu aliwaadhibu watu wa Ashdodi wakati Wafilisti walipoiba sanduku la agano na kuliweka katika hekalu la kipangani huko Ashdodi.
- Jina la kigiriki la huu mji lilikuwa Azoto. Ulikuwa moja kati ya miji ambayo mwinjilisti Philipo alihubiri injili.

Ashera, sanamu ya ashera, Ashtorethi

Ufafanuzi

Ashera lilikuwa jina la mungu wa kike aliyeabuniwa na Wakaanani kipindi cha agano la kale. Ashtorethi ni jina lingine la Ashera.

- Sanamu ya Ashera ni kinyago kilichochongwa kwa mbao au mti uliochongwa kwa ajili ya kumwakilisha mungu wa kike.
- Sanamu za Ashera zilikuwa zinawekwa karibu na madhabahu za mungu Baali, aliyekuwa anadhaniwa kuwa mume wa Ashera. Watu wengine walikuwa wanamuabudu Baali kama mungu wa jua na Ashera kama mungu wa mwezi.
- Mungu aliwaamuru Waisraeli wahaaribu vinyago vyote vilivyochongwa vya Ashera.
- Baadhi ya Waisraeli kama Gideoni, mfalme Asia na mfalme Yosia walimtii Mungu na kuwaongoza watu kuharibu sanamu hizo.
- Lakini viongozi wengine wa Israeli kama mfalme Solomoni, Mfalme Manase na mfalme Ahabu hawakuziharibu sanamu za Ashera na waliwashawishi watu waziabudu.

Asheri

Ufafanuzi

Asheri alikuwa mtoto wa nane wa Yakobo. Uzao wake unaunda moja ya makabila kumi na mbili ya Israeli ambalo pia linaitwa Asheri.

- Mama yake na Asheri aliitwa Zilpa, mtumwa wa Lea.
- Maana ya jina lake ni "furaha" au "baraka."
- Asheri pia lilikuwa jina la ngome ambayo kabila la Asheri walipewa baada ya Waisraeli kuingia nchi ya ahadi.

Ashikelo

Ufafanuzi

Katika Biblia, Ashikelo ni mji wa wafilisti ulioko pwani Bahari ya Mediterania. Bado ipo mpaka leo Israeli.

- Ashikelo ulikuwa mji wa muhimu sana wa Wafilisti pamoja na Ashdodi, Ekironi, Gati na Gaza.
- Waisraeli hawakuiteka kabisa Ashikelo japokuwa ufalme wa Yuda ulisambaa nchi nzima.
- Ashikelo iliendelea kukaliwa na Wafilisti kwa miaka mia.

Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru

Ufafanuzi

Ashuru lilikuwa taifa lenye nguvu kipindi ambacho wana wa Israeli walikuwa wakiishi Kaanani. Ngome ya waashuru ilikuwa ni kundi la mataifa waliotawaliwa na mfalme wa Ashuru.

- Taifa la Ashuru lilikuwa sehemu ambayo kwa sasa ni nchi ya Iraq.
- Mwaka 722 BC Waashuru waliuteka ufalme wa Israeli na kuwalazimisha Waisraeli wengi kwenda Ashuru.
- Waisraeli waliobaki waliwaoa wageni walioletwa na Waashuru toka Samaria. Kizazi cha watu hao waliotokana na mwingiliano huo wa kuoana waliitwa Wasamaria.

Asia

Ufafanuzi

Katika Biblia Asia ni jina la jimbo la utawala wa Kirumi. Ilikuwa magharibi mwa nchi inayoitwa Uturuki kwa sasa.

- Paulo alisafiri mpaka Asia kueneza injili katika miji mbalimbali huko. Baadhi ya miji hiyo ni Efeso na Kolose.
- Ili kuondoa utata wa kuchanganya na Asia ya sasa, ni vizuri kuitafsiri Asia hii kama "mkoa wa zamani wa Kirumi ulioitwa Asia" au "mkoa wa Asia."
- Makanisa yote yanayotazamwa katika Ufunuo yalikuwa katika mkoa wa Kirumi uitwao Asia.

Athalia.

Ufafanuzi

Athalia alikuwa mke mbaya wa Yehoramu mfalme wa Yuda. Alikuwa mjukuu wa mfalme muovu wa Israeli, mfalme Omri.

- Ahazia mtoto wa Athalia alikuwa mfalme baada ya kifo cha Yehoramu.
- Ahazia alipokufa, Athalia alipanga kuwauwa ndugu waliosalia wa familia ya mfalme.
- Lakini mjukuu mdogo wa Athalia Yoashi alifichwa na shangazi yake hivyo hakuuawa. Baadaye alikuwa mfalme wa Yuda.

Ayubu

Ufafanuzi

Ayubu alikuwa mtu anayeelezwa katika Biblia kama mtu asiye na hatia na mwenye haki mbele ya Mungu. Anajulikana zaidi kwa kutunza imani yake katika Mungu katika nyakati za mateso makali.

Ayubu aliishi katika nchi ya Usi iliyokuwa sehemu ndani ya nchi ya Kanaani, inawezekana katika maeneo ya Edomu. Inafikiriwa kuwa aliishi wakati wa Esau na Yakobo kwa sababu mmoja wa marafiki wa Ayubu alikuwa "Mtemani," ambalo lilikuwa jina la kundi lililoitwa baada ya mjukuu wa Esau. Kitabu cha Agano la Kale cha Ayubu kinaelezea jinsi Ayubu na wengine walivyoitikia mateso yake. Pia inatoa mtazamo wa Mungu kama muumbaji mwenye enzi na mtawala wa ulimwengu. Baada ya maafa hayo yote, hatimaye Mungu alimponya Ayubu na kumpa watoto wengine na utajiri. Kitabu cha Ayubu kinasema kuwa alikuwa mzee sana alipokufa.

Azaria

Ufafanuzi

Azaria ni jina la watu kadhaa kwenye agano jipya.

- Aharia wa kwanza alijulikana sana kwa jina lake la Kibabiloni kama Abedinego. Alikuwa mmoja kati ya Waisraeli wengi toka Yuda waliokamatwa na jeshi la Nebukadneza na kupelekwa kuishi Babiloni.
- Mfalme Uzia wa Yuda pia alijulikana kama Azaria.
- Azaria mwingine alikuwa kuhani mkuu katika agano la kale.
- Katika kipindi cha nabii Yeremia, Azaria aliwataka Waisraeli wasimtii Mungu kwa kuondoka kwenye nchi yao.

Baali

Ufafanuzi

"Baali" maana yake "bwana" lilikuwa jina la mungu wa kwanza wa uongo aliyekuwa akiabudiwa na Wakanaani.

- Pia kulikuwa na miungu mingine ya uongo yenye jina "Baali, kama vile "Baali wa Peori." Wakati mwingine miungu hii kwa pamoja inarejerewa kama "Mabaali."
- Baadhi ya watu walikuwa na majina yenye jina "Baali" ndani yake.
- Ibada ya Baali ilihusisha matendo maovu kama vile kutoa watoto kama sadaka na ukahaba.
- Kwa nyakati tofauti katika historia, Waisraeli pia walijiingiza katika ibada ya Baali, kwa kufuata mfano wa mataifa ya kipagani yaliyowazunguka.
- Wakati wa utawala wa Mfalme Ahabu, Eliya nabii wa Mungu aliweka jaribio la kuwathibitishia watu kwamba Baali si mungu wa kweli na kwamba Yahwe pekee ndiye aliyekuwa Mungu wa kweli. Matokeo yake, manabii wa Baali waliangamizwa na watu wakaanza kumwabudu Yahwe tena.

Baasha

Ufafanuzi

Baasha alikuwa miongoni mwa wafalme waovu wa Israeli,waliowashawishi Waisraeli kuabudu vinyago.

- Baasha alikuwa mfalme wa tatu wa Israeli na alimiliki kwa miaka ishirini na minne, wakati Asa akiwa mfalme wa Yuda.
- Alikuwa jemedari wa jeshi aliyejifanya mfalme baada ya kumwua mfalme Nadabu, mtangulizi wake.
- Kulikuwa na mapigano mengi wakati wa utawala wa Baasha kati ya ufalme wa Israeli na Yuda, hasa na Asa mfalme wa Yuda.
- Dhambi nyingi alizozitenda Baasha hatimaye zilimfanya Mungu kumwondoa katika nafasi yake kwa kifo.

Babeli

Ufafanuzi

Babeli ulikuwa mji mkuu katika eneo lililoitwa Shinari kusini mwa Mesopotamia. Shinari ulikuja baadaye kuitwa Babiloni.

- Mji wa Babeli ulianzishwa na Nimrodi, mjukuu wa Hamu, aliyemiliki eneo la Shinari.
- Watu wa Shinari hatimaye wakawa na kiburi kwa kuamua kujenga mnara mrefu wa kuweza kufika mbinguni. Baada ulijulikana kama "Mnara wa Babeli."
- Kwa kuwa kwa kujenga mnara watu walikataa kutawanyika kama Mungu alivyokuwa ameagiza, yeye alichanganya lugha zao ili wasielewane. Hii iliwalazimisha kuondoka na kwenda kuishi maeneo mbalimbali ya dunia.
- Kiini cha maana ya neno "Babeli" ni "machafuko," likitokana na wakati Mungu alipochanganya lugha ya watu.

Bahari ya Chumvi, Bahari iliyo Kufa

Ufafanuzi

Bahari ya Chumvi(inayo itwa pia Bahari iliyo Kufa) ilikuwa kati ya kusini mwa Israeli upande wa magharibi na Moabu upande wa mashariki.

- Mto Yordani una shuka kusini kwenye Bahari ya Chumvi.
- Kwasababu ni ndogo kuliko bahari nyingine, hii yaweza itwa "Ziwa la Chumvi."
- Hii bahari ina idadi kubwa ya madini (au "chumvi) inayo maanisha kwamba hakuna kinacho weza kuishi ndani ya maji yake. Hapo ndipo jina "Bahari iliyo Kufa" limetoka.
- Kati Agano la Kale, hii bahari inaitwa pia "Bahari ya Araba" na "Bahari ya Negevi" kwasababu ya maeneo yake karibu na pande za Araba na Negevi.

Bahari ya Galilaya, Bahari ya Shinerethi, Ziwa la Genezareti, Bahari ya Tiberia

Ufafanuzi

"Bahari ya Galilaya" ni jina la ziwa mashariki mwa Israeli. Katika Agano la Kale liliitwa "Bahari ya Shinerethi."

- Maji ya hii bahari yana shuka kusini kupitia Mto Yordani kwenda Bahari ya Chumvi.
- Kapernaumu, Bethsaida, Genezareti, na Tiberia zilikuwa baadhi ya miji ambayo ilikuwa upande wa Bahari ya Galilaya kipindi cha Agano Jipya.
- Matukio mengi ya maisha ya Yesu yalitokea karibu na Bahari ya Galilaya.
- Bahari ya Galilaya ili tajwa pia kama "Bahari ya Tiberia" na "Ziwa la Genezareti."

Bahari ya shamu

Ufafanuzi

Bahari ya shamu ni jina la la bahari iliyokuwa Misri na Uarabbuni. Sasa inaitwa bahari ya Shamu.

- Bahari ya shamu ni ndefu na nyembamba. Ni kubwa zaidi ya ziwa au mto lakini ndogo kuliko bahari.
- Waisraeli walivuka bahari ya shamu walipotoka Misri. Mungu aliwafanyia muujiza na kusababisha maji kugawanyika na watu wakapita.
- Nchi ya Kanaani ilikuwa kaskazini mwa bahari hii.

bahari, Bahari Kuu, bahari ya magharibi, Bahari ya Medeterenia

Ufafanuzi

Katika Biblia, "Bahari Kuu" au " bahari ya magharibi" inaelezea ile ambayo sasa ujulikana "Bahari ya Medeterenia," ambayo ilikuwa ni eneo la maji lilokulikana na watu wa Biblia.

- Bahari ya Medeterenia ina pakana: Israeli (mashariki), Ulaya (kaskazini na magharibi), na Africa (kusini)
- Bahari ilikuwa muhimu kipindi cha kale kwa ajili ya biashara na kusafiri maana ili pakana na nchi zingine. Miji na makundi ya watu yaliyo pwani ya hii bahari yalifanikiwa sana kwasababu ya urahisi wa kupata bidha nchi zingine kwa meli.

Balaamu

Ufafanuzi

Balaamu alikuwa nabii wa kipagani aliyeajiriwa na Mfalme Balaki kuwalaani Israeli walipokuwa wamepiga kambi katika Mto Yordan kaskazini mwa Moabu, wakijiandaa kuingia nchi ya Kanaani.

- Balaamu alikuwa akitoka katika mji wa Pethori, ulikuwa katika eneo karibu na Mto Frati, umbali wa maili 400 kutoka katika nchi ya Moabu.
- Balaki, mfalme wa Wamidiani, alitishwa na nguvu na idadi ya Waisraeli, hivyo akamwajiri Balaamu kuwalaani.
- Kadiri Balaamu alivyosafiri kuwaelekea Israeli, malaika wa Mungu alisimama katika njia yake hivyo punda wa Balaamu alipomwona alisimama. Mungu akampa punda uweza wa kuongea na Balaamu.
- Mungu hakumuruhusu Balaamu kuwalaani Israeli badala yake alimwagiza kuwabariki.
- Baadaye, Balaamu bado alilete uovu juu ya Israeli alipowafuta kuabudu mungu wa Baar- peori.

Baraba

Ufafanuzi

Baraba alikuwa mfungwa huko Yerusalemu wakati Yesu anakamatwa.

- Baraba alikuwa mwalifu aliyekuwa ametenda makosa ya kuuwa na uasi dhidi ya serikali ya Kirumi.
- Pontio Pilato alipotoa msamaha wa kumfungua kati ya Baraba au Yesu, watu walimchagua Baraba.
- Hivyo Pilato alimwacha huru Baraba, lakini akamhukumu Yesu auawe.

Barnaba

Ufafanuzi

Barnaba ni miongoni mwa wakristo wa mwanzo aliyeishi wakati wa mitume.

- Barnaba alikuwa wa kabila ya Lawi na alikuwa mwenyeji wa kisiwa cha Mileto.
- Wakati Sauli (Paulo) anakuwa mkristo, Barnaba aliwasihi waamini wangine kumpokea kama mwamini mwenzao.
- Barnaba na Paulo walisafiri kwa pamoja katika miji mbalimbali ili kuhubiri injili.
- Jina lake lilikuwa Yusufu, lakini aliitwa "Barnaba," jina linalomaanisha "mwana wa faraja."

Baruku

Ufafanuzi

Baruku ni jina la watu kadhaa katika Agano la Kale.

- Baruku wa kwanza (mwana wa Zabeli) alifanya kazi ya Nehemia kujenga upya kuta za Yerusalemu.
- Lakini pia katika nyakati za Nehemia, Baruku mwingine (mwana wa Kol-Hoze) alikuwa miongoni mwa viongozi walioishi Yerusalemu baada ya kuta zake kujengwa.
- Baruku mwingine (mwana wa Neria) alikuwa mhudumu wa nabii Yeremia, kwa kumsaidia kazi mbalimbali kama vile kuandika jumbe Mungu alizompa Yeremia na kisha kuwasomea watu.

Bashani

Ufafanuzi

Bashani lilikuwa ni enea mashariki mwa Bahari ya Galilaya. Ilihusisha eneo ambalo kwa sasa ni sehemu ya Syria na milima ya Golani.

- Mji wa makimbilio katika Agano la Kale ulioitwa "Golani" ulikuwa katika eneo la Bashani.
- Bashani lilikuwa eneo lenye rutuba sana likijulikana kwa miti yake ya mitende na malisho ya wanyama.
- Mwanzo 14 inataarifu kuwa Bashani ilikuwa eneo la vita kati ya wafalme kadhaa na mataifa yao.
- Wakati Waisraeli wakitangatanga jangwani baada ya kutoka Misri, walichukua sehemu ya eneo la Bashani.
- Miaka kadhaa baadaye, mfalme Sulemani alipokea mahitaji kutoka katika eneo hilo.

Batholomayo

Ufafanuzi

Batholomayo alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi kumi na mbili wa Yesu.

- Batholomayo alitumwa pamoja na wale mitume wengini kuhubiri injili na kufanya miujiza kwa jina la Yesu.
- Alikuwa miongoni mwa wale waliomwona Yesu akienda mbinguni.
- Majuma kadhaa baada ya hayo, alikuwa pamoja na mitume wengine huko Yerusalemu siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alipowashukia.

Bathsheba

Ufafanuzi

Bathsheba alikuwa mke wa Uria, askari katika jeshi la Daudi. Baada ya kifo cha Uria, akawa mke wa Daudi, na mama wa Sulemani.

- Daudi alizini na Bethsheba akiwa mke wa Uria.
- Bathsheba alipokuwa mjamzito kwa Daudi, Daudi alisababisha Uria kuuawa vitani.
- Kisha Daudi alimwoa Bethsheba na akazaa mwana.
- Mungu alimwadhibu Daudi kwa dhambi yake kwa kufanya mtoto afe siku chache baada ya kuzaliwa.
- Baadaye, Bethsheba alizaa mwana mwingine, Sulemani, aliyekuja kuwa mfalme baada ya Daudi.

Beelzebuli

Ufafanuzi

Beelzebuli ni jina lingine kwa Shetani, au mwasi. Wakati mwingine linaandikwa "Beelzebubu."

- Jina hili kwa kawaida linamaanisha "bwana wa nzi" kumaanisha, mtawala wa mapepe." Lakini ni vizuri zaidi kutafasiri neno karibu na herufi zake za asili kuliko kutafasiri maana.
- Ingeweza pia kutafasiriwa kama "Beelzebubu mwovu" kuweka wazi anayetajwa.
- Jina hili linahusiana na jina la Baal-Zebubu mungu wa Ekroni.

Beersheba

Ufafanuzi

Katika nyakati za Agano la Kale, Beersheba ulikuwa mji uliokuwa umbali wa maili 45 kusini magharibi mwa Yerusalemu katika eneo la jangwa ambalo kwa sasa linaitwa Negevu.

- Jangwa lililouzunguka Beersheba lilikuwa ni eneo la nyika ambapo Hajiri na Ishmaeli walipotelea baada ya Ibrahimu kuwafukuza kutoka katika hema zake.
- Jina la mji linamaanisha "kisima cha nadhiri." Ulipewa jina hili Ibrahimu walipoapa kwa kiapo kutokuwaadhibu watu wa Mfalme Abimeleki kwa kukatalia mojawapo ya visima vya Ibrahimu.

Benaya

Ufafanuzi

Benaya lilikuwa jina la watu kadhaa katika Agano la Kale.

- Benaya mwana wa Yehoyada alikuwa miongoni mwa mashujaa wa Daudi. Alikuwa shujaa mwenye ujuzi na aliwekwa kuwa mlinzi wa Daudi.
- Sulemani alipotawazwa kuwa mfalme, Benaya alimsaidia kuwaaribu adui zake, hatimaye akawa jemedari wa jeshi la Israeli.
- Watu wengine wenye jina Benaya katika Agano la Kale ni pamoja na Walawi watatu: kuhani, mwimbaji, na mwana wa Asafu.

Benjamini

Ufafanuzi

Benjamini alikuwa mwana wa mwisho wa Yakobo aliyezaliwa na Raheli mkewe. Jina lake linamaanisha mwana wa "mkono wangu wa kulia."

- Yeye na Yusufu, nduguye mkubwa walikuwa wana pekee wa Raheli, aliyekufa baada ya kuzaliwa kwa Benjamini.
- Wana wa Benjamini walikuwa mojawapo ya makabila ya Israeli.
- Mfalme Sauli alikuwa akitokea katika kabila la Benjamini.
- Mtume Paulo pia alikuwa wa kutoka katika kabila la Benjamini.

Berea (Beroya)

Ufafanuzi

Katika nyakati za Agano Jipya, Berea(Beroya) ulikuwa mji wa Kigriki wenye mafanikio kusini mashariki mwa Masedonia, umbali wa kilometa 80 kusini mwa Thesalonike.

- Paulo walikimbilia katika mji wa Berea baada ya Wakristo wenzao kuwasaidi kutoroka kutoka kwa Wayahudu kadhaa waliowasababishia shida huko Thesalonike.
- Watu waliokuwa wakiishi Berea walipomsikia Paulo akihubiri, waliyachunguza maandiko kuthibitisha ikiwa alichokuwa akiwambia kilikuwa kweli.

Beth Shemeshi

Ufafanuzi

Beth Shemeshi lilikuwa jina la mji wa Kikanaani kama kilometa 30 magharibi ya Yerusalemu.

- Waisraeli waliuteka mji wa Beth Shemeshi wakati wa uongozi wa Yoshua.
- Beth Shemeshi ulikuwa mji uliokuwa umetengwa kama sehemu ya makuhani Walawi kuishi.
- Wafilisiti walipokuwa wakilirudisha Yerusalemu sanduku la agano walilokuwa wameliteka, Beth Shemeshi ni mji wa kwanza waliposimama pamoja nalo.

Betheli

Ufafanuzi

Betheli ulikuwa mji uliokuwa kaskazini mwa Yerusalemu katika nchi ya Kanaani. Hapo mwanzo uliitwa "Luzu."

- Baada ya kupokea ahadi za Mungu kwa mara ya kwanza, Ibrahimu alimjengea Mungu madhabahu karibu na Betheli. Jina lake wakati huo halikuwa Betheli, lakini kwa kawaida ulirejerea kama "Betheli" uliokuwa unatambuliwa sana.
- Wakati akikimbia kutoka kwa Esau nduguye, Yakobo alikaa usiku kucha karibu na mji huu na akalala pale nje juu ya ardhi. Alipokuwa amelala, aliota ndoto malaika wakipanda na kushuka mbinguni juu ya ngazi.
- Mji huu haukuwa na jina hilo mpaka Yakobo alipouita hivyo. Kwa kuwa wazi zaidi, baadhi ya tafasiri zaweza kuiita Luzu "(baadaye ukaitwa Betheli)" katika kifungu kuhusu Ibrahimu, vilevile wakati Yakobo anafika pale kwa mara ya kwanza (kabla hajabadili jina lake).
- Betheli imetajwa mara kwa mara katika Agano la Kale na ilikuwa sehemu ambapo matukio mengi mhimu yalitokea.

Bethlehemu

Ufafanuzi

Bethlehemu ulikuwa mji mdogo katika nchi ya Israeli, karibu na mji wa Yerusalemu. Ulijulikana pia kama "Efratha," ambalo pengine ndilo jina lake la awali.

- Bethlehemu umekuwa ukiitwa mji wa "Daudi," kwa kuwa Daudi alizaliwa pale.
- Nabii Mika alitabiri kuwa Masiya angekuja kutokea katika "Bethlehemu ya Efratha."
- Ili kutimiza unabii huo, Yesu alizaliwa Bethlehemu, miaka mingi baadaye.
- Jina "Bethlehemu" maana yake ni "nyumba ya mikate" au "nyumba ya chakula."

Bethueli

Ufafanuzi

Bethueli alikuwa mwana wa Nahori ndiguye Ibrahimu.

- Bethueli alikuwa baba wa Rebeka na Labani.
- Pia kulikuwa na mji uliokuwa ikiitwa Bethueli, ambao yawezekana ulikuwa kusini mwa Yuda, siyo mbali kutoka mji wa Beersheba.

Boazi

Ufafanuzi

Boazi alikuwa mwisraeli aliyekuwa amemwoa Ruthi, babu wa mfalme Daudi, na babu wa Yesu Kristo.

- Boazi aliishi nyakati za Waamzi katika Israeli.
- Alikuwa ndugu wa Naomi mwanamke wa Kiisraeli aliyekuwa amerudi kutoka Moabu baada ya mmewe na wanawe kufariki.
- Boazi "alimkomboa" Ruthi mkwewe Naomi, kwa kumwoa Ruthi na kumpa hatima njema, mme na watoto.
- Yeye ni taswira ya jinsi Yesu alivyotuokoa na kutukomboa kutoka dhambini.

Bonde la Kidroni

Ufafanuzi

Bonde la Kidroni ni bonde refu nje kidogo ya mji wa Yerusalemu, katikati ya ukuta wa mashariki na mlima wa Mizeituni.

Bonde lina kina zaidi ya mita 1,000 na urefu karibu wa kilomita 32. Wakati mfalme Daudi alipokuwaakimtoroka mwanaye Absalomu, alipita bonde la Kidroni kufika mlima wa Mizeituni. Mfalme Yosia na mfalme Asa wa Yuda waliamuru kwamba sehemu zilizoinuka na madhabahu za miungu wa uongo zivunjwe na kuchomwa; majivu yalitupwa bonde la Kidroni. Wakati wa utawala wa mfalme Hezekia, bonde la Kidroni ndipo makuhani walipotupa kila kitu kisicho kisafi walichokitoa kwenye hekalu. Malkia muovu Athalia aliuliwa katika bonde kwa sababu ya maovu aliyoyafanya.

Dameski

Ufafanuzi

Dameski ni mji mkuu wa nchi ya Shamu. Bado upo sehemu ile ile kama ulipokuwa kipindi cha Biblia.

Dameski ni moja ya miji kongwe, inayoendelea kukaliwa kwa uendelevu duniani.

Katika kipindi cha Abrahamu, Shamu ulikuwa mji mkuu wa ufalme wa Aramu (ulio mahali ambapo sasa ni Shamu).

Katika Agano la Kale lote, kuna marejeo mengi ya miingiliano kati ya wakazi wa Dameski na watu wa Israeli.

Baadhi ya unabii wa Kibiblia zinatabiri uharibifu wa Dameski. Unabii huu unaweza kuwa umekamilika pale ambapo Shamu iliangamiza mji ule katika wakati wa Agano la Kale, au kunaweza kuwa na muda wa baadaye, utakaokuwa na uharibifu kamili wa mji huu.

Katika Agano Jipya, Mfarisayo Sauli (aliyejulikana baadaye kama Paulo) alikuwa njiani kukamata Wakristo katika mji wa Dameski ambapo Yesu alimkabili na kumfanya awe muumini.

Dani

Ufafanuzi

Dani alikuwa mwana wa tano wa Yakobo na alikuwa mmoja wa makabila kumi na mawili ya Israeli. Eneo lililokaliwa na kabila la Dani sehemu ya kaskazini ya Kaanani pia lilipatiwa jina hili.

Katika kipindi cha Abrahamu, kulikuwa na mji ulioitwa Dani uliokuwa magharibi mwa Yerusalemu.

Miaka ya baadaye, katika kipindi ambapo taifa la Israeli lilipoingia katika nchi ya ahadi, mji tofauti ulioitwa Dani ulikuwa kama maili 60 kaskazini mwa Yerusalemu.

Msemo "Wadani" una maana ya vizazi vya Dani, ambao pia ni wanajumuiya wa ukoo wake.

Danieli

Ufafanuzi

Danieli alikuwa nabii wa Kiisraeli ambaye alikuwa kijana mdogo aliyechukuliwa mateka na mfalme wa Babeli Nebukadreza mnamo wa 600 KK.

Huu ulikuwa wakati ambapo Waisraeli wengine wengi kutoka Yuda walishikwa mateka huko Babeli kwa miaka 70.

Danieli alipewa jina la Kibabeli la Belteshaza.

Danieli alikuwa kijana aliyeheshimika na mwenye haki aliyemtii Mungu.

Mungu alimwezesha Danieli kutafsiri ndoto kadhaa au maono kwa wafalme wa Babeli.

Kwa sababu ya uwezo huu na kwa sababu ya hulka yake ya heshima, Danieli alipewa nafasi ya juu ya uongozi katika ufalme wa Kibabeli.

Miaka mingi baadaye, maadui wa Danieli walimdanganya mfalme wa Babeli Dario kutunga sheria inayokataza kumwabudu mtu yeyote isipokuwa mfalme. Danieli aliendelea kuomba kwa Mungu, kwa hiyo alikamatwa na kutupwa katika tundu la simba. Lakini Mungu alimkomboa na hakudhuriwa kabisa.

Dario

Ufafanuzi

Dario lilikuwa jina la wafalme kadhaa wa Uajemi. Inawezekana "Dario" ilikuwa ni cheo na siyo jina.

"Dario, Mmedi" alikuwa mfalme aliyedanganywa kumfanya nabii Danieli kutupwa katika tundu la simba kama adhabu ya kumwabudu Mungu.

"Dario Muajemi" alisaidia kurahisisha ujenzi tena wa hekalu Yerusalemu katika kipindi cha Ezra na Nehemia.

Daudi

Ufafanuzi

Daudi alikuwa mfalme wa pili wa Israeli na alimpenda na kumtumikia Mungu. Alikuwa mwandishi mkuu wa kitabu cha Zaburi.

Daudi alipokuwa mvulana mdogo akichunga kondoo wa familia yake, Mungu alimchagua kuwa mfalme afuataye wa Israeli.

Daudi alikuwa mpiganaji hodari na aliongoza jeshi la Israeli katika vita dhidi ya maadui zake. Kumshinda kwake Goliati na Wafilisti kunajulikana sana.

Mfalme Sauli alijaribu kumuua Daudi, lakini Mungu alimlinda, na kumfanya awe mfalme baada ya kifo cha Sauli.

Daudi alitenda dhambi mbaya sana, lakini alitubu na Mungu alimsamehe.

Yesu, Masihi, anaitwa "Mwana wa Daudi" kwa sababu ni uzao wa Mfalme Daudi.

Delila

Ufafanuzi

Delila alikuwa mwanamke wa Kifilisti aliyependwa na Samsoni, lakini hakuwa mke wake.

Delila alipenda pesa zaidi ya alivyompenda Samsoni.

Wafilisti walimhonga Delila kumdanganya Samsoni amwambie jinsi awezavyo kufanywa mnyonge. Nguvu yake ilipotoweka, Wafilisti walimkamata.

Edeni, bustani ya Edeni

Ufafanuzi

Katika kipindi cha zamani, Edeni ilikuwa eneo ambalo lilikuwa na bustani ambapo Mungu aliweka mwanamume na mwanamke wa kwanza kuishi.

Bustani ambayo Adamu na Hawa waliishi ilikuwa sehemu tu ambayo waliishi.

Sehemu husika ya eneo la Edeni halina uhakika, lakini Mito ya Hidekeli na Frati zilitiririka katikati yake.

Neno "Edeni" hutokana na neno la Kiebrania lenye maana ya "kufurahishwa sana na".

Edomu, Muedomu, Idumaya

Ufafanuzi

Edomu ilikuwa jina lingine la Esau. Eneo ambalo aliishi pia kukajulikana kama "Edomu" na baadaye, "Idumaya". "Waedomu" walikuwa vizazi vyake.

Eneo la Edomu lilibadilisha maeneo baada ya muda. Ulikuwa zaidi kusini ya Israeli na baadaye kupanuka katika kusini mwa Yuda.

Katika wakati wa Agano Jipya, Edomu ilifunika nusu ya kusini ya mkoa wa Yuda. Wagiriki waliita "Idumaya"

Jina "Edomu" ina maana ya "nyekundu" ambayo inaweza kumaanisha ukweli kwamba Esau alifunikwa na nywele nyekundu alipozaliwa. Au inaweza kumaanisha mchuzi mwekundu ambao Esau aliuza kwa haki yake ya mzawa wa kwanza.

Katika Agano la Kale, nchi ya Edomu mara kwa mara hutajwa kama adui wa Israeli.

Kitabu kizima cha Obadia kinahusu uharibifu wa Edomu. Manabii wengine wa Agano la Kale pia walizungumza tabiri hasi dhidi ya Edomu.

Efeso

Ufafanuzi

Efeso ulikuwa mji wa zamani wa Kigiriki katika fukwe ya magharibi ya pale ambapo siku ya sasa ni Uturuki.

Katika kipindi cha Wakristo wa kwanza, Efeso ilikuwa mji mkuu wa Asia, ambao ulikuwa mkoa mdogo wa Kirumi katika kipindi hicho.

Kwa sababu ya eneo lake, mji huu ulikuwa kitovu muhimu sana katika biashara na safari.

Hekalu la kipagani linalojulikana kwa kuabudu mungu wa Artemi (Diana) ilikuwa Efeso.

Paulo aliishi na kufanya kazi Efeso kwa zaidi ya miaka miwili na baadaye kumteua Timotheo kuwaongoza waumini mapya kule.

Kitanu cha Waefeso katika Agano Jipya ni barua ambayo Paulo aliandika kwa waumini wa Efeso.

Efraimu

Ufafanuzi

Efraimu alikuwa mwana wa pili wa Yusufu. Vizazi vyake, Waefraimu, waliunda moja ya kabila kumi na mbili za Israeli.

Kabila la Efraimu lilikuwa moja la makabila kumi ambayo yalikuwa katika sehemu ya kaskazini ya Israeli.

Mara nyingine jina la Efraimu linatumika katika Biblia kumaanisha ufalme wote wa kaskazini wa Israeli.

Efraimu ilikuwa eneo lenye milima na miinuko mingi sana, kutokana na kumbukumbu zenye "nchi yenye milima Efraimu" au "milima ya Efraimu".

Efrata, Mwefrathi

Ufafanuzi

Efrata ilikuwa jina la mji na eneo katika sehemu ya kaskazini ya Israeli. Mji wa Efrata baadaye uliitwa "Bethehemu" au "Efrata-Bethlehemu".

Efrata ilikuwa jina la mmoja wa wana wa Kalebu. Mji wa Efrata yawezekana uliitwa baada yake.

Mtu ambaye alikuwa ametoka mji wa Efrata alikuwa akijulikana kama "Mwefrathi".

Boazi, babu mkuu wa Daudi, alikuwa Mwefrathi.

Ekroni

Ufafanuzi

Ekroni ni mji mkuu wa Wafilisti, uliopo maili tisa barani kutoka bahari ya Mediteraniani.

Hekalu la mungu wa uongo Baal-zebubu ilikuwa Ekroni.

Pale Wafilisti walipokamata sanduku la agano, walilichukua hadi Ashdodi, kisha kuhamisha hadi Gathi na Ekroni kwa sababu Mungu aliendelea kusababisha watu kuugua na kufa katika kila mji sanduku lilipokuwa likipelekwa. Hatimaye Wafilisti walirudisha sanduku Israeli.

Pale mfalme Ahazia alipoanguka kutoka kwenye paa ya nyumba yake na kujiumiza, alifanya dhambi kwa kujaribu kutafuta kutoka kwa mungu wa uongo Baal-zebubu wa Ekroni kama angekufa au la kutokana na majeraha yake. Kwa sababu ya dhambi hii, Yahwe alisema ya kuwa angekufa.

Elamu

Ufafanuzi

Elamu alikuwa mwana wa Shemu na mjukuu wa Nuhu.

Vizazi vya Elamu vilikuwa vinaitwa "Waelami" na waliishi katika eneo lililoitwa "Elamu".

Eneo la Elamu lilikuwa kusini mashariki mwa Mto Hidekeli, ambayo sasa ni Irani magharibi.

Eleazari

Ufafanuzi

Eleazari lilikuwa jina la wanamume kadhaa katika Biblia.

Eleazari alikuwa mwana wa tatu wa kaka yake Musa Haruni. Baada ya Haruni kufa, Eleazari akawa kuhani mkuu Israeli.

Eleazari lilikuwa pia jina la mmoja wa "wanamume hodari" wa Daudi.

Eleazari mwingine alikuwa mmoja wa uzao wa Yesu.

Eliakimu

Ufafanuzi

Eliakimu lilikuwa jina la wanamume wawili katika Agano la Kale.

Mwanamume mmoja aliyeitwa Eliakimu alikuwa msimamizi wa kasri chini ya Mfalme Hezekia.

Mwanamume mwingine aliyeitwa Eliakimu alikuwa mwana wa Mfalme Yosia. Alifanywa mfalme wa Yuda na farao wa Misri, Necho.

Necho alibadili jina la Eliakimu kuwa Yehoyakimu.

Elisabeti

Ufafanuzi

Elisabeti alikuwa mama wa Yohana Mbatizaji. Jina la mume wake lilikuwa Zakaria.

Zakaria na Elisabeti hawakuwahi kuweza kupata watoto, lakini katika uzee wao, Mungu alimuahidi Zakaria ya kwamba Elisabeti angezaa mtoto wa kiume.

Mungu alitunza ahadi yake, na punde Zakaria na Elisabeti wakaweza kupata mimba, naye akazaa mtoto wa kiume. Walimuita mtoto yule Yohana.

Elisabeti pia alikuwa jamaa kwa Mariamu, mama wa Yesu.

Elisha

Ufafanuzi

Elisha alikuwa nabii katika Israeli wakati wa tawala za wafalme wa Israeli: Ahanu, Ahazia, Yehoramu, Yehu, Yehoahazi, na Yehoashi.

Mungu alimwambia nabii Eliya kumpaka mafuta Elisha kama nabii.

Eliya alipochukuliwa kwenda mbinguni katika kibandawazi cha moto, Elisha akawa nabii wa Mungu kwa wafalme wa Israeli.

Elisha alifanya miujiza mingi, ikiwemo kuponya mwanamume kutoka Shamu aliyekuwa na ukoma na kufufua kutoka kwa wafu mtoto wa mwanamke kutoka Shunemu.

Eliya

Ufafanuzi

Eliya alikuwa mmoja wa manabii muhimu sana wa Yahwe. Eliya alitabiri katika wakati wa tawala za wafalme kadhaa wa Israeli au Yuda, akiwemo Mfalme Ahabu.

Mungu alifanya miujiza mingi kupitia Eliya, ikiwemo kumfufua mvulana mfu kurudi katika uhai.

Eliya alimkaripia Mfalme Ahabu kwa kuabudu mungu wa uongo Baali.

Aliwapa changamoto manabii wa Baali katika mtihani ambao ulithibitisha ya kwamba Yahwe ni Mungu mmoja wa kweli.

Katika mwisho wa maisha ya Eliya, Mungu alimchukua kimuujiza juu mbinguni angali bado yu hai.

Miaka mia moja baadaye, Eliya, pamoja na Musa, walijitokeza na Yesu juu ya mlima na waliongea pamoja juu ya kurudi, kuteseka na kufa kwa Yesu Yerusalemu.

Engedi

Ufafanuzi

Engedi ni jina la mji katika nyika ya Yuda kusini mashariki mwa Yerusalemu.

Engedi ilikuwa mahali mwa ukingo wa magharibi wa Bahari ya Chumvi.

Sehemu ya jina lake, "chemichemi" ina maana ya chemichemi ya maji ambayo inatiririka chini kutoka kwenye mji hadi baharini.

Engedi ilijulikana kwa kuwa na mashamba ya mizabibu mizuri na ardhi yenye rutuba nyingine, yawezekana kutokana na mwendelezo wa umwagiliaji kutoka kwa chemichemi ya maji.

Kulikuwa na ngome katika Engedi ambayo Daudi alitoroka kule alipokuwa akifukuzwa na Mfalme Sauli.

Esau

Ufafanuzi

Esau alikuwa mmoja wa mapacha wana wa Isaka na Rebeka. Alikuwa mtoto wa kwanza kuzaliwa. Pacha ndugu yake alikuwa Yakobo.

Esau aliuza haki yake ya mzawa wa kwanza kwa kaka yake Yakobo kwa kubadilishana na bakuri la chakula.

Kwa kuwa Esau alizaliwa kwanza, baba yake Isaka alitakuwa kumpatia baraka maalumu. Lakini Yakobo alimdanganya Isaka kumpatia hiyo baraka badala yake. Mara ya kwanza Esau alikuwa na hasira sana hadi alitaka kumuua Yakobo, lakini baadaye alimsamehe.

Esau alikuwa na watoto wengi na wajukuu, na vizazi hivi viliunda kuni kubwa la watu walioishi katika nchi ya Kaanani.

Esta

Ufafanuzi

Esta alikuwa mwanamke wa Kiyahudi ambaye alikuwa malkia wa ufalme wa Ashuri katika kipindi cha mateka ya Babeli kwa Wayahudi.

Kitabu cha Esta kinaelezea simulizi ya jinsi Esta alivyokuwa mke wa mfalme wa Waashuri Ahasuero na jinsi Mungu alivyomtumia kukomboa watu wake.

Esta alikuwa yatima ambaye alikuzwa na binamu yake mkubwa, Mordekai.

Kutii kwake kwa baba yake wa kambo kulimsaidia kuwa mtiifu kwa Mungu.

Esta alimtii Mungu na kuweka maisha yake hatarini ili kuwakomboa watu wake, Wayahudi.

Simulizi ya Esta inaelezea utawala wa Mungu wa enzi juu ya matukio na historia, haswa jinsi anavyolinda watu wake na kutumika kupitia wale wanaomtii.

Ethiopia, Mtu wa Ethiopia

Ufafanuzi

Ethiopia ni nchi katika Afrika iliyo kusini mwa Misri mpakana mwa Mto wa Naili magharibi na katika Bahari ya Shamu mashariki. Mtu kutoka Ethiopia na "mtu wa Ethiopia".

Ethiopia ya zamani ilikuwa kusini mwa Misri na ilijumuisha nchi ambayo kwa sasa ni sehemu ya baadhi ya nchi za Afrika, kama Sudani, Ethiopia ya sasa, Somalia, Kenya, Uganda, Afrika ya Kati na Chadi.

Katika Biblia, Ethiopia mara nyingine huitwa "Kushi" au "Nubia".

Nchi za Ethiopia ('Kushi') na Misri mara nyingine hutajwa pamoja katika Biblia, labda kwa sababu zilikuwa karibu na nyenzake na watu wake yawezekana walikuwa na mababu wa kufanana.

Mungu alimtuma Filipo mwinjilisti katika jangwa ambapo alisambaza habari njema kuhusu Yesu na towashi wa Ethiopia.

Ezekieli

Ufafanuzi

Ezekieli alikuwa nabii wa Mungu wakati wa kipindi cha uhamisho ambapo Wayahudi wengi walipelekwa Babeli.

Ezekieli alikuwa kuhani aliyeishi katika ufalme wa Yuda ambapo yeye na Wayahudi wengine wengi walikamatwa na jeshi la Babeli.

Kwa zaidi ya miaka ishirini, yeye na mke wake waliishi Babeli karibu na mto, na Wayahudi walikuja pale kumsikiliza akizungumza ujumbe kutoka kwa Mungu.

Miongoni mwa wafalme wengine, Ezekieli alitabiri juu ya uharibifu na ujenzi wa Yerusalemu na hekalu.

Pia alitabiri kuhusu ufalme wa baadaye wa Masihi.

Ezra

Ufafanuzi

Ezra alikuwa kuhani wa Israeli na mtaalamu wa sheria ya Kiyahudi ambaye aliweka kumbukumbu ya historia ya kurudi kwa Waisraeli Yerusalemu kutoka Babeli ambapo Israeli alikuwa mateka kwa miaka 70.

Ezra aliweka kumbukumbu ya sehemu hii ya historia ya Israeli katika kitabu cha kibiblia cha Ezra. Inawezekana aliandika kitabu cha Nehemia, kwa maana vitabu hivi viwili asili yake ilikuwa kitabu kimoja.

Ezra aliporudi Yerusalemu aliimarisha Sheria, kwa maana Waisraeli waliacha kutii Ssheria za Sabato na walioana na wanawake ambao walitenda dini za kipagani.

Ezra pia alisaidia kujenga hekalu ambalo lililharibiwa na Wababeli walipoteka Yerusalemu.

Kuna wanamume wengine wawili wanaoitwa Ezra waliotajwa katika Agano la Kale.

Farao, mfalme wa Misri.

Ufafanuzi

Hapo nyakati za kale wafalme waliotawala nchi ya Misri waliitwa Mafarao.

- Kwa pamoja zaidi ya wafalme 300 walitawala Misri kwa miaka zaidi ya 2,000.
- Wafalme hawa wa Misri walikuwa na nguvu na utajiri.
- Baadhi ya Mafarao hawa wametajwa kwenye Biblia.
- Mara nyingi cheo hiki kimetajwa kama jina na sio cheo.

Filipi

Ufafanuzi

Filipi ulikuwa mji muhimu na koloni la Rumi lililokuwa Makedonia kaskazini mwa Ugiriki ya kale.

- Paulo na Sila walisafiri kuhubiri kuhusu Yesu kwa watu wa huko.
- Wakiwa Filipi Paulo na Sila walikamatwa, lakini Mungu aliwaweka huru kwa muujiza.
- Katika agano jipya kitabu cha Wafilipi ni barua ya mtume Paulo aliyowaandikia Wakristo katika kanisa la Filipi.
- Kumbuka kuwa huu ni mji tofauti na Kaisaria Failipi ambayo ilikuwa kaskazini mashariki mwa Israeli karibu na mlima Hermoni.

Filipo, mtume

Ufafanuzi

Mtume Filipo alikuwa mmoja wa wanafunzi kumi na mbili wa Yesu alikuwa anatoka mji wa Bethsaida.

- Filipo alimleta Nathanaeli kumwona Yesu,
- Yesu alimuuliza Filipo namna ya kuwapa chakula kundi la watu zaidi ya 5,000.
- Katika chakula cha mwisho cha pasaka ambacho Yesu alikula na wanafunzi wake alizungumza nao kuhusu Mungu baba yake. Filipo aliuliza swali awaoneshe baba.
- Lugha zingine huwa zinaandika herufi tofauti ili kutofautisha jina la Filipo na Filipo wengine kama Mwinjilisti Filipo ili kuondoa utata.

Filipo, mwinjilisti

Ufafanuzi

Katika kanisa la kwanza huko Yerusalemu Filipo alikuwa mmoja wa viongozi saba waliochaguliwa ili kuwajali masikini, Wakristo wenye uhitaji hasa wajane.

- Mungu alimtumia Filipo kushirikisha Injili kwa watu katika miji mingi tofauti huko Yudea na Galilaya akiwepo mtu wa Ethiopia aliyekutana naye katika njia za jangwa la Gaza toka Yerusalemu.
- Miaka mingine baadaye Filipo aliishi Kaisaria ambapo Paulo na wafuasi wake waliishi katika nyumba yake walipokuwa wakirudi Yerusalemu.
- Wanafunzi wengi wa Biblia wanafikiri kwamba mwinjilisti Filipo hakuwa yule mtume wa Yesu aliyeitwa jina hilo.

Finehasi

Ufafanuzi

Finehasi ni jina la watu wawili katika agano la kale.

- Mmoja wa wajukuu wa Haruni alikuwa kuhani aliyeitwa finehasi aliyepinga kwa nguvu kuabudu miungu ya uongo.
- Finehasi aliwaokoa Waisraeli toka kwenye pigo ambalo bwana alilituma ili kuwaadhibu kwa kuwaoa wanawake wa Midiani na kuabudu miungu yao ya uongo.
- Katika matukio mbali mbali Finehasi alikwenda na jeshi la Israeli kuwapiga Wamidiani.
- Finehasi mwingine aliyetajwa kwenye agano la kale alikuwa mmoja wa wana waovu wa kuhani Eli katika kipindi cha nabii Samweli.
- Finehasi na kaka yake Hofini waliuawa kipindi ambacho Wafilisti walivamia Israeli na kuiba sanduku la agano.

Finisia

Ufafanuzi

Nyakati za kale Finisia lilikuwa taifa lenye utajiri lililokuwa Kanaani karibu na pwani ya barari ya Mediteraniani, kaskazini mwa Israeli.

- Finisia ilijumuisha sehemu ya nchi iliyokuwa magharibi mwa mji ambao kwa sasa ni Lebanoni.
- Katika agano jipya Mji kuu wa Finisia ulikuwa Tire. Mji mwingine wa Muhimu ulikuwa Sidoni.
- Wafinisia alijulikana sana kwa ustadi wao wa kutendeneza mbao kwa kutumia mwerezi, pia walijulikana kwa uwezo wao wa kusafiri na kufanya biashara baharini. Walikuwa na uwezo mkubwa wa kutengeneza Boti.
- Moja ya alfabeti za mwanzoni kabisa ziliundwa na Wafinisia. Alfabeti zao zilitumika sana kwa sababu ya mwingiliano mkubwa waliokuwa nao na makundi ya watu kupitia biashara.

Gabrieli

Ufafanuzi

Gabrieli ni jina la mmoja wa malaika wa Mungu. Anatajwa kwa majina kadhaa, kote katika Agano la kale na Jipya.

Mungu alimtuma Gabrieli kumwambia nabii Danieli maana ya maono aliyoyaona. Muda mwingine, Danieli alipokuwa akiomba, malaika Gabrieli alipaa kwake na kutabiri kuhusu kile kitakachotokea hapo baadaye. Danieli alimfafanua kama "mwanamume". Katika Agano Jipya inaandikwa ya kwamba Gabrieli alitokana na Zakaria kutabiri ya kwamba mke wake mzee Elizabeti angepata mwana wa kiume, Yohana. Miezi sita baada ya hapo, Gabrieli alitumwa kwa Mariamu kumwambia ya kwamba Mungu angemuwezesha kwa miujiza kupata mimba ya mtoto amabye angekuwa "Mwana wa Mungu". Gabrieli alimwambia Mariamu kumuita mwanawe "Yesu" .

Gadi

Ufafanuzi

Gadi ni jina la mmoja wa wana wa Yakobo, yaani, Israeli.

Familia ya Gadi ilikuja kuwa moja ya makabila kumi na mawili ya Israeli. Mwanamume mwingine katika Biblia aitwaye Gadi alikuwa nabii, ambaye alimkabili Mfalme Daudi kwa dhambi ya kufanya sensa ya watu wa Israeli. Miji ya Baalgadi na Migdalgadi kila moja wapo ni maneno mawili katika maandishi asili na mara nyigine huandikwa " Baali gadi" na "Migdali Gadi".

Galatia

Ufafanuzi

Katika kipindi cha Agano Jipya, Galataia ulikuwa mkoa mkubwa wa Kirumi ulioko sehemu ya kati ya mahali ambapo sasa ni nchi ya Uturuki.

Sehemu ya Galatia ilikuwa mpaka na Bahari Nyeusi upande wa Kaskazini. Ilikuwa mpakani na mikoa ya Asia, Bithinia, Kapadocia, Selisia na Pamfilia.

Mtume Paulo aliandika barua kwa Wakristo walioishi katika mkoa wa Galatia. Barua hii ni kitabu cha Agano Jipya cha "Wagalatia".

Sababu moja ambayo Paulo aliandika barua yake kwa Wagalatia ilikuwa kusisitiza tena injili ya wokovu kwa neema, na sio kazi.

Wakristo Wayunani wa Galatia walifundishwa na Wakristo wa Kiyahudi kule ya kwamba ilikuwa lazima kwa waumini kukaa na baadhi ya sheria za Kiyahudi.

Galilaya, Mgalilaya

Ufafanuzi

Galilaya ni eneo la kaskazini ya Israeli, kaskazini ya Samaria. "Mgalilaya" alikuwa mtu ambaye aliishi Galilaya.

Galilaya, Samaria, na Yudea ilikuwa miji mitatu ya msingi ya Israeli wakati wa Agano Jipya.

Galilaya imepakana upande wa mashariki na ziwa kubwa liitwalo "Ziwa la Galilaya".

Yesu alikua na kuishi katika mji wa Nazareti Galilaya.

Miujiza mingi na mafundisho ya Yesu yalifanyika katika eneo la Galilaya.

Gathi

Ufafanuzi

Gathi ilikuwa moja ya miji mikubwa mitano ya Wafilisti. Ilikuwa kaskazini mwa Ekroni na mashariki ya Ashdodi na Ashkeloni.

Hodari wa Kifilisti Goliati alitoka katika mji wa Gathi.

Katika wakati wa Samueli, Wafilisti waliiba sanduku la agano kutoka Israeli na kulipeleka katika hekalu lao la kipagani kule Ashdodi. Baadaye likahamishwa kwenda Gathi na baadaye Ekroni. Lakini Mungu aliwaadhibu watu wa miji hiyo na maradhi, kwa hiyo walilirudisha Israeli tena.

Daudi alipokuwa akitoroka kutoka kwa Mfalme Sauli, alielekea Gathi na kuishi kule kwa muda pamoja na wake zake wawili na wanamume mia sita waliokuwa wafuasi wake waaminifu.

Gaza

Ufafanuzi

Wakati wa Biblia, Gaza ulikuwa mji tajiri wa Kifilisti uliokuwa pwani mwa Bahari ya Mediteranea, kama kilomita 38 kusini ya Ashdodi. Ilikuwa moja ya miji mitano mikuu ya Filisti.

Kwa sababu ya mahali ilipo, Gaza ilikuwa bandari muhimu ambapo masuala ya kibiashara yalifanyika kati ya makundi ya watu wengi tofauti na mataifa.

Leo, mji wa Gaza bado ni bandari muhimu katika kanda ya Gaza, ambayo ni eneo la nchi iliyoko katika pwani ya Bahari ya Mediteranea iliyopakana na Israeli upande wa kaskazini na mashariki, na kusini mwa Misri.

Gaza ilikuwa mji ambao Wafilisti walimchukua Samsoni baada ya kumkamata.

Filipo mwinjilisti alikuwa akitembea katika barabara ya jangwa kuelekea Gaza alipokutana na towashi wa Ethiopia.

Gerari

Ufafanuzi

Gerari ni mji na sehemu katika nchi ya Kaanani, iliyopo kusini magharibi mwa Hebroni na kaskazini magharibi mwa Beersheba.

Mfalme Abimeleki alikuwa mtawala wa Gerari pale Abrahamu na Sara walipokuwa pale.

Wafilisti walitawala eneo la Gerari wakati wa kipindi Waisraeli waliishi Kaanani.

Geshuri

Ufafanuzi

Katika kipindi cha Mfalme Daudi, Geshuri ilikuwa ufalme mdogo uliokuwa upande wa mashariki wa Ziwa la Galilaya, kati ya nchi za Israeli na Aramu.

Mfalme Daudi alimuoa Maaka, binti wa mfalme wa Geshuri na akamzalia mwana wa kiume, Absalomu.

Baada ya kumuua ndugu yake Amnoni, Absalomu alikimbilia kaskazini mashariki mwa Yerusalemu hadi Geshuri, umbali wa kama maili 88. Alikaa kule miaka mitatu.

Gethsemane

Ufafanuzi

Gethsemane ilikuwa bustani ya mizeituni mashariki mwa Yerusalemu mbali ya bonde la Kidroni karibu na Mlima wa Mizeutuni.

Bustani ya Gethsemane ilikuwa sehemu ambapo Yesu na wafuasi wake walienda kuwa wenyewe na kupumzika, mbali na mikusanyiko.

Ilikuwa Gethsemane ambapo Yesu aliomba kwa huzuni kubwa, kabla ya kukamatwa pale na viongozi wa Kiyahudi.

Gibea

Ufafanuzi

Gibea ni jina la mji ambao ulikuwa kaskazini mwa Yerusalemu na kusini ya Betheli.

Gibea ilikuwa eneo la kabila la Benyamini.

Ilikuwa eneo la vita kubwa kati ya Wabenyamini na Israeli.

Gibeoni. Wagibeoni

Ufafanuzi

Gibeoni ilikuwa mji ambao ulikuwa kama kilomita 13 kaskazini magharibi mwa Yerusalemu. Watu walioishi Gibeoni walikuwa Wagibeoni.

Wagibeoni waliposikia jinsi Waisraeli wameangamiza miji ya Yeriko na Ai, waliogopa.

Kwa hiyo Wagibeoni walikuja kwa viongozi wa Israeli Gilgali na kuvunga kuwa watu kutoka nchi ya mbali.

Viongozi wa Israeli walidanganywa na kufanya makubaliano na Wagibeoni ya kwamba watawalinda na kutowaangamiza.

Gideoni

Ufafanuzi

Gideoni alikuwa mwanamume wa Kiisraeli ambaye aliinuliwa na Mungu kuwakomboa Waisraeli kutoka kwa adui zao.

Katika kipindi ambacho Gideoni aliishi, kundi la watu lijulikanalo kama Midiani waliendelea kuwashambulia Waisraeli na kuangamiza mazao yao.

Ingawa Gideoni aliogopa, Mungu alimtumia kuwaongoza Waisraeli kupigana dhidi ya Midiani na kuwashinda.

Gideoni pia alimtii Mungu kwa kuangusha madhabahu chini ya miungu wa uongo wa Baali na Ashera.

Hakuwaongoza tu watu katika kuwashinda adui zao lakini pia aliwatia moyo kutii na kumwabudu Yahwe, Mungu mmoja wa ukweli.

Gileadi

Ufafanuzi

Gileadi ni jina na eneo la milima mashariki mwa mto Yordani, ambapo kabila la Waisraeli la Gadi, Rubeni na Manase waliishi.

Eneo hili pia lilijulikana kama "nchi ya mlima wa Gileadi" au "Mlima Gileadi".

"Gileadi" ilikuwa jina la wanamume kadhaa katika Agano la Kale. Mmoja wa wanamume hawa alikuwa mjukuu wa Manase. Gileadi mwingine alikuwa baba wa Yefta.

Gilgali

Ufafanuzi

Msemo Gilgali ulikuwa mji kaskazini mwa Yeriko na ilikuwa sehemu ya kwanza ambayo Waisraeli waliweka kambi baada ya kuvuka mto Yordani kuingia Kaanani.

Kula Gilgali, Yoshua aliweka mawe kumi na mawili kutoka mto uliokauka wa Mto Yordani ambao walimaliza kuuvuka.

Gilgali ulikuwa mji ambao Eliya na Elisha walishi walipovuka Yordani pale Eliya alipochukuliwa kwenda mbinguni.

Kulikuwa na sehemu zingine pia zijulikanazo kama "Gilgali" katika Agano la Kale.

Neno "gilgali" lina maana ya "mduara wa mawe" labda kumaanisha sehemu ambapo dhabahu ya mduara ilijengwa.

Katika Agano la Kale, jina hili mara nyingi hujitokeza kama "gilgali". Hii inaweza kuonyesha ya kwamba haikuwa mahali bayana lakini ilikuwa ufafanuzi wa ain fulani ya sehemu.

Giriki

Ufafanuzi

Katika kipindi cha Agano Jipya, Giriki ilikuwa mkoa katika Ufalme wa Kirumi.

Kama nchi ya siku ya sasa ya Giriki, ilikuwa katika peninsula ambayo ilikuwa mpakani na Bahari ya Mediteranea, Bahari ya Aegea, na Bahari ya Ionia.

Mtume Paulo alizuru miji kadhaa ya Giriki, na kuimarisha makanisa katika miji ya Korintho, Thesalonike, na Filipi na labda mingine.

Watu ambao hutoka Giriki wanaitwa "Wagiriki" na lugha yao ni "Kigiriki". Watu kutoka mikoa mingine ya Kirumi pia walizungumza Kigiriki, ikiwemo Wayahudi wengine.

Mara nyingine msemo "Giriki" hutumika kumaanisha Mataifa.

Golgotha

Ufafanuzi

Msemo "Golgotha" ni jina la mahali ambapo Yesu alisulubiwa. Inatokana na neno la Kiaramea ambalo lina maana ya "Fuvu la kichwa" au "Mahali pa fuvu la kichwa".

Golgotha ilikuwa mahali nje ya kuta za mji wa Yerusalemu, eneo la karibu. Labda ilikuwa mahali ya mteremko wa Mlima wa Mizeituni.

Katika tafsiri za Kiingereza za zamani za Biblia, Golgotha inatafsiriwa kama "Kalivari" ambayo inatokana na neno la Kilatini kwa ajili ya "fuvu la kichwa".

Tafsiri nyingi za Biblia hutumia neno ambalo huonekana au kusikika kama "Golgotha" kwa maana maana yake tayari imefafanuliwa katika maandisha ya Biblia.

Goliati

Ufafanuzi

Goliati alikuwa mwanajeshi mrefu sana, na mkubwa sana katika jeshi la Wafilisti ambaye aliuwawa na Daudi.

Goliati alikuwa kati ya mita mbili au tatu kwa urefu. Mara nyingi huchukuliwa kama jitu kwa sababu ya umbo lake kubwa.

Ingawa Goliati alikuwa na silaha bora zaidi na mkubwa kuliko Daudi, Mungu alimpa Daudi nguvu na uwezo wa kumshinda Goliati.

Waisraeli walitangazwa washindi juu ya Wafilisti kama matokea ya ushindi wa Daudi juu ya Goliati.

Gomora

Ufafanuzi

Gomora ilikuwa mji katika bonde lenye rutuba, karibu na Sodoma ambapo mpwa wa Abrahamu Lutu alichagua kuishi.

Mahali haswa pa Gomora na Sodoma hapajulikani, lakina kuna viashiria ya kwamba inaweza kuwa mahali moja kwa moja kusini mwa Bahari ya Chumvi, karibu na Bonde la Sidimu.

Kulikuwa na wafalme wengi vitani katika eneo ambapo Sodoma na Gomora na ilikuwepo.

Familia ya Lutu ilipokamtwa katika ugomvi kati ya Sodoma na miji mingine, Abrahamu na wanamume wake waliwakomboa.

Sio muda baada ya hapo, Sodoma na Gomora ziliteketezwa na Mungu kwa sababu ya uovu wa watu walioishi pale.

Gosheni

Ufafanuzi

Gosheni ni jina la eneo la nchi yenye rutuba ambalo lilikuwa mahali katika Mto Naili katika sehemu ya kusini ya Misri.

Yusufi alipokuwa mtawala wa Misri, baba yake na ndugu na familia zao walikuja kuishi Gosheni kutoroka njaa Kaanani.

Wao na uzao wao waliishi vzuri Gosheni kwa zaidi ya miaka 400, lakini walilazimishwa katika utumwa na farao wa Kimisri.

Hatimaye Mungu alimtuma Musa kuwasaidia watu wa Israeli kuondoka nchi ya Gosheni na kutoroka utumwa.

Habakuki

Ufafanuzi

Habakuki alikuwa ni nabii wa Agano la Kale aliyeishi kipindi cha Mfalme Yehoyakimu alipokuwa akiitawala Yuda. Pia, nabii Yeremia alikuwa bado yuko hai katika kipindi hicho. Nabii huyu aliandika kitabu cha Habakuki mnamo mwaka 600 KK, katika kipindi ambacho Wababeli walikuwa wameuhusuru mji wa Yerusalem na kuchukua watu wengi wa Yuda na kuwapeleka matekani. Yahweh alimpa Habakuki unabii kuhusu Wakaldayo (Wababeli) ambao wangekuja na kuwateka watu wa Yuda. Moja kati ya misemo maarufu na iliyojulikana sana ya nabii Habakuki ni "Mwenye haki ataishi kwa imani."

Habili

Ufafanuzi

Habili alikuwa mtoto wa Adamu na Hawa. Alikuwa ndogo wake na Kaini. Habili alikuwa mfugaji. Habili alitoa sadaka ya baadhi ya mifugo yake kwa Mungu. Mungu alipendezwa na sadaka ya Habili.
Mtoto wa kwanza wa Adamu na Hawa, Kaini alimuua Habili.

Hagai

Ufafanuzi

Hagai alikuwa ni nabii wa Yuda katika kipindi ambacho Wayahudi walikuwa wamerudi kutoka matekani huko Babeli. Hagai alitabiri katika kipindi ambacho watu wa Israeli walikuwa chini ya utawala wa liwali Zerubabeli. katika kipindi hiki pia, nabii Zekaria alikuwa akitabiri yaani Hagai na Zekaria walifanya kazi katika kipindi kimoja. Hagai na Zekaria waliwasihi sana Wayahudi ili walijenge Hekalu ambalo lilikuwa limebomolewa na Wababeli chini ya mfalme Nebukadreza.

Hajiri

Ufafanuzi

Hajiri alikuwa ni mwanamke wa Kimisri alikuwa mtumwa wa Sara. Sara alimtoa Hajiri kwa Ibrahimu ili aweze kuzaa naye, baada ya kuona kuwa yeye (Sara) hana uwezo wa kuzaa . Hajiri alipata mimba na akamzalia Ibrahim mwana, Ishmaeli. Mungu aliiangalia taabu ya Hajiri katika jangwa na akaahidi kuubariki uzao wa Hajiri.

Hamathi, Lebo Hamathi, Wahamathi

Ufafanuzi

Hamathi ulikuwa ni mji muhimu sana kasikazini mwa Kanaani. Wahamathi walikuwa ni uzao wa mtoto wa Nuhu, Kanaani. Jina 'Lebo Hamathi' huenda linarejelea mlima ulikuwa karibu na mji wa Hamathi. Baadhi ya tafsiri hufasiri 'Lebo Hamathi' kama "Mlango wa Hamathi" Mfalme Daudi alimshinda mfalme Tou wa Hamathi, ushindi ambao uliwafanya kuwa katika makubaliano na mahusiano mazuri. Hamathi ulikuwa ni mji wa bohari au ghala la mfalme Sulemani, mahali ambapo alitunza hazina yake. Ni katika nchi hii ya Hamathi ambapo mfalme Zedekia aliuawa na mfalme Nebukadreza, pia ni mahali ambapo mfalme Yehoyazi alikamatwa na Farao wa Misri. Neno 'Wahamathi' laweza kutafsiriwa kama ' watu wa Hamathi'

Hamori

Ufafanuzi

Hamori alikuwa mkanaani aliyeishi katika mji wa Shekemu katika kipindi ambacho Yakobo na familia yake walikuwa wakiishi karibu na Sukothi. Alikuwa ni Mhivi. Yakobo alinunu eneo la maziko kutoka kwa wana wa Hamori. Wakali wakiwa huko mwana mmoja wa Hamori, Shekemu alimbaka binti wa Yakobo aliyeitwa Dina. Kaka zake na Dina walilipiza kisasi kwa familia ya Hamori na kuwaua watu wote katika mji wa shekemu.

Hamu

Ufafanuzi

Hamu ni mtoto wa pili kati ya wana watatu wa Nuhu. katika gharika kuu la kidunia ambalo liliigharikisha dunia yote, Hamu na ndugu zake pamoja na wake zao walikuwa pamoja na baba yao, Nuhu katika safina. Baada ya gharika, kulikuwa na tukio la Hamu kutomweshimu baba yake, Nuhu. Na matokeo yake, Nuhu alimlaani mtoto wa Hamu alilyeitwa Kanaani pamoja na uzao wake wote, ambao baadaye walijulikana kama Wakanaani.

Hana

Ufafanuzi

Hana alikuwa ni mama wa nabii Samwel. Alikuwa ni mmoja kati ya wake waili wa Elikana. Hana alikuwa tasa, alikuwa hawezi kuzaa mtoto. Hiki kilikuwa ni kilio kikubwa sana kwa Hana. Hana alimwomba Mungu kwa bidii sana hekaluni ili apate mtoto. Hana alimwahidi Mungu kumtoa mtoto huyu ili amtumikie Mungu. Mungu alimpa haja yake na mtoto Samweli alipokuwa na umri wa kutosha, alimleta ili atumike hekaluni hekaluni.
Mungu alimpa Hana watoto wengine baada ya hayo.

Hanania

Ufafanuzi

Jina Hanania limetumika katika Agano la Kale kurejelea watu mbalimbali. Hanania mmoja alikuwa ni mwisraeli aliyechukuliwa matekani huko Babeli ambaye Jina lake lilibadilishwa na kuwa 'Shadraka.' kutoka na tabia na uwezo wake, alipewa nafasi nzuri maana alikuwa mtumwa wa kifalme. Hanania (Shadraka) na vijana wengine wawili wa Kiisraeli walitupwa katika tanuru la mot kwasababu walikataa kumwabudu wa mfalme wa Babeli. Mungu alionesha uwezo wake kwa kuwalinda ili wasije wakadhurika. Hanania mwingine alikuwa ni mzao wa ukoo wa Mfalme Sulemani. Kulikuwa na Hanania mwingine tofauti aliyekuwa nabii wa uongo katika kipindi cha nabii Yeremia. Mtu mmoja aliyeitwa Hanania alikuwa ni kuhani aliyesaidia kuongoza sherehe katika kipindi cha Nehemia.

Harani

Ufafanuzi

Harani alikuwa kaka mdogo wa Ibrahimu na baba yake na Lutu. harani pia lilikuwa ni jina la mji ambao Ibrahimu na familia yake waliishi kwa muda mfupi walipokuwa njiani kutoka Uru kwenda nchi ya Kanaani. Mtu mwingine tofauti aliyeitwa Harani alikuwa ni mtoto wa Kalebu. Mtu wa tatu katika Biblia aliyeitwa Harani alikuwa ni wa uzao wa Lawi.

Haruni

Ufafanuzi

Haruni alikuwa kaka yake na Musa. Mungu alimchagua Haruni kuwa kuhani mkuu wa kwanza wa watu wa Israeli. Haruni alimsaidia Musa kuzungumza na Farao kuhusu kuwaachia huru wana wa Israeli. Wakati wana wa Israeli wanasafiri jangwani, Haruni alitenda dhambi kwa kutengeneza sanamu ili watu waiabudu. Pia Mungu alimchagua Haruni na uzao wake kuwa makuhani.

Hawa

Ufafanuzi

Hili lilikuwa jina la mwanamke wa kwanza. Jina lake linamaanisha "uhai" au "kuishi".

Mungu alimuumba Hawa kutoka kwa ubavu ambao aliuchukua kutoka kwa Adamu.

Hawa aliumbwa kuwa "msaidizi" wa Adamu. Alikuja kando ya Adamu kumsaidia katika kazi ambayo Mungu aliwapa kufanya.

Hawa alijaribiwa na Shetani (kwa mfano wa nyoka) na alikuwa wa kwanza kufanya dhambi kwa kula tunda ambalo Mungu aliwaambia kutokula.

Hebroni

Ufafanuzi

Hebroni ulikuwa ni mji uliokuwa katika milima mirefu na ya miamba kama maili 20 hivi kusini mwa Yerusalemu. Mji huu ulijengwa mnamo mwaka 2000 KK katika kipindi cha Abramu. Mji huu ulitajwa mara nyingi katika mtiririko wa matukio mbalimbali katika Agano la Kale. Mji wa Hebroni ulikuwa na wajibu na nafasi ya muhimu sana katika maisha ya Mfalme Daudi. Wana kadhaa wa Mfalme Daudi kama vile Absalomu walizaliwa huko. Mji huu uliharibiwa na Warumi mnamo mwaka 70 BK.

Henoko

Ufafanuzi

Henoko ni jina la wanamume wawili katika Agano la Kale.

Mwanamume mmoja aliyeitwa Henoko alitokana kwa Sethi. Alikuwa babu mkuu wa Nuhu.

Henoko huyu alikuwa na uhusiano wa karibu na Mungu na alipokuwa na miaka 365, Mungu alimchukua kwenda mbinguni bila ya kufa.

Mwanamume tofauti aliyeitwa Henoko alikuwa mwana wa Kaini.

Herode Antipa

Ufafanuzi

Katika kipindi kirefu cha maisha ya Yesu, Herode Antipa alikuwa ni mtawala wa Dola ya Kirumi iliyojumuisha jimbo la Galilaya. Antipa mara nyingine alitajwa kama 'Mfalme" kama alivyokuwa baba yake, Herode Mkuu, ingawa hakuwa mfalme kweli. Herode Antipa alitawala robo au moja ya nne ya Dola ya Kirumi na hivyo aliitwa Herode 'Tetraki' yaani mkuu wa mkoa. Antipa ni 'Herode' aliye Yohamuru Yohana mbatizaji auawe kwa kukatwa kichwa. Alikuwa ni Herode Antipa pia aliyemwuuliza Yesu maswali kabla ya kusulubiwa kwake. Maherode wengine katika Agano Jipya walikuwa ni mtoto wa Antipa (Agripa) na mjukuu (Agripa wa pili) aliyetawala kipindi cha mitume.

Herode Mkuu

Ufafanuzi

Herode mkuu alikuwa akitawala Uyahudi

Herodia

Ufafanuzi

Herodia alikuwa ni mke wa Herode Antipa huko Uyahudi kipindi cha Yohana Mbatizaji. Herodia alikuwa mke halali wa kaka yake na Antipa, aliyeitwa Philipo, lakini baadaye aliolewa na Herodi Antipa kinyume na sheria. Yohana mbatizaji aliwakemea Herode na Herodia kwa sababu ya ndoa yao haramu. Na kwasababu hiyo, Yohana alifungwa gerezani na baadaye aliuawa kwa kukatwa kichwa.

Hezekia

Ufafanuzi

Hezekia alikuwa ni mfalme wa 13 wa ufalme wa Yuda. Alikuwa ni mfalme aliyemtumaini Mungu na kumtii. Tofauti na baba yake, Ahazi aliyekuwa mfalme mwovu, Mfalme Hezekia alikuwa ni mfalme mzuri aliyeharibu maeneo yote ya ibada ya miungu katika Yuda. Wakati Hezekia alipougua na alipokuwa karibu kufa, alimwomba Mungu sana ili alinde na kuhifadhi maisha yake. Mungu alimponya na alimruhusu kuishi miaka 15 zaidi. Mungu alifanya muujiza kwa Hezekia kwa kurudisha muda nyuma. Mungu alijibu maombi ya Hezekia kwa kuwaokoa watu wake kutoka mikononi mwa Mfalme Senakaribu wa Siria, aliyekuwa akiwashambulia.

Hilikia

Ufafanuzi

Hilikia lilikuwa ni jina la kuhani mkuu katika kipindi cha utawala wa mfalme Yosia. Hilikia alipata kitabu cha sheria, katika kipindi ambacho hekalu lilifanyiwa matengenezo na akamuru kitabu hicho kipelekwe kwa mfalme Yosia. Baada ya kusomewa kitabu cha sheria, Yosia alihuzunika na aliwafanya watu wa Israeli kumwabudu Yahweh tena na kutii sheria zake. Mtu mwingine aliyeitwa Hilikia alikuwa ni mwana wa Eliyakimu na alifanya kazi ikulu kipindi cha utawala wa mfalme Hezekia.

Horebu

Ufafanuzi

Mlima Horebu ni jina jingine la mlima Sinai, mahali ambapo Mungu alimpa Musa vipande vya mawe vya amri kumi za Mungu. Mlima Horebu huitwa Mlima wa Mungu Musa aliiona kichaka kilichokuwa kinawaka moto wakati akichunga kondoo katika mlima Horebu. Katika mlima Horebu, Mungu alifunua agano lake kwa Waisraeli kwa kuwapa vipande vya mawe vilivyo na Amri juu yake. Ni mahali ambapo Mungu alimwambia Musa kuupiga mwamba ili maji yatoke kwa ajili ya waisraeli katika kipindi walichokuwa wanazunguka jangwani. Sehemu maalumu ulipo mlima huu haijulikani, huenda ni sehemu ya kusini ambayo kwa sasa inajulikana kama 'Penisula ya Sinai Inawezekana kuwa Horebu lilikuwa ni jina kamili la mlima na kwamba Mlima Sinai ina maana ya milima ya Sinai kwa kurejelea ukweli kwamba Mlima Horebu ulikuwa katika jangwa la Sinai.

Hosea

Ufafanuzi

Hosea alikuwa ni nabii wa Israeli aliyeishi na kutabiri mnamo mwaka 750 KK. Huduma yake Hosea ilidumu kwa miaka mingi katika vipindi vya wafalme kadhaa, kama vile Yeroboam, Zekaria, Yotham, Ahazi, Hoshea, Uzia na Hezekia. Hosea aliambiwa na Mungu kuoa kahaba aliyeitwa Gomeri . Ingawa alikuwa mwanamke aliyekuwa si mwaminifu, Hosea aliambiwa aendelee kumpenda. Hii ilikuwa picha inayoonyesha Upendo wa Mungu kwa ajli ya watu wake, Israeli waliokuwa si waaminifu. Hosea alitabiri kinyume na watu wa Israeli kwasababu ya dhambi zao, akiwaonya kugeuka na kuacha kuabudu miungu.

Hoshea

Ufafanuzi

Hoshea lilikuwa ni jina la Mfalme wa Israeli na baadhi ya watu wengine katika Biblia. Hoshea mwana wa Ala, alikuwa ni Mfalme wa Israeli kwa miaka tisa katika kipindi ambacho Ahazi na Hezekia walikuwa wafalme wa Yuda. Yoshua mwana wa Nuni aliitwa Hoshea hapo awali. Musa alilibadilisha jina lake na kuwa Yoshua kabla ya kumtuma pamoja na wale wanaume kumi na mmoja kuipeleleza nchi ya Wakanaani. Baada ya kufa kwa Musa, Joshua aliwaongoza watu wa Israeli kuimiliki nchi ya Kanaani. Mtu mwingine aliyeitwa Hoshea alikuwa ni mwana wa Azazia na alikuwa ni mmoja wa viongozi wa Waefraimu.

Ikonio

Ufafanuzi

Ikonio ulikuwa mji sehemu ya kusini kati ya nchi ambayo sasa ni Uturuki.

Katika safari ya kwanza ya kimisionari ya Paulo, yeye na Barnaba walienda Ikonio baada ya Wayahudi kuwalazimisha kuondoka katika mji wa Antiokia. Kisha wayahudi wasioamini na Wayunani ndani ya Ikonio walipanga pia kumponda mawe Paulo na watumishi wenzeka, lakini walitoroka katika mji wa karibu wa Listra. Baada ya watu kutoka Antiokia na Ikonia kuja Listra na kuwachochea watu kumponda mawe Paulo.

Isaka

Ufafanuzi

Isaka alikuwa mwana pekee wa Abrahamu na Sara. Mungu aliwaahidi kuwapa mwana wa kiume ingiwa walikuwa wazee sana.

Jina "Isaka" linamaanisha "kicheko." Mungu alipomuambia Abrahamu kuwa Sara atazaa mwana wa kiume, Abrahamu alicheka kwa sababu wote walikuwa wazee sana. Baada ya muda, Sara pia alicheka aliposikia taarifa hii. Lakini Mungu alitimiza ahadi yake na Isaka alizaliwa kwa Abrahamu na sara katika uzee wao. Mungu alimuambia Abrahamu kuwa agano alilofanya na Abrahamu itakuwa pia ya Isaka na vizazi vyake milele. Wakati Isaka alikuwa kijana, Mungu aliijaribu imani ya Abrahamu kwa kumuamuru kumtoa isaka kama sadaka. Mwana wa Isaka, Yakobo, alikuwa na wana kumi na mbili ambao uzao wao baadaye ukawa makabila kumi na mbili ya taifa la Israeli.

Isakari

Ufafanuzi

Isakari alikuwa mwana wa tano wa Yakobo. Mama yake alikuwa Lea.

Kabila la Isakari lilikuwa moja ya makabila kumi na mbili ya Israeli. Nchi ya Isakari ilikuwa jirani na Naftali, Zabuloni, Manase, na Gadi. Ilikuwa chini ya bahari la Galilaya.

Isaya

Ufafanuzi

Isaya alikuwa nabii wa Mungu aliyetabiri wakati wa utawala wa wafalme wanne wa Yuda: Uzia, Yothamu, Ahazi, na Hezekia.

Aliishi Yerusalemu wakati Waashuri walipokuwa wakivamia mji, wakati wa utawala wa Hezekia. Kitabu cha Agano la Kale cha Isaya ni moja ya vitabu vikuu vya Biblia. Isaya aliandika unabii mwingi ulitokea wakati wa uhai wake. Isaya anajulikana zaidi kwa unabii alioandika kumhusu Masihi uliotimia miaka 700 baadaye wakati Yesu alipoishi duniani. Yesu na wanafunzi wake walinukuu utabiri wa Isaya kuwafundisha watu kuhusu Masihi.

Ishmaeli

Ufafanuzi

Ishmaeli alikuwa mwana wa Abrahamu na mtumwa wa Kimisri Hagai. Kuna wana kadhaa pia katika Agano la Kale wanaoitwa Ishmaeli.

Jina "Ishmaeli" linamaanisha, "Mungu husikia." Mungu aliahidi kumbariki mwana wa Abrahamu, Ishmaeli, lakini hakuwa mwana ambaye Mungu aliye ahidi kuweka agano lake naye. Mungu alimlinda Hagai na Ishmaeli walipotumwa jangwani. Wakati Ishmaeli alipokuwa akiishi katika jangwa la Parani, alimuoa mwanamke wa Misri. Ishmaeli mwana wa Nethania alikuwa afisa wa jeshi kutoka Yuda aliyeongoza kundi la wanaume kumua gavana aliyeteuliwa na mfalme wa Kibabeli, Nebukadreza. Pia kuna wanaume wengine wanne walioitwa Ishmaeli katika Agano la Kale.

Kadeshi, Kadesh-Barnea, Meriba Kadeshi

Ufafanuzi

Majina Kadeshi, Kadesh-Barnea, na Meriba Kadeshi yote yanazungumzia mji muhimu katika historia ya Israeli ambao ulikuwa sehemu ya kusini ya Israeli, karibu na eneo la Edomu.

Mji wa Kadeshi palikuwa oasisi, mahali palipokuwa na maji na udongo wenye virutubisho katikati ya jangwa liitwalo Sini. Musa alituma wapelelezi kumi na mbili katika nchi ya Kanaani kutoka Kadesh-Barnea. Israeli pia waliweka kambi Kadeshi wakati wakizunguka-zunguka jangwani. Kadesh-Barnea ndipo Miriamu alipofia. Ilikuwa Kadesh-Barnea ambapo Musa hakumtii Mungu na kuupiga mwamba kupata maji kwa ajili ya Waisraeli, badala ya kuzungumza nayo kama Mungu alivyomuagiza. Jina "Kadeshi" linatoka katika neno la Kihebrania lenye maana ya "takatifu" au "kuwekwa tofauti."

Kaini

Ufafanuzi

Kaini na mdogo wake Abeli walikuwa atoto wakwanza wa Adam na Hawa wametajwa katika Biblia.

- Kaini alikuwa mkulima ambaye alizalisha mazao ya chakula wakati Abeli alikuwa mfuga Kondoo.
- Kaini alimuua kaka yake Abeli kwa sababu ya wivu, kwa sababu Mungu aliipokea sadaka ya kuteketeza ya Abeli.
- Kama adhabu, Mungu alimpeleka mbali na Edeni na kumwambia kwamba aridhi hatatoa mazao kwa ajili yake.
- Mungu aliweka alama kwenye paji la uso la Kaini kama ishara kwamba Mungu atamlinda ili asiuawe na watu wengine wakati akizurura.

Kaisari

Ufafanuzi

Neno "Kaisari" lilikuwa jina au jina la heshima lililotumika kwa watawala wengi wa Dola ya Rumi. Katika Biblia, hili neno linahusisha kwa tawala tatu tofauti tofauti.

- Mtawala wa kwanza wa Rumi alikuwa anaitwa Kaisari alikuwa "Kaisaria Agustino," ambaye alitawala katika kipindi ambacho Yesu alizaliwa.
- Kama miaka thelathini baadaye, katika kipindi wakati Yohana Mbatizaji alipokuwa akihubiri, Tiberia Kaisari alikuwa mtawala wa dola ya Rumi.
- Tibaria Kaisari Alikuwa bado anatawala Rumi wakati Yesu alipowaambia watu kumlipa Kaisari kile alichokuwa anastahili na kumpa Mungu alichokuwa anastahili.
- Wakati Paulo alipokata rufaa kwa Kaisari, hii ilimhusu mtawala mkuu wa Rumi, Neru, ambaye pia alikuwa na cheo "Kaisari"
- Wakati "Kaisari" linatumika lenyewe kama cheo, pia linaweza kutafsiriwa kama: "Dola" au "Utawala wa Rumi."

Katika majina kama Kaisari Agustino au Tiberia Kaisari, "Kaisari" inaweza kutamkwa karibia na vile lugha ya taifa inavolitamka.

Kaisaria, Kaisaria Filipi

Ufafanuzi

Kaisaria ulikuwa mji wa muhimu katika pwani ya Bahari ya Meditrania, kama 39 kilomita kusini mwa Mlima Karmeli Kaisaria Filipi ulikuwa mji unaoonyesha kusinimagharibi sehemu ya Israeli, karibu na Mlima Herimoni.

- Hii miji iliitwa kwa ajili ya Makaisari ambao walitawala Dola ya Rumi.
- Pwani ya Kaisaria ilikuja ikawa mji mkuu wa Rumi mkoa wa Yudea karibia na mda wa kuzaliwa kwa Yesu.
- Mtume Petro alihubiri kwa mara ya kwanza kwa Wayunani katika Kaisaria.
- Paulo alianza safari yake kutoka Kaisaria kwenda Tarso na pia alipitia huu mji mara mbili katika safari zake za kimisionari.
- Yesu pamoja na wanafunzi wake walisafiri hadi mkoa kuzunguka Kaisaria Filipi. katika Siria. Miji yote iliitwa baada ya Herodi Filipi.

Kalebu

Ufafanuzi

Kalebu alikuwa mmoja wa wapelelezi wa Israeli ambao walitumwa na Munsa kuipeleleza nchi ya Kanaani.

- Yeye na Yoshua waliwaambia watu wamwamini Mungu ili awasaidie wawashinde Wakanaani.
- Yoshua na Kalebu walikuwa watu pekee katika uzao wao waliokubaliwa kuingia katika nchi ya ahadi ya Kanaani.
- Kalebu aliomba kuwa nchi ya Hebroni apewe yeye na familia yake. Alijua kuwa Mungu atamsaidia kuwashinda watu wanaoishi huko.

Kana

Ufafanuzi

Kana kilikuwa kijiji au mji katika Galilaya, maili tisa kaskazini mwa Nazareti.

- Kana palikuwa nyumbani kwa Nathanaeli mmoja wa wale kumi na mbili.
- Yesu alihudhuria sherehe ya harusi huko Kana na akafanya muujiza huko wa kugeuza maji kuwa divai.
- Baadaye Yesu alirudi tena Kana na akakutana na viongozi toka Kapernaumu waliomuomba amponye mtoto wao.

Kanaani, Mkanaani

Ufafanuzi

Kanaani alikuwa mtoto wa Hamu, ambaye alikuwa moja ya watoto wa Nuhu. Wakanaani walikuwa vizazi vya Kanaani.

- Neno "Kanaani" au "nchi ya Kanaani" pia limerejelewa kwenye eneo la nchi kati ya Mto Yordani na Bahari ya Meditrenia. Iliendelea kusini mpaka kwenye mpaka wa Misri na kaskazini ya mpaka wa Siria.
- Hii nchi ilikuwa makazi kwa Wakanani, na makundi ya watu wengine wengi.
- Mungu aliahidi kumpa Ibrahim na uzo wake nchi ya Kanaani, Waisraeli.

Kapranaumu

Ufafanuzi

Kapranaumu kilikuwa kijiji cha uvuvi katika kusini magaharibi ya pwani ya Bahari ya Galilaya.

- Yesu aliishi Kaperanaumu wakati alipokuwa akifundisha Kalilaya.
- Baadhi ya wanafunzi wake walitokea Kaperanaumu.
- Yesu pia alifanya miujiza mingi katika mji huu, pamoja na kumfufua binti aliyekuwa amekufa.
- Kapranaumu ilikuwa moja ya miji mitatu ambayo Yesu aliwaonya hadharani kwa sababu watu wao walimkataa na hawakuamini ujumbe wake. Aliwaonya kwamba Mungu angewaadhibu kwa kutokuamini kwao.

Karmeli, Mlima Karmeli

Ufafanuzi

Mlima Karmeli ni mlima uliokuwa pwani mwa bahari ya Mediteraniani kaskazini mwa nchi tambarare ya Sharon. Urefu wake ni mita 546.

- Pia kulikuwa na mji ulioitwa Karmeli uliokuwepo Yuda kusini mwa bahari ya chunvi.
- Tajiri aliyemilikia ardhi Nabali na mke wake Abigaili waliishi karibu na mji wa Karmeli ambapo Daudi na watu wake walimsaidia Kulinda manyoya ya kondoo.
- Katika mlia Karmeli Eliya alishindana na manabii wa Baali ili kuthibitisha kuwa Bwana ni Mungu wa kweli pekee.
- Kuliweka hili sawa huu haukuwa mlima mmoja. Mlima Karmeli waweza kutafsiriwa kama "mlima katika safu ya milima ya Karmeli."

Kedari

Ufafanuzi

Kedari lilikuwa jina la mwana wa pili wa Ishmaeli. Lilikuwa pia jina la mji muhimu ambalo linawezekana kuwa liliitwa baada ya huyo mwanamme

Mji wa Kaderi inapatikana katika eneo la kaskazini la Arabia karibu na mpaka wa kusini ya Filisti. Katika nyakati za Biblia, palikuwa panajulikana kwa ukuu na uzuri wake. Wazawa wa Kaderi waliunda kundi kubwa la watu linaloitwa "Kaderi." Usemi "hema za Kedari nyeusi" inamaanisha hema za nywele nyeusi za mbuzi ambamo watu wa Kaderi waliishi. Watu hawa walifuga kondoo na mbuzi. Pia walitumia ngamia kwa kusarifishia vitu. Katika Biblia, usemi "utukufu wa Kedari" inamaanisha ukuu wa mji na watu wake.

Kedeshi

Ufafanuzi

Kedeshi ulikuwa mji wa Kanaani uliochukuliwa na Waisraeli walipoingia Kanaani.

Mji huu ulikuwa sehemu ya kaskazini mwa Israeli, katika kipande walichopewa kabila la Naftali. Kedeshi ulikuwa moja ya miji iliyochaguliwa kwa ajili ya makuhani wa Kilawi kuishi, kwa sababu hawakuwa na ardhi yao wenyewe. Ilitengwa pia kama "mji wa ukimbizi."

Kefa

Ufafanuzi

Kefa alikuwa kuhani wa Israeli katika kipindi cha Yohana Mbatizaji na Yesu.

- Kefa alicheza nafasi kubwa katika kujaribu kumlaani Yesu.
- Kuhani mkuu Anasi na Kefa walijaribu kuwajaribu Petro na Yohana wakati walipokuwa wamekamatwa baada ya kumponya kiwete.
- Kefa ndiye aliyesema kwamba ilikuwa vyema mtu mmoja afe kwa ajili ya taifa kuliko kwa taifa zima kuangamia. Mungu alimfanya kusema hii kama unabii unaohusu ambavyo Yesu angeweza kufa kuokoa watu wake.

Kilikia

Ufafanuzi

Kilikia ni mkoa mdogo wa Rumi uliokuwa kusini mashariki mwa nchi ya Uturuki.

- Mtume Paulo alikuwa mwananchi wa mji wa Tarso uliokuwa Kilikia.
- Paulo alikaa miaka saba Kilikia baada ya kukutana na Yesu njiani Damaskas.
- Baadhi ya Wayahudi toka Kilikia walikuwa wale waliomfuata Stefano na kuwashawishi watu wampige kwa mawe mpaka kufa.

Kipro

Ufafanuzi

Kipro ni kisiwa katika bahari ya Mediteraniani karibu kilometa 64 kusini mwa nchi ya sasa ya Uturuki.

- Barnaba alikuwa anatokea Kipro hivyo inawezekana binamu yake Johana Marko alitokea huko pia.
- Paulo na Barnaba walihubiri kwa pamoja katika kisiwa cha Kipro katika mwanzo wa safari yao ya Kimisionari. Yohana Marko alikuja baadaye kuwasaidia katika safari zao.
- Baadae Barnaba na Marko walitembelea tena Kipro. Katika agano la kale Kipro imetajwa kama eneo lenye utajiri wa miti ya Miteashuri.

Kolosai, Wakolosai

Ufafanuzi

Katika agano jipya Kolosai ulikuwa mji katika Rumi nchi ambayo sasa ni kusini mangharibi mwa uturuki. Wakolosai ni watu walioishi Kolosai.

- Ilikuwa kama maili 100 toka bahari ya mediteraniani, Kolosai ilikuwa njia kuu ya biashara kati ya mji wa Efeso na mto Efrata.
- Alipokuwa gerezani Rumi Paulo aliandika barua kwa Wakolosai ili kusahihisha mafundisho ya uongo kati ya waamini waliokuwa Kolosai.
- Alipokuwa akiandika barua Paulo hakutembelea kanisa katika Kolosai lakini alisikia habari za waamini toka kwa mtumishi mwenzake Epafra.
- Epafra alikuwa mfanyakazi wa Kikristo aliyeanzisha kanisa Kolosai.
- Kitabu cha Filemoni ni barua ya Paulo kwa waliokuwa wakimiliki watumwa huko Kolosai.

Kora

Ufafanuzi

Kora lilikuwa jina la wanaume watatu katika Agano la Kale.

Mmoja wa wana wa Esau aliitwa Kora. Alikuwa kiongozi katika jamii yake. Kora pia alikuwa mzawa wa Lawi na kwa hiyo alitumika katika maskani kama kuhani. Alikuwa na wivu juu ya Musa na Haruni na kuongoza kundi la watu kuwapinga. Mwanamme wa tatu aliyeitwa Kora aliorodheshwa kama uzao wa Yuda.

Koreshi

Ufafanuzi

Koreshi alikuwa mfalme wa Uajemi aliyetengeneza himaya ya Uajemi katika mwaka wa 550 Kabla ya Kristo kwa njia ya kutawala Kijeshi. Katika historia alijulikana kama Koreshi mkuu.

- Mfalme Koreshi aliishinda Babeli na kusababisha kuachiwa kwa Waisraeli waliokuwa mateka huko.
- Koreshi alijulikana kwa tabia yake ya tabia yake ya uvumilivu kwa watu wa taifa alilolishinda. Ukarimu wake kwa Wayahudi ukapelekea kujengwa upya kwa hekalu ya Yerusalemu baada ya kipindi cha mateka.
- Koreshi alitawala katika kipindi cha Danieli, Ezra na Nehemia.

Korintho, Wakorintho

Ufafanuzi

Korintho ulikuwa mji katika nchi ya Ugiriki maili 50 mangharibi mwa Athene. Wakorintho walikuwa watu walioishi Korintho.

- Korintho ilikuwa moja kati ya sehemu ya makanisa ya kwanza.
- Vitabu vya agano jipya kitabu cha kwanza cha Wakorintho na kitabu cha pili cha Wakorintho ni barua zilizoandikwa na Paulo kwa wakristo walioishi Korintho.
- Paulo alikutana na waamini Akila na Prisila alipokuwa Korintho.
- Viongozi wengine wa mwanzo wa Korintho waliokuwa na mahusiano na Korintho ni Timotheo, Tito, Apolo na Sila.

Kornelio

Ufafanuzi

Kornerio alikuwa mtu wa Mataifa, asiye Myahudi afisa wa jeshi la Rumi.

- Aliomba mara kwa mara kwa Mungu na alikuwa akiwasaidia masikini.
- Kornelio na familia yake waliposikia kuwa mtume Petro anafafanua injili walikuja kuwa wanaomwamini Yesu.
- Watu wa nyumba ya Kornelio walikuwa watu wa kwanza wasio Wayahudi kumwamini Yesu.
- Hii iliwaonesha wafuasi wa Yesu kuwa alikuja kuwaokoa watu wote wakiwemo na wamataifa.

Krene

Ufafanuzi

Krene ulikuwa mji wa Kigiriki kaskazini mwa pwani ya Afrika kwa upande wa bahari ya Mediteraniani, moja kwa moja kusini mwa kisiwa cha Krene.

- Katika agano jipya Wayahudi na Wakristo waliishi Krene.
- Krene yaweza kuwa maarudu sana kwenye Biblia kama mji wa mtu aliyeitwa Simoni aliyebeba msalaba wa Yesu.

Krete, Mkrete

Ufafanuzi

Krete ni kisiwa kilichokuwepo kusini mwa fukwe ya Ugiriki. Mkrene ni mtu aliyeishi katika kisiwa hicho.

- Mtume Paulo alisafiri katika kisiwa cha Krene akiwa katika safari zake za Kimishenari.
- Paulo alimuacha mfanyakazi mwenzake Toto huko Krene ili kuwafundisha Wakristo na kuwasaidia kuchagua viongozi huko.

Kushi

Ufafanuzi

Kushi lilikuwa jina la mtoto mkubwa na Nuhu, Hamu. Pia alikuwa babu wa Nimrodi. Kaka zake wawili waliitwa Misri na Kanaani.

- Katika agano la kale Kushi lilikuwa jina la mkoa mkubwa katika nchi ya kusini kwa Israeli.
- Mkoa wa zamani wa Kushi ulikuwa ardhi ya nchi iliyokuwa na sehemu za nchi kama Sudani, Misri, Ethiopia na Saudi Arabia.
- Mtu mwingine aliyeitwa Kushi ametajwa katika Zaburi. Alikuwa Mbenyamini.

Labani

Ufafanuzi

Katika Agano la Kale, Labani alikuwa mjomba na baba mkwe wa Yakobo.

Yakobo aliishi na nyumba ya Labani Padan-aramu na kuchunga kondoo na mbuzi wake kama sharti la ndoa kwa binti wa Labani. Pendeleo la Yakobo kwa mabinti wa Labani lilikuwa Raheli kuwa mke wake. Labani alimdanganya Yakobo na kumfanya kumuoa binti yake mkubwa Lea kabla ya kumpa Raheli kama mke wa pili.

Lameki

Ufafanuzi

Lameki lilikuwa jina la wanaume wawili waliotajwa katika kitabu cha Mwanzo.

Lameki wa kwanza aliyetajwa alikuwa uzao wa Kaini. Alijivunia kwa wake zake wawili kuwa alimuua mtu kwa kumuumiza. Lameki wa pili alikuwa uzao wa Sethi. Alikuwa pia baba wa Nuhu.

Lazaro

Ufafanuzi

Lazaro na dada zake, Mariamu na Martha, walikuwa marafika wa karibu wa Yesu. Mara nyingi alikaa nao katika nyumba yao Bethania.

Lazaro anajulikana zaidi kwa kufufuliwa na Yesu kutoka wafu baada ya kuzikwa kaburini kwa siku kadhaa. Viongozi wa Kiyahudi walikasirika na kuwa na wivu kuwa Yesu alifanya muijiza huu na wakatafuta njia ya kumua Yesu na Lazaro. Yesu pia alitoa fumbo kuhusu maskini ombaomba na mtu tajiri ambapo ombaomba aliitwa "Lazaro."

Lea

Ufafanuzi

Lea alikuwa mmoja wa wake wa Yakobo. Alikuwa mama wa wana kumi wa Yakobo ambao uzao wao ni miongoni wa makabila kumi na mbili ya Israeli.

Baba wa Lea alikuwa Labani, aliyekuwa kaka wa mama yake Yakobo, Rebeka. Yakobo hakumpenda Lea kama alivyompenda mke wake mwingine Raheli, lakini Mungu alimbariki kwa wingi Lea kwa kumpa watoto wengi. Mmoja wa wana wa Lea, Yuda, alikuwa babu wa mfalme Daudi na Yesu.

Lebanoni

Ufafanuzi

Labanoni ni sehemu nzuri yenye milima iliyopo mwambao wa Bahari Kuu, kaskazini mwa Israeli. Katika nyakati za Biblia, eneo hili lilikuwa limejaa misonobari, kama seda na mvinje.

Mfalme Sulemani alituma wafanyakazi Lebanoni kuvuna miti ya seda kwa ajili ya kujengea hekalu la Mungu. Lebanoni ya zamani waliishi watu wa Fonikia ambao walikuwa wajenzi wenye ujuzi wa meli zilizotumika kwa viwanda vya biashara vizuri. Miji ya Tiro na Sidoni ilikuwa Lebanoni. Ilikuwa katika miji hii ambamo rangi ya zambarau ilitumika kwanza.

Lewiathani

Ufafanuzi

Neno "Lewiathani" linamaanisha mnyama mkubwa sana aliyekuwepo zamani katika maandishi ya kwanza ya Agano la Kale, katika vitabu vya Ayubu, Zaburi na Isaya.

Lewiathani anaelezwa kuwa kama joka, mwenye nguvu na mkali na mwenye uwezo wa kufanya maji yaliyomzunguka "kuchemka." Maelezo yake yanakaribiana na yale ya wanyama wakubwa sana waliokuwepo zamani. Nabii Isaya anaelezea Lewiathani kama "joka wa kutereza". Ayubu anaandika kama mtu mwenye ujuzi mzuri wa Lewiathani, kwa hiyo inawezekana kuwa huyu mnyama alikuwepo wakati wa uhai wake.

Listra

Ufafanuzi

Listra ni jina mji katika Asia ndogo ambao Paulo alitembelea katika moja ya safari zake za kimisionari. Ilikuwa katika eneo la Likaonia ambapo sasa ni nchi ya Uturuki ya leo.

Paulo na wenzake walitoroka kwenda Derbe na Listra walipotishwa na Wayahudi Ikonio. Akiwa Listra, Paulo alikutana na Timotheo aliyekuwa mwinjilisti mwenzake na mpandaji wa makanisa. Baada ya Paulo kumponya kilema Listra, watu walijaribu kuwaabudu Paulo na Barnaba kama miungu, lakini mitume waliwakemea na kuwazuia kufanya hivyo.

Luka

Ufafanuzi

Luka alikuwa mwandishi wa vitabu viwili vya Agano Jipya: injili ya Luka na kitabu cha Matendo ya Mitume.

Katika barua yake kwa Wakolosai,Paulo alimtaja Luka kama daktari. Paulo anamtaja Luka kwenye barua zake mbili. Inadhaniwa kuwa Luka alikuwa Mgiriki na Myunani kabla hajamjua Kristo. Katika injili yake, Luka anajumuisha matukio yanayoonesha upendo wa Yesu kwa watu wote, Wayahudi na Wayunani. Luka alifuatana na Paulo katika safari mbili za kimisionari na kumsaidia na kazi zake, Katika maandiko kadhaa ya awali ya kanisa, inasemekana kuwa Luka alizaliwa katika mji wa Antiokia ndani ya Shamu.

Lutu

Ufafanuzi

Lutu lilikuwa jina la mpwa wa Abrahamu. Alikuwa mwana wa ndugu yake Abrahamu, Harani. Lutu alisafiri na Abrahamu kwenda nchi ya Kanaani na kuishi katika mji wa Sodoma Lutu alikuwa babu wa Wamoabi na Waamoni. Wafalme maadui walipovamia Sodoma na kumteka Lutu, Abrahamu alikuja na mamia kadha ya wanaume kumuokoa Lutu na kurudisha mali zake. Watu walioishi katika mji wa Sodoma walikuwa watu waovu sana kwa hiyo Mungu aliuangamiza mji huo. Lakini kwanza alimwambia Lutu na familia ya kuuondoka mji ili watoroke.

Maaka

Ufafanuzi

Maaka alikuwa mmoja wa wana wa kaka yake Ibrahimu Nahori. Watu wengine katika Agano la kale walikuwa na jina hili.

- Mji wa Maaka au Bethi Maaka ulikuwa upande wa mbali wa kaskazini mwa Israeli, eneo lililo tawaliwa na kabila la Naftali.
- Ulikuwa mji muhimu na ulishambuliwa na maadui mara kadhaa.
- Maaka lilikuwa jina la baadhi ya wanawake, akiwepo mama yake na mwana wa Daudi Absalomu.
- Mfalme Asa alimuondoa bibi yake Maaka kutoka kuwa malikia kwasababu alipenda kuabudu Ashera.

Makedonia

Ufafanuzi

Katika Agano jipya, eneo lililo upande wa kaskazini wa Ugiriki.

- Miji Muhimu ilikuwa Berea, Filipi, na Thesalonika.
- Katika maono, Mungu alimwambia Paulo kuhubiri injili kwa watu wa Makedonia.
- Paulo na wafanya kazi wake walienda Makedonia na kuwa fundisha watu kuhusu Yesu na kuwasaidia kukua kiimani.
- Katika Biblia kuna barua ambazo Paulo aliandika kwa waaminin wa Makedonia katika miji ya Filipi na Thesalonike.

Malaki

Ufafanuzi

Malaki alikuwa mmoja wa manabii wa Mungu kwa ufalme wa Yuda. Aliishi katika ya miaka 500 kabla Kristo kuwa ulimwenguni.

- Malaki alitabiri kipindi ambacho hekalu la Israeli lilikuwa likijengwa baada ya kurudi kutoka matekani ya Babiloni.
- Ezra na Nehemia waliishi kipindi kimoja na Malaki.
- Kitabu cha Malaki ni kitabu cha mwisho cha Agano la Kale.
- Kama manabii wa Agano la Kale, Malaki alisisitiza watu kutubu dhambi zao na kumrudia kumuabudu Yahweh.

Manase

Ufafanuzi

Hawa walikuw wanaume watano kwa jina Manase katika Agano la Kale:

- Manase lilikuwa jina la mzaliwa wa kwanza wa Yusufu.
- Manase na mdogo wake Efraimu walichukuliwa na baba Yusufu, Yakobo walipe nafasi ya kuwa miongoni mwa makabila kumi na mbili ya Israeli.
- Uzao wa Manase uliunda kabila moja la Israeli.
- Kabila la Manase lilikuwa mara nyingi la itwa "kabila nusu la Manase" kwasababu nusu tu ya kabila ili ishi Kanani, kwa upande wa magharibi wa Mto Yordani. Sehemu nyingine ili ishi upande wa mashariki wa Yordani.
- Mmoja wa wafalme wa Yuda aliitwa pia Manase.
- Mfalme Manase alikuwa muovu aliye toa dhabihu za watoto wake kama sadaka za kuteketeza kwa miungu ya uongo.
- Mungu alimuadhibu Mfalme Manase kwa kuruhusu akamatwe na jeshi la adui. Manase alimgeukia Mungu na kuharibu madhabahu sanamu zilipo kuwa zikiabudiwa.
- Wanaume wawili waliyo itwa Manase waliishi kipindi cha Ezra. Hawa wanaume walitakiwa kuwapa talaka wake zao wa kipagani, waliyo washawishi kuabudu miungu ya uongo.
- Manase mwingine alikuwa babu wa Wadani waliyo kuwa makuhani wa miungu ya uongo.

Mariamu (dada wa Martha)

Ufafanuzi

Mariamu alikuwa mwanamke kutoka Bethania aliye mfuata Yesu.

- Mariamu alikuwa na dada jina la Martha na kaka jina Lazaro aliye mfuata Yesu.
- Siku moja Yesu alisema kwamba Mariamu alichagua kilicho bora alipo chagua kumsikiliza akifundisha kuliko kuwa na wasiwasi kuhusu kuandaa chakula kama Mariamu alivyo kuwa.
- Yesu alimleta kaka yake Lazaro na kumpa uzima.
- Baada ya hapo, Yesu alipo kuwa anakula nyumbani kwa mtu Bethania, Mariamu alimmiminia mafuta ya gharama miguuni ili kumuabudu.
- Yesu alimsifu kwa kufanya hili na kusema anaanda mwili wake kwa kuzikwa.

Mariamu Magdalena

Ufafanuzi

Mariamu Magdalena alikuwa miongoni mwa wanawake waliyo muamini Yesu na kumfuata katika huduma yake. Alijulikana kama kama Yesu aliye mponya kutoka kwa mapepo saba waliyo mtawala.

- Mariamu Magdalena na wanawake wengine walimsaidia Yesu na mitume kwa kutoa kwa.
- Pia anatajwa kama mmoja wa wanawake waliyo muona Yesu alipoo fufuka.

Mariamu, mama yake Yesu

Ufafanuzi

Mariamu alikuwa mwanamke mdogo aliye ishi katika mji wa Nazarethi aliye poswa kuolewa na Yusufu. Mungu alimchagua Mariamu kuwa mama wa Yesu Mesia, Mwana wa Mungu.

- Roho Mtakatifu kimiujiza alisababisha Mariamu kuwa na mimba wakati akiwa bikra
- Malaika alimwambia Mariamu kuwa mtoto atakaye zaliwa ni Mwana wa Mungu na kuwa amwite Yesu.
- Mariamu alimpenda Mungu na akamsifu kwa kuwa na neema kwake.
- Yusufu alimuoa Mariamu , lakini alibaki bikra mpaka mtoto kuzaliwa.
- Mariamu alidhani kwa undani kuhusu vitu vya ajabu wachungaji na mamajusi alivyo visema kuhusu Yesu.
- Mariamu na Yusufu walimchukuwa mtoto Yesu kuwekwa wakfu hekaluni. Baadae wakamchukuwa Misri kutoroka njama ya Farao kuuwa watoto. Hatimae wakarudi Nazarethi.

Martha

Ufafanuzi

Martha alikuwa mwanamke kutoka Bethania alimfuta Yesu.

- Martha alikuwa na dada aliye itwa Mariamu na kaka jina la Lazaro, aliye mfuata Yesu.
- Wakati mmoja Yesu alikwenda watembelea nyumbani, Martha alisumbuliwa na maandalizi ya chakula wakati dada yake Mariamu kaketi na kumsikiliza Yesu akifundisha
- Lazaro alipo kufa, Martha alimwambia Yesu kuwa ana amini Yesu ni Kristo, mwana wa Mungu.

Mathayo, Lawi

Ufafanuzi

Mathayo alikuwa mmoja wa wanaume kumi na mbili Yesu aliyo wachagua kuwa mitume wake. Alijulikana kama pia kama Lawi, mwana wa Alfayo.

- Lawi (Mathayo) alikuwa mtoza ushuru kutoka Kapernaumu kabla kukutana na Yesu.
- Mathayo aliandika injili iliyo beba jina lake.
- Kuna wanaume wengine kadhaa waitwao Lawi kwenye Bibli.

Mede, Media

Ufafanuzi

Media ulikuwa mji wa zamani uliyo kuwa mashariki mwa Asiria na Babilonia, na kaskazini mwa Elamu na Persia. Watu waliyo ishi katika utawala wa Media walitwa "Wamede."

- Utawala wa Media ulikuwa maeneo yote ya Uturuki, Irani, Syria, Iraq na Afghanistani.
- Wamede walikuwa karibu na Waajemi na tawala hizi mbili ziliungana kuwashinda Wababilonia.
- Babilonia ilivamiwa na Darius Mmede kipindi cha nabii Danieli kuishi huko.

Melkizedeki

Ufafanuzi

Kipindi cha Abramu akiishi, Melkizedeki alikuwa mfalme wa mji wa Salemu (baadae, "Yerusalelmu")

- Jina la Melkizedeki lina maana ya, "mfalme wa haki" na cheo chake "mfalme wa Salemu" ina maana ya, "mfalme wa amani"
- Pia aliitwa "kuhani wa Mungu wa Juu Sana"
- Melkizedeki anatajwa katika Biblia alipo mtumikia Abramu kwa mkate na mvinyo baada ya Abramu kumuokoa binamu yake Lutu kutoka kwa wafalme wenye nguvu. Abramu alimpa Melkizedeki moja ya kumi ya mali alizo chukuwa kwenye pambano.
- Katika Agano la Kale, Melkizedeki anaelezwa kama mtu asiye na baba na mama. Aliitwa kuhani na mfalme atakaye tawala milele.

Memfisi

Ufafanuzi

Memfisi ilikuwa mji mkuu wa Misri wa zamani, pembeni mwa Mto Nile.

- Memfisi ili kuwa upande wa chini mwa Misri, kusini mwa Mto Nile, ambapo udogo ulikuwa wenye rotuba na mazao mengi.
- Ardhi yake ya rotuba na eneo lake muhimu katika ya Misri ya Juu na ya Chini ili sababisha Memfisi kuwa mji mkuu wa biashara.

Mesheki

Ufafanuzi

Mesheki ni jina la wanaume wawili katika Agano la Kale.

- Mesheki mmoja alikuwa mwana wa Yafeti.
- Mwingine alikuwa mjukuu wa Shemu.
- Mesheki pia lilikuwa jina la eneo la nchi, ambalo labda lilipewa jina baada ya hawa wanaume.
- Eneo la Mesheki liliweza kuwa upande wa kule ambapo sasa ni nchi ya Uturuki.

Mesopotamia, Aramu Naharaimu

Ufafanuzi

Mesopotamia ni sehemu ya nchi katika ya Tigrisi na Mto Frati. Sasa ipo katika nchi inayo julikana kama Iraqi.

- Katika Agano la Kale, hili eneo liliitwa "Aramu Naharaimu."
- Neno "Mesopotamia" lina maana "katika ya mito." Maneno "Aramu Naharaimu" yana maana "Aramu ya mito miwili"
- Ibrahimu aliishi katika miji ya Mesopotamia Uri na Harani kabla ya kuamia nchi ya Kanani.
- Babiloni ilikuwa mji mwingine muhimu katika Mesopotamia.
- Eneo linalo itwa "Kaldea" ili kuwa sehemu ya Mesopotamia.

Mgirgashi

Ufafanuzi

Wagirgashi walikuwa kundi la watu wanaoishi karibu na Bahari ya Galilaya katika nchi ya Kaanani.

Walikuwa uzao wa mwana wa Hamu Kaanani na kwa hiyo walikuwa moja wa kundi la watu wengi ambao pia walijulikana kama "Wakaanani".

Mungu aliahidi Waisraeli ya kwamba angewasaidia kuwashinda Wagirgashi na makundi mengine ya Wakaanani.

Kama watu wote wa Kaanani, Wagirgashi waliabudu miungu ya uongo na kufanya mambo maouvu kama sehemu ya ibaaa hiyo.

Mgiriki, Kigiriki

Ufafanuzi

Msemo "Mgiriki" una maana ya lugha inayozungumzwa katika nchi ya Giriki. Giriki pia ilizungumziwa kote katika Ufalme wa Kirumi. Msemo "Kigiriki" una maana ya "kuzungumza Kigiriki".

Kwa kuwa watu wasiokuwa Wayahudi katika Ufalme wa Kirumi walizungumza Kigiriki, Watu wa mataifa mara kwa mara humaanisha "Wagiriki" katika Agano Jipya, haswa inapolinganishwa na Wayahudi.

Msemo "Wayahudi wa Kigiriki" walikuwa wakimaanisha Wayahudi ambao walizungumza Kigiriki kulinganisha na "Wayahudi wa Kiebrania" ambao walizungumza Kiebrania pekee, au labda Kiaramea.

Njia zingine za kutafsiri "Kigiriki" zinaweza kujumuisha "kuzungumza Kigiriki" au "Kigiriki cha kitamaduni" au "Kigiriki".

Pale inapomaanisha wasio Wayahudi, "Giriki" inaweza kutafsiriwa kama "watu wa mataifa"

Mhiti

Ufafanuzi

Wahiti walikuwa ni uzao wa Hamu kupitia kwa mtoto wake Kanaani. Walifanyika kuwa dola kubwa katika eneo ambalo kwa sasa linaitwa Uturuki na Kaskazini mwa Palestina. Ibrahimu alinunua sehemu ya ardhi kutoka kwa Efroni, Mhiti ili aweze kumzika Sara katika pango huko. Hatimaye, Ibrahimu na wazao wake kadhaa walizikwa katika pango hilo pia. Wazazi wa Esau walihuzunika sana baada ya Esau kuoa wanawake Wahiti. Mmoja kati ya watu wa Daudi aliyekuwa na nguvu aliitwa Uria Mhiti. Miongoni mwa wanawake aliowaoa Sulemani walikuwa ni Wahiti. Wanawake hawa wa kigeni waliugeuza moyo wa Sulemani kutoka kwa Mungu kwasababu ya miungu waliyoiabudu. Wahiti walikuwa mara zote ni hofu kwa waisraeli, kimwili na kiroho pia.

Mhivi

Ufafanuzi

Wahivi walikuwa ni moja kati ya makundi saba ya watu walioishi katika nchi ya Kanaani. Kama ilivyokuwa kwa makundi yote, Wahivi walikuwa ni uzao wa Kanaani, aliyekuwa ni mjukuu wa Nuhu. Shekemu mhivi alimbaka Dina, binti wa Yakobo na kaka zake na Dina walilipiza kisasi kwa kuwauwa Wahivi wengi. Katika kipindi ambacho Yoshua aliwaongoza waisraeli kuiteka nchi ya Kanaani, Waisraeli walidanganywa na kufunga mkataba na Wahivi badala ya kuwaangamiza.

Midiani, Wamidiani

Ufafanuzi

Midiani alikuwa mwana wa Ibrahimu na mkewe Ketura. Pia ni jina la kundi la watu na eneo upande wa kaskazini mwa Jangwa la Kiarabu sehemu ya kusini mwa nchi ya Kanani. Kundi la watu liliitwa "Wamidiani."

- Musa alipo ondoka Misri, alienda eneo la Midiani alipo kutana na binti wa Yethro na kuwasaidia kunyeshwa maji mifugo yao. Baadae Musa alimuoa mmoja wa binti wa Yethro.
- Yusufu alichukuliwa Misri na kundi la wanfanya biashara ya watumwa Wamidiani.
- Miaka mingi baadae Wamidiani alishambulia na kuvamia Waisraeli katika nchi ya Kanani. Gidioni aliongoza Waisraeli katika ushindi wao.
- Waarabu wengi wa leo ni wa kabila la uzao wa hili kundi.

Mika

Ufafanuzi

Mika alikuwa nabii wa Yuda katika ya miaka 700 kabla ya Yesu, wakati nabii Isaya alipo kuwa ana hudumu Yuda. Mwanaume mwingine aliye itwa Mika aliishi kipindi cha waamuzi.

- Kitabu cha Mika ni karibu na mwisho wa Agano la Kale.
- Mika alitabiri uharibifu wa Samaria kwa Waasiria.
- Mika aliwakemea watu wa Yuda kwa kuto mtii Mungu na kuwaonya kuwa maadui wao watawashambulia.
- Unabii unaisha na ujumbe wa matumaini kwa Mungu, aliye mwaminifu na kuokoa watu wake.
- Katika kitabu cha waamuzi, adithi ya mtu aitwaye Mika anaye ishi Efraimu aliye tengeneza sanamu kwa fedha ya simuliwa. Kijana wa kikuhani aliye kuja kuishi naye akiiba sanamu huyo na vitu vingine, na kuondoka na kundi la Wadani. Hatimaye Wadani na kuhani huyo wakaishi mji wa Laishi na wakaweka sanamu huyo huyo wa kumuabudu.

Mikaeli

Ufafanuzi

Mikaeli ni mkuu wa malaika wa tiiifu na watakatifu. Yeye ni malaika pekee anaye tajwa kama "malaika mkuu" wa Mungu.

- Neno "malaika mkuu" lina maana "malaika kiongozi."
- Mikaeli ni shujaa anaye pigana dhidi maadui wa Mungu na kulinda watu wa Mungu.
- Aliongoza Waisraeli kupigana dhidi ya jeshi la Wajemii. Katika siku za mwisho ataongoza jeshi la Israeli katika pambano la mwisho dhidi ya majeshi maovu, kama alivyo tabiri Danieli.
- Pia kuna baadhi ya wanaume katika Biblia wenye jina Mikaeli. Baadhi ya wanaume wana tajwa kama "wana wa Mikaeli"

Miriamu

Ufafanuzi

Alipo kuwa mdogo, Miriamu aliongozwa na mama yake kumlinda mdogo wake Musa aliye kuwa katika kikapu miongoni mwa Mto Nile.

- Miriamu aliwaongoza Waisraeli katika kucheza kwa furaha na shukurani baada ya kutoroka kwa Wamisri kwa kuvuka Bahari ya Shamu.
- Miaka mingi baadae Waisraeli walipo kuwa wana tanga jangwani, Miriamu na Aruni walianza kunena vibaya kuhusu Musa kwasababu alimuoa mwanamke wa Kikushi.
- Kwasababu ya uasi wake wakuongea viabya dhidi ya Musa, Mungu alimsababishi ukoma. Lakini baadae Mungu alimponya Musa alipo muombea.

Misri, Mmisri

Ufafanuzi

Misri ni nchi katika sehemu ya kaskazini ya Afrika, kusini mashariki mwa nchi ya Kaanani. Mmisri ni mtu ambaye anatoka katika nchi ya Misri.

Katika miaka ya zamani, Misri ilikuwa nchi yenye nguvu na utajiri.

Misri ya zamani iligawanyika katika sehemu mbili, Misri ya Chini (sehemu ya kaskazini ambapo mto hutiririka chini kuelekea baharini) na Misri ya Juu (sehemu ya kusini). Katika Agano la Kale, sehemu hizi zinajulikana kama "Misri" na "Pathrosi" katika lugha ya maandishi asili.

Wakati mwingine ambapo kuna chakula kichache Kaanani, wakuu wa koo walisafiri kwenda Misri kununua chakula kwa ajili ya familia zao.

Kwa miaka mia moja hivi, Waisraeli walikuwa watumwa Misri.

Yusufu na Mariamu walishuka chini Misri na mtoto mdogo Yesu kutoroka kwa Herode Mkuu.

Mizpa

Ufafanuzi

Mizpa ni jina la baadhi ya miji inayo tajwa katika Agano la Kale. Ina maana, "mnara wa doria"

- Daudi alipo kuwa anakimbizwa na Sauli, aliwaacha wazazi wake Mizpa, chini ya ulinzi wa mfalme Moabu.
- Mji moja unaoitwa Mizpa ulikuwa mpakani katika ya falme za Yuda na Israeli. Ilikuwa sehemu kubwa ya kijeshi.

Mji wa Babeli

Ufafanuzi

Mji wa Babeli ulikuwa makao makuu wa jimbo la Babeli ya kale, ambao pia ulikuwa sehemu ya Himaya ya Babeli.

- Babeli ulikuwa kandokando ya Mto Frati, katika eneo ambalo mnara wa Bebeli ulikuwa umejengwa mamia ya miaka iliyokuwa imepeita.
- Wakati mwingine jina "Babeli" linarejerea Himaya yote ya Babeli. Kwa mfano, "mfalme wa Babeli alitawala himaya yote ya Babeli, siyo mji tu.
- Watu wa Babeli walikuwa wenye nguvu walioishambuli Yuda na kuwapeleka watu katika uhamisho huko Babeli kwa miaka 70.
- Sehemu yake iliitwa "Ukalidayo" na watu walioishi pale waliitwa "Wakalidayo." Matokeo yake neno "Ukalidayo mara kwa mara lilitumika kurejerea Babeli.
- Katika Agano Jipya, neno "Babeli" wakati mwingine linatumika kama sitiari kurejerea maeneo, watu, na vitu vya kufikirika viusianishwavyo na ibada ya sanamu na tabia nyingine za dhambi.
- Kirai "Babeli Mkuu" au "Babeli mji mkuu" kisitiari inarejerea kwa mji au taifa kubwa, tajiri, na lenye dhambi, kama ulivyokuwa mji wa kale wa Babeli.

Mji wa Bethani

Ufafanuzi

Mji wa Bethani ulikuwa katika bonde la mteremko wa Mlima wa Mizeituni, kama maili mbili mashariki ya Yerusalemu,

- Bethani ulikuwa karibu na njia iliyokwenda kati ya Yerusalemu na Yeriko.
- Yesu alitembelea Bethani mara kwa mara walipokuwa wakiishi Lazaro, Matha na Mariamu, rafiki zake wa karibu.
- Bethani unajulikana maalumu kama sehemu Yesu alipomfufua Lazaro kutoka kwa wafu.

Mji wa Daudi

Ufafanuzi

Mji wa Daudi ni jina la Yerusalemu na Bethlehemu.

- Yerusalemu ni mahali ambapo Daudi aliishi alipotawala Israeli.
- Bethlehemu ni mahali ambapo Daudi alizaliwa.

Mlawi, Lawi

Ufafanuzi

Lawi alikuwa mmoja wa wana kumi na mbili wa Yakobo, au Israeli. Neno "Mlawi" inamaanisha mtu aliyemmoja wa kabila la Israeli ambalo babu yao alikuwa Lawi.

Walawi walihusika na kulitunza hekalu na kuendesha taratibu za kidini, zikiwemo kutoa sadaka na maombi. Makuhani wote wa Kiyahudi walikuwa Walawi, wazawa wa Lawi na sehemu ya kabila la Lawi. (Ingawa Walawi wote hakuwa makuhani.) Makuhani wa Kilawi walitengwa na kuwekwa wakfu kwa kazi maalum ya kumtumikia Mungu hekaluni. Wanaume wengine wawili wenye jina "Lawi" walikuwa mababu wa Yesu na majina yao yako kwenye ukoo katika injili ya Luka. Mwanafuzi wa Yesu, Mathayo, pia aliitwa Lawi.

Mlima Hermoni

Ufafanuzi

Mlima Hermoni ni jina la mlima mrefu wa Israeli chini ya Lebanoni.

- Upo kaskazini mwa Bahari ya Galilaya, kaskazini mwa mpaka wa Israeli na Syria.
- Majina mengine yaliyo pewa Mlima Hermoni na watu wengine ni "Mlima Sirioni"
- Mlima Hermoni una vilele vitatu. Kikubwa ni karibu mita 2,800 kwenda juu.

Mlima wa Mizeituni

Ufafanuzi

Mlima wa Mizeituni ni mlima au kilima kikubwa karibu na mashariki mwa mji wa Yerusalemu. Una mita787 kwenda juu.

- Katika Agano la Kale, huu mlima unatajwa kama "mlima mashariki mwa Yerusalemu."
- Nakala za Agano Jipya zataja maeneo ambayo Yesu na wanafunzi wake walienda Mlima wa Mizeituni kuomba na kupumzika.
- Yesu alikamatwa Bustani ya Gethsemane, uliyo upande wa Mlima wa Mizeituni.

Moabu, Mmoabu

Ufafanuzi

Moabu alikuwa mwana wa kwanza wa binti wa Lutu. Pia likawa jina la nchi ambapo yeye na familia yake waliishi. Neno "Moabu" la husu mtu wa uzao wa Moabu au anaishi katika nchi ya Moabu.

- Nchi ya Moabu ilikuwa mashariki mwa Bahari ya chumvi.
- Moabu ilikuwa kusini mashariki kutoka mji wa Bethelehemu ambapo Naomi na familia yake waliishi.
- Watu wa Bethelehemu wallimuita Ruthi "Mwanamke Mmoabu" kwasababu alikuwa mwanamke wa nchi ya Moabu.

Modekai

Ufafanuzi

Modekai alikuwa mwanaume wa Kiyahudi katika nchi ya Jemi. Alikuwa mlinzi wa binamu wake Esta, ambaye baadae alikuwa mke wa mfalme wa Kijemi, Ahasuerusi

- Wakati akifanya kazi hikulu, Modekai alisikia watu wakipanga njama kumuua mfalme Ahasuerusi. Alitoa taarifa na maisha ya mfalme yakapona.
- Wakati mwengine, Modekai aligundua mbinu ya kuua Wayahudi wote katika ufalme wa Kijemi. Alimshauri Esta kumuomba mfalme kuokoa watu wake.

Moleki, Moloki

Ufafanuzi

Moleki lilkuwa jina la miungu wa uongo ambao Wakanani waliabudu.

- Watu waliyo abudu Moleki alitoa dhabihu watoto wao kwake kwa moto.
- Waisraeli wengine pia waliabudu Moleki badala ya Mungu wa kweli, Yahweh. Walifuata matendo maovu ya waabudu Moleki, pamoja na kutoa dhabihu watoto wao

Mperizi

Ufafanuzi

Waperizi walikuwa watu wa kundi fulani katika nchi ya Kanaani. Ni machache yamezungumzwa juu ya kundi hili.

- Waperizi wanatajwa sana katika agano la kale kitabu cha Waamuzi ambapo ilirekodiwa kuwa Waperizi walioana na Wisraeli na kuwashawishi kuabudu miungu ya uongo.
- Ukoo wa Perezi ulioitwa "waperezi" lilikuwa kundi tofauti na Waperizi.

Mshaeli

Ufafanuzi

Mishaeli ni jina la wanaume wa tatu katika Agano la Kale.

- Mwanaume mmoja anaye itwa Mishaeli alikuwa binamu wa Aruni. Wana wawili wa Aruni walipo uliwa na Mungu baada ya kufukiza uvumba kwa namna ambayo haikumpendeza Mungu, Mishaeli na kaka yake walipewa jukumu la kubeba maiti nje ya kambi ya Waisraeli.
- Mwanaume mwingne aitwaye Mishaeli alisimama kando ya Ezra alipo soma hadharani sheria aliyo ikuta.

Mto Frati

Ufafanuzi

Frati ni jina la moja ya mito minne ambayo ilitiririka katika bustani ya Edeni. Ni mto ambao umetajwa sana katika Biblia.

Mto wa sasa unaitwa Frati na upo eneo la Mashariki ya Kati na ni mrefu zaidi na mto muhimu zaidi Asia.

Pamoja na Mto Hidekeli, Frati inapakana na eneo la nchi inayojulikana kama Mesopotamia.

Mji wa zamani wa Uri ambapo Abrahamu alitoka ulikuwa mdomo wa Mto Frati.

Mto huu ulikuwa moja ya mipaka ya nchi ambayo Mungu aliahidi kumpa Abrahamu (Mwanzo 15:18).

Wakati mwingine Mto Frati hujulikana kama "ule Mto"

Mto Nili, Mto wa Misri

Ufafanuzi

Nili ni mto mrefu na mpana katika kaskazini mashariki mwa Africa. Unajulikana kama mto rasmi wa Misri.

- Mto Nili unapita kaskazini kupita Misri na kwenda Bahari ya Medetarenia.
- Mimea ina kua kwenye nchi ya rotuba pande zote mbili za Mto Nili.
- Wamisri wengi wanaishi karibu na Mto Nili maan ni muhimu kwa maji na mazao ya chakula.
- Waisraeli waliishi nchi ya Gosheni iliyo kuwa na rotuba kwababu ilikuwa upande wa Mto Nile

Mto Yordani, Yordani

Ufafanuzi

Mto Yordani ni mto unaotiririka toka kaskazini hadi kusini, na inaunda mpaka wa mashariki wa nchi iliyokuwa inaitwa Kanaani.

Leo, mto Yordani unatenganisha Israeli magharibi kutoka Yordani mashariki. Mto Yordani unatiririka katikati ya Bahari ya Galilaya na kuishia katika Bahari iliyo Kufa. Wakati Yoshua anawaongoza Waisraeli kuelekea Kanaani, ilibidi wavuke mto Yordani. Kwa sababu palikuwa parefu sana, Mungu alisimamisha maji kutembea kwa miujiza ili watu wavuke. Mara nyingi Biblia katika Biblia Mto Yordani unajulikana ka "Yordani."

mtu wa Mungu

Ufafanuzi

Msemo "mtu wa Mungu" ni heshima ya kutaja nabii wa Yahweh. Pia utumika kuhusu malaika wa Yahweh.

- Unapo taja nabii, hii yaweza pia tafsiriwa kama " mtu aliye wa Mungu" au "mwanaume Mungu aliye mchagua" au "mwanaume anaye mtumikia Mungu"

Musa

Ufafanuzi

Musa alikuwa nabii na kiongozi wa watu wa Israeli kwa miaka 40.

- Musa alipo kuwa mtoto, wazazi wa Musa walimueka kwenye kikapu Mto Nile kumficha na Farao wa Misri. Dada wa Miriamu alimwangalia hapo. Maisha ya Musa yalinusurika binti wa Farao alipo mkuta na kumchukuwa kama mwanae.
- Mungu alimchagau Musa kuwa toa Waisraeli utumwani Misri na kuwaongoza Nchi ya Ahadi.
- Baada ya Waisraeli kutoka Misri na walipo kuwa jangwani wakitanga, Mungu alipa Musa mawe mawili ya mbao yenye Amri Kumi.
- Mwisho wa maisha yake, Musa aliona Nchi ya Ahadi, lakini hakuishi sababu hakumtii Mungu.

Muumbaji

Ufafanuzi

Kwa ujmla, "muumbaji" ni mtu anaye tengeneza au kufanya vitu.

- Katika Biblia, neno "Muumbaji" mara nyingine linatumika kama jina au cheo cha Yahweh, kwasababu ameumba kila kitu.
- Mara kwa mara hili neno lina ambatana na "wake" au "wangu" au "wako"

Mwamori

Ufafanuzi

Waamori walikuwa watu wenye nguvu sana ambao ni uzao wa mjukuu wa Nuhu Kanani.

- Jina lao lilikuwa na maana ya "aliye juu" ambalo lilimaanisha miji ya milima ambapo walikuwa wakiishi au kwa sababu walijulikana kuwa ni watu warefu kwa kimo.
- Waamori waliishi katika majimbo yote yaliyokuwa kandokando ya mto Yordani. Mji wa Ai ulikaliwa na Waamori.
- Mungu alisema "dhambi za waamori" akiwa anajumuisha waliabudu miungu ya uongo na walitenda dhambi.
- Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuwaangamiza Waamori kama ambavyo Mungu alimuamuru afanye.

Myebusi, Yebusi

Ufafanuzi

Wayebusi walikuwa kundi la watu walioishi nchi ya Kanaani. Walikuwa uzao wa mwana wa Hamu, Kanaani.

Wayebusi waliishi katika mji wa Yebusi, ambalo jina lake lilibadilishwa baadaye kuwa Yerusalemu mfalme Daudi alipoutawala. Melkizedeki, mfalme wa Salemu, inawezekana alikuwa Myebusi kwa asili.

Naamani

Ufafanuzi

Katika Agano la Kale, Naamani alikuwa mkuu wa jeshi wa mfalme Aramu.

- Naamani alikuwa na ungonjwa mbaya wa ngozi uitwao ukoma usiyo tibika.
- Myahudi mtumwa katika nyumba ya Naamani alimwambia aende kwa nabii Elisha apone.
- Elisha alimwambia Naamani ajisafishe mara saba katika Mto Yordani. Naamani alipo tii, Mungu akamponya ugonjwa wake.
- Baada ya matokeo, Naamani alikuja kuamini kuwa Mungu ndiye wa kweli, Yahweh.
- Wanaume wengine wawili waliitwa Naamani walikuwa uzao wa mjukuu wa Yakobo Benjamini.

Naftali

Ufafanuzi

Naftali alikuwa mwana wa sita wa Yakobo. Uzao wake uliunda kabila la Naftali, ambalo lilikuwa moja ya kabila la Israeli.

- Wakati mwingine jina Nafatali linatumika kueleza nchi kabila lipo ishi.
- Nchi ya Naftali ilikuwa upande wa kaskazini mwa Israeli, karibu na kabila la Dani na Asheri. Pia lilikuwa mpaka wa magharibi wa Bahari ya Chinerethi.
- Hili ni kabila lilotajwa katika Agano la Kale na Jipya katika Biblia.

Nahori

Ufafanuzi

Nahori lilikuwa jina la ndugu wawili wa Ibrahimu: babu yake na kaka.

- Kaka yake Ibrahimu Nahori alikuwa babu wa mke wa Isaka Rebeka.
- Maneno "mji wa Nahori" ulimaanisha, "mji uliyo itwa Nahori" au "mji ambao Nahori aliishi" au " Mji wa Nahori"

Nahumu

Ufafanuzi

Nahumu alikuwa nabii aliye ubiri kipindi ambacho mfalme mouvu Manase alitawala Yuda.

- Nahumu alitoka mji wa Elkoshi, maili 20 kutoka Yerusalemu.
- Agano la Kale kitabu cha Nahumu kimeandika unabii wake kuhusu uharibifu wa mji wa Ninewi.

Nathani

Ufafanuzi

Nathani alikuwa nabii mwaminifu wa Mungu aliye ishi kipindi cha Daudi akiwa mfalme wa Israeli.

- Mungu alimtuma Nathani kumuona Daudi alipo tenda dhambi dhidi ya Uria.
- Nathani alimkemea Daudi, japo kuwa Daudi alikuwa mfalme.
- Daudi alitubu dhambi yake baada ya Nathani kumfuata.

Nazarethi, Nazarini

Ufafanuzi

Nazarethi ni mji katika mji wa Galilaya kusini mwa Israeli. Ilikuwa kama kilomita 100 kaskazini mwa Yerusalemu, iliyo chukuwa kam siku tatu hadi tano kufika kwa miguu.

- Yusufu na Maria walitoka Nazarethi, na hapo ndipo walipo mlelea Yesu.
- Ndio maana Yesu alijulikana kama "Mnazarini"
- Wayahudi wengi wanao ishi Nazarethi hawaku muheshimu Yesu na mafundisho yake, kwasababu alikulia miongoni mwao na wakadhani alikuwa mtu tu wa kawaida.
- Wakati Yesu alipo kuwa anafundisha sinagogi la Nazarethi, Wayahudi walijaribu kumuua kwasababu alidai kuwa Mesia na akawakemea kwa kumkataa.

Nebukadneza

Ufafanuzi

Nebukadneza alikuwa mfalme wa Utawala wa Babiloni ambaye jeshi lake kuu liliwashinda makundi ya watu na mataifa.

- Chini ya uongozi wa Nebukadneza, jeshi la Wababiloni walishambulia na kuishinda Yuda, na kuchukuwa watu wa Yuda kwenda Babiloni. Hii ndio "Mateka ya Babiloni" kwa miaka 70.
- Mmoja wa mateka, Danieli, alitafsiri ndoto ambazo Nebukadneza alikuwa nazo.
- Waisraeli wengine wa tatu, Hanania, Meshaeli, na Azaria, walitupwa katika tanuru kali walipo kataa kuinama kwa sanamu kubwa Nebukadneza alilo tengeneza.
- Mfalme Nebukadneza alikuwa na kiburi na kuabudu miungu ya uongo. Alipo shinda Yuda, aliiba dhahabu nyingi na fedha kutoka hekaluni Yerusalemu.
- Kwasababu Nebukadneza alikuwa na kiburi na kukataa kugeuka pembeni asiabudu miungu ya uongo, Yahweh alimsababisha kuwa na uwitaji kwa miaka saba, akiishi kama mnyama. Baada ya miaka saba Mungu alimrejesha Nebukadneza alipo jinyenyekesha na kumuabudu Mungu wa kweli, Yahweh.

Negevi

Ufafanuzi

Negevi ni jangwa kusini mwa Israeli, kusini magharibi wa Bahari ya Chumvi.

- Neno halisi lina maana "Kusini."
- Ina wezekana kuwa hili eneo la kusini sio eneo la leo la Jangwa la Negevi.
- Ibrahimu alipo ishi nchi ya Kadeshi, alikuwa Negevi au kusini.
- Isaka alikuwa anaishi Negevi Rebeka alipo safiri kukutana naye na kuwa mke wake.
- Makabila ya Yuda na Simeoni yaliishi Kusini mwa eneo.

Nehemia

Ufafanuzi

Nehemia alikuwa Muisraeli aliye ishi Babiloni wakati watu wa Israeli na Yuda walip chukuliwa mateka na Wababiloni.

- Alipo kuwa mbeba kikombe wa mfalme wa Jemi, Artaxerxesi, Nehemia aliomba ruhusu kwa mfalme kurudi Yerusalemu.
- Nehemia waliwaongoza Waisraeli kujenga kuta za Yerusalemu iliyo haribiwa na Wababiloni.
- Kwa miaka kumi na mbili Nehemia alikuwa mkuu wa Yerusalemu kabla ya kurudi kwa nyumba ya mfalme.
- Kitabu cha Agano la Kale cha Nehemia kinaeleza habari ya Nehemian kazi yake kwa kujenga kuta na kuongoza watu wa Yerusalemu.

Ninawi, Mninwai

Ufafanuzi

Ninawi ilikuwa mji mkuu wa Asyria. Mninawi alikuwa mtu aliye ishi Ninawi.

- Mungu alimtuma nabii Yona kuwaonya Waninawi kugeuka kutoka njia zao mbaya. Watu walitubu na Mungu hakuwa haribu.
- Waasyria baadae waliacha kumtumikia Mungu. Walishinda ufalme wa Israeli na kubeba watu kwenda Ninawi.

Nuhu

Ufafanuzi

Nuhu alikuwa mwanaume aliye ishi miaka 4,000 iliyo pita, kipindi ambacho Mungu alipotuma garika duniani kuharibu watu waovu. Mungu alimwambia Nuhu ajenge meli kubwa ambayo yeye na familia yake waliweza kuishi wakati mafuriko yalipo funika dunia.

- Nuhu alikuwa mwenye haki aliye mtii Mungu kwa kila kitu.
- Wakati Mungu alipo mwambia Nuhu kujenga meli kubwa, Nuhu alijenga kama Mungu alivyo mweleza.
- Ndani ya hiyo meli, Nuhu na familia yake walihifadhiwa salama na baadae watoto wao na wajukuu wao walijaza dunia na watu tena.
- Kila mtu aliye zaliwa kipindi cha garika ni mzao wa Nuhu.

Nyumba ya Daudi.

Ufafanuzi

Maelezo 'nyumba ya Daudi' yanarejelea familia au uzao wa Mfalme Daudi. Neno 'nyumba ya Daudi' laweza kutafsiriwa kama '' uzao wa Daudi'' au ''familia ya Daudi." Yesu ni sehemu ya nyumba ya Daudi kwasababu alikuwa ni uzao wa Daudi. Wakati mwingine neno 'nyumba ya Daudi' hurejelea watu wa familia ya Daudi wale ambao wakali hai. Mara nyingine laweza kuwajumuisha wazao wa Daudi hata wale waliokwisha kufa.

Obadia

Ufafanuzi

Obadia alikuwa nabii wa Agano la Kale aliye tabiri dhidi ya watu wa Edomu, waliyo kuwa wazao wa Esau. Pia palikuwa na wanaume wengine waliyo itwa Obadia katika Agano la Kale.

- Kitabu cha Obadia ni kifupi katika Agano la Kale na kinaeleza unabii Obadia aliyo upokea kupitia maono kutoka kwa Mungu.
- Sio wazi sana lini Obadia aliishi na kutabiri. Inawezekana kipindi cha utawala wa Yehoramu, Ahazia, Yoashi, na Athalia, mfalme wa Yuda. Nabii Danieli, Ezekieli, na Yeremia walikuwa wakitabiri kipindi hichi.
- Obadia pia ina wezekana aliishi kipindi cha mwisho cha muda huu, wakati wa utawala wa Mfalme Zedekia na mateka ya Babiloni.
- Wanaume wengine wa wenye jina Obadia ni mzao wa Sauli, Mgadi aliye kuwa mmoja wa wanaume wa Daudi; mtumishi wa hikulu wa Mfalme Ahabu; afisa wa Mfalme Yehoshafati; Mlawi aliye kuwa mlinzi wa lango kipindi cha Nehemia.
- Ina weza kuwa mwandishi wa kitabu cha Obadia alikuwa mmoja wapo.

Omri

Ufafanuzi

Omri alikuwa mkuu wajeshi aliye kuwa mfalme wa sita wa Israeli.

- Mfalme Omri alitawala miaka 12 katika mji wa Tirza.
- Kama wafalme wote wa Israeli kabla yake, Omri alikuwa muovu aliye ongoza watu wa Israeli kuabudu sanamu.
- Omri pia alikuwa baba wa mfalme Ahabu.

Padan-aramu

Ufafanuzi

Padan-aramu lilikuwa jina la mji ambao familia ya Abrahamu waliishi kabla ya kuhamia kwenye nchi ya Kanaani. Inamaanisha "uwazi wa Aramu."

- Abrahamu alipoondoka Harani kule Padan-aramu akasafiri kwenda nchi ya Kanaani watu wengi wa familia yake walibaki Harani.
- Miaka mingi baadae mtumishi wa Abrahamu alikwenda Padan-aramu kutafuta mke kwa ajili ya Isaka miongoni mwa ndugu zake na akampata Rebeka, mjukuu wa Bethueli.
- Pia mtoto wa Isaka na Rebeka Yakobo alisafiri mpaka Padan-aramu na kuoa mabinti wawili wa kaka yake na Rebeka, Labani aliyekuwa akiishi Harani.

Aramu, Padan-aramu na Aramu-Nahariamu zilikuwa sehemu za mji mmoja ambao kwa sasa ni zipo katika nchi ya Syria.

Parani

Ufafanuzi

Parani ni jangwa lililopo mashariki mwa Misri na kusini mwa nchi ya Kanaani. Pia kulikuwa na mlima Parani ambalo yaweza kuwa jina lingine la mlima Sinai.

- Mtumwa Hagari na mtoto wake walikwenda kuishi katika jangwa la Parani baada ya Sara kumuamuru Abrahamu amfukuze.
- Musa alipowaongoza Waisraeli kutoka Misri walipitia jangwa la Parani.
- Ilikuwa toka Kadesh-barnea kupitia jangwa la Parani ambalo Musa aliwatuma wapelelezi kumi na mbili kupeleleza nchi ya Kanaani na kuleta ripoti.
- Jangwa la Sini lilikuwa kaskazini mwa Parani.

Paulo, Sauli

Ufafanuzi

Paulo alikuwa kiongozo wa kanisa la kwanza aliyetumwa na Mungu kupeleka habari njema kwa makundi mengi ya watu.

- Paulo alikuwa Myahudi aliyezaliwa Rumi kwenye mji wa Tarso hivyo alikuwa raia wa Rumi.
- Paulo kwa jina la Kiyahudi aliitwa Sauli.
- Sauli alikuwa kiongozi wa dini ya Kiyahudi na aliwafunga Wayahudi waliokuwa Wakristo kwa sababu alifikiri kuwa hawakumuheshimu Mungu kwa kumwamini Yesu.
- Yesu alijidhihirisha mwenyewe kwa Sauli kwa kutumia mwanga unaopofua na kumwambia aache kuwatesa Wakristo.
- Sauli alimwamini Yesu na akaanza kuwahubiria Wayahudi wenzake kuhusu Yesu.
- Baadaye Mungu akamtuma Sauli kwenda kuwahubiria wasio Wayahudi kuhusu Yesu na kuanzisha makanisa katika miji na vijiji mbalimbali. Wakati huu sasa akaanza kuitwa Paulo.
- Paulo pia aliandika barua ili kuwatia moyo Wakristo katika makanisa kwenye miji hiyo. Barua hizi zipo katika agano jipya.

Peori, Mlima Peori, Baali Peori

Ufafanuzi

Peori na Mlima Peori ni mlima uliokuwepo kaskazini mwa bahari ya chunvi katika mji wa Moabu.

- Beth Peori lilikuwa jina la mji uliokuwepo karibu na mlima ule. Hapa ni mahali ambapo Musa alikufa baada ya Mungu kumuonesha nchi ya ahadi.
- "Baali Peori" alikuwa mungu wa uongo wa Wamoabu walioabudiwa katika mlima Peori. Waisraeli pia walianda kuabudu sanamu hii na Mungu akawaadhibu kwa hili.

Petro, Simoni Petro, Kefa

Ufafanuzi

Petro alikuwa mmoja wa mitume wa Yesu. Alikuwa kiongozi wa muhimu katika kanisa la kwanza.

- Kabla Yesu hajamuita kuwa mwanafunzi wake aliitwa Simoni.
- Baadae Yesu akamuita Kefa yenye maana ya "jiwe" au "mwamba." Jina Petro pia linamaana ya "jiwe" au "mwamba" kwa lugha ya Kigiriki.
- Mungu alifanya kazi kupitia Petro kwa kuwaponya watu na kuhubiri habari njema kuhusu Yesu.
- Vitabu viwili vya agano jipya ni barua ambazo Petro aliandika kuwatia moyo na kuwafundisha waamini wenzake.

Pilato

Ufafanuzi

Pilato alikuwa kiongozi wa serikali ya Rumi katika Yudea aliyumuhukumu Yesu kifo.

- Kwa sababu Pilato alikuwa gavana alikuwa na mamlaka ya kuamua hukumu ya kifo kwa watu wenye hatia.
- Viongozi wa dini ya Kiyahudi walimtaka Pilato amsulubishe Yesu hivyo wakadanganya na kusema Yesu alikuwa mhalifu.
- Pilato aligundua kuwa Yesu hakuwa na makosa lakini aliwaogopa makutano na akataka kuwaridhisha hivyo akawaamuru askari wake wamsulubishe Yesu.

Ponto

Ufafanuzi

Ponto ulikuwa mkoa wa Rumi katika kipindi cha himaya ya Rumi na kanisa la kwanza. ilikuwa karibu na kusini mwa pwani ya Bahari nyeusi na kaskazini ambapo sasa ni nchi ya Uturuki.

- Kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Matendo ya mitume watu toka mkoa wa Ponto walikuwa Yerusalemu wakati ambao Roho mtakatifu alikuja kwa mitume siku ya Pentekoste.
- Akula aliyeamini alitokea Ponto.
- Wakati Petro anawaandikia Wakristo waliotawanyika katika miji mbali mbali Ponto ilikuwa mmoja wa miji iliyotajwa.

Potifa

Ufafanuzi

Potifa alikuwa kiongozi wamuhimu sana kwa Farao wa Misri katika kipindi ambacho Yusufu aliuzwa utumwani kwa Waishmaili.

- Potifa alimchukua Yusufu kwa Waishamaili na akamteua kuwa msimamizi wa nyumba yake.
- Yusufu aliposingiziwa kwa kutenda kosa Potifa alimuweka Yusufu gerezani.

Prisila

Ufafanuzi

Prisila na Akula mume wake walikuwa Wakristo wa Kiyahudi waliofanya kazi na mtume Paulo katika kazi yake ya kimishenari.

- Prisila na Akula waliondoka Rumi kwa sababu mtawala aliwalazimisha Wakristo kuondoka.
- Paulo alikutana na Akula na Prisila Korintho. Walikuwa watengeneza mahema na Paulo akaungana nao katika kazi hiyo.
- Pauli alipoondoka Korintho kwenda Syria Prisila na Akula walikwenda pamoja naye.
- Toka Syria watatu hao wakaenda Efeso. Paulo alipoondoka Efeso Prisila na Akula walibaki na kuendelea kuhubiri injili.

Rabai

Ufafanuzi

Rabai ulikuwa mji wa muhimu sana kwa watu wa Waamoni.

- Katika vita dhidi ya Waamoni Waisraeli walivamia Rabai.
- Mfalme Daudi wa Israeli aliiteka Rabai kama mateka yake ya mwisho.
- Katika nyakati za sasa mji wa Amman Yordani ni sehemu ambayo Rabai ilikuwepo.

Rahabu

Ufafanuzi

Rahabu alikuwa mwanamke aliyeishi Yeriko Waisraeli walipovamia mji. Alikuwa kahaba.

- Rahabu aliwaficha Waisraeli wawili waliokuja kupeleleza Yeriko kabla ya Waisraeli kuvamia. Aliwasaidia wapelelezi kurudi kwenye kambi ya Israeli.
- Rahabu akamwamini Bwana.
- Yeye na familia yake hawakudhuriwa Yeriko ilipoharibiwa na wakaenda kuishi Israeli.

Raheli

Ufafanuzi

Raheli alikuwa mmoja wa wake wa Yakobo. Yeye na dada yake Lea walikuwa watoto wa mjomba wake Yakobo.

- Raheli alikuwa mama yake na Yusufu na Benyamini ambao uzao wake ukaja kuwa moja ya kabila la Israeli.
- Kwa miaka mingi Raheli hakuweza kupata mtoto. Mungu alimuwezesha kumzaa Yusufu.
- Miaka mingine baadae alimzaa Benyamini, Raheli alikufa na Yakobo alimzika karibu na Bethelehemu.

Rama

Ufafanuzi

Rama ulikuwa mji wa zamani wa Israeli uliokuwa kilometa 8 toka Yerusalemu. Ulikuwa mji ambao Benyamini aliishi.

- Rama ni mahali ambapo Raheli alimzaa Benyamini.
- Waisraeli walipochukuliwa mateka Babeli Waliletwa kwanza Rama kabla ya kwenda Babeli.
- Rama ilikuwa nyumbani kwa mama na baba yake Samweli.

Ramothi

Ufafanuzi

Ramothi ulikuwa mji wa muhimu sana katika milima ya Gileadi karibu na mto Yordani. Pia iliitwa Romothi Gileadi.

- Ramothi ni milki ya Israeli kabila la Gadi na ulikuwa mji wa makimbilio.
- Mfalme Ahabu wa Israeli na mfalme Yohoshafati wa Yuda walipanga vita dhidi ya mfalme Aramu wa Ramothi. Ahabu aliuawa vitani.
- Baadae mfalme Ahazia na mfalme Yoramu walijaribu kuchukua mjiwa Ramothi toka kwa mfalme Aramu.
- Ramothi Gileadi ni mahali ambapo Yehu aliteuliwa kuwa mfalme juu ya Israeli.

Rebeka

Ufafanuzi

Rebeka alikuwa mjukuu wa kaka yake na Abrahamu yaani Nuhu.

- Mungu alimchagua Rebeka kuwa mke wa mtoto wa Abrahamu, Isaka.
- Rebeka alitoka mjia wa Aramu alipokuwa akiishi na kwenda na mtumishi wa Abrahamu katika mji wa Negevu ambapo Isaka aliishi.
- Kwa muda mrefu Rebeka hakuwa na mtoto lakini baadaye Mungu akambariki na mapacha Esau na Yakobo.

Rehoboamu

Ufafanuzi

Rehoboamu alikuwa mmoja wa wana wa mfalme Sulemani na alikuja kuwa mfalme baada ya Sulemani kufa.

- Katika mwanzo wa utawala wake Rehoboamu alikuwa mkali sana kwa watu wake hivyo makabila kumi ya Israeli waliasi dhidi yake na kuunda ufalme wa Israeli huko Kaskazini.
- Rehoboamu aliendelea kuwa mfalme wa ufalme wa Kusini wa Yuda ambapo kulikuwa na makabila mawili Yuda na Benyamini.
- Rehoboamu alikuwa kiongozi mbaya asiyemtii Mungu na kuabudu miungu ya uongo.

Rimoni

Ufafanuzi

Rimoni ni jina la mtu na jina la mahali lililotajwa sehemu katika Biblia. Pia lilikuwa jina la mungu wa uongo.

- Mtu aliyeitwa Rimoni alikuwa mbenyamini toka mji ya Zebuloni. Mtoto wa mtu huyu alimuua Ishboshethi mwana kilema wa Yonathani.
- Rimoni ulikuwa mji uliokuwa Kusini mwa Yuda katika mkoa uliotawaliwa na kabila la Benyamini.
- Mwamba wa Rimoni palikuwa mahali pa usalama ambapo Wabenyamini walikimbilia wakitoroka kuuawa vitani.
- Rimoni Perezi ni mji usiojulikana ulipokuwa katika jangwa la Yuda.
- Naamani jemedari wa Shamu aliongea katika hekalu la mungu wa uongo Rimoni ambapo watu wa Shamu waliabudu.

Rubeni

Ufafanuzi

Rubeni alikuwa mtoto wa kwanza wa Yakobo. Mama yake alikuwa Lea.

- Kaka zake walipopanga kumuua mdogo wao Yusufu, Rubeni aliyaokoa maisha ya Yusufu kwa kuwaambia wamtupe katika shimo.
- Robeni alikuja baadae kumuokoa Yusufu lakini kaka zake wengine walikuwa wameshamuuza kama mtumwa kwa wafanyabiashara waliokuwa wakipita.
- Uzao wa Rubeni ulikuja kuwa moja ya makabila ya Israeli.

Rumi

Ufafanuzi

Katika agano jipya mji wa Rumi ulikuwa mji muhimu wa himaya ya Warumi. Sasa ni mji kuu wa Itali.

- Himaya ya Warumi ilitawala miji yote kuzunguka bahari ya Mediteraniani pamoja na Israeli.
- Rumi ni neno linaloelezea chochote kinachozungumzia miji iliyotawaliwa na serikali ya Rumi.
- Mtume Paulo alipelekwa mji wa Rumi kama mfungwa kwa sababu alihubiri habari njema kuhusu Yesu. Kitabu cha Warumi ni barua ya Paulo kwa Wakristo waliokuwa Rumi.

Ruthu

Ufafanuzi

Ruthu alikuwa mwanamke Mmoabu aliyeolewa na Muisraeli aliyeamia Moabu na familia yake wakati ambao waamuzi wanaongoza Israeli.

- Mume wa Ruthu alikufa na baada ya hayo aliondoka Moabu akasafiri na mama mkwe wake Naomi aliyerejea mjini kwao Bethelehemu iliyoko Israeli.
- Ruthu alikuwa mwaminifu kwa Naomi na alifanya kazi kwa bidii ili kumpatia chakula Naomi.
- Ruthu alijitoa kumtumikia Mungu wa kweli wa Israeli.
- Ruthu aliolewa na Muisraeli aliyeitwa Boazi na akazaa mtoto mwanaume aliyekuja kuwa babu yake na mfalme Daudi na uzao wa Yesu Kristo.

Sadoki

Ufafanuzi

Sadoki lilikuwa ni jina la kuhani mkuu aliyekuwa mtu mhimu katika Israeli wakati wa utawala wa Mfalme Daudi.

- Wakati Absalomu aliasi dhidi ya Mfalme Daudi, Sadoki alimsaidia Daudi na alisaidia kwa kulirudisha Yerusalemu sanduku la agano.
- Miaka kadhaa baadaye, alihusika katika sherehe ya kumtia mafuta Sulemani mwana wa Daudi kuwa mfalme.
- Watu wawili tofauti wenye jina Sadoki walihusika katika kujenga kuta za Yerusalemu nyakati za Nehemia.
- Sadoki pia lilikuwa ni jina la babu yake Mfalme Yothamu.

Sakothi

Ufafanuzi

Sakothi ni jina la miji miwili ya Agano la Kale. Neno, "sakothi" lina maana ya "hifadhi."

- Mji wa kwanza uliyo itwa Sakothi ulikuwa mashariki mwa Mto Yordani.
- Yakobo alibaki Sakothi na familia yake na mifugo, akijenga mahifadhi yao hapo.
- Miaka mia na zaidi baadae, Gideoni na wanaume wake waliyo choka alisimama Sakothi walipo kuwa wakiwakimbiza Wamidiani, lakini watu huko walikataa kuwapa chakula chochote.
- Sakothi ya pili ipo kaskazini mwa mpaka wa Misri na ilikuwa sehemu moja Waisraeli walisimama walipo vuka Bahari ya Shamu walipo kuwa wanatoroka utumwa Misri.

Samaria, Msamaria

Ufafanuzi

Samaria ilikuwa jina la mji na maeneo yake jirani kaskazini mwa Israeli. Eneo hili lilikuwa katikati ya Milima ya Sharoni magharibi na Mto Yordani mashariki.

- Katika Agano la Kale, Samaria ulikuwa mji mkuu wa ufalme wa kaskazini wa Israeli. Baadae eneo lililo kuwa jirani liliitwa Samaria.
- Wakati Waassiria walipo chukuwa ufalme wa kaskazini wa Israeli, waliteka mji wa Samaria na kuwa lazimisha Waisraeli wa kaskazini kuondoka eneo hilo na kuwa hamisha maeneo tofauti katika miji ya Assiria.
- Waassiria pia walileta wageni wengi katika eneo la Samaria kuwaweka katika maeneo Waisraeli waliyo ondolewa.
- Baadhi ya Waisraeli waliyo baki eneo hilo walioa wageni waliyo hamia, na wazao wao waliitwa Wasamaria.
- Wayahudi waliwadharau Wasamaria kwasababu walikuwa nusu Wayahudi na kwasababu mababu zao waliabudu miungu ya wapagani.
- Katika kipindi cha Agano Jipya, eneo la Samaria lilipakana na Galilaya upande wa kaskazini na eneo la Yudea upande wa kusini.

Samsoni

Ufafanuzi

Samsoni alikuwa mmoja wa waamuzi, au mkombozi, wa Israeli. Alitoka kabila la Dani.

- Mungu alimpa Samsoni uwezo mkubwa wa kibanadamu aliyo tumia kupigana na maadui wa Israeli, Wafilisti.
- Samsoni aliwekwa chini ya kiapo kutonyoa nywele na kutokunywa mvinyo au kinywaji chochote kilicho chachwa. Kadri alivyo shika hichi kiapo, Mungu aliendelea kumpa uwezo.
- Hatimaye alivunja kiapo chake na kuruhusu nywele zake kunyolewa, ambao ili ruhusu Wafilisti kumkamata.
- Wakati Samsoni alipo kuwa matekani, Mungu alimruhusu kupata tena uwezo wake na kumpa nafasi ya kuharibu hekalu la mungu wa uongo Dagoni, pamoja na Wafilisti wengi.

Samweli

Ufafanuzi

Samweli alikuwa nabii na muamuzi wa mwisho wa Israeli. Alimpaka mafuta Sauli na Daudi kama wafalme juu ya Israeli.

- Samweli alizaliwa kwa Elikana na Hanna katika mji wa Rama.
- Hanna alikuwa tasa, hivyo aliomba kwa shauku kwamba Mungu ampe mtoto. Samweli alikuwa jibu la hilo ombi.
- Samweli alivyo kuwa mvulana mdogo, Hanna alimtuma kumsaidia Eli kuhani katika hekalu kutimiza ahadi yake kwa Mungu.
- Mungu alimuinua Samweli kuwa nabii mkuu wake.

Sara, Sarai

Ufafanuzi

Sara alikuwa mke wa Ibrahimu.

- Jina lake awali lilikuwa "Sarai," lakini Mungu akalibadilisha kuwa "Sara"
- Sara alimza mwana Mungu alilye muahidi kumpa yeye na Ibrahimu.

Sauli (A K)

Ufafanuzi

Sauli alikuwa mwanaume wa Kiisraeli ambaye Mungu alimchagua kuwa mfalme wa kwanza wa Israeli.

- Sauli alikuwa mrefu na mtanashati, na mwanajeshi mwenye nguvu. Alikuwa aina ya mwanaume Waisraeli walitaka awe mfalme wao.
- Japo kuwa alimtumikia Mungu mwanzoni, Sauli baadae alikuwa na kiburi na hakumtii Mung. Matokeo yake, Mungu alimteua Daudi kuchukuwa nafasi ya mfalme na kumruhusu Sauli kuuawa katika pambano.
- Katika Agano Jipya, kulikuwa na Myahudi aliye itwa Sauli ambaye pia alijulikana kama Paulo na akawa mtume wa Yesu Kristo.

Sedekia

Ufafanuzi

Sedekia, mwana wa Yosia, alikuwa mfalme wa mwisho wa Yuda (597- 587 KK). Lakini pia kuna watu kadhaa katika Agano la Kale wenye jina Sedekia.

- Mfalme Nebukadneza alimtawaza Sedekia kuwa mfalme wa Yuda baada ya kumteka Mfalme Yehoyakini na kwenda naye huko Babeli. Baadaye Sedekia aliasi jambo lililomfanya Nebukadneza kumkamata na kuuangamiza Yerusalemu.
- Sedekia, mwana wa Kenaana, alikuwa nabii wa uongo wakati wa Mfalme Ahabu wa Israeli.
- Mtu aliyeitwa Sedekia alikuwa mmojawapo wa wale waliosaini mkataba kwa Bwana nyakati za Nehemia.

Senakeribu

Ufafanuzi

Senakeribu alikuwa mfalme mkubwa wa Assiria aliye sababisha Ninawi kuwa tajiri, na mji wa muhimu.

- Mfalme Senakeribu anajulikana kwa vita vyake dhidi ya Babiloni na ufalme wa Yuda.
- Alikuwa mfalme mwenye kiburi na kumdhihaki Yahweh.
- Senakeribu alishambulia Yerusalemu kipindi cha Mfalme Hezekia.
- Yahweh alisababisha jeshi la Senakeribu kuharibiwa.
- Vitabu vya Agano la Kale vya Wafalme na Nyakati vina adisia baadhi ya matukio ya Senakeribu na utawala wake.

Sethi

Ufafanuzi

Katika kitabu cha Mwanzo, Sethi alikuwa mwana wa tatu wa Adamu na Hawa.

- Hawa alisema kwamba Sethi alipewa kwake kwa sehemu ya mwanae Abeli, aliye uawa na kaka yake Kaini.
- Nuhu alikuwa mzao wa Sethi, hivyo kila mtu aliye ishi tangu kipindi cha gharika ni mzao wa Sethi.
- Sethi na familia yake walikuwa watu wa kwanza "kuliita jina la Bwana."

Sharoni, Milima ya Sharoni

Ufafanuzi

Sharoni lilikuwa jina la ardhi ya rotuba pembeni ya Bahari ya Mediterenia, kusini mwa Mlima Karmeli. Unajulikana pia kama "Mlima wa Sharoni."

- Miji kadhaa iliyo tajwa kwenye Biblia ilikuwa karibu na Mlima wa Sharoni, pamoja na Jopa, Lidia, na Kaesarea.
- Hii yaweza tafsiriwa kama "mlima unao itwa Sharoni" au "Mlima Sharoni."
- Watu waliyo ishi maeneo haya ya Sharoni waliitwa "Washaroni."

Sheba

Ufafanuzi

Wakati wa zamani, Sheba ulikuwa mji wa zamani wa kisasa au eneo la nchi lililo kuwa karibu na kusini mwa Arabia.

- Nchi ya Sheba au eneo lilikuwa karibu na nchi inayo julikana sasa kama Yemeni au Ethiopia.
- Wakazi wake walikuwa wazao wa Hamu.
- Malikia wa Sheba alienda mtembelea Mfalme Sulemani alipo sikia umaarufu wa utajiri wake na hekima.
- Pia kuna baadhi ya wanaume wanao itwa "Sheba" waliyo tajwa kwenye kizazi cha Agano la Kale. Yawezekana jina la eneo lilitokana na mmoja wa hawa watu.
- Mji wa Beersheba umefupishwa kwa Sheba mara moja katika Agano la Kale.

Shekemi

Ufafanuzi

Shekemi ni mji uliyopo maili 40 kaskazini mwa Yerusalemu. Shekemi ni jina pia la mwanaume katika Agano la Kale.

- Mji wa Shekemi ndipo Yakobo alipo ishi baada ya kupatana na kaka yake Esau.
- Yakobo alinunua ardhi kutoka kwa wana wa Hamori na Wahivi huko Shekemi, ambao baadae wakawa makaburi ya familia yake na sehemu wana wa Yakobo walipo zikwa.
- Mwana wa Hamori Shekemi alimbaka binti wa Yakobo Dina, ambao ilileta wana wa Yakobo kuuwa wanaume wote wa mji wa Shekemi.

Shemu

Ufafanuzi

Shemu alikuwa mmoja wa wana wa Nuhu aliye enda nae kwenye safina kipindi cha gharika ya ulimwengu inayo elezwa katika kitabu cha Mwanzo.

- Shemu alikuwa babu wa Ibrahimu na wazao wake.
- Wazao wa Shemu wanajulikana kama "Wasemi" wanao zungumza lugha za "Kisemi" kama vile Kiebrania na Kiarabu.
- Biblia ina kumbukumbu ya maisha ya Shemu kuwa takribani miaka 600.

Shilo

Ufafanuzi

Shilo ulikuwa mji wa ukuta wa Kikanani uliyo shindwa na Waisraeli chini ya uongozi wa Yoshua.

- Mji wa Shilo ulikuwa magharibi mwa Mto Yordani na kaskazini mashariki mwa mji wa Betheli.
- Kipindi Yoshua alipo waongoza Israeli, mji wa Shilo ulikuwa sehemu ya kukutana watu wa Israeli.
- Makabila kumi na mbili ya Israeli yalikutana pamoja Shilo kusikia Yoshua akiwaambia kiasi gani cha nchi ya Kanani ilipangiwa kila mmoja.

Shimei

Ufafanuzi

Shimei ni jina la wanaume kadhaa wa Agano la Kale.

- Shimei mwana wa Gera, alikuwa Mbenjamini aliye mlaani Mfalme Daudi na kutupa mawe kwake alipo kuwa akikimbia Yerusalemu kutoroka asiuliwe na mwanaye Absalomu.
- Pia kulikuwa na makuhani wa Kilawi katika Agano la Kale waliyo itwa Shimei.

Shinari

Ufafanuzi

Shinari ina maana ya "nchi ya mito miwili" na lilikuwa jina la mlima au eneo kusini mwa Mesopotamia.

- Shinari baadae ilijulikana kama "Kaldea" na baadae, "Babilonia."
- Watu wa kale waliyo ishi mji wa Babeli katika Mlima wa Shinari walijenga mnara mrefu kujaribu kujifanya wakuu.
- Vizazi baadae, mababa wa Kiyahudi Ibrahimu aliishi katika mji wa Uri katika hili eneo, ambalo liliitwa "Kaldeo."

Sidoni, Wasidoni

Ufafanuzi

Sidoni alikuwa mwana wa kwanza wa Kanani. Pia kuna mji wa Kikanani unao itwa Sidoni, labda uliitwa baada ya mwana wa Kanani.

- Mji wa Sidoni ulikuwa upanda wa kaskazini mgharibi pwani ya Bahari ya Mediterenia eneo lililo sasa Lebanoni.
- "Wasidoni" wa kundi la Foenisi waliyo ishi Sidoni na maeneo yanayo zunguka.
- Katika Biblia, Sidoni ipo karibu na mji wa Tairi, na miji yote miwili ilijulikana kwa utajiri na uhuni wa tabia za watu wao.

Sila, Silivanu

Ufafanuzi

Sila alikuwa kiongozi miongoni mwa waamini wa Yerusalemu.

- Wazee wa kanisa la Yerusalemu alichagua Sila na Paulo na Barnaba kuleta barua kwa mji wa Antioki.
- Sila baadae alisafiria na Paulo kwenye miji mingine kufundisha watu kuhusu Yesu.
- Paulo na Sila waliwekwa gerezani katika mji wa Filipi. Waliimba nyimbo kwa Mungu wakati walipo kuwa huko na Mungu akawafungua kutoka gerezani. Askari wa gereza akawa Mkristo sababu ya ushuhuda wao.

Simeoni

Ufafanuzi

Katika Biblia, kuna wanaume kadhaa wenye jina Simeoni.

- Katika Agano la Kale, mwana wa pili wa Yakobo (Israeli) na Leah aliitwa Simeoni. Wazao wake walikuwa moja ya makabila kumi na mbili ya Israeli.
- Kabila la Simeoni lilitawala eneo la kusini katika nchi ya ahadi ya Kanani, eneo lilio kuwa sehemu ya urithi wa Yuda.
- Wakati Yusufu na Mariamu walipo mleta mtoto Yesu kwenye hekalu Yerusalemu kumtoa kwa Mungu, mzee mmoja jina lake Simeoni alimsifu Mungu kwa kumruhusu kumuona Mesiya.

Simoni

Ufafanuzi

Simoni alikuwa mmoja wa wanafunzi kumi na mbili wa Yesu.

- Simoni anatajwa mara tatu katika orodha ya wanafunzi wa Yesu, lakini machache yana julikana kuhusu yeye.
- Simoni alikuwa mmoja wa wale Kumi na Moja waliyo kutana kuomba pamoja Yerusalemu baada ya Yesu kurudi mbinguni.

Sinai, Mlima Sinai

Ufafanuzi

Mlima Sinai ni jina la mlima uliyo upande wa kusini wa unao julikana kama Sinai Peninsula kwa sasa. Pia ulijulikana kama "Mlima wa Horebu."

- Mlima Sinai ni sehemu kubwa ya jangwa la mawe.
- Waisraeli walikuja Mlima Sinai walipo kuwa wanasafiri kutoka Misri kwenda nchi ya ahadi.
- Mungu alimpa Musa amri kumi Mlima Sinai.

Soari

Ufafanuzi

Soari ulikuwa mji mdogo Alipokimbilia Lutu wakati Mungu alipoiaribu Sodoma na Gomora.

- Hapo mwanzo ilikuwa inajulikana kama "Bela" lakini baadaye yake uliitwa "Soari" wakati Lutu alipomwomba Mungu kuuifadhi mji huu "mdogo".
- Soari unaaminiwa kuwa ulikuwa katika tambarare za Mto Yordani au katika mpaka wa kusini wa Bahari ya Chumvi.

Sodoma

Ufafanuzi

Sodoma ulikuwa mji kusini mwa kanani ambapo mpwa wa Ibrahimu Lutu aliishi na mke na watoto wake.

- Nchi ya eneo linalo zunguka Sodoma ulinyeshewa vizuri na kurotubishwa, hapo ndipo Lutu alichagua kuishi alipo hamia Kanani.
- Sehemu maalumu ya huu mji haujulikana kwasababu Sodoma na mji wa jirani wa Gomora ili haribiwa kabisa na Mungu kama adhabu kwa matendo maovu waliyo kuwa wanafanya.

Stefano

Ufafanuzi

Stefano anajulikana kama Mkristo wa kwanza kuuawa, sababu ya imani yake kwa Yesu. Maisha yake na kifo yameandikwa kwenye kitabu cha Matendo.

- Stefano alichaguliwa na Kanisa la awali la Yerusalemu kutumikia Wakristo kama shemasi kuwapa chakula wajane na wengine Wakristo wenye maitaji.
- Baadhi ya Wayahudi walimshtumu kwa uongo Stefano kuzungumza dhidi ya Mungu na dhidi ya sheria ya Musa.
- Stefano kwa ujasiri alisema ukweli kuhusu Yesu Mesiya, kwa kuanza na historia ya matendo ya Mungu kwa Waisraeli.
- Viongozi wa Wayahudi walikasirika na kumuua Stefano kwa kumpiga mawe hadi kufa nje ya mji.
- Kifo chake kilishuhudiwa na Sauli wa Tarso, baade kuwa mtume Paulo.
- Stefano anajulikana pia kwa maneno yake ya mwisho kabla ya kufa: Bwana, tafadhali usihesabu dhambi hii dhidi yao," iliyo onyesha upendo aliyo kuwa nao kwa wengine.

Sulemani

Ufafanuzi

Sulemani alikuwa mmoja wa wana wa Mfalme Daudi. Mama yake alikuwa ni Bathsheba.

- Sulemani alipo kuwa mfalme, Mungu alimwambia aulize chochote alicho taka. Hivyo Sulemani aliomba hekima kutawala watu wake kwa haki na kweli. Mungu alifurahishwa na Sulemani na kumpa hekima na utajiri.
- Sulemani ni al maarufu kwa kuwa na hekalu zuri Yerusalemu.
- Japo kuwa Sulemani alitawala kwa hekima mwanzoni mwa utawala wake, baadae alioa kijinga wanawake wengi wa kigeni na kuanza kuabudu miungu yao.
- Kwasababu ya kutokuwa mwaminifu, baada ya kifo chake Mungu aligawanya Waisraeli kwenye falme mbili: Israeli na Yuda. Hizi falme mara nyingi zilipigana.

Syria

Ufafanuzi

Syria ni nchi iliyopo kaskazini mashariki ya Israeli. Wakati wa kipindi cha Agano Jipya, ilikuwa mkoa chini ya utawala wa Serikali ya Kirumi.

- Katika Agano la Kale, Wasyria walikuwa jeshi kubwa la maadui wa Israeli.
- Naamani alikuwa kiongozi mkuu wa jsehi la Syria aliye ponywa ukoma na nabii Elisha.
- Wakazi wengi wa Syria ni wazao wa Aramu, aliye mzao wa mwana wa Nuhu Shemu.
- Damasko, mji mkuu wa Syria, unatajwa mara nyingi kwenye Biblia.
- Sauli alienda mji wa Damasko kwa mpango wa kutesa Wakristo, lakini Yesu alimzuia

Tairi, Watairi

Ufafanuzi

Tairi ulikuwa mji wa zamani wa Kanani eneo la pwani mwa Bahari ya Mediterenia, katika eneo ambalo sasa ni sehemu nchi ya Lebanoni. Watu wake waliitwa "Watairi."

- Sehemu ya mji pia ulikuwa katika kisiwa kwenye bahari, karibu na kilomita moja na pwani.
- Kwasababu ya eneo na thamani ya mali halisi kama miti mierezi, Tairi ulikuwa na biashara iliyo fanikiwa ya masoko na ilikuwa tajiri sana.
- Mfalme Hiramu wa Tairi alituma mbao kutoka mti wa mierezi na wa jenzi wa ujuzi wa kujenga jumba ya Mfalme Daudi.
- Miaka mingi baadae, Hiramu pia alimpa Mfalme Sulemani mbao na wajenzi wa ujuzi wa kutengeneza hekalu. Sulemani alimlipa kiasi kikubwa cha ngano na mafuta ya mzaituni.

Tamari

Ufafanuzi

Tamari ni jina la wanawake kadhaa katika Agano la Kale. Ni jina la miji ya maeno kadhaa katika Agano la Kale.

- Tamari alikuwa mke wa mtoto wa Yuda. Alimzaa Perezi aliye kuwa babu wa Yesu Kristo.
- Mmoja wa mabinti wa Mfalme Daudi pia aliitwa Tamari; alikuwa dada wa Absalomu. Kaka yake wa kambo Amnoni alimbaka na kutelekeza.
- Absalomu pia alikuwa na binti aitwaye Tamari.
- Mji unao itwa "Hazezoni Tamari" ni mji sawa na mji wa Engedi magharibi mwa pwani ya Bahari ya Chumvi.

Tarishishi

Ufafanuzi

Tarishishi lilikuwa jina la wanaume wawili wa Agano la Kale. Lilikuwa jina la mji.

- Mmoja wa wajukuu wa Yafeti aliitwa Tarishishi.
- Tarishishi pia lilikuwa ni jina la mmoja wa wanaume wenye hekima wa mfalme Ahashuerusi.
- Mjia wa Tarishishi ulikuwa wa kitajiri wa bandari, ambao mali zake zilibeba bidha za kuuza au kubadilisha.
- Huu mji ulishirikiana na Tairi na wazo lake wakuwa mji wa Foenisia lilikuwa mbali na Israeli, yamkini kusini ya pwani ya Spain
- Nabii wa Agano la kale Yona alipanda meli iliyo kuwa yaelekea Tarishishi badala ya kutii amri ya Mungu kwenda kuubiri Ninawi.

Tarso

Ufafanuzi

Tarso ulikuwa mji uliyo fanikiwa katika mko wa Kirumi wa Silisia, ambao sasa ni Uturuki ya kati.

- Tarso ulikuwa kando ya mto mkubwa na karibu na Bahari ya Mediterenia, uliyo ufanya njia muhimu ya biashara.
- Wakati mmoja katika historia, ulikuwa mji mkuu wa Silisia.
- Katika Agano Jipya, Tarso ulikuwa maarufu kwa kuwa mji wa nyumbani wa Paulo Mtume.

Tera

Ufafanuzi

Tera alikuwa mzao wa mwana wa Nuhu, Shemu. Alikuwa mwana wa Abramu, Nahori na Harani.

- Tera aliondoka nyumbani Uri ilikuweza kwenda kwenye nchi ya Kanani na mwanae Abramu, mtoto wa mjomba yake Lutu, na mke wa Abramu Sarai.
- Alipo kuwa njiani kwenda Kanani, Tera na familia yake waliishi miaka mingi mji wa Harani Mesopotamia. Tera alikufa Harani na miaka 205.

Thesalonike, Wathesalonike

Ufafanuzi

Katika kipindi cha Agano Jipya, Thesalonika ulikuwa mji mkuu wa Makedonia katika utawala wa zamani wa Rumi. Watu waliyo ishi kwenye mji waliitwa "Wathesalonike."

- Mji wa Thesalonike ulikuwa muhimu kwa bandari na pia ulikuwa karibu na barabara iliyo unganisha na Rumi mashariki mwa serikali ya Rumi.
- Paulo, na sila na Timotheo, walitembelea Thesalonike katika safari yake ya pili ya kimisheni na matokeo yake, kanisa lilijengwa. Baadae, Paulo alitembelea mji huu kwenye safari yake ya pili ya umisheni.
- Paulo aliandika barua mbili kwa Wakristo wa Thesalonike.

Thomaso

Ufafanuzi

Thomaso alikuwa mmoja wa wanaume kumi na mbili Yesu aliye wachagua kuwa wanafunzi na baadae, mitume. Alijulikana kama "Didimasi" yenye maana ya "pacha."

- Mwisho wa maisha ya Yesu, aliwaambia wanafunzi wake anaenda kuwa na Baba na ata andaa sehemu ya wao kuwa naye. Thomaso alimuuliza Yesu jinsi gani watajua njia ya kufika huko wakati hawakujua wapi anaenda.
- Baada ya Yesu kufa na kufufuka, Thomaso alisema hataamini kwamba Yesu yu hai tena mpaka atakapo ona na kugusa makovu ya Yesu.

Tikiko

Ufafanuzi

Tikiko alikuwa mmoja wa watumishi wa Paulo wa injili.

- Tikiko alienda na Paulo kati ya moja ya safari ya kimisheni ya Paulo huko Asia.
- Paulo alimueleza kama "mpendwa" na "mwaminifu."
- Tikiko alibeba barua za Paulo kwenda Efeso na Kolosai

Timotheo

Ufafanuzi

Timotheo alikuwa jina mdogo kutoka Lystra aliye kuwa mwaamini katika Kristo kutokana na huduma ya Paulo mjini kwake. Baadae alijiunga na Paulo kwenye safari kadhaa za misheni na kusaidia chunga waamini wapya.

- Baba yake Timotheo alikuwa Mgiriki, lakini bibi yake na mama walikuwa Wayahudi na waamini wa Kristo.
- Wazee na Paulo walimchagua Timotheo kwenye huduma kwa kumuekea mikono na kumuombea.
- Vitabu viwili kwenye Agano Jipya (1Timotheo na 2Timotheo) ni barua zilizo andikwa na Paulo, akitoa muongozo kwa Timotheo kama kiongozi mdogo wa kanisa.

Tirza

Ufafanuzi

Tirza ulikuwa mji muhimu wa Kanani uliyo chukuliwa na Waisraeli. Lilikuwa jina la binti wa Gileadi, mzao wa Manase.

- Mji Tirza ulikuwa eneo lenye wakazi wa kabila la Manase. Inadhaniwa kuwa mji ulikuwa maili 10 kaskazini mwa mji wa Shekemi.
- Miaka baadae, Tirza ukawa mji mkuu wa ufalme wa kaskazini wa Israeli kwa muda mfupi, kipindi cha wafalme wa nne wa Israeli.
- Tirza pia lilikuwa jina la mjukuu mmoja wa Manase aliye omba apewa kiasi cha ardhi, maana hawakuwa na kaka wa kurithi kama ilivyo kuwa kawaida.

Tito

Ufafanuzi

Tito alikuwa Mpagani alikuja kuwa mwamini kupitia huduma ya Paulo mtume. Alifunzwa na Paulo kuwa kiongozi mwanzo wa makanisa.

- Barua kwa Tito na Paulo ni moja ya vitabu vya Agano Jipya.
- Katika hii barua Paulo ana muelekeza Titp kuteua viongozi wa kanisa katika kisiwa cha Krete.
- Katika barua zake zingine kwa Wakristo, Paulo anamtaja Tito kama mtu aliye mtia moyo na kumletea furaha

Troa

Ufafanuzi

Mji wa Troa ulikuwa bandari kaskazini magharibi mwa pwani ya eneo la Rumi huko Asia.

- Paulo alitembelea Troas mara tatu kipindi cha safari zake maeneo tofauti kuhubiri injili.
- Siku moja huko Troa Paulo alihubiri muda mrefu hadi usiku na kijana mmoja Eutiko alianguka chini kwasababu ya usingizi kwa kumsikiliza. Maana alikuwa ameketi katika dirisha lillio wazi, Eutiko alianguka chini sana na kufa. Kwa nguvu za Mungu, Paulo alimleta kijana huyu uzimani.
- Paulo alipo kuwa Rumi, alimuomba Timotheo kuleta vitabu vyake na koti, aliyo acha Troa.

Tubali

Ufafanuzi

Kuna wanaume kadhaa kwenye Agano la Kale waliyo kuwa na majina "Tubali."

- Mwanaume mmoja aliye itwa Tubali alikuwa mmoja wa wana wa Yafeti.
- Mwanaume aliye itwa "Tubali Kaini" alikuwa mwana wa Lameki na mzaliwa wa Kaini.
- Tubali pia ni jina la kundi la watu linalo tajwa na nabii Isaya na Ezekieli.

Uajemi, Waajemi

Ufafanuzi

Uajeni ni nchi ambayo ilikuja kuwa ngome kubwa iliyoundwa na mfalme Cyrus mwaka 550 kabla ya Kristo. Nchi ya uajemi ilikuwa kusini mashariki mwa Babeli na Ashuru ambayo kwa sasa ni Irani.

- Watu wa Uajemi waliitwa Waajemi.
- Mfalme Cyrus alisema kuwa Wayahudi wapo huru toka mateka huko Babeli na akawaruhusu kurudi nyumbani na hekalu la Yerusalemu likajengwa kwa pesa zilizotoka katika ngome ya Uajemi.
- Mfalme Artashasta alikuwa kiongozi wa ngome ya Uajemi wakati ambao Ezra na Nehemia walirudi Yerusalemu na kujenga tena ukuta wa Yerusalemu.
- Esta akawa malkia wa ngome ya Uajemi alipoolewa na mfalme Ahusuero.

Uarabuni, mwarabu

Ufafanuzi

Uarabuni ni sehemu kubwa sana duniani yenye kilomita za mraba 3,000,000. Inapatikana kusini mashariki mwa Israeli na imepakana na bahari ya shamu, bahari ya Arabia na ghuba ya uajemi.

- Mwarabu ni mtu anayeishi uarabuni.
- Watu wa kwanza kuishi uarabuni walikuwa wajukuu wa Shemu. Mwingine ni mtoto wa Abrahamu Ishmaeli na kizazi chake pamoja na kizazi cha Esau.
- Jangwa ambalo Waisraeli walizunguka miaka 40 lilikuwa Uarabuni.
- Baada ya kumwamini Yesu mtume Paulo aliishi miaka michache katika jangwa la Arabia.
- Katika barua yake kwa Wakristo wa Galatia, Paulo anataja mlima Sinai uliopo Uarabuni.

ufalme wa Israeli

Ufafanuzi

Usemi "ufalme wa Israeli" unamaanisha sehemu ya kaskazini mwa taifa la Israeli wakati makabila kumi na mbili ya Israeli yalipogawanyika katika falme mbili baada ya Sulemani kufa.

Ufalme wa Israeli wa kaskazini ulikuwa na makabila kumi na ufalme wa Yuda ulikuwa na makabila mawili. Mji mkuu wa ufalme wa Israeli ulikuwa Samaria. Ilikuwa kama kilomita 50 kutoka Yerusalemu, mji mkuu wa Yuda. Wafalme wote wa ufalme wa Israeli walikuwa waovu. Waliwashawishi watu kutumikia sanamu na miungu ya uongo. Mungu aliwatuma Waashuri kuvamia taifa la Israeli. Waisraeli wengi walikamatwa na kupelekwa kuishi Ashuru. Waashuri waliwaleta wageni kuishi miongoni mwa watu waliobaki wa Israeli. wageni hawa waliowana na Waisraeli, na uzao wao ukawa watu wa Samaria.

Ufilisti

Ufafanuzi

Ufilisti ni jina la mji mkubwa katika nchi ya Kanaani iliyopo pwani mwa Bahari ya Mediteraniani.

- Mji huu ulikuwa kando ya pwani yenye rutuba toka Yopa kaskazini kwenda Gaza kusini. Ilikuwa Kilometa 64 urefu na upana Kilometa 16.
- Ufilisti ilikaliwa na "Wafilisti" kundi la watu lenye nguvu ambao mara nyingi walikuwa maadui wa Waisraeli.

Ukaldayo, Wakaldayo

Ufafanuzi

Ukaldayo ulikuwa mkoa wa kusini mwa Mesopotamia au Babeli. Watu walioishi katika mkoa huo waliitwa Wakaldayo.

- Katika mji wa Uri alipotoka Abrahamu ulikuwepo Ukaldayo. Hutajwa kama "Uri ya Ukaldayo.
- Mfalme Nebukadreza alikuwa mmoja wa Wakaldayo waliokuwa wafalme katika Bebeli.
- Baada ya miaka mingi katika mwaka wa 600 Kabla ya Kristo Ukaldayo ilikuja kuwa na maana ya Babeli.
- Katika kitabu cha Danieli "Wakaldayo" walikuwa ni kundi fulani maalumu la watu waliokuwa na elimu kubwa na wataalamu wa nyota.

Uri

Ufafanuzi

Uri ulikuwa mji muhimu pembeni mwa Mto Frati katika mji wa zamani wa Kalidea, ambao ulikuwa sehemu ya Mesopotamia. Hili eneo lilikuwa ambapo sasa ni Iraqi.

- Ibrahimu alitoka mji wa Uri na ndipo huko Mungu alimuita kuondoka kwenda nchi ya Kanani.
- Harani, kaka wa Ibrahimu na baba wa Lutu, alikufa Uri. Hii inawezana ikawa sababu Lutu aliondoka Uri na Ibrahimu.

Uria

Ufafanuzi

Uria alikuwa mwanaume mwenye haki na mmoja wanajeshi hodari wa Mfalme Daudi. Utajwa kama "Uria Mhiti"

- Uria alikuwa na mke mzuri sana aliye itwa Bathisheba.
- Daudi alifanya uasherati na mke wa Uria, na akashikwa mimba na mtoto wa Daudi.
- Kufunika hii dhambi, Daudi alisababisha Uria kufa kwenye pambano. Kisha Daudi akamuoa Bathisheba.
- Mwanaume mwingine aliye itwa Uria alikuwa kuhani wakati wa Mfalme Ahazi.

Uzia, Azaria

Ufafanuzi

Uzia alikuwa mfalme wa Yuda akiwa ni umri wa miaka 16 na akatawala miaka 52, ambao ulikuwa utawala mrefu. Uzia alijulikana kama "Azaria."

- Mfalme Uzia alijulikana kwa mpangilio na ujuzi wa kijeshi. Alikuwa na maghorofa yaliyo jengwa kulinda mji na silaha maalumu za vita zilizo undwa na kuwekwa juu yake kubeba mishale na mawe makubwa.
- Kadri Uzia alivyo mtumikia Bwana, alifanikiwa. Mwisho utawala wake, walakini, alipatwa na kiburi na hakumtii Bwana kwa kuchoma uvumba kwenye hekalu, ambaye kuhani tu ndiye aliruhusiwa kufanya hivyo.
- Kwasababu ya dhambi hii, Uzia aliumwa na ukoma na alibidi aishi mbali na watu hadi mwisho wa utawala wake.

Vashti

Ufafanuzi

Katika agano la kale kwenye kitabu cha Esta, Vashti alikuwa mke wa Ahasuero mfalme wa Uajemi.

- Mfalme Ahasuero alimfukuza malkia Vashti baada ya kukataa kutii amri zake yake ya kwenda kwenye chakula cha jioni na kuonesha uzuri wake kwa wageni.
- Matokeo yake mfalme alikwenda kutafuta malkia mpya na Esta akachaguliwa kuwa mke mpya wa Mfalme.

Wafilisti

Ufafanuzi

Wafilisti walikuwa kundi la watu waliokaa katika mji wa Ufilisti kando ya bahari ya Mediteraniani. Jina lao linamaana ya "watu wa baharini"

- Kulikuwa na miji mikuu mitano ya Wafilisti: Ashodi, Ashkelon, Ekroni, Gathi, na Gaza.
- Mji wa Ashodi ulikuwa kaskazini mwa Ufilisti na mji wa Gaza ulikuwa kusini.
- Wafilisti walijulikana kwa miaka mingi walikuwa katika vita na Waisraeli.
- Mwamuzi Samsoni alikuwa shujaa aliyejulikana sana dhidi ya Wafilisti aliyetumia nguvu zake toka kwa Mungu.
- Mfalme Daudi alionfoza vita dhidi ya Wafilisti ikiwemo kipindi alipokuwa kijana alipomshinda shujaa wa Wafilisti Goliati.

Wakerethi

Ufafanuzi

Wakerethi walikuwa kundi la watu ambao walikuwa kama sehemu ya Wafilisti. Pia imeandikwa kama "Wakerethi."

- "Wakerethi na Waperisi" walikuwa kundi maalumu la maaskari kutoka jeshi la mfalme Daudi. ambao walikuwa wametengwa kwa ajili yake kama walizi.
- Benaya, mwana wa Yehoyada, mdau wa msimamizi wa watu wa Daudi, alikuw akiongozi wa Waperithi na Waperesi.
- Waperethi walibaki na Daudi wakati alipokuwa anakimbia Yerusalimu kwa sababu ya kuchukizwa na Absalomo.

Yafa

Ufafanuzi

Katika nyakati za Biblia, mji wa Yafa ulikuwa mji muhimu wa kibiashara uliopo Bahari ya Kati, kusini mwa uwanda wa Sharoni.

Eneo la zamani la Yafa ndio mji wa leo wa Yafa, ambayo sasa ni sehemu ya Tel Aviv. Katika Agano la Kale, Yafa ndio mji ambao Yona alipanda boti kwenda Tarshishi. Katika Agano Jipya, mwanamke wa Kikristo aitwaye Tabitha alifia Yafa na Petro alimfufua.

Yafethi

Ufafanuzi

Yafethi alikuwa mmoja wa wana watatu wa Nuhu.

Wakati wa mafuriko wa ulimwengu wote uliofunika dunia yote, Yafethi na ndugu zake wawili walikuwa na Nuhu katika safina, pamoja na wake zao. Wana wa Nuhu kawaida huorodheshwa hivi, "Shemu, Hamu, na Yafethi." Hii inaashiria kuwa Yafethi alikuwa mdogo kati ya hao ndugu.

Yakobo (mwana wa Alfayo)

Ufafanuzi

Yakobo, mwana wa Alfayo, alikuwa mmoja wa wanafunzi kumi na mbili wa Yesu.

Jina lake linatolewa katika orodha ya wanafunzi wa Yesu katika injili za Mathayo, Marko, na Luka. Ametajwa pia katika kitabu cha Matendo ya Mitume kama mmoja wa kumi na moja ambao walikuwa pamoja wakiomba Yerusalemu baada ya Yesu kurudi juu mbinguni.

Yakobo (mwana wa Zebedayo)

Ufafanuzi

Yakobo, mwana wa Zebedayo, alikuwa mmoja wa wanafunzi kumi na mbili. Alikuwa na ndugu yake mdogo aliyeitwa Yohana ambaye pia alikuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu.

Yakobo na ndugu yake Yohana walifanya kazi kwa kuvua samaki na baba yao Zebedayo. Yakobo na Yohana waliitwa jina la utani "wana wa ngurumo," labda kwa sabau walikuwa wepesi kukasirika. Petro, Yakobo, na Yohana walikuwa wanafunzi wa karibu zaidi na Yesu na walikuwa naye kwa matukio ya ajabu kama vile Yesu alipokuwa juu ya mlima na Eliya na Musa na Yesu alipomfanya msichana aliyekufa kurudia uhai wake. Huyu ni Yakobo tofauti na yule aliyeandika kitabu katika Biblia. Lugha zingine zinalazimika kuandika majina yao tofauti ili kuweka wazi kuwa walikuwa watu wawili tofauti.

Yakobo (ndugu wa Yesu)

Ufafanuzi

Yakobo alikuwa mwana wa Mariamu na Yusufu. Alikuwa mmoja wapo wa wadogo zake Yesu.

Ndugu zake wengine Yesu walikuwa ni, Yusufu, Yuda na Simoni Wakati wa uhai wa Yesu, Yakobo na ndugu zake hawakuamini kuwa Yesu ndiye Masihi. Baadaye, baada ya Yesu kufufuka katika wafu, Yakobo alimuamini na kuwa kiongozi katika kanisa la Yerusalemu. Kitabu cha Agano Jipya cha Yakobo ni barau ambayo Yakobo aliwaandikia Wakristo waliokimbilia nchi zingine kutoroka mateso.

Yakobo, Israeli

Ufafanuzi

Yakobo alikuwa pacha mdogo aliyekuwa mwana wa Isaka na Rebeka.

Jina la Yakobo linamaanisha "anakamata kisigino" ambao ni usemi unaomaanisha, "hudanganya." Wakati yakobo alipozaliwa, alikuwa akishilia kisigino cha pacha wake Esau. Miaka mingi baadaye, Mungu alibalisha jina la Yakobo kuwa "Israeli," inayomaanisha, "anashindana na Mungu." Yakobo alikuwa mjanja na muongo. Alipata njia ya kupata baraka za mwana wa kwanza na kurithi haki kutoka kwa kaka yake, Esau. Esau alikasirika na kupanga kumuua, kwa hiyo Yakobo akaondoka nchini mwake. Lakini baada ya miaka Yakobo alirudi na wake zake na watoto katika nchi ya Kanaani ambamo Esau alikuwa akiishi, na familia zao ziliishi kwa amani zikiwa jirani. Yakobo alikuwa na wana kumi na mbili. Uzao wao ukawa makabila kumi na mbili ya Israeli. Mwanaume tofauti aitwaye Yakobo ameorodheshwa kama baba wa Yusufu katika ukoo wa Mathayo.

Yeftha

Ufafanuzi

Yeftha alikuwa mpiganaji kutoka Gileadi aliyetumika kama mhukumu juu ya Israeli.

Katika Wahebrania 11:32, Yeftha anasifiwa kama kiongozi muhimu aliyewatoa watu wake kutoka kwa maadui zake. Aliwaokoa Waisraeli kutoka kwa wamoabi na kuwaongoza watu wake kuwashinda Waefraimu. Hata hivyo, Yeftha alifanya kiapo cha kipumbavu na haraka kwa Mungu kilichosababisha yeye kumtoa sadaka binti yake.

Yehoramu, Yoramu

Ufafanuzi

Yehoramu lilikuwa jina la wafalme wawili tofauti katika Agano la Kale. Wafalme wote hao wawili walijulikana kama "Yoramu."

Mfalme mmoja Yehoramu alitawala ufalme wa Yuda kwa miaka minane. Alikuwa mwana wa Mfalme Yehoshafati. Huyu ndiye mfalme anayejulikna zaidi kama Yoramu. Mfalme Yehoramu mwingine alitawala ufalme wa Israeli kwa miaka kumi na mbili. Alikuwa mwana wa Mfalme Ahabu. Mfalme Yehoramu wa Yuda alitawala wakati wa manabii Yeremia, Danieli, Obadia, na Ezekieli wakitabiri katika ufalme wa Yuda. Yehoramu pia alitawala kwa muda kiasi wakati baba yake Yehoshafati alipokuwa akitawala Yuda. Tafsiri zingine zinaweza kuchagua kutumia jina "Yehoramu" pale ambapo huyu mfalme wa Israeli anatajwa na "Yoramu" kwa mfalme wa Yuda. Njia nyingine ya kumtambua vizuri kila mmoja ni kuongeza jina la baba yake.

Yehoshafati

Ufafanuzi

Yehoshafati ni jina la angalua watu wawili katika Agano la Kale.

Mtu anayejulikana vizuri zaidi kwa hili jina ni Mfalme Yehoshafati ambaye alikuwa mfalme wa nne kutawala ufalme wa Yuda. Alirejesha amani kati ya Yuda na Israeli, na kuangamiza madhabahu ya miungu wa uongo. Yehoshafati mwingine alikuwa "mtunza kumbukumbu" wa Daudi na Sulemani. Kazi yake ilikuwa pamoja na kuandika nyaraka kwa ajili ya mfalme kusaini na kurekodi historia ya matukio muhumi yaliyotokea katika ufalme.

Yehoyada

Ufafanuzi

Yehoyada alikuwa kuhani aliyemsaidia kumficha na kumlinda mwana wa mfalme Ahazia, Yoashi hadi alipofikisha umri wa kuweza kutangazwa kuwa mfalme.

Yehoyada alimpangia mamia ya walinzi kumlinda Yoashi alipokuwa mdogo wakati akitangazwa kuwa mfalmena watu hekaluni. Yehoyada aliwaongoza watu kuondoa madhabahu yote ya mungu wa uongo Baali. Maisha yake yote yaliyosalia, kuhani Yehoyada alimshauri mfalme Yoashi kwa kumsaidia kumtii Mungu na kuwatawala watu kwa hekima. Mwanamme mwingine aliyeitwa Yehoyada alikuwa baba wa Benaya.

Yehoyakimu

Ufafanuzi

Yehoyakimu alikuwa mfalme muovu aliyetawala ufalme wa Yuda, kuanzia mwaka 608 K.K. Alikuwa mwana wa mfalme Yosia. jina lake mwanzoni lilikuwa Eliakimu.

Farao wa Misri Neko alibadili jina la Eliakimu kuwa Yehoyakimu na kumfanya kuwa mfalme wa Yuda. Neko alimlazimisha Yehoyakimu kulipa kodi ya juu kwa Misri. Yuda ilipovamiwa baadaye na mfalme Nebukadreza, Yehoyakimu alikuwa miongoni mwao wale walikamatwa na kupelekwa Babeli. Yehoyakimu alikuwa mfalme mwovu aliyeingoza Yuda mbali na Yahwe. Nabii Yeremia alitabiri dhidi yake.

Yehu

Ufafanuzi

Yehu lilikuwa jina la wanaume wawili katika Agano la Kale.

Yehu mwana wa Hanani alikuwa nabii wakati wa utawala wa Mfalme Ahabu na Mfalme Yehoshafati wa Yuda. Yehu mwana (uzao) wa Yehoshafati alikuwa jemedari katika jeshi la Israeli ambaye alitiwa mafuta kuwa mfalme kwa amri ya nabii Elisha. Yehu aliua vitu viwili viovu: Mfalme Yoramu wa Israeli na Mfalme Ahazia wa Yuda. Mfalme Yehu pia aliwaua ndugu wote wa mfalme wa zamani Ahabu, na akafanya yule malkia muovu Yezebeli auwawe. Yehu aliaangamiza sehemu zote za kumuabudia Baali ndani ya Samaria na kuwaua manabii wote wa Baali. Mfalme Yehu alimtumikia Mungu mmoja wa kweli, Yahwe, na alikuwa mfalme juu ya Israeli kwa miaka ishiri na nane.

Yeremia

Ufafanuzi

Yeremia alikuwa nabii wa Mungu katika ufalme wa yuda. Kitabu cha Agano la Kale cha Yeremia kina unabii wake.

Kama manabii wengi, Yeremia mara nyingi ilimbidi kuwaonya watu wa Israeli kuwa Mungu atawaadabisha kwa dhambi zao. Yeremia alitabiri kuwa Wababeli wataiteka Yerusalemu, jambo lililowafanya baadhi ya watu wa Yuda kukasirika. Kwa hiyo walimuweka katika kisima kilichokauka na kumuacha humo kufa. Lakini mfalme wa Yuda aliwaamuru watumishi wake kumuokoa Yeremia kutoka katika kisima. Yeremia aliandika kuwa alitamani macho yake yawe "chemchemi ya machozi," kuonesha masikitiko yake makali kuhusu uasi na mateso ya watu wake.

Yeriko

Ufafanuzi

Yeriko ulikuwa mji wenye nguvu katika nchi ya Kanaani. Ulikuwa magharabi mwa mto wa Yordani na kaskazini mwa Bahari ya Chumvi.

Kama Wakanaani wote, watu wa Yeriko waliabudu miungu ya uongo. Yeriko ulikuwa mji wa kwanza katika nchi ya Kanaani ambao Mungu aliwaambia Waisraeli kuuteka. Wakati Yoshua alipowaongoza Waisraeli dhidi ya Yeriko, Mungu alifanya muujiza mkubwa kuwasaidia kuushinda huo mji.

Yeroboamu

Ufafanuzi

Yeroboamu mwana wa Nebati alikuwa mfalme wa kwanza wa ufalme wa kaskazini wa Israeli kati ya 900-910 K.K. Yeroboamu mwingine, mwana wa mfalme Yoashi, alitawala juu ya Israeli karibu miaka 120 baadaye.

Yahwe alimpa Yeroboamu mwana wa Nebati utabiri kwamba atakuwa mfalme baada ya Sulemani na kwamba atayatawala makabila kumi ya Israeli. Sulemani alipokufa, makabila kumi ya kaskazini mwa Israeli yalimkaidi mwana wa Sulemani, Rehoboamu na badala yake walimfanya Yeroboamu kuwa mfalme wao, wakimuacha Rehoboamu kama mfalme wa makabila mawili tu ya kusini, Yuda na Benyamini. Yeroboamu alikuwa mfalme muovu aliyewaongoza watu kutomuabudu Yahwe na badala yake aliweka sanamu kwa ajili yao kuabudu. Waflame wengine wote wa Israeli walifuata mfano wa Yeroboamu na walikuwa wafalme waovu kama yeye alivyokuwa. Karibu miaka 120 baadaye, mfalme mwingine Yeroboamu alianza kutawala ufalme wa kaskazini mwa Israeli. Yeroboamu huyu alikuwa mwana wa Yoashi na alikuwa muovu kama wafalme wengine wote waliopita wa Israeli walivyokuwa. Licha ya haya yote, Mungu alikuwa na huruma juu ya Israeli na kumsaidia huyu mfalme Yeroboamu kuongeza ardhi na kuimarisha mipaka ya eneo lao.

Yerusalemu

Ufafanuzi

Yerusalemu mwanzoni ulikuwa mji wa zamani wa Kikanaani ambao baadaye ulikuwa mji muhimu zaidi katika Israeli. Inapatikana karibu kilomita 34 magharibi mwa Bahari ya Chumvi na kaskazini mwa Bethlehemu. Bado ni mji mkuu wa Israeli ya leo.

Jina "Yerusalemu" imetajwa kwa mara ya kwanza katika kitabu cha Yoshua. Majina mengine ya mji huu katika Agano la Kale ni pamoja na "Salemu", "mji wa Yebusi," na "Sayuni." "Yerusalemu" na "Salemu" zote zina msingi wa "amani" katika maana. Yerusalemu mwanzoni ilikuwa ngome ya Yebusi iitwayo "Sayuni" amabyo mfalme Daudi aliikamata na kuifanya kuwa mji wake mkuu. Mwana wa Daudi Sulemani alijenga hekalu la kwanza Yerusalemu, katika mlima Moria, ambao ulikuwa mlima ambao Abrahamu alimtoa Isaka kama sadaka kwa Mungu. Hekalu lilirudiwa kujengwa hapo baada ya kutetezwa na Wababeli. Kwa sababu hekalu lilikuwa Yerusalemu, sherehe kuu za Kiyahudi ziliadhimishwa huko. Watu kawaida husema kwenda "juu" Yerusalemu kwa sababu palikuwa mlimani.

Yese

Ufafanuzi

Yese Yese alikuwa baba wa mfalme Daudi, na mjukuu wa Ruthu na Boazi.

- Yese alikuwa kutoka kabila la Yuda.
- Alikuwa "Muefrathi," inayomaanisha alikuwa kutoka mji wa Efrathi (Bethlehemu).
- Nabii Isaya alitabiri kuhusu "tawi" ambalo litatoka katika "mzizi wa Yese" na kuzaa matunda. Hii inamaanisha Yesu aliyekuwa uzao wa Yese.

Yethro, Reueli

Ufafanuzi

Majina "Yethro" na "Reueli" yote yanamaanisha baba wa mke wa Musa, Sipora. Kulikuwa kuna watu wawili wengine wenye jina "Reueli" katika Agano la Kale.

Wakati Musa alipokuwa mchungaji katika nchi ya Medani, alimuoa binti wa mwanamme wa Medani aitwaye Reueli. Baadaye Reueli anajulikana kama "Yethro, kuhani wa Medani." Inawezekana kuwa "Reueli" lilikua jina la ukoo. Mungu alipozungumza na Musa kutoka kichaka cha moto, Musa alikuwa akichunga kondoo wa Yethro. Muda mwingine baadaye, baada ya Mungu kuwaokoa Waisraeli kutoka Misri, Yethro alikuja kwa Waisraeli jangwani na kumpa Musa ushauri mzuri kuhusu kuhukumu mambo ya watu. Alimuamini Mungu aliposikia miujiza yote Mungu aliyoifanya kwa watu Waisraeli ndani ya Misri. Mmoja wa wana wa Esau alitwa Reueli. Mwanamme mwingine Reueli anatajwa katika uzao wa Waisraeli aliyerudi kutishi Yuda baada ya kutekwa kwa Babeli kuisha.

Yezebeli

Ufafanuzi

Yezebeli alikuwa mke muovu wa mfalme Ahabu wa Israeli.

Yezebeli alimshawishi Ahabu na Israeli nzima kuabudu sanamu. Pia aliua manabii wengi wa Mungu. Yezebeli alisababisha mtu asiye na hatia aitwaye Nabothi kuuwawa ili Ahabu aibe shamba la mizabibu la Nabothi. Yezebeli hatimaye aliuwawa kutokana na maovu yote aliyotenda. Eliya alitabiri jinsi atakavyokufa na ikatokea hivyo hivyo kama alivyotabiri.

Yezreeli

Ufafanuzi

Yezreeli lilikuwa jina la mji muhimu Israeli katika eneo la kabila la Isakari, lililokuwa kusini magharibi mwa Bahari ya Chumvi.

Mji wa Yezreeli ni moja ya alama za magharibi za uwanda wa Megido, ambayo pia unaitwa "Bonde la Yezreeli." Wafalme kadhaa wa Israeli walikuwa na majumba yao ya utawala katika mji wa Yezreeli. Bustani la mizabibu la Nabothi ilikuwa karibu na nyumba ya mfalme Ahabu ndani ya Yezreeli. Nabii Eliya alitabiri dhidi ya Ahabu huko. Mke muovu wa Ahabu, Yezebeli, aliuwawa Yezreeli. Matukio mengine ya muhimu yalitokea katika mji huu, yakiwemo mapigano kadhaa.

Yoabu

Ufafanuzi

Yoabu alikuwa kiongozi muhimu wa jeshi kwa mfalme Daudi katika utawala wake wote.

Kabla Daudi hajawa mfalme, Yoabu tayari alikuwa mmoja wa wafuasi wake waminifu. Baadaye, wakati wa utawala wa Daudi kama mfalme wa Israeli, Yoabu alikuwa kamanda mkuu wa jeshi la mfalme Daudi. Yoabu alikuwa pia mpwa wa mfalme Daudi kwa kuwa mama yake alikuwa mmoja wa madada zake Daudi. Wakati mwana wa Daudi, Absalomu, alipomsaliti kwa kujaribu kuuchukua ufalme, Yoabu alimuua Absalomu ili kumlinda mfalme. Yoabu alikuwa mpambanaji mwenye hima na aliua watu wengi waliokuwa maadui wa Israeli.

Yoashi

Ufafanuzi

Yoashi lilikuwa jina la watu kadhaa katika Agano la Kale.

Yoashi mmoja alikuwa baba wa mkombozi mmoja wa Israeli, Gideoni. Mwanamme mwingine aliyeitwa Yoashi alikuwa uzao wa mwana wa mwisho wa Yakobo, Benyamini. Yoashi anayejulikanai vizuri zaidi alikuwa mfalme wa Yuda akiwa na umri wa miaka saba. Alikuwa mwana wa Ahazia, mfalme wa Yuda aliyeuwawa. Yoashi alipokuwa mtoto mdogo, shangazi yake alimuokoa kuuliwa kwa kumficha hadi alipokuwa na umri wa kutosha kufanywa mfalme. Mfalme Yoashi alikuwa mfalme mzuri ambaye mwanzoni alimtii Mungu. Ila hakutoa sehemu zilizo inuka na Waisreali wakaanza tena kuabudu sanamu. Mfalme Yoashi alitawala Yuda wakati wa baadhi ya miaka mfalme Yehoashi alipotawala Israeli. Walikuwa wafalme wawili tofauti.

Yoeli

Ufafanuzi

Yoeli ni jina la nabii ambaye inawezekana aliishi wakati wa utawala wa mfalme Yoashi wa Yuda. Kuna watu wengine pia katika Agano la Kale wenye jina Yoeli.

Kitabu cha Yoeli ni moja ya vitabu vifupi vya kinabii katika sehemu ya mwisho ya Agano la Kale. Maelezo pekee tuliyonayo kumhusu nabii Yoeli ni kwamba jina la baba yake ni Pethueli. Katika mahubiri yake ya Pentekoste, mtume Paulo alinukuu kutoka kitabu cha Yoeli.

Yohana (Mbatizaji)

Ufafanuzi

Yohana alikwa mwana wa Zekaria na Elisabeti. Kwa kuwa "Yohana" lilikuwa jina lililozoeleka, mara nyingi huitwa "Yohana Mbatizaji" ili kumtofautisha na watu wengine waitwao Yohana, kama mtume Yohana.

Yohana alikuwa nabii ambaye Mungu alimtuma kuwaanda watu kumuamini na kumfuata Masihi. Yohana aliwaambia watu kutubu dhambi zao, kumgeukia Mungu, na kuacha kutenda dhambi, ili wawe tayari kumpokea Masihi. Yohana alibatiza watu wengi katika maji kama ishara ya kwamba wanatubu dhambi zao na kuziacha. Yohana aliitwa "Yohana Mbatizaji" kwa sababu alibatiza watu wengi. Hakikisha kuwa watu wataelewa kuwa "Mbatizaji" haiimaanishi kanisa kwa hili jina. Inaweza kulazimu kusema, "Yohana aliyebatiza".

Yohana (mtume)

Ufafanuzi

Yohana alikuwa mmoja wa mitume kumi na mbili na rafiki wa karibu wa Yesu.

Yohana na ndugu yake Yakobo walikuwa wana wa mvuvi wa samaki aitwaye Zebedayo. Katika injili aliyoandika kuhusu maisha ya Yesu, Yohana alijieleza kama "mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda." Hii inaonehsa kuwa Yohana alikuwa rafiki wa karibu wa Yesu. Mtume Yohana aliandika vitabu vitano katika Agano Jipya: injili ya Yohana, Ufuno wa Yesu Kristo, na barua tatu zilionadikwa kwa waumini wengine. Noti kuwa mtume Yohana alikuwa mtu tofauti na Yohana mbatizaji.

Yohana Marko

Ufafanuzi

Yohana Marko, pia akijulikana kama "Marko," alikuwa mmoja wa wanaume waliosafiri na Paulo katika safari zake za kimisionari. Inawezekana kuwa yeye ndiye mwandishi wa Injili ya Marko.

Yohana Marko alifuatana na binamu ya Barnaba na Paulo katika safiri yao ya kwanza ya kimisonari. Wakati Paulo alipowekwa gerezani Yerusalemu, waumini walikuwakimuombea katika nyumba ya mama yake Yohana Marko. Marko hakuwa mmoja wa mitume wa awali, lakini alifundishwa na Paulo na Petro na alifanya nao kazi katika huduma.

Yona

Ufafanuzi

Yona alikuwa nabii wa Kihebrania katika Agano la Kale.

Kitabu cha Yona kinaelezea hadithi ya wakati Mungu alipomtuma Yona kuhubiri kwa watu wa Ninawi. Yona alikataa kwenda Ninawi na badala yake akapanda katika meli iliyokuwa inaelekea mji mwingine. Mungu alisababisha dhoruba kali kuilemea meli. Watu waliukuwa wakidafiri katika meli walipogundua kuwa Yona hakuwaanamtii Mungu, walimtupa katika bahari na dhoruba ikakoma. Yona alimezwa na samaki mkubwa na akawa tumboni mwake kwa siku tatu, mchana na usiku. Baada ya hayo, Yona alienda Ninawi na kuwahubiri watu wa huko, na wakaziacha dhambi zao.

Yonathani

Ufafanuzi

Yonathani ni jina la angalau wanaume kumi katika Agano la Kale. Jina linamaanisha "Yahwe ametoa."

Rafiki wa karibu wa Daudi , Yonathani, ndiye anayejulikna zaidi katika Biblia kwa hili jina. Yonathani alikuwa mwana kwanza wa mfalme Sauli. Yonathani wengine waliotajwa katika Agano la Kale ni pamoja na: uzao wa Musa, mpwa wa mfalme Daudi, makuhani kadhaa, akiwemo mwana wa Abiathari; na mwandishi wa Agano la Kale ambaye nyumba yake ilitumika kumfunga nabii Yeremia.

Yoramu

Ufafanuzi

Yoramu mwana wa Ahabu alikuwa mfalme Israeli. Wakati mwingine anajulikana kama "Yehoramu."

Mfalme Yoramu wa Israeli alitawala wakati mmoja kama Yehoramu wa Yuda. Yoramu alikuwa mfalme muovu aliyeabudu miungu ya uongo na kusababisha watu wa Israeli kutenda dhambi. Mfalme Yoramu wa Israeli pia alitawala wakati wa nabii Eliya na Obadia. Mwanamme mwingine aitwaye Yoramu alikua mwana wa mfalme wa Hamathi wakati Daudi ni mfalme.

Yoshua

Ufafanuzi

Kuna Waisraeli kadhaa kwenye Biblia waitwao Yoshua. Anayejulikana zaidi ni Yoshua mwana wa Nuni aliyekuwa msaidizi wa Musa na baadaye kuwa kiongozi muhimu wa watu wa Mungu.

Yoshua alikuwa mmoja wa wapelelezi kumi na mbili amabo Musa aliwatuma tafiti nchi ya ahadi. Pamoja na Kalebu, Yoshua aliwasihi watu wa Israeli watu kutii amri ya Mungu kuingia nchi ya ahadi na kuwashinda Wakanaani. Miaka mingi baadaye, baada ya Musa kufa, Mungu alimchagua Yoshua kuwaongoza watu Waisraeli kwenda nchi ya ahadi. Katika mapambano ya kwanza na maarufu zaidi dhidi ya Wakanaani, Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuuangamiza mji wa Yeriko. Kitabu cha Agano la Kale cha Yoshua kinaelezea jinsi Yoshua alivyowaongoza Waisraeli katika kuichukua mamlaka nchi ya ahadi na jinsi alivyopanga sehemu tofauti za nchi kwa kila kabila la Israeli kuishi. Yoshua mwana wa Yosadaki anatajwa katika vitabu vya Hagai na Zekaria; alikuwa kuhani mkuu aliyesaidia kujenga tena kuta za Yerusalemu. Kuna wanaume kadhaa wengine waitwao Yoshua waliotajwa katika koo na sehemu zingine katika Biblia.

Yosia

Ufafanuzi

Yosia alikuwa mfalme mcha Mungu aliyetawala juu ya ufalme wa Yuda kwa miaka thelathini na moja. Aliwaongoza watu wa Yuda kutubu na kumuabudu Yahwe.

Baada ya baba yake mfalme Amoni kuuwawa, Yosia akawa mfalme juu ya Yuda akiwa na miaka minane. Katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wake, mfalme Yosia alimuamuru kuhani mkuu Hilkia kulijenga tena hekalu la Mungu. Wakati hili likifanyika, vitabu vya Sheria vilipatikana. Vitabu vya Sheria viliposomwa kwa Yosia, alisikitishwa na jinsi watu wake walivyokuwa hawamtii Mungu. Aliamuru kwamba sehemu zote za kuabudia sanamu ziteketezwe na makuhani wa miungu wa uongo wauwawe. Pia aliwaamuru watu kuanza kuadhimisha sherehe ya Pasaka tena.

Yothamu

Ufafanuzi

Katika Agano la Kale kuna wanaume watatu wenye jina Yothamu.

Mwanaume mmoja aitwaye Yothamu alikuwa mwana wa mwisho wa Gideoni. Yothamu alisaidia kumshinda kaka yake mkubwa Abimeleki, ambaye aliwauwa ndugu zake wengine wote. Mwanamme mwingine aitwaye Yothamu alikuwa mfalme juu ya Yuda kwa miaka kumi na sita baada ya kifo cha baba yake Uzia (Azaria). Kama baba yake, Yothamu alimtii Mungu na likuwa mfalme mzuri. Lakini hakuondoa sehemu za kuabudia sanamu na hii ilisababisha watu wa Yuda baadaye kumgeuka Mungu tena.

Yuda

Ufafanuzi

Neno "Yuda" linamaanisha sehemu katika nchi ya Israeli ya zamani. Wakati mwingine linatumika katika maana finyu na wakati mwingine katika maana pana.

Wakati mwingine"Yuda" inatumika katika maana finyu kumaanisha jimbo lililo sehemu ya kusini ya Israeli ya zamani magharibi tu mwa Bahari iliyo Kufa. Wakati mwingine "Yuda" inamaana pana na inamaanisha majimbo yote ya Israeli ya zamani, ikiwemo Galilaya, Samaria, Perea, Edomu na Yuda. Maana pana ya Yuda (mfano. Luka 1:5) inaweza kutafsiriwa kama "nchi ya Yuda" na katika maana finyu (mfano Luka 1:39) inaweza kutafsiriwa kama "jimbo la Yuda" kwa sababu hii ndio sehemu ya nchi ya Israeli ya zamani ambapo kabila la Yuda ya lilikuwepo.

Yuda Iskariote

Ufafanuzi

Yuda Iskariote alikuwa mmoja wa mitume wa Yesu. Alikuwa ndiye aliyemsaliti Yesu kwa viongozi wa Kiyahudi.

Jina "Iskariote" inaweza kumaanisha "kutoka Keriothi", labada kuashiria kuwa Yuda alikulia katika huo mji. Yuda Iskariote alitunza fedha ya mitume na mara kwa mara aliiba kutumia kwa ajili yake. Yuda alimsaliti Yesu kwa kuwaambia viongozi wa dini mahali alipo Yesu ili wamkamate. Baada ya viongozi wa dini kumhukumu Yesu kifo, Yuda alijuta kuwa alimsaliti Yesu kwa hiyo akarudisha fedha ya usaliti kwa viongozi wa Kiyahudi na kisha kujiua. Mtume mwingine pia aliitwa Yuda na alikuwa mmoja wandugu wa Yesu. Kuna wanaume wengi waitwao Yuda katika Biblia, kama vile ndugu yake Yesu na mtume mwingine.

Yuda mwana wa Yakobo

Ufafanuzi

Yuda mwana wa Yakobo alikuwa mmoja wa mitume kumi na mbili wa Yesu. Huyu hakuwa Yuda Iskariote.

Mara nyingi katika Biblia, wanaume wenye majina ya kufanana hutofautishwa kwa kutaja walikuwa wana wa nani. Hapa Yuda anatajwa kama "mwana wa Yakobo." Mwanamme mwingine aitwaye Yuda alikuwa ndugu yake Yesu. Kitabu cha Agano Jipya cha"Yuda" kinawezekana kuwa kimeandikwa na ndugu yake Yesu Yuda, kwa kuwa anajitambulisha kama "ndugu yake Yakobo." Yakobo alikuwa ndugu mwingine wa Yesu. Inawezekana kuwa kitabu cha Yuda kiliandikwa na mwanafunzi wa yesu, Yuda mwana wa Yakobo.

Yuda, ufalme wa Yuda

Ufafanuzi

Kabila la Yuda lilikuwa kubwa zaidi kati ya makabila kumi na mbili ya Israeli. Ufalme wa Yuda uliundwa na makanila ya Yuda na Benyamini.

Baada ya mfalme Sulemani kufa, taifa la Israeli liligawanyika katika falme mbili: Israeli na Yuda. Ufalme wa Yuda ulikuwa ufalme wa kusini, uliokuwa magharabi mwa Bahari ya Chumvi. Mji mkuu wa ufalme wa Yuda ulikuwa Yerusalemu. Wafalme wanane wa Yuda walimtii Yahwe na kuwaongoza watu kumwabudu yeye. Wafalme wengine wa Yuda walikuwa waovu na kuwaongoza watu kuabudu sanamu. Zaidi ya miaka 120 baada ya Ashuru kuishinda Israeli (ufalme wa kaskazini), Yuda ilitekwa na taifa la Babeli. Wababeli waliangamiza mji na hekalu, na kuwachukua watu wengi wa Yuda kwenda Babeli kama watekwa.

Yusufu (Agano Jipya)

Ufafanuzi

Yusufu alikuwa baba wa duniani wa Yesu na kumkuza kama mwanaye. Alikuwa mtu mwenye haki aliyefanya kazi kama seremala.

Yusufu alikuwa amemchumbia binti wa Kiyahudi aitwaye Mariamu, ambaye Mungu alimchagua kuwa mama wa Yesu Masihi. Malaika alimuambia Yusufu kwamba Roho Mtakatifu alimsababisha Mariamu kuwa na mimba, na kwamba mtoto wa Mariamu alikuwa ni mwana wa Mungu. Baada ya Yesu kuzaliwa, malaika alimuonya Yusufu kumpeleka mtoto na Mariamu Misri ili kumtoroka Herode. Yusufu na familia yake waliishi katika mji wa Nazareti ya Galilaya alipojipatia kipato kwa kufanya kazi ya useremala.

Yusufu (Agano la Kale)

Ufafanuzi

Yusufu alikuwa mwana wa kumi na moja wa Yakobo na mwana wa kwanza wa mama yake Raheli.

Yusufu alikuwa mwana kipenzi wa baba yake. Ndugu zake walimuonea wivu na wakamuuza katika utumwa. Wakati akiwa Misri, alisingiziwa na kuwekwa gerezani. Licha ya mateso yake, Yusufu alibaki mwaminifu kwa Mungu. Mungu alimuweka katika nafasi ya pili ya madaraka katika Misri na kumtumia kuwaokoa watu katika kipindi ambapo kulikuwa na chakula kidogo. Watu wa Misri, pamoja na watu wake, waliepusha na njaa.

Zabuloni

Ufafanuzi

Zabuloni alikuwa mwana wa mwisho wa Yakobo na Lea na ni jina la mojawapo wa makabila kumi na mbili ya Israeli

- Waisraeli wa kabila la Zabuloni walikuwa wamepewa nchi magharibi ya Bahari ya Chumvi.
- Wakati mwingine jina "Zabuloni" limetumika pia kurejerea nchi hii ambayo kabila hili la Waisraeli liliishi.

Zakaria

Ufafanuzi

Zakaria alikuwa nabii aliyetabiri wakati wa utawala wa Mfalme Dario I wa Uajemi. Kitabu cha Zakari katika Agano la Kale kina unabii wake, ambacho kinawasihi mateka waliorudi kulijenga tena hekalu.

- Nabii Zakaria aliishi wakati mmoja na Ezra, Nehemia, Zerubabeli na Hagai. Alitajwa na Yesu kama nabii wa mwisho kati ya wale waliouawa katika nyakati za Agano la Kale.
- Mtu mwingine mwenye jina la Zakaria alikuwa bawabu katika hekalu wakati wa Daudi.
- Mmoja wa wana wa Mfalme Yehoshafati aliyeitwa Zakaria aliuliwa na Yehoramu nduguye.
- Zakaria alikuwa kuhani aliyeuawa kwa kupigwa mawe na watu wa Israeli alipowakemea kwa ibada yao ya sanamu.
- Mfalme Zakaria alikuwa mwana wa Yeroboamu na alimiliki juu ya Israeli kwa miezi sita tu kable ya kuuawa.

Zakaria (Agano Jipya)

Ufafanuzi

Katika Agano Jipya, Zakaria alikuwa kuhani wa kiyahudi aliyekuja kumzaa Yohana Mbatizaji.

- Zakari alimpenda Mungu na kumtii.
- Zakari na Elsabethi mkewe waliomba miaka mingi kwa uaminifu ili wapate mtoto lakini hawakupata. Lakini Mungu alijibu maombi yao wakiwa wazee, kwa kuwapa mtoto.
- Zakaria alitabiri kuwa Yohana mwanawe angekuwa nabii ambaye angetangaza na kuandaa njia ya Masiya.

Zakayo

Ufafanuzi

Zakayo alikuwa mtoza ushuru katika mji wa Yeriko aliyepanda katika mti ili aweze kumwona Yesu aliyekuwa amezungukwa na kundi kubwa la watu.

- Zakayo alibadilishwa kabisa alipomwamini Yesu.
- Alitubu dhambi yake ya kuwaibia watu na kuahidi kuwapa masikini nusu ya mali yake.
- Aliahidi pia kwamba angewarudishia mara nne watu aliokuwa amewatoza zaidi.

Zebedayo

Ufafanuzi

Zebedayo alikuwa mvuvi kutoka Galilaya anayejulikana kwa sababu ya wanawe, Yakobo na Yohana, waliokuwa wanafunzi wa Yesu. Hawa wamekuwa wakitajwa katika Agano Jipya kama "wana wa Zebedayo."

- Wana wa Zebedayo walikuwa wavuvi pia na walifanya naye kazi ya kuvua samaki.
- Yakobo na Yohana waliacha kazi yao ya kuvua na Zebedayo baba yao na wakamfuata Yesu.

Zefania

Ufafanuzi

Zefania, mwana wa Kushu, alikuwa nabii aliyeishi Yerusalemu na kutabiri wakati wa utawala wa Mfalme Yosia. Aliishi wakati mmoja na Yeremia.

- Aliwakemea watu wa Yuda kwa kuabudu miungu ya uongo. Unabii wake umeandikwa katika kitabu cha Zefania katika Agano la Kale.
- Kulikuwa na watu kadhaa katika Agano la Kale wenye jina Zefania, wengi wao wakiwa makuhani.

Zerubabeli

Ufafanuzi

Zerubabeli lilikuwa jina la Waisraeli wawili katika Agano la Kale.

- Mmoja wao alikuwa mzao wa Yehoyakimu na Sedakia.
- Zerubabeli mwingine, mwana wa Shealitieli, alikuwa kiongozi wa kabila la Yuda wakati wa Ezra na Nehemia, Koreshi mfalme wa Uajemi alipowaacha huru Waisraeli kutoka katika utumwa wao huko Babeli.
- Zerubabeli na Yoshua kuhani mkuu walikuwa miongoni mwa waliohusika kujenga upya hekalu na madhabahu ya Mungu.

translationWords

Other

Adui

Ufafanuzi

"Adui" ni mtu au kundi lililo kinyume na mtu au kitu fulani.

- Adui ni mtu ambaye anajaribu kukupinga au kukudhuru.
- Taifa linaweza kuitwa adui linapopigana na taifa jingine.
- Kwenye Biblia Ibilisi ni adui.

agano jipya

Ufafanuzi

Neno "agano jipya" la husu kujitolea au makubaliano Mungu aliyo fanya na watu wake kupitia dhabihu ya Mwanae, Yesu.

- "agano jipya" la Mungu linaelezwa sehemu ya Biblia itwayo "Agano Jipya"
- Hili agano jipya ni kinyume na lile la "kale" au "zamani" ambalo Mungu alifanya na Waisraeli katika Agano la Kale.
- Agano jipya ni bora kuliko la kale kwasababu lina husu dhabihu ya Yesu, lilo patanisha dhambi za watu milele.
- Mungu ana andika agano jipya ndani ya mioyo ya waamini wa Yesu. Hii ina sababisha wao kutii Mungu na kuishi maisha matakatifu.
- Agano jipya litatimia siku za mwisho ambapo Mungu ataweka utawala wake duniani.

agizo

Ufafanuzi

Agizo ni sharti au sheria ya hadhara inayo toa amri au maelekezo ya watu kufuata. Hili neno lina maana sawa na "kisimika"

- Wakati mwingine agizo ni pokeo lilo imarishwa kwa miaka ya kulifanyia zoezi.
- Katika Biblia, agizo lilikuwa kitu ambacho Mungu aliamuru Waisraeli kufanya. Wakati mwingine aliwaamuru kufanya milele.

Ahadi

Ufafanuzi

"Ahadi" hii ni ya kuweka matumaini ya kufanya kitu au kutoa kitu.

- Katika agano la kale viongozi wa Israeli waliweka ahadi ya kuwa waaminifu kwa mfalme Daudi.
- Kitu kitakachotolewa kama ahadi kitarudishwa kwa mmiliki wake muda ambao ahadi hiyo itatimizwa.
- Ahadi pia yaweza kutafsiriwa kama "kufanya rasmi" au "kuahidi kwa nguvu."
- Pia ahadi yaweza kuwa kifaa kinachotolewa kama ahadi kwamba deni litalipwa.

aibisha, ya kuaibisha

Ufafanuzi

Msemo wa "aibisha" una maana ya kufanya kitu ambacho si cha heshima kwa mtu. Hii inaweza pia kumsababishia mtu huyo aibu au fedheha.

Msemo "ya kuaibisha" inaelezea tendo ambalo ni la aibu au litasababisha mtu kupungukiwa na sifa.

Mara nyingine "kuabisha" inatumika kumaanisha vyombo ambavyo havina kazi kwa jambo lolote muhimu.

Watoto wanaamuriwa kuwaheshimu na kuwatii wazazi wao. Pale ambapo watoto hawatii, wanakuwa hawaheshimu wazazi wao. Wanawafanya wazazi wao kwa njia ambayo haiwapi heshima kwao.

Waisraeli walipunguza sifa kwa Yahwe walipoabudu miungu ya uongo na kutenda mwenendo muovu.

Wayahudi hawakumheshimu Yesu kwa kusema ya kwamba alikuwa amepagawa na pepo.

Hii inaweza kutafsiriwa kama "kutoheshimu" au "kutenda bila heshima.

Nomino ya "kutoheshimu" inaweza kutafsiriwa kama "kutoheshimu" au "kupotea kwa sifa".

Kutegemea na muktadha, "ya kuaibisha" inaweza kutafsiriwa kama "siyo na heshima" au "ya aibu" au "haifai" au "haina thamani".

aibu, fedhehesha

Ufafanuzi

Msemo "aibu" una maana ya kupotea kwa utukufu na heshima.

Mtu anapofanya jambo la dhambi, inaweza kumsababisha awe katika hali ya aibu au kupoteza heshima.

Msemo "fedhehesha" unatumika kuelezea tendo la dhambi au mtu aliyeifanya..

Mara nyingine mtu anayefanya mambo mema anatendewa kwa njia ambayo inamsababishia mtu fedheha au aibu.

Kwa mfano, Yesu alipouwawa msalabani, hii ilikuwa njia ya fedheha kufa. Yesu hakufanya jambo lolote baya kustahili fedheha hii.

Njia za kutafsiri "fedheha" zinaweza kujumuisha "aibu" au "kutokuwa na heshima.

Njia za kutafsiri "fedhehesha" zinaweza kujumuisha "aibu" au kutokuwa na heshima.

aina

Ufafanuzi

Neno "aina" linamaanisha makundi ya vitu vilivyoungana kwa kugawana tabia.

Katika Biblia, usemi huu unatumika bayana kumaanisha aina tofauti za mimea na wanyama ambao Mungu alivyotengeza alipoumba ulimwengu. Mara nyingi kuna tofauti nyingi za spishi katika kila "aina." Kwa mfano, farasi, punda milia, na punda zote ni sehemu ya "aina" moja lakini ni spishi tofauti. Kitu kikuu kinachotofautisha kila "aina" kama kundi tofauti ni kwamba kila mmoja wa hilo kundi anaweza kuzaa zaidi wa "aina" hiyo. Viumbe wa aina tofauti hawawezi kufanya hivyo pamoja.

Amani

Ufafanuzi

Amani ni kitendo cha kutokuwa na migogoro au hofu. Mtu mwenye amani anahisi shwari na ana uhakika wa kuwa salama.

- Amani pia inaweza kuelezewa kama kipindi ambacho kundi la watu au nchi hawapo katika vita na watu wengine. Watu hawa wanasemwa kuwa na "mahusiano ya amani.
- "Kutengeneza amani" na watu au kundi la watu linamaanisha kuchukua hatua ya kusababisha ugonvi uishe.
- "mtengeneza amani" ni mtu anayefanya kitu au kusema kitu ili kuwashawishi watu waishi kwa amani na watu wengine.
- Kuwa na amani na watu wengine inamaanisha kuwa katika hali ya kutogombana na watu hao.
- Uhusiano mzuri kati ya Mungu na wanadamu hutokea pale ambapo Mungu aliwaokoa watu toka kwenye dhambi zao. Hii inaitwa kuwa na amani na Mungu.
- Salamu "neema na amani" ilitumiwa na mitume katika barua zao kwa waamini aka baraka.
- Amani pia inaweza kuonesha kuwa katika mahusiano mazuri na watu wengine au na Mungu.

amri

Ufafanuzi

Amri ni sheria maalumu iliyo andikwa inayo toa muongozo watu kuishi.

- Neno "amri" ni swa na "agizo" au "tamko" au "sheria."
- Mfalme Daudi alisema alifurahia amri za Yahweh.
- Neno "amri" la weza tafsiriwa "amri maalumu" au "tamko maalum."

Amri kumi

Ufafanuzi

"Amri Kumi" zilikuwa amri ambazo Mungu alimpa Musa Mlima Sinai wakati Waisraeli waliishi jangwani wakiwa njiani kwenda nchi ya Kanani. Mungu aliandika hizi amri kwenye mawe makubwa mawili.

- Mungu aliwapa Waisraeli amri nyingi za kutii, lakini Amri Kumi zilikuwa maalumu kuwasaidia Waisraeli kumpenda na kumuabudu Mungu na kupenda watu wengine.
- Hizi amri pia zilikuwa sehemu ya agano la Mungu na watu wake. Kwa kumtii Mungu na aliyo waamuru kufanya, watu wa Israeli walionyesha kuwa wana mpenda Mungu na kuwa ni wao.
- Amri kwenye mawe zilihifadhiwa katika Agano lililo kuwa pa takatifu zaidi mwa maskani na baadae, hekalu.

Angalia, Mlinzi

Ufafanuzi

"Angalia" inamaanisha kuwa kutazama kitu kwa ukaribu na kwa makini. "Mlinzi" ni mtu ambaye kazi yake ni kuulinda mji kwa kuangalia kwa makini vyote vinavyomzunguka kama kuna hatari yoyote kwa watu wa mji ule.

- Amri ya "angalia maisha yako na mafundisho kwa makini" inamaanisha kuwa ishi kwa makini na usiamini mafundisho ya uongo.
- "Angalia" ni onyo la kuwa makini ili kukwepa hatari au ushawishi wa hatari.
- "Angalia" inamaana ya kuwa makini dhidi ya dhambi na uovu.
- Neno lingine la mlinzi ni mlindaji.

angika au nyonga

Ufafanuzi

Neno hili nyonga au angika lina maana ya ninginiza au tundika kitu au mtu. kifo cha kunyongwa au kujinyonga hufanyika kwa kutumia kamba ambayo mtu humfungwa shingoni na kumning'niza kwa kitu kilicho juu kama vile mti. Yuda alijiua mwenyewe kwa kujinyonga. Kifo cha Yesu kwa kuangikwa kwenye msalaba wa mbao kilifanyika kwa utofauti: askari walimtundika Yesu kwa kumpigilia misumali miguuni na mikononi katika msalaba. kuangika au kunyonga mtu mara zote ni njia ya kumwua mtu kwa kumnyonga kwa kutumia kamba inayofungwa shingoni mwa mtu.

Asali, sega la asali

Ufafanuzi

Asali ni kimiminika kitamu kinachotengenezwa na nyuki kutokana na maua. Sega ni fremu ya nta ambayo nyuki hutumia kutunzia asali. Asali inaweza kuwa na rangi ya njano au kikahawia kutegemea na aina. Asali yaweza kupatikana mstuni hasa katika mashimo ya miti au mahali popote ambapo nyuki zaweza kuweka makao. Watu pia hutunza asali katika mizinga ili kuzalisha asali za kula au kuuza, lakini huenda asali inayotajwa kwenye Biblia ni asali ya msituni. Biblia inawataja watu watatu walioishi kwa kula asali, watu hawa ni Yonathani, Samsoni na Yohana Mbatizaji. Neno hili 'asali' hutumika pia kimfano kumaanisha kitu kitamu au kitu cha kustarehesha. Mfano, Maneno na sheria za Mungu husemwa kuwa ni tamu sana kuliko asali. Wakati mwingine maneno ya mtu yanaweza kusemwa kuwa ni matamu kama asali, lakini matokeo yake huwa ni udanganyifu na kuwaumiza watu wengine.

asiye amini, kuto amini

Ufafanuzi

Neno "kuto amini" la eleza kuto kuwa na imani ya kitu au mtu.

- Katika Biblia, "kuto amini" kwa eleza kuto mwamini au kuto mtegemea Yesu kama mwokozi mmoja.
- Mtu asiye mwamini Yesu anaitwa "asiye amini."

Balozi, mwakilishi

Ufafanuzi

Balozi ni mtu aliyechaguliwa rasmi kuwakilisha nchi yake katika mataifa ya kigeni. Mara nyingine hutafsiriwa kama mwakilishi.

- Balozi au mwakilishi huwapa watu ujumbe aliopewa na mtu au serikali iliyomtuma.
- "Mwakilishi" ni yule aliyepewa mamlaka ya kufanya au kuzungumza kwa niaba ya yule anayemwakilisha.
- Mtume Paulo anawafundisha Wakristo kuwa ni mabalozi wa Kristo au wawakilishi kwa kuwa wanamwakilisha Kristo duniani na kuwafundisha wengine ujumbe huu.

barua, waraka

Ufafanuzi

Barua ni ujumbe wa kuandikwa unaotumwa kwa mtu au kundi la watu ambaokwaida wako mbali kutoka kwa mwandishi. Waraka ni barua maalum, mara nyingi huandikwa kwa njia rasmi, kwa kusudi maalum, kama kufundisha.

Katika nyakati za Agano Jipya, waraka na aina zingine za barua ziliandikwa kwenye kartasi zilizotengenezwa kwa ngozi ya wanyama au kwenye karatasi za mafunjo ilitengenezwa kutoka kwenye ufumwele wa mimea. Nyaraka za Agano Jipya kutoka kwa Paulo, Yohana, Yakobo, Yuda na Petro ni barua za maelekezo walizoandika kuwatia moyo, kuwasihi, na kuwafundishia Wakristo wa kwanza katika miji tofauti katika ufalme wa Rumi. Njia za kutafsiri hili neno ni pamoja na, "ujumbe wa kuandikwa" au " maneno yalioandikwa" au "maandishi."

Bibi harusi

Ufafanuzi

Bibi harusi ni mwanamke ambaye katika sherehe ya harusi anaolewa kwa mmewe, ambaye ni bwana harusi.

- Neno "bibi harusi" linatumika kama sitiari kwa wanaomwanini Yesu, Kanisa.
- Kwa sitiari Yesu anaitwa "bwana harusi" kwa ajili ya Kanisa.

Bikira

Ufafanuzi

Bikira ni mwanamke ambaye hajawahi kuwa na mahusiano ya ngono.

- Nabii Isaya alisema kuwa Masihi atazaliwa na bikira.
- Mariamu alikuwa Bikira alipokuwa na mimba ya Yesu. Yesu hakuwa na baba wa kibinadamu.
- Lugha nyingine zaweza kuwa na neno zuri badala ya neno bikira.

Bure, ubatili

Ufafanuzi

Neno "bure" linaelezea kitu ambacho hakina maana au hakifai. Vitu vilivyo bure ni vitu tupu au vitu visivyo na maana.

- Ubatili ni kitu ambacho hakifai au kipo tupu. Pia yaweza kuwa na maana ya kiburi au madaha.
- Katika agano la kale sanamu zilielezewa kama vitu vya bure visivyoweza kuokoa au kukomboa. Havina kazi wala maana.
- Kama kitu kilifanywa pasipo na maana hata matokeo yake sio mazuri.
- Kuamini katika kitu kilicho tupu na maana ni kuamini katika kitu kisicho cha kweli na kinachokupa matumaini ya uongo.

Busara

Ufafanuzi

Neno "busara" humuelezea mtu anayefikiri kwa makini kuhusu matendo yake na kufanya maamuzi ya hekima.

- Busara ni uwezo wa kufanya maamuzi ya hekuma kuhusu mambo ya kimwili kama matumizi mauri ya pesa au mali.
- Japokuwa busara ya hekuma vina maana sawa lakini hekima ni kwa ujumla zaidi na imelenga hasa mambo ya kiroho.

Busu

Ufafanuzi

Busu ni tendo ambalo mtu mmoja anaweka mdomo wake juu ya mdomo wa mwingine au uso. Msemo huu unaweza pia kutumika kitamathali.

Tamaduni zingine hubusiana kwenye shavu kama ishara ya salamu au kuaga. Busu linaweza kupitisha ujumbe wa upendo mkubwa kati ya watu wawili, kama mme na mke. Usemi "kumbusu mtu kwaheri" inamaanisha kumuagamtu kwa busu. Wakati mwingine neno "busu" linatumika kumaanisha "kusema kwaheri kwa." Wakati Elisha aliposema kwa Eliya, "Niache niende kumbusu baba na mama yangu," alitaka kuwaaga wazazi wake kabla yakuwaacha na kumfuata Eliya.

Bwana

Ufafanuzi

Neno "Bwana" linamaanisha mtu anayemiliki na mwenye mamlaka juu ya watu wengine. Inapokuwa na herufi kubwa, ni jina linalomaanisha Mungu. (Noti hata hivyo inapotumika kama njia ya kumtambua mtu mwanzo mwa sentesi inaweza kuwa na herufi kubwa na kuwa na maana ya "mkuu.")

Katika Agano la Kale, msemo huu pia unatumika maneno kama, "Bwana Mungu Mkuu" au "Bwana Yahwe" au "Yahwe Bwana wetu." Katika Agano Jipya, mitume walitumia neno hili katika misemo kama, "Bwana Yesu" na "Bwana Yesu Kristo," illiyoonyesha kuwa Yesu ni Mungu. Neno "Bwana" katika Agano Jipya pia linatumika peke yake kama njia ya moja kwa moja ya kumtambua Mungu, hasa katika nukuu za kutoka Agano la Kale. Kwa mfano, maandishi ya Agano la Kale ya, "Amebarikiwa ajaye kwa jina la Yahwe" na Agano Jipya lina, "Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana." Katika ULB na UDB, jina "Bwana" linatumika tu kutafsiri maneno halisi ya Kihebrania na Kigriki yanayomaanisha "Bwana." Halitumiki kama tafsiri ya jina la Mungu (Yahwe), kama inavyofanywa na tafsiri zingine.

Bwana harusi

Ufafanuzi

Bwana harusi ni mtu anayemwoa bibi arusi katika sherehe ya harusi.

- Katika utamaduni wa Kiyahudi nyakati za Biblia, sherehe iliwekwa siku ambayo bwana arusi alikuja kumchukua bibi harusi wake.
- Katika Biblia, kwa kutumia tamathari ya semi, Yesu anaitwa "Bwana harusi" atakayetuijia siku moja "Bibi harusi wake," kanisa.
- Yesu aliwafananisha thenashara na rafiki za Bwana harusi wanaosherehekea bwana harusi anapokuwa pamoja nao, lakini wanahuzunika anapoondoka.

chafu

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "chafu" utumika kama fumbo kueleza vitu ambavyo Mungu alitangaza sio sahihi kwa watu wake kugusa,kula, au kutoa dhabihu.

- Mungu aliwapa Waisraeli maelekezo kuhusu mnyama yupi alikuwa "msafi" na yupi alikuwa "mchafu." Wanyama wachafu hawakuruhusiwa kutumika kula au kutolea dhabihu.
- Watu wenye aina fulani ya ugonjwa wa ngozi walisemekana kuwa "wachafu" mpaka walipo ponywa.
- Waisraeli kama walipo shika kitu "kichafu" wao wenyewe walihesabika kuwa wachafu kwa kipindi cha muda fulani.
- Kutii amri za Mungu kuhusu kutogusa au kula vitu vichafu kuliwatenga Waisraeli kwa huduma ya Mungu.
- Hii hali ya uchafu wa mwili na mila ilikuwa ishara ya uchafu wa kijamii.
- Maana nyingine ya fumbo, "roho chafu" ina eleza pepo.

chemchem, kisima

Ufafanuzi

Msemo wa "chemchem" na "kisima" mara kwa mara una maana ya kiasi kikubwa cha maji ambacho kinatiririka kiasili kutoka kwenye ardhi.

Maneno haya yanatumika kitamathali katika Biblia kumaanisha baraka inayotiririka kutoka kwa Mungu au kumaanisha kitu ambacho kinasafisha au kutakasa.

Katika muda wa sasa, chemchem mara nyingi ni chombo kilichoundwa na mtu ambacho kina maji yakitiririka kutoka kwake, kama vile chemchem ya maji ya kunywa. Hakikisha ya kwamba tafsiri ya msemo huu una maana ya chanzo cha asili ya maji yanayotiririka.

Fananisha tafsiri ya msemo huu na jinsi msemo "mafuriko" unavyotafsiriwa.

chinja, chinjwa

Ufafanuzi

Neno "chinja" lina maana ya kuua mtu au mnyama. Mara nyingi ina maana ya kuua kwa vita au vurugu.

- Neno "ua" la weza pia tumika kutafsiri hili neno.
- Maneno "waliyo chinjwa" ya weza pia tumika kutafsiri "watu waliyo chinjwa" au "watu waliyo uawa."

Chochea

Ufafanuzi

Neno "kuchochea" linamaanisha kumsababisha mtu apate hisia hasi.

- Kumchochea mtu kwenye hasira inamaanisha kufanya kitu kitakachosababisha mtu huyo apate hasira. Hii inaweza kutafsiriwa kama "kumsababishia mtu apate hasira."
- Unapokutana na maneno kama "usimchochee " maneno haya yaweza kutafsiriwa kama "usimsababishie hasira."

chui

Ufafanuzi

Chui ni mnyama pori mkubwa kama paka, mwenye rangi ya kahawa na madoa meusi.

Chui ni aina ya mnyama anayeshika wanyama wengine na kuwala. Katika Biblia, ughafla wa maafa unalinganishwa na chui anaye shambulia mawindo yake ghafla. Nabii Danieli na mtume Yohana wanazungumzia maono ambayo waliona mnyama aliyefanana na chui.

chukiza, chukia

Ufafanuzi

Msemo "chukiza" unaelezea jambo ambalo linapaswa kutopendwa na kukataliwa. "Kuchukia" kitu ina maan ya kutokipenda kabisa.

Mara nyingi Biblia huzungumzia kuhusu kuchukia uovu. Hii ina maana kuchukia uovu na kuukataa.

Mungu alitumia neno "chukiza" kuelezea matendo maovu ya wale waliomwabudu miungu ya uongo.

Waisraeli waliamriwa "kuchukia" matendo ya dhambi, na kinyume na maadili ambayo baadhi ya makundi ya watu majirani waliyafanya.

Mungu aliyataja matendo yote ya uasherati kuwa "chukizo".

Uaguzi, uchawi, na sadaka za mtoto yote yalikuwa "chukizo" kwa Mungu.

Msemo "chukizo" unaweza kutafsiriwa kama "uovu mbaya" au "inayochukiza" au "inayostahili kukataliwa".

Inapotumika na kiumbe takatifu "chukizo kwa" waovu, hii inaweza kutafsiriwa kama "kuchukuliwa kutotamanika kwa" au "kutokuwa na ladha" au "kukataliwa na"

Mungu aliwaambia Waisraeli "kuchukia" aina kadhaa ya wanyama ambao Mungu alitamka kuwa "wachafu" na kutofaa kwa chakula. Hii inaweza kutafsiriwa kama "kuchukia kwa uzito" au "kukataa" au "kuchukua kama kutokubalika".

dada

Ufafanuzi

Dada ni mtu wa jinsi ya kike anaye shiriki wastani wa mzazi mmoja na mtu mwingine.

- Katika Agano Jipya, "dada" linatumika kimafumbo kumuelezea mwanamke aliye mwamini katika Yesu Kristo.
- Wakati mwingine neno, "kaka na dada" linatumika kueleza waamini wote katika Kristo, wanaume na wanawake.
- Katika cha Agano la kale cha, Nyimbo iliyo Bora, "dada" ina maana ya mpenzi.

desturi

Ufafanuzi

Neno "desturi" la eleza tamaduni na mapokeo yaliyo tunzwa kwa muda na yanayo pokelewa na vizazi vijavyo.

- Mara nyingi katika Biblia neno "desturi" la eleza mafundisho na mapokea watu waliyo fanya, sio amri za Mungu. Misemo "desturi za wanadamu" au "desturi za binadamu" inaeleza vizuri hii maana.
- Maneno kama "desturi za wazee" au "desturi za baba zangu" ya maanisha tamaduni za Wayahudi na mapokeo viongozi wa kiyahudi kwa muda mrefu waliyo ongeza katika sheria ya Mungu kwa Waisraeli kupitia Musa. Ingawaje hizi desturi hazikutoka kwa Mungu, watu walidhani wana paswa kutii kuwa wenye haki.
- Mtume Paulo pia utumia "desturi" katika maana tofauti kueleza mafundisho kuhusu mapokeo ya Kikristo yaliyo toka kwa Mungu na yeye na mitume wengine walifundisha waamini wapya.

dhabihu, sadaka

Ufafanuzi

Katika Biblia, maneno "dhabihu" na "sadaka" ya husu zawadi maalumu anazopewa Mungu kama kitendo cha kumuabudu. Watu pia walitoa sadaka kwa miungu ya uongo.

- Neno "sadaka" la husu chochote kinacho tolewa au kupewa. Neno "dhabihu" la husu kitu kinacho tolewa au kufanywa kwa gharama kubwa kwa mtoaji.
- Sadaka kwa Mungu zilikuwa vitu maalumu alizo waamuru Waisraeli kutoa ili kuonyesha upendo na utii kwake.
- Maneno ya sadaka tofauti, kama "sadaka ya kuteketeza" na "sadaka ya amani," ili hashiria aina gani ya sadaka ilitolewa.
- Dhabihu kwa Mungu kulihusisha kuua mnyama.
- Dhabihu peke yake ya Yesu, Mwana mkamilifu, asiye na dhambi, wa Mungu, anaweza kutakasa watu na dhambi. Mnyama hakuweza kufanya hivyo.
- Mfano wa msemo "jitoeni kama dhabihu hai" ina maana, "ishi maisha yako kwa kumtii Mungu, kuacha kila kitu ili kuweza kumtumikia.

dhahabu

Ufafanuzi

Dhahabu ni chuma cha manjano, cha ubora wa juu sana kinachotumika kutengeneza vito na vyombo vya dini. Ilikuwa chuma ya thamani zaidi katika kipindi cha zamani.

Katika kipindi cha Biblia, aina nyingi tofauti ya vyombo vilitengezwa kwa dhahabu ngumu au kufunikwa na safu nyembamba ya dhahabu.

Vyombo hivi vilijumuisha heleni na vito vingine, sanamu, madhabahu, na vyombo vingine vilivyotumika katika tabenakulo au hekalu, kama vile sanduku la agano.

Katika Agano la Kale, dhahabu ilitumika kama njia ya kubadilishana katika kununua na kuuza. Ilipimwa juu ya mizani kupata thamani yake.

Baadaye, dhahabu na vyuma vingine kama vile fedha vilitumika kutengeneza sarafu kutumiwa kununua na kuuza.

Pale inapomaanisha kitu ambacho sio dhahabu ngumu, lakini ina safu nyembamba tu ya dhahabu, msemo "ya dhahabu" au "kufunikwa kwa dhahabu" inaweza kutumika.

Mara nyingi chombo kinaelezewa kama "rangi ya dhahabu" ambayo ina maana ina rangi ya njano ya dhahabu, lakini haijatengenezwa kwa dhahabu.

dhalimu, kwa dhalimu, udhalimu

Ufafanuzi

Maneno "dhalimu" na "kwa dhalimu" yanaeleza kutendea watu pasipo haki, na mara nyingi, namna ya kudhuru.

- "Udhalimu" ni kitu kibaya kinacho fanywa kwa mtu asiye stahili. Inaeleza kufanyia watu pasipo haki.
- Udhalimu pia una maana kuwa watu wengine wana tendewa vibaya wakati wengine wanatendewa vizuri.
- Mtu anaye tenda kwa namna dhalimu ana kuwa na "upendeleo" au "ubaguzi" kwasababu hawatendei watu sawa.

Dharau, kudharauliwa

Ufafanuzi

Dharau ni kitendo cha kutokuheshimu kinachooneshwa kwa mtu au kitu. Kitu kisichoheshimiwa kinaitwa kilichodharauliwa.

- Mtu au tabia ambayo inaonesha kutokumuheshimu Mungu inaitwa kudharau.
- Kushikilia katika dharau inamaanisha kumuona mtu kama asiye na thamani au kumuhukumu mtu kwa kumuona hana thamani.
- Mfalme Daudi alipotenda dhambi ya uzingi na kuua Mungu alimwambia kuwa Daudi ameonesha "dharau" kwa Mungu. Hii inamaanisha kuwa amemdharau Mungu kwa kufanya hivyo.

Dhifa

Ufafanuzi

Dhifa ni sherehe maalumu ya mlo ambayo kwa kawaida inahusisha aina tofauti ya vyakula.

- Katika nyakati za kale, wafalme mara kwa mara waliandaa dhifa kuwaburudisha viongozi wa kisiasa na wageni wengine mhimu.
- Hii yaweza pia kutafasiriwa kama, "mlo maalumu" au "sherehe mhimu" au "mlo wa mchanganyiko"

dhihaki

Ufafanuzi

Neno kudhihaki ni kumtania mtu, kwa namna mbaya.

- Kudhihaki mara kadha kuna husisha muingiza maneno ya watu au matendo kwa kusudi kuwaaibisha au kuonyesha kuchukizwa nao.
- Wanajeshi wa Kirumi walidhihaki Yesu walipo mvalisha joho na kujifanya kumheshimu kama mfalme.
- Kikundi cha vijana walimdhihaki Elisha walipo muita jina, wakimtania kichwa chake cha upara.

dhiki

Ufafanuzi

Neno "dhiki" la husu kipindi cha ugumu, mateso, na msongo wa mawazo.

- Agano Jipya lina sema kwamba Wakristo watavumilia kipindi cha mateso na dhiki tofauti kwasababu watu wengi ulimwenguni wana fahamu mafundisho ya Yesu.
- Biblia inatumia neno "Dhiki kuu" kueleza kipindi cha Muda kabla ya Yesu kurudi mara ya pili amabapo gadhabu ya Mungu itamwaga duniani kwa miaka kadhaa.
- Neno "dhiki" la weza tafsiriwa kama, "kipindi cha mateso sana" au "hali ngumu"

Divai, kiriba, divai mpya

Ufafanuzi

Katika nyakati za Biblia "divai" ni kinywaji kilichotengenezwa na maji ya matunda yanayoitwa zabibu. Divai ilihifadhiwa kwenye viriba ambayo ni vyombo vilivyotengenezwa kwa ngozi ya wanyama.

- Divai mpya ni maji ya zabibu ambayo hayajatolewa bado kwenye zabibu.
- Kutengeneza divai zabibu hupondwa kwenye shinikizo na maji ya zabibu hutoka ndani yake. Maji haya huchachushwa na kuleo hutoka ndani yake.
- Katika nyakati za Biblia divai kilikuwa kinywaji cha kawaida kikiambatana na mlo. Haikuwa na kilevi sana kama divai za wakati huu.
- Kabla divai haijawekwa kwa ajili ya kutumika ilichanganywa na maji.
- Viriba vilivyochakaa vilikuwa vimepasuka na kuruhusu divai kuvuja. Lakini viriba vupya havikuvuja na vilihifadhi divai vizuri.

Dubu

Ufafanuzi

Dubu ni mnyama mkali mkubwa mwenye miguu minne na ana manyoa meusi, meno na makucha makali. Dubu walikuwa wamezoeleka katika Israeli nyakati za Biblia.

- Wanyama hawa wanaishi misituni na katika maeneo ya milimani; wanakula samaki, wadudu, na mimea.
- Katika Agano la Kale, dubu hutumika kama alama ya nguvu.
- Wakati akichucha kondoo, Daudi kama mchungaji alipambana na dubu na kumshinda.
- Dubu wawili walitoka msituni na kulishambulia kundi la vijana waliomdhihaki nabii Elisha.

dunia, kidunia

Ufafanuzi

Msemo "dunia" una maana ya dunia ambayo wanadamu wanaishi, pamoja na kila aina ya viumbe hai.

"Dunia" pia inaweza kumaanisha ardhi au udongo ambayo hufunika nchi.

Msemo huu mara kwa mara hutumika kitamathali kumaanisha watu wanaoishi juu ya dunia.

Misemo, "acha dunia iwe na furaha" na "Atahukumu dunia" ni mifano ya matumizi ya tamathali ya msemo huu.

Msemo "kidunia" mara kwa mara humaanisha vitu vya kimwili kinyume na vitu vya kiroho.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo ambao lugha ya taifa hutumia kumaanisha sayari ya dunia ambayo tunaishi.

Kulingana na muktadha, "dunia" pia inaweza kutafsiriwa kama, "ulimwengu" au "ardhi" au "udongo".

Unapotumika kitamathali, "dunia" inaweza kutafsiriwa kama, "watu wa dunia" au "watu wanaoishi juu ya dunia" au "kila kitu juu ya dunia".

Njia za kutafsiri "kidunia" zinaweza kujumuisha, "kimwili" au "vitu vya dunia hii" au "vinavyoonekana".

elekeza, maelekezo

Ufafanuzi

Usemi "elekeza" na "maelekezo" yanamaanisha kutoka uongozo bayana ya nini cha kufanya.

"Kutoa maelekezo" inamaanisha kumuambia mtu bayana kitu anachotakiwa kufanya. Yesu alipowapa wanafunzi wake mikate na samaki kuwapa watu, aliwapa maelekezo bayana ya jinsi ya kuifanya. Kulingana na mazingira, neno "elekeza" inaweza kutafsiriwa kama "kumuambia" au "kuongoza" au "kufundisha" au "kutoa maelekezo kwa." Neno "maelekezo" inaweza kutafsiriwa kama "uongozo" au"ufafanuzi" au "kitu alichokuambia kufanya." Mungu akikupa maelekezo, huu usemi wakati mwingine unatafsiriwa kama "kuamuru" au "kuamrisha."

erevu

Ufafanuzi

Neno "erevu" la elezea mtu enye akili na mahiri, hususani katika mambo ya utendaji.

- Mara kadhaa "erevu" lina maana hasi kwa sehemu tangu linatumika kuonyesha ubinafsi.
- Mtu erevu mara nyingi anaji tazama yeye, sio wengine.

fagia

Ufafanuzi

Neno "fagia" mara nyingi ueleza maana pana, ya kuondoa kwa haraka uchafu kwa kutumia ufagio.

- Neno "fagia" linatumika kifumbo kueleza jinsi jeshi linavyo shambulia kwa wepesi, umakini.
- Kwa mfano, Isaya alitabiri kuwa wa Assiria wata "fagia" Ufalme wa Yuda. Hii ina maana wa haribu Yuda na kukamata watu wake.
- Neno "fagia" lina weza kuleza maji yanayo tiririka ya navyo sukuma vitu na kuondoa.

fahamu, ufahamu

Ufafanuzi

Neno "fahamu" lina maana ya kusikia ua kupokea taarifa na kuelewa ina maana gani.

- Neno "ufahamu" lina weza eleza "maarifa" au "hekima" au kutambua jinsi ya kufanya kitu.
- Kumfahamu mtu inaweza maanisha kujua jinsi huyo mtu ana jihisije.
- Wakati wakutembea kwenye njia ya Emao, Yesu alisababisha kufahamu maana ya maandiko kuhusu Mesiya.
- Kulingana na muktadha, neno "fahamu" la weza tafsiriwa kama "jua" au "amini" au "elewa" au "jua nini kitu kinavyo maanisha."
- Mara nyingi neno "ufahamu" la weza tafsiriwa kama "maarifa" au "hekima" au "upeo."

Faida

Ufafanuzi

Kwa ujumla "faida" ni kitendo cha kupata kitu kizuri kwa kufanya jambo fulani au kitu fulani kizuri ambacho mtu anakipata. Kitu kina faida kwa mtu ikiwa kinaleta mambo mazuri au kinasaidia kuleta mambo mazuri kwa watu wengine.

- Mara nyingi faida inamaanisha pesa inayopatikana baada ya kufanya biashara. Biashara ina faida ikiwa inaongeza pesa zaidi ya zilizotumika.
- Matendo yana faida ikiwa yanasababisha mambo mazuri kwa watu.
- 2 Timotheo 3:16 maandiko yanazungumza kuwa kuna faida ya kumsahihisha mtu au kumfundisha mtu katika haki. Hii inamaanisha kuwa mafundisho ya Biblia yana faida na yanasaidia kufundisha watu kuishi sawasawa na mapenzi ya Mungu.

familia

Ufafanuzi

Msemo "familia" una maana ya kundi la watu ambao wana uhusiano wa damu na mara nyingi hujumuisha baba, mama, na watoto wao. Mara kwa mara pia hujumuisha ndugu wengine kama babu na bibi, wajukuu, wajomba na shangazi.

Familia ya Kiebrania ilikuwa jamii ya kidini inayopitisha utamaduni kupitia ibaada na maagizo.

Mara kwa mara baba alikuwa mwenye mamlaka ya familia.

Familia pia inaweza kujumuisha watumishi, masuria, na hata wageni.

Baadhi ya lugha zina neno pana kama vile "ukoo" au "nyumba" ambayo litafaa zaidi kwa muktadha ambapo zaidi ya wazazi na watoto wanatajwa.

Msemo "familia" pia unatumika kumaanisha watu ambao wana uhusiano wa kiroho, watu kama hawa ambao ni sehemu ya familia ya Mungu kwa sababu wanmwamini Yesu.

Faraja, mfariji

Ufafanuzi

Faraja ni kumsaidia mtu anayeteseka kimwili au kihisia.

- Mtu anayefariji anaitwa mfariji.
- Katika agano la kale faraja imetumika kuelezea namna ambavyo Mungu anavyowajali na kuwapenda watu wake na kuwasaidia wanapoteseka.
- Katika agano jipya inasema kuwa Mungu atawafariji watu wake kwa kupitia roho mtakatifu. Wale waliopokea faraja wanauwezo wa kutoa faraja kwa wanaoteseka.
- "Mfariji wa Israeli" ni Masihi aliyekuja kuwaokoa watu wake.
- Yesu anamuelezea roho mtakatifu kama mfariji anayewasaidia wanaomwamini Yesu.

Farasi

Ufafanuzi

Farasi ni mnyama mkubwa mwenye miguu minne ambaye katika kipindi cha Biblia alitumiak katika kufanya kazi za shambani na katika usafirishaji. Baadhi ya farasi walitumika katika kuvuta gari, na wengine walipandwa na mpanda farasi binafsi. Farasi walivalishwa hatamu katika vichwa vyao ili waweze kuongozwa Katika Biblia, farasi walihesabiwa kama mali ya thamani, na kipimo cha utajiri, hasa hasa kwa ajili ya matumizi yake katika vita. Wanyama walikuwa wanafanana na farasi ni punda.

fedha

Ufafanuzi

Fedha ya ng'aa, ni ya chuma ya kijivu inayo tumika kufanya sarafu, mikufu, vyombo, na mapambo.

- Vyombo ni pamoja na vikombe vya fedha na mabakuli, miongoni mwa vitu vingine vinavyo tumika kupikia, kulia, au kutumikia.
- Fedha na dhahabu vilitumika kujenga maskani na hekalu.
- Kipindi cha Biblia, sarafu za fedha na fedha nzito zilizo itwa shekeli zilitumika.
- Kaka yake Yusufu alimuuza kama mtumwa kwa shekeli ishirini za fedha.
- Yuda alilipwa sarafu thelathini za fedha kumsaliti Yesu.

fedhehesha. fedheha

Ufafanuzi

Neno 'fedhehesha' lina maana ya kumfanya mtu aaibike au adhalilike. Hii ni kwasababu mara kwa mara hufanyika hadharani. Tendo la kumwaibisha mtu huitwa " fedheha." KIpindi ambacho Mungu humshusha mtu, humaanisha kwamba Mungu humfanya mtu apate mambo mabaya ili kumsaidia mtu aachane na kiburi. Hii ni tofauti na kumdhalilisha mtu, maana fedheha ni kitendo ambacho hufanywa ili kumuumiza mtu. Kumfedhehesha mtu yaweza kutafsiriwa kama 'kumwaibisha' au kumdhalilisha mtu. kuna njia nyingi za kutafsiri neno 'fedheha' kwa kutegemea na Muktadha. Maneno kama 'udhalilishaji' na aibu,''

filimbi, zumari

Ufafanuzi

Katika kipindi cha Biblia, zumari ilikuwa vyombo vya muziki iliyotengenezwa kwa mfupa au mbao na mashimo inayoruhusu sauti kutoka nje. Filimbi ilikuwa aina ya zumari.

Zumari nyingi ilikuwa na matete yaliyotengenezwa kutoka kwa nyasi nene ambayo hutikisika pale hewa inapopulizwa kwake.

Zumari bila matete mara kwa mara ilijulikana kama "filimbi".

Mfugaji alicheza filimbi kutuliza mifugo yao ya kondoo.

Zumari na filimbi ilitumika kucheza muziki wa huzuni na furaha.

Fimbo

Ufafanuzi

Fimbo hiki ni kifaa chembamba kama fimbo kinachotumika kwa njia mbali mbali.

- Fimbo ya mbao inatumiwa na mchungaji kuwalinda kondoo dhidi ya wanyama wengine. Pia kwa ajili ya kumrejesho katika kundi kondoo anayetangatanga.
- Katika Zaburi ya 23 mfalme Daudi anatumia maneno fimbo na gongo kuelezea mwongozo wa Mungu na nidhamu kwa watu wake.
- Fimbo ya mchungaji pia ilitumika kuhesabia mifugo.
- Pia fimbo ya chuma inaelezea adhabu ya Mungu kwa watu wanaomuasi na kufanya mambo maovu.
- Hapo kale fimbo za kupimia zilizotengenezwa kwa chuma au mbao zilitumika kupimia urefu wa majengo.
- Katika Biblia fimbo ya chuma inaelezea kifaa cha kumfundishia adabu mtoto.

fimbo ya kifalme

Ufafanuzi

Neno "fimbo ya kifalme" ina husu gongo zuri linalo shikiliwa na mtawala, kama mfalme.

- Fimbo hizi zilikuwa tawi la mbao lenye mapindo ya mapambo. Baadae fimbo za kifalme zilitengenezwa kwa vyuma vya dhahabu.
- Fimbo ya kifalme ilikuwa alama ya ufalme na mamlaka iliyo hashiria heshima na ukuu wa mfalme.
- Katika Agano la Kale, Mungu anaelezwa kuwa na fimbo ya haki. Hii ina husu Mungu kutawala kama mfalme wa watu wake.
- Unabii wa Agano la Kale kuhusu Mesiya unamueleza kuwa kama mfano wa fimbo ambayo itakuja kutoka Israeli kutawala mataifa yote.
- Hii yaweza tafsiriwa kama, "gongo la utawala" au "gongo la mfalme."

fundisha, kufundisha, mwalimu, fundishwa

Ufafanuzi

Haya maneno "fundisha" na "kufundisha" yanaeleza kuambia watu wengine taarifa wasiyo ijua kabla. Mara nyingi maelezo utolewa rasmi au kwa utaratibu.

- "mwalimu" ni mtu anaye fundisha. Kitenzi kilicho pita cha "fundisha" ni "fundishwa."
- Yesu alipo kuwa ana fundisha, alikuwa anaeleza vitu kuhusu Mungu na ufalme wake.
- Wanafunzi wa Yesu walimuita "Mwalimu" kama heshima ya mtu aliye wafundisha kuhusu Mungu.
- Taarifa inayo fundishwa yaweza onyeshwa au kuelezwa.
- Neno "mafundisho" inaeleza baadhi ya mafunzo kutoka kwa Mungu kuhusu yeye pamoja na maelekezo ya jinsi ya kuishi.
- Maneno "kile ulicho fundishwa" yaweza tafsiriwa kama, "kile watu walicho kufundisha" au "Mungu alicho kufundisha," kulingana na muktadha.

funga

Ufafanuzi

Msemo "funga" una maana ya kufunga kitu kuzunguka kitu kingine. Mara kwa mara humaanisha kutumia mkanda kuzunguka kiuno kuweka kanzu au gwanda mahali pake.

Msemo wa kibliblia unaojulikana, "funga kiuno" una maana ya kuchomekea chini ya vazi ndani ya mkanda kuruhusu mtu kusogea kwa uhuru zaidi, mara nyingi kufanya kazi.

Msemo una maana ya kujiweka tayari kufanya kazi au kujiandaa kufanya kitu kigumu.

Msemo "funga kiuno" unaweza kutafsiriwa kutumia msemo katika lugha husika yenye maana moja. Au inaweza kutafsiriwa bila tamathali kama "jiandae kwa ajili ya tukio" au "jiandae"

Msemo "kufngwa na" inaweza kutafsiriwa kama "kuzungushwa na" au "kufungwa na".

Furaha

Ufafanuzi

"Furaha" ni jambo ambalo linamfurahisha mtu sana na kuleta furaha kubwa.

"Kufurahishwa" na jambo ina maana ya "kuwa na furaha" au "kufurahia juu ya" kitu.

Pale ambapo kitu kinakubalika sana au kupendeza kinasemekana kama "furahisha".

Kama furaha ya mtu ipo katika kitu ina maana ya kwamba anakifurahia sana.

Msemo wa, "furaha yangu ipo katika sheria ya Yahwe" inaweza kutafsiriwa kama, "sheria ya Yahwe inanipa furaha kubwa" au "Ninapenda kutii sheria za Yahwe" au "Nina furaha kutii amri za Yahwe".

Misemo "kufurahia" na "kuwa na furaha katika" inaweza kutafsiriwa kama "sifurahishwi kabisa na" au "sina furaha juu ya".

Msemo "kufurahishwa mwenyewe na" ina maana, "anafurahia kufanya" kitu au "ana furaha sana juu ya" kitu au mtu.

Msemo "hufurahia" una maana ya vitu ambavyo mtu hufurahia. Hii inaweza kutafsiriwa kama "starehe" au "vitu vinavyoleta furaha".

Msemo kama wa, "Ninafurahi kufanya mapenzi yako" unaweza kutafsiriwa kama, "Ninafurahi kufanya mapenzi yako" au "Nina furaha sana ninapokutii".

furaha, mwenye furaha

Ufafanuzi

Furaha ni hisia ya kupendezwa au kuridhika inayotoka kwa Mungu. Maana inayokaribiana, "mwenye furaha" inaelezea mtu anayejisikia vizuri sana na mwenye furaha nyingi.

Mtu anasikia furaha anapokua anahisi kuwa anachopitia ni chema sana. Mungu ndiye anayegawa furaha ya kweli kwa watu. Kuwa na furaha hakutegemei hali nzuri. Mungu anaweza kuwapa watu furaha hata kama vitu vigumu kabisa vinatokea katika maisha yao. Sehemu zingine zinaelezwa kama za furaha, kama nyumba na miji. Hii inamaanisha kuwa watu waiishio humo ni wenye furaha.

furahia sana, mwenye furaha

Ufafanuzi

Msemo "furahia sana" na "mwenye furaha" una maana ya kuwa na shangwe sana kwa sababu ya mafanikio au baraka maalumu.

"Kufurahia sana" kunajumuisha hisia za kushangilia jambo zuri.

Mtu anaweza kufurahia sana ndani ya wema wa Mungu.

Msemo "mwenye furaha" unaweza kujumuisha kuwa na kiburi ndani ya hisia za furaha juu ya mafanikio au utajiri.

Msemo "furaha sana" unaweza kutafsiriwa kama "kushangilia kwa furaha" au "kusifu na furaha kubwa".

Kulingana na muktadha, msemo "mwenye furaha" unaweza kutafsiriwa kama "kusifu kwa kishindo" au "kushangilia na sifaf binafsi" au "kiburi"

fuvu

Ufafanuzi

Neno "fuvu" la eleza kichwa cha mifupa kisicho na nyama cha mtu au mnyama

Gari

Ufafanuzi

Zamani za kale magari yalikuwa mepesi, yenye matairi mawili yalioendeshwa na farasi.

- Watu walikaa au kusimama katika magari, waliyatumia katika vita au safari.
- Katika vita jeshi lenye magari lilikuwa na faida ya kuwa na kasi na uwezo juu ya jeshi ambalo halikuwa na magari.
- Katika nyakati za Wamisri na Rumi walijulikana sana kwa kutumia farasi na magari.

gavana, kutawala, mtawala, serikali

Ufafanuzi

"Gavana" ni mtu anayetawala mkoa, eneo au mahali. Neno "kutawala" lina maana ya koungoza au kusimamia watu.

Msemo "mtawala" ilikuwa jina mahususi kwa gavana aliyetawala juu ya mkoa wa Kirumi.

Katika kipindi cha Biblia, magavana waliteuliwa na mfalme au mfalme mkuu na walikuwa chini ya mamlaka yake.

"Serikali" inaundwa na viongozi wote ambao wanatawala nchi au ufalme fulani. Watawala hawa hutengeza sheria ambazo huongoza tabia ya wanachi il kwamba kuwepo na amani, ulinzi, na mafanikio kwa watu wato wa taifa hilo.

Gereza, mfungwa , jela

Ufafanuzi

Gereza nisehemu ambayo wahalifu huwekwa kama adhabu kwa uhalifu waliofanya. Mfungwa ni mtu anayewekwa gerezani.

- Mtu anaweza kuwekwa gerezani akiwa anasubiria hukumu ya kesi.
- Neno "kufungwa" inamaanisha "kuwekwa gerezani" au "kuwekwa kifungoni."
- Manabii wengi na watumishi wengine wa Mungu waliwekwa gerezani japokuwa hawakufanya jambo lolote baya.

geuka, geuka kando, geuka nyuma

Ufafanuzi

"Kugeuka" kuna maana ya kubadili mwelekeo wa mwili au kusababisha kitu kingine kubadilisha muelekeo.

- Neno "geuka" pia la weza "kugeuka nyuma" kuangalia nyuma au kuelekea mwelekeo mwingine.
- "Kugeuka nyuma" au "geuka mbali" kuna maana ya "kurudi nyuma" au "kwenda mbali" au "kusababisha kwenda mbali."
- "Kugeuka mbali na" ina weza maanisha "kusimama" kutofanya kitu au kumkataa mtu.
- "kugeuka kuelekea" mtu ina maana ya kumuangalia huyo mtu.
- "Kugeuka na kuondoka" au "kugeuza mgongo wake kwa kuondoka" ina maana ya "kwenda mbali."
- "Kugeuka na kurudia" ina maana ya "kuanza kufanya kitu tena."
- "Kugeuka mbali kutoka" ina maana ya "kuacha kufanya kitu."

Ghadhabu

Ufafanuzi

Ghadhabu ni hasira iliyopitiliza isiyoweza kuzuilika. Mtu anapokuwa na ghadhabu inamaana mtu anaonesha hasira yenye uharibifu.

- Ghadhabu inatokea pale ambapo hasira inashindwa kuzuiliwa.
- Unapotawaliwa na adhabu waweza kufanya au kutenda jambo lenye kuharibu.
- Mataifa yenye hasira ni watu wasiomtii Mungu na kuasi dhidi yake.
- Kujazwa na gahadhabu ni kuwa na hasira iliyopitiliza.

Giza

Ufafanuzi

Msemo "giza" una maana ya kutokuwepo kwa nuru. Kuna maana kadhaa za kitamathali za msemo huu:

Kama sitiari, "giza" ina maana ya "uchafu" au "uovu" au "upofu wa kiroho".

Pia ina maana ya jambo lolote linalohusu dhambi au uharibifu wa maadili.

Msemo, "mamlaka ya giza" una maana ya kila kilicho kiovu na kinachotawaliwa na Shetani.

Msemo "giza" unaweza pia kutumika kama sitiari ya kifo.

Watu wasiomjua Mungu wanasemekana kuwa "wanaishi gizani", ambayo ina maana hawaelewi au hawatenda haki.

Mungu ni nuru (utakatifu) na giza (uovu) haliwezi kushinda nuru hiyo.

Mahali pa adhabu kwa wale wanaomkataa Mungu mara nyingi hujulikana kama "giza la nje".

Mapendekezo ya Tafsiri

Ni bora kutafsiri msemo huu kihalisia, kwa neno la lugha ya mradi ambalo lina maanisha kutokuwepo kwa nuru. Huu unaweza kuwa msemo wenye maana ya giza la chumba ambalo halina mwanga au wakati wa siku ambapo hakuna mwanga.

Kwa matumizi ya kitamathali, ni muhimu kuweka picha ya giza kwa kutofautisha na mwanga, kama njia ya kuelezea uovu na udanganyifu kulinganisha na wema na ukweli.

Kutegemea na muktadha, njia zingine za kutafsiri hili zaweza kuwa, "giza la usiku"

gongo

Ufafanuzi

Ngo ni fimbo ndefu ya mbao, utumika kama fimbo ya kutembelea.

- Yakabo alipokuwa mzee, alitumia bakora kumsaidia kutembea.
- Mungu aligeuza gongo la Musa kuwa nyoka kuonyesha nguvu yake kwa Farao.
- Wachungaji pia walitumia gongo kusaidia kuongoza kondoo zao, au kuokoa kondoo walipo anguka au kupotea.
- Gongo la mchungaji lilikuwa na kishikio mwisho, kilicho kuwa tofauti na bakora ya mchungaji, lililo kuwa wima na lilitumika kuua wanyama waliyo jaribu kushambulia kondoo.

gumia

Ufafanuzi

Msemo "gumia" una maana ya kutoa sauti ya chini, nzito ambayo inasababishwa na mateso ya kihisia au kimwili. Mara kwa mara gumia hutengenezwa bila maneno.

Mtu anaweza kugumia kwa sababu ya kuhisi majonzi.

Kugumia inaweza kusababishwa kwa kujisikia vibaya, mzigo wa kundamiza.

Njia zingine za kutafsiri "gumia" zinaweza kujumuisha "kutoa sauti ya chini ya maumivu" au "kulia kwa kulalamika".

Kama nomino, hii inaweza kutafsiriwa kama "kilio cha chini cha mateso" au "mnung'uniko wa chini wa maumivu"

hakimu

Ufafanuzi

Hakimu ni mtu anayeamua nini kiko sawa au la ukiwepo ugomvi kati ya watu, mara nyingi katika mambo yanayofungamana na sheria.

Katika Biblia, Mungu mara nyingi anatajwa kama hakimu kwa sababu yeye ndiye hakimu aliye kamili anayefanya maamuzi ya mwisho kuhusu nini kiko sawa au kisicho sawa. Baada ya watu wa Israeli kuingia nchi ya Kanaani na kabla hawajawa na wafalme wa kuwatawala, Mungu aliwapa viongozi waitwao "waamuzi" kuwaongoza nyakati za shida. Mara nyingi waamuzi hao walikuwa viongozi wa kijeshi waliowaokoa Waisraeli kwa kuwaangamiza maadui zao. Neno "hakimu" linaweza pia kuitwa "muamuzi" au "kiongozi" au "mkombozi" au "gavana," kutegemea na mazingira.

halali, ipasavyo, kinyume na sheria

Ufafanuzi

Msemo "halali" unamaanisha kitu kinachoruhusiwa kufanywa kulingana na sheria au mahitaji mengine. Kinyume cha hiki ni "kinyume na sheria" inyomaanisha "sio halali."

Katika Biblia, kama kitu kinasemwa kuwa "halali" inamaanisha inaruhusiwa na sheria ya kimaadili ya Mungu, au kwa sheria ya Musa au sheria zingine za Kiyahudi. Kitu ambacho "sio halali" "hakiruhusiwi" na sheria hizo. Kufanya kitu "ipasavyo" inamaanisha kuifanya "sawa" au "katika njia sahihi." Mambo mengi Wayahudi waliyoona ni halali au sio halali hayakuwa kwenye makubaliano na sheria za Mungu kuhusu kuwapenda wengine. Kulinga na mazingira, njia za kuafsiri "halali" ni pamoja na, "kuruhusu" au "kulingana na sheria ya Mungu" au "kufuatana na sheria zetu" au "sawa" au inafaa." Msemo "Je ni halali" inaweza pia kutafsiriwa kama "Je, sheria zetu zinaruhusu" au "Hilo ni jambo ambalo sheria zetu zinaruhusu?"

hali ya chini, kuwa chini

Ufafanuzi

Misemo "wa hali ya chini" na "kuwa chini" inamaanisha kuwa maskini auna hadhi ya chini. Usemi huu pia unaweza kuwa na maana ya kuwa mnyenyekevu.

Yesu alijinyenyekesha hadi nafasi ya chini ya kuwa binadamu na kuwatumikia wengine. Kuzaliwa kwake kulikuwa kwa hali ya chini kwa sababu alizaliwa mahali ambapo wanyama walitunzwa; sio katika nyumba ya kifalme. Kuwa na mtazamo wa chini ni kinyume na kuwa na majivuno. Njia za kutafsiri "hali ya chini" ni pamoja na , "unyenyekevu" au "hadhi ya chini" au "kutokua muhimu." Msemo "kuwa chini" unaweza pia kutafsiriwa kama "unyenyekevu" au "umuhimu mdogo."

Halmashauri

Ufafanuzi

Halmashauri ni kundi la watu wanaokutana kujadili, kutoa ushauri na kufanya maamuzi juu ya masuala ya muhimu.

- Halmashauri huratibiwa kwa namna maalumu kwa ajili ya lengo fulani kwa mfano kufanya maamuzi juu ya masuala ya kisheria.
- "Halmashauri ya kiyahudi" katika Yerusalemu inayojulikana kama "Baraza" lilikuwa na wajumbe 70 wakiwemo viongozi wa kiyahudi, kuhani mkuu, waandishi, mafarisayo na masadukayo waliokusanyika mara kwa mara kuamua mambo ya sheria za Kiyahudi. Halmashauri hii ya viongozi wa dini iliyomuweka Yesu kwenye mashtaka na kuamua auawe.
- Pia kulikuwa na halmashauri ndogo za Kiyahudi katika miji mingine.
- Mtume Paulo alipelekwa mbele ya halmashauri ya Rumi alipokamatwa akihubiri injili.

Hamira, Chachu

Ufafanuzi

"Chachu" ni neno la jumla la kitu kinachosababisha unga wa mkate kuumuka. "Hamira" ni aina ya chachu.

- Katika kafsiri nyingine za Kiingereza neno chachu linatafsiriwa kama "hamira" ambayo hufanya unga wa mkate kujaa kabla ya kuoka.
- Katika nyakati za agano la kale chachu ilitengenezwa kwa kuruhusu unga kukaa kwa mda.
- Waisraeli walipotoroka Misri hawakuwa na muda wa kusubiria unga wa mkate ujae hivyo walitengeneza mkate usiokuwa na chachu na kuondoka nao. Kwa kumbukumbu hii kila mwaka Wayahudi hufanya sherehe kusherehekea sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu.
- Pia chachu au hamira imetumika kwenye Biblia kama lugha ya picha kuelezea namna ambavyo dhambi inasambaa katika maisha ya watu au namna ambavyo dhambi inaweza kumchochea mtu mwingine.
- Pia inaweza kuwa na maana ya mafundisho ya uongo ambayo husaambaa kwa watu wengi.
- Pia chachu inaweza kutumika kwa namna hasi ikielezea namna ambavyo ushawishi wa ufalme wa Mungu unasambaa toka kwa mtu kwenda kwa mtu.

Hasira

Ufafanuzi

"Kukasirika" au "kupata hasira" ina maana ya kutofurahishwa au kuhangaishwa juu ya jambo fulani au mtu fulani.

- Watu wanapokasirika ni dhambi na ubinafsi lakini wakati mwingine kuna hasira ya haki dhidi ya udhalimu au mateso.
- Hasira ya Mungu inaelezea namna ambavyo hapendezwi na dhambi.
- "kuwatia hasira" maana yake ni "kuwasababisha wakasirike"

hati

Ufafanuzi

Zamani za kale, hati ilikuwa aina ya kitabu kilicho tengenezwa kwa karatasi ndefu ya mafunjo au ngozi.

- Baada ya kuandika kwenye hati au kusoma, watu waliviringisha kwa kutumia ufito kwenye miisho.
- Hati zilitumika kwa ajili ya nyaraka na maandiko.
- Wakati wingine hati zilizo tolewa na mjumbe zilifungwa kwa nta. Hii inazuia mtu ye yote kufungua hati na kuandika.
- Hati zilizo kuwa na maandiko ya Kiebrania zilisomwa kwa sauti katika masinagogi.

haya, aibu

Ufafanuzi

Neno "haya" la husu hali ya maumivu ya kuumizwa kihisia kwa kuaibishwa kwasababu ya kitu cha fedheha ambacho yeye au mtu mwingine amefanya.

- Neno "kuona haya" la eleza jinsi mtu anavyo jisikia wakati amefanya kitu cha aibu.
- Maneno "acha aibike" yana maana ya kushinda watu au kuweka wazi dhambi zao ili wajione haya.
- Nabii Isaya alisema kwamba wao wanao fanya na kuabudu sanamu wataaibishwa.
- Mungu anaweza leta aibu kwa mtu asiye tubu, kwa kudhihirisha dhambi na kusababisha kuaibika.

hema

Ufafanuzi

Hema ni hifadhi linalo hama lililo tengenezwa na uzi uliyo zungushiwa kwenye nguzo pamoja.

- Mahema yanaweza kuwa madogo, yenye kiasi cha nafasi cha watu kulala humo, au yanaweza kuwa makubwa, yenye nafasi ya familia nzima kulala, kupika, na kuishi.
- Kwa watu wengi, mahema yanatumika kama sehemu ya kudumu ya kuishi. Kwa mfano, wakati wa muda mwingi familia ya Ibrahimu iliishi katika nchi ya Kanani, waliishi katika mahema makubwa yaliyo tengenezwa na nywele za mbuzi.
- Waisraeli pia waliishi katika mahema kipindi cha miaka yao arobaini wakizunguka jangwa la Sinai.
- Jengo la maskani lilikuwa aina ya hema kubwa, yenye kuta nene zilizo tengenezwa na vitambaa.
- Wakati mtume Paulo alipo safiri miji tofauti kueneza injili, alifanya mahema kupata pesa kujikimu.
- Wakati mwingine neno "hema" linaweza tumika kifumbo kueleza wapi watu wanaishi.

hema la kukutania

Ufafanuzi

Neno "hema la kukutania" la husu hema ambalo lilikuwa la muda mfupi Mungu alipo kutana na Musa kabla ya maskani kujengwa.

- Hema la kukutania lilikuwa nje ya kambi ya Waisraeli.
- Wakati Musa alipoenda kwenye hema ya kukutania kukutana na Mungu, nguzo ya wingu ilisimama katika mwingilio wa hema kama ishara ya uwepo wa Mungu hapo.
- Baada ya Waisraeli kujenga maskani, hema ya muda mfupi haiku hitajika tena na neno "hema la kukutania" lilitumika kueleza maskani.

Heshima

Ufafanuzi

Heshima ni hisia za kumuheshimu mtu au kitu kwa hali ya juu.

- Hisia za heshima zinaweza kuonekana kwa vitendo vinavyompa heshima mtu anayepokea.
- Hofu ya Mungu ni heshima ya ndani inayojionesha yenyewe katika utii wa amri za Mungu.

hudumu, huduma

Ufafanuzi

Neno "hudumu" lina maana kufanya vitu kusaidia watu wengine. Linaweza pia maanisha "kuabudu."

- Katika muktadha wa mwanamke anatumikia wageni wake, hili neno lina maana "kujali" au "kutoa chakula" au "kutoa chakula kwa ajili."
- Wakati Yesu alipo waambia wanafunzi kuhudumia watu na samaki, lina weza tafsiriwa kama "kusambaza" au "toa kwa ajili ya" au "kumpa yeye"
- Neno "huduma" lina husu tendo la kuhudumu. Linaweza pia tumika kumanisha "mkutano" wa Wakristo wanapo mtumikia Mungu kwa pamoja.
- Neno "hudumu" laweza tafsiriwa kama, "muhudumia" au "kumfanyia kazi" au "kujali" au "kutii," kulingana na muktadha.
- "Kumtumikia Mungu" yaweza tafsiriwa kama "kumuabudu na kumtii Mungu" au "kufanya kazi Mungu aliyo amuru."
- "Kutumikia meza" ina maana ya kuleta chakula kwa watu waliyo keti mezani.
- Watu wanao fundisha wengine kuhusu Mungu anaelezwa kuwa ni wanamtumikia Mungu na wale wanao wafundisha.
- Mtume Paulo aliandika kwa wa Kristo wa Korintho jinsi walivyo "hudumia" Agano la Kale. Hii ina maana ya kutii sheria ya Musa.
- Sasa wana "hudumia" agano jipya, ambalo ni, kwasababu ya dhabihu ya Yesu msalabani, waamini katika Yesu wanawezeshwa na Roho Mtakatifu kumpendeza Mungu na kuishi maisha matakatifu.

huru, uhuru

Ufafanuzi

Msemo "huru" au "uhuru" una maana ya kutokuwa katika utumwa au aina yoyote ya kifungo.

Msemo "kumweka mtu huru" au "kumweka huru mtu" ina maana ya kutoa njia kwa mtu ili asiwe katika utumwa au kifungo.

Katika Biblia, misemo hii mara kwa mara hutumika kitamathali kumaanisha jinsi gani muamini katika Yesu hayupo chini ya nguvu ya dhambi.

Kuwa "huru" au "uhuru" inaweza kumaanisha kutohitajika kutii Sheria ya Musa, lakini badala yake kuwa huru kuishi kwa mafunzo na uongozi wa Roho Mtakatifu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "huru" unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo ambao una maana ya "kutofungwa" au "kutokuwa katika utumwa" au "kutokuwa katika kifungo".

Msemo "ukuru" unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo ambao una maana, "hali ya kuwa huru" au "hali ya kutokuwa mtumwa" au "kutofungwa".

Msemo "kuweka huru" unaweza kutafsiriwa kama "kusababisha kuwa huru" au "kukomboa mtu kutoka utumwani" au "kumwachia kutoka kifungoni".

Mtu ambaye "amewekwa huru" atakauwa "ameachiliwa" au "kutolewa kutoka" katika kifungo au utumwa.

iga, mwigaji

Ufafanuzi

Maneno "iga" na "mwigaji" yanamaanisha kumuiga mtu mwingine na kuigiza sawa na mtu huyu afanyavyo.

Wakristo wanafundishwa kumuiga Yesu Kristo kwa kumtii Mungu na kuwapenda wengine, kama Yesu alivyofanya. Mtume Paulo aliliambia kanisa la awali kumuiga yeye, kama yeye alivyomuiga Yesu.

Ikulu

Ufafanuzi

Neno "ikulu" linamaanisha jengo au nyumba ambayo mfalme aliishi pamoja na familia yake na watumishi wake.

- Kuhani mkuu pia aliishi katika ikulu kama ilivyotajwa katika agano jipya.
- Ikulu ilikuwa imepambwa sana kwa usanifu na vifaa vizuri.
- Majengo na vifaa vya ikulu vilitengenezwa kwa mawe na mbao na mara nyingi vilikuwa vinashikiliwa na mbao za thamani, dhahabu na ndovu.
- Watu wengi pia walikuwa wakiishi na kufanya kazi katika ikulu ambayo ilijumuisha majengo kadhaa na uwanja.

Imeandikwa

Ufafanuzi

maneno haya "Kama ilivyoandikwa" au "kilichoandikwa" yametokea mara nyingi katika agano jipya na yameelezea amri au unabii ulioandikwa katika maandiko ya Kiebrania.

- Pia "kama ilivyoandikwa"m inamaanisha maneno yaliyoandikwa katika sheria ya Musa.
- Mara nyingine ni nukuu toka kwa moja wa manabii walioandika katika agano la kale.
- Yaweza kutafsiriwa kama "kama ilivyoandikwa katika sheria ya Musa" au "kama manabii walivyoandika zamani."

inua, inuka

Ufafanuzi

Inua, inua juu inamaana ya kuinua kitu juu au kukuweka juu.

- Kuinua juu ni kusababisha kitu kionekane. Pia yaweza kuwa kumteua mtu afanye kitu fulani.
- "Inua" ina maan ya pekee katika "kuinuka toka kwenye kifo" ikiwa inamaanisha kusababisha mtu aliyekufa aishi tena.
- Mara nyingine "kuinua juu" inamaana ya "kupandisha" kitu au mtu.
- Mtu anapoinuka kwenda mahali fulani inamaana kuwa amenyanyuka na kwenda.
- Yesu alitabiri kuwa atainuka toka kwa wafu . Baada ya siku tatu malaika akasema "ameinuka"

jamaa wa karibu

Ufafanuzi

Usemi "jamaa wa karibu" unamaanisha ndugu wa damu wa mtu. Mara nyingi neno hili hutumika zaidi kumaanisha ndugu wa kiume.

Usemi huu unaweza kumaanisha ndugu wa karibu, kama vile mzazi au kaka, au kwa ndugu wa mbali zaidi, kama vile shangazi, mjomba au binamu. Katika Israeli ya zamani, kama mwanamme akifa, ndugu yake wa karibu wa kiume alitarajiwa kumuoa mjane wake, kutunza mali zake, na kusaidia kulibeba jina la familia yake. Ndugu huyu alikuwa anaitwa "jamaa mkombozi." Usemi unaweza pia kutafsiriwa kama, "ndugu" au "mwana familia."

jangwa, njika

Ufafanuzi

jangwa, au nyika, ni sehemu iliyokauka, isiyokuwa na mazao ambayo mimea na miti michache inaweza kuota pale.

Jangwa ni eneo la ardhi lenye tabia ya nchi ya ukavu na mimea na wanyama wachache.

Kwa sababu ya mazingira magumu, watu wachache sana wanaweza kuishi katika jangwa, kwa hiyo pia inajulikana kama "nyika".

"Nyika" inaleta maana ya sehemu iliyojitenga, ya kipekee mbali na watu.

Neno hili pia linaweza kutafsiriwa kama "sehemu ya jangwa" au "sehemu iliyojitenga" au "sehemu isiyokaliwa".

jasiri, ujasiri, ushujaa

Ufafanuzi

Maneno yote haya yanamaanisha kuwa na ujasiri na ushujaa kwa kuongea ukweli kuhusu jambo halali hata kama ni vigumu na hatari.

- Mtu "jasiri" haogopi kusema jambo jema na la haki, ikiwa ni pamoja na kuwatetea watu wanaonyanyaswa. Hii yaweza kufasiriwa kama "ujasiri" au "bila hofu".
- Katika Agano Jipya, wanafunzi waliendelea kuhubiri kwa "ujasiri" kuhusu Kristo hadharani, bila kujari hatari ya kufungwa au kuuawa. Hii inatafasiriwa kama "ujasiri" au "ushujaa" au "kwa ujasiri."
- "Ujasiri" wa wanafunzi hawa wa mwanzo katika kuhubiri habari njema ya kifo kiokoacho cha Kristo msalabani kilisababisha injili kuenea katika Israeli yote na nchi za jirani na hatimaye, katika dunia yote. "Ujasiri" waweza pia kutafasiriwa kama "ushujaa."

jikwaa

Ufafanuzi

Neno "jikwaa" lina maana ya "karibu kuanguka" wakati wakutembea au kukimbia. Kujikwaa juu ya kitu.

- Kifumbo, "kujikwaa" yaweza maanisha "kufanya dhambi" au "kuyumba" katika kuamini.
- Hili neno laweza elezea kuyumba au kuonyesha udhahifu wakati wa pambano au kipindi cha mateso au adhabu.

jirani

Ufafanuzi

Neno "jirani" mara kwa mara la mueleza mtu anaye ishi karibu. Pia yaweza kueleza kwa ujumla mtu anaye ishi katika jamii moja au kundi la watu.

- "Jirani" ni mtu atakaye lindwa na kutendewa vizuri kwasababu anaishi kwenye jamii moja.
- Katika Agano Jipya mfano wa Msamaria Mwema, Yesu alitumia "jirani" kifumbo, akitanua maana yake kumaanisha wanadamu wote, ata mtu anaye onekana kama adui.

jitu

Ufafanuzi

Jitu mara nyingi ilimaanisha mtu ambaye alikuwa na ukubwa usio wa kawaida wa urefu na nguvu.

Goliati, mwanajeshi wa Kifilisti aliyepigana na Daudi, aliitwa Daudi kwa sababu alikuwa mrefu sana, mkubwa, na mtu mwenye nguvu.

Wapelelezi wa Israeli waliotafiti nchi ya Kaanani walisema ya kwamba watu wanaoishi pale walikuwa kama majitu.

jiwe la kujikwaa

Ufafanuzi

Neno "jiwe la kijikwaa" la eleza kitu cha kimwili kinacho msababisha mtu kijikwaa na kuanguka.

- Katika Agano Jipya, hili neno lilieleza fimbo au kitu kingine kilicho mtega mnyama aliye kanyaga.
- Kifumbo jiwe la kijikwaa ni kitu chochote kinacho sababisha mtu kushindwa kimwili au kiroho.
- Mara nyingi ni dhambi ambayo ni jiwe la kujikwaa kwa mtu.
- Wakati mwingine Mungu anaweka jiwe la kujikwaa njiani kwa mtu anaye hasi dhidi yake.

joho

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "joho" uleza vazi lililo valiwa chini ya ngozi, chini nguo nyingine.

- Joho lilifika juu hadi chini kwenye kiuno au magoti na lilivaliwa na mkanda. Majoho yaliyo valiwa na watu matajiri yalikuwa na mikono mirefu na kufika hadi kwenye miguu.
- Majoho yalitengenezwa na ngozi, manyoa vitambaa, sufi, au kitani, na yalivaliwa na wanaume na wanawake.
- Joho lilivaliwa kawaida chini ya nguo ya ndani, kama toga au vazi la nje. Katika kipindi cha joto joho halikuvaliwa na nguo ya njee.

juma

Ufafanuzi

Neno "juma" kwa kawaida lamaanisha kipindi cha kuishia siku saba.

- Katika mfumo wa mahesabu ya Kiyahudi, juma huanza wakati wa jua kuzama Jumamosi na kuishia wakati wa jua kuzama Jumamosi inayofuata.
- Katika Biblia, neno "juma" wakati mwingine linatumika kitamathari kurejerea kundi la uniti saba za wakati, kama vile miaka saba.
- "Sikukuu ya majiuma" ni sherehe ya mavuno inayofanyika majuma saba baada ya Pasaka. Inajulikana kama Pentecoste.

juu, juu sana

Ufafanuzi

Maneno " juu" na " juu sana" ni misemo inayo maanisha, "mbinguni."

- Maana ingine ya msemo "juu sana" yaweza kuwa, "mwenye heshima sana"
- Huu msemo waweza tumika kihalisia, kama katika msemo, "kwenye mti wa juu sana" unao maanisha "kwenye mti mrefu zaidi"
- Msemo, "juu" waweza maanisha kuwa juu katika mbingu, kama kiota cha ndege kilicho juu. Katika Muktadha huo yaweza tafsiriwa, "juu katika mbingu" au "juu ya mti mrefu."
- Neno "juu" pia la eleza sehemu iliyo inuka au ya umuhimu wa mtu au kitu.
- Msemo "kutoka juu" yaweza tafsiriwa kama "kutoka mbinguni."

kabila

Ufafanuzi

Kabila ni kundi la watu waliyo toka kwa babu mmoja.

- Watu kutoka kabila moja mara nyingi walishiriki lugha moja na tamaduni.
- Katika Agano la Kale, Mungu aligawanya watu wa Israeli katika makabila kumi na mbili. Kila kabila lilitoka kwa mwana au mjukuu wa Yakobo.
- Kabila ni dogo kuliko taifa, lakini kubwa kuliko ukoo.

kaburi

Ufafanuzi

Neno "kaburi" ni sehemu watu wanapo weka mwili wa mtu aliye kufa.

- Wayahudi wakati mwingine walitumia mapango ya asili na makaburi, na wakati mwingine walichimba mapango katika miamba ya vilima.
- Wakati wa Agano Jipya, ilikuwa ni kawaida kuviringisha, jiwe kubwa mbele ya uwazi wa kaburi ilikufunga.
- Neno "kaburi" utumika kwa mfano wa kumaanisha hali ya kufa au sehemu nafsi za watu waliyo kufa zipo.

Kahaba

Ufafanuzi

"Kahaba" ni mtu anayefanya vitendo vya uzinzi kwa sababu ya pesa au ibada za kidini. Mara nyingi kahaba huwa mwanamke ila kuna wanaume pia.

- Katika Biblia "kahaba" imetumika kama lugha ya picha kumaanisha kitendo cha kuabudu miungu ya uongo au kufanya uganga.
- Ukahaba ni kitendo cha kufanya kama kahaba. Hii imetumika kwenye Biblia kuelezea mtu anayeabudu sanamu.
- Katika mahekalu ya wapagani hutumia makahaba kama sehemu ya ibada zao.

kama, mfano

Ufafanuzi

Misemo "kama" na "mfano" inamaanisha kitu kuwa sawa au kufanana na kitu kingine.

Neno "kama" pia inatumika katika mithali zinazoitwa "mfanano" ambapo kitu kinalinganishwa na kitu kingine, kawaida huonyesha tabia zinazolingana. Kwa mfano, "nguo zake zinang'aa kama jua" na "sauti ilivuma kama ngurumo." "Kuwa kama" au "kusikika kama" au "kuonekana kama" kitu au mtu inamaana kuwa na sifa zinazofanana na kitu anacholinganishwa nacho au mtu anayelingishwa naye. Watu waliumbwa katika "mfano" wa Mungu. Inamaanisha wana sifa au tabia ambazo ni "kama" au "zizafanana" na sifa ambazo Mungu anazo, kama uwezo wakufikiri, kuhisi na kuwasiliana. Kuwa na "mfano" wa kitu au mtu inamaana kuwa na tabia zinazofanana na hicho kitu au mtu.

Kamanda, amri

Ufafanuzi

Kamanda ni kiongozi wa jeshimwenye jukumu la kuongoza kundi fulani la askari.

- Kuamuru jeshi inamaanisha kuongoza jeshi na kuwa msimamizi kwa kila kitu.
- Kamanda anaweza kuwa kiongozi kwa kundi dogo au kubwa kama watu elfu moja.
- Neno hili pia linamuelezea Yesu kama kamanda wa jeshi la malaika.
- Kamanda pia yaweza kutafsiriwa kama "kiongozi" au "afisa."
- Kuamuru jeshi yaweza kutafsiriwa kama "kuongoza" au "kusimamia."

kamata

Ufafanuzi

Neno "kamata" la maanisha kuchukuwa au kumteka mtu au kitu kwa nguvu. Inaweza maanisha ya kumzidi nguvu au kumtawala mtu.

- Wakati mji ulipo chukuliwa kwa nguvu za kijeshi, wanajeshi walikamata mali za thamani za watu waliyo wa shinda.
- Linapo tumika kifumbo, mtu anaeza elezwa kuwa "kakamatwa na hofu." Hii ya maanisha kuwa mtu "alichukuliwa kwa hofu" ghafla. Inaweza tafsiriwa kama, "ghafla alikuwa muoga sana."
- Katika muktadha wa maumivu ya kujifungua yanayo "mkamata" mwanamke, maana ni kwamba maumivu ni ya ghafla na yazidi nguvu.
- Hili neno la weza tafsiriwa kama, "chukuwa mamlaka juu ya" au "ghafla chukuwa."

Kamili

Ufafanuzi

Katika Biblia neno kamili linamaana ya kukua katika maisha yetu ya Kikristo. Kukifanya kitu kuwa kamili ni kitendo cha kukifanyia kazi mpaka kikamilike bila dosari.

- Kuwa kamili au kukua inamaanisha kuwa Mkristo ni mtii hatendi dhambi.
- Katika kitabu cha Yakobo kinaeleza kuwa kupita katika majaribu kutetengeneza ukamilifu na kukua kwa waamini.
- Wakristo wakijifunza Biblia na kutii watakuwa wakamilifu zaidi kiroho na kukua kwa sababu watafanana sana na Yesu kwa tabia zao.

kanuni

Ufafanuzi

Neno "kanuni" lina maana ya "kufundisha". Mara nyingi lina maana ya mafunzo ya dini.

Katika muktadha wa mafunzo ya Kikristo, "kanuni" ina maana ya mafundisho yote kuhusu Mungu - Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu - ikijumlisha silika yake yote na kila kitu alichofanya.

Pia ina maana ya kila kitu Mungu anafundisha Wakristo juu ya namna ya kuishi maisha matakatifu ambayo yanaleta utukufu kwake.

Neno "kanuni" mara nyingnie linatumika kumaanisha mafunzo ya dini ya kidunia ya uongo ambayo hutoka kwa wanadamu. Muktadha hufanya maana wazi.

Msemo huu pia unaweza kutafsiriwa kama "mafunzo".

kanyaga

Ufafanuzi

"Kanyaga" ina maana ya kukanyaga kitu na kukisaga kwa mguu. Neno pia utumika kimfano katika Biblia kumaanisha "haribu" au "shinda" au "aibisha."

- Mfano wa "kukanyaga" utakuwa kama watu wakikimbia katika shamba la nyasi na kusigina nyasi na miguu yao.
- Zama za kale, mvinyo mara nyingine ulifanywa kwa kukanyaga mizabibu kuondoa juisi ndani yake.
- Wakati mwingine neno "kanyaga" lina maana ya umbo likimaanisha luadhibu kwa kuaibisha.
- Neno "kanyaga" linatumika kiumbo kueleza jinsi Yahweh atavyo wadhibu watu wake Israeli kwa kiburi chao na uhasi.

kanzu au vazi

Ufafanuzi

Kanzu ni vazi la mikono mirefu ambalo laweza kuvaliwa na mwanamke au mwanaume. Inafanana na koti.

- Kanzu zipo wazi mbele na hufungwa kwa mkanda.
- Kanzu yaweza kuwa fupi au ndefu.
- Kanzu za zambarau zilivaliwa na wafalme kama ishara ua ufalme, utajiri na ufahari.

karamu

Ufafanuzi

Msemo "karamu" una maana ya tukio ambapo kundi la watu hula chakula kingi sana pamoja, mara nyingi kwa kusudi ya kusherehekea kitu. Tendo "kula karamu" lina maana ya kula kiasi kikubwa cha chakula au kushiriki katika kula karamu pamoja.

Mara nyingi kuna aina maalumu za chakula ambavyo huliwa katika karamu maalumu.

Sherehe za kidini ambazo Mungu aliamuru Wayahudi kusherehekea mara kwa mara zilijumuisha kuwa na karamu ya pamoja. Kwa sababu hii sherehe hizo mara nyingi zilijulikana kama "karamu".

Katika kipindi cha Biblia, wafalme na watu wengine matajiri na wenye nguvu walifanya karamu kuwafurahisha familia zao au marafiki.

Katika simulizi kuhusu mwana mpotevu, baba yake alikuwa na karamu iliyoandaliwa kusherehekea ujio wa mwanawe.

Karamu mara zingine hudumu siku kadhaa au zaidi.

Msemo "kusherehekea" unaweza kutafsiriwa kama "kula kwa wingi mno" au "kusherehekea kwa kula chakula kingi" au "kula chakula kingi maalumu".

Kulingana na muktadha, "karamu" inaweza kutafsiriwa kama "kusherehekea pamoja kwa chakula kingi" au "mlo wenye chakula kingi" au "mlo wa sherehe"

kashfa, mtoa kashfa

Ufafanuzi

Kukashifu ina maana ya kusema kitu hasi, cha kudhalilisha kwa mtu mwingine.

- Kashfa yaweza kuwa kweli au taarifa ya kuongo ya kusingizia, lakini lengo ni kusababisha wengine kumfikiria vibaya mtu anaye kashifiwa.

kaya/famlia

Ufafanuzi

Istilahi 'kaya' hurejelea watu wote wanaoishi pamoja katika nyumba, ikijumuisha wana familia pamoja na watumishi walio nao. Mtu anaposimamia kaya, hujumuisha kuwaelekeza watumishi pamoja na kuangalia na kulinda mali. Wakati mwingine neno ' kaya' laweza kutumika kimfano kumaanisha ''ukoo wa mtu, hasa hasa wazao wake''

kazi, mfanyakazi

Ufafanuzi

Neno "kazi" linamaanisha kufanya kazi ngumu ya aina yoyote.

Kwa ujumla, kazi ni shughuli inayotumia nguvu, mara nyingi inaashiria kuwa shughuli ni ngumu. Mfanyakazi ni mtu afanyae aina yoyote ya kazi.

kereza meno, saga meno

Ufafanuzi

Kukereza au kusaga meno ina maana ya kukaza meno na kuyakwangua kwenda na kurudi dhidi yao. Hii mara kwa mara huonyesha maumivu na hasira kubwa mno.

Biblia inatuambia ya kwamba kusaga meno ni jambo moja ambalo wale walio jehanamu watafanya katika dhiki yao kuu.

Msemo huu pia unaweza kutafsiriwa kama "kukwangua meno dhidi yao" au "kama haipo wazi nini tendo hili linamaanisha "kusaga meno kwa maumivu" au "kusaga meno katika uchungu".

kiapo, kuapa,

Ufafanuzi

Katika Biblia, kiapo ni ahadi rasmi ya kufanya kitu. Mtu anaye kiapo anapswa kutimiza hiyo ahadi. Kiapo kinahusu kuwa mwaminifu na wa kweli.

- Mara nyingi katika mahakama ya sheria, shahidi anatoa kiapo kuahidi kwamba chochote anachosema kitakuwa kweli na hakika.
- Katika Biblia, neno "apa" lina maana ya kiapo.
- Neno "kuapa" lina maana ya kutumia jina la kitu au mtu kama chanzo au nguvu ambayo kiapo kinatolewa.
- Wakati mwengine haya maneno yanatumika pamoja kama, "apa kiapo"
- Ibrahimu na Abimeleki waliapa kiapo walipo wafanya agano pamoja kuhusu matumizi ya kisima.
- Ibrahimu alimwambia mtumishi wake aape kuwa atampatia Isaka mke kutoka miongoni mwa ndugu wa Ibrahimu.
- Mungu pia alifanya kiapo ambacho alitoa ahadi kwa watu wake.

kiasi

Ufafanuzi

Kiasi ni uwezo wa kutawala tabia ya mtu ili kuepusha kutenda dhambi.

- Ina husu tabia njema, kuepuka mawazo mabaya, lugha, na matendo.
- Kiasi ni tunda au tabia ambalo Roho Mtakatifu anawapa Wakristo.
- Mtu anaye tumia kiasi anaweza jizuia kutofanya kitu kibaya anacho weza fanya. Mungu ndiye anaye mpa mtu uwezo wa kuwa na kiasi.

Kiburi

Ufafanuzi

Kiburi ni hali ya mtu kujifikiria mwenyewe na kudhani kuwa yeye ni bora kuliko wengine.

- Mtu mwenye kiburi huwa hakubali makosa yake. Sio mnyenyekevu.
- Kiburi kinaweza kusababisha usimtii Mungu katika njia nyingine.
- Pia kiburi kinaweza kuelezwa katika mtazamo chanya kwa mfano "kujivunia" kwa kitu ambacho mtu fulani amefanikiwa au "kujivunia" watoto wako.
- Mtu anaweza kujivunia kwa alichokifanya bila kuwa na kiburi juu ya hilo.

Kichwa

Ufafanuzi

Katika Biblia neno 'kichwa' lilmetumika kama tamathali ya semi likiwa lina maana nyingi: Mara nyingi neno hili limetumika kurejelea hali ya kuwa na mamlaka juu ya watu , kwa mfano, "mmenifanya kichwa cha mataifa" Sentensi hiyo yaweza kutafsiriwa kuwa "mmenifanya kuwa mtawala" au "mmenipa mamlaka juu ya..." Yesu anaitwa 'kichwa cha kanisa.' Kama ambavyo kichwa cha mtu huongoza viungo vingine vya mwili, hivyo na Yesu huongoza na huelekeza viungo vingine vya mwili wake, yaani kanisa. Agano la Jipya linatufundisha kuwa mme ni "kichwa'' au mwenye mamlaka kwa mkewe. Amepewa wajibu wa kumwongoza na kumwelekeza mkewe na familia. Maneno yanayosema "wembe hautagusa kich chake" maana yake ni kwamba" hatakata au hatanyoa nywele zake. Neno 'kichwa' laweza pia kurejelea mwanzo au asili ya kitu fulani, mfano 'kichwa cha mtaa" Maneno kama "kichwa cha nafaka" hurejelea sehemu ya juu ya ngano au mche wa shayiri ambao una mbegu ndani yake. Mfano mwingine wa 'kichwa' ni pale unapotumika kuwakilisha mtu mzima. Mfano, 'kichwa cheupe' humrejelea mtu mzee au tunaposema ' kicha cha Yusufu, tunamaanisha Yusufu mwenyewe. Msemo unaosema 'acha damu yao iwe juu ya kichwa chake' humaanisha kuwa mtu yule anawajibika kwa vifo vyao na atapokea adhabu/hukumu yake.

Mapendekezo ya tafsiri Neno 'kichwa' laweza kutafsiriwa kama 'mamlaka' au 'mtu anayeongoza na kuelekeza' au 'mtu anayewajibika kwa..' kwa kutegemea na muktadha wenyewe. Maneno kama ' kichwa cha' hurejelea mtu mwenyewe mzima, na hivyo maneno hayo yaweza kutafsiriwa kwa kutumia jina la mtu husika. kwa mfano ''kichwa cha Yusufu'' ina maana ya 'Yusufu' Maelezo kama ' itakuwa juu ya kichwa chake' yanaweza kutafsiriwa kama " itakuwa juu yake'' au 'ataadhibiw'a kwa ajili ya' au 'atawajibika kwa ajili ya... Kwa kutegemea na muktadha wenyewe, maana zingine za neno kichwa zaweza kuwa "mwanzo' au "asili'' au ''chanzo'' au "mtawala" au ''juu ya''

kifo, kufa, mfu

Ufafanuzi

Msemo huu unatumika kumaanisha vyote kifo cha kimwili na kiroho. Kimwili, ina maana ya mwili wa kihalisia wa mtu kukoma kuishi. Kiroho, ina maana ya wenye dhambi kutengwa na Mungu mtakatifu kwa sababu ya dhambi yao.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kutafsiri msemo huu, ni vyema kutumia neno la kila siku au usemi ambao una maana ya kifo katika lugha husika.

Katika baadhi ya lugha, "kufa" inaweza kuelezwa kama "kutokuishi". Msemo "kufa" unaweza kutafsiriwa kama "kutokuwa hai" au "kutokuwa na uhai wowote" au "kutokuishi".

Lugha nyingi zinatumia msemo wa tamathali kuelezea kifo, kama "kuondoka" kwa Kiingereza. Ila katika Biblia ni bora kutumia msemo wa moja kwa moja kwa ajili ya kifo ambao unatumika kila siku katika lugha.

Katika Biblia, uhai na kifo wa kimwili mara kwa mara hulinganishwa na uhai na kifo cha kiroho. Ni muhimu katika tafsiri kutumia neno moja au msemo kwa ajili kifo cha kimwili na kifo cha kiroho.

Katika baadhi ya lugha inaweza kuwa wazi zaidi kusema, "kifo cha kiroho" ambapo muktadha unahitaji maana hiyo. Watafsiri wengine wanaweza kuhisi ni bora kusema, "kifo cha kimwili" katika muktadha ambapo unalinganishwa na kifo cha kiroho.

Msemo wa "wafu" ni kivumishi chenye maana ya watu waliokufa. Baadhi ya lugha zitatafsiri hili kama, "watu waliokufa" au "watu ambao wamekufa"

kifuko cha kifuani

Ufafanuzi

Neno "dirii" ni kipande cha silaha kinachofunika kifua kumlinda askari wakati wa vita. Neno "kifuko cha kifuani" linamaanisha kipande maalumu cha nguo ambacho kuhani mkuu wa Kiisraeli alivaa katika sehemu yake ya mbele kifuani.

- "Dirii" iliyotumiwa na askari ilitengenezwa kwa miti, chuma au ngozi ya mnyama. Ilikuwa imetengenezwa kuzuia mishale, mikuke, na upanga katika kuchoma kifua cha askari.
- "Kifuniko" kilichovaliwa na kuhani mkuu kilikuwa kimetengenezwa kwa nguo na kilikuwa kitu kilichounganiswa nacho. Kuhani alikivaa alipokuwa katika majukumu yake ya kumtumikia Mungu hekaluni.
- Njia nyingine ya kutafasiri "dirii" ni pamoja na, "kifaa cha chuma cha kufunika kifua" au delaya ya kulinda kifua."
- Neno "kifuniko" litafasiriwe kwa neno limaanishalo, vazi la kikuhani lifunikalo kifua" au "kipande cha vazi la kikuhani" au "kipande cha mbele cha vazi la kuhani."

kikapu

Ufafanuzi

Neno "kikapu" linamaanisha chombo kilichotengenezwa kwa kusukwa.

- Nyakati za Biblia, vikapu pengine vilitengenezwa kwa mimea, kama vile kutoka katika matawi ya miti au magome.
- Kikapu kiliweza kuwekewa vitu vya kuzuia maji ili kiweze kuelea.
- Musa alipokuwa mtoto, mama yake alitengeneza kikapu kisichopenyeza maji kwa kumweka humo na kukieleza katika mafunjo katika Mto Nile.
- Neno lililotafasiriwa kama "kikapu" katika habari hiyo ni sawa na neno "safina" kurejerea mtumbwi alioutengeneza Musa. Maana ya kawaida ya matumizi yake katika mazingira mawili hayo yaweza kuwa' "chombo kieleacho."

Kimbia

Ufafanuzi

Kukimbia ni kitendo cha kutembea haraka kwa miguu, haraka zaidi ya kutembea. Pia kukimbia yaweza kuwa na maana zifuatazo.

- "Kukimbia ili kushinda taji" - hii inamaanisha kuwa kufanya mapenzi ya Mungu kama kukimbia mbio ili ushinde.
- "Kukimbia ili kufanya uliyoamriwa" hii inamaana ya kwamba kutii haraka amri za Mungu.
- "Kukimbilia miungu mingine"- Hii inamaanisha kwenda kuabudu miungu mingine.
- "Kukimbilia kwako ili unifiche" - hii inamaanisha kuwa kukimbilia haraka kwa Mungu ili kupata usalama unapokutana na mambo magumu.

Kimbilio, malazi

Ufafanuzi

"Kimbilio" ni sehemu au hali ya usalama na ulinzi. "Malazi" ni sehemu yenye muundo wa kimwili ambayo inakulinda kutokana na hali ya hewa au hatari.

- Katika Biblia Mungu anaelezwa kama kimbilio ambapo watu wake huwa salama na kupata ulinzi kwake.
- "Mji wa makimbilio" katika agano la kale ni miji ambayo mtu akiua kwa bahati mbaya hukimbilia huko kwa ajili ya usalama toka kwa watu wanaotaka kumvamia na kulipa kisasi.
- Malazi ni sehemu inayojengwa kama jengo ambalo laweza kutoa ulinzi kwa watu au wanyama.
- Mara nyinginge malazi humaanisha usalama. Lutu aliposema wageni wake wapo chini ya malazi ya paa lake alikuwa na maana kuwa walikuwa salama kwa sababu walikuwa kwenye nyumba yake.

kinanda, kinubi

Ufafanuzi

Kinanda na kinubi ni vyombo vidogo vya muziki vyenye nyuzi zilizotumika na Waisraeli kumuabudu Mungu.

Kinanda kinafanana sana na gita la siku hizi, lina sanduku ya mbao na shingo ndefu ambapo nyuzi zimefungwa. Kucheza kinanda au kinubi, nyuzi flani zinashikiliwa na mkono mmoja wakati nyuzi zingine zinapigwa na mkono mwingine. Kinanda na kinubi zote zinachezwa kwa kupigwa au kuvutwa nyuzi. Idadi ya nyuzi ilitofautiana, lakini Agano la Kale lilitaja bayana vyombo vyenye nyuzi kumi.

kinara cha taa.

Ufafanuzi

Katika Biblia, usemi "kinara cha taa" kwa ujumla inamaanisha umbo ambapo taa inawekwa ili kutoa mwanga kwa chumba.

Kinara cha taa cha kawaida kilibeba taa moja na kilitengenezwa kwa udongo, mbao au chuma (kama shaba, fedha, au dhahabu.) Katika hekalu la Yerusalemu kulikuwa na kinara cha taa maalumu cha dhahabu kilichokuwa na matawi saba kwa kushikilia taa saba.

kinubi

Ufafanuzi

Kinubi ni chombo au kifaa cha muziki mara nyingi huwa na muundo ulio na uwazi mkubwa na nyuzi za wima. Katika Biblia, mbao za msonobari zilitumika kutengenezea vinubi pamoja na vyombo vingnei vya muziki. Vinubi mara kwa mara vilishikiliwa mikononi na kupigwa wakati mtu akiwa anatembea. Sehemu nyingi katika Biblia, vinubi vilikuwa vikitumika katika kumsifu na kumwabudu Mungu. Daudi aliandika Zaburi kadhaa ambazo zilikuwa zimepangwa kwa muziki wa kinubi. Daudi pia alicheza kinubi kwa mfalme Sauli ili kutuliza na kuburudisha roho ya mfalme iliyotaabika.

kinyume cha sheria

Ufafanuzi

Maneno "kinyume cha sheria" na "sio kisheria" yanatumika kueleza matendo yanayo vunja sheria.

- Katika Agano Jipya, neno "kinyume cha sheria" sio tu la tumika kueleza kuvunja amri ya Mungu, bali pia kuvunja sheria za Kiyahudi.
- Baada ya miaka, Wayahudi waliongeza kwenye sheria Mungu alizowapa. Viongozi wa Kiyahudi waliita kitu "kinyume cha sheria" kama hakikuendana na sheria zao wao.
- Yesu na wanafunzi wake walipo kuwa wana nyofoa nafaka siku ya Sabato, Mafarisayo waliwashtaki kufanya "kinyume cha sheria" kwasababu ilikuwa ina vunja sheria za Wayahudi za kutofanya kazi hiyo siku.
- Wakati Petro alipo sema kula chakula najisi ni "kinyume cha sheria" kwake, alimaanisha kama angekula vyakula angekuwa na vunja sheria Munug alizo wapa Waisraeli kuhusu kuto kula baadhi ya vyakula.

kinywaji kikali

Ufafanuzi

Neno "kinywaji kikali" ina eleza vinywaji vilivyo zindikwa na vina vilevi.

- Vinywaji vya vilevi utengenezwa na nafaka au matunda na vimepitia njia ya kuzindikwa.
- Aina ya "kinywaji kikali" ni mvinyo wa mzabibu, mvinyo wa mtende, bia. Katika Biblia, mvinyo wa mzabibu ndio unao tumika sana.
- Makuhani na mtu ye yote walio chukuwa kiapo maalumu kama "kiapo cha Naziri" hawaku ruhusiwa kunywa kilevi.

Kisasi

Ufafanuzi

"Kisasi" ni kitendo cha kumuadhibu mtu kama malipo ya yale mabaya aliyoyatenda.

- Mara nyingi lengo la kisasi ni kuona kuwa haki inatendeka au kurekebisha kosa.
- Kwa binadamu kulipa kisasi inajumuisha kumuadhibu mtu aliyefanya makosa.
- Mungu akilipa kisasi anafanya kwa haki kwa sababu anahukumu watenda dhambi na waasi.

Kisima,birika

Ufafanuzi

Kisima na birika ni vyanzo viwili tofauti vya maji katika nyakati za Biblia.

- Kisima ni shimo refu linalochimbwa ardhini ili maji ya chini yamiminike juu yake.
- Birika ni shimo refu lililopo kwenye mwamba linalotumika kushikilia tangi kwa ajili ya kukusanya maji.
- Maranyingi birika huchimbwa kwenye mwamba na kukandikwa na plasta ili kuyahifadhi maji ndani.
- Birika maranyingi huwekwa maeneo ya uani kwenye nyumba za watu ili kuvuna maji ya mvua yanayotiririka juu ya paa.
- Visima vilichimbwa sehemu ambayo ilikuwa rahisi kwa familia au jamii kufika.
- Kwa sababu maji yalikuwa muhimu kwa watu na wanyama mara nyingine haki ya kutumia maji ilileta ugonvi.
- Kisima na birika vilifunikwa na jiwe kubwa ili kuzuia chochote kisianguke juu yake.
- Mara nyingine birika lililokauka lilitumika kama gereza kwa mfano Yusufu na Yeremia walifungwa kwenye birika.

Kitabu cha uzima

Ufafanuzi

Neno "Kitabu cha uzima" linatumika kumaanisha Mungu alipoandika majina ya watu aliowakomboa na kuwapa uzima wa milele.

- Kitabu cha ufunuo kinarejerea kitabu hiki kama "Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo." Ingeweza kutafasiriwa kama "kitabu cha Yesu cha uzima, Mwanakondoo wa Mungu." Sadaka ya Yesu msalabani ililipa adhabu ya dhambi za watu ili waweze kuwa na uzima wa milele kwa njia ya kumwamini.
- Neno kwa "kitabu" laweza pia kumaanisha, "gombo" au "andiko" "kitabu cha sheria." Inaweza kuwa na maana halisia au ya kimafumbo.

kiti cha enzi

Ufafanuzi

Kiti cha enzi ni kiti ambacho mfalme ana keti kuamua mambo muhimu na kusikiliza maombi ya watu wake.

- Kiti cha enzi ni ishara ya mamlaka na nguvu ambayo mfalme anayo.
- Neno "kiti cha enzi" utumika mara nyingi kifumbo kumueleza mfalme, utawala wake, au nguvu yake.
- Katika Biblia, Mungu anaonyeshwa kama mfalme anaye keti katika kiti chake cha enzi. Yesu anaelezwa akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba kwenye kiti chake cha enzi.

Kiumbe

Ufafanuzi

Kiumbe ni kila kitu kilicho hai ambacho Mungu alikiumba, binadamu na wanyama.

- Nabii Ezekieli anaelezea kuona "viumbe hai" katika maono ya utukufu wa Mungu. Hakujua ni nini hivyo akaviita hivyo.
- Tambua kuwa neno kiumbe ina maana tofauti na kwa kuwa inajumuisha kila kitu ambacho Mungu amekiumba vilivyo hai na visivyo hai. Kiumbe ni vitu vilivyo hai peke yake.

Kivuli

Ufafanuzi

Neno "kivuli" lina maana ya giza linalo sababishwa na kitu kinacho ziba mwanga. Pia lina maana kadhaa ya mafumbo.

- "Kivuli cha mauti" ina maana kwamba kifo kipo karibu, kama vile kivuli kinavyo hashiria uwepo kitu.
- Mara nyingi katika Biblia, maisha ya mwanadamu yana linganishwa na kivuli, ambacho hakidumu muda mrefu sana na hakina kiini.
- Wakati mwingine, "kivuli" lina tumika kama neno lingine la "giza."
- Biblia inaongea kuhusu kujificha au kulindwa ndani ya kivuli cha mabawa ya Mungu au mikono. Hii ni picha ya kulindwa na kufichwa kutoka kwenye hatari.

kizazi

Ufafanuzi

Msemo "kizazi" una maana ya kundi la watu ambao wote wamezaliwa katika kipindi cha kufanana.

Kizazi pia kinaweza kumaanisha kipindi cha muda. Katika kipindi cha Biblia, kizazi kilichukuliwa kuwa kama miaka 40.

Wazazi na watoto waoo wanatoka katika vizazi viwili tofauti.

Katika Biblia, msemo "kizazi" pia hutumika kitamathali kumaanisha kwa ujumla watu ambao huwa na tabia za kufanana.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo " kizazi hiki" au "watu wa kizazi hiki" unaweza kutafsiriwa kama "watu wanaoishi sasa" au "nyie watu".

"Kizazi hiki kiovu" inaweza kutafsiriwa kama "watu hawa waovu wanaoishi sasa".

Msemo "kutoka kizazi hadi kizazi" au "kutoka kizazi kimoja hadi kingine" inaweza kutafsiriwa kama "watu wanaoishi sasa, pamoja na watoto na wajukuu wao" au "watu katika kipini chote" au "watu wa kipindi hili na vipindi vya baadaye" au "watu wote na uzao wao".

"Kizazi kinachokuja kitamtumikia; watawaambia kizazi kifuatacho juu ya Yahwe" inaweza kutafsiriwa kama "Watu wengi hapo baadaye watamtumikia Yahwe na kuwaambia watoto na wajukuu wao juu yangu".

kizingiti

Ufafanuzi

Neno "kizingiti" la eleza sehemu ya chini ya mlango au sehemu jengo ambayo ipo ndani ya mlango.

- Wakati mwingine kizingiti ni kijiti cha ambao ambcho lazima kikanyagwe ilikuingia chumbani au kwenye jengo.
- Lango pamoja na uwazi wa hema la weza kuwa na kizingiti.

Komamanga

Ufafanuzi

Komamanga ni aina ya tunda nene lenye ngozi ngumu lililojaa mbegu nyingi ndani zilizozungukwa na chakula chenye rangi nyekundu.

- Komamanga mara nyingi huota katika nchi zenye joto, ukame kama Miisri na Israeli.
- Bwana aliwaahidi wa Israeli kuwa Kanaani ni chi yenye maji ya kutosha na ardhi yenye rutuba iliyo na vyakula vya kutosha ikiwemo makomamanga.
- Ujenzi wa hekalu la Sulemani lilikuwa na mapambo yaliyo katika muundo wa komamanga.

komboa, mkombozi, ukombozi

Ufafanuzi

"Kukomboa" mtu ina maana ya kumukokoa mtu huyo. Msmo "mkombozi" una maana ya mtu ambaye hukomboa au kuweka huru watu kutoka utumwani, mateso au hatari zingine. Msemo "ukombozi" una maana ya kile kinachotokea pale mtu anapookoa au kuweka watu huru kutoka utumwani, matesoni, au hatari zingine.

Katika Agano la Kale, Mungu aliwaweka wakombozi kuwalinda Waisraeli kwa kuwaongoza katika vita dhidi ya makundi ya watu wengine waliokuja kuwashambulia.

Wakombozi hawa pia walijulikana kama "waamuzi" na kitabu cha Agano la Kale cha Waamuzi kimeweka kumbukumbu ya kipindi katika historia ambapo waamuzi hawa walikuwa wakitawala Israeli.

Mungu pia anaitwa "mkombozi". Kote katika historia ya Israeli, aliwakomboa au kuwaokoa watu wake kutoka kwa maadui zao.

Msemo "kutoa kwa" ina maana tofauti kabisa ya kumtoa mtu kwa adui, kama pale Yuda alipomtoa Yesu kwa viongozi wa Kiyahudi.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika muktadha wa kusaidia watu kutoroka kutoka kwa adui zao, msemo "komboa" unaweza kutafsiriwa kama "okoa" au "kuweka huru" au "nusuru".

Pale inapomaanisha kukabidhi mtu kwa adui, "kukabidhi" inaweza kutafsiriwa kama "kusaliti" au "kumpatia" au "kutoa kwa".

Neno "mkombozi" linaweza kutafsiriwa kama, "mkombozi" au "mweka huru".

Pale ambapo msemo "mkombozi" una maana ya waamuzi waliongoza Israeli, inaweza pia kutafsiriwa kama "bosi au "mwamuzi" au "kiongozi"

kondoo, kondoo dume, kondoo jike

Ufafanuzi

"kondoo" ni mnyama wa saizi ya kati wa miguu minne mwenye manyoya mwili mzima.

- Waisraeli mara kadhaa walitumia kondoo kwa dhabihu, hususani dume na kondoo mdogo.
- Watu ula nyama ya kondoo na kutumia manyoya yake kufanya nguo na vitu vingine.
- Kondoo ni wa piole, dhahifu, na waoga. Wanashawishika haraka kupotea. Wanaitaji mchungaji kuwaongoza, kuwalinda, na kuwapa chakula, maji, na hifadhi.
- Katika Biblia, watu wanalinganishwa na kondoo waliyo na Mungu kama mchungaji wao.

Kosa, mateso, kuumiza

Ufafanuzi

"kumkosea" mtu inamaanisha kumfanyia mtu isivyo haki na kwa udanganyifu.

- Mateso ni kumtendea mtu vibaya na kumsabaishia maumivu ya kimwili au kihisia.
- Kuumiza ni neno la jumla lenye maana ya kusababisha maumivu kwa mtu. Yawza kuwa kumsababishia majeraha ya kimwili.
- Inategemea na mukhtadha maneno haya yanaweza kuwa na maana ya "kumtendea mtu kosa" au "kutomtendea haki" au "kusababisha maumivu" au "kujeruhi."

kuachwa, kuacha

Ufafanuzi

Msemo wa "kuachwa" na "kuacha" ina maana ya kuangamiza sehemu isiyokuwa na watu ili kwamba isiwe ya makazi.

Inapomaanisha mtu, msemo "kuachwa" inaelezea hali ya uharibifu, upweke, au majonzi.

Msemo "kuacha" ni hali ya kuachwa.

Iwapo shamba ambapo mimea inaota linaachwa, ina maana kitu kimeaangamiza mimea, kama wadudu au uvamizi wa jeshi.

"Eneo lilioachwa" lina maana ya eneo ya ardhi ambapo watu wachache wanaishi kwa sababu kuna mazao machache au mimea mingine inayoota pale.

"Ardhi iliyoachwa" au "nyika" mara kwa mara ilitengwa kwa watu waliotengwa na jamii (kama wakoma) na wanyama wa hatari.

Kama mji "unatengwa" ina maana ya kwamba majengo yake na mali vimeharibiwa au kuibiwa, na watu wake wameuwawa au kukamtwa. Mji unakuwa "tupu" na "kuharibika". Hii ni sawa na maana ya "teketeza" au "teketezwa", lakini kwa msisitizo zaidi kwa utupu.

Kutegemea muktadha, msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "kuharibiwa" au "kuangamizwa" au "kuwekwa kama takataka" au "mpweke/iliyotengwa" au "kutelekezwa"

Kuadhibu, adhabu

Ufafanuzi

"Kuadhibu" inamaana ya kusababisha mtu ateseke baada ya kufanya makosa. Adhabu ni matokeo hasi anayopewa mtu baada ya kufanya jambo baya.

- Adhabu hutumika kumfanya mtu aache dhambi.
- Mungu aliwaadhibu Waisraeli walipomuasi hasa walipoabudu miungu ya uongo, Mungu aliruhsu adui zao kuwavamia na kuwateka.
- Mungu ni wa haki hivyo huadhibu wenye dhambi. Kila binadamu ametenda dhambi na anastahili adhabu.
- Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya makosa ya kila mtu. Alipokea adhabu ya kila mtu japokuwa yeye hakuwa na kosa lolote.
- Maneno kama "bila kuadhibiwa" au "kuacha kuadhibiwa" yanamaana kuamua kutokuadhibu watu kwa matendo yao maovu. Mungu mara nyingine anawaacha wenye dhambi bila kuwaadhibu akisubiria watubu.

kubeba

Ufafanuzi

Neno "kubeba" linamaanisha "kubeba" kitu fulani. Lakini pia kuna kuna matumizi ya tamathari mbalimbali ya neno hili.

- Unapoongelea mwanamke atakayebeba mtoto, inamaanisha, "kuzaa" mtoto.
- "kubeba mzigo" inamaanisha "kupitia magumu." Magumu haya yaweza kuwa ya kimwili au ya kihisia.
- Matumizi yake yaliyozoeleka katika Biblia ni "kuzaa matunda" inayomaanisha, " "kuzalisha matunda" au "kuwa na matunda."
- Kifungu "kubeba ushahidi" inamaanisha "kushuhudia" au "kutoa taarifa ya kile ulichokiona au kukipitia."
- Taarifa ya "mwana hatabeba uovu wa mzazi" inamaanisha "hatawajibika kwa ajili ya" au "hataadhibiwa kwa ajili ya "dhambi za baba yake".
- Kwa ujumla, neno laweza kutafasiriwa kama, "kubeba" au "kuwajibika kwa" au "kuzaa" au "kuwa na" au "kustaimili," kutegemeana na mazingira.

kuchinja

Ufafanuzi

Neno "kuchinja" Maneno waliyo chinjwa ya weza pia tumika kutafsiri watu waliyo chinjwa au watu waliyo uawa. Pia la weza tumika kumaanisha mkua mnyama kwa kusudi la kumla.

- Wakati Ibrahimu alipo pokea wageni watu katika hema yake jagwani, aliamuru watumishi wake kuua na kupika ndama kwa ajili ya wageni wake.
- Nabii Ezekieli alitabiri kwamba Mungu atatuma malaika kuchinja wote wasio fuata neno lake.
- 1 Samweli ya eleza kuchinjwa kwa Waisraeli 30,000 waliyo uliwa na adui zao. Kwasababu ya kutomtii Mungu.
- "silaha za kuchinja" yaweza tafsiriwa kama "silaha za kuua."

kudanganya, udanganyifu, hila, mdanganyifu

Ufafanuzi

Msemo wa"kudanganya" una maana ya kumfanya mtu aamini jambo ambalo sio la kweli. Tendo la kumdanganya mtu linajulikana kama "udanganyifu".

Msemo mwingine, "udanganyifu" pia una maana ya tendo la kumfanya mtu aamini jambo ambalo sio kweli.

Mtu anayefanya wengine kuamini jambo la uongo ni "mdanganyifu". Kwa mfano, Shetani anaitwa "mdanganyifu". Roho chafu anazoziongoza pia zinajulikana kama wadanganyifu.

Mtu, tendo, au ujumbe ambao sio wa kweli unaweza kuelezwa kama "udanganyifu".

Misemo ya "udanganyifu" na "hila" zina maana moja, lakini kuna tofauti kadhaa ndogo jinsi zinavyotumika.

Misemo inayojieleza ya "udanganyifu" na "hila" ina maana moja na hutumika katika muktadha moja.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri "kudanganya" zinaweza kujumuisha "uongo" au "kusababisha kuwa na na imani potofu" au "kusababisha mtu afikiri jambo sio la kweli".

Msemo "kudanganywa" unaweza kutafsiriwa kama "kusababisha kufikiri jambo ni la uongo" au "alidanganywa" au "alifanyiwa hila" au "alipumbazwa" au "alipotoshwa".

"Mdanganyifu" inaweza kutafsiriwa kama, "mwongo" au "mtu mpotoshaji" au "mtu anayedanganya".

Kulingana na muktadha, msemo wa "udanganyifu" au "hila" unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo unaomaanisha "uongo" au "kudanganya" au "upotoshaji" au "kutokuwa na uaminifu".

Msemo "kudanganya" au "udanganyifu" unaweza kutafsiriwa kwa "uongo" au "upotoshaji" au "kudanganya" kumuelezea mtu anayezungumza au kutenda kwa njia ambayo inasababisha watu wengine kuamini mambo ambayo sio ya kweli.

Kufanikiwa, mafanikio

Ufafanuzi

"Kufanikiwa" ni kitendo cha kuishi vizuri na kuwa na mafanikio kimwili na kiroho. Nchi inayofanikiwa inamaanisha wana utajiri na wanakila kitu wanachohitaji.

- Mafanikio ni kufanikiwa kwa kuwa na pesa na mali.
- Katika Biblia "mafanikio" yanajumuisha afya njema au kubarikiwa kuwa na watoto.
- Mji wenye mafanikio ni mji wenye watu wengi, uzalishaji mzuri wa chakula na biashara inayozalisha pesa nyingi.
- Biblia inafundisha kuwa mtu atafanikiwa kiroho pale atakapotii mafundisho ya Mungu. Pia tapata baraka ya furaha na amani. Mungu hawabariki tuu watu kwa kuwapa mali bali huwabariki pia kiroho.
- Mafanikio pia yaweza kutafsiriwa kama "utajiri" au "matunda ya kiroho."

Kufanya, nia, kujituma

Ufafanuzi

Kufanya au kujituma ni kitendo cha kufanya maamuzi au kuahidi kufanya jambo fulani.

- Mtu anayeahidi kufanya jambo ni mtu mwenye nia ya kufanya jambo hilo.
- Kumpa mtu afanye jambo fulani inmaanisha kumkabidhi mtu shughuli fulani ya kufanya
- Kufanya pia yaweza kuwa na maana ya kufanya dhambi au kufanya uzinzi au kufanya uuaji.
- Kujituma yaweza kutafsiriwa kama "kazi iliyotolewa" au "ahadi iliyotolewa."

kufanywa haki

Ufafanuzi

Usemi "kufanywa haki" inamaanisha kumfanya mtu mwenye hatia kuwa mwenye haki. Mungu pekee ndiye awezaye kuwafanya watu kuwa na haki.

Mungu anapowafanya haki watu, huwasamehe dhambi zao na kuwafanya kana kwamba hawana dhambi. Huwafanya haki watenda dhambi wanaotubu na kumuamini Yesu kuwaokoa kutoka dhambi zao. "kufanywa haki" inamaanisha kile Mungu anachofanya anaposamehe dhambi za mtu na kutamka kuwa mtu huyo ni mwenye haki machoni pake.

kufinyanga

Ufafanuzi

Kufinyanga ni kutengeneza mbao, chuma, au udogo ilikutimia kuunda umbo kutokana na dhahabu, fedha, au vitu vingine vinavyo weza kumika kwa kufinyangwa.

- Vituvya ufinyazi vilitumika kutengeneza mikufu, vyombo, na vitu vya kulia.
- Katika Biblia, vitu vya ufinyazi vinatumika mara nyingi kwa kutengeneza sanamu.
- Chuma zilipaswa kuchomwa ili kwamba viweze kufinyangwa.

Kufurani

Ufafanuzi

Kufurahi inamaana ya kuwa na furaha.

- Neno hili limetumika kuelezea hali ya kuwa na furaha sana juu ya mambo mazuri aliyoyafanya Mungu.
- Hii inaweza kutafsiriwa kama "kuwa na furaha sana."
- Mariamu aliposema kuwa "nafsi yangu inafurahi ndani ya Mungu mwokozi wangu" alimaanisha kuwa "Mungu mwokozi wangu amenifanya kuwa na furaha" au " ninasikia furaha kwa sababu ya kitu ambacho Mungu mwokozi wangu amefanya kwangu."

kufuru

Ufafanuzi

Neno la "kufuru" lina maana ya kuharibu au kuchafua sehemu takatifu au kitu katika namna ambayo haikubaliki kutumika katika kuabudu.

Mara kwa mara kukufuru kitu inahusisha kuonyesha okosefu mkubwa wa keshima kwake.

Kwa mfano, wafalme wa kipagani walikufuru vyombo maalumu kutoka hekalu la Mungu kwa kuvitumia kwa ajili ya sherehe katika kasri zao.

Mifupa kutoka watu waliokufa ilitumika na maadui kukufuru madhabahu katika hekalu la Mungu.

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kama, "kusababisha kutokuwa mtakatifu" au "kumvunjia heshima kwa kufanya asiwe mtakatifu" au "kukufuru kwa kuvunja heshima" au "kusababisha kutokuwa msafi".

kufuta

Ufafanuzi

Maneno "kufuta" au "kuondoa" ni vifungu vinavyomaanisha kuondoa kabisa au kuangamisa kitu au mtu.

- Vifungu hivi vyaweza kutumika katika maana chanya, kama ambavyo Mungu "hufuta" dhambi kwa kusamehe na kuchagua kutokukumbuka tena.
- Lakini pia yaweza kutumika katika maana mbaya, kama ambavyo Mungu "hufuta" au "kuondoa" kundi la watu, kuwaharibu kwa sababu ya dhambi.
- Biblia inazungumzia juu ya jina la mtu "kufutwa" au "kuondolewa" katika kitabu cha Mungu, kumaanisha mtu hatapokea uzima wa milele.

Maone ya Kutafasiri

- Kwa kutegemea mazingira, vifungu hivi vyaweza kutafasiriwa kama "kuondoa" au "kutoa" au " kuharibu kabisa" au "kuondoa kabisa."
- Kwa kurejerea kufuta jina la mtu katika Kitabu cha Uzima, yaweza kutafasiriwa kama "kuondoa kutoka" au "iliyofutwa."

Kugawa, kupewa

Ufafanuzi

Kugawa au kupewa ni kitendo cha kumteua mtu kwa ajili ya kufanya kazi maalumu.

- Nabii Samweli aliambiwa kuwa mfalme Sauli atateua vijana wazuri wa Israeli kwa ajili ya kulihudumia jeshi.
- Musa aliwapa kila kabila la Israeli sehemu ya ardhi ya Kaanani ili waishi.
- Katika sheria ya agano la kale, baadhi ya makabila walipewa kazi ya kuwahudumia makuhani, waimbaji na wajenzi.
- Neno kugawa li naweza kutafsiriwa kama "kuchagua" au "kupewa kazi."

kuhamisha, Uhamisho

Ufafanuzi

Msemo "kuhamisha" una maana ya watu waliolazimishwa kuishi mahali mbali na nchi yao ya nyumbani.

Watu mara kwa mara hutumwa uhamishoni kwa ajili ya adhabu au sababu za kisiasa.

Watu walioshindwa wanaweza kupelekwa uhamishoni katika nchi ya jeshi iliyowashinda ili kuwafanyia kazi.

"Uhamisho wa Babeli" (au "Uhamisho") ni kipindi katika historia ya Biblia ambapo raia wengi wa Kiyahudi wa eneo la Yuda walichukuliwa kutoka nyumbani mwao na kulazimishwa kuishi Babeli. Ilidumu miaka 70.

Msemo "waliohamishwa" una maana ya watu ambao wanaishi katika uhamisho, mbali na nchi yao ya nyumbani.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo wa "kuhamisha" unaweza kutafsiriwa kama "kufukuza" au "kulazimisha kutoka nje" au "kuondoa".

Msemo "Uhamisho" unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo ambao una maana "muda ambao walifukuzwa" au "muda wa kufukuzwa" au "muda wa kulazimishwa kutokuwepo" au "kuondolewa".

Njia za kutafsiri "waliofukuzwa" zinaweza kujumuisha, "watu waliofukuzwa" au "watu ambao waliondolewa" au "watu walifukuzwa kwenda Babeli"

Kuhani mkuu

Ufafanuzi

Kuhani mkuu alikuwa kiongozi wa muhimu sana katika dini ya kiyahudi wakati ambao Yesu aliishi duniani.

- Makuhani mkuu walikuwa na wajibu kwa kila kitu kilichohitajika katika ibada ya kuabudu hekaluni. Pia walikuwa wanasimamia pesa zilizotolewa hekaluni.
- Kilikuwa ni cheo cha juu na chenye nguvu kuliko cha kuhani. Kunahi wa juu ndiye aliyekuwa na mamlaka.
- Makuhani wakuu baadhi yao walikuwa maadui wa Yesu na waliwashawishi sana viongozi wa Kirumi wamkamate Yesu na wamuue.

Kuharibu

Ufafanuzi

Kuharibu kitu ni hali ya kuangamiza, kukiteketeza au kukifanya kisiwe na maana tena.

- Nabii Zefania anazungumza juu ya siku ya ghadhabu ya Mungu kama "siku ya kuharibu" ambapo ulimwengu utahukumiwa na kuadhibiwa.
- Katika kitabu cha Mithali kinasema kuharibu na kuteketeza kunawasubiri wale wasio na Mungu.
- Kutegemeana na mukhtadha kuharibu yaweza kutafsiriwa kama "kuangamiza" au "kufanya isifae" au "kuvunja" au "uharibifu."

Kuhitimu, waliohitimu

Ufafanuzi

Neno "kuhitimu" ni kitendo cha kupata haki ya kupokea faida fulani au kujulikana kwa kuwa na ujuzi fulani.

- Mtu aliyehitimu kwa ajili ya kazi fulani ana ujuzi na amefundishwa kwa ajili ya kazi hiyo.
- Katika barua ya mtume Paulo kwa kanisa la Korintho aliandika kuwa Mungu baba amewafanya waamini kuhitimu katika kushiriki kwenye ufalme wa mwanga.
- Mwamini hawezi kupata haki ya kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu. Bali anahitimu kwa sababu Mungu amemkomboa yeye kwa damu ya Kristo.

Kuhubiri

Ufafanuzi

Kuzungumza na kundi la watu kuwafundisha kuhusu Mungu na kuwasihi wamtii Mungu.

- Mara nyingi kuhubiri hufanywa na mtu mmoja kwa kundi kubwa la watu. Mara nyingi huzungumzwa na sio kuandikwa.
- "kuhubiri" na "kufundisha" ni sawa japo haifanani sana.
- "Kuhubiri" ni kitendo cha kutanganza hadharani ukweli wa kiroho na kuwasihi wasikilizaji watekeleze. "Kufundisha" ni kitendo cha kusisitiza maelekezo yanayotolewa kwa watu au kuwafundisha kitu cha kufanya.
- Neno "kuhubiri" mara nyingi kunaambatana na neno "injili."

Kuinama chini

Ufafanuzi

Kuinama maana yake kujikunja kwa unyenyekevu kuonesha heshima kwa mtu. "Kuinama chini" inamaanisha kupiga magoti chini sana, kwa kawaida uso na mikono ikielekea ardhini.

- Viashiria vingine ni pamoja na "kupiga goti" na "kuinamisha kichwa"(maana yake ni kuinamisha kichwa mbele kwa heshima ya unyenyekevu au katika huzuni).
- Kuinama chini pia kwaweza kuwa ishara ya mfadhaiko au maombolezo. Mtu "anayeinamishwa chini" amewekwa katika kiwango cha chini sana cha unyenyekevu.
- Kwa kawaida mtu atainama mbele ya mtu mwenye heshima ya juu kuliko yake au mwenye umuhimu mkubwa, kama wafalme na viongozi wengine.
- Kuinama mbele ya Mungu ni ishara ya kumwabudu.
- Katika Biblia, watu walimwinamia Yesu walipotambua kutokana na miujiza yake na mafundisho yake kwamba alikuwa ametoka kwa Mungu.
- Biblia inasema kwamba Yesu atakaporudi, kila mtu atapiga goti kumwabudu.

Maoni ya Kutafasiri

- Kwa kutegemea na mazingira, neno hili laweza kutafasiriwa kwa neno au kifungu kinachomaanisha, "kuinamia" au "kuinamisha kichwa" au "piga goti".
- Neno "inama chini" laweza kutafasiriwa kama "Piga magoti" au "jinyenyekesha".
- Baadhi ya lugha zitakuwa na njia zaidi ya moja ya kutafasiri neno hili, kutegemea na mazingira.

kujiamini, ujasiri

Ufafanuzi

Kujiamini ni kuwa na uhakika kuwa jambo fulani ni la kweli au litatokea.

- Katika Biblia neno "tumaini" linamaana ya kusubiri kwa kutegemea jambo fulani litakalotokea. Hii pia imetafsiriwa kama kujiamini hasa inapokuwa na maana ya kuwa na uhakika wa kupokea ambacho Mungu alikiahidi kwa wanaomwamini Yesu.
- Kujiamini inamaana ya uhakika ambao wanaomwamini Yesu wanao kuwa siku moja watakuwa na Mungu mbinguni.
- "kuwa na ujasiri kwa Mungu" inamaana kuwa kutegemea kupokea yale ambayo Mungu ameahidi.
- Kuwa na ujasiri inamaanisha kuwa kuamini katika ahadi za Mungu na kujua kuwa Mungu ataafanya kama alivyosema.

Kujivuna

Ufafanuzi

Kujikweza ni kitendo cha mtu kujivuna au kuwa na majivuno.

- Mtu anayejivuna ana tabia ya kujiona bora kuliko wengine.
- Paulo anazungumza kuwa kufahamu mambo mengi au kujua mambo ya dini kunaweza kusababisha mtu akajivuna.
- Pia inaweza kutafsiriwa kama "kujivunia" au "kuwabeza wengine" au "kujiona bora kuliko wengine."

Kujua kabla

Ufafanuzi

Msemo "kujua kabla" unatokana na maana ya kujua jambo kabla halijatokea.

Mungu hazuiliwi na muda. Anajua kila kitu ambacho hutokea kipindi cha nyuma, sasa na baadaye.

Neno hili mara kwa mara hutumika katika muktadha ya Mungu kujua tayari nani ataokolewa kupitia kumpokea Yesu Kristo.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "kujua kabla" unaweza kutafsiriwa kama "kujua kabla" au "kujua kabla ya wakati" au "kujua kabla ya" au "kujua tayari".

kujua, ufahamu, kufanya kujulikana

Ufafanuzi

"Kujua" inamaanisha kuelewa kitu au kuwa na ufahamu wa jambo. Usemi "kufanya kujulikana" ni usemi unaomaanisha kutoa taarifa.

Neno "ufahamu" linamaanisha taarifa ambazo watu wanajua. Inaweza kuwa kujua vitu katika dunia ya kimwili na kiroho. "Kujua kuhusu" Mungu inamaanisha kuelewa mambo kumhusu kwa sababu ya yale aliyotufunulia. "Kumjua" Mungu inamaanisha kuwa na uhusiano naye. Hii inamaanisha pia kuwajua watu wake. Kujua mapenzi ya Mungu inamaanisha kuwa na ufahamu wa yale aliyetoagiza, au kuelewa ni nini anataka mtu afanye. "Kujua Sheria" inamaanisha kuwa na ufahamu wa yale Mungu aliyoagiza au kuelewa yale Mungu aliyoagiza katika sheria alizompa Musa. Wakati mwingine "ufahamu" unatumika kama neno lingine la "hekima," linalojumuisha kuishi katika njia inayompendeza Mungu. "Ufahamu wa Mungu" wakati mwingine unatumika kama njia nyingine ya kusema hofu ya Yahwe.

kukandamiza, ukandamizaji, mkandamizaji

Ufafanuzi

Meneo, "kukandamiza," "ukandamizaji," "mkandamizaji" ya husu kumtendea mtu kwa ukali. "mkandamizaji" ni mtu anaye kandamiza watu.

- Neno "ukandamizaji" haswa la husu hali watu wa nguvu kubwa wanapo tendea vibaya au kufanya watumwa watu waliyo chini ya nguvu au utawala wao.
- Neno "kukandamizwa" la eleza watu wanao tendewa vibaya.
- Mara nyingi mataifa ya maadui na viongozi wao walikuwa wakandamizaji kwa watu wa Israeli.

Kukataa

Ufafanuzi

"Kukataa" kitu au mtu inamaana kuacha kumkubali mtu au kitu.

- Neno kukataa pia laweza kuwa na maana ya kuacha kuamini kwenye kitu fulani.
- Kumkataa Mungu inamaana kutomtii Yeye.
- Waisraeli walipomkataa kiongozi wao Munsa inamaana kuwa walikuwa wanaasi dhidi ya mamlaka yake. Hawakutaka kumtii.
- Waisraeli walionesha kuwa walimkataa Mungu walipoabudu miungu ya uongo/

Kukatwa

Ufafanuzi

Kukatwa ni kitendo cha kuondolewa, kufukuzwa au kutengwa toka kwenye kundi. Pia inaweza kuwa na maana ya kuuawa kama tendo la hukumu kwa ajili ya dhambi.

- Katika agano la kale kutotii amri za Mungu hupelekea kukatwa au kutengwa na watu wa Mungu na uwepo wake.
- Mungu pia alisema atawakata au kuwaharibu mataifa ambayo sio Waisraeli kwa sababu hawakumwabudu au kumtii yeye na walikuwa maadui wa Israeli.
- Pia kukata inaweza kutumika kuonesha Mungu akisababisha mtu kuacha kutiririsha maji.

Kukemea

Ufafanuzi

Kukemea ni kitendo cha kumrekebisha mtu ili kumsaidia mtu yule kuacha dhambi.

- Katika agano jipya linawaamuru Wakristo wawakemee waamini wengine wanapoacha kumtii Mungu.
- Katika kitabu cha Mithali kinaelekeza wazazi kuwakemea watoto wao wanapoacha kuwa watii.
- Kukemea ni kumzuia mtu aliyetenda dhambi asirudie tena kutenda dhambi.
- Kukemea pia kunaweza kutafsiriwa kama marekebisho.

kukesha

Ufafanuzi

Katika nyakati za Biblia, "kukesha" ulikuwa wakati wa usiku ambao katika huo mlinzi au mwangalizi wa mji alikuwa kazini akiangalia hatari yoyote kutoka kwa maadui.

- Katika Agano la Kale, Waisraeli walikuwa na zamu tatu zikiitwa "mwanzo"(machweo hadi saa 4:00 usiku), "katikati" (saa 4:00 usiku hadi saa 8:00 usiku), na "asubuhi" (saa 8:00 hadi mawio).
- Katika Agano Jipya, Wayahudi walifuata mfumo wa Kirumi na walikuwa na zamu nne, zikiitwa "ya kwanza" (machweo hadi saa 3 usiku) "pili" (3 usiku hadi saa 6 usiku), "tatu" (6 usiku hadi 9 usiku), na ya "nne" (saa 9 hadi mawio).
- Hizi pia zaweza kutafasiriwa kwa vifungu vya jumla kama vile "jioni" au "katikati ya usiku" au "alfajiri," kutegemea na zamu inayotajwa.

Kula

Ufafanuzi

Kula ni kitendo cha kutumia kitu fulani. Pia ina maana nyingine.

- Katika Biblia kutumia inamaana ya kuharibu vitu au watu.
- Moto unaelezewa kula vitu ikiwa na maana ya kuharibu kwa kuviteketeza kwa moto.
- Mungu anajielezea kama moto ulao akiwa na maana ya kuelezea hasira yake dhidi ya dhambi. Hasira yake inasababisha adhabu kali kwa watenda dhambi wasiotubu.
- Kula chakula ni kitendo cha kuchukua na kula chakula au kinywaji.
- "kuila nchi" inamaana ya "kuiharibu nchi."

kulala na, kuwa na mahusiano na, fanya mapenzi

Ufafanuzi

Katika Biblia, haya maneno ni tafsida yanayo eleza kufanya ngono.

- "kulala na" mtu ni namna maarufu ya kueleza kuwa na mahusiano ya kimapenzi.
- Katika Agano la Kale, "Wimbo wa Sulemani," tafsiri ya ULB inatumia "kufanya mapenzi" kutafsiri neno "mapenzi," ambalo katika muktadha la eleza mahusiano ya kingono. Hii ina husiano na msemo, "kufanya mapenzi na."

kulewa, mlevi

Ufafanuzi

Msemo "kulewa" ina maana ya kuleweshwa kutokana na kunywa kileo.

"Mlevi" ni mtu ambaye hulewa mara kwa mara. Mtu wa aina hii anajulikana kama "mlevi".

Biblia inawaambia waumini kutolewa na vilevi, lakini kutawaliwa na Roho Mtakatifu wa Mungu.

Biblia inafundisha ya kwamba ulevi sio busara na inamshawishi mtu kutenda dhambi kwa njia zingine.

Njia zingine za kutafsiri "kulewa" zinaweza kujumuisha "levya" au "kulewa" au "kupata kilevi kingi sana" au "kushiba kwa kinywaji chachu"

kumbukumbu, sadaka ya kumbukumbu

Ufafanuzi

Neno "kumbukumbu" la husu tendo au kitu kinacho msababisha mtu au kitu kukumbukwa.

- Hili neno linatumika kama kitenzi kueleza kitu kitakacho wakumbusha kuhusu kitu, kama katika "sadaka ya kumbukumbu," au "mawe ya kumbukumbu"
- Katika Agano la Kale sadaka ya kumbukumbu ilitolewa ili Waisraeli wakumbuke ni Mungu alicho wafanyia.
- Mungu aliwaambia makuhani wa Kiisraeli kuvaa mavazi maalumu yaliyo kuwa na mawe. Haya mawe yalikuwa na majina ya makabila kumi na mbili ya Israeli yaliyo andikwa juu yake. Hii ilikuwa kuwa kumbusha kuwa uwaminifu wa Mungu kwao.
- Katika Agano Jipya, Mungu alimueshimu mtu mwenye jina Kornelio kwasababu ya matendo yake mema kwa maskini. Haya matendo yalisemwa kuwa "kumbukumbu" mbele za Mungu.

Kumiliki, Miliki

Ufafanuzi

"Kumiliki" au "miliki" ni kitendo cha kuwa na kitu fulani. Pia inaweza kuwa na maana ya kuwa na mamlaka juu ya kitu fulani au kumiliki eneo la ardhi.

- Katika agano la kale neno hili limetumika kama kumiliki ardhi katika eneo.
- Bwana alipowaamuru Waisraeli wamiliki nchi ya Kanaani inamaanisha kuwa walitakiwa kwenda kwenye nchi ile na kukaa huko. Hii inajumuisha kuwashinda watu wa Kanaani waliokuwa wakiishi huko.
- Bwana aliwaambia Waisraeli kwamba amewapa nchi ya Kanaani kama milki yao. Hii inaweza kutafsiriwa kama "sehemu sahihi ya kuishi."

Kumuachia

Ufafanuzi

Neno "kumuachia" lina maana ya kukiri wazu kuwa mtu fulani hana hatia kwa kosa fulani au tabia fulani alikuwa ameshitakiwa.

- Neno hili wakati mwingine kwenye Biblia hutumika kuzungumzia juu ya kusamehewa dhambi.
- Hii inaweza kutafsiriwa kama "kutangaza hana hatia"

kumwaga damu

Ufafanuzi

Neno "kumwaga damu" linamaanisha kifo cha mwanadamu kwa sababu ya mauaji, vita, au sababu nyingine ya kikatiri.

- Neno hili "kumwaga damu," kwa kawaida linamaanisha wakati damu inapotoka katika jeraha katika mwili wa mtu.
- Neno "kumwaga damu" linatumika mara kwa mara kurejerea mauaji ya watu yaliyoenea.
- Lakini pia linatumika kama kumbukumbu ya jumla kwa dhambi ya kuuwa.

Maoni ya Kutafasiri

- "Kumwaga damu" kwaweza kutafasiriwa kama, "mauaji ya watu" au "watu wengi waliouawa".
- "Kupitia umwagaji wa damu" yaweza pia kutafasiriwa kama, "kwa kuuwa watu."
- "Kumwaga damu ya wasio na hatia" yaweza kutafasiriwa kama "kuuwa watu wasio na hatia".
- "Kumwaga damu kunafuata kumwaga damu" kwaweza kutafasiriwa kama, "wanaendelea kuuwa watu" au "kuuawa kwa watu kunaendelea" au "wameua watu wengi na wanaendelea kufanya hivyo" au "watu wanaendelea kuuwa wengine."
- Matumizi mengine ya tamathari, "kumwaga damu kutakufuata" kwaweza kutafasiriwa kama "watu wako wataendelea kushuudia mauaji" au "watu wako wataendelea kuuawa" au "watu wako wataendelea kuwa katika vita na mataifa mengine na watu wataendelea kufa.

Kundi la watu, watu

Ufafanuzi

"Watu" au "kundi la watu" linamaana ya makundi ya watu wenye lugha moja na utamaduni mmoja. Pia yaweza kuwa na maana ya watu waliokusanyika sehemu fulani au kwa ajili ya tukio fulani.

- Mungu alipotenga "watu" kwa ajili yake inamaanisha aliwachagua watu wawe wake na wamtumikie yeye.
- Katika nyakati za Biblia kundi la watu mara nyingi lilikuwa na mababu na waliishi pamoja katika nchi fulani au eneo fulani la nchi.
- Inategemea na lengo katika kifungu fulani "watu wako" inaweza kuwa na maana ya "kundi lako la watu" au "famila yako" au "ndugu zako"
- Neno "Watu" mara nyingi hutumika kuelezea watu wa makundi yote duniani.

kundi, mifugo

Ufafanuzi

Katika Biblia "kundi" ina maana ya kundi la kondoo na mbuzi na "mifugo" ina maana ya kikundi cha ng'ombe, maksai, au nguruwe.

Lugha tofauti zinaweza kuwa na njia tofauti za kutaja makundi ya wanyama au ndege.

Kwa mfano, katika Kiingereza msemo "kundi" unaweza pia kutumika kwa ajili ya kondoo au mbuzi, lakini katika maandishi ya Biblia haitumiki kwa njia hii.

Msemo "kundi" katika Kiingereza pia hutumika kwa ajili ya kundi la ndege, lakini unaweza kutumika kwa ajili ya nguruwe, maksai au ng'ombe.

Fikiria ni misemo gani inatumika katika lugha yako kumaanisha makundi tofauti ya wanyama.

Kwa mistari ambayo ina maana ya "makundi au mifugo" inaweza kuwa bora kuongeza "ya kondoo" au "ya ng'ombe" kwa mfano, kama lugha haina maneno tofauti kumaanisha aina tofauti za makundi ya wanyama.

kuomba

Ufafanuzi

Neno "kuomba" lamaanisha kumwomba mtu kitu fulani kwa umuhimu. Mara kwa mara inamaanisha kuomba pesa, lakini pia limetumika kuonesha kuombeleza jambo fulani.

- Mara kwa mara watu wanaomba wakati wanapoitaji jambo fulani kwa uzito, lakini wasijue kwamba kuna mtu atawapa waombacho.
- "Mwombaji" ni mtu ambaye mara kwa mara hukaa au kusimama katika maeneo ya wazi kuomba pesa kwa watu.
- Kwa kutegemea mazingira, neno hili lingetafsiriwa kama "kusihi" "omba kwa uzito" "kudai pesa" au "kuomba pesa mara kwa mara."

kuomboleza

Ufafanuzi

"Kuomboleza" kwa husu huzuni ya ndani, mara nyingi wakati wa kifo cha mtu.

- Katika tamaduni nyingi, kuomboleza kuna kuna husisha matendo ya njee yanayo onyesha uzuni.
- Waisraeli na watu wengine zama za kale walionyesha kwa kilio kikubwa. Pia walivaa nguo za magunia na majivu.
- Waombolezaji wakuajiriwa, wanawake sana sana, walilia kwa sauti kutoka kipindi cha kifo hadi mwili kuzikwa kaburini.
- Kipindi cha kuomboleza kilikuwa siku saba, lakini ziliweza kwenda hadi siku thelathini (kama Musa na Aruni) au siku sabini (kama za Yakobo)

kupiku

Ufafanuzi

Neno "kupiku" ina maana ya kupata uweza juu ya mtu au kitu. Mara nyingi ina maana ya kufikia kitu na kukipita baada ya kukufukuzia.

- Wakati majeshi "yakipiku" adui, ina maana wamemshinda adui vitani.
- Mnyama mwindaji anapo piku windo lake, ina maana kuwa imemkimbiza na kumkamata adui yake.
- Kama laana "ikipiku" mtu, ina maana kuwa chochote kilicho semwa kwenye laana hiyo kitatokea.
- Kama baraka zita wapiku watu, ina maana kuwa hao watu watapata hizo baraka.
- Kulingana na muktadha, "kupiku" ya weza tafsiriwa kama "kushinda" au "kuchukuwa" au "kufikia"
- Linapo tumika kama onyo kuwa giza au adhabu lita pikuwa watu kwasababu ya dhambi zao, ina maana kuwa hao watu watapata vitu vibaya kama wasipo tubu.

Kupokea

Ufafanuzi

Kupokea ni kupata au kukubali kitu unachopewa au kuletewa.

- "Kupokea" pia yaweza kumaanisha kuteseka au kupitia jambo fulani kama "alipokea adhabu kwa alichokifanya."
- Pia kuna namna ya pekee ya kumpokea mtu. Kwa mfano kumpokea mgeni inamaanisha kumkaribisha na kumfanyia jambo la heshima ili kujenga mahusiano naye.
- "Kupokea zawadi ya roho mtakatifu" inamaanisha tumepewa roho mtakatifu na kumkaribisha afanye kazi kwenye maisha yetu.
- Kumpokea Yesu inamaana kukubali wokovu wa Yesu kwa njia ya Yesu Kristo.
- Yule kipofu alipopokea uponyaji inamaana kuwa Mungu alimponya na kumuwezesha kuona tena.

Kupotea, akipotea, kupotoshwa

Ufafanuzi

Kupotea ina maana ya kutomtii Mungu. Watu wanaopotoshwa wamewaruhusu watu wengine kuwasababisha wasimtii Mungu.

- Kupotea inatuppa picha sahihi ya kuacha njia nzuri au sehemu salama na kwenda njia mbaya au sehemu yenye hatari.
- Kondoo wanaoacha malisho wanayopewa na mchungaji wao Mungu anawafananisha wa watu waliomuacha yeye.

kupumua, pumzi

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "kupumua" na "pumzi" yanatumika mara kwa mara kitamathari kumaanisha kutoa uhai au kuwa na uhai.

- Biblia inafundisha kwamba Mungu "alimpulizia" Adamu pumzi ya uhai. Ikawa Adamu akawa kiumbe hai.
- Wakati Yesu alipowapulizia wanafunzi na kuwaambia "pokeeni Roho," pengine kiualisia alipulizia hewa kwao kumaanisha "Roho Mtakatifu kuja kwao.
- Wakati mwingine neno "kupumua" na "kupumua nje" yanamaanisha kuongea.
- Kifungu cha kitamathali "pumzi ya Mungu" au "pumzi ya Yahwe" mara kwa mara inarejerea gadhabu ya Mungu ikimiminwa kwa uasi au mataifa yasiyomcha Mungu. Inaonesha nguvu yake.

Maoni ya Kutafasiri

- Kifungu "alipumua mara ya mwisho" inamaanisha kusema "alikufa." Inaweza pia ikatafasiriwa kama, "alichukua pumzi yake ya mwisho" au "aliacha kupumua na akafa" au "alivuta pumzi mara ya mwisho."
- Kuelezea Maandiko kama "Pumze ya Mungu" inamaanisha Mungu alisema au aliyatia nguvu maneno ya Maandiko ambayo baadaye wanadamu waliandika. Pengine inafaa zaidi, ikiwa inawezekana, kutafasiri "enye kupuliziwa na Mungu" kwa kawaida kwa kuwa ni vigumu kuwasilisha maana yake halisi.
- Ikiwa tafasiri ya moja kwa moja ya "enye pumzi ya Mungu" haikubaliki, njia nyingine yaweza kutumika, "kuongozwa na Mungu" au "kuandikwa na Mungu" au "kusemwa na Mungu." Yaweza pia kusemwa kwamba "Mungu alipuliza neno la Maandiko."
- Kifungu "kuweka pumzi ndani" au kupulizia uhai ndani ya" au "kutoa uhai kwa" yaweza kutafisiriwa kama, "kusababisha kupumua" au "kufufua" au "kuwawezesha kuishi na kupumua" au "kumpa uzima."
- Ikiwa inawezekana, ni vema kutafasiri "pumzi ya Mungu" kwa neno halisi litumikalo kwa "pumzi" katika lugha. Ikiwa Mungu hasemwi kuwa na "pumzi" hii itafasiriwe kama "nguvu ya Mungu" au "sauti ya Mungu."
- Kifungu "shika pumzi yangu" au "pata uzima wangu" itafasiriwe kama, "tulia ili upumua taratibu" au "acha kukimbia ili upumue kawaida.
- Kifungu "ni pumzi tu" chamaanisha "inaishia kitambo kidogo".
- Vilevile kifungu "mtu ni pumzi moja" chamaanisha "watu huishi muda mfupi sana" au "maisha ya wanadamu ni mafupi sana, kama pumzi moja" au "kwa kulinganisha na Mungu, maisha ya mtu yaonekana mafupi sana kama inavyochukua kuvuta pumzi mara moja."

kura, kupiga kura

Ufafanuzi

"Kura" ni kitu kilichowekwa alama kinachochaguliwa miongoni mwa vitu vya kufanana kama naamna ya kuamua jambo. "Kupiga kura" inamaanisha kurusha vitu vilivyo wekwa alama kwenye sakafu au ardhi yoyote.

Mara nyingi kura yalikuwa mawe madogo yenye alama au vipande vidogo vilivyovunjika vya udongo. Tamaduni zingine zinafanya "bahati nasibu" au "kuvuta" kura kwa kutumia majani makavu. Mtu anayashikilia majani makavu ili asiwepo wakuona yana urefu gani. Kila mtu anavuta jani na yule atakayepata jani kavu refu zaidi (au fupi) ndiye atakayekuwa amechaguliwa. Zoezi la kupiga kura lilitumika na Waisraeli kujua ni nini Mungu aliwataka wafanye. Kama nyakati za Zekaria na Elisabeti, ilitumika pia kuchagua ni kuhani yupi atatenda jukumu bayana hekaluni katika muda maalumu. Askari walio msulubisha Yesu walipiga kura kuamua ni nani atakaa na joho la Yesu. Usemi "kupiga kura" inawezakutafsiriwa kama "kufanya bahati nasibu" au "kurusha kura". Kulinga na mazingira, neno "kura" inaweza pia kutafsiriwa kama "jiwe lenye alama" au "kipande cha udongo" au "kijiti" au "kipande cha jani." Kama maamuzi yakifanyika "kwa kura" hii inaweza kutafsiriwa kama "kufanya bahati nasibu (au kurusha) ya kura."

kusaliti

Ufafanuzi

Neno "kusaliti" lamaanisha tendo la kumdanganya na kumdhuru mwingine. "Msaliti" ni mtu amsalitiye rafiki yake mwenye kumwamini.

- Yuda alikuwa "msaliti" kwa sababu aliwaeleza viongozi wa Kiyahudi jinsi ya kumkamata Yesu.
- Tendo la Yesu kuwalitiwa na Yuda ulikuwa uovu kwa sababu alikuwa mwanafunzi wake aliyepokea pesa kama malipo juu ya habari aliyowapa ya kumkamata Yesu kwa kifo kisicho cha haki.

Maoni ya Tafasiri

- Kwa kutegemea mazingira, neno "kusaliti" laweza kutafasiriwa kama "kudanganya na kusababisha madhara" au "kumsaidia adui" au "kufanya uhaini."
- Neno "msaliti" laweza kutafasiriwa kama "mtu asalitiye" au "mfanya biashara mbili" au "msaliti."

kusanya, kukusanya

Ufafanuzi

Msemo "kusanya" una maana ya kupita katika shamba au shamba la matunda kuokota nafaka yoyote au tunda ambao wavunaji wameacha nyuma.

Mungu aliwaambia Waisraeli kuruhusu wajane, watu maskini, na wageni kukusanya mabaki ya nafaka ili kwamba wapate chakula kwa ajili yao.

Mara nyingine mmiliki wa shamba angeruhusu wakusanyaji kwenda moja kwa moja nyuma ya wavunaji kukusanya, ambayo iliwawezesha wao kukusanya nafaka zaidi.

Mfano wa wazi ni jinsi hii ilivyofanya kazi katika simulizi ya Ruhtu, ambaye aliruhusiwa kwa ukarimu kukusanya miongoni mwa wavunaji katika mashamba ya ndugu wa Boazi.

Kushangaa, kushangaza

Ufafanuzi

"Kushangaa" ni hali ya mshangao na heshima kubwa inayokuja baada ya kuona jambo kubwa limefanyika na lenye nguvu.

- "kushangaza" ni hali ya mtu au kitu kusababisha hali ya kushangaa.
- Maono ya utukufu wa Mungu aliyoyaona nabii Ezekieli yalikuwa ya kushangaza.
- Katika kuonesha hisia za kibinadamu pale ambapobinadamu anatambua kuwa Mungu anashangaza mara nyingi huogopa, husujudu au kupiga magoti, hufunika uso wake na kutetemeka.

Kushangaa, mshangao

Ufafanuzi

Maneno haya yote yanamaana ya kushangazwa kwa sababu ya jambo fulani lisilo la kawaida ambalo limetokea.

- Baadhi ya maneno haya yanatafsiriwa kwa Kigiriki yakiwa na maana ya "akapigwa kwa mshangao." Hii inaelezea ni kwa namna gani mtu amejisikia baada ya kushanganwa na jambo fulani.
- Mara nyingi tukio linalosababisha mshangao ni muujiza ambao Mungu pekee ndo mwenye uwezo wa kufanya.
- Maana nyingine ya maneno haya hujumuisha hisia za kuchanganyikiwa kwa sababu jambo lililotokea halikutegemewa kabisa.
- Kwa ujumla maneno haya hutumika kwa mtazamo chanya kwamba watu wana furaha juu ya jambo fulani lililotokea.

Kusifu

Ufafanuzi

Kumsifu mtu ni kuonesha pongezi au heshima kwa mtu yule.

- Watu wanamsifu Mungu kwa namna alivyo mkuu na kwa sababu ya mambo ya ajabu anayoyafanya kama muumbaji na mwokozi wa dunia.
- Kumsifu Mungu kunajumuisha kumshukuru kwa aliyoyafanya.
- Muziki na kuimba hutumiwa kama njia ya kumsifu Mungu.
- Kumsifu Mungu ni sehemu ya kumwabudu.
- Neno "kusifu" yaweza kutafsiriwa kama "kusema mazuri" au "kusifia kwa maneno."

Kusihi, ng'ang'ania

Ufafanuzi

"Kusihi" inamaana ya kumuomba mtu afanye jambo fulani. Ng'ang'ania ni ombi la haraka.

- Kusihi ni kitendo cha mtu kuwa katika hali ya uhitaji mkubwa na anahitaji msaada.
- Watu wanaweza wakamsihi Mungu kwa haraka awahurumie au kumuomba awapatie kitu fulani kwa ajili yao au kwa ajili ya watu wengine.
- Njia nyingine za kutafsiri neno hili yaweza kuwa "kuomba."

kusimika

Ufafanuzi

Kusimika kuna maana ya kuteuwa mtu kwa kazi maalumu au jukumu. Pia ina maana ya kufanya uamuzi au tamko.

- Neno "kusimika" mara nyingi umaanisha kuteuwa mtu kuwa kuhani, mtumushi, au rabi.
- Kwa mfano, Mungu aliwasimika Aruni na uzao wake kuwa makuhani.
- Lina weza kuanzisha au kuimarisha kitu, kama sherehe ya dini au agano.

Kusujudu

Ufafanuzi

Kusujudu ni kitendo cha kuinamisha uso chini kwenye ardhi.

- "Kusujudu" mbele ya mtu kuna maana ya kuinama mbele ya huyo mtu.
- Kitendo cha kusujudu ni kitendo cha kuonesha hofu kwa sababu muujiza fulani umetokea. Pia inaonesha heshima kwa mtu anayesujudiwa.
- Kusujudu pia ni njia moja wapo ya kumwabudu Mungu. Watu wengi walifanya hivi kwa Yesu kama kumshukuru na kumwabudu baada ya kufanya muujuza fulani au kuonesha heshima kwa mafundisho yake mazuri.

Kusukuma

Ufafanuzi

Hiki ni kitendo cha kuhamisha kitu kimwili kwa kutumia nguvu. Kuna maana mbali mbali za neno hili

- "Kusukuma mbali" inamaana ya "kukataa" au "kukataa kusaidia."
- "Kusukumachini" inamaana ya "kunyanyasa" au "kutesa." Pia yaweza kuwa namaana ya kusukuma kitu kwenda chini.
- "Kusukuma mbele" inamaana ya kuvumilia au kuendelea kufanya jambo.

Kutangaza, tangazo

Ufafanuzi

Kutanganza ni kitendo cha kutoa tamko hadharani.

- Katika Biblia kutangaza nikutamka hadharani jambo ambalo Mungu ameliamuru au kuwaambia wengine juu ya Mungu na namna alivyo mkuu.
- Katika agano jipya mitume walitangaza habari njema kuhusu Yesu kwa watu wengi katika miji mingi na mikoa.
- Pia kutamka yaweza kutumiwa kama amri anayotolewa na wafalme kwa kupinga uovu katika jamii.
- Neno "tangazo" pia laweza kutafsiriwa kama "kuhubiri hadharani."

Kutawala

Ufafanuzi

Neno "kutawala" linamaana ya kuongoza kama mfalme juu ya watu wa nchi fulani au ufalme. Utawala wa kifalme ni wakati ambao mfalme alitawala.

- Kutawala pia kunamuelezea Mungu anayetawala kama mfalme wa ulimwengu mzima.
- Mungu aliwaruhusu wafalme wa kibinadamu kutawala juu ya Israeli walipomkataa yeye kama mfalme.
- Yesu atakaporudi atatawala kama mfalme juu ya ulimwengu wote na Wakristo watatawala pamoja naye.
- Hii pia yaweza kutafsiriwa kama "kutawala kama mfalme" au "kuongoza kama mfalme."

Kutoboa

Ufafanuzi

"Kutoboa" ni kitendo cha kuchoma kitu kwa kutumia kitu chenye ncha. Pia hutumika kuelezea tendo la kusababisha maumivu makali ya kihisia kwa mtu.

- Askari walimtoboa Yesu ubavuni alipokuwa msalabani.
- Katika nyakati za Biblia mtumwa aliyeachiwa huru alitobolewa sikio kama ishara kuwa alichaguliwa kuendelea kufanya kazi kwa Bwana wake.
- Simeoni anazungumza kwa lugha ya picha kumwambia maria kuwa upanga utatoboa moyo wake akimaanisha kuwa atapitia maumivu makali kwa kitakachotokea kwa Yesu mtoto wake.

Kutupwa nje, kutupa nje

Ufafanuzi

"kutupwa nje" mtu au "kutupa nje" kitu inamaanisha kulazimisha kitu au mtu kuondoka.

- Neno "kutupa" inamaanisha "kurusha." Kutupa nyavu inamaanisha kurusha nyavu.
- Kumtupa mtu nje yaweza kuwa na maana ya kumkataa mtu na kumuondoa.

Kuvika

Ufafanuzi

Kujivika na kitu ni kutafuta kuwa na tabia fulani.

- Katika hali ya kawaida ya kuvaa inaonekana nje ya mwili wako na watu wote pia unapojivika tabia fulani nzuri watu wengine huona. "Kujivika wema" ina maana ya kuacha tabia zako zioneshe wema ambao utaonekana kwa kila mtu.
- Kujivika nguvu toka juu ni kuwa na nguvu utakayopewa.
- Pia neno hili linaweza kuwa na maana hasi kama "kujivika aibu" au "kujivika hofu."

Kuvuna, mvunaji

Ufafanuzi

Kuvuna inamana ya kuvuna mazao kama nafaka. Mvunaji ni mtu anayevuna mazao.

- Mara nyingi mvunaji huvuna mavuno kwa mkono kwa kung'oa mmea au kukata kwa kifaa chenye ncha kali.
- Kuvuna mavuno pia hutumika kama lugha ya picha ikiwaelezea watu habari njema kuhusu Yesu na kuwaleta katika familia ya Mungu.
- Pia huelezea matokeo anayoyapata mtu kutokana na matendo yake. "mtu atavuna alichokipanda.

Kuwa "tasa" maana yake ni kutoweza kuzaa.

Ufafanuzi

Ardhi au nchi ambayo ni tasa haiwezi kuotesha mmea wowote. Mwanamke tasa ni yule asiyeweza kuzaa mto.

Maoni ya Tafasiri Neno "tasa" linapotumika kurejerea nchi, lingeweza kutafasiriwa kama "isiyozaa" "isiyozalisha" au "isiyo na mimiea." Linapotumika kumtaja mwanamke mgumba, liliweza kutafasiriwa kama "asiye na mtoto" au "asiyeweza kuzaa watoto" au "asiyeweza kutunga mtoto."

Kuwatesa, mateso

Ufafanuzi

"Kuwatesa" au "mateso" ni kitendo endelevu cha kumfanyia mtu au kundi la watu kitu katika namna mbaya ya kuwasababishia madhara.

- Mateso yanaweza kuwa dhidi ya mtu mmoja au watu wengi na mara nyingi huhusisha mashambulizi ya kuendelea.
- Waisraeli waliteswa na makundi mbalimbali ya watu waliowavamia, wakawakamata na kuwaibia vitu vyao.
- Mara nyingi watu huwatesa watu wengine wenye dini tofauti na wao au wanyinge.
- Dini ya Kiyahudi walimtesa Yesu kwa sababu hawakupenda alichokuwa akifundisha.
- Baada ya Yesu kurudi mbinguni viongozi wa kidini wa Kiyahudi na serikali ya Rumi iliwatesa wafuasi wake.
- "Mateso" pia yanaweza kutafsiriwa kama "manyanyaso."

kuza

Ufafanuzi

Neno "kuza" lina maana ya kufanya kitu au mtu mkubwa au kuvuta umakini kwa ukuu wa mtu.

- Linapo tumika kwenye Biblia, "kuza" mara nyingi la husu kutukuza mfalme au Mungu mwenyewe.
- Mtu anapo jikuza yeye, ina maana ana jisifu na kujaribu kujifanya wa muhimu zaidi kuliko wengine.

kuzidisha

Ufafanuzi

neno "kuzidisha" lina maana ya kuongezeka kiidadi. Pia yaweza kusababisha kitu kuongezeka kwa kiasi, kama vile kuzidisha maumivu.

- Mungu aliwaambia wanyama na binadamu "kuongezeka" na kujaza dunia.
- Yesu alifanya mkate na samaki kuongezeka ili kulisha watu 5000. Kiasi cha chakula kiliendelea kuongezeka kiasi kwamba kulikuwa na chakula zaidi kumlisha kila mtu.
- Kulingana na muktadha, hili neno la weza tafsiriwa kama"ongeza"
- Neno "kuongeza maumivu yako sana" ya weza tafsiriwa kama "maumivu yako kuwa makali sana"
- "Kuzidisha farasi" ina maana ya "kuongeza farasi zaidi kwa tamaa"

kuzika, zika

Ufafanuzi

Neno "zika" kwa kawaida linamaanisha kuweka kaburini mwili wa mtu aliyekufa. Neno "kuzika" ni kitendo cha kuzika kitu au linaweza kutumika kueleza sehemu itumikayo kuzikia.

- Mara kwa mara watu uzika maiti kwa kuweka katika kaburi ardhini na kufukia kwa udongo
- Wakati mwingine mwili huwekwa katika kitu chenye muundo wa boksi, kama vile jeneza kabla ya kuzika.
- Nyakati za Biblia, mara kwa mara wafu walizikwa katika pango au eneo linalofanana na hilo. Baada ya Yesu kufa, mwili wake ulifunikwa kwa sanda na kuwekwa katika kaburi mwambani lililowekwa mhuri mkubwa.
- Maneno "makaburini" au "chumba cha kuzikia" au "sehemu ya kuzikia" au "pango la kuzikia" yote kwa ujumla yanamaanisha mahali wafu wanapozikwa.
- Vitu vingine pia vyaweza kuzikwa, kwa mfano Akani alifukia fedha na vitu vingine alivyokuwa ameviiba huko Yeriko.
- Kirai "alifunika uso wake" kwa kawaida humaanisha, "kufunika uso kwa kutumia mikono."
- Wakati mwingine neno "ficha" laweza kumaanisha "fukia" kama Akani alivyoficha ardhini vitu alivyokuwa ameviiba kutoka Yeriko. Hii inamaanisha alivifukia ardhini.

Kuzima

Ufafanuzi

"Kuzima" inamaana kutoa au kusimamisha kitu ambacho kinatakiwa kikamilike.

- Neno hili linatumika kwenye mukhtadha wa kuzima kiu na inamaana ya kusababisha kiu isimame kwa kunywa kitu.
- Pia yaweza kutumika kama kutoa nje ya moto.
- Kiu na moto vyote huzimwa na maji.
- Paulo anatumia neno kuzima akiwa anamaanisha kuwa waamini "wasimzimishe Roho mtakatifu." Hii inamaana kuwa wasiwazuie watu kumruhuru Roho mtakatifu kuzalisha matunda yake na zawadi ndani yao. Kumzimisha Roho mtakatifu inamaana kumzuia Roho mtakatifu asidhihirishe nguvu zake na kufanya kazi ndani ya watu.

kwato,

Ufafanuzi

Hizi ni sehemu ngumu za chini katika miguu ya wanyama kama vile ngamia, ng'ombe, farasi, punda, nguruwe, kondoo, mbuzi n.k Kwato za wanyama humlinda mnyama anapokuwa anatembea Baadhi ya wanyama wana kwato zilizogawanyika katika sehemu mbili, na wanyama wengine wana kwato ambazo hazijagawanyika.

la kumi, zaka

Ufafanuzi

Maneno "la kumi" na "zaka" yanaeleza "asilimia ya kumi" au "moja-kati-ya -sehemu- ya-kumi" ya pesa, mazao, mifugo, au mali za mtu anazo mpa Mungu.

- Katika Agano la Kale, Mungu aliwaelekeza Waisraeli kueka kando asilimia kumi ya mali zao kutoa kama sadaka ya shukurani kwake.
- Hii sadaka ilitumika kufadhili kabila la Walawi wa Israeli waliyo tumikia Waisraeli kama makuhani na watunzi wa maskani na baadae, hekalu.
- Katika Agano Jipya, Mungu haitaji asilimia kumi, lakini na waelekeza waamini kutoa kwa furaha na kwa hiari kusaidia watu wenye mahitaji na kufadhili huduma ya Kikristo.

lala, kulala, aliye lala

Ufafanuzi

Haya maneno yana maana ya kimafumbo kuhusu kifo.

- "lala" au "kulala" yaweza kuwa umbo linalo maanisha "kufa"
- Msemo "aliye lala" yaeleza kipindi mtu anapo anza kulala, au kimfano, wakati mtu anapo kufa."
- "kulala na mababu"

lango, nguzo ya lango

Ufafanuzi

"Lango" ni kizuizi chenye bawaba katika njia ya kufikia ya uzio au ukuta ambao huzunguka nyumba au mji. "Nguzo ya lango" ina maana ya nguzo ya chuma au mbao ambayo inaweza kusogezwa katika sehemu kufunga lango.

Lango la mji linaweza kufunguliwa kuruhusu watu, wanyama, na mizigo kusafiri ndani na nje ya mji.

Kulinda mji, kuta zake na malango ilikuwa nene na imara. Malango yalifungwa na kukazwa na nguzo ya chuma au mbao kuzuia wanajeshi wa maadui kuingia mji.

Lango la mji mara kwa mara ilikuwa kiini cha habari na katikati ya jamii ya kijiji. Pia ilikuwa mahali ambapo mihamala ya kibiashara hufanyika na hukumu kufanyika, kwa sababu kuta za mji zilikuwa na unene wa kutosha kuwa na njia ambayo ilitoa kivuli cha baridi kutoka kwa jua kali. Raia walifurahia kukaa chini ya kivui na kufanya biashara zao na pia kuhumu masuala ya kisheria.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, njia zingine za kutafsiri "lango" inaweza kuwa "mlango" au "uwazi wa ukuta" au "kizuizi" au "njia ya kuingia".

Msemo "nguzo za lango" unaweza kutafsiriwa kama "komeo za lango" au "mihimili ya mbao ya kufunga lango" au "chuma cha kufunga lango"

Laumu

Ufafanuzi

Kumlaumi mtu ni kumkosoa au kukataa matendo au tabia za mtu. Kulaumu ni maoni hasi kuhusu mtu.

- Kusema kwamba mtu huyu "hana lawama" inamaanisha kuwa anaishi kwa namna ya kuheshimu njia za Mungu hivuo kuna kidogo au hamna kabisa kitu ambacho kitasababisha akosolewe.
- Laumu pia yaweza kutafsiriwa kama "aibu" au "kulaumiwa."

Lia, kupiga kelele

Ufafanuzi

Lia au piga kelele inamaana ya kusema kitu kwa nguvu au ghafla. Kupiga kelele kwa maumivu au hasira.

- Kupiga kelele inamaanisha kuita kwa nguvu kwa lengo la kuomba msaada.
- "Nakulilia wewe" inaweza kutafsiriwa kama "nakuita unisaidie" au "ninakuomba msaada."

lsio huru, kuwa chini ya, chini ya

Ufafanuzi

Neno "sio huru" la eleza kuwa chini ya mamlaka ya mtu. Maneno "kuwa chini ya" ni amri inayo maanisha "tii" au "nyenyekea mamlaka ya."

- Msemo "chini ya" ya eleza kusababisha watu kuwa chini ya mamlaka ya kiongozi au mtawala.
- "Kumueka mtu chini ya kitu" ina maana kusababisha huyo mtu kupitia kitu hasi, kama adhabu.

maangamizi

Ufafanuzi

Msemo "maangamizi" una maana ya hukumu ya shutuma ambayo haina uwezekano wa rufaa au utorokaji.

Taifa la Israeli lilipochukuliwa mateka Babeli, nabii Ezekieli alisema, "maangamizi yamekuja juu yao".

Kutegemea na muktadha, msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "maafa" au "adhabu" au "uharibifu usio na matumaini".

Madhabahu ya kufukizia.

Ufafanuzi

Madhabahu ya kufukizia ilikuwa sehemu ya samani ambayo kuhani aliitumia kuchoma uvumba kama sadaka kwa Mungu. Ilikuwa inaitwa madhabahu ya dhahabu.

- Madhabahu ya kufukizia ilitengenezwa kwa mbao, pembeni na juu yake ilifunikwa kwa dhahabu. Ilikuwa kama nusu mita kwa urefuna nusu mita upana.
- Kila siku asubuhi na jioni kuhani alifukiza uvumba.
- Hii inaweza kutafsiriwa kama "madhabahu ya kuchoma uvumba" au "madhabahu ya dhahabu" au "madhabahu ya kufukizia" au "meza ya kufukizia."

mafuriko

Ufafanuzi

Msemo "mafuriko" ina maana ya kiasi kikubwa cha maji ambacho kinafunika juu ya nchi.

Msemo huu pia hutumika kitamathali kumaanisha kiasi kikubwa cha kitu, haswa kitu ambacho hutokea ghafla.

Katika kipindi cha Nuhu, watu walikuwa waovu hadi Mungu akasababisha mafuriko duniani kote kuwa juu ya uso wote wa dunia, hata kufunika juu za milima. Kila mtu ambaye hakuwa katika mtumbwi pamoja na Nuhu alizama. Mafuriko yote mengine hufunika eneo dogo la nchi.

Msemo huu pia unaweza kuwa tendo kama, "nchi ilifurika na maji ya mto".

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia za kutafsiri maana halisi ya "mafuriko" inaweza kujumuisha, "maji yanayomwagikia" au "kiasi kikubwa cha maji"

Mlinganisho wa kitamathali, "kama mafuriko" unaweza kukaa na msemo halisi, au msemo mbadala unaweza kutumika ambao una maana ya kitu ambacho kina hali ya kutiririka kwake, kama vile mto.

Kwa msemo "kama mafuriko ya maji" pale ambapo maji yametajwa tayari, neno "mafuriko" linaweza kutafsiriwa kama "kiasi kikubwa sana" au "yanayomwagikia".

Msemo huu unaweza kutumika kama sitiari kama, "usiruhusu mafuriko kunizoa juu yangu", ambayo ina maana ya "usiruhusu maafa haya makubwa kutokea kwangu" au "usiniache niteketezwe kwa maafa" au "usiache hasira yako initeketeze".

mafuta

Ufafanuzi

Mafuta ni maji mazito yanayo chukuliwa kutoka kwenye mimea au matunda. Katika Biblia, mafuta yalito kwenye mizeituni.

- Mafuta ya mizeituni utumika kupika, kupaka, kutoa dhabihu, taa, na dawa.
- Zama za kale, mafuta ya mizeituni yalikuwa na gharama na kuwa na mafuta ni kipimo cha utajiri.

Maji

Ufafanuzi

Pamoja na maana yake ya kawaida maji yaweza kuwelezea vyanzo vya maji kama vile bahari, mto au ziwa.

- Pia maji yanaweza kuelezea majanga makubwa, majaribu na mateso. Kwa mfano Mungu ameahidi kuwa tukipita katika maji mengi atakuwa pamoja nasi.
- Maji mengi inasisitiza ni kwa namna gani mambo yalivyo magumu.
- Kunywesha wanyama inamaanisha kuwapatia maji. Katika nyakati za Biblia ilijumuisha kuchota maji na ndoo na kuyamimina kwenye chombo kwa ajili ya wanyama kunywa.
- Katika agano jipya Mungu anaelezwa kama maji yaliyo hai kwa watu wake. Hii inamaanisha kuwa yeye ndo chanzo cha nguvu na raha.
- Katika agano jipya Yesu anatumia neno maji yaliyo hai kuelezea kazi za roho mtakatifu ndani ya mtu katika kumgeuza na kumpa maisha mapya.

majivu, vumbi

Ufafanuzi

Majivu ni vumbi la kijivu linalobaki baada ya kuni kuungua. Hutumika pia kama lugha ya picha kuonesha kitu kisicho na thamani.

- Kwenye Biblia mara nyingine neno "vumbi" linatumika kuzungumzia majivu. pia inaweza kuwa uchafu unaotoka katika ardhi kavu.
- "Majivu mengi" ni sawa na kusema "rundo la majivu."
- Zamani kukaa kwenye majivu ilikuwa ishara ya kuomboleza.
- Wakati wa kuomboleza, ilikuwa ni tamaduni kuvaa mavazi ya magunia, kukaa kwenye majivu nakujipaka majivu kwenye kichwa.

Majuto

Ufafanuzi

"majuto" maana yake ni maumivu makali au dhiki.

- Majuto yanaweza kuwa ya kimwili au maumivu ya kihisia.
- Mara nyingi watu wenye majuto huonesha hata kwenye nyuso na tabia zao.
- Mfano mtu mwenye maumivu makali au majuto anaweza kusaga meno yake au kulia kwa sauti.
- Neno "majuto" linaweza kutafsiriwa pia kama "dhiki ya kihisia" au "maumivu ya ndani.

Makabila kumi na mbili ya Israeli

Ufafanuzi

Makabila kumi na mbili inamaanisha watoto kumi na mbili wa Yakobo na uzao wao. Yakobo alikuwa mjukuu wa Abrahamu. Baadae Mungu alibadili jina lake na kumuita Israeli. Haya ndio majina ya makabila ya Israeli; Rubeni, Simoni, Lawi, Yuda, Naftali, Gadi, Asheri, Isakari, Zabuloni, Yusufu na Benjamini. Kizazi cha Lawi hakikurithi nchi ya Kaanani kwa sababu lilikuwa kabila la Kikuhani waliotengwa kumtumikia Mungu na watu wake. Yusufu alipokea urithi wa ardhi mara mbili ambapo aliwapatia watoto wake wawili Efraimu na Manase. Kuna mahali pengine kwenye Biblia orodha ya makabila kumi na mbili yamenukuliwa tofauti. Sehemu nyingine Lawi, Yusufu na Dani hawakuwekwa kwenye orodha na sehem nyingine watoto wawili wa Yusufu Efraimu na Manase wamewekwa kwenye orodha.

makapi

Ufafanuzi

Makapi ni ganda kavu linalolinda mbegu ya nafaka. Makapi sio mazuri kwa chakula hivyo watu hutenganisha na mbegu na kuyatupa.

- Makapi hutenganishwa na mbegu kwa kupeta nafaka juu ya hewa. Upepo hupeperusha makapi na mbegu huanguka chini. Hii huitwa kupeta.
- Katika Biblia Neno hili hutumika kuelezea watu waovu na uovu, au vitu visovyofaa.

Makerubi, Kerubi

Ufafanuzi

Kerubi ni umoja na makerubi ni wingi. Hivi ni viumbe vya pekee vya mbinguni alivyoviumba Mungu. Biblia inawaelezea makerubi kuwa wana mabawa na moto.

- Makerubi wanadhihirisha utukufu na nguvu za Mungu na pia ni walinzi wa vitu vitakatifu.
- Baada ya Adamu na Eva kutenda dhambi Mungu aliweka makerubi wenye upanga wa moto katika upande wa mashariki mwa bustani ya Edeni ili mtu yeyote asiweze kuupata mti wa uzima.
- Mungu aliwaamuru Waisraeli kuchonga makerubi wawili wanaoangaliana mabawa yao yakiwa yamegusana kwenye mfuniko wa upatanisho wa sanduku la agano.
- Pia aliwaambia wafume picha za makerubi katika mapazia ya maskani.
- Katika vifungu vingine viumbe hawa wameelezewa kuwa na nyuso nne, ya mtu, simba, ng'ombe na malaika.
- Makerubi wakati mwingine wanadhaniwa kuwa ni malaika japokuwa Biblia haijaeleza hivyo.

Malkia

Ufafanuzi

Malkia ni kiongozi mwanamke wa nchi fulani au mke wa mfalme.

- Esta alikuja kuwa Malkia wa himaya ya Uajemi alipoolewa na mfalme Ahusuero.
- Malkia Yezebeli alikuwa mke muovu wa mfalme Ahabu.
- Malkia wa Sheba alikuwa kiongozi maarufu aliyeenda kumtembelea mfalme Sulemani.

Mambo ya nyakati

Ufafanuzi

Mambo ya nyakati ni kumbukumbu zilizoandikwa kwa kipindi fulani cha wakati.

- Katika agano la kale kuna vitabu viwili "Kitabu cha kwanza cha mambo ya nyakati" na "kitabu cha pili cha mambo ya nyakati."
- Kitabu cha mambo ya nyakati Kimerekodi sehemu ya simulizi ya wana wa Israeli mwanzoni imeorodhesha majina ya watu kwa kila kizazi kuanzia Adamu.
- "Kitabu cha kwanza cha mambo ya nyakati" kimerekodi mwisho wa maisha ya Sauli na matukio ya utawala wa mfalme Daudi.
- "kitabu cha pili cha mambo ya nyakati" Kimerekodi utawala wa mfalme Sulemani na baadhi ya wafalme pamoja na kujenga hekalu na kutenganisha ufalme wa kaskazini wa Israeli na ufalme wa kusini wa Israeli.
- Mwishoni mwa 2 Mambo ya nyakati kinaelezea mwanzo wa mateka ya babeli.

Maono

Ufafanuzi

Maono ni kitu ambacho mtu anakiona. Mara nyingi kitu hiki huwa sio cha kawaida au huwa chenye nguvu ambapo Mungu humuonesha mtu kwa lengo la kumpa ujumbe.

- Mtu huona maono akiwa macho na maranyingine huona maono kwenye ndoto akiwa amelala.
- Mungu hutuma maono ili kuwaambia watu jambo fulani la muhimu. Kwa mfano Patro aliona maono akiambiwa kuwa Mungu anamtaka awakaribishe Mataifa.

mateka, kifungo

Ufafanuzi

Neno "mateka" au "kifungo" ni kitendo cha kukamata watu na kuwalazimisha waishi mahali ambapo hawataki kuishi kama kwenye nchi ya kigeni.

- Waisraeli toka ufalme wa Yuda walichukuliwa mateka katika ufalme wa Babiloni kwa miaka 70.
- Mateka mara nyingi hufanya kazi za watu au za taifa lililowateka.
- Danieli na Nehemia walikuwa mateka wa Israeli waliofanya kazi kwa mfalme wa Babeli.
- "kuchukua mateka" inamaana ya kumkamata mtu.
- "kukuchukua mateka" inaweza kutafsiriwa kama "kukulazimisha kuishi kama mateka" au "kukupeleka kwenye nchi nyingine kama mfungwa."
- Mtume paulo anawaambia Wakristo "kuchukua mateka" kila wazo na kufanya imtii Kristo.
- Pia anazungumzia ni kwa namna gani watu wanaweza kuchukuliwa mateka kwa dhambi ikiwa na maana ya kutawaliwa na dhambi.

Mateso

Ufafanuzi

Mateso ni kitendo cha kumsababishia mtu mateso. Mateso ni ugonjwa, huzuni ya kihisia au majanga mengine yatokanayo na mateso.

- Mungu aliwapa mateso watu wake kupitia magonjwa na tabu zingine ili kuwasababisha watubu dhambi zao na wamrudie yeye.
- Mungu alisababisha mateso au mapigo kwa wana wa Israeli kwa sababu mfalme wao alikataa kumtii Mungu.

Matete

Ufafanuzi

Matete ni mimea nyenye mabua marefu yanayoota katika maji.

- Matete katika mto Nile ambapo Musa alifichwa kama mtoto paliitwa kwenye nyasi. Zilikuwa ndefu zilizomea kwenye mto wa maji.
- Matete haya yalitumiwa na Wamisri kutengeneza karatasi, vikapu na boti.
- Matete haya ni laini na rahisi kupinda zinapopulizwa na upepo.

maumivu makali

Ufafanuzi

Neno "maumivu makali" yaeleza kutesa sana. Kumtesa mtu ina maana ya kusababisha mtu kuteseka, mara nyingi kwa namna mbaya.

- Wakati mwingine neno "maumivu makali" yaeleza maumivu na kuteseka.
- Kuteseka pia kuna maana ya kiroho na maumivu ya hisia kama yale ya Ayubu.
- Kwa maelezo ya kitabu cha Ufunuo, watu wasiyo amini katika Yesu kama mwokozi watapitia maumivu makali ya milele katika ziwa la moto.

mavi, mbolea

Ufafanuzi

Msemo "mavi" una maana ya takataka ya binadamu au mnyama, na pia kinaitwa kinyesi. Unapotumika kama kirutubisho cha kurutubisha udongo, inajulikana kama "mbolea"

Misemo hii pia inaweza kutumika kitamathali kumaanisha kitu ambacho hakina thamani au sio muhimu.

Kinyesi kilichokaushwa cha mnyama mara kwa mara hutumika kama kichochea.

Msemo "kuwa kama kinyesi katika uso wa dunia" unaweza kutafsiriwa kama "kusambazwa kama kinyesi kisicho na maana juu ya nchi".

"Malango ya Kinyesi" katika Ukuta wa Kusini wa Yerusalemu yawezekana ulikuwa mlango ambapo takataka zote zilichukuliwa nje ya mji.

mavuno/kuvuna

Ufafanuzi

Neno 'mavuno' hurejelea mkusanyiko wa matunda, mazao au mboga zilizoiva au kukomaa kutoka katika mimea iliyokuwa imepanda na kustawishwa. Muda wa mavuno mara kwa mara hutokea mwishoni mwa msimu wa kilimo. Waisraeli walikuwa na 'sherehe za mavuno' au 'sherehe ya ukusanyaji' ili kusherehekea uvunaji wa mazao ya chakula. Mungu aliwaagiza kutoa mazao ya kwanza ya mazao haya kama sadaka kwake. Katika lugha ya picha, neno mavuno laweza kutumika kutumika kurejelea watu wanaomwamini Yesu au kueleza juu ya ukuaji wa kiroho wa mtu. Wazo la mavuno ya mazao ya kiroho hukubaliana na huendana na mfano wa picha wa matunda kama picha ya mwenendo na tabia nzuri.

Mapendekezo ya tafsiri Ni vizuri kutafsiri neno hili pamoja na neno ambalo hutumika mara kwa mara katika lugha husika kurejelea uvunaji wa mazao. Tukio la uvunaji laweza kutafsiriwa kama 'kipindi cha ukusanyaji' au ' kipindi cha ukusanyaji wa mazao' au ' kipindi cha kuchuma matunda' Kitenzi 'kuvuna' chaweza kutafsiriwa kama ' kukusanya' au 'kuchuma' or 'kuweka pamoja.'

mawaa

Ufafanuzi

Neno "mawaa" humaanisha kasoro juu ya mtu au mnyama. Yaweza pia kumaanisha upungufu wa kiroho kwa mtu.

- Kwa baadhi ya sadaka, Mungu aliwaagiza Waisraeli watoe mnyama asiye na kasoro au kosa.
- Hii ni taswira ya jinsi Yesu Kristo alivyokuwa sadaka kamilifu, bila dhambi yoyote.
- Waamini katika Kristo wamesafishwa kutokana na dhambi zao kwa damu yake na wanahesabiwa hawana makosa.
- Njia ya kutafasiri neno hili laweza kujumuisha, "kasoro" au "upungufu" au "dhambi," kwa kutegemea mazingira.

Mawaidha

Ufafanuzi

Neno "mawaidha" linamaana ya kuonya au kumshauri mtu.

- Mara nyingi "mawaidha" huwa na maana ya kumshauri mtu asifanye jambo fulani.
- Katika mwili wa Kristo, waamini wanafundishwa kupeana mawaidha wao kwa wao ili kuepuka dhambi na kuishi maisha matakatifu.
- Neno mawaidha linaweza kutafsiriwa kama "kumhimiza mtu asitende dhambi."

Mawindo, kwa mawindo ya

Ufafanuzi

"Mawindo" ni kitu kinachowindwa hasa mnyama anayetumika kwa ajili ya chakula.

- Katika lugha ya picha mawindo anaweza kuwa mtu anayefanyiwa ukatili au kunyanyaswa na mtu mwenye nguvu.
- Mawindo ya watu ni kitendo cha kuwanyanyasa watu au kuwaibia vitu walivyonavyo.
- Pia mawindo yanaweza kutafsiriwa kama "mnyama anayewindwa"

mazao ya kwanza

Ufafanuzi

Msemo "mazao ya kwanza" ina maana ya sehemu ya matunda ya kwanza ya mazao na mimea ambayo yalivunwa katika kila majira ya mavuno.

Waisraeli walitoa mazao haya ya kwanza kwa Mungu kama sadaka ya toleo.

Msemo huu unatumika kitamathali katika Biblia kumaanisha mzaliwa wa kiume wa kwanza kuwa mazao ya kwanza ya familia. Yaani, kwa sababu alikuwa mwana wa kiume wa kwanza kuzaliwa katika familia, yeye ndiye aliyekuwa akibeba jina na heshima ya familia.

Kwa sababu Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, anaitwa "mzawa wa kwanza" wa waumini wake wote ambao wamekufa lakini ambao hapo baadaye watafufuka.

Waumini katika Yesu pia wanaitwa "wazawa wa kwanza" wa uumbaji wote, kuonyesha faida maalumu na nafasi ya wale ambao Yesu amewakomboa na kuwaita kuwa watu wake.

Mapendekezo ya Tafsiri

Matumizi halisi ya msemo huu yanaweza kutafsiriwa kama "sehemu ya kwanza"

mbawala, paa, paa dume, paa mdogo

Ufafanuzi

Mbawala ni mnyama mkubwa, mwenye madaha, na miguu minne ambaye anaishi katika msitu au milimani. Mnyama wa kiume ana pembe kubwa kichwani mwake.

Msemo wa "paa" una maana ya mbawala wa kike na "paa mdogo" ni jina la mtoto wa paa.

Msemo wa "paa" una maana ya paa wa kiume.

"Paa dume" ni dume wa aina ya "mbawala".

Mbawala wana miguu myembamba na yenye nguvu inayowasaidia kuruka juu na kukimbia kwa kasi.

Nyayo zao ina kwato iliyogawanyika ambayo huwasaidia kutembea au kupanda kwa urahisi kwenye mandhari ya kila aina.

mbegu, manii

Ufafanuzi

Mbegu ni sehemu ya mmea unao oteshwa kwenye ardhi kuzalisha aina moja zaidi ya mmea huo. Pia ina maana kadha ya mafumbo.

- Neno "mbegu" linatumika kwa fumbo na tafsida kuelezea seli ndogo ndani ya mwanaume au mwanamke zinazo jumuika kusababisha mtoto kukua ndani ya mwanamke, hii ina itwa manii.
- Pamoja na hii, "mbegu" inatumika kueleza uzao wa mtu.
- Neno hili lina maana ya wingi, likieleza zaidi ya mbegu moja au zaidi ya mzao mmoja.
- Katika mfano wa mkulima akipanda mbegu, Yesu alifananisha mbegu na Neno la Mungu lililo pandwa katika mioyo ya watu ilikuweza kuzalisha matunda mazuri ya kiroho.
- Mtume Paulo pia anatumia neno "mbegu" kumaanisha Neno la Mungu.

mbuzi, mwanakibuzi

Ufafanuzi

Mbuzi ni mnyama wa ukubwa wa kati, mwenye miguu minne ambaye analingana na kondoo na hukuzwa kimsingi kwa ajili ya maziwa yake na nyama. Mtoto wa mbuzi huitwa "mwanakibuzi".

Kama kondoo, mbuzi walikuwa wanyama muhimu wa sadaka, haswa wakati wa Pasaka.

Ingawa mbuzi na kondoo wanaweza kufanana, kuna namna ambavyo wako tofauti.

Mbuzi wanya manyoya ya kukwaruza; kondoo wana sufu.

Mkia wa mbuzi husimama juu; mkia wa kondoo huning'inia chini.

Kondoo mara kwa mara hupenda kukaa katika kundi lake, lakini mbuzi wanajitegemea zaidi na kutembea mbali na kundi lao.

Katika kipindi cha Biblia, mbuzi walikuwa chanzo kikuu cha maziwa Israeli.

Ngozi ya mbuzi ilitumika kwa ajili ya kufunika mahema na kutengeza mifuko ya kubeba divai.

Pote katika Agano la Kale na Jipya, mbuzi alitumika kama ishara ya ukosefu wa utakatifu wa watu, labda kwa sababu ya mazoea yao ya kutangatanga mbali na yule aliyekuwa akiwatunza.

Waisraeli pia walitumia mbuzi kama mfano wa mtu mwenye dhambi. Mbuzi mmoja anapotolewa sadaka, kuhani huweka mikono yake juu ya mbuzi wa pili aliye hai na kumwachilia jangwani kama alama ya mnyama kubeba dhambi ya watu.

mbwa mwitu

Ufafanuzi

Mbwa mwitu ni mnyama mkali, anayekula nyama na anafanana na mbwa.

- Mbwa mwitu mara nyingi huwinda kwa makundi na hunyemelea mawindo yao kwa werevu.
- Katika Biblia "mbwa mwitu" imetumika kuelezea walimu wa uongo au manabii wa uongo wanaoharibu waamini wanaofananishwa na kondoo. Mafundisho ya uongo yanasababisha watu waamini uongo na kuwaletea madhara kwao.
- Mfanano huu unaonesha kuwa kondoo ni rahisi sana kuvamiwa na kuliwa na mbwa mwitu kwa sababu hawana nguvu na hawawezi kujitetea.

mchungaji, kuchunga

Ufafanuzi

Mchungaji ni mtu anaye linda kondoo. Kitenzi "kuchunga" ina maana ya kulinda kondoo na kuwapa chakula na maji.

- Wachungaji wanachunga kondoo, kuwa ongoza sehemu yenye chakula kizuri na maji. Wachungaji pia wana chunga kondoo wasipotee na kuwalinda na wanyama hatari.
- Hili neno linatumika kifumbo kwenye Biblia kueleza kutunza maitaji ya kiroho ya watu. Hii ni pamoja na kuwa fundisha nini Mungu alicho waambia kwenye Biblia na kuwa ongoza kwenye njia ya kuishi.
- Katika Agano la Kale, Mungu amewaita "wachungaji" wa watu wake kwasababu ana watunza na maitaji yao yote na kuwalinda. Pia uwaongoza na kuwa elekeza.
- Musa alikuwa mchungaji wa Waisraeli alipo waongoza kiroho katika kumuabudu Yahweh na kuwa ongoza kimwili katika safari yao kwenye nchi ya Kanani.
- Katika Agano Jipya, Yesu anajitaja "mchungaji mwema." Mtume Paulo pia anamtaja kama "mchungaji mkuu" juu ya Kanisa.

meneja, wakili

Ufafanuzi

Neno "meneja" au "wakili" katika Biblia ya husu mtumishi aliye kabidhiwa jukumu la kutunza mali na biashara.

- Wakili alipewa majukumu mengi, yaliyo jumuisha kusimamia kazi za watumishi.
- Neno "meneja" ni la kisasa zaidi kwa neno wakili. Maneno yote ya husu mtu aneye simamia kazi za mtu mwingine.

Methali

Ufafanuzi

Methali ni sentensi fupi zinazoelezea hekima au kweli.

- Methali zina nguvu kwa sababu ni rahisi kukumbukwa na kurudiwa.
- Mara nyingi methali hujumuisha mifano ya maisha ya kila siku.
- Mithali nyingine zipo wazi na nyingine ni ngumu kuzielewa.
- Mfalme Sulemani alifahamika kwa hekima zake na aliandika mithali 1,000.
- Yesu pia alitumia mithali au mifano katika mafundisho yake.

meza

Ufafanuzi

Msemo wa "meza" una maana ya kula au kutumia kwa hali ya fujo.

Kutumia neno hili kwa hisi ya tamathali, Paulo anatahadharisha waumini kutojimeza wao kwa wao, akimaanisha kutojishambulia au kuangamizana wao kwa wao kwa maneno au matendo (Wagalitia 5:15).

Pia katika hisi ya tamathali, msemo "kumeza" mara kwa mara hutumika kwa maana ya "kuangamiza kabisa" kama kuzungumzia juu ya mataifa kumeza mengine au moto kumeza majengo na watu.

Msemo huu pia unaweza kutafsiriwa kama "kumeza kabisa" au "kuangamiza kabisa".

mfalme

Ufafanuzi

Neno "mfalme" linamaanisha mwanamme ambaye ni mtawala mkuu wa mji, jimbo, au nchi.

Mfalme kawaida huchaguliwa kutawala kwa sababu ya uhsiano wake kifamilia na wafalme wa nyuma. Mfalme anapokufa, kawaida mwana wake mkubwa ndiye anayekuwa mfalme mpya. Katika nyakati za zamani, mfalme alikuwa na mamlaka yote juu ya watu katika ufalme wake. Neno "mfalme" halitumiki sana kwa mtu asiye mfalme wa kweli, kama "mfalme Herode" katika Agano Jipya. Katika Biblia, Mungu anajulikana kama mfalme anaye tawala juu ya watu wake. "Ufalme wa Mungu" unamaanisha utawala wa Mungu juu ya watu wake. Yesu aliitwa "Mfalme wa Wayahudi," "mfalme wa Israeli," na "mfalme wa wafalme." Yesu atakaporudi, atatawala kama mfalme wa dunia. Neno hili linaweza kutafsiriwa kama, "mkuu" au "kiongozi kamili" au "mtawala mwenye nguvu." Usemi "mfalme wa wafalme" unaweza kutasiriwa kama "mfalme anayetawala juu ya wafalme wengine wote" au "kiongozi mkuu aliye na mamlaka juu ya viongozi wengine wote."

mgeni, ugeni, mgeni

Ufafanuzi

Msemo, "mgeni" una maana ya mtu anayeishi katika nchi ambayo sio yake.

Katika Agano la Kale, msemo huu haswa humaanisha mtu yeyote ambaye alikuja kutoka kwa kundi tofauti la watu na watu ambao anaishi miongoni mwao.

Mgeni pia ni mtu ambaye lugha yake na utamaduni ni tofauti na ya kwako.

Kwa mfano, Naomi na familia yake alipohama kwenda Moabu, walikuwa wageni kule. Naomi na mkwe wake Ruthu walipohamia Israeli baadaye, Ruthu aliitwa "mgeni" kule kwa saba hakuwa wa Israeli kiasili.

Mtume Paulo aliwaambia Waefeso ya kuwa kabla hawajamjua Kristo, walikuwa "wageni" kwa agano la Mungu.

Mara nyingi, "mgeni" hutafsiriwa kama "mgeni" mtu ambaye hajulikani au hajazoeleka.

mhenga, baba, mababu

Ufafanuzi

Inapotumika kihalisia, msemo "baba" una maana ya mzazi wa kiume wa mtu. Kuna baadhi ya matumizi ya tamathali ya msemo huu.

Misemo "baba" na "babu" hutumika kumaanisha mababu wa mtu fulani au kundi la watu. Hii inaweza kutafsiriwa kama "babu" au "baba wa zamani".

Msemo "baba wa" unaweza kumaanisha kitamathali mtu ambaye ni kiongozi wa kundi la watu wanaohusika au wenye chanzo na kitu. Kwa mfano, katika Mwanzo 4, "baba wa wale wote waishio katika mahema" inaweza kumaanisha "kiongozi wa kwanza wa ukoo wa watu wa kwanza ambao waliishi katika mahema".

Mtume Paulo alijiita kitamathali "baba" wa wale ambao aliwasaidia kuwa Wakristo kupitia kutangaza injili pamoja nao.

Mapendekezo ya Tafsiri

Unapozungumza juu ya baba na mtoto wake halisi, msemo huu unatakiwa kutafsiriwa kutumia neno la kawaida kumaanisha baba katika lugha hiyo.

"Mungu Baba" inatakiwa kutafsiriwa kutumia neno la kawaida la "baba".

Unapomaanisha mababu, msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "babu" au "baba wa zamani".

Paulo anapomaanisha mwenyewe kitamathali kuwa baba wa waumini katika Kristo, hii inaweza kutafsiriwa kama "baba wa kiroho" au "baba katika Kristo".

Mara nyingine neno "baba" linaweza kutafsiriwa kama "kiongozi wa ukoo".

Msemo "baba wa uongo wote" unaweza kutafsiriwa kama "chanzo cha uongo wote" au "yule ambaye uongo wote hutokana".

mifugo

Ufafanuzi

Neno "mfugo" linamaanisha wanyama wanaotunzwa kwa ajili ya chakula na mazao mengine ya maana. Aina zingine za mifugo wanafundishwa kuwa wanyama wa kazi.

Aina wa mifugo ni pamoja na kondoo, ng'ombe, mbuzi, farasi, na punda. Katika nyakati za Biblia, utajiri kwa sehemu ulipimwa kwa idadi ya mifudo aliyonayo mtu. Mifugo inatumika kwa kuzalisha vitu kama sufu, maziwa, jibini, vifaa vya ujenzi, na nguo. Hii inaweza pia kutafsiriwa kama "wanyama wa shambani."

milele

Ufafanuzi

Katika Biblia, msemo "milele" una maana ya muda usiofika mwisho. Mara kwa mara hutumika kitamathali kumaanisha, "muda mrefu sana".

Msemo "milele na milele" unasisitiza ya kwamba jambo litakuwepo milele.

Msemo "milele na milele" ni njia ya kuelezea maisha ya milele yakoje. Pia una wazo la muda ambao hauishi.

Mungu alisema ya kwamba ufalme wa Daudi utakuwepo "milele". Hii inamaanisha ukweli ya kwamba uzao wa Daudi Yesu atatawala kama mfalme milele.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "mara zote" au "kutokuwa na mwisho". Msemo, "utadumu milele" unaweza kutafsiriwa kama "kuwepo mara zote" au "hautakoma" au "utaendelea mara zote". Msemo wa kishindo, "milele na milele" unaweza kutafsiriwa kama "kwa mara zote na zote" au "kutomalizika" au "ambayo haifiki mwisho". Ufalme wa Daudi kudumu milele unaweza kutafsiriwa kama, "uzao wa Daudi atatawala milele" au "uzao wangu ataendelea kutawala".

Mimi, Yahwe

Ufafanuzi

Mara nyingi katika Agano la Kale, wakati Mungu akijizungumzia, hutumia jina lake badala ya nomino kiwakilishi.

Kwa mfano, badala ya kusema, "Niheshimu mimi," husema "Mheshimu Yahwe." Kuiweka wazi kuwa ni Mungu anayejizungumzia, ULB kawaida hutafsiri hii kwa kuongezea nomino kiwakilishi kama, "Niheshimu mimi, Yahwe" au "Mimi, Yahwe ninasema." Kwa kuongeza nomino kiwakilishi "mimi", ULB inaashiria kwa msomaji kuwa Mungu ndiye anayezungumza.

Mizabibu

Ufafanuzi

Mizabibu ni bustani kubwa ambayo zabibu zinakua na kulimwa.

- Mizabibu mara nyingi huwa na ukuta ili kulinda matunda dhidi ya wezi na wanyama.
- Mungu anawafananisha wana wa Israeli na Mizabibu isiyozaa matunda.
- Mizabibu inaweza kutafsiriwa kama "bustani ya zabibui" au "zao la zabibu".

Mji mtakatifu

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno mji mtakatifu hurejelea mji wa Yerusalemu. Neno hili hurejelea mji wa zamani Yerusalemu pamoja na Yerusalemu mpya ya mbinguni mahali ambapo Mungu ataishi na kutawala miongoni mwa watu wake. Neno hili laweza kutafsiriwa kwa kuunganisha maneno 'takatifu' na 'mji' tafsiri ambayo imetumika katika tafsiri zote.

mjumbe

Ufafanuzi

Neno, "mjumbe" la husu mtu anaye pewa ujumbe kuwa ambia wengine.

- Katika zama za kale, mjumbe alitumwa katika mapambano kuwaambia watu waliyo mjini kinacho endelea.
- Malaika ni aina ya mjumbe maalumu ambaye Mungu anamtuma kuwapa watu ujumbe.
- Yohana Mbatizaji aliitwa mjumbe aliye kuja kabla ya Yesu kutangaza ujio wa Mesia na kuandaa watu kumpokea.
- Mitume wa Yesu walikuwa wajumbe wake wa kwenda kushirikisha watu habari njema za ufalme wa Mungu.

Mkate

Ufafanuzi

Mkate ni chakula kitengenezwacho kutokana na unga uliochanganywa na maji na matuta ili kutengeneza donge. Kisha donge linatengenezwa katika hali ya vipande na kuokwa.

- Neno "boflo" linapotokea peke yake, linamaanisha, "kipande cha mkate."
- Donge la mkate kwa kawaida linatengenezwa kwa kiti kinachofanya liumuke, kama vile amira.
- Lakini pia mkate waweza kutengenezwa bila amira hivyo hauwezi kuumuka. Katika Biblia huu unaitwa "mkate usiotiwa chachu" na ulitumiwa na Wayahudi wakati wa mlo wa Pasaka.
- Kwa vile mkate ulikuwa chakula kikuu kwa watu wengi katika nyakati za Biblia, hivyo neno hili linatumika katika Biblia pia kurejerea chakula kwa ujumla.
- Neno "mkate wa wonyesho" linataja vipande kumi na mbili vya mkate vilivyokuwa vikiwekwa katika meza ya dhahabu katika hema ya kukutania au hekaluni kama sadaka kwa Mungu. Mikate hii inawakilisha makabila kumi na mbili ya Israeli na ililiwa na makuhani tu. Hii inatafasiri kama "mkate uoneshao kwamba Mungu aliishi kati yao."
- Neno la kitamathari, "mkate kutoka mbinguni" linarejerea chakula maalumu cheupe kilichoitwa 'mana" alichokitoa Mungu kwa Waisraeli walipokuwa wakitangatanga jangwani.
- Yesu alijiita "mkate ulioshuka kutoka mbinguni" na "mkate wa uzima."
- Wakati Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wanaila Pasaka kabla ya kifo chake, alilinganisha, mkate usiotiwa chachu wa Pasaka na mwili wake ambao ungejeruhiwa na kufishwa msalabani.
- Mara nyingi neno "mkate" laweza kutafasiriwa kwa ujumla kama "chakula."

Mkoa, wilaya

Ufafanuzi

Mkoa ni sehemu ya nchi au himaya.

- Kwa mfano katika zama za Himaya ya Uajemi iligawanyika katika mikoa kama Uajemi, Syria na Misri.
- Katika nyakati za agano jipya himaya ya Roma iligawanyika katika mikoa kama Makedonia, Asia, Yudea, Samaria, Galatia, Galilaya.
- Kila mkoa ulikuwa na mamlaka yake inayoongoza ambao walikuwa chini ya mfalme au kiongozi wa himaya. Viongozi hawa waliitwa magavana wa mikoa.

mkono, mkono wa kuume,

Ufafanuzi

Neno 'mkono' limetumika katika Biblia kama lugha ya picha kwa njia mbalimbali Kuweka kitu katika mikono ya mtu fulani inamaana ya kukabidhi kitu hicho. Neno 'mkono' limetumika kurejelea uweza au nguvu ya Mungu na matendo yake. kwa mfano, Mungu anaposema "je si mkono wangu uliyoyafanya haya?" Neno "kabidhi" hurejelea maana ya kuweka kitu katika mkono au utawala wa mtu fulani. Kuweka mikono juu ya mtu fulani mara nyingi huambatana na utoaji wa baraka kwa mtu huyo. Pia kitendo cha 'kuweka mikono" juu ya mtu kinamaanisha kumweka mtu huyo wakfu kwa ajili ya kazi ya Mungu au kwa ajili ya kumwombea mtu huyo uponyaji. Baadhi ya lugha za picha za neno mkono ni: Kunyosha mkono juu ya mtu maana yake ni kumdhuru. ''kumwokoa kutoka katika mkono wa..." ni kumzuia mtu ili asimdhuru mtu mwingine. matumizi mengine ya mkono ni kama: "kunyosha mkono" ina maana ya 'kudhuru' au kuumiza" "kumwokoa mtu mikononi mwa" ina maana ya kumzuia mtu ili asimdhuru mtu mwingine. "kuwa karibu na mkono " kuwa 'karibu' "kuwa mkono wa kuume" humaanisha kuwa 'nafasi'' au ''sehemu ya'' au "upande wa kulia" Maelezo yanayosema "kwa mkono wa'' au ''kupitia mkono'' ina maana kuwa kitendo kimefanya na mtu huyo. kwa mfano, "kwa mkono wa Bwana'' ina maana kuwa Bwana ndiye amefanya tendo hilo. Wakati Paulo anasema " imeandikwa kwa mkono wangu" ina maana kuwa sehemu hii ya barua iliandikwa kwa mkono wake kabisa, badala tu kusema na mtu mwingine akayaandika.

Mapendekezo ya tafsiri. Maelezo haya na tamathali hizi za semi zaweza kutafsiriwa kwa kutumia lugha zingine za picha ambazo zina maana sawa. Au maana inaweza kutafsiriwa kwa kutumia lugha ya moja kwa moja.

mkuki

Ufafanuzi

Mkuki ni silaha ndefu ya mbao yenye ncha kali ya chuma mwishoni inayo tupwa umbali mrefu.

- Mikuki ilitumika mara nyingi kwenye vita kipindi cha Biblia. Wakati mwingine utumika ata sasa katika malumbano katika ya makundi ya watu.
- Mkuki ulitumika na mwanajeshi wa Kirumi kutoboa ubavu wa Yesu alipo kuwa ameni'ng'nia msalabani.
- Wakati mwingine watu wanatupa mikuki kudaka samaki au mawindo mingine kula.

Mkutano, kukusanyika

Ufafanuzi

Mkutano ni kundi la watu wanaokusanyika pamoja kujadili matatizo, kupeana ushauri na kufanya maamuzi.

- Mkutano ni kundi la watu wanaokusanyika pamoja kwa mda mfupi kwa ajili ya jambo maalumu au tukio maalumu.
- Katika agano la kale kulikuwa na mkutano maalumu ulioitwa mkutano takatifu ambapo wana wa Israeli walikusanyika kumuabudu Yahweh.
- Mara nyingine mkutano ina maanisha Waisraeli kwa ujumla kama kundi.
- Katika agano jipya viongozi wa Kiyahudi 70 katika miji mikuu kama Yerusalemu walikusanyika ili kutatua masuala ya kisheria na kutatua migogoro kati ya watu. Mkutano huo ulikuwa unajulikana kama Baraza.

Mkuu

Ufafanuzi

"Mkuu" ni kiongozi wa muhimu na mwenye nguvu sana katika kundi fulani.

- Kwa mfano "mkuu wa muziki," "kuhani mkuu," mkusanyaji mkuu wa kodi," na "kiongozi mkuu."
- Pia inaweza kutumiwa kwa kiongozi wa familia fulani, katika Mwanzo 36 kulikuwa na watu walioitwa wakuu wa koo zao.
- Inapotumika kama nomino neno hili laweza kutafsiriwa kama "kuongoza" au "mtawala wa kikuhani."

Mkuu, Binti wa Mfalme

Ufafanuzi

Mkuu ni mtoto wa kiume wa mfalme. Binti wa mfalme ni mtoto wa kike wa mfalme.

- "mkuu" imetumika mara nyingi kumuelezea kiongozi, mtawala au mtu mwenye nguvu.
- Kwa sababu ya utajiri wa Abrahamu alielezewa kama mkuu kwa Wahiti aliokuwa akiishi kati yao.
- Katika kitabu cha Danieli neno "mkuu" limetumika kuelezea roho chafu zilizokuwa zinatawala maeneo kama "wakuu wa uajemu" na "wakuu wa ugiriki."
- Katika kitabu cha Danieli pia malaika mkuu Mikaeli anazungumwa kama Mkuu.
- Pia katika Biblia Shetani anazungumzwa kama "mkuu wa ulimwengu huu."
- Yesu anaitwa "Mkuu wa amani."
- Katika Matendo ya mitume 2:26 Yesu anafananishwa na "Bwana na Kristo" Pia katika matendo ya mitume 5:31 anafananishwa kama "Mkuu na mwokozi" kuonesha maana kati ya "Bwana" na "Mkuu."

mkuyu

Ufafanuzi

Mkuyu ni mrefu, mti wa kivuli wenye shina kubwa na lenye matawi mapana.

- Mkuyu ina mbao ngumu iliyo tumika kutengeneza meli na kutengeneza majembe, na fimbo za kutembelea wazee.
- Shina la badhi ya mikuyu inaweza kuwa na mita 6.
- Miti ya mikuyu ilikuwa ni mfano wa maisha marefu na ilikuwa na maana zingine za kiroho. Katika Biblia, ilihusishwa na maeneo matakatifu.

Mnara

Ufafanuzi

Mnara ni jengo refu kwa umbo ambalo hujengwa kwa ajili ya walinzi kuangalia kama kuna hatari yoyote. Minara hii mara nyingi ilijengwa kwa kutumia mawe.

- Wamiliki wa ardhi maranyingi walijenga minara ili waweze kulinda mazao yao yasiibiwe.
- Minara pia ilijumuisha vyumba ambavyo walinzi au familia ziliishi ili ziweze kulinda mazao mchana na usiku.
- Minara ya jiji ilikuwa mirefu sana kuliko minara ya mji ili walinzi waweze kuona adui yeyote anayekuja kwenye jiji.
- Neno "mnara" linatumika kama ishara ya ulinzi toka kwa adui.

mnyama

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "mnyama" ni njia nyingine ya kusema "mnyama".

- Mnyama wa porini ni aina ya mnyama anayeishi huru msituni au kondeni na hayawai kufundishwa na watu.
- Mnyama wa kufugwa anaishi na watu na anatunzwa kwa mboga au kufanya kazi, kama vile kulima shamba. Mara kwa mara neno "mifugo" linatumika kurejerea aina hii ya wanyama.
- Kitabu cha Danieli katika Agano la Kale na kitabu cha Ufunuo katika Agano Jipya vinaeleza maono yenye wanyama wanaowakilisha nguvu au mamlaka ya uovu inayompinga Mungu.
- Baadhi ya wanyama hawa wanaelezwa wakiwa na tabia tofauti, kama vile vichwa kadhaa na pembe nyingi. Mara kwa mara wanakuwa na nguvu na mamlaka, kuonesha kwamba waweza kuwakilisha nchi, taifa au mamlaka nyingine ya kisiasa.
- Njia ya kutafasiri hii yaweza kuhusisha, "kiumbe" au "kitu kilichoumbwa" au "mnyama" au "mnyama wa porini," kutegemea mazingira.

Mnyweshaji

Ufafanuzi

Katika agano jipya "mnyweshaji" alikuwa mtumsihi wa mfalme aliyepewa kazi ya kupeleka kwa mfalme kikombe cha mvinyo, huonja mvinyo na kuhakikisha haujawekewa sumu.

- Pia maana ya kawaida ya mnyweshaji ni mtu anayeleta kikombe.
- Mnyweshaji alijulikana kwa kuwa mwaminifu kwa mfalme.
- Kwa sababu ya nafasi yake ua uaminifu mnyweshaji alikuwa na nafasi kubwa ya ushawishi kwa maamuzi anayotoa kiongozi.
- nehemia alikuwa mnyweshaji wa mfalme Artashasts wa Uajemi wakati ambao Waisraeli walikuwa mateka Babeli.

moto

Ufafanuzi

Moto ni joto, mwanga na miale ambayo hutokana pale kitu kinapochomwa.

Kuchoma mbao kwa moto hugeuza mbao kuwa majivu.

Msemo "moto" pia hutumika kitamathali, mara kwa mara kumaanisha hukumu au utakaso.

Hukumu ya mwisho ya wasioamini ipo katika moto wa jehanamu.

Moto hutumika kusafisha dhahabu na vyuma vingine. Katika Biblia, hatua hii hutumika kuelezea jinsi Mungu husafisha watu kupitia mambo magumu ambayo hutokea katika maisha yao.

Msemo "kuwabatiza kwa moto" unaweza kutafsiriwa kama "kukusababisha upitie mateso ili kwamba yakusafishe"

mpagao

Ufafanuzi

Mpagao ni hali ya fikra ambayo mtu yupo macho lakini hatambui yanayo mzunguka kwasababu anaona na kupitia vitu tofauti.

- Katika Agano Jipya, hili neno linaeleza hali ya kimuujiza ya fikra amabyo Petro na Paulo walikuwa nayo Mungu alipo zungumza nao kwenye maono.
- Katika kila hali, Petro na Paulo walikuwa katika maombi walipo patwa na mpagao.
- Mungu ndiye aliye sababisha wawe katika mpagao.
- Neno "mpagao" ni neno tofauti na "maono" au "ndoto" na itafsiriwe tofauti.
- Msemo "kuanguka katika mpagao" ina maana "kuwa katika hali ya usingizi ghafla" wakati bado macho.

Mpanda farasi

Ufafanuzi

katika nyakati za Biblia, istilahi, ' mpanda farasi walikuwa ni wanaume ambao waliendesha farasi katika vita. Mashujaa walioendesha gari la kukokotwa na farasi waliitwa wapanda farasi, ingawa jina hili hurejelea watu ambao kiuhalisia huongoza farasi. Waisraeli waliamini kuwa kwa kutumia farasi katika vita ilitia mkazo katika nguvu zao kuliko kumtegemea Yahweh, hivyo hawakutumia wapanda farasi sana.. Neno hili laweza kutafsiriwa kama ' waendesha farasi

Mpatanishi

Ufafanuzi

Mpatanishi ni mtu anaye saidia watu wawili au zaidi kusuluhisha malumbano yao au ugomvi baina yao. Ana wasaidia na kuwapatanisha.

- Kwasababu watu wametenda dhambi, ni maadui wa Mungu wanoa stahili gadhabu yake na adhabu. Kwasababu dhambi, mahusino katika ya Mungu na watu wake umevunjwa.
- Yesu ni mpatanishi katika ya Mungu Baba na watu wake, akirejesha uhusiano uliyo vunjika kupitia kifo chake kama malipo ya dhambi zao.

mpenzi

Ufafanuzi

Neno "mpenzi" linamaanisha "mtu anayependa." Kawaida hii inamaanisha watu walio katika mahusiano ya kimapenzi.

Neno "mpenzi" linapotumika katika Biblia, kawaida lina maana ya mtu aliye na uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye hajamuoa au kuolewa naye. Huu uhusiano mbaya wa kimapenzi hutumika kwenye Biblia kumaanisha kutokutii kwa Israeli katika kuabudu sanamu, Kwa hiyo neno "wapenzi" pia hutumika kimafumbo kumaanisha sanamu ambazo watu wa Israeli waliabudu. Katika mazingira haya, neno hili linaweza kutafsiriwa kuwa, "wenzi waovu" au "wenzi katika kuzini" au "sanamu." "Mpenzi" wa fedha ni mtu anayeweka msisitizo mkubwa sana kupata fedha na kuwa tajiri. Katika kitabu cha Agano la Kale cha Wimbo ulio Bora, neno "mpenzi" linatumika kwa njia nzuri.

Mpiga mishale

Ufafanuzi

Mpiga mishale ni mtu mwenye ujuzi wa kutumia upinde na mshale kama silaha.

- Kwenye Biblia mpiga mishale mara nyingi ni askari anayetumia upinde na mshale kupigana vitani.
- Wapiga mishale walikuwa watu wa muhimu sana katika Jeshi la Siria.

Mrithi

Ufafanuzi

Mrithi ni mtu ambaye kisheria hupoke mali au pesa za mtu aliyekufa. Katika nyakati za Biblia, mrithi mkuu alikuwa ni mtoto wa kwanza ambaye alipokea sehemu kubwa ya mali au pesa za baba yake. Biblia hutumia neno mrithi kama lugha ya picha kumaanisha Wakristo wanapopokea baraka za kiroho kutoka kwa Mungu, baba yao wa kiroho. Kama watoto wa Mungu, Wakristo ni warithi pamoja na Yesu Kristo. Hii inaweza kutafsiriwa kama "warithi wenza.'

Msamaha

Ufafanuzi

"Msamaha" ni kusamehe au kutokumhukumu mtu kwa sababu ya dhambi zake.

- Neno hili pia linaweza kuwa na maana ya kutokuamua kumhukumu mtu kwa sababu ana makosa.
- Kwenye mahakama, hakimu anaweza kumsamehe mtu anayekutwa na hatia katika kosa.
- Japokuwa sisi tuna hatia ya dhambi Yesu alitusamehe toka kwenye hukumu kwa kufa msalabani.

mshiriki

Ufafanuzi

Neno "mshiriki" la husu sehemu moja ya mwili au kundi.

- Agano Jipya la elezea Wakristo kama "washiriki" wa Mwili wa Kristo.
- Yesu Kristo ni "kichwa" wa mwili na waamini moja moja wanatumika kama washiriki wa mwili. Roho Mtakatifu anampa kila mshiriki wa mwili nafasi maalumu kusaidia mwili wote kufanya kazi vizuri.
- Watu wanao shiriki katika makundi kama Baraza la Wayahudi na Mafarisayo pia wanaitwa "washiriki" wa haya makundi.

Mshita

Ufafanuzi

Mshita ni mti uliopatikana katika nchi ya Kaanani katika nyakati za zamani.

- Mbao za Mshita ni ngumu na zinazodumu, hutumika kutengenezea vifaa kwa ajili ya ujenzi.
- Ni vigumu sana kwa mbao hii kuharibika, ni nene sana na aihifandhi maji, ina namna ya asili ya kujitunza ili isiharibiwe na wadudu.
- Kwenye Biblia mbao za Mshita zilitumika kujengea hema na sanduku la agano.

msimamizi

Ufafanuzi

Neno "msimamizi" la husu mtu aliye mwangalizi wa kazi na maendeleo ya watu wengine.

- Katika Agano la Kale, msimamizi alikuwa na kazi ya kuhakikisha wafanya kazi chini yake walifanya kazi yao vizuri.
- Katika Agano Jipya, hili neno la tumika kueleza viongozi wa kanisa la kwanza la Kristo. Kazi yao ilikuwa ilikuwa kushughulikia waamini wanapokea mafundisho sahihi ya Biblia.
- Paulo anataja msimamizi kama kuwa mchungaji anaye jali waamini katika kanisa, waliyo "kundi" lake"
- Msimamizi, kama mchungaji, anaangalia kondoo wake. Analinda na kutunza waamini kutoka mafundisho ya uongo na mambo mengine maovu.
- Katika Agano Jipya, maneno "msimamizi," "mzee," na "mchungaji" ni namna tofauti za kutaja viongozi wale wale wa kiroho.

msingi, kuanzishwa

Ufafanuzi

Kitenzi cha "kuanzishwa" ina maana ya kujengwa juu ya au kutokana na kitu. Msingi ni sehemu ya chini ambapo kitu kunajengwa.

Msingi wa nyumba or jengo lazima uwe na nguvu na kutegemewa ili kuimarisha umbo lote.

Msemo "msingi" unawvza kumaanisha mwanzo wa jambo au muda ambao kitu kiliumbwa.

Kwa kitenzi cha kitamathali, waumini katika Kristo wanalinganishwa na jengo ambalo limejengwa juu ya mafunzo ya mitume na manabii, na Kristo mwenyewe kuwa jiwe la pembeni la jengo.

"Jiwe la msingi" lilikuwa jiwe ambalo lililazwa kama sehemu ya msingi. Mawe haya yalijaribiwa kuhakikisha yalikuwa na nguvu ya kutosha kuimarisha jengo kamili.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "kabla ya msingi wa dunia" inaweza kutafsiriwa kama "kabla ya uumbaji wa ulimwengu" au "kabla ya muda ambapo dunia ilianza kuwepo".

Msemo "kujengwa juu ya" inaweza kutafsiriwa kama "kujengwa kwa imara juu ya" au "kujengwa kwa imara kwa".

Kulingana na muktadha, "msingi" inaweza kutafsiriwa kama "msingi imara" au "uimara wa kudumu" au "mwanzo" au "uumbaji"

msonobari

Ufafanuzi

Msemo "msonobari" una maana ya aina ya mti ambao hubaki kijani mwaka wote na una pia zenye mbegu kwa ndani.

Miti wa msonobari pia humaanisha mti wa "kijani" daima.

Katika nyakati za zamani, mbao za msonobari zilitumika kutengenezea vyombo vya muziki na kwa ujenzi wa maumbo kama vile mitumbwi, nyumba, na hekalu.

Baadhi ya mifano ya msonobari iliyotajwa katika Biblia ni msonobari, seda, mvinje na mreteni.

Mtamba/Mfarika wa ng'ombe

Ufafanuzi

Neno Mtamba' lina maana ya ng'ombe jike mkubwa ambaye hajazaa bado.

Mtawala, watawala, tawala

Ufafanuzi

"Mtawala" ni mtu mwenye mamlaka juu ya watu wengine kama vile kiongozi wa dini, ufalme au nchi.

- Katika agano la kale Mfalme alitambulika kama Mtawala. Sentensi zingine zimesema "walimchagua yeye kuwa mtawala juu ya Israeli."
- Mungu anazungumzwa kama mtawala mkuu anayetawala juu ya watawala wote.
- Katika agano jipya kiongozi wa sinagogo aliitwa mtawala.
- Aina nyingine ya mtawala katika agano jipya mi "gavana."
- Kutegemeana na mukhtadha mtawala inaweza kutafsiriwa kama kiongozi au mtu mwenye mamlaka.

mtego

Ufafanuzi

Neno mtego lina maana ya kifaa kinacho tumika kudaka wanyama na kuwazuia wasitoroke. Katika Biblia, hili neno linatumika kifumbo kueleza kuhusu jinsi dhambi na jaribu ni mitego inayo wanasa watu na kuwadhuru.

- "mtego" una kamba au waya unao vuta kwa ghafla pindi mnyama anapo ingia ndani yake, na kutega miguu yake.
- Mara nyingi mtego unafichwa ili kwamba mawindo yake ya naswe ghafla.
- Maneno "tega mtego" ina maana kuanda mtego tayari kunasa kitu.
- "kuanguka kwenye mtego" ina eleza kuanguka kwenye shimo refu lililo chimbwa na kufichwa kuweza kumdaka mnyama.

mtenda uovu

Ufafanuzi

Msemo "mtenda uovu" ni kumbukumbu ya jumla kwa watu ambao hufanya mambo ya dhambi na maovu.

Inaweza pia kuwa neno la jumla la watu ambao hawamtii Mungu.

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kwa kutumia neno kwa ajili ya "uovu" au "ubaya" na neno kwa ajili ya "kufanya" au "kutengeneza" au "kusababisha" kitu.

Mtende

Ufafanuzi

"mtende" ni mti mrefu wenye matawi marefu, rahisi na yanayosambaa kutoka juu.

- Mti wa mtende kwenye Biblia umeelezewa kuwa ni mti unaotoa matunda yanayoitwa "tende." Majani yake yako kama manyoya.
- Miti ya mitende huota sehemu zilizo na joto na majani yake hubaki kuwa ya kujani mwaka mzima.
- Yesu alipoingia Yerusalemu akiwa juu ya punda, watu walitandika chini majani ya mitende mbele yake.
- Majani ya mitende yanaonesha ishara ya amani na kusherehekea ushindi.

Mteserusi

Ufafanuzi

Neno Mteserusi ni jina la aina ya mti ambao ulipatikana kwa wingi katika maeneo ambapo waliishi watu nyakati za Kibiblia.

mtini

Ufafanuzi

Tini ni tunda dogo, laini, tamu ambalo huota juu ya miti. Linapoiva, tunda hili linaweza kuwa na rangi nyingi, ikiwemo kahawia, njano na zambarau.

Mitini inaweza kuota kuwa urefu wa mita 6 na matawi yao makubwa hutoa kivuli kizuri. Tunda hili lina urefu wa sentimita 3-5.

Adamu na Hawa walitumia majani ya mtini kutengeneza mavazi kwa ajili yao baada ya kutenda dhambi.

Mitini inaweza kuliwa mibichi, ikiwa imepikwa, au kukaushwa. Watu pia walikata katika vipande vidogo vidogo na kuzikandamiza kuwa keki kuliwa baadaye.

Katika kipindi cha Biblia, mitini ilikuwa muhimu kama chanzo cha chakula na kipato.

Uwepo wa mitini inayozaa mara kwa mara hutajwa katika Biblia kama ishara ya mafanikio.

Mara kadhaa Yesu alitumia mitini kama mfano wa kufundisha wanafunzi wake kweli za kiroho.

mtumishi, mtumwa, utumwa

Ufafanuzi

Neno "mtumishi" la weza pia maanisha "mtumwa" na kumueleza mtu anaye mfanyia mtu mwingine kazi, iwe kwa uwamuzi au kwa lazima. Muktadha wa maneno yaliyo zunguka yanaweka dhahiri kuwa kama mtumishi au mtumwa ndiye anaye tajwa.

- Katika nyakati za Biblia, kulikuwa na tofauti ndogo katika ya mtumishi na mtumwa kuliko ilivyo leo. Wote watumishi na watumwa walikuwa sehemu muhimu ya nyumba ya bwana wao na wengi walichukuliwa kama ndugu wa familia.
- Mtumwa ni aina ya mtumishi ambaye ni mali ya mtu anaye mfanyia kazi. Mtu anaye nunua mtumwa anaitwa "mmiliki" au "bwana." Mabwana wengine wanawatendea watumwa wao kwa ukatili sana, wakati wengine wana watendea vizuri.
- Zamani za kale, watu wengine kwa hiari walikuwa watumwa kwa mtu aliye wadai ilikulipa deni lao.
- Katika Biblia, maneno "mimi ni mtumishi wako" yalitumika kama alama ya heshima na huduma kwa mtu wa ngazi ya juu, kama mfalme. Haimanishi kwamba mtu anaye zungumza alikuwa mtumishi halisi.
- Katika Agano la Kale, manabii wa Mungu na watu wengine waliyo muabudu Mungu mara nyingi waliitwa "watumishi."
- Wakristo pia wanaitwa "watumwa wa haki," ambayo ni mfano unao linganisha uwaminifu wa kumtii Mungu kama mtu anavyo mtii bwana wake.

muamuzi, waamuzi

Ufafanuzi

Muamuzi ni afisa aliye teuliwa anaye kuwa kama hakimu anaye amua mambo ya sheria.

- Katika Biblia, muamuzi alitatua ugomvi baina ya watu.
- Kulingana na muktadha, namna ya kutafsiri hili neno ya weza kuwa, "hakimu anaye amua" au "afisa wa sheria" au "kiongozi wa mji"

muda

Ufafanuzi

Katika Biblia neno "muda" utumika sana kama fumbo kueleza wakati maalumu au kipindi cha muda fulani matukio yametokea. Lina maana sawa na "umri" au "wakati."

- Danieli na Ufunuo unaeleza "muda" wa kipindi kigumu au dhiki itakayo kuja duniani.
- Katika maneno "muda, mida, na nusu muda" neno "muda" lina maana ya "mwaka." Haya manano yanaeleza kipindi cha nusu mwaka wakati wa dhiki kuu mwisho wa muda huu uliyopo.
- Maneno kama "wakati wa pili" au "mara nyingi" ueleza idadi ya marudio kitu kilicho tokea.
- Kulingana na muktadha, neno "muda" uweza tafsiriwa kama, "majira" au "kipindi cha muda"

muhuri, kutia muhuri

Ufafanuzi

Kutia muhuri kitu ina maana ya kufunga kwa kitu ambacho inafanya ngumu kufungua pasipo kuvunja muhuri.

- Mara nyingi muhuri unatiwa alama ya kuonyesha mmiliki.
- Nta iliyo yayushwa ilitumika kueka muhuri barua au nyaraka zilizo itaji kulindwa. Nta ilipo pata baridi na kuwa ngumu, barua haikuweza kufunguliwa pasipo kuvunja nta ya muhuri.
- Kama muhuri uliweka katika jiwe mbele ya kaburi la Yesu kuweza kuzuia ye yote asisogeze jiwe.
- Paulo kwa fumbo ana mtaja Roho Mtakatifu kama "muhuri" kuonyesha kuwa wokovu wetu ni wa salama.

Mvua ya mawe

Ufafanuzi

Mvua ya mawe ni vipande vidogo vidogo au vikubwa vya maji yaliyoganda ambayo hushuka kutoka mawinguni. Mawe ya Mvua hushuka kutoka mawinguni katika umbo la kama mpira au vipande vya barafu. Mawe haya ya mvua mara nyingi huwa ni madogo madogo, lakini wakati mwingine yanaweza kuwa makubwa yenye upana wa sentimita 20 hivi na uzito wa kilogramu moja hivi. Kitabu cha Ufunuo katika Agano la Jipya kinazungumzia juu ya mawe ya mvua makubwa yenye uzito wa kilogramu 50 hivi ambayo Mungu atayashusha juu ya dunia ili kuhukumu watu waovu katika siku za mwisho.

mwaka linapotumika

Ufafanuzi

Neno "mwaka linapotumika, kwa hali ya kawaida katika Biblia linamaanisha kipindi cha muda wa siku 354. Hii ni kulingana na kalenda inayotumia mfumo wa mwezi unaochukua kuizunguka dunia.

- Mwaka katika siku hizi unakamilisha siku 365 kwa kugawanywa katika miezi 12, kutegemea siku ambazo dunia inatumia kulizunguka jua.
- Katika mifumo yote miwili mwaka una miezi 12. Lakini wakati mwingine ziada ya mwezi wa 13 unaongezwa katika mwaka unaotumia kalenda ya mwezi kwa kuzingatia kuwa kalenda ya mwezi ina siku 11 pungufu ya ule wa jua. Hii inasaidia kuzilinganisha kalenda zote mbili.
- Katika Biblia, neno "mwaka" pia limetumika kwa tamathari kuonesha muda wa jumla tukio maalumu linapotokea. Mfano wake ni "mwaka wa Yahwe" au "katika mwaka wa kianganzi" au "mwaka wa Bwana uliokubarika." Katika mazingira haya, "mwaka" waweza kutafasiriwa kama "wakati" au "majira" au "kipindi cha wakati".

mwalimu,Mwalimu

Ufafanuzi

Mwalimu ni mtu anaye toa taarifa mpya. Waalimu wanasaidiana kupata na kutumia maarifa na ujuzi.

- Katika Biblia, neno "mwalimu" linatumika kwa namna maalumu kumueleza mtu anaye fundisha kuhusu Mungu. Haimuelezi mwalimu wa shule.
- Watu wanao jifunza kutoka kwa mwalimu wanaitwa "wanafunzi."
- Katika baadhi ya fasiri za Biblia, hili jina limewekwa herufi kubwa ("Mwalimu") wakati linapo tumika kama jina la Yesu.

mwamini

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "mwamini" larejerea mtu anayeamini na kumtegemea Yesu Kristo kama Mwokozi.

- Neno "mwamini" kwa maana halisi linamaanisha "mtu anayeamini."
- Neno "Mkristo" lilikuja hatimaye kuwa jina la waamini kwa sababu linaonesha kwamba wanamwamini Kristo na kutii mafundisho yake.

Maoni ya Kutafasiri.

- Baadhi ya tafasiri zaweza kupendelea kusema, "mwamini wa Yesu" au "anayemwamini Kristo."
- Neno hili pia laweza kufasiriwa kwa neno au kirai kinachomaanisha, "mtu anaye mwamini Yesu" au "mtu anayemfahamu Yesu na kuishi kwa ajili yake."
- Njia nyingine ya kutafasiri "mwamini" laweza kuwa, "mfuasi wa Yesu" au "Mtu anayemjua na kumtii Yesu."
- Neno "mwamini" ni neno la jumla kwa kila anayemwamini Kristo, wakati "mfuasi" na "mtume" yalitumika maalumu kwa watu waliomfahamu Yesu alipokuwa hai. Ni vema kutafasiri maneno haya kwa njia tofauti, ili kuyatofautisha.

Mwananchi

Ufafanuzi

Mwananchi ni mtu anayeishi katika mji fulani au nchi au ufalme. Ni mtu ambaye anajulikana ni mkazi wa kisheria wa eneo hilo.

- Inategemea na mukhtadha hii inaweza kutafsiriwa pia kama "mwenyeji."
- Mwanamchi anaweza kuishi katika mkoa ambao ni sehemu ya ufalme mkubwa unaoongozwa na mfalme au kiongozi. Kwa mfano Paulo alikuwa mwananchi wa Rumi iliyokuwa na mikoa mingi. Paulo aliishi katika moja ya mikoa hiyo.
- Kwa tafsiri nyingine wanaomwamini Yesu wanaitwa Wananchi wa Mbinguni kwa maana ya kuwa wataishi huko siku moja.

Mwangamizi

Ufafanuzi

Msemo wa "mwangamizi" una maana ya, "mtu anayeangamiza".

Msemo huu unatumika mara kwa mara katika Agano la Kale kama mrejesho wa jumla ya mtu yeyote anayeangamiza watu wengine, kama vile jeshi vamizi.

Mungu alipotuma malaika kuua wana wote wa kiume wa kwanza Misri, malaika huyo alijulikana kama, "mwangamizi wa wana wa kwanza". Hii inaweza kutafsiriwa kama, "yule (au malaika) ambaye alwaua wana wa kiume wa kwanza".

Katika kitabu cha Ufunuo kuhusu nyakati za mwisho, Shetani au roho nyingine chafu inajulikana kama, "Mwangamizi". Yeye ni "yule anayeangamiza" kwa sababu kusudi lake ni kuangamiza na kuharibu kila kitu alichoumba Mungu.

mwenzi

Ufafanuzi

Mwenzi ni mtu anayekwenda na mtu mwingine au mwenye ushirika na mtu mwingine kwa mfano urafiki au ndoa.

- Mwenzi hupitia katika jambo analipitia mwenzake kama kula pamoja na kutiana moyo.
- Inategemea na mukhtadha neno hili laweza kutafsiriwa kama "rafiki" au "msafiri mwenzako" au "mtu anayekutia moyo."

mwerezi

Ufafanuzi

"Mwerezi" ni mberoshi mkubwa ambao una rangi nyekundu. Kama miberoshi mingine ina umbo la sonobari na majani kama sindano.

- Katika agano la kale mti wa mwerezi umetajwa ukihusishwa na labanoni ambapo ilikua kwa wingi.
- Mbao ya mwerezi ilitumika kujenga hekalu la Yerusalemu.
- Pia ilitumika katika sadaka ya kutakaswa na dhabihu.

mwezi

Ufafanuzi

Neno "mwezi" linataja kipindi cha kuishia karibia majuma manne. Idadi ya majuma katika kila mwezi yalitofautiana kulingana na matumizi ya kalenda iliyotumika kwamba ilikumia jua au mwezi.

- Katika kalenda ya mwezi, urefu wa mwezi unategemea kiwango cha muda mwezi unaotumia kuizunguka dunia, kama siku 29. Katika utaratibu huu kuna miezi 12 au 13 katika mwaka. Pamoja na mwaka kuwa na miezi 12 au 13, mwezi wa kwanza unaitwa kwa jina lilelile hata kama ni majira tofauti.
- "Mwezi mpya," kuanza kwa awamu ya mwezi pamoja na nuru yake, unaashiria kuanza kwa kila mwezi katika kalenda ya mwezi.
- Majina yote ya miezi yaliyotajwa katika Biblia yanatumia kalenda ya mwezi kwa kuwa ndio mfumo uliokuwa unatumiwa na Waisraeli. Wayahudu wa sasa bado wanatumia mfumo huu katika shughuri na makusudi ya kidini.
- Kalenda ya siku hizi inayotumia jua imejengwa juu ya muda unaoichukua dunia kulizunguka jua (kama siku 365). Katika mfumo huu, mwaka kwa kawaida umegawanywa katika miezi 12, mwezi ukichukua kati ya siku 28-31.

mwezi mpya

Ufafanuzi

Neno "mwezi mpya" katika Biblia ya husu mwezi unapo onekana mdogo, wa mwanga wa fedha. Huu ni mwanzo wa mwezi unapo hama na kuzunguka dunia.

- Zama za kale, mwezi mpya ulitumika kuweka alama ya mwanzo wa nyakati.
- Waisraeli walisherehekea mwezi mpya uliyo adhimishwa kwa kupuliza pembe la kondoo.
- Biblia pia yataja hichi kipindi kama "mwanzo wa mwezi"

mwiba, mbaruti

Ufafanuzi

Vicha vya miba na mbaruti ni majani matawi yaliyo chongoka au maua. Haya majani haya zalishi matunda au chochote kinacho tumika.

- "Mwiba" ni mgumu, umechongoka katika tawi au jani. "Kichaka cha mwiba" ni aina ya mti mdogo mwenye miba mingi kwenye matawi yake.
- "Mbaruti" ni mmea wenye majani yalichongoka. Mara nyingi majani yake ni ya zambarau.
- Mwiba na mbaruti uota haraka na uweza shababisha mimea ya karibu kutostawi. Hii ni sura ya jinsi dhambi ina mzuia mtu kutozalisha matunda mazuri ya kiroho.
- Taji lililo tengenzwa na matawi ya miba liliwekwa kwenye kichwa cha Yesu kabla ya kusulubiwa.

mwizi, wezi, jambazi

Ufafanuzi

Haya maneno "mwizi" na "wezi" yanaeleza kwa jumla watu wanao iba pesa au mali kwa wengine. Neno "jambazi" mara nyingi la eleza mwizi anaye dhuru kimwili au kutishia watu anao waibia.

- Yesu alitoa mfano kuhusu mwanaume mmoja Msamaria aliye msaidia mtu aliye shambuliwa na majambazi. Majambazi walimpiga na kumjeruhi kabla ya kuiba pesa na nguo zake.
- Wezi na majambazi wanakuja ghafla kuiba, watu wasipo tarajia. Mara kadhaa wanatumia giza kuficha wanacho fanya.
- Kwa fumbo, Agano Jipya la eleza Shetani kama mwizi anaye kuja kuiba, kuua, na kuharibu. Hii ina maana kuwa Shetani mpango wake ni kujaribu kushawishi watu wa Mungu kutomtii, kuiba vitu vizuri Mungu alivyo panga kwao.

mwokovu

Ufafanuzi

Neno "mwokovu" la husu kuwa umeokolewa au kukombolewa kutoka kwenye uovu au hatari.

- Katika Biblia, "mwokovu" wa husu ukombozi wakiroho na wa milele unao tolewa na Mungu kwa hao wanao tubu dhambi zao na kumuamini Yesu.
- Biblia pia yazungumzia kuhusu Mungu kuokoa au kukomboa watu wake kutoka kwa maadui zao wa mwili.

Mzabibu

Ufafanuzi

Mzabibu ni mmea unaopandwa na kukua kwa kutambaa ardhini au kwa kusimamisghwa juu ya mtu au kitu kingine. Katika Biblia neno mzabibu ni tunda pekee lililizalisha zabibu na kutoa mvinyo.

- Matawi ya zabibu yanashikiliwa na shina kuu ambalo huyapa maji na virutubisho vingine ili iweze kukua.
- Yesu alijiita mzabibu na akawaita watu wake matawi. Kwa mukhtadha huu mzabibu waweza kutafsiriwa kama shina la mzabibu.

mzaliwa

Ufafanuzi

Neno "mzaliwa" ni fahirisi ya jumla kwa wazao wa kibaiolojia ya watu au wanyama.

- Mara nyingi katika Biblia, "mzaliwa" ina maana moja na "watoto" au "wazao"\
- Neno "mbegu" wakati mwingine utumika kifumbo kumaanisha mzaliwa.

mzawa wa kwanza

Ufafanuzi

Msemo "mzawa wa kwanza" una maana ya uzao wa watu au wanyama ambao huzaliwa kwanza, kabla ya wazawa wengine kuzaliwa. Mara kwa mara mzawa wa kwanza

Katika Biblia, "mzawa wa kwanza" humaanisha mzaliwa wa kiume ambaye anazaliwa.

Katika kipindi cha Biblia, mzawa wa kwanza wa kiume alipewa nafasi ya kujulikana na mara mbili ya urithi wa familia yake ya wana wengine.

Mara nyingi ilikuwa mzawa wa kwanza wa kiume wa mnyama ambaye alitolewa sadaka kwa Mungu.

Dhana hii inaweza kutumika kitamathali. Kwa mfano, taifa la Israeli linaitwa mzaliwa wa kwanza wa Mungu kwa sababu Mungu aliwapa faida maalumu kuliko mataifa mengine.

Yesu, Mwana wa Mungu anaitwa mzawa wa kwanza wa Mungu kwa sababu ya umuhimu wake na mamlaka juu ya kila mtu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Pale ambapo "mzaliwa wa kwanza" inajitokeza katika maandishi pekee, inaweza kutafsiriwa kama "mzawa wa kiume wa kwanza" kwa maana ndiyo kile kinachokusudiwa.

mzeituni

Ufafanuzi

Mzeituni ni mdogo, tunda la mviringo kutoka mti wa mzeituni, ambayo uota maeneo yanayo zunguka Bahari ya Mediterenia.

- Miti ya mizeituni ni ya majani makubwa yenye maua meupe. Uota vizuri sehemu za joto na kustahimili maji kidogo.
- Matunda ya mzeituni ni ya kijani kwa rangi, ubadilika meusi yanapo komaa. Mzeituni utumika kula na kukamua mafuta.
- Mafuta ya mzeituni yalitumika kupika, kuwasha taa, na sherehe za kidini.
- Katika Biblia, miti ya mizeituni na matawi utumika kifumbo kumaanisha watu.

mzigo

Ufafanuzi

Mzigo ni kitu kizito. Kwa uhalisia inamaanisha uzito wa kitu ambacho mnyama wa kazi angeweza kubeba. Neno "mzigo" pia linamaana kadhaa za kimafumbo:

- Mzigo waweza kumaanisha kazi ngumu au wajibu wa mhimu ambao mtu anapaswa kuufanya. Anaswemwa "kuuchukua" au "kuubeba" "mzigo mzito."
- Kiongozi katili aweza kuweka mizigo mizito kwa watu anaowaongoza, mfano kwa kuwalazimisha kulipa kiwango kikubwa cha ushuru.
- Mtu asiyependa kuwa mzigo kwa mtu mwingine hapendi kumsababishia mtu huyo shida yoyote.
- Hatia ya dhambi za mtu ni mzigo kwake.
- "Mzigo wa Bwana" ni tamathari ya usemi kumaanisha "ujumbe kutoka kwa Mungu" ambao nabii anapaswa kuutoa kwa watu wa Mungu.
- Neno "mzigo" laweza kufasiriwa kuwa "wajibu" au "jukumu" au "mzigo mzito" au"ujumbe," kutegemeana na mazingira.

nabii wa uongo

Ufafanuzi

Nabii wa uongo ni mtu ambaye hudai kimakosa ya kwamba ujumbe wake unatoka kwa Mungu.

Tabiri za manabii wa uongo mara kwa mara hazitimiliki. Yaani, haziji kuwa kweli.

Manabii wa uongo hufundisha ujumbe ambao kwa juu juu au kwa ukamili hupingana na kile ambacho Biblia husema.

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "mtu ambaye hudai kwa uongo ya kuwa ni msemaji wa Mungu" au "mtu ambaye hudai kimakosa kuzungumza maneno ya Mungu".

Agano Jipya hufundisha ya kwamba kipindi cha mwisho kutakuwa na manabii wengi wa uongo ambao watajaribu kudanganya watu kufikiri ya kwamba wanatoka kwa Mungu.

nafaka

Ufafanuzi

Msemo "nafaka" mara nyingi ulimaanisha mbegu ya mmea wa chakula kama vile ngano, shayiri, mahindi, mtama, au mchele. Inaweza pia kumaanisha mmea wote.

Katika Biblia, nafaka kuu ambayo inazungumziwa ni ngano na shayiri.

Vichwa vya nafaka ni sehemu ya mmea ambao hushikilia nafaka.

Kumbuka ya kwamba baadhi ya tafsiri za zamani za Biblia hutumia neno "mahindi" kumaanisha nafaka kwa ujumla. Hata hivyo katika lugha ya Kiingereza ya sasa, "mahindi" humaanisha aina moja ya nafaka tu.

Najisi

Ufafanuzi

Kukinajisi kitu inamaana ya kufanya jambo kwa namna ya unajisi au kutokukiheshimu kitu ambacho ni kitakatifu.

- Mtu ambaye ni najisi ni mtu ambaye anafanya mambo ambayo sio matakatifu na hamuheshimu Mungu.
- Mungu aliwaambia Waisraeli kwamba wamejinajisi wenyewe kwa sanamu akiwa ana maana ya kwamba wamejichafua kwa dhambi hiyo. Pia hawakumuheshimu Mungu.

najisi, kunajisiwa

Ufafanuzi

Msemo wa "najisi" na "kunajisiwa" ina maana ya kuchafuliwa au uchafu. Kitu kinaweza kunajisiwa kihalisia, kimaadili au kwa kaida za dini.

Mungu aliwaonya Waisraeli wasijinajisi kwa kula au kugusa vitu ambavyo vimewekwa wakfu kuwa "chafu" au "kiovu".

Baadhi ya vitu kama maiti na magonjwa ya kuambukiza vilitamkwa na Mungu kuwa vichafu na vinaweza kunajisi mtu iwapo atavigusa.

Mungu aliwaamuru Waisraeli kuacha uasherati. Hivi vingewatia unajisi na kuwafanya kutokubalika kwa Mungu.

Pia kulikuwa na aina kadhaa ya hatua za kimwili ambazo zilimnajisi mtu kwa muda mfupi hadi atakapokuwa safi kwa kaida za dini tena.

Katika Agano Jipya, Yesu alifundisha ya kwamba mawazo ya dhambi na matendo ndiyo haswa yanayomnajisi mtu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo wa "najisi" unaweza kutafsiriwa kama "kusababisha kuwa chafu" au "kusababisha kuwa muovu" au "kusababisha kutokubalika kwa kaida za dini".

"Kunajisiwa" kunaweza kutafsiriwa kama "kuwa mchafu" au "kusababisha kutokubalika kimaadili"

ndara

Ufafanuzi

Ndara ni kiatu chenye soli bapa kilicho shika mguu na kamba iliyo zunguka mguu au kisigino. Ndara zinavaliwa na wanaume na wanawake.

- Ndara wakati mwingine ilitumika kuthibitisha muhamala halali, kama kuuza mali kwa mtu mmoja kutoa ndara na kumpatia mwingine.
- Kuondoa kiatu cha mtu au ndara ilikuwa ishara ya heshima, hususani katika uwepo wa Mungu.
- Yohana alisema hakustahili kufungua kamba za ndara za Yesu, ambayo ingekuwa kazi ya mtumishi wa chini au mtumwa.

ndoto

Ufafanuzi

Ndoto ni kitu ambacho watu huna au kupitia akilini mwao wanapokuwa wamelala.

Ndoto mara kwa mara huonekana kama zinatokea kihalisia, lakini haziko hivyo.

Mara nyingine Mungu husababisha watu kuota juu ya kitu ili waweze kujifunza kutoka na hicho kitu. Pia anaweza kuzungumza moja kwa moja na watu ndani ya ndoto zao.

Katika Biblia, Mungu alitoa ndoto maalumu kwa baadhi ya watu kuwapa ujumbe, mara nyingi kuhusu jambo ambalo lingetoke hapo baadaye.

Ndoto ni tofauti na maono. Ndoto hutokea wakati mtu amelala, lakini maono mara kwa mara hutokea wakati mtu yupo macho.

Neno

Ufafanuzi

Neno ni kitu ambacho mtu husema.

- Kwa mfano wakati ambao malaika alimwambia Zakaria "hauamini maneno yangu," alikuwa na maana ya kuwa "huamini nilichokisema."
- Neno humaanisha ujumbe mzima na sio neno moja.
- Kwenye Biblia neno ni kilakitu alichosema Mungu au kuamuru, "neno la Mungu" au "neno la kweli."
- Matumizi ya pekee ya neno ni wakati Yesu anapoitwa "neno."

Neno la kweli

Ufafanuzi

"Neno la kweli" ni njia nyingine ya kuelezea neno la Mungu au mafundisho yake.

- Neno la kweli la Mungu ni pamoja na kilakitu ambacho Mungu anafundisha watu wake kuhusu yeye, uumbaji wake na mipango yake ya ukumbozi kupitia Yesu.
- Neno la kweli linasisitiza kuwa anachotuambia Mungu ni kweli na hakika.

ng'ombe

Ufafanuzi

"ng'ombe" lina husu aina ya mifugo waliyo fundishwa kulima mazao.

- Katika Biblia, ng'ombe wana hashiriwa kama wanyama waliyo fungwa na nira kuvuta gari au kulima.
- Ng'ombe wakifanya kazi pamoja chini ya nira ilikuwa kawaida ya tukio katika Biblia hadi kwamba msemo "kuwa chini ya nira" ilikuwa umbo la kazi ngumu.
- Ng'ombe dume, hajatahiriwa walakufunidshwa kuwa mnyama wa kazi.

Ng'ombe, fahali, ndama, mifugo

Ufafanuzi

Mifugo ni kundi kubwa la wanyama wenye miguu minne wanaokula majani na hufugwa kwa ajili ya maziwa na nyama.

- Ng'ombe dume huitwa fahali na ng'ombe mdogo huitwa ndama.
- Mara nyingine ng'ombe hutumika kuwakilisha aina zote za mifugo.
- Katika tamaduni zingine ng'ombe hubadilishwa na bidhaa katika biashara. Mara nyingine hutumika kama zawadi itolewayo kwa wazazi wa binti na mwanaume anayetaka kumuoa.
- Katika Biblia Wayahudi walitumia mifugo kwa ajili ya dhabihu hasa ng'ombe mwekundu.
- Ng'ombe mwekundu ni ng'ombe ambaye hajazaa bado.
- Pia kuna ng'ombe dume ambaye hutumika katika shughuli za kilimo.

Ngamia

Ufafanuzi

Ni mnyama mkubwa mwenye miguu minne na mwenye nundu moja au mbili mgongoni.

Ngano

Ufafanuzi

Ngano ni aina ya nafaka ambayo watu huzalisha kwa ajili ya chakula. Biblia inapotaja ngano au mbegu inazungumza juu ya nafaka ya ngano au mbegu.

- Mbegu za ngano au nafaka huota juu ya mmea wa ngano.
- Baada ya kuvuna ngano, nafaka hutenganishwa na shina la mmea kwa kupura. Shina ala ngano pia huitwa mabua na mara nyingine huwekwa chini kwa ajili ya wanyama kulalia.
- Watu husaga ngano kwenye sakafu na hutumia kutengenezea mkate.

ngao

Ufafanuzi

Ngao ni chombo kinacho shikiliwa na mwanajeshi katika pambano kuweza kujilinda hasiumizwe na silaha za maadui.

- Ngao zilikuwa za mviringo na zilitengenezwa na vifaa kama vile ngozi, mbao, au chuma ngumu na nene kuweza kuzuia upanga au mshale kutoboa.
- Kwa kutumia hili neno kama mfano, Biblia inamtaja Mungu kama ngao ya ulinzi kwa watu wake.
- Paulo Pia anaeleza "ngao ya imani," ambayo ni umbo linalo onyesha kuwa kuishi kwa kumuamini Yesu, na kumtii Mungu, kutawalinda waamini kutokana na mashambulio ya kiroho ya Shetani.

ngome, kimbilio

Ufafanuzi

Maneno "ngome" na "kimbilio" yote ueleza maeneo yaliyo lindwa dhidi ya shambulio na maadui wanajeshi.

- Mara kadhaa, ngome na kimbilio ni sehemu zilizo tengenezwa na kuta kijihami. Zaweza pia kuwa sehemu zilizo inuka kama milimani.
- Watu uimarisha ngome kwa kujenga kuta nene au majengo mengine yanayo fanya vigumu kwa adui kuingia.
- "Ngome" au "kimbilio" yaweza tafsiriwa kama "sehemu iliyo lindwa"
- Hili neno pia utumika kifumbo kumanisha Mungu ni ngome au kimbilio kwa wao wanao muamini.

ngumu, ugumu, fanya - gumu

Ufafanuzi

Neno 'ngumu' lina maana nyingi sana kutegemea na muktadha. Mara nyingi hueleza kuwa kitu fulani ni kigumu, kuvumilia au kutotoa/kutozaa. Maelezo kama "moyo mgumu" au " kichwa kigumu" inarejelea watu wakaidi wasiotubu. Maneno haya yanaongelea watu wanaoendelea kumwasi Mungu. Lugha ya picha ya maneno 'ugumu wa moyo" na "ugumu wa mioyo yao' yana maana pia ya kuwa na kiburi na uasi. Kama moyo wa Mtu umefanywa 'kuwa mgumu' hii ina maana kuwa mtu huyo anakataa kumtii na kubaki kuwa mkaidi asiyetaka kutubu. Neno moyo likitumika kama kielezi " kwa moyo" likimaanisha kufanya kazi kwa nguvu na kwa juhudi ili kufanya kitu vizuri.

Mapendekezo ya tafsiri Neno ' -gumu"laweza kufasiriwa kama 'ukaidi' au "ugumu' au 'changamoto' kwa kutegemea na muktadha. Maneno kama 'ugumu' au 'ugumu wa moyo'' .yanaweza kutafsiriwa kama " ukaidi' au kudumu katika uasi' au 'mtazamo wa uasi' au ' uasi' au hali ya kutotubu.
"Usiufanye moyo wako kuwa mgumu" inaweza kufasiriwa kama "usikate kutubu '' au "usiendelee kuasi kwa ukaidi." Maneno kama "kuwatesa watu kwa kazi ngumu" yaweza kutafsiriwa kama "lazimisha watu kufanya kazi ngumu kwa kiwango cha kuwatesa au kusababisha mateso kwa watu kwa kuwalazimsha kufanya kazi ngumu. "kazi ngumu" neno hili huhusishwa zaidi na kazi ngumu au ugumu anaokutana nao mwanamke katika kipindi cha kujifungua mtoto.

nguo ya gunia

Ufafanuzi

Nguo ya gunia ilikuwa ya kukwaruza, nguo iliyo tengenezwa kwa nywele ya mbuzi au nywele ya ngamia.

- Nguo zilizo tengenezwa kwa gunia ili kuwa sio nzuri mwilini kwa mtu aliyo vaa. Ilivaliwa kwa ajili ya kuonyesha kilio, uzuni, au toa ya unyenyekevu.
- Maneno "nguo ya magunia na majivu" ilikuwa ni msemo uliyo zoeleka ukihashiria namna ya kitamaduni ya uzuni na toba.

Nguruwe

Ufafanuzi

Mguruwe ni mnyama mwenye mihuu minne anayefugwa kwa ajili ya nyama. Nyama yake inaitwa nyama ya nguruwe.

- Mungu aliwaambia Waisraeli wasile nguruwe na kuiona kuwa ni najisi. Mpaka leo Wayahudi wanaona nguruwe kuwa ni najisi na hafai kuliwa.
- Nguruwe wanafugwa kwenye mashamba na kuuzwa kwa watu wengine kwa ajili ya nyama.

nguva

Ufafanuzi

Neno "nguva" ni mnyama mkubwa wa baharini anaye kula nyasi na mimea mingine katika sakafu ya bahari.

- Nguva ni wa kijivu mwenye ngozi nene. Anatembea kwenye maji kwa kutumia kikono.
- Ngozi za nguva zilitumika na watu wa Biblia kwa kutengeneza mahema. Hizi ngozi za wanyama zilitumika kwa vifuniko vya maskani.

nguzo ya mlango

Ufafanuzi

"Nguzo ya mlango" ni mhimili ulio wima katika pande zote za mlango, ambao unategemeza kiunzi cha mlango cha juu.

Kabla tu Mungu hajawasaidia Waisraeli kutoroka kutoka Misri, aliwaelekeza kuua mwanakondoo na kuweka damu yake juu ya nguzo za milango.

Katika Agano la Kale, mtumwa aliyetamani kumtumikia bwana wake maisha yake yote aliweka sikio lake juu ya nguzo ya mlango wa nyumba ya bwana wake na msumari kupigiliwa katika sikio lake katika nguzo ya mlango.

Hii inaweza kutafsiriwa kama "nguzo ya mbao iliyo katika kila upande wa mlango" au "pande za viunzi vya mlango" au "nguzo za mbao zilizo pande za mlango".

nguzo, safu

Ufafanuzi

"Nguzo" ni nguzo kubwa zilizosimama wima zinazotumika kushikilia paa au sehemu nyingine ya jengo. Jina lingine la nguzo ni safu.

- Katika nyakati za Biblia Nguzo zilitumika kushikilia majengo ambayo mara nyingi yalichongwa toka kwenye kipande cha jiwe.
- Samsoni katika agano la kale alipokamatwa na Wafilisti aliharibu hekalu lao la kipagani kwa kuzisukuma nguzo zilizoshikilia na kusababisha hekalu kuanguka.
- Nguzo pia inaweza kuwa jiwe kubwa lililowelwa kama alama ya kaburi au alama ya sehemu ambayo tukio la muhimu lilifanyika.
- Pia nguzo yaweza kuwa sanamu iliyotengenezwa kwa ajili ya kuabudu miungu ya uongo.
- Nguzo pia yaweza kuwa kitu kilichotengenezwa kama nguzo mfano "nguzo ya moto" iliyowaongoza Waisraeli usiku katika jangwa au "nguzo ya chunvi" ambayo mke wa Lutu alikuja kuwa hivyo baada ya kuangalia nyuma.

nia

Ufafanuzi

Neno "nia" la husu sehemu ya mtu inayo fikiri na kufanya maamuzi.

- Nia ya kila mtu ni jumla ya mawazo na fikra yake.
- Kuwa na "nia ya Kristo" ina maana kufikiri na kutenda kama Yesu Kristo alivyo waza na kufanya. Ina maana kuwa mtiifu kwa Mungu Baba, kutii mafundisho ya Kristo, kuwezeshwa kufanya hivi kupitia nguvu ya Roho mtakatifu.
- "Kubadilisha nia yake" ina maana mtu alifanya uwamuzi tofauti au alikuwa na maoni tofauti na yale alikuwa nayo.

Nira

Ufafanuzi

Nira ni kipande cha mbao au chuma kinachowekwa kwa wanyama wawili au zaidi ili kuwaunganisha kwa ajili ya lengo la kuvuta plau au gari.

- Pia nira imetumika kuelezea kitu kilichowaunganisha watu kwa ajili ya lengo la kufanya kazi pamoja kwa mfano kumtumikia Yesu.
- Paulo anatumia neno "mjoli" kumaanisha mtu anayemtumikia Yesu kama alivyo.
- Neno "nira" pia linaweza kutumika kama mzigo mzito ambao mtu anaubeba kwa mfano anayetumikishwa utumwani au kwenye mateso.
- Namna nyingine ya kutafsiri neno hili waweza kutumia neno "mzigo mzito".

njaa

Ufafanuzi

Msemo "njaa" una maana ya upungufu mkubwa sana wa chakula katika nchi au eneo lote, mara nyingi kutokana na kutokuwa na mvua ya kutosha.

Mazao ya chakula yanawvza kushindwa kutokana na sababu za asili kama vile ukosefu wa mvua, magonjwa ya mazao, au wadudu.

Upungufu wa chakula pia unaweza kusababishwa na watu, kama vile adui kuangamiza mazao.

Katika Biblia, Mungu mara nyingi huleta njaa kama njia ya kuadhibu mataifa wanapotenda dhambi dhidi yake.

Katika Amosi 8:11 msemo "njaa" unatumika kitamathali kumaanisha kipindi ambapo Mungu aliadhibu watu wake kwa kutozungumza nao. Hii naweza kutafsiriwa kwa neno moja kwa ajili ya "njaa" kwa lugha yako, au kwa msemo kama wa "upungufu mkubwa".

njiwa, ninga

Ufafanuzi

Njiwa na ninga ni aina mbili ya ndege wadogo wa kijivu na kahawia ambao wanafanana. Njiwa mara nyingi hufikiriwa kuwa na rangi iliyo nyepesi, karibu na nyeupe.

Baadhi ya lugha zina majina mawili tofauti kwa ajili yao, wakati wengine wanatumia jina moja kwa wote wawili.

Njiwa na ninga walitumiwa katika sadaka kwa Mungu, hasa kwa watu ambao hawakuweza kununua wanyama wakubwa.

Njiwa mara nyingine huashiria usafi, sio na hatia, au amani.

Kama njiwa au ninga hawajulikani katika lugha ambayo tafsiri inafanywa, msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "ndege mdogo, wa kijivu na kahawia anayeitwa njiwa".

Kama njiwa na ninga wote wanawekwa katika mstari mmoja, ni vyema kutumia maneno mawili tofauti kwa ndege hawa, ikiwezekana.

nuru

Ufafanuzi

Kuna matumizi kadhaa ya kimafumbo ya neno "nuru" katika Biblia. Mara nyingi inatumika kama sitiari ya haki, utakatifu, na ukweli.

Yesu alisema, "Mimi ni nuru ya ulimwengu" kumaanisha kuwa analeta ujumbe wa kweli wa Mungu duniani na kuwaokoa watu kutoka kwenye giza la dhambi zao. Wakristo wanaamriwa "kutembea nuruni," ambayo inamaanisha wanatakiwa kuishi jinsi Mungu anavyotaka waishi na kuacha kutenda maovu. Mtume Paulo alisema kuwa "Mungu ni nuru," na hakuna giza ndani yake. Nuru na giza ni tofauti kabisa. Giza ni ukosefu wa nuru. Yesu alisema kuwa yeye "ni nuru ya ulimwengu" na kwamba wafuasi wake wanapaswa kung'aa kama nuru duniani, kwa kuishi kwa naamna inayoonesha ukubwa wa Mungu. "Kutembea nuruni" inaonesha kuishi njia inayompendeza Mungu, kufanya yaliyo mema na sawa. Kutembea gizani inaonesha kuishi kwa kuasi dhidi ya Mungu, kufanya mambo maovu.

nyakuliwa, nyakuliwa pamoja

Ufafanuzi

Neno "nyakua" mara nyingi linamrejea Mungu akimchukua mtu juu mbinguni ghafula, katika njia ya muujiza.

- Tafsiri ya "nyakua pamoja" inaonyesha kuja kwa mwingine baada kumfikia kwa haraka. Neno hili ni kitu kile kile na "pita."
- Mtume Paulo alizungumzia kuhusu hali ya "nyakuliwa" pamoja kuonana naye mawinguni.
- Paulo alisema kwamba wakati Kristo atakaporudi, Wakristo wata "nyakuliwa" pamoja kuonana naye hewani.
- Maana ya fumbo, "dhambi zangu zimechukuliwa na mimi" inaweza kutafsiriwa kama, "Ninapokea matokeo ya dhambi zangu" au "kwa sababu ya dhambi zangu ninasumbuku" au "dhambi zangu zinanifanya nisumbuke"

nyenyekea, kwa unyenyekevu

Ufafanuzi

Neno "nyenyekea" mara nyingi umanisha kumueka mtu chini

- Biblia uwaambia waamini wa Yesu kunyenyekea kwa Mungu na mamlaka nyingine katika maisha yao.
- Maelekezo "kunyenyekea ninyi kwa ninyi" ina maana ya kukubali marekebisho na kuangalia mahitaji ya wengine.

nyoka

Ufafanuzi

Neno "nyoka" la husu

Nyumba

Ufafanuzi

Istilahi 'nyumba' hutumika kama tamathali ya semi (mfano) katika Biblia. Mara nyingine hutumika kumaanisha 'kaya' kurejelea watu wanaoishi pamoja katika nyumba. Mara zote neno 'nyumba' humaanisha wazao au watoto au ndugu wengine. Mfano, nyumba ya Daudi huwa na maana ya uzao wa Daudi. Maneno kama 'nyumba ya Mungu' au 'nyumba ya Yahweh' huwa na maana ya hekalu au hema la kukutania au sehemu Mungu alipo. Katika Waebrania 3, "Nyumba ya Mungu" ni sitiari ikimaanisha Watu wa Mungu. Kifungu cha maneno ' nyumba ya Israeli" kwa ujumla huwa na maana ya taifa laote la Israeli au hasa hasa kwa makabila ya ufalme wa Kasikazini wa Israeli.

Mapendekezo ya tafsiri kwa kutegemeana na muktadha, neno, nyumba linaweza kuwa na maana ya 'kaya' ' watu, familia, uzao, hekalu au sehemu ya kukaa.'' "Nyumba ya Daudi' in maana ya ''ukoo wa Daudi, familia ya Daudi au uzao wa Daudi. "Nyumba ya Israeli' ina maana ya watu wa Israeli au wazao wa Israeli au waisraeli. 'Nyumba ya Yahweh' ina maana ya hekalu au sehemu ya kumwabudia Mungu.

nyumba ya ghala

Ufafanuzi

"nyumba ya ghala" ni jengo kubwa linalo tumika kuhifadhi chakula au vitu vingine, mara nyingi kwa muda mrefu.

- Katika Biblia "nyumba ya ghala" ilitumika kuhifadhi nafaka na vyakula vingine kutumika baadae palipo kuwa na uaba wa chakula kwasababu ya ukame.
- Nyumba za ghala la hekalu lilikuwa na hifadhi ya vitu vingi, kama dhahabu na fedha, vilivyo tolewa kwa Yahweh. Vingine vilitumika kukarabati hekalu.

nzige

Ufafanuzi

Neno "nzige" linamaanisha aina kubwa ya panzi anayepaa ambaye wakati mwingine hupaa katika makundi makubwa ambayo huleta madhara makubwa, wakila mboga zote njiani.

Nzige na panzi wengine ni wakubwa, wenye mabawa yaliyo wima na miguu ya nyuma mirefu inayowapa uwezo wa kuruka mbali. Katika Agano la Kale, makundi ya nzige yanazungumziwa kimafumbo kama alama au picha ya uharibifu mkubwa utakaokuja kama matokeo ya kutokutii kwa Israeli. Mungu alituma nzige kama moja ya mapigo kumi dhidi ya Wamisri. Agano Jipya linasema kuwa nzige walikuwa chanzo kikubwa cha chakula cha Yohana mbatizaji alipokuwa akiishi jangwani.

Onyo

Ufafanuzi

Onyo ni kitu ambacho kinawatahadharisha watu juu ya jambo fulani ambalo linaweza kuwadhuru. "kuonywa" ni kuambiwa juu ya jambo fulani la hatari.

- Mfalme Yehoshafati alionywa aliposikia Wamoabu wanapanga kuvamia ufalme wa Yuda.
- Yesu aliwaambia wanafunzi wake wasiwe na wasiwasi watakaposikia juu ya majanga yatakayotokea siku za mwisho.
- "kutoa onyo" inamaanisha kutoa tahadhari. Zamani mtu aliweza kupaza sauti za kutoa onyo kwa kupiga kelele ya kitu kama kengele.

Pagani

Ufafanuzi

Katika nyakati za Biblia neno "pagani" lilitumika kuwaelezea watu ambao waliabudu miungu ya uongo badala ya Bwana.

- Kilakitu kilichokuwa kinahusiana na watu hawa kama madhabahu walizokuwa wanaabudia, ibada walizokuwa wakifanya na imani zao zote zilikuwa zikiitwa "pagani"
- Mfumo wa imani wa kipagani ulijumuisha kuabudu miungu ya uongo na kuabudu asili
- Baadhi ya dini za kipagani zilijumuisha ibada za uzinzi na mauaji ya watu kama sehemu ya kuabudu kwao.

panda, mpandaji, mmea

Ufafanuzi

"kupanda" ina maana kuweka mbegu kwenye ardhi ilikuweza kuotesha mimea. "Mpandaji" ni mtu anaye mpanda au kupanda mbegu.

- Njia ya kupanda au kuotesha kwa tafautiana, lakini mbinu moja ni kuchukuwa mkono uliyo jaa mbegu na kusambaza kwenye ardhi.
- Mbinu nyingine ya kuotesha ni kufanya mashimo katika udogo na kuweka mbegu katika kila shimo.
- Neno "panda" laweza tumika kimfano kama vile, "mtu atavuna alicho panda."

Pazia

Ufafanuzi

Katika Biblia pazia ni kitu kinene, chenye nyenzo nzito kinachotumika kutengenezea maskani na hekalu.

- Maskani ilitengemezwa kwa matabaka manne ya pazia kwa juu na pembeni. Mapazia haya yanayofunika yalitengenezwa kwa nguo au ngozi za wanyama.
- Mapazia ya nguo yalitumika pia kutengeneza ukuta uliozunguka ua la maskani.
- Yote maskani na jengo la hekalu, pazia zito lilikuwa kati ya patakatifu na patakatifu pa patakatifu. Ni pazia hili lililopasuka kwa miujiza Yesu alipokufa.

Pembe, Mapembe

Ufafanuzi

Mapembe ni sehemu za juu katika kichwa cha mnyama zilizo ngumu, za kudumu na zilizochongoka. Wanyama wa aina nyingi huwa na mapembe, wanyama kama ng'ombe, kondoo, mbuzi, swala n.k. Pembe la kondoo dume lilitumika kutengeneza chombo cha muziki kilichoitwa 'sofari' ambacho kilipulizwa katika matukio maalumu ya sikukuu za kidini. Mungu aliwaambia waisraeli kutengeneza pembe nzuri katika kila kona ya madhabahu ya uvumba. Neno pembe wakati mwingine lilitumika kurejelea chupa iliyokuwa imetengenezwa kwa muundo kama pembe na ilitumika kwa ajili ya kutunza maji au mafuta. Chupa hii ilitumika katika kuwatia mafuta wafalme kama vile Samweli alivyofanya kwa Daudi. Neno hili inabidi litafsiriwe kwa neno tofauti na tarumbeta. Neno hili 'lpembe' hutumika pia kama lugha ya picha kumaanisha ' nguvu, uwezo, na mamlaka

pepeta, chekecha

Ufafanuzi

"Pepeta" na "chekecha" ni kutenganisha ngano na makapi. Katika Biblia maneno yote mawili yametumika yakimaanisha kutenganisha au kuwagawa watu.

- Kupepeta inamaana ya kutenganisha ngano na makapi kwa kupepeta juu ya hewa na kuruhusu upepo kupeperusha makapi.
- Kuchekecha ni kutingisha ngano iliyopepetwa kwenye ungo ili kutoa makapi yaliyobaki kama mawe.
- Katika agano la kale kupepeta na kuchekecha imetumika kuelezea ugumu unaotenganisha watu wenye haki na wasio haki.
- Yesu pia anatumia neno kuchekecha kumwambia Simoni Petro ni kwa namna gani yeye na wanafunzi wengine watajaribiwa imani yao.

Pigo

Ufafanuzi

Mapigo ni matukio yanayosababisha mateso au kifo kwa idadi kubwa ya watu. Mara nyingi pigo laweza kuwa magonjwa yanayosambaa kwa haraka na kusababisha watu wengi kufa kabla ya kuweza kudhibitiwa.

- Mapigo mengi yana sababu zake lakini mengine yanatumwa na Mungu ili kuwaadhibu wenye dhambi.
- Nyakati za Musa Mungu alituma mapigo kumi juu ya Wamisri ili kumfanya Farao awaache Waisraeli waondoke Misri. Mapigo haya yalikuwa maji kugeuka kuwa damu, magonjwa, wadudu kuharibu mazao, siku tatu za giza na vifo vya watoto wa kwanza.
- Hii yaweza kutafsiriwa kama "majanga makubwa" au "ugonjwa unaoenea" kutegemea na muktadha.

Plau

Ufafanuzi

"Plau" hiki i kifaa cha shambani kinachotumika kuvunjavunja udongo na kuandaa shamba kwa ajili ya kupanda.

- Plau ina makali, na meno ya jembe yanayochimba kwenye udongo. Mara nyingi huwa na mpini ambao mkulima hutumia kuiongoza plau.
- Katika nyakati za Biblia plau zilisukumwa na jozi ya ng'ombe au mnyama mwingine wa kazi.
- Plau nyingi zimetengenezwa na mbao ngumu isipokuwa sehemu ya mcha ambayo hutengenezwa na chuma.

Ponya, tibu

Ufafanuzi

Maneno 'ponya' na 'tibu' yote mawili yana maana ya kumfanya mtu aliye mgonjwa, aliyejeruhika na asiyejiweza (mlemavu) kuwa na afya nzuri tena. Mtu aliyeponya au kutibiwa amekuwa amefanywa mzima na mwenye afya nzuri tena. Uponyaji waweza kutokea tu kiuasilia bila kutumia kitu chochote, hii ni kwasababu Mungu alitupa miili yenye uwezo wa kupona na kurudia hali yake ya kawaida hata kama ina vidonda au magonjwa ya aina mbalimbali. Aina hii ya uponyaji hutokea polepole. Hata hivyo hali zingine kama kuwa upofu au ulemavu, na magonjwa mengine kama ukoma hayawezi kupona menyewe tu. Wakati watu wenye magonjwa kama haya wanapoponywa huwa ni muujiza ambao hautokei mara kwa mara. Kwa mfano, Yesu aliponya watu wengi walikuwa vipofu, vilema na wagonjwa na wakapona hapo hapo. Mitume pia waliponya watu kwa miujiza, kwa mfano Petro alimfanya mlevu aweze kutembea mara hiyo.

pukuta, pukuchua

Ufafanuzi

Maneno "pukuta" na "pukuchua" yanaeleza sehemu ya kwanza ya gawanya nafaka ya ngano kutoka kwenye mmea wa ngano.

- Kupukuta mmea wa ngano una legeza nafaka kutoka kwenye ganda lake. Baada ya hapo nafaka ina "pepetwa" kugawanya kabisa nafaka kutoka kwenye majani yote yasio itajika, ikiacha sehemu ya nafaka inayo lika.
- Wakati wa Biblia, "eneo la kupukuta" lilikuwa sakafu au sehemu iliyo shindiliwa udongo, ikiweka ugumu, kwenye sakafu kusagia nafaka.
- "Gari la kupukuta" wakati mwingine lilitumika kusaga nafaka na kusaidia kugawanya kutoka kwenye jani lake.

Pumzika

Ufafanuzi

Pumzika inamaana ya kuacha kufanya kazi kwa nia ya kupumzika na kupata nguvu.

- Kitu kikiwa kimepumzika ina maana kuwa kimesimama au kukaa mahali.
- Meli iliyopumzika mahali imesimama na kutia nanga.
- Mtu au mnyama anapopumzika yaweza kuwa amekaa au amelala kwa ajili ya kustarehe.
- Mungu aliwaamuru Waisraeli wapumzike siku ya saba ya wiki. Siku hii ya kutokufanya kazi iliitwa Sabato.

punda, nyumbu

Ufafanuzi

Punda ni mnyama wa kazi mwenye miguu minne, anayefanana na farasi, lakini mdogo kidogo na mwenye masikio marefu zaidi.

Nyumbu ni uzao tasa atokanaye na punda dume na farasi jike.

Nyumbu ni wanyama wenye nguvu sana na kwa hiyo ni wanyama wa kazi wenye thamani sana.

Punda na nyumbu wote wanatumika kubeba mizigo na watu wanaposafiri.

Katika kipindi cha Biblia, wafalme huendesha punda katika wakati wa amani, kuliko farasi, ambaye alitumika katika kipindi cha vita.

Yesu aliendesha kuingia Yerusalemu juu ya punda mdogo wiki moja kabla hajasulubiwa kule.

Ripoti

Ufafanuzi

Ripoti inamaana kuwaambia watu kuhusu kitu kilichotokea kutoa habari juu ya tukio hilo. Ripoti yaweza kutamkwa au kuandikwa.

- "Ripoti" yaweza kutafsiriwa kama "kusema" au "kuelezea kwa kina."
- Sentensi inayosema "usiripoti hili kwa mtu yeyote" inamaana kuwa "usiseme jambo hili kwa mtu yeyote."

Rudi

Ufafanuzi

Neno "rudi" linamaanisha kurudi au kurudisha kitu.

- "Kurudia" ni kitendo cha kuanza kufanya kitu tena.
- Waisraeli walipoirudia miungu yao walianza kuiabudu tena.
- Waliporudi kwa Bwana, walitubu na walimwabudu Mungu tena.
- Kurudisha ardhi au vitu vilivyochukuliwa au kupokelewa toka kwa mtu inamaana ya kurudisha mali ile kwa mwenye mali.
- "Kurudi" yaweza kutafsiriwa kama "kurudi nyuma" au "kurudisha"

rushwa

Ufafanuzi

Neno "rushwa" inamaanisha kumpa mtu kitu cha thamani, kama pesa, kumshawishi afanye jambo bila uaminifu.

- Askari waliolilinda kaburi wazi la Yesu walipewa rushwa ya pesa wakasema uongo juu ya kilichotokea.
- Wakati mwingine maofisa wa serikali wanapewa rushwa ili wasilione kosa au kupiga kura kwa njia nyingine.
- Biblia inazuia kutoa au kupokea rushwa.
- Neno, "rushwa" laweza kutafasiriwa kama "malipo yasiyo harali" au "malipo ya uongo" au "thamani ya kuvunja sheria".
- "Kufanya ongo" kwaweza kutafasiriwa kwa neno au kifungu kinachomaanisha, "kulipa ili kushawishi (mtu)" au "kulipa ili upendeleo usio halari ufanyike" au "kulipa kwa ajili ya upendeleo."

Rushwa

Ufafanuzi

Rushwa ni hali ambayo watu wameharibika,hawana maadili na sio waaminifu.

- Rusha inamaana ya kuharibika kimaadili.
- Mtu ambaye ni fisadi ameacha kabisa kweli na kufanya mambo yasiyofaa na yaliyoharibika.
- Pia kuna kitendo cha kumfanya mtu awe fisadi kwa kumchochea asiwe mwaminifu na afanye mambo yasiyo na maadili.

saa

Ufafanuzi

Neno "saa" linatumika mara kwa mara katika Biblia kuonesha muda wa siku jambo fulani lilipotendeka. Pia linatumia tamathari kumaanisha "wakati" au "kitambo"

- Wayahudi walihesabu masaa ya kutwa kuanzia mawio ya jua (kama saa 12:00 asubuhi). Kwa mfano, "saa tisa" alasiri.
- Masaa ya usiku yalihesabiwa kuanzia machweo (kama saa 12: 00 jioni). Kwa mfano, "saa tatu ya usiku" kumaanisha karibia saa tisa za usiku" katika mfumo wetu wa siku hizi.
- Kwa kuwa kumbukumbu za muda katika Biblia hazitalingana kamili na mfumu wa siku hizi, vifungu kama vile "karibia saa tisa" au "kama saa sita kamili" yaweza kutumika.
- Baadhi ya tafasiri zaweza kuonesha vifungu kama vile "wakati wa jioni" au "wakati wa asubuhi" au "wakati wa mchana" kuweka wazi ni muda upi wa siku unaozungumzwa.
- Kirai, "wakati uo" chaweza kutafasiriwa kama "katika wakati ule" au "katika kitambo hicho".
- Kwa kumtaja Yesu, kifungu "wakati wake umefika" yaweza kutafasiriwa kama, "muda wake wa kufanya" au "muda uliowekwa kwa ajili yake ulikuwa umefika."

Saa

Ufafanuzi

Pamoja na kutumika kuonesha wakati au muda gani jambo lilitokea, neno 'saa' hutumika kwa namna nyingi kimfano kama tamathali za semi. Wakati mwingine 'saa' hutumika kuonesha muda maalumu uliopangwa, kwa mfano 'saa ya maombi.' Wakati maandiko yanaposema kuwa saa imefika kwa Yesu kuteswa na kuuawa, ilikuwa na maana ya muda maalumu uliowekwa ambao MUngu alikuwa ameukusudia muda mrefu uliopita kuwa ungetokea. Neno 'saa' laweza kutumika pia kumaanisha 'kitambo' au 'wakati huo' Kifungu kinapozungumzia " saa kuchelwa" in maana kwamba ' ilichelewa katika siku wakati juu lingelikuwa linazama upesi'

Mapendekezo ya tafsiri Neno 'saa' linapotumika kimfano laweza kuwa na maana ya 'muda' kitambo' au 'wakati ulioteuliwa.' Virai kama "katika saa ile" au ''saa ile ile'' vyaweza kutafsiriwa kama "kitambo kile'' au ''muda ule'' au mara'' au '' ghafla'' au ''hapo hapo'' Maelezo kuwa '' saa ilichelewa'' yana maana ya '' ilichelewa katika siku''

Sadaka

Ufafanuzi

"Sadaka" yaweza kuwa ppesa, chakula au chochote ambacho masikini anaweza kupewa kama msaada.

- Mara nyingi kutoa sadaka ilionekana kuwa jambo ambalo dini zao ziliwataka wafanye hivyo ili kuwa na haki.
- Yesu alisema kutoa sadaka hakupaswi kuwa wazi wazi ili watu wengine wakuone.
- Neno hili laweza kuafsiriwa kama "pesa" au "zawadi kwa masikini" au "kuwasaidia masikini."

Sadaka ya amani.

Ufafanuzi

Sadaka ya amani ilikuwa moja ya sadaka ambayo Mungu aliwaamuru Waisraeli watoe. Mara nyingine iliitwa sadaka ya shukrani au sadaka ya ushirika.

- Sadaka hii inajumuisha kutoa mnyama asiye na kasoro na kuinyunyuzia damu ya myama katika madhabahi na kuteketeza mafuta ya mnyama pamoja na vipande vya mnyama vilivyobaki kwa kutenganisha.
- Katika sadaka hii iliambatana na mkate wenye chachu na usiotiwa chachu ambayo iliteketezwa juu ya sadaka.
- Kuhani na mtoa sadaka waliruhusiwa kula chakula kilichotolewa kama sadaka.
- Sadaka hii ilionesha ushirika wa Mungu na watu wake.

sadaka ya dhambi

Ufafanuzi

"sadaka ya dhambi" ilikuwa moja ya dhabihu ambazo Mungu aliamuru Waisraeli kutoa.

- Hii sadaka ilihusisha kumtoa dhabihu ng'ombe dume, kuchoma damu yake na mafuta kwenye madhabahu, na kuchukuwa mwili wa huyo mnyama na kuuchoma kwenye ardhi nje ya kambi ya Waisraeli.
- Uchomwaji mzima wa huyu mnyama unaonyesha jinsi Mungu alivyo mtakatifu na jinsi dhambi ilivyo mbaya.
- Biblia inafundisha ilikuweze kuwa na utakaso wa dhambi, damu alazima imwagwe kulipa gharama ya dhambi iliyo tendwa.
- Dhabihu za wanyama hazikuweza kuleta daima msamaha wa dhambi.

sadaka ya hatia

Ufafanuzi

Sadaka ya hatia ilikuwa sadaka ambayo Mungu alihitaji kwa Waisraeli kufanya kama walifanya jambo kwa bahati mbaya kibaya kama vile kutomheshimu Mungu au kuharibu mali ya mtu mwingine.

Sadaka hii ilihusisha kutoa mnyama na kulipa faini, kwa pesa ya fedha au dhahabu.

Kwa kuongeza, mtu mwenye kosa alikuwa na wajibu wa kulipa kwa uharibifu wowote ambao ulifanyika.

sadaka ya kinywaji

Ufafanuzi

Sadaka ya kinywaji kilikuwa sadaka kwa Mungu amabyo ilihusisha kumwaga divai juu ya madhabahu. Mara kwa mara ilitolewa pamoja na sadaka ya kuteketeza na sadaka ya mazao.

Paulo anamaanisha maisha yake kama kumwagwa nje kama sadaka cha kinywaji. Hii ina maana ya kwamba aliwekwa wakfu kabisa kumtumikia Mungu na kuwaambia watu juu ya Yesu, hata kama alijua angeteseka na labda kuuwawa kwa sababu ya hiyo.

Kifo cha Yesu juu ya msalaba kilikuwa sadaka ya kinywaji ya mwisho, na damu yake ilimwagwa juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia nyingine ya kutafsiri msemo huu unaweza kuwa, "saaka ya divai ya mizabibu".

Paulo anaposema anakuwa "anamwagwa kama sadaka" hii inaweza kutafsiriwa kama, "nimejikabidhi kufundisha ujumbe wa Mungu kwa watu, kama sadaka ya divai inavyomwagwa kabisa juu ya madhabahu".

sadaka ya kujitolea

Ufafanuzi

Sadaka ya kujitolea ilikuwa aina ya sadaka kwa Mungu ambayo haikuhitajika kwa Sheria ya Musa. Ilikuwa ni uchaguzi binafsi wa mtu kutoa sadaka hii.

Kama sadaka ya kujitolea ilikuwa mnyama wa kutolewa sadaka, mnyama aliruhusiwa kuwa na kasoro chache kwa kuwa ilikuwa sadaka ya kujitolea.

Waisraeli walikula wanyama waliotolewa sadaka kama sehemu ya sherehe ya karamu.

Pale ambapo sadaka ya kujitolea inaweza kutolewa, hii ilikuwa sababu ya kufurahia kwa Israeli kwa kuwa ilionyesha ya kwamba mavuno yalikuwa mazuri ili kwamba watu wawe na chakula kingi.

Kitabu cha Ezra kinaelezea aina tofauti ya sadaka ya kujitolea ambayo ililetwa kwa kujenga tena hekalu. Sadaka hii ilijumuisha pesa ya dhahabu na fedha, pamoja na mabakuri na vyombo vingine vilivyoundwa kwa dhahabu na fedha.

Sadaka ya kuteketezwa

Ufafanuzi

"Sadaka ya kuteketezwa" ilikuwa ni aina ya sadaka iliyotolewa kwa Mungu kwa njia ya moto juu ya madhabahu. Ilitolewa ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu. Hii pia ilikuwa ikiitwa "toleo kwa njia ya moto."

- Wanyama waliotolewa kwa njia hii kwa kawaida walikuwa kondoo na mbuzi, lakini ng'ombe na ndege pia walikuwa wakitolewa.
- Nyama yote ya mnyama iliteketezwa kwa njia hii, isipokuwa ngozi. Ngozi alipewa kuhani.
- Mungu aliwaagiza Wayahudi kutoa sadaka ya kuteketezwa mara mbili kwa siku.

sadaka ya mlo

Ufafanuzi

"Sadaka ya mlo" ilikuwa dhabihu ya Mungu katika umbo la nafaka au mkate uliyo tengenezwa kwa unga.

- Neno "mlo" la husu nafaka iliyo sagwa kuwa unga
- Unga ulichanganywa na maji au mafuta kufanya mkate. Wakati mwingine mafuta yalisabazwa juu ya mkate.
- Aina hii ya sadaka kawaida iliwekwa pamoja na sadaka ya kuteketeza

sadaka ya nafaka

Ufafanuzi

Sadaka ya nafaka ilikuwa zawadi ya unga wa ngano au shayiri iliyotolewa kwa Mungu, mara nyingi baada ya sadaka ya kuteketeza.

Nafaka iliyotumika kwa ajili ya sadaka ya nafaka ilitakiwa kuwa safi kutoka ardhini. Mara nyingi ilipikwa kabla ya kutolewa, lakini muda mwingine iliachwa bila kupikwa.

Mafuta na chumvi yaliongezwa kwa unga wa nafaka, lakini hamira au asali haikuruhusiwa.

Sehemu ya sadaka ya nafaka ilichomwa na sehemu yake kuliwa na makuhani.

sadaka ya ushirika

Ufafanuzi

Katika Agano la Kale, "sadaka ya ushirika" ilikuwa aina ya sadaka ambayo ilitolewa kwa sababu tofauti, kama vile kutoa shukrani kwa Mungu na kutimiza kiapo.

Sadaka hii ilihitaji sadaka ya mnyama, ambaye alikuwa wa kiume au kike. Hii ilikuwa tofauti na sadaka ya kuteketeza ambayo ilihitaji mnyama wa jinsia ya kiume.

Baada ya kutoa sehemu ya sadaka kwa Mungu, mtu aliyeleta sadaka ya ushirika aligawana nyama na makuhani na Waisraeli wengine.

Kulikuwa na mlo unaohusishwa na sadaka hii ambayo hujumuisha mkate usiotiwa chachu.

Hii mara zingine unaitwa "sadaka ya amani"

salfa

Ufafanuzi

Salfa ni kitu chenye rangi ya njano kinacho kuwa kimiminiko kinacho waka moto kinapo chomwa.

- Salfa ina harufu kali kama mayai viza.
- Katika Biblia, salfa ilikuwa yachomwa ni hishara ya hukumu ya Mungu watu wa hasi.
- Wakati wa Lutu, Mungu alinyesha moto na salfa kwenye miji miovu ya Sodoma na Gomora.

sanamu, waabudu sanamu

Ufafanuzi

Sanamu ni kitu ambacho watu hutengeza ili waiabudu. Kitu kinaitwa "kuabudu sanamu" kama kinahusisha kutoa heshima kwa kitu tofauti na Mungu wa kweli.

Watu hutengeneza sanamu kuwakilisha miungu ya uongo wanayo abudu. Miungu hii ya uongo haiko hai; hakuna Mungu tofauti na Yahwe. Wakati mwingine mapepo hufanya kazi kupitia sanamu kuifanya ionekane kama vile ina nguvu, licha ya kuwa haina. Sanamu kawaida huundwa kwa vitu vya dhamani kama dhahabu, fedha, shaba, au mbao ya dhamani. "Ufalme unaoabudu sanamu" inamaanisha "ufalme wa watu wanaoabudu sanamu" au "ufalme wa watu wanaoabudu vitu vya duniani." Neno "umbo la waabudu sanamu" ni neno lingine kwa ajili ya "sanamu ya kuchonga" au "sanamu."

Sauti

Ufafanuzi

Sauti hutumika kumaanisha kuongea au kuwasiliana kitu au jambo.

- Mungu hutumia sauti yake japokuwa hana sauti kama ya mwanadamu.
- Neno hili laweza kutumika kumaanisha mtu, kwa mfano kwenye sentensi "sauti ilisikika jangwani ikisema, tengenezeni njia ya Bwana." Hii inaweza kutafsiriwa kuwa "Mtu alisikika akisema huko jangwani...."
- "Kusikia sauti ya mtu" inaweza kutafsiriwa kama "kusikia mtu akizungumza."
- Wakati mwingine "sauti" inaweza kutumika kwa vitu ambavyo haviwezi kuzungumza. Mfano mfalme Dauti katika zaburi anasema "Sauti" ya mbinguni inatangaza matendo makuu ya Mungu. Hii inaweza kutafsiriwa kama "mapambo yao yanaonesha wazi ukuu wa Mungu ulivyo."

Sehemu za juu

Ufafanuzi

Maneno 'sehemu za juu' yanarejelea madhabahu na maeneo matakatifu yaliyokuwa yakitumika katika kuabudu miungu. Mara zote maeneo haya yalikuwa sehemu za juu kama vile milimani au sehemu za vilima. Wafalme wengi wa Israeli walitenda dhambi kinyume na Mungu kwa kujenga madhabahu kwa ajili ya miungu katika sehemu hizi za juu. Hii iliwafanya watu kujishughulisha kwa undani katika ibada ya miungu. Wakati mfalme aliyemcha Mungu, alipoanza kutawala juu ya Yuda au Israeli, mara kwa mara waliweza kuonda sehemu hizi za juu na madhabahu ili kuzuia ibada za hizi miungu. Hata hivyo, baadhi ya wafalme wazuri hawakuwa makini sana na hawakuziondoa sehemu hizi za juu, na matokeo yake taifa lote la Israeli liliendelea kuabudu miungu.

Mapendekezo ya tafsiri Namna nyingine ya kutafsiri maneno haya twaweza kusema, " maeneo/sehemu iliyoinuliwa kwa ajili ya ibada ya miungu' au 'kilele cha mlima cha ibada ya miungu.' Hakikisha kuwa maneno unayoyatumia yawe na maana ya madhabahu ya miungu na siyo tu maeneo ya juu zilipo madhabahu hizo.

sela

Ufafanuzi

Neno "sela" ni la Kiebrania lililopo sana katika kitabu cha Zaburi. Lina maana kadhaa.

- Lina weza maanisha "kituo na sifa," litakalo wakaribisha wasomaji kufikiria kwa makini kuhusu kile kilicho zungumzwa.
- Kwasababu Zaburi nyingi ziliandikwa kama nyimbo, ina fahamika kwamba "sela" yaweza kuwa neno la kimziki kuelekeza muimbaji kueka kituo katika uimbaji wake kuruhusu vyombo vya mziki kucheza au kufariji wasikilizaji kufikiria kuhusu maneno ya nyimbo.

sensa

Ufafanuzi

Neno "sensa" lilitumika kuhesabu kawaida hesabu ya watu katika taifa au ufalme.

- Agano la Kale limetunza idadi kwa mda tofauti tofauti wakati Mungu alipowaagiza kwamba wanaume wa Israeli wahesabiwe, kama vile wakati walipoondoka Misri kwa mara ya kwanza na baadaye tena kabla ya kuingia Kanaani.
- Mara nyingi lengo la sensa lilikuwa kwa ajili kujua ni watu wangapi watatakiwa kulipa kodi.
- Kwa mfano, mara moja katika Kutoka wanaume wa Waisraeli walihesabiwa ili kwamba kila mmoja angeweza kulipa nusu shekeli kwa ajili ya kutunza hekalu.
- Wakati Yesu alipokuwa mtoto, serikali ya Rumi ilifanya sensa kuwahesabu watu wote walioishi katika ufalme wao, kuwataka walipe ushuru.

shaba

Ufafanuzi

Neno "shaba" linamaanisha aina ya madini yatengenezwayo kwa kuyeyusha kwa pamoja metali, shaba nyekundu na bati. Ina rangi nyeusi inayoelekea njano, nyekundu kiasi.

- Shaba huzuia kutu na kipitisho kizuri cha joto
- Hapo kale, shaba ilitumika kutengeneza dhana, silaha, madhabahu, vyungu, silaha za askari na vitu vingine.
- Vifaa vingi vya kujengea hema la kukutania na hekalu vilikuwa vimetengenezwa kwa shaba.
- Kwa kawaida vinyago vya miungu ya uongo vilitengenezwa kwa madini ya shaba.
- Dhana za shaba zilitengenezwa baada ya kuyeyusha madini ya shaba na kisha kuyamimina katika chombo cha kutengenezea. Mchakato huu uliitwa "kutupa."

shahidi wa uongo, shahidi aliyepotoka, ushuhuda wa uongo, taarifa ya uongo

Ufafanuzi

Misemo ya "shahidi wa uongo" na "shahidi aliyepotoka" ina maana ya mtu anayesema vitu vya uongo juu ya mtu au tukio, mara kwa mara katika mahala rasmi kama mahakamani.

"Ushuhuda wa uongo" au "taarifa ya uongo" ni uongo halisia ambao unaambiwa.

"kutoa ushahidi wa uongo" ina maana ya kudanganya au kutoa taarifa ya uongo kuhusu jambo.

Biblia hutoa habari kadhaa ambapo mashahidi wa uongo waliajiriwa kudanganya kuhusu mtu ili kumfanya mtu huyo kuadhibiwa au kuuwawa.

Mapendekezo ya Tafsiri

"Kuwa shahidi wa uongo" au "kutoa ushahidi wa uongo" unaweza kutafsiriwa kama "kushuhudia uongo" au "kutoa taarifa ya uongo juu ya mtu" au "kuzungumza uongo dhidi ya mtu" au "uongo".

Pale ambapo "shahidi wa uongo" ina maana ya mtu, inaweza kutafsiriwa kama "mtu anayedanganya" au "mtu anayeshuhudia uongo" au "mtu anayesema mambo ambayo siyo ya kweli".

shahidi, Shahidi

Ufafanuzi

Shahidi ni mtu ambaye amepata uzoefu binafsi wa kitu kilichotokea. Maranyingi shahidi ni mtu anayetoa ushahidi wa jambo analijua kuwa ni kweli. Shahidi pia aneweza kuwa mtu aliyekuwepo pale na kuona kilichotokea.

- Kushuhudia kitu ni kuona kikitokea.
- Katika kesi shahidi hutoa ushahidi.
- Shahidi anatazamiwa kusema ukweli wa kile kilichotokea na sio uongo.
- Shahidi atakayesema uongo juu ya kilichotokea ushahidi wake unaitwa "ushahidi wauongo."

shayiri

Ufafanuzi

Neno "shayiri" limamaanisha aina ya nafaka iliyokuwa ikitumika kutengeneza mkate.

- Mche wa shayiri una bua refu lenye suke juu yake ambamo ndani yake punje au nafaka inakua.
- Shayiri hustawi wakati wa joto hivyo kwa kawaida inavunwa wakati wa kiangazi.
- Wakati shayiri inapopurwa, mbegu ya kuliwa inatenganishwa na makapi.
- Nafaka ya shayiri inasagwa na kuwa unga, ambao hatimaye unachanganywa na maji na mafuta ili kutengeneza mkate.

sheria, kanuni

Ufafanuzi

"Sheria" ni amri ambayo kawaida huandikwa chini na kushurutishwa na mtu aliye madarakani. "Kanuni" ni uongozo kwa ajili ya kufanya maamuzi na tabia.

Zote "sheria" na "kanuni" zinaweza kumaanisha amri au imani inayoongoza tabia ya mtu. Maana hii ya "sheria" ni tofauti kwa maana ya kutoka "sheria ya Musa" ambapo inamaanisha amri na maelekezo ambayo Mungu aliwapa Waisraeli. Wakati sheria ya ujumla inapotajwa,"sheria" inaweza kutafsiriwa kama "kanuni" au "amri ya jumla."

Shimo

Ufafanuzi

Shimo ni sehemu yenye kina kwenda chini iliyochimbwa kwenye ardhi.

- Watu hichimba shimo kwa lengo la kuweka mtego wa wanyama au kutafuta maji.
- Shimo pia linaweza kutumika kama sehemu ya muda ya kumuweka mfungwa.
- Mara nyingine shimo linazungumzwa kama jehanamu.
- Neno shimo pia hutumika kama lugha ya pivha kuonesha "shimo la uharibifu" ambayo huelezea kutekwa katika hali mbaya au kujiingiza katika dhambi na matendo ya uharibifu.

Shimo lisilo na mwisho

Ufafanuzi

"Shimo lisilo na mwisho" ni shimo kubwa, lenye kina kirefu au pengo lisilo na mwisho.

- Kwenye Bilblia "shimo lisilo na mwisho" ni sehemu ya adhabu.
- Kwa mfano, Yesu alipokuwa anawaamuru pepo wachafu wamtoke yule mtu, walimuomba asiwapeleke kwenye shimo lisilo na mwisho.
- Pia "shimo lisilo na mwisho" linaweza kutafsiriwa kama "kuzimu"

shingo ngumu, kiburi

Ufafanuzi

Neno "shingo ngumu" ni msemo katika Biblia unao tumika kueleza watu wasio mtii Mungu na wanao kataa kutubu. Wana kiburi na hawata tii mamlaka ya Mungu.

- Sambamba, neno "kiburi" umaanisha kukataa kubadili nia au matendo ata unapo shawishiwa kufanya hivyo. Watu wenye kiburi hawata sikiliza ushauri mzuri au maonyo watu wengine wanao wapa.
- Agano la Kale liliwaeleza Waisraeli kama wenye "shingo ngumu" kwasababu hawakusikiliza jumbe nyingi kutoka kwa manabii wa Mungu waliyo wasii watubu na kumgeukia Yahweh.
- Kama shingo ni "ngumu" ina maana haipindi kirahisi.

Shinikizo la divai

Ufafanuzi

Katika nyakati za Biblia shinikizo la divai ni vyombo vikubwa au sehemu ya wazi ambapo maji ya zabibu yalitengenezwa na kufanywa kuwa divai.

- Katika Israeli shinikizo la divai lilikuwa beseni kubwa lililochimbwa kwenye mwamba. Na watu walikanyaga zabibu kwa miguu yao ili wapate maji ya zabibu.
- Shinikizo la divai lilikuwa na hatua mbili, zabizu zilizokanyagwa kwenye hatua ya juu ili maji ya zabibu yatiririke chini kwenye hatua ya chini ambapo hukusanywa.
- Pia shinikizo la divai limetumika kuonesha picha ya hasira ya Mungu atakayoimimina juu ya watu waovu.

Shoka

Ufafanuzi

Shoka ni kifaa kinachotumika kukatia miti au mbao.

- Mara nyingi shoka huwa na mpini wa mbao.
- Kama kwenye jamii yako kuna kifaa kinafanana na shoka ni vizuri kutumia jina la kifaa hicho kutafsiri "shoka."
- Namna nyingine ya kutafsiri neno hili ni "kifaa cha kukatia mti au mbao."

Shtaki, Mashtaka, Mshtaki

Ufafanuzi

Neno "shtaki au Mashtaka" linamaanisha kumlaumu mtu kwa kufanya jambo baya. Mtu anayeshitaki wengine anaitwa "mshtaki."

- Mashtaka ya uongo ni pale ambapo makosa dhidi ya mtu fulani si ya kweli, ni kama vile Yesu alipopewa mashtaka ya uongo na viongozi wa Kiyahudi.
- Katika agano jipya kwenye kitabu cha Ufunuo, shetani anaitwa "mshtaki."

shtakio

Ufafanuzi

Neno "shtakiwa" la eleza hali ambayo mtu au kitu kina "jaribiwa."

- Shtakio lina weza kuwa mahakamani ambapo ushahidi unatolewa kuthibitisha kama mtu hana hatia au ana kosa.
- Neno "shtakio" lina weza maanisha hali ngumu mtu anayo pitia Mungu anapo jaribu imani zao. Maneno mengine ni "jaribu."
- Watu wengi katika Biblia walijaribiwa kuona kama wataendelea kumuamini Mungu na kumtii. Walipitia mashtaka yaliyo husisha kupigwa, kufungwa, au kuuawa kwasababu ya imani yao.

Shujaa, askari

Ufafanuzi

Shujaa na askari ni mtu anayepigana kwenye jeshi. Lakini pia kuna tofauti kadhaa.

- Shujaa maranyingi ni neno la jumla kumaanisha mtu aliyebarikiwa na mwenye ujasiri vitani.
- Yaweh anazungumzwa kama shujaa.
- Askari ni mtu ambaye anatoka kwenye jeshi fulani au anayepigana katika vita fulani.
- Askari wa Kirumi huko Yerusalemu walikuwa wakifuata amri na kufanya majukumu yao kama vile kuwalinda wafungwa. Walimlinda Yesu kabla ya kumsulubisha na wengine waliambiwa walilinde kaburi lake.

si mcha Mungu, siye na Mungu

Ufafanuzi

Meneno "si mcha Mungu" na "siye na Mungu" ina eleza watu waliyo hasi dhidi ya Mungu. Kuishi kwa uovu, pasipo na wazo la Mungu uitwa "siye mcha Mungu" au "pasipo na Mungu."

- Maana ya haya maneno yana fanana. Walakini, "siye na Mungu" na "pasipo na Mungu" ya weza eleza hali ambayo watu au mataifa hawamtambui Mungu au utawala wake kwao.
- Mungu anatangaza hukumu na ghadhabu watu hasi, kwa wote waliyo mkataa na njia zake.

si takatifu

Ufafanuzi

Neno "si takatifu" lina maana "kuto kuwa takatifu." Inaelezea mtu au kitu kisicho mtii Mungu.

- Hili neno linatumika kueleza mtu asiye muheshimu Mungu kwa kuhasi dhidi yake.
- Kitu kinacho itwa "si takatifu" kinaweza elezwa kama kuwa kawaida, upunjufu, chafu. Sio cha Mungu.

si wa haki,

Ufafanuzi

Neno "si wa haki" ina maana ya wenye dhambi asiye na maadili.

- Haya maneno yana maana ya kuishi kwa namna inayo kosea mfundisho ya Mungu na amri.
- Watu ambao si wa haki hawana maadili katika fikra zao na matendo.
- Wakati mwingine "asiye wa haki" ueleza watu wasiyo mwamini Yesu.

sifa, mashuhuri

Ufafanuzi

Sifa ni kitendo cha kujulikana na kuwa na sifa.

- Mtu mashuhuri ni mtu anayejulikana na anayenyenyekewa.
- "Sifa" mara nyngi huwa nzuri na inayojulikana kwa mda mrefu.
- Mji wenye sifa mara nyingi hujulikana kwa utajiri wake na mali.

siku

Ufafanuzi

Neno "siku" kwa kawaida lamaanisha kipindi cha masaa 24 kuanzia kuzama kwa jua. Linatumika pia kitamathari.

- Kwa Waisraeli na Wayahudi, siku ilianza wakati wa jua kuzama na kuishia wakati wa kuzama kwa jua siku iliyofuata.
- Wakati mwingine neno "siku" latumika kitamathari kurejerea wakati mrefu, kama vile "siku ya Yahwe" au "siku za mwisho."
- Baadhi ya lugha hutumia taarifa nyingine kutafasiri matumizi ya tamathari hili au zitatafasiri "siku" bila tamathari.
- Tafasiri nyingine za "siku" zaweza kuhusisha, "wakati" au "majira" au "tukio" kutegemea na mazingira.

sikukuu

Ufafanuzi

Kwa ujumla, sikukuu ni sherehe iliyofanyika na jamii ya watu.

Neno kwa ajili ya "sikukuu" katika Agano la Kale lina maana ya "muda ulioteuliwa".

Sikukuu zinazosherehekewa na Waisraeli zilikuwa nyakati maalumu zilizoteuliwa au nyakati ambazo Mungu aliwaamuru wao kuzifuata.

Katika baadhi ya tafasiri za Kiingereza, neno "sikukuu" linatumika badala ya karamu kwa sababu sherehe zilijumuisha mlo mkubwa wa pamoja.

Kulikuwa na karamu kadhaa ambazo Waisraeli walisherehekea kila mwaka: Pasaka Sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu Mavuno ya Kwanza Sikukuu ya Wiki (Pentakuki) Sikukuu ya Tarumbeta Sikukuu ya Kulipia Kosa Sikukuu ya Vibanda Kusudi la sikukuu hizi ilikuwa kumshukuru Mungu na kukumbuka mambo ya ajabu aliyofanya kuwaokoa, kuwalinda na kuwapa watu wake.

Silaha

Ufafanuzi

Silaha ni kifaa anachokitumia askari kupigana akiwa vitani na kujilinda dhidi ya maadui. Pia inaweza kutumika kama lugha ya picha ikimaanisha silaha za kiroho.

- Baadhi ya silaha za askari ni kofia ya chuma, ngao, mguu, vifuniko vya miguu na upanga.
- Kama lugha ya picha Paulo anafananisha silaha za kimwili na silaha za kiroho ambazo Mungu anawapa wamwaminio ili waweze kupigana vita vya kiroho. -
- Silaha za kiroho ambazo Mungu amewapa watu wake ni ukweli, haki, injili ya amani, wokovu na roho mtakatifu.

simba

Ufafanuzi

Simba ni mnyama mkubwa wa porini anayefanana na paka, mwenye meno yenye nguvu na makucha ya kuulia na kurarua mawindo yake.

Simba wana miili yenye nguvu na kasi kubwa ya kushika mawindo yao. Manyoya yao ni mafupi na yana rangi ya mchanganyiko wa kahawa na dhahabu. Simba dume wana manyoya ya shingoni yanayozunguka vichwa vyao. Simba huua wanyama wengine ili kuwala na pia wanaweza kuwa hatari kwa binadamu. Mfalme Daudi alipokuwa mvulana, aliua simba waliojaribu kuvamia kondoo wake aliokuwa akiwachunga. Samsoni pia aliua simba kwa mikono yake.

sio aminifu, kosa uaminifu

Ufafanuzi

Neno "sio aminifu"la eleza watu wasio fanya kile Mungu alicho amuru wafanye. Hali au ktitendo cha kuwa sio aminifu ni "kuso uaminifu."

- Watu wa Israeli waliitwa "sio aminifu" walipo anza abudu sanamu na walipo kosa mtii Mungu kwa namna nyingine.
- Katika ndoa, mtu anafanya uasherati ni "sio aminifu" kwa mpenzi wake.
- Mungu alitumia neno "kosa aminifu" kueleza tabia hasi ya Israeli. Hawakumtii wala kumheshimu Mungu.

sio leta faida

Ufafanuzi

Neno "sio leta faida" ina maana ya kuto kuwa na manufaa.

- Ina maana ya kuto pata faida ya chochote au kuto msaidia mtu kupata kitu.
- Kitu ambacho sio leta faida hakina maana ya kufanya kwasasabu hakitoi manufaa.

siotahiriwa, kutotahiriwa

Ufafanuzi

Maneno "siotahiriwa" na "kutotahiriwa" ueleza mwanaume ambaye hajatahiriwa kimwili. Haya maneno utumika pia kifumbo.

- Misri lilikuwa taifa lililo taka tohara. Hivyo Mungu anapo ongelea Misri kushindwa na wale "siotahiriwa," anasema watu Wamisri wanao wadharau kwa kutotahiriwa.
- Biblia ina eleza watu wasio tahiriwa "mioyo siotahiriwa" au ambaye "hajatahiriwa moyoni." Hii ni njia ya fumbo ya kusema kuwa hawa watu sio wa Mungu, na hawa mtii.

siri, ukweli uliyo fichika

Ufafanuzi

Katika Biblia, neno "siri" la husu kitu kisicho julikana au kigumu kuelewa ambacho Mungu sasa anaelezea.

- Katika Agano Jipya linaeleza kuwa Kristo alikuwa siri ambayo haikujulikana awali.
- Katika ya vitu maalumu vinavyo julikana kama siri ni kwamba Wayahudi na Wamataifa watakuwa sawa ndani ya Kristo.

stuli ya mguu

Ufafanuzi

Msemo "stuli ya mguu" una maana ya chombo ambacho mtu huweka miguu yake kwa juu, mara nyingi kupumzisha anapokuwa ameketi. Msemo huu pia una maana za tamathali kwa kujishusha na hadhi ya chini.

Watu katika kipindi cha Biblia walichukulia miguu kuwa sehemu yenye heshima ya chini kabisa ya mwili. Kwa hiyo "stuli ya mguu" ilikuwa heshima ya chini zaidi kwa sababu miguu ilipumzishwa juu yake.

Mungu anaposema "Nitawafanya adui zangu stuli ya mguu kwa ajili ya miguu yangu" anatamka nguvu, utawala na ushindi juu ya watu ambao wanaasi dhidi yake. Watashushwa na kushindwa hadi hatua ya kujishusha kwa mapenzi ya Mungu.

"Kuabudu katika stuli ya mguu ya Mungu" ina maana ya kuinama chini katika kuabudu mbele yake anapokuwa amekaa juu ya kiti chake cha enzi. Hii tena inatoa unyenyekevu na kujishusha kwa Mungu.

Daudi anamaanisha hekalu kama "stuli ya mguu" ya Mungu. Hii inaweza kumaanisha mamlaka yake ya hakika juu ya watu wake. Hii inaweza pia kumpiga picha Mungu Mfalme juu ya kiti chake cha enzi, na miguu yake ikupumzika juu ya stuli ya mguu, ambayo inawakilisha kila kilcho chini yake.

Suria

Ufafanuzi

Suria ni mwanamke ambaye ni mke wa pili wa mwanaume ambaye tayari ana mke. Suria mara nyingi sio mke halali wa mwanaume huyo.

- Katika agano la kale masuria walikuwa wanawake watumwa.
- Suria anaweza kupatikana kwa kununuliwa, kwa kushinda vita au kwa njia ya kulipa deni.
- Kwa mfalme kuwa na masuria wengi ilikuwa alama ya mamlaka.
- Katika agano jipya inafundisha kuwa kuwa na masuria ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

taa

Ufafanuzi

Neno "taa" kawaida inamaanisha kitu kinachotoa mwanga. Taa zilizotumika nyakati za Biblia kawaida zilikuwa taa za mafuta. Aina ya taa iliyotumika katika Biblia ni chombo na sehemu ya kuwekea mafuta, yanayotoa mwanga inapowashwa.

Kawaida taa za mafuta zilitengenezwa kwa chombo cha kawaida cha udongo kilichojaa mafuta ya mzeituni, na utambi ukiwekwa kwenye mafuta ili uwake. Kwa baadhi ya taa, chombo lilikuwa na umbo la yai, na sehemu moja ikiwa imefinywa karibu kuushikilia utambi. Taa ya mafuta iliweza kubebwa au kuwekwa katika kinara ili mwanga wake ujaze chumba au nyumba. Katika maandiko, taa zinatumika kwa njia kadhaa kimithali kama ishara ya mwanaga na uhai.

taabu, mataabiko, taabika

Ufafanuzi

Neno "taabu" ina eleza hali ya maisha ambayo ni ngumu na kusumbua. "Kutaabika" ina maanisha kusikia vibaya au kusongwa na mawazo ya jambo.

- Taabu zina weka kuwa kimwili, kihisia, au vitu vya kiroho vinavyo muumiza mtu.
- Katika Biblia, mara nyingi taabu ni kipindi cha majaribu Mungu anayo tumia kusaidia waamini kukua na kukomaa kiimani.
- Agano la Kale lina tumia "taabu" kama hukumu iliyo kuja kwa makundi ya watu waliyo kuwa waasi na wamemkataa Mungu.
- Tendo "kutaabisha" mtu lina maana ya "kusumbua" mtu au kusababisha mawazo.

tafakari

Ufafanuzi

Neno "tafakari" lina maana ya kutumia muda kufiria jambo kwa umakini na undani.

- Hili neno mara nyingi lina tumika kwenye Biblia kuhusu kuwaza Mungu na mafundisho.
- Zaburi 1 inasema mtu anaye tafakari sheria ya Bwana "usiku na mchana" atabarikiwa sana.

tafsiri, ufafanuzi

Ufafanuzi

Neno "tafsiri" na "ufafanuzi" inamaanisha kuelewa na kufafanua maana ya jambo ambalo haloki wazi.

Mara nyingi Biblia inatumia misemo hii katika kueleza maana za ndoto na maono. Wakati mfalme wa Babeli alipopata ndoto za kuchanganya, Mungu alimsaidia Danieli kuzitafsiri na kufafanua maana zake. "Tafsiri" ya ndoto ni "ufafanuzi" wa maana ya ndoto. Katika Agano la Kale, wakati mwingine Mungu hutumia ndoto kuwafunulia watu kitakachotokea siku za usoni. Kwa hiyo ufafanuzi wa hizo ndoto zilikuwa ni utabiri. Neno "tafsiri" inaweza pia kumaanisha kuelewa maana ya vitu vingine, kama kuelewa hali ya hewa itakuaje kutokana na ubaridi au joto lililopo, upepo uliopo, na anga ilivyo. Njia za kutafsiri neno "tafsiri" ni pamoja na , "kuelewa maana ya" au "kufafanua" au "kutoa maana ya." Usemi "tafsiri" inaweza kutafsiriwa kama "maelezo" au "maana."

tafuta

Ufafanuzi

Neno "tafuta" la maanisha kutafuta kitu au mtu. Inaweza kuwa na maana ya "jaribu kwa bidii" au "tia juhudi" kufanya kitu.

- "tafuta" au "kuangalia" fursa ina maana ya "kujaribu kutafuta muda" kufanya kitu muhimu
- "kumtafuta Yahweh" ina maana ya "kutumia muda na uweza kupata kumjua Yahweh na kujifunza kumtii."
- "kutafuta ulinzi" ina maana ya "kujaribu kumpata mtu au sehemu itakayo kulinda na hatari."
- "kutafuta haki" ina maana ya "kufanya juhudi kuona kwamba watu wana tendewa sawa."
- "kutafuta ukweli" ina maana ya "kufanya juhudi kujua nini ni ukweli."
- "kutafuta upendeleo" ina maana ya "kujaribu kupata upendeleo" au "kufanya vitu kumsababisha mtu akusaidie."

tai

Ufafanuzi

Tai ni ndege mbua mkubwa sana, mwenye nguvu ambaye hula wanyama wadogo kama vile samaki, panya, nyoka na kuku.

Biblia hulinganisha kasi na nguvu ya jeshi kwa jinsi tai hupaa chini kukamata nyama yake kwa kasi na ghafla.

Isaya anasema ya kwamba wale wanaomtumaini Bwana watapaa juu kama tai afanyavyo. Hii ni lugha ya tamathali inayotumika kuelezea uhuru na nguvu ambao unakuja kutokana na kumuamini na kumtii Mungu.

Katika kitabu cha Danieli, urefu wa nywele za Mfalme Nebukadreza zililinganishwa na urefu wa manyoya ya tai, ambayo yanaweza kuwa zaidi ya sentimita 50.

Taifa

Ufafanuzi

Taifa ni kundi kubwa la watu wanao tawaliwa na serikali. Watu wa taifa mara nyingi wa mababu sawa na ni wajamii moja.

- Neno "taifa" mara nyingi lina maana ya utamaduni ulifahamika vizuri na kuwa na mipaka ya eneo.
- Katika Biblia, "taifa" la weza kuwa nchi (kama Misri au Ethiopia) lakini wakatik mwingine ni kwa ujumla na uhusu kundi la watu, sana inapotumika katika wingi.
- Taifa katika Biblia ni Waisraeli, Wafilisti, Waasyria, Wababiloni, Wakanani, Warumi, Wayunani.
- Wakati mwingine neno "taifa" linatumika kifumbo kutaja mababu wa kundi la watu, kama Rebeka alivyo ambiwa na Mungu kuwa mtoto wake tumboni alikuwa ni "mataifa" watakao pigana wenywe.

Taji, kuvalisha taji

Ufafanuzi

Taji ni pambo la mviringo linalovaliwa kichwani kwa kiongozi wa juu kama mfalme na malkia. Kuvika taji ni kuweka taji juu ya kichwa cha mtu. Au yaweza kuwa na maana ya "kuheshimu."

- Mataji hutengenezwa kwa dhahabu au fedha pia hupambwa kwa zumaridi au rubi.
- Taji ni alama ya nguvu na utajiri wa mfalme.
- Taji lililotengenezwa kwa miba ambalo askari wa Rumi walimvalisha Yesu kichwani lilikuwa kwa ajili ya kumdhihaki.
- Zamani za kale mshindi wa mashindano ya riadha alizawadiwa taji iliyotengenezwa kwa majani ya mzeituni. Mtume Paulo aliitaja taji hii katika barua yake ya pili kwa Timotheo.
- Kuvisha taji pia inaweza kuwa na maana ya kumuheshimu mtu. Tunamuheshimu Mungu kwa kumtii yeye na kumsifu yeye. Hii ni kama kuweka taji kichwa ni mwake na kumtambua kama mfalme.
- Taji pia inaweza kuwa na maana ya "zawadi" au "heshima" au "ujira."

takatifu

Ufafanuzi

Neno "takatifu" la elezea kitu kinacho husu kumuabudu Mungu au wapagani wanao abudu miungu ya uongo.

- Katika Agano la Kale, mara nyingi neno "takatifu" la tumika kueleza nguzo za mawe na vitu vingine vinavyo tumika katika kuabudu miungu ya uongo. Hii yaweza tafsiriwa kama kama "kidini"
- "nyimbo Takatifu" au "miziki takatifu" ya husu mziki unao imbwa au kuchezwa kwa utukufu wa Mungu. Hii yaweza tafsiriwa kama "mziki wa kumuabudu Yaheweh" au "nyimbo zinazo muabudu Yahweh."
- Msemo "majukumu takatifu" ya husu "majukumu ya kidini" au "mila" ambazo kuhani ana tenda kuongoza watu katika kumuabudu Mungu. Yaweza pia husu mila zinazo tendwa na kuhani mpagani kumuabudu mungu wa uongo.

takdiri, majaliwa, jaliwa

Ufafanuzi

Msemo wa "takdiri" una maana ya kile kitakachotokea kwa watu hapo baadaye. Kama mtu ana "takdiri" ya jambo, ina maana ya kwamba kile mtu huyo atafanya hapo baadaye kimepangwa na Mungu.

Mungu anapopanga taifa kupatwa na ghadhabu, hii ina maana ya kwamba ameamua au kuchagua kuwaadhibu taifa hilo kwa sababu ya dhambi yao.

Yuda alikuwa na "takdiri" ya kuangamizwa, ina maana ya kwamba Mungu aliamua ya kwamba Yuda angeangamizwa kwa sababu ya kuasi kwake.

Kila mtu ana takdiri ya mwisho, ya milele, moja wapo mbinguni au jehanamu.

Pale mwandishi wa Mhubiri anaposema ya kwamba kila mtu takdiri yake inafanana, anamaanisha ya kwamba kila mtu hatma yake atakufa.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "kupangwa kwa ghadhabu" unaweza pia kutafsiriwa kama "kuamua ya kwamba utaadhibiwa" au "kuamuliwa ya kwamba utapitia ghadhabu yangu".

Msemo wa kitamathali, "wana takdiri ya upanga" inaweza kutafsiriwa kama, "Mungu ameamua ya kwamba wataangamizwa na adui zake ambao watawaua kwa upanga" au "Mungu ameamua ya kwamba adui wao watawaua kwa upanga".

Msemo, "una takdiri ya" inaweza kutafsiriwa kutumia msemo kama, "Mungu ameamua ya kwamba utakuwa"

Kutegemea na muktadha, "takdiri" inaweza kutafsiriwa kama "hitimisho la mwisho" au "kitakachotokea mwishoni" au "kile alichoamua Mungu kitatokea"

Talaka

Ufafanuzi

Talaka ni tendo la kisheria la kusitisha ndoa. Msemo "kutengana" ina maana ya kutengana rasmi na kihalali kutoka kwa mwenzi wa mtu ili kusitisha ndoa.

Maana halisi ya neno "kutengana" ni "kufukuza" au "kuachana rasmi kutoka kwa". Lugha zingine zinaweza kuwa na misemo ya kufanana yenye maana ya talaka.

"cheti cha talaka" kinaweza kutafsiriwa kama, "karatasi inayosema ya kwamba ndoa imefika mwisho".

tamaa

Ufafanuzi

Tamaa ni hamu kubwa sana, mara nyingi katika mazingira ya kutaka kitu kiouvu au kisicho na maadili mema.

Katika Biblia, "tamaa" mara nyingi inamaanisha hamu ya kimwili kwa mtu mwingine tofauti na mme au mke wake. Wakati mwingine neno hili linatumika kimafumbo kumaanisha kuabudu sanamu. Kulingana na mazingira, "tamaa" inaweza kutafsiriwa kama "hamu mbaya" au "hamu kali" au "hamu mbaya ya kimwili" au "hamu kubwa isiyo ya kimaadili mema" au "kuwa na hamu kubwa ya kutenda dhambi." Msemo "kutamani kitu" inaweza pia kutafsiriwa kama "kuwa na hamu vibaya" au " kuwaza kinyume na maadili kuhusu" au "kuwa na hamu mbaya kimaadili."

Tambua

Ufafanuzi

Neno "tambua" lina maana ya kutambua kwa usahihi kitu fulani au mtu.

- Kumtambua Mungu pia inajumuisha kutenda kwa namna ambayo itaonesha kuwa anayoyasema ni kweli.
- Watu wanaomtambua Mungu huonesha kwa kumtii Mungu ambayo huleta utukufu kwa jina lake.
- Kutambua kitu ina maana ya kuamini kuwa ni kweli, kwa maneno na matendo yanayothibitisha hayo.

tambua, tambuzi

Ufafanuzi

Msemo "tambua" una maana ya kuweza kuelewa jambo, haswa kuweza kujua kama jambo ni sahihi au baya.

Msemo wa "tambuzi" una maana ya kuelewa na kuamua kwa hekima kuhusu jambo fulani.

Ina maana kuwa na hekima na maamuzi mazuri.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "tambua" inaweza pia kutafsiriwa kama "kuelewa" au "kujua tofauti kati ya" au "kutofautisha mema na mabaya" au "kuhukumu sahihi kuhusu" au "kuelewa mema kwa mabaya".

"Tambuzi" inaweza kutafsiriwa kama, "uelewa" au "uwezo wa kuchambua mema na mabaya"

tamka, tamko

Ufafanuzi

Msemo wa "tamka" au "tamko" una maana ya kutoa kauli maalumu kwa umma, mara nyingi kusisitiza jambo.

"Tamko" halisisitizi umuhimu tu wa kile kinachotamkwa, lakini inavuta nadhari kwa yule anayetoa tamko hilo.

Kwa mfano, katika Agano la Kale, ujumbe kutoka kwa Mungu mara nyingi hutanguliwa na "tamko la Yahwe" au "hivi ndivyo Yahwe asemavyo". Msemo huu unasisitiza ya kwamba ni Yahwe mwenyewe anayesema hivi. Ukweli ya kwamba ujumbe unatoka kwa Yahwe unaonyesha jinsi ujumbe ulivyo na umuhimu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "tamka" inaweza pia kutafsiriwa kama "tangaza" au "eneza wazi" au "sema kwa nguvu" au "tamka kwa kishindo".

Msemo "tamko" unaweza kutafsiriwa kama, "kauli" au "tangazo".

Msemo, "hili ni tamko la Yahwe" linaweza kutafsiriwa kama, "hivi ndivyo Yahwe anavyotamka" au "hivi ndivyo Yahwe anavyosema".

tanuu

Ufafanuzi

Tanuu ilikuwa joko kubwa sana liyotumika kuchemsha vyombo katika halijoto la juu.

Katika kipindi cha nyuma, tanuu nyingi zilitumika kuyeyusha vyuma kutengeneza vyombo kama vile vyungu vya kupikia, mapambo ya vito, silaha, na sanamu.

Tanuu zilitumika pia kutengeneza vyungu vya udongo.

Mara nyingine tanuu hujulikana kitamathali kufafanua ya kwamba kitu ni cha moto sana.

Tapanya, nyika

Ufafanuzi

Kutapanya kitu ni kukitupa au kutokukitumia kwa hekima. Nchi ambayo ni nyika ni nchi au mji ulioharibiwa ili kitu chochote kisiishi ndani yake tena.

- "Kuchakaa" inamaana ya kuwa na ugonjwa au kuharibiwa. Mtu aliyechakaa maranyingi anakuwa mwembamba kutokana na ugonjwa au kukosa chakula.
- Neno lingine linalomaanisha nyika nin jangwa. Lakini nyika pia inamaanisha kuwa watu waliishi hapo na nchi ilikuwa na miti na mimea inayotoa chakula.

tarumbeta

Ufafanuzi

Neno "tarumbeta" la eleza chombo cha kutoa mziki au kuita watu pamoka kwa mkutano au kikao.

- Tarumbeta lilitumika na chuma, kombe, au pembe la mnyama.
- Matarumbeta yalipigwa kuita watu kuja pamoja kwa pambano, na kukusanyika kwa Waisraeli.
- Kitabu cha Ufunuo kinaeleza tukio la mwisho wa nyakati ambapo malaika walipenga matarumbeta kuhashiria kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu duniani.

tawanya, mtawanyiko

Ufafanuzi

Msemo "tawanya" na "mtawanyiko" ina maana ya kutawanya watu au vitu katika pande nyingi tofauti.

Katika Agano la Kale, Mungu anazungumza kuhusu "kutawanya" watu, kusababisha wao wajitenge na kuishi katika maeneo tofauti kati yao. Alifanya hivi kuwaadhibu kwa dhambi yao. Huenda kutawanyika ingeweza kuwasaidia kutubu na kuanza kumwabudu Mungu tena.

Msemo "mtawanyiko" unatumika katika Agano Jipya kumaanisha Wakristo ambao walitakiwa kuacha nyumba zao na kuhamia katika mahali tofauti nyingi kutoroka mateso.

Msemo "tawanyiko" unaweza kutafsiriwa kama "waumini katika maeneo mengi tofauti" au "watu waliohama kuishi katika mataifa tofauti".

Msemo "tawanya" unaweza kutafsiriwa kama "kutuma mbali katika maeneo mengi tofauti" au "kusambaza ng'ambo" au "kusababisha kuhamisha mbali kuishi katika nchi tofauti"

teketeza, uharibifu

Ufafanuzi

Msemo wa "kuteketezwa" au "uharibifu" ina maana ya kufanya mali ya mtu au ardhi kuharibika au kuangamizwa. Pia mara kwa mara hujumuisha kuangamiza au kukamata watu waishio katika ardhi hiyo.

Hii ina maana ya maangamizi kamili na makali sana.

Kwa mfano, mji wa Sodoma uliteketezwa na Mungu kama adhabu kwa dhambi za watu walioishi pale.

Msemo "uharibifu" unaweza kujumuisha kusababisha majonzi ya hisia yatokanayo na hiyo adhabu au uharibifu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "teketeza" unaweza kutafsiriwa kama "kuangamiza kabisa" au "kuharibu kabisa".

Kulingana na muktadha, "uharibifu" inaweza kutafsiriwa kama "maangamizi kamili" au "uharibifu kamili" au "majonzi ya juu sana" au "balaa".

Tembea

Ufafanuzi

Neno "tembea" mara nyingi hutumika ikiwa na maana ya "ishi."

- "Enoko alitembea na Mungu" inamaanisha kuwa "Enoko aliishi kwa kuwa na mahusiano ya ukaribu sana na Mungu."
- "Kutembea kwa roho" inamaanisha kuongozwa na Roho Mtakatifu ili kufanya mambo yanayomtukuza na kumpa heshima Mungu.
- Mungu anaposema atatembea kati ya watu wake inamaana kuwa anaishi kati yao au anahusiana nao kwa karibu.
- "Kutembea kinyume" inamaanisha kuwa kuishi au kufanya kinyume na mtu au kitu fulani.

teseka, kuteseka

Ufafanuzi

Maneno "teseka" na "kuteseka" yanaeleza kupitia kitu kisicho pendeza, kama ugonjwa, maumivu, au magumu.

- Watu wanapo teswa au kuumwa, wana teseka.
- Wakati mwingine watu wana teseka kwasababu ya vitu vibaya walivyo fanya; wakati mwingine kwasababu ya dhambi na magonjwa duniani.
- Kuteseka kunaweza kuwa kimwili, kama maumivi au ugonjwa. Inaweza pia kuwa hisia kama hofu, kusononeka, au upweke.

tetemeka

Ufafanuzi

Neno "tetemeka" lina maana ya kutikisika kwa hofu au msongamano wa mawazo.

- Hili utumika kifumbo kumaanisha "kuogopa sana"
- Wakati mwingine neno "tetemeka" la eleza ardhi kutikisika kwasababu ya kelele kubwa.
- Biblia ina sema katika uwepo wa Bwana dunia itatetemeka. Hii inaweza maanisha kwamba watu wa dunia watatikisika kwa hofu ya Mungu au dunia yenyewe itatikisika.

Thamani

Ufafanuzi

"Thamani" ni watu au kitu kinachoonekana kuwa kina ubora.

- Neno "mawe ya thamani" ni miamba na madini yenye dangi na yenye thamani inayofanya yawe mazuri na yenye kufaa.
- Mfano wa mawe ya thamani ni kama dhahabu, rubi na zamaradi.
- Dhahabu na fedha huitwa madini ya thamani.
- Bwana alisema kuwa watu wake ni wa thamani kwenye macho yake (Isaya 43:4)
- Petro aliandika kuwa Mataifa ni wa thamani mbele za Macho ya Mungu (1Petro 3:4)

theluji

Ufafanuzi

Neno "theluji" ya husu chembe nyeupe za maji yaliyo ganda yanayo anguka kutoka mawinguni sehemu ambazo hali ya hewa ni ya baridi.

- Theluji ya anguka sehemu ya muinuko Israeli, lakini inaweza isibaki muda wote kwenye ardhi kabla ya kuyayuka. Vilele vya mlima mara nyingi ubakiwa na theluji kwa muda mrefu. Mfano mmoja wa Biblia ni ule wa Mlima Lebanoni.
- Kitu ambacho ni cheupe mara nyingi kinalinganishwa na rangi ya theluji, kama vazi au nywele za Yesu zinavyo elezewa "nyeupe kama theluji."
- Weupe wa theluji pia una ashiria kuwa safi.

thibitisha, uthibitisho

Ufafanuzi

Thibitisha au uthibitisho ni kuwa na hakika kuwa jambo fulani ni la kweli au kuaminika.

- Katika agano la kale Mungu anawaambia watu wake kuwa atalithibitisha agano lake kwao. Hii inamaana kuwa anasema kuwa atatunza ahadi aliyoiweka katika lile agano.
- Mfalme anathibitishwa hii inamaana ya kuwa maamuzi ya yeye kuwa mfalme yamekubalika na watu.
- Kuthibitisha alichokiandika mtu inamaana ya kuwa kilichoandikwa ni kweli.
- Uthibitisho wa agano maana yake ni kuwafundisha watu kuhusu habari njema za Yesu kwa namna ambavyo inaonesha kuwa ni kweli.
- Kutoa kiapo kama uthibitisho inamanisha kuapa kuwa jambo fulani ni la kweli au la kuaminika

tia moyo, kutia moyo

Ufafanuzi

Msemo "tia moyo" na "kutia moyo" ina maana ya kusema na kufanya mambo kusababisha mtu kuwa na faraja, matumaini, kujiamini na ujasiri.

Msemo wa kufanana ni "shawishi", ambao una maana ya kumsihi mtu kukataa tendo ambalo ni baya na badala yake kufanya mambo ambayo ni mazuri na sahihi.

Mtume Paulo na waandishi wengine wa Agano Jipya walifundisha Wakristo wajitie moyo wao kwa wao kupendana na kutumikiana.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, njia za kutafsiri "tia moyo" zinaweza kujumuisha, "kusihi" au "kufariji" au "kusema vitu vya upole" au "kusaidia na kuimarisha".

Msemo, "toa maneno ya faraja" una maana ya "kusema mambo ambayo yatasababisha watu wengine kujisikia kupendwa, kukubalika, na kuwezeshwa".

tia utumwani, katika kifungo

Ufafanuzi

"Kutia utumwani" mtu ina maana ya kumlazimisha mtu huyo kumtumikia bwana au nchi tawala. "Kutiwa utumwani" au "kuwa kifungoni" ina maana ya kuwa chini ya utawala wa kitu au mtu.

Mtu ambaye yupo katika utumwa au kifungoni anatakiwa kutumikia wengine bila malipo; hayupo huru kufanya anavyotaka.

"kutia utumwani" pia ina maana ya kuchukua uhuru wa mtu.

Neno lingine la "kifungoni" ni "utumwa".

Kwa njia ya tamathali, wanadamu ni "wafungwa" wa dhambi hadi Yesu awaweke huru kutoka katika utwala na nguvu yake.

Mtu anapompokea maisha mapya ndani ya Yesu, anasitisha kuwa mtumwa wa dhambi na anakuwa mtumwa wa utakatifu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "tia utumwani mwa" au "kuwa kifungoni mwa" unaweza kutafsiriwa kama "kulazimishwa kuwa mtumwa wa" au "kulazimishwa kumtumikia" au "kuwa chini ya utawala wa".

tii, mtiifu, utiifu

Ufafanuzi

Neno "tii" lina maana ya kufanya unachopaswa au kuamriwa. Neno "mtiifu" la eleza tabia ya mtu anaye tii. Wakati mwengine amri ni kuhusu kutofanya kitu, "usiibe"

- Mara kwa mara "tii" lina tumika katika muktadha wa kutii amri au sheria ya mtu mwenye mamlaka.
- Kwa mfano, watu wanatii sheria zinazo tengenezwa na viongozi wa nchi, ufalme, au taasisi ingine.
- Watoto wanatii wazazi wao, watumwa wanatii bwana zao, watu na mtii Mungu, na rahia wanatii sheria ya nchi.
- Wakati mtu katika mamlaka anapo amuru watu wasifanye kitu, wanatii kwa kutofanya.
- Neno "utiifu" la weza tafsiriwa kama, "kufanya kilicho amriwa" au "kufuata utaratibu"
- Neno "utiifu" la weza tafsiriwa kama, "kufanya kilicho amriwa" au "kufuata utaratibu"

totii, mkaidi, kutotii

Ufafanuzi

Msemo wa "totii" una maana ya kutotii kile mtu mwenye mamlaka ameamuru au kuagiza. Mtu anayefanya hivi anakuwa "mkaidi".

Mtu anayefanya jambo aliloambiwa kutofanya anakuwa hatii.

Kutotii pia ina maana ya kukataa kufanya jambo ambalo liliamriwa.

Msemo "mkaidi" pia hutumika kuelezea silika ya mtu ambaye kimazoea hatii au huasi. Ina maana ya kwamba ni wenye dhambi au waovu.

Msemo "ukaidi" una maana "tendo la kutotii" au "tabia ambayo ni kinyume na kile Mungu anataka".

"Mtu kaidi" anaweza kutafsiriwa kwa "watu wanaondelea kutii" au "watu ambao hawafanyi kile Mungu anaamuru"

tukuza

Ufafanuzi

Msemo "tukuza" ina maana ya kuonyesha au kunena jinsi gani kitu au mtu ni mkubwa au muhimu. Ina maana ya "kutoa utukufu".

Watu wanaweza kumtukuza Mungu kwa kunena juu ya mambo mazuri aliyoyafanya.

Wanaweza kumtukuza Mungu kwa kuishi kwa njia ambayo inampa heshima na kuonyesha jinsi alivyo mkuu na wa ajabu.

Biblia inaposema ya kwamba Mungu hujitukuza mwenyewe, ina maana anajifunua kwa watu ukubwa wake wa ajabu, mara kwa mara kupitia miujiza.

Mungu Baba atamtukuza Mungu Mwana kwa kudhihirisha kwa watu ukamilifu wa Mwana, ufaharu na ukuu.

Kila mtu anayemwamini Kristo atatukuzwa na yeye. Wanapofufuliwa katika uzima, watabadilishwa kuakisi utukufu wake na kuonyesha neema yake kwa uumbaji wote.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "kutoa utukufu kwa" au "kuleta utukufu kwa" au "kusababisha kuonekana kubwa".

Msemo "mtukuza Mungu" unaweza kutafsiriwa kama "kumsifu Mungu" au "kuzungumza juu ya ukuu wa Mungu" au "kuonyesha jinsi Mungu alivyo mkuu" au "kumheshimu Mungu"

tuma, kutuma nje, kutumwa

Ufafanuzi

"Kutuma" ni kusababisha mtu au kitu kwenda sehemu. "Kutuma nje" mtu ni kumwambia huyu mtu kwenda na kufanya japo au shughuli.

- Mara nyingi mtu anaye "tumwa nje" amechaguliwa kufanya kazi maalumu.
- Maneno kama "tuma mvua" au "tuma janga" ina maana "kusababisha ...kuja." Aina hii ya msemo utumika kumuelezea Mungu akisababisha vitu kutokea.
- Neno "tuma" pia la tumika katika msemo "tuma neno" au "tuma ujumbe" inayo maanisha kumpa mtu ujumbe ampe mtu mwingine.
- "Kumtuma" mtu "na" inaweza maanisha "kumpa" hicho kitu "kwa" mtu mwingine.
- Yesu mara nyingi utumia maneno "yeye aliye nituma" kumuelezea Mungu Baba aliye "mtu" duniani kuokoa watu.

Tumbo la uzazi

Ufafanuzi

Tumbo la uzazi ni mahali ambapo mtoto hukua ndani ya mama yake.

- Hili ni neno la zamani lililotumika kupunguza ukali wa neno.
- Neno la kisasa ni kizazi.
- Lunga nyingine hutumia neno tumbo.

tunda, kuzaa

Ufafanuzi

Msemo "tunda" lina maana ya sehemu ya mmea ambao inaweza kuliwa. Kitu ambacho "kinazaa" kina matunda mengi. Misemo hii pia hutumika kitamathali katika Biblia.

Biblia mara kwa mara hutumia "tunda" kumaanisha matendo na mawazo ya mtu. Kama vile tunda juu ya mti linavyoonyesha ni aina gani ya mti, vile vile maneno na matendo ya mtu hudhihirisha silika yake ikoje.

Mtu anaweza kuzaa matunda ya kiroho mazuri au mabaya, lakini msemo "kuzaa" mara kwa mara una maana chanya ya kuzaa matunda mema.

Msemo "kuzaa" pia hutumika kitamathali kumaanisha "mafanikio". Hii mara kwa mara humaanisha kuwa na watoto na uzao mwingi, pamoja na kuwa na chakula kingi na utajiri mwingine.

Kwa ujumla, msemo "tunda la" una maana ya kitu chochote ambacho hutoka kwa au ambacho huzalishwa na kitu kingine. Kwa mfano, "tunda la hekima" lina maana ya mambo mazuri ambayo hutokana na kuwa na hekima.

Msemo "tunda la roho" una maana kijumla ya kila kitu ambacho nchi huzaa kwa ajili ya watu kula. Hii inajumlisha sio matunda pekee kama mizabibu au tende, lakini pia mboga, karanga na nafaka.

Msemo wa tamathali "tunda la Roho" una maana ya sifa nzuri ambazo Roho Mtakatifu hutoa katika maisha ya watu ambao humtii yeye.

Msemo "tunda la tumbo" una maana ya "kile ambacho tumbo huzaa" yaani, watotot.

Tunga mimba

Ufafanuzi

Kutunga mimba ni kitendo cha kuwa na mimba ya mtoto. Pia inaweza kutumika kwa wanyama wanapokuwa na mimba.

- "Kupata mtoto" inaweza kutafsiriwa kama "kupata mimba."
- "kutunga mimba" inaweza kutafsiriwa kama "mwanzo wa mimba" au "wakati wa kuwa na mimba."
- Neno hili pia laweza kuwa na maana ya kuumba kitu au kufikiria kitu kama wazo au mipango.
- Pia neno hili limetumika kama "dhambi ikitunga mimba" ikiwa na maana ya "dhambi inapofikiriwa" au "mwanzo wa dhambi" au "dhambi inapoanza."

ua, mahakama

Ufafanuzi

"Ua" ni eneo ambalo liko wazi juu na limezungukwa na ukuta. Neno "mahakama" linamaanisha sehemu ambayo hakimu huamua mambo ya sheria na jinai.

- Maskani ilizungukwa na ua ambalo lilikuwa na ukuta uliotengenezwa kwa mapazia mazito.
- Jengo la hekalu lilikuwa na ua tatu za ndani moja kwa ajili ya kuhani, nyingine ya wanaume wa Kiyahudi, nyingine ya wanawake wa Kiyahudi.
- Ua za ndani zilitenganishwa kwa ukuta wa mawe uliowatenganisha na ua wa nje ambapo Mataifa waliruhusiwa kuabudu.
- Ua wa nyumba ilikuwa sehemu ya wazi katikati ya nyumba.
- Mahakama ya mfalme ni sehemu ambayo ilikuwa ikulu ambapo Mfalme aliitumia kutoa hukumu.

uadilifu

Ufafanuzi

Neno "uadilifu" inamaanisha kuwa mwaminifu, na mwenye msimamo mkali wa maadili na tabia.

Kuwa na uadilifu ni kuchagua kutenda kilicho kweli na sawa hata wakati hakuna mwingine anayetazama. Baadhi ya watu katika Biblia, kama Yusufu na Danieli, walionesha uadilifu walipokataa kufanya uovu na kuchagua kumtii Mungu. Kitabu cha Mithali kinasema kuwa ni bora kuwa maskini na kuwa na uadilifu kuliko kuwa tajiri na mfisadi na muongo.

uaguzi, mwaguzi, kutabiri, mtabiri

Ufafanuzi

Msemo "uaguzi" na "kutabiri" ina maana ya tendo la kujaribu kupata taarifa kutoka kwa roho katika ulimwengu wa rohoni. Mtu anayefanya hivi mara nyingine hujulikana kama "mwaguzi" au "mtabiri".

Katika kipindi cha Agano la Kale, Mungu aliamuru Waisraeli kutofanya uaguzi au utabiri.

Mungu hakuruhusu watu wake kutafuta taarifa kutoka kwake kutumia Urimu na Thumimu, ambayo yalikuwa mawe aliyoyatenga kutumika na makuhani wa juu kwa kusudi hilo. Lakini hakuruhusu watu wake kutafuta taarifa kupitia msaada wa roho chafu.

Waaguzi wa kipagani walitumia taratibu tofauti za kujaribu kutafuta taarifa kutoka kwenye ulimwengu wa roho. Mara zingine walichunguza sehemu za ndani za mnyama aliyekufa au kurusha mifupa ya wanyama juu ya ardhi, wakitafuta violezo ambavyo vingeweza fasiri ujumbe kutoka kwa miungu yao ya uongo.

Katika Agano Jipya, Yesu na mitume pia walikataa uaguzi, uchawi, ulozi na mazingaombwe. Matendo haya yote yalihusisha matumizi ya nguvu kutoka roho chafu na yanalaaniwa na Mungu.

Ubaguzi

Ufafanuzi

"Kuonesha ubaguzi" ni kitendo cha kuamua kuwaonesha watu umuhimu zaidi ya watu wengine.

- Hii ni sawa na kuonesha upendeleo ambayo ni kuwafanyia watu wengine vizuri zaidi ya watu wengine.
- Ubaguzi au Upendeleo unaoneshwa kwa watu kwa sababu wana mali au wanajulikana sana kuliko watu wengine.
- Biblia inawaelekeza watu wake wasioneshe ubaguzi wala upendeleo lwa watu matajiri au wenye cheo.
- Barua kwa Warumi Paulo anafundisha kuwa Mungu atawahukumu watu bila ubaguzi.
- Kitabu cha Yakobo kinatufundisha kuwa ni makosa kuwapendelea watu kwa sababu ni matajiri.

ubani

Ufafanuzi

Ubani ni harufu nzuri ya kiungo kutoka kwenye mti wa utomvu. Inatumika kutengeneza manukato na udi.

Katika kipindi cha Biblia, ubani ilikuwa kiungo muhimu kilichotumika kuandaa maiti kwa maziko.

Kiungo hiki kilikuwa cha thamani kwa sifa zake za uponyaji na kutuliza.

Wanaume wasomi walipokuja kutoka nchi ya mashariki kumwona mtoto Yesu Bethlehemu, ubani ilikuwa moja ya zawadi tatu walizoleta kwake.

Uchawi, mchawi

Ufafanuzi

Neno "uchawi" lina husu zoezi la kutumia nguvu hisio ya kawaida ambayo haitoki kwa Mungu. "Mchawi" ni mtu anaye tumia uchawi.

- Katika Misri, Mungu alipo fanya vitu vya maajabu kupitia Musa, wachawi wa Kimisri wa Farao aliweza kufanya baadhi ya vitu hivyo, lakini nguvu haikuwa ya Mungu.
- Uchawi mara nyingi wa husu kupiga rambli au kurudia maneno kuweza kufanya kitu cha ajabu kutokea.
- Mungu ana amuru watu wake wasifanye vitu hivi vya kichawi.

uchawi, mchawi, uganga

Ufafanuzi

"Uchawi" au "uganga" umaanisha kutumia mazinga umbwe, inayo maanisha kufanya vitu venye nguvu kupitia msaada wa roho chafu. "Mchawi" ni mtu ni mtu anaye fanya hivi vitu venye nguvu vya kimazinga umbwe.

- Matumizi ya mazinga umbwe na uchawi yaweza usisha vitu vyenye faida (kama kumponya mtu) na vitu kudhuru (kama kumlaani mtu). Lakini aina zote za uchawi si sawa, kwasababu utumia nguvu za roho chafu.
- Katika Biblia, Mungu anasema kuwa matumizi ya uchawi ni uovu kama dhambi zote mbaya.
- Maneno "uchawi" na "uganga" yaweza tafsiriwa kama, "roho chafu za nguvu"

uchungu wa kuzaa

Ufafanuzi

Mwanamke aliye katika "uchungu" anapitia uchungu unaofatiwa na kujifungua mtoto wake. Huu unaitwa "uchungu wa kuzaa."

Katika barua yake kwa Wagalatia, mtume Paulo alitumia neno hili kama mithali kuelezea jitihada yake kubwa ya kuwasaidia waumini wenzake kuwa kama Yesu zaidi na zaidi. Mfano wa uchungu wa kuzaa unatumika katika Biblia kuelezea jinsi maafa ya siku za mwisho yatakavyotokea kwa kasi na nguvu.

udaku

Ufafanuzi

Msemo "udaku" una maana ya watu kuzungumza juu ya masuala binafsi ya mtu mwingine, mara nyingi katika hali ya hasi na isiyo na faida. Mara nyingi kile kinachozungumzwa hakijathibitishwa kuwa kweli.

Biblia inasema ya kwamba kusambaza taarifa hasi kuhusu mtu ni kosa. Udaku na kashfa ni mifano ya aina hii ya kauli hasi.

Udaku ni wa madhara kwa mtu anayezungumzwa kwa sababu mara nyingi humuumiza uhusiano wa mtu na watu wengine.

ufalme

Ufafanuzi

Ufalme ni kundi la watu linalotawalwana mfalme. Linamaanisha pia dola au sehemu za kisiasa ambalo mfalme au kiongozi mwingine ana madaraka na mamlaka.

Ufalme unaweza kuwa na ukubwa wowote kijiografia. Mfalme anaweza kutawala taifa au nchi au mji mmoja tu. Neno "ufalme" linaweza pia kumaanisha utawala wa kiroho au madaraka, kama usemi "ufalme wa Mungu." Mungu ni mtawala wa viumbe vyote, lakini usemi "ufalme wa Mungu" kwa mahsusi linamaanisha utawala juu ya watu waliomwamini Yesu na walionyenyekea kwa utawala wake. Biblia pia inazungumzia kuhusu Shetani kuwa na "ufalme" anao tawala kwa muda juu ya vitu vingi duniani. Ufalme wake ni uovu na unajulikana kama wa "giza."

Ufalme

Ufafanuzi

Neno ufalme linawaelezea watu au vitu ambavyo vinahusiana na mfalme au malkia.

- Mfano wa vitu vinavyoweza kuitwa vya kifalme ni kama mavazi ya mfalme, nyumba ya kifalme au taji.
- Mfalme na malkia huwa wanaishi katika nyumba ya kifalme.
- Mfalme huvaa mavazi maalumu yaitwayo "nguo ya kifalme." Mara nyingi nguo hii huwa na rangi ya zambarau ambayo ilikuwa hadimu na ya bei ghali.
- Katika agano jipya Yesu aliitwa kuhani wa kifalme.

ugomvi

Ufafanuzi

Neno "ugomvi" la eleza malumbano ya kimwili au kihisia kati ya watu.

- Mtu anaye sababisha ugomvi anafanya vitu vinavyo sababisha kutoelewana.
- Ugomvi wakati mwingine una hashiria kuwa hisia kali zinahusishwa, kama hasira au uchungu.

Uhalifu, mhalifu

Ufafanuzi

Uhalifu ni dhambi inayohusisha kuvunja sheria za nchi. Mhalifu ni mtu anayefanya uhalifu.

- Aina ya uhalifu ni kama kumuua mtu au kuiba mali ya mtu.
- Mhalifu hukamatwa na kuwekwa mateka kama mfungwa.
- Katika Biblia wahalifu wengine huwa wakimbizi, wakitoka sehemu moja hadi nyingine wakiwakimbia watu wanaotaka kuwadhuru kwa kulipa kisasi kwa uhalifu waliofanya.

uhalifu, uasi

Ufafanuzi

Neno "uhalifu" linamuelezea mtu ambaye hatii sheria na maagizo. Wakati nchi au kundi la watu wako katika hali ya "uasi" inamaanisha kuna kutokutii na upotevu wa maadili kulikoenea.

Mtu muasi ni mtu aliyekaidi na hatii amri za Mungu. Mtu Paulo aliandika kuwa katika siku za mwisho kutakuwa na "mwanamme wa uasi," au "yule mhalifu" atakaye shawishiwa na Shetani kufanya mambo maovu.

ujasiri, jasiri

Ufafanuzi

Ujasiri ni kitendo cha kukabiliana au kufanya jambo gumu au la hatari.

- Jasiri ni mtu anayefanya jambo la jema hatakama anahisi kuogopa au anakatishwa tamaa.
- Mtu anaonesha ujasiri anapokutana na maumivu ya mwili au hisia na kukabiliana nayo.
- "kuchukua ujasiri" ni "kutoogopa" au "kuwa na uhakika kuwa mambo yatakuwa sawa."
- Joshua alipokuwa anajiandaa kwenda kwenye nchi hatari ya Kanaani Munsa alimwambia awe mwenye nguvu na jasiri.
- Ujasiri inaweza kutafsiriwa kama "kutoogopa" au "imara."
- Kuongea kwa ujasiri inaweza kutafsiriwa kama "kuongea bila kuogopa"

ukoma, mkoma

Ufafanuzi

Neno "ukoma" linatumika katika Biblia kumaanisha aina kadhaaza magonjwa ya ngozi. "Mkoma" ni mtu mwenye ukoma. Neno "ukoma" pia linaweza kutumika kuelezea mtu au sehemu ya mwili iliyoadhirika na ukoma.

Aina flani za ukoma zinasababisha ngozi kupoteza rangi na mabaka meupe, kama Miriamu na Naamani walivyokuwa na ukoma. Katika nyakati za sasa, ukoma mara nyingi husababisha mikono, miguu, na sehemu zingine za mwili kuharibika. Kulingana na maelekezo ambayo Mungu aliwapa Waisraeli, mtu akiwa na ukoma, alionekana "mchafu" na ilimbidi kukaa mbali na watu wengine ili asiwaambukize na ugonjwa. Mkoma kawaida angasema "mchafu" ili wengine waonywe wasije karibu yake. Yesu aliponya wakoma wengi, pamoja na aina zingine za magonjwa.

Ukoo

Ufafanuzi

Ukoo ni kundi la wana familia wanaotokana na mababu.

- Katika agano la kale Waisraeli walihesabiwa kutokana na koo zao au makundi ya familia.
- Koo zilipewa majina kutokana na babu aliyejulikana sana.
- Mtu mmoja mmoja mara nyingine huitwa kwa jina la ukoo wake. Kwa mfano baba mkwe wa Musa mara nyingine aliitwa kwa jina la ukoo wake Reueli.
- Ukoo waweza kutafsiriwa kama "kundi la familia" au "ndugu."

ulimi

Ufafanuzi

Kuna maana kadhaa katika Biblia ya "ulimi."

- Katika Biblia, maana iliyo zoeleka ni "lugha" au "hotuba."
- Wakati mwingine "ulimi" unaweza maanisha lugha inayo zungumzwa na baadhi ya makundi ya watu.
- Wakati mwingine ina maana ya lugha ya kimuujiza ambayo Roho Mtakatifu anawapa waamini wa Kristo kama "karama za Roho"
- Msemo "ndimi" za moto uleza "miyale" ya moto.
- Katika maneno "ulimi wangu wafurahia," neno "ulimi" waeleza mtu wote.
- Msemo "ulimi wa uongo" waeleza sauti ya mtu au hotuba.

ulizia

Ufafanuzi

Usemi "ulizia" inamaana kumuomba mtu taarifa. Usemi wa "kuulizia kwa"mara nyingi unatumika kumaanisha kumuomba Mungu hekima au msaada.

Agano la kale limetunza kumbukumbu ya mifano kadhaa ambapo watu walimuuliza Mungu. Neno pia linaweza kutumika kwa mfalme au afisa wa serikalini kufanya utafiti katika kumbukumbu za maandishi rasmi. Kulingana na mazingira, "ulizia" inaweza kutafsiriwa kama "kuomba" au "kuomba taarifa." Usemi "kumuuliza Yahwe" inaewza kutafsiriwa kama "kumuomba Yahwe uongozo" au "kumuuliza Yahwe nini cha kufanya." "Kuulizia juu ya" kitu inaweza kutafsiriwa ka "kuuliza maswali kuhusu" au "kuulizia taarifa kuhusu." Yahwe anaposema, "Sitaulizwa na wewe" hii inaweza kutafsiriwa kama, "Sita kuruhusu wewe uniombe taarifa" au "hautaruhusiwa kutafuta msaada kutoka kwangu."

Umba, Uumbaji, Muumbaji

Ufafanuzi

Kuumba ni kutengeneza kitu au kusababisha kitu kitokee. Kitu kinachoumbwa kinaitwa uumbaji. Mungu anaitwa muumbaji kwa sabau alisababisha vitu vyote vya dunia vikatokea.

- Neno hili linapotumika kumuelezea Mungu alipoumba dunia inaonesha kuwa aliiumba bila kutumia kitu.
- Wanadamu wanapoumba vitu wanaviumba kwa kutumia vitu ambavyo vipo tayari.
- Maranyingine uumbaji inatumika kuelezea vitu vya dhahania kama "kuumba amani au kuumba moyo safi kwa mtu."
- Neno Uumbaji inaelezea mwanzo wa ulimwengu ambapo Mungu kwanza aliumba kila kitu

umbo, sanamu ya kuchonga, umbo la kuchonga, umbo la chuma

Ufafanuzi

Maneno haya yote yanatumika kumaanisha sanamu ambazo zimetengenezwa kwa ajili ya kuabudu miungu ya uongo. Katika mazingira ya kuabudu sanamu, neno "sanamu" ni njia fupi ya kusema "sanamu ya kuchonga."

"Sanamu ya kuchonga" au "umbo la kuchonga" ni kitu cha mbao kilichofanywa kuonekana kama mnyama, mtu, au kitu. "Umbo la chuma" ni kitu au sanamu iliyoundwa kwa kuyeyusha chuma na kuimwaga katika umbo tupu ambalo lina umbo la kitu, mnyama, au mtu. Vitu hivi vya mbao na chuma vilitumika katika kuabudu miungu ya uongo. Neno "umbo" wakati wa kuzungumzia sanamu inamaanisha kati ya sanamu ya mbao au ya chuma.

Umri

Ufafanuzi

"Umri" ni idadi ya miaka aishiyo mwanadamu. pia hutumika kuonesha nyakati kwa ujumla.

- Maneno mengine yanayotumika kuelezea wakati ni kipindi au msimu.
- Yesu anarejea "nyakati hizi" kama wakati wa sasa ambapo dhambi, uovu na kutokutii kumeijaza dunia.
- Kutakuwa na nyakati zijazo ambapo haki itatawala mbinguni na duniani pote.

unyofu

Ufafanuzi

Neno "unyofu" ueleza kutenda kwa namna inayo fuata sheria za Mungu.]

- Maana ya hili neno ni pamoja kusimama wima na kuangalia mbele.
- Mtu aliye "mnyofu" ni mtu anaye tii maagizo ya Mungu na hafanyi vitu vilivyo nje ya mapenzi yake.
- Maneno kama "uadilifu" na "haki" yana maana moja na wakati mwingine utumika sambamba kama "audilifu na haki."

uongo, ukaidi, kuipotosha

Ufafanuzi

Neno "kilichopotoka" linatumika kumuelezea mtu au tendo fulani ambalo linapotosha kimaadili. Neno "ukaidi" linamaana ya tabia ya kikaidi". Kupotosha kitu inamaana ya kugeuza jambo toka kwenye usahihi wake au uzuri wake.

- Mtu au kitu ambacho kimepotoka kimegeuzwa toka kwenye kilicho kizuri au sahihi.
- Katika Biblia Waisraeli walifanya kwa ukaidi walipomkosea Mungu. Walifanya hivi kwa kuabudu miungu ya uongo.
- Tendo lolote lililo kinyume na tabia za Mungu linaelezewa kama lililopotoka.
- "Hotuba iliyopotoka" inaweza kutafsiriwa kama "kuzungumza kwa namna mbaya.
- "Matendo ya ukaidi" inaweza kutafsiriwa kama "kutenda matendo mabaya" au "kufanya mambo kinyume na amri za Mungu."

upanga

Ufafanuzi

Upanga ni silaha ya chuma nyembamba inayo tumika kukata au kuchoma. Ina mshikio na nch ndefu.

upinde

Ufafanuzi

Aina hii ya silaha ambayo inajumuisha mishale ya kurusha kutoka katika upinde. Katika nyakati za Biblia ilitumika kupigana na maadui na kuwindia.

- Upinde unatengenezwa kwa mti, mfupa au chuma au vitu vingine vigumu, kama vile jino la dubu. Imepinda na kufungwa kwa kamba.
- Mshale ni kitu chembamba chenye ncha kali, upande mmojawapo. Nyakati za kale, mshale ulitengenezwa kwa kutumia vitu mbalimbali kama vile mtu, mfupa, jiwe, au chuma.
- Pinde na mishale kwa kawaida inatumiwa na wawindaji au maaskari.
- Neno "mshale" wakati mwingine linatumika kitamathari katika Biblia kurejerea shambulio la adui au hukumu ya ki- Mungu.

upole

Ufafanuzi

Neno "upole" la elezea mtu aliye mtaratibu, mnyenyekevu, na aliye tayari kuteseka dhuluma. Upole ni uwezo wa kuwa mtaratibu ata kama ukali au nguvu inaonekana ni sahihi.

- Upole una endana na unyenyekevu.
- Hili neno la weza tafsiriwa kama "utaratibu".
- Neno "upole" la weza tafsiriwa kama "utaratibu" au "unyenyekevu."

ushauri, mshauri

Ufafanuzi

Ushauri inamaana ya kumsaidia mtu kuamua kwa busara juu ya jambo fulani. Mshauri mwenye busara ni mtu anayetoa ushauri ambao utamsaidia mtu kuamua kwa usahihi.

- Wafalme wana washauri maalumu wanaowasaidia kuamua mambo ya muhimu juu ya watu wanaowaongoza.
- Mara nyingine ushauri unaotolewa waweza ukawa mbaya. Mshauri mbaya anaweza kumshauri mfalme kufanya maamuzi ya kuwadhuru watu.
- Inategemea na mukhtadha ushauri yaweza kutafsiriwa kama "kusaidia kuamua." au "onyo" au "mwongozo."

ushuru

Ufafanuzi

Neno "ushuru" la husu zawadi kutoka kwa mtawala mmoja kwenda kwa mwingine, kwa kusudi la ulinzi na mausiano mema kati ya mataifa yao.

- Ushuru unaweza kuwa malipo ambayo mtawala au serikali ina itaji kutoka kwa watu, kama kodi.
- Katika Biblia, wafalme wasafiri au watawala walilipa ushuru kwa mfalme wa eneo waliyo kuwa wanasafiri kupita kuhakikisha watalindwa na kuwa salama.
- Mara nyingi ushuru una jumuisha vitu vingine kuacha pesa, kama vya kula, manukato, nguo za bei, na vitu vya gharama kama dhahabu.

uso

Ufafanuzi

Neno "uso" lina maana ya sehemu ya mbele ya kichwa cha mtu. Msemo huu pia una maana kadhaa za tamathali.

Msemo wa "uso wako" mara kwa mara ni njia ya tamathali ya kusema "wewe". Vivyo hivyo, msemo "uso wangu" mara kwa mara una maana ya "Mimi".

Katika hali ya kimwili, "kumkabili" mtu au kitu ina maana ya kutazama upande wa huyo mtu au kitu.

"Kukabiliana" ina maana ya "kutazamana"

Kuwa "uso kwa uso" ina maana ya kwamba watu wawili wanatazamana katika umbali wa karibu.

Yesu "alipoweka uso wake kuelekea Yerusalemu" ina maana ya kwamba aliamua kwa dhati kwenda.

"Kuweka uso dhidi ya" watu au mji ina maana kuamua kwa nguvu: kutoimarisha tena, au kumkataa mtu au mji huo.

Msemo "uso wa nchi" una maana ya sehemu ya juu ya dunia na mara kwa mara ni kumbukumbu ya jumla ya dunia nzima. Kwa mfano, "njaa inayofunika uso wa dunia" ina maana ya njaa inayosambaa ambayo hugusa watu wengi wanaoishi juu ya nchi.

Msemo wa tamathali, "usifiche uso wako kwa watu wako" una maana "usiwakatae watu wako" au "usiwaache watu wako" au "usiache kuwatunza watu wako".

Mapendekezo ya Tafsiri

Ikiwezekana, ni bora kubaki na msemo au kutumia msemo katika lugha hii ambayo ina maana ya kufanana.

Msemo "kukabili" unaweza kutafsiriwa kama "kugeuka upande wa" au "kutazama moja kwa moja" au "kuangalia uso wa".

Msemo "uso kwa uso" unaweza kutafsiriwa kama "karibu kabisa" au "mbele ya" au "katika uwepo wa".

Kulingana na muktadha, msemo "mbele ya uso wake" unaweza kutafsiriwa kama "kabla yake" au "mbele yake" au "katika uwepo wake".

Msemo "weka uso wake kuelekea" unaweza kutafsiriwa kama "kuanza kusafiri kuelekea" au "aliamua akilini mwake kuondoka".

Msemo "kuficha uso wake kutoka kwa" unaweza kutafsiriwa kama "kugeuka kutoka kwa" au "kuacha kusaidia au kulinda" au "kukataa".

"Kuweka uso wake dhidi ya" mji au watu inaweza kutafsiri kama "kutazama kwa hasira na kushutumu" au "kukataa kukubali" au "kuamua kukataa" au "kulaumu na kukataa" au "kutoa kuhukumu".

Msemo "tamka mbele ya uso wao" inaweza kutafsiriwa kama "sema kwao moja kwa moja".

Msemo " katika uso wa nchi" inaweza kutafsiriwa kama "katika nchi yote" au "juu ya dunia nzima" au "kuishi katika dunia".

Utaji

Ufafanuzi

Utaji ni kipande cha nguo kinachotumika kufunikia kichwa au uso ili usionekane.

- Musa alifunika uso wake na utaji baada ya kuwa katika uwepo wa Bwana ili mwanga wa uso wake usionekane kwa watu.
- Katika Biblia mwanamke hutumia utaji kujifunika kichwa chake au uso wake mbele za watu au katika uwepo wa wanaume.
- Kitenzi "kufunika" inamaana ya kufunika kwa utaji.
- Katika tafsiri zingine za Kiingereza Utaji inatumika kuelezea pazia kubwa lililitumika kufunikia mlango wa kuingilia patakatifu pa patakatifu.

Utawala, mtawala

Ufafanuzi

Maneno "utawala" au "mtawala" yana maana ya kusimamia na kuongoza watu wa nchi ili kuwasaidia wafanye sawasawa na inavyotakiwa.

- Danieli pamoja na vijana wengine watatu wa Kiyahudi walichaguliwa kuwa watawala au viongozi wa serikali katika eneo fulani la Babiloni.
- Kwenye agano jipya neno "utawala" limetumika kumuelezea mtu aliye na karama za roho mtakatifu.
- Mtu aliye na karama ya rohoni ya utawala ana uwezo wa kuongoza watu na kuwasimamia katika usimamizi wa majengo na mali nyingine.

utukufu

Ufafanuzi

Neno "utukufu" la eleza uzuri wa ajabu na umaridadi ambao una ambatana na utajiri na muonekano wa kuvutia.

- Mara nyingi utukufu utumika kufafanua utajiri ambao mfalme anao, au jinsi anavyo katika nguo zake nzurui na za gharama.
- Neno "utukufu" lina weza pia kutumikakueleza uzuri wa miti, milima, na vitu vingine Mungu alivyo umba.
- Badhi ya miji inasemwa kuwa na utukufu, ikielezea mali asili zao, majengo makubwa na barabara, na utajiri wa watu, pamoja na nguo za gharama, dhahabu na fedha.

uvumba

Ufafanuzi

Neno "uvumba" linamaanisha mchanganyiko wa vikolezo vyenye manukato mazuri vinavyochomwa kutoa moshi wenye harufu nzuri.

Mungu aliwaambia Waisraeli kuchoma uvumba kama sadaka kwake. Huu uvumba ulitakiwa kutengenezwa kwa kuchanganya kiwango sawa cha vikolezo maalumu vitano kama Mungu alivyoagiza. Huu ulikuwa uvumba mtakatifu, kwa hiyo hawakutakiwa kuutumia kwa kitu kingine chochote. "Madhabahu ya kufukuzia uvumba" ilikuwa madhabahu maalumu ya kuchomea uvumba. Uvumba ulitolewa angalau mara nne kwa siku, kwa kila saa ya maombi. Ilitolewa pia kila wakati sadaka ya kuteketeza ilipotolewa. Kuchomwa kwa uvumba kunaashiria maombi na kuabudu vinaponyanyuka juu kwa Mungu kutoka kwa watu wake. Njia zingine za kutafsiri "uvumba" zinaweza kuwa, "vikolezo vya manukato mazuri" au "mimea yenye harufu nzuri."

Uvumilivu

Ufafanuzi

Uvumilivu ni kitendo cha kupita katika wakati mgumu na kuwa na subira.

- Mtu akiwa na uvumilivu kwa mtu fulani inamaana kuwa anampenda yule mtu na atamsamehe kosa lolote ambalo mtu yule atafanya.
- Biblia inawafundisha watu wa Mungu kuwa wavumilivu wanapopitia magumu na kuwavumilia watu pia.
- Kwa sababu ya rehema zake Mungu anawavumilia watu wake japokuwa ni wenye dhambi wanaostahili adhabu.

uwezo

Ufafanuzi

Neno "uwezo" la husu hali ya kuwa na nguvu kimwili, kihisia, au kiroho.

- "Uwezo" yaweza elezea kuweza kusimama dhidi ya aina ya nguvu.
- Mtu ana uwezo wa nia kama anaweza kutoanguka kwenye jaribu.
- Mwandishi mmoja wa Zaburi anamuita Yahweh uwezo wake, inayo maanisha Mungu ana msaidia kuwa na nguvu.

Uyahudi, dini ya Kiyahudi

Ufafanuzi

Neno "Uyahudi" inamaanisha dini inayofuatwa na Wayahudi. Inajulikana piakama "dini ya Kiyahudi."

Katika Agano la Kale, neno "dini ya Kiyahudi" inatumika wakati katika Agano Jipya neno "Uyahudi" ndio linatumika. Uyahudi inajumuisha sheria zote za na maelekezo ya Agano la Kale ambayo Mungu aliwapa Wasiraeli kutii. Inajumuisha pia desturi na tamaduni zilizoongezwa katika dini ya Kiyahudi kadri muda ulivyoenda. Wakati wakutafsiri, usemi "dini ya Kiyahudi" au "dini ya Wayahudi" zinaweza kutumika katika Agano la Kale au Jipya. Lakini, neno "Uyahudi" linapaswa kutumika tu kwenye Agano Jipya, kwa sababu neno hilo halikuwepo kabla ya wakati huo

uzao, kutokana na

Ufafanuzi

"Uzao" ni mtu ambaye ni ndugu wa damu moja kwa moja wa mtu mwingine nyuma kabisa katika historia.

Kwa mfano, Abrahamu alikuwa uzao wa Nuhu. Uzao wa mtu ni watoto wake, wajukuu, na watukuu, na kuendelea. Vizazi vya Yakobo vilikuwa makabila kumi na mawili ya Israeli.

msemo "kutokana na" ni njia nyingine ya kusema "uzao wa" kama vile "Abrahamu alitokana na Nuhu". Hii inaweza kutafsiriwa kama "kutokana na uzao wa"

viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini

Ufafanuzi

Usemi "viongozi wa Kiyahudi" au "mamlaka ya Kiyahudi" inamaanisha viongozi wa dini kama makuhani na walimu wa sheria za Mungu. Walikuwa na mamlaka yakufanya maamuzi ya mambo yasiyo yakidini pia.

- Viongozi wa Kiyahudi walikuwa ndio makuhani wakuu, waandishi (walimu wa sheria za Mungu).
- Makundi mawili makuu ya viongozi wa Kiyahudi walikuwa Mafarisayo na Masadukayo.
- Viongozi sabini wa Kiyahudi walikutana pamoja katika Baraza la Wayahudi Yerusalemu kufanya maamuzi kuhusiana na mambo ya sheria.
- Viongozi wengi wa Kiyahudi walikuwa na majivuno na walidhani ni watakatifu. Walimuonea wivu Yesu na walitaka kumdhuru. Walidai kumjua Mungu ila hawakumtii.
- Mara nyingi usemi "Wayahudi" inamaanisha viongozi wa Kiyahudi, hasa katika mazingira walipokuwa na hasira na Yesu na walipojaribu kumtega au kumdhuru.
- Maneno haya yanaweza pia kutafsiriwa kama "viongozi wa Kiyahudi" au "watu waliotawala juu watu wa Kiyahudi" au "Viongozi wa dini wa Kiyahudi."

viuno

Ufafanuzi

Neno "viuno" kinamaanisha sehemu ya mwili ya mnyama au mtu aliyo katikati ya mbavu za chini na mifupa ya nyonga, pia ikijulikana kama tumbo la chini.

Msemo "kaza viuno" unamaanisha kujiandaa kufanya kazi ngumu. Inatokea katika utamaduni wa kuchomekea sehemu ya chini ya joho kwenye mkanda kiunoni ili kusogea kwa urahisi. Neno "viuno" mara nyingi linatumika katika Biblia kumaanisha sehemu ya chini ya mnyama iliyotolewa sadaka. Katika Biblia, msemo "viuno" mara nyingi humaanisha sehemu za siri za mwanamme kimafumbo na kitasifida kama chanzo cha uzao wake. Msemo "atatoka katika viuno vyako" unaweza pia kutafsiriwa kama, "atakuwa uzao wako" au "atazaliwa kutokana na mbegu yako" au "Mungu atasababisha kutoka kwako." Inapozungumzia sehemu ya mwili, hii inaweza pia kutafsiriwa kama "tumbo" au "nyonga" au "kiuno," kulingana na mazingira.

vumilia, uvumilivu

Ufafanuzi

Msemo "vumilia" una maana ya kudumu muda mrefu au kustahamili jambo gumu kwa uvumilivu.

Pia ina maana ya kusimama imara wakati wa mitihani kuwepo, bila kukata tamaa.

Msemo "uvumilivu" unaweza kumaanisha "subira", "ustahamilivu katika majaribu" au "kustahamili pale unapoteswa".

Faraja kwa Wakristo "kuvumilia mpaka mwisho" ni kuwaambia wamtii Yesu, hata kama hili litasababisha wao kuteseka.

"Kuvumilia mateso" pia inaweza kumaanisha "kupitia mateso".

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia za kutafsiri msemo "vumilia" zinaweza kujumuisha "stahamili" au "kuendelea kuamini" au "kuendelea kufanya kile Mungu anachotaka ufanye" au "simama imara".

Katika baadhi ya muktadha, "kuvumilia" kunaweza kutafsiriwa kama, "kupitia jaribu" au "kupitia".

Kwa maana ya kudumu muda mrefu, msemo "vumilia" unaweza kutafsiriwa kama "kudumu" au "kuendelea". Msemo, "hatavumilia" unaweza kutafsiriwa kama, "hatadumu" au "hataendele kuishi".

Njia za kutafsiri "uvumilivu" unaweza kujumuisha "ustahamilivu" au "kuendelea kuamini" au "kubaki mwaminifu".

Vumilia, uvumilivu

Ufafanuzi

"vumilia" au "uvumilivu" ni kitendo cha kuendelea kufanya kitu fulani hatakama ni ngumu sana kufanya au itachukua mda mrefu.

- Kuvumilia pia inamaana ya kuendelea kufanya kama Kristo alivyofanya japokuwa alipita katika majaribu magumu alivumilia.
- Mtu kama ni "mvumilivu" inamaana ana uwezo wa kuendelea kufanya anachopaswa kufanya hatakama kuna maumivu ay ugumu.
- Kuendelea kuamini anachofundisha Mungu kunahitaji uvumilivu hasa unapokutana na mafundisho ya uongo.

Waasi, uasi.

Ufafanuzi

Uasi ni kukataa kuitumikia mamlaka ya mtu fulani. Waasi ni watu wasiotii na kufanya mambo maovu. Mtu huyu anaitwa muasi.

- Mtu anaasi pale anapofanya jambo ambalo mamlaka iliyo juu yake imemkataza asifanye.
- Pia mtu anaweza kuasi akikataa kufanya analoamriwa afanye na mamlaka yake.
- Mara nyingine watu wanaasi juu ya serikali yao au kiongozi anayewaongoza.
- Uasi inamaana ya kukataa kutii au kuvunja sheria.

waheshima, heshima

Ufafanuzi

Neno "heshima" la husu kitu ambacho ni bora na chenye ubora. "mtu wa heshima" ni mtu aliye wa siasa au wa jamii ya juu.

- Mtu waheshima alikuwa ni afisa wa jimbo, mtumishi wa karibu wa mfalme.
- Neno "heshima" la weza tafsiriwa kwa, "afisa wa mfalme" au "afisa wa serikali" au "mtu wa uzao wa heshima"

wanaume wasomi, mamajusi

Ufafanuzi

Katika akaunti ya Mathayo ya kuzaliwa kwa Yesu, hawa wanaume "wasomi" au "wenye elimu" walikuwa "wanaume wenye hekima" walioleta zawadi kwa Yesu Bethlehemu muda baada ya kuzaliwa huko. Inawezekana walikuwa "mamajusi," ambao ni watu wanaofuatilia nyota.

Wanaume hawa walisafiri mbali kutoka nchi ya mbali kaskazini mwa Israeli. Haijulikani haswa ni wapi walipotokea na walikuwa kina nani. Lakini ni dhahiri walikuwa wasomi waliozisoma nyota. Wanaweza kuwa wazawa wa wanaume wenye hekima waliowatumikia wafalme wa Babeli wakati wa Danieli na waliofundishwa mambo mengi,ikiwemo kuzisoma nyota na kufafanua ndoto. Kiutamaduni inasemekana kuwa walikuwa wanaume watatu wenye hekima au wanaume wasomi kwa sababu ya zawadi tatu walizoleta kwa Yesu. Lakini, Biblia haisemi walikuwa wangapi.

watoza ushuru

Ufafanuzi

"Mtoza ushuru" alikuwa mfanya kazi wa serikali ambaye kazi yake ilikuwa kupokea pesa watu waliyo paswa kulipa serikali ushuru.

- Wakati wa Yesu na mitume, serikali ya Rumi

watu wenye busara

Ufafanuzi

Kwenye Biblia watu wenye busara ni watu wanaomtumikia Mungu na kutenda kwa busara na sio wapumbavu. Pia ni neno lililotumika kuwalelezea watu wenye ufahamu wa kipekee na uwezo wanaotumika kama sehemu katika mahakama ya mfalme.

- Maranyingine watu wenye busara huelezewa kwa kumumia maneno kama "watu wenye uelewa au watu wanaotenda kwa busara na haki kwa sababu wanamtii Mungu.
- Watu wenye busara waliomtumikia Farao na wafalme wengine walikuwa wasomi wa nyota ambao walitafuta maana ya nyota ilivyokaa angani.
- Pia watu wenye busara walitegemewa kutafsiri maana ya ndoto. Mfano mfalme Nebukadreza aliwataka watu wenye busara wamuelezee ndoto yake na kumwambia maana yake lakini hakuna aliyeweza kufanya hivyo isipokuwa Danieli aliyepokea ufahamu toka kwa Mungu.
- Mara nyingine watu wenye busara hufanya miujiza kupitia roho chafu.
- Katika agano jipya Yesu aliitwa mwanaume wenye busara.

wavuvi

Ufafanuzi

Wavuvi ni wanamume ambao hukamata samaki kutoka majini kama njia ya kupata pesa. Katika Agano Jipya, wavuvi walitumia mitego mikubwa kukamata samaki. Msemo "wavuvi" ni jina lingine la mvuvi.

Petro na mitume wengine walifanya kazi kabla ya kuitwa na Yesu.

Kwa kuwa nchi ya Israeli ilikuwa karibu na maji, Biblia ina kumbukumbu nyingi ya samaki na wavuvi.

Msemo huu unaweza kutafsiriwa na msemo kama "wanamume wanaokamata samaki" au "wanamume wanaopata pesa kwa kukamata samaki"

Wazee

Ufafanuzi

Wazee ni wanamume wa kiroho waliokomaa ambao wana majukumu ya kiroho na uongozi wa utendaji miongoni mwa watu wa Mungu.

Msemo "mzee" umetokana na kweli ya kwamba wazee asili yao walikuwa wanamume wa umri mkubwa ambao, kwa sababu ya umri wao na uzoefu, walikuwa na hekima kubwa.

Katika Agano la Kale, wazee walisaidia kuongoza Waisraeli katika masuala ya haki ya jamii na Sheria ya Musa.

Katika Agano Jipya, wazee wa Kiyahudi waliendelea kuwa viongozi katika jamii zao na pia walikuwa waamuzi kwa watu.

Katika makanisa ya mwanzo ya Wakristo, wazee wa Kikristo walitoa uongozi wa kiroho kwa mikusanyiko ya jamii ya waumini.

Wazee katika makanisa haya walijumuisha wanamume vijana ambao walikomaa kiroho.

Msemo huu unaweza kutafsiriwa kama "wanamume wazee" au "wanamume waliokomaa kiroho wanaoongoza kanisa".

Wazee wa ukoo

Ufafanuzi

Katika agano la kale "wazee wa ukoo" ni mababa wa Wayahudi hasa Abrahamu, Isaka na Yakobo.

- Pia inaweza kuwaelezea wana kumi na mbili wa Yakobo ambao ni wazee wa koo 12 za kabila la Israeli.
- Wazee wa ukoo ni sawa na mababu lakini mara nyingi inawaelezea hasa mababu wanaojulikana ambao ni viongozi wa kundi fulani la watu.

weka wakfu, kuwekwa wakfu kwa

Ufafanuzi

Kuweka wakfu ni kuweka kando kitu kwa ajili ya kusudi maalumu au shughuli.

Daudi aliweka wakfu dhahabu na fedha zake kwa Bwana.

Mara kwa mara, neno "kujitolea" lina maana ya tukio rasmi au sherehe ya kuweka kando kitu kwa ajili ya kusudi maalumu.

Kuweka wakfu kwa madhabahu ilijumuisha kutoa sadaka kwa Mungu.

Nehemia aliwaongoza Waisraeli katika kuweka wakfu kwa kuta za Yerusalemu zilizotengenezwa kwa ahadi mpya ya kumtumikia Yahwe pekee kwa vyombo vya muziki na kuimba.

Msemo wa "kuweka wakfu" unaweza kutafsiriwa kama "kutenga kusudi maalumu" au "kabidhi kitu kutumika kwa kazi maalumu" au "kabidhi mtu kutenda tendo maalumu".

wivu, tamani

Ufafanuzi

Msemo "wivu" una maana ya kuwa na wivu kwa mtu kwa sababu ya kile ambacho mtu huyo anamiliki au kwa sababu ya sifa za kutamanisha za mtu huyo. Msemo "tamani" una maana ya kumuonea wivu mtu hadi hatua ya kutamani kwa nguvu kuwa na kitu ambacho mtu huyo anacho.

Kwa kawaida wivu ni hisia ya hasi ya kuchukia kwa sababu ya mafanikio, bahati nzuri, au mali za mtu mwingine.

Kutamani ni hamu kali ya kutaka mali ya mtu mwingine, au hata mke au mume wa mtu mwingine.

woga, kutishwa

Ufafanuzi

Istilahi ' hofu' hurejelea hisia kali za woga or kitisho. Mtu aliye na hofu huwa ameogopa. woga ni hali kali na kubwa zaidi ya hofu, zaidi ya hofu ya kawaida. Mara kwa mara mtu anapokuwa ametishwa huwa ameshitushwa na ameshangazwa sana.

woga, kuogopesha

Ufafanuzi

Neno "woga" uelezea hisia ya hofu kuu. "Kuogopesha" mtu ina maana ya kusababisha huyo mtu kujisikia wasi wasi sana.

- "Woga" ni kitu au mtu anaye sababisha hofu kubwa.
- Hizi oga zinaweza elezwa kama "kuogopesha." Hili neno la weza tafsiriwa kama, "kisababisha hofu" au "kizalisha woga"
- Hukumu ya Mungu wakati mmoja itasababisha woga kwa wasio tubu waliyo kataa neema yake.

yayuka, yayushwa

Ufafanuzi

Neno "yayusha" la husu kitu kuwa maji kinapo pashwa. Pia utumika kimfano.

- Namna tofauti za vyuma vinapashwa hadi kuyayuka na kumiminwa katika vifaa ilikutengeneza vitu kama silaha au sanamu.
- Kama mshuma unavyo waka, kasha lake lina yayuka na kutiririka. Enzi za kale, maandishi yalitiwa muhuri kwa kumimina kiasi kidogo cha kasha lililo yakuka kwenye miisho yake.
- Matumizi ya mfano wa "yayuka" ina maana yakuwa nyepesi na dhaifu.
- Msemo, "mioyo yao itayayuka" ina maana watakuwa dhaifu sana kwasababu ya hofu.
- Msemo, "mioyo yao itayayuka na kuondoka" ina maana watalazimishwa kuondoka au wataonyeshwa kuwa dhaifu na kuondoka kwa kushindwa.

Zabibu

Ufafanuzi

Mzabibu ni tunda dogo, la duara, laini ambalo huota katika vishada vya mizabibu. Juisi ya mizabibu hutumika kutengeneza divai.

Kuna aina tofauti ya rangi ya mizabibu, kama vile kijani iliyoiva, zambarau au nyekundu.

Mizabibu binafsi inaweza kuwa na ukubwa kama sentimita moja au tatu.

Watu huotesha mizabibu katika bustani inayoitwa mashamba ya mizabibu. Hii huwa mistari mirefu ya zabibu.

Mizabibu ilikuwa chakula muhimu sana wakati wa Biblia na kuwa na mashamba ya zabibu ilikuwa ishara ya utajiri.

Ili kukaa na mizabibu isioze, watu mara kwa mara waliikausha. Mizabibu ya kukaushwa iliitwa "zabibu kavu" na ilitumika kutengeneza keki za zabibu kavu.

Yesu alitoa fumbo juu ya shamba la zabibu kuwafundisha wanafunzi wake juu ya ufalme wa Mungu.

Zambarau

Ufafanuzi

Hii ni rangi ambayo ni mchanganyiko kati ya rangu ya bluu na nyekundu.

- Hapo kale rangi ya zambarau ilikuwa hadimu na ya thamani sana ilitumika kama vazi kwa wafalme na viongozi wakuu.
- Kwa sababu ilikuwa ya gharama na ilichukua muda kutengeneza vazi la rangi ya zambarau ilikuwa alama ya utajiri na ufalme.
- Pia zambarau ilikuwa rangi iliyotumika kwenye mapazia ya hekalu na nguo zilizovaliwa na makuhani.
- Askari wa Rumi walimvalisha Yesu vazi la zambarau kabla hawajamsulubisha ili kumdhihaki kwa kuwa alisema yeye ni mfalme wa Wayahudi.
- Lidia toka katika mji wa Filipi alikuwa mwanamke aliyejipatia kipato kwa kuuza nguo za zambarau.

Zawadi

Ufafanuzi

Zawadi ni kitu anachopokea mtu kwa sababu amefanya jambo fulani liwe baya au zuri. Kumpa mtu zawadi ni kumpa mtu kitu anachostahili.

- Zawadi yaweza kuwa kitu kizuri ambacho mtu hupokea kwa sababu amefanya vizuri au amemtii Mungu.
- Maranyingine zawadi yaweza kuwa vitu hasi vinavyotokana na tabia mbaya. Haya ni matokeo hasi anayopata mtu baada ya kufanya matendo ya dhambi.

zinaa

Ufafanuzi

Msemo "zinaa" una maana ya tendo la ngono ambalo hufanyika nje ya mahusiano ya ndoa ya mwanamume na mwanamke. Hii ni kinyume na mpango wa Mungu.

Msemo huu unaweza kumaanisha tendo lolote la kingono ambalo ni kinyume na mapenzi ya Mungu, ikiwemo matendo ya usenge na ponografia.

Aina moja ya zinaa ni uzinzi, ambayo ni tendo la ngono haswa kati ya mtu aliyeoa na mtu ambaye sio mke au mume wake.

Aina nyingine ya zinaa ni "ukahaba" ambayo uhusisha kulipwa kufanya ngono na mtu.

Msemo huu pia hutumika kitamathali kumaanisha ukosefu wa uaminifu wa Israeli kwa Mungu walipoabudu miungu ya uongo.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "zinaa" unaweza kutafsiriwa kama "uzinzi" ikiwa maana sahihi ya msemo inaeleweka.

Njia zingine za kutafsiri msemo huu zinaweza kujumuisha "matendo mabaya ya ngono" au "ngono nje ya ndoa".

Msemo huu unaweza kutafsiriwa katika njia nyingine kutoka kwa neno "uzinzi".

Tafsiri ya matumizi ya tamathali ya msemo huu unatakiwa kukaa na maana halisi ikiwezekana kwa kuwa kuna ulinganisho wa kufanana katika Biblia kati ya kutokuwa mwaminifu kwa Mungu na kutokuwa mwaminifu katika mahusiano ya kimapenzi.

zingira, kuzingira

Ufafanuzi

Neno "kuzingira" la husu pale jeshi shambulizi linapo zunguka mji na kuusababisha usiweze kupokea maitaji na maji. "Kuzingira" mji ina maana kusababisha mji kuwa chini ya kuzungukwa.

- Wakati Babiloni ilipo kuja kushambulia Israeli, walitumia mbinu ya kuzingira Yerusalemu kudhohofisha watu kwenye mji.
- Mara nyingi wakati wa kuzingira, mapande ya mchanga yana undwa taratibu kuwezesha jeshi shambulizi kuvuka kuta za mji na kuvamia mji.

Washiriki

translationWords Washiriki

Rev. Yohana Batano
Ev. Lazaro Chalomhola
Pst. Jordan
Rev. Philipo Kanwele
Kazwanomo
Pst. John Kerim
Rev. Charles Mabisa
Yohana Magera
Rev. Erasmus Malelo
Joyce Gilbert Masasi
Bariki Malisa
Daudi Nungwana
Enoch Nungwana
Karen Riecks
Ev. Cloud Roman
Mr. James Semnkai

unfoldingWord® Translation Academy Washiriki

Jesse Griffin, BA in Biblical Studies, MA in Biblical Languages
Perry Oakes, PhD in Old Testament, MA in Linguistics, MA in Theology, BA in Biblical Studies
Susan Quigley, MA in Linguistics
Henry Whitney, BA in Linguistics
James N. Pohlig, M.Div., MA in Linguistics, D. Litt. in Biblical Languages
Ben Jore, BA Biblical Studies, M.Div.
Joel D. Ruark, PhD in Old Testament, MA in Theology
Todd L. Price, PhD in New Testament/Linguistics
Bev Staley
Carol Brinneman
Jody Garcia
Kara Anderson
Kim Puterbaugh
Lizz Carlton
Door43 World Missions Community